

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA
HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI
KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA
KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA
UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2021**

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
S.L.P 258, Maisara - Zanzibar, Simu: +255 24 2234009, Nukushi: +255 24 2234009
Baruapepe: info@ocagz.go.tz, Tovuti: www.ocagz.go.tz



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU
ZA SERIKALI ZANZIBAR**

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA
HESABU ZA SERIKALI
KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA
KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA
TAREHE 30 JUNI, 2021**

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112 pamoja na Sheria Nambari 12 ya mwaka 2016 ya Usimamizi wa Fedha za Umma kifungu namba 123 (4) Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo kila mwaka.

DIRA

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi

DHAMIRA

Kusimamia uwajibikaji katika Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

Katika kutoa huduma zenye ubora na zinazostahiki, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi kama vifuatavyo:-

Uaminifu

Kuhakikisha Ofisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria.

Uadilifu

Kuwa ni Ofisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

Kuwa Huru

Kuwa ni Ofisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria

Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi

Kuwa ni Ofisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

Kutunza Siri

Kuwa ni Ofisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

Uwazi na Uwajibikaji

Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma.

YALIYOMO

ORODHA YA MAJADWELI.....	ix
VIFUPISHO	xii
SHUKURANI	xiv
DIBAJI	xv
MUHTASARI	xvii
SURA YA KWANZA	1
UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI	1
1.2 WIGO NA MADHUMUNI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA.....	2
1.3 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA	2
1.4 UDHIBITI WA USALAMA WA MTANDAO	2
1.5 UTENGENEZAJI NA UDUMISHAJI WA MIFUMO.....	3
1.6 UDHIBITI WA UJUMLA WA TEKNOLOJIA YA HABARI	4
1.7 USIMAMIZI WA WATOA HUDUMA WA TEHAMA, UTOAJI WA HUDUMA ZA TEHAMA NA USIMAMIZI WA MATUKIO.....	5
SURA YA PILI	8
UKAGUZI WA MIFUMO YA BOHARI KUU YA DAWA.....	8
2.0 UTANGULIZI	8
2.1 MUUNDO WA IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA	8
2.2 KAZI ZA BOHARI KUU YA DAWA	12
2.3 MIFUMO YA TEHAMA INAYOTUMIKA BOHARI KUU YA DAWA	9
2.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI	12
SURA YA TATU	29
MUENDELEZO WA UKAGUZI WA MIFUMO WA USIMAMIZI WA FEDHA (IFMIS) KATIKA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO.....	29
3.0 UTANGULIZI	29
3.1 UANZISHWAJI WA MIFUMO WA IFMIS.....	29
3.2 MALENGO YA UKAGUZI	29

3.3	UPEO WA UKAGUZI.....	30
3.4	NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	30
3.5	CHANGAMOTO ZA UKAGUZI	31
3.6	HALI HALISI YA KIWANGO CHA UTUMIAJI WA MFUMO WA IFMIS KWA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO, WIZARA, IDARA PAMOJA NA WAKALA WA SERIKALI (MDAS).	33
3.7	KIWANGO CHA UTUMIAJI WA MFUMO WA IFMIS KATIKA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.	35
3.8	MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO.....	39
3.9	MAPENDEKEZO	57
3.10	HITIMISHO	58
SURA YA NNE	59
	UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO KATIKA BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021	59
4.0	UTANGULIZI	59
4.1	MALENGO YA UKAGUZI	60
4.2	UPEO WA UKAGUZI.....	60
4.3	MIONGOZO YA UKAGUZI	60
4.4	TAARIFA YA MFUMO UNAOTUMIKA KWA KUKUSANYIA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO.....	61
4.5	USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA MAKUSANYO YA MAEGESHO.....	61
4.6	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MAKUSANYO WA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO	65
4.6	MATOKEO YA UKAGUZI	65
SURA YA TANO	78
	UKAGUZI WA MFUMO WA KUSIMAMIA MALI ZA KUDUMU ZA SERIKALI (ASSET MANAGEMENT SYSTEM)	78
5.0	UTANGULIZI	78
5.1	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA.....	78
5.2	MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI.....	78
5.3	NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	79
5.4	TAARIFA ZA MFUMO WA USIMAMIZI WA MALI ZA KUDUMU ZA SERIKALI (ASSET MANAGEMENT SYSTEM).....	79

5.5	MAMBO YALIYOBAINIKA KWENYE MFUMO WA USIMAMIZI WA MALI.....	80
SURA YA SITA		89
UKAGUZI WA MFUMO WA MISHAHARA WA SERIKALI (GOVERNMENT PAYROLL SYSTEM)		89
6.0	UTANGULIZI	89
6.1	YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MISHAHARA WA SERIKALI.....	89
6.2	MATOKEO YA UKAGUZI KWENYE UDHIBITI WA TEHAMA KWA UJUMLA	94
SURA YA SABA		96
UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI NA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII (CRVS).....		96
7.0	UTANGULIZI	96
7.1	KAZI ZA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII	96
7.2	MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA	97
7.3	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA.....	97
7.4	MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI.....	97
7.5	NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	98
7.6	MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI	98
7.7	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA USAJILI NA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII(CRVS).....	99
SURA YA NANE		107
8.0	UTANGULIZI	107
8.1	MFUMO WA MALARIA EARLY DETECTION OF DISEASE	109
8.2	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA.....	110
8.3	UPEO NA MALENGO YA UKAGUZI.....	110
8.4	NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	111
8.5	MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KWENYE MFUMO WA UVIKO 19.....	112
8.6	MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KWENYE UKAGUZI WA MFUMO WA MALARIA.	113
8.7	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA UVIKO 19.....	113
8.8	UKAGUZI WA MFUMO WA MALARIA (MEEDS)	148
SURA YA TISA		150
UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI WA VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI		150
9.0	UTANGULIZI	150
9.1	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA.....	150

9.2	MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI.....	150
9.3	NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	151
9.4	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI WA VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI	152
SURA YA KUMI		159
UKAGUZI WA MFUMO WA MALIPO YA PENSHEMI JAMII KWA WAZEE WALIOTIMIZA UMRI WA MIAKA SABINI (70) NA KUENDELEA		159
10.0	UTANGULIZI	159
10.1	CHIMBUKO LA PENSHEMI JAMII	159
10.2	UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PENSHEMI JAMII KISHERIA	159
10.3	MAOMBI NA SIFA ZA KUIINGIZWA KATIKA PENSHEMI JAMII	159
10.4	KUSITISHWA AU KUONDOLEWA KATIKA MPANGO WA PENSHEMI JAMII	160
10.5	MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA.....	160
10.6	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA	161
10.7	MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI	161
10.8	NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	162
10.9	MUHTASARI WA HOJA ZA UKAGUZI.....	163
10.10	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WAMS ACCESS DATABASE SYSTEM WAZEE	164
10.11	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA ZANZIBAR UNIVERSAL PENSION SCHEME MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM	169
SURA YA KUMI NA MOJA.....		193
UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA MAPATO (MUTM).....		193
11.0	UTANGULIZI	193
11.1	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA	194
11.2	MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI	194
11.3	NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	195
11.4	MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MUTM.....	195
11.5	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA MAPATO (MUTM)	197
SURA YA KUMI NA MBILI.....		223
12.0	UTANGULIZI	223

12.1	UKAGUZI WA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI.....	223
12.2	WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA	226
12.3	UPEO NA MALENGO YA UKAGUZI	226
12.4	NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI	227
12.5	MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA MFUMO WA ZAMANI WA ZANMALIPO	228
12.6	MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA MFUMO MPYA WA ZANMALIPO	228
12.7	MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA UDHIBITI WA JUMLA NA UENDESHAJI WA TEHAMA	228
12.8	MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA ZANMALIPO	228
SURA YA KUMI NA TATU		246
	UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BODI YA MAPATO ZANZIBAR-ZRB	246
13.0	UTANGULIZI	246
13.1	UANZISHWAJI WA BODI YA MAPATO ZANZIBAR	246
SURA YA KUMI NA NNE		256
	UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR - PBZ.....	256
14.0	UTANGULIZI	256
14.1	UANZISHWAJI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR	256
14.2	MALENGO YA UKAGUZI.....	256
SURA YA KUMI NA TANO		264
	UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR – ZECO	264
15.0	UTANGULIZI	264
15.1	UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR.....	264
15.2	MALENGO YA UKAGUZI.....	264
SURA YA KUMI NA SITA		273
	UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR – (ZSSF). 273	
16.0	UTANGULIZI	273
16.1	UANZISHWAJI WA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR	273
16.2	LENGO LA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA YA ZSSF.....	273
SURA YA KUMI NA SABA		278
	UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR –(ZIC).....	278

17.0	UTANGULIZI	278
17.1	UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR	278
17.2	MALENGO YA UKAGUZI.....	278

ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Wasambazaji ambao hufanya manunuzi na Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia Mfumo.....	17
Jadweli Nambari 2: Ankara zenye namba za utambulisho uliofanana	19
Jadweli Nambari 3 : Ankara za madeni ambazo taarifa zake hazikuthibitishwa na wasambazaji	20
Jadweli Nambari 4: Mifumo inayotumika katika Vituo vya Afya na Hospitali zilizofanyiwa Ukaguzi.	23
Jadweli Nambari 5 : Taarifa zilizokuwa pungufu	31
Jadweli Nambari 6: Gharama zinazolipwa za "SLA" kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021.....	34
Jadweli Nambari 7 : Viwango vya matumizi ya moduli za mfumo wa IFMIS.....	35
Jadweli Nambari 8: Taarifa za hesabu za hazina zilizokuwa hazijaunganishwa kwenye mfumo.	39
Jadweli Nambari 9: Tofauti zilizobainika katika taarifa za usuluhishi wa kibenki za hesabu za Ofisi kuu ya malipo.....	41
Jadweli Nambari 10: Taarifa za fedha ambazo hazikuoneshwa katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki za mwisho wa mwaka.	42
Jadweli Nambari 11: Uchambuzi wa matumzi ya fedha yaliyofanyika nje ya mfumo wa IFMIS	43
Jadweli Nambari 12 : Matumizi yaliyofanyika katika hesabu ya Katibu Mkuu nje ya Mfumo wa IFMIS	44
Jadweli Nambari 13: Matumizi katika hesabu ya CPO iliyopo BOT yanayofanyika nje ya Mfumo	45
Jadweli Nambari 14 : Fedha zilizolipwa benki ambazo taarifa zake hazijaonekana katika Daftari la Fedha Taslim.....	47
Jadweli Nambari 15: Baadhi ya Miamala ya fedha ya hesabu ya Mfuko wa Miundombinu iliyokosa maelezo.....	47
Jadweli Nambari 16 : Fedha ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu za CPO-Reccurrent	48
Jadweli Nambari 17 : Fedha ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu za CPO-Development	49
Jadweli Nambari 18: Fedha za makusanyo ya kodi za TRA ambazo hazikuthibitishwa	

kupokelewa katika hesabu ya Hazina	49
Jadweli Nambari 19 : Uhaulishwaji wa fedha ambazo zimekosa maelezo	50
Jadweli Nambari 20 : Fedha za mapato ya ZRB ambayo huchelewa kuhaulishwa	53
Jadweli Nambari 21 : Fedha za mapato ya ZRB yaliyokosa uthibitisho wa kupelekwa katika hesabu ya BOT katika kipindi cha Julai 2016 hadi Oktoba 2016	54
Jadweli Nambari 22: Mchanganuo wa malipo ya "Application Consultant"	56
Jadweli Nambari 23: Mchanganuo wa malipo ya "Technical Consultant"	56
Jadweli Nambari 24: Mchanganuo wa malipo ya "Support Manager"	57
Jadweli Nambari 25: Mchanganuo wa malipo ya " System Development Consultant ".....	57
Jadweli Nambari 26: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto.....	62
Jadweli Nambari 27: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto.....	63
Jadweli Nambari 28: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto.....	64
Jadweli Nambari 29 : Mapato yanayotokana na faini yaliyokusanywa kwa miezi sita kuanzia Januari 2021 hadi Juni 2021	71
Jadweli Nambari 30 : Miamala ya Mapato ya madeni ambayo yamefutwa.....	74
Jadweli Nambari 31: Baadhi ya malipo yasiyotolewa stakabadhi (Receipts).....	76
Jadweli Nambari 32: Baadhi ya malipo yanayotolewa stakabadhi za mkono.....	76
Jadweli Nambari 33: Mchanganuo wa nakala za taarifa zilizobainika katika taarifa za vyeti vya watoto vilivyotolewa.....	103
Jadweli Nambari 34 :Orodha ya watoto wenye nambari ya utambulisho zaidi ya moja	104
Jadweli Nambari 35 : Mchanganuo wa Wastani wa Makusanyo kupitia taarifa za Hesabu mbali mbali.....	109
Jadweli Nambari 36 : Baadhi ya taarifa za vyeti vya kughushi vilivyobainika na ukaguzi	120
Jadweli Nambari 37: Baadhi ya Miamala ya USD 80 iliyoingizwa kwenye Hesabu ya TZS ya PBZ COVID RESCUE FUND TZS kama TZS 80 na baadhi ya Maafisa wa PBZ na kutumika kutoa huduma kwa wateja kupitia baadhi ya wahudumu wa Zan Medicals.....	138
Jadweli Nambari 38: Orodha ya taarifa zilizoombwa na kukosekana kwa ukaguzi.....	156
Jadweli Nambari 39 : Udhaifu wa usimamizi wa mfumo	178
Jadweli Nambari 40 : Nambari za utambuzi na kiwango cha Makusanyo katika Mfumo wa zamani wa ZanMalipo	224

Jadweli Nambari 41: Taasisi za Serikali zilizosajiliwa na zinazotumia mfumo mpya wa ZanMalipo.....	225
Jadweli Nambari 42: Nambari za utambuzi na kiwango cha Makusanyo katika Mfumo mpya wa ZanMalipo	226
Jadweli Nambari 43 : Hali halisi ya Utendaji kazi wa mifumo ya ZRB	249
Jadweli Nambari 44 : Programu zinazoendelea kutumika PBZ ambazo zimeisha muda wa matumizi	263
Jadweli Nambari 45: Malengo ya mfumo wa CIMIS ambayo hayakuweza kufikiwa	280

VIFUPISHO

ADDENDUM	Mkataba wa Nyongeza.
AFROSAI-E	African Organisation of English-Speaking Supreme Audit Institutions.
BANKS	Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Benki ya PBZ
BARAZA	Baraza la Manispaa.
BOT	Benki Kuu ya Tanzania
CIMIS	Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Bima
COBIT- 5	Control Objectives for Information and Related Technology.
CPO	Ofisi Kuu ya Malipo
DA	Msimamizi wa Kanzidata
DANIDA	Shirika la Maendeleo la Denmark.
ECONEX	Kampuni itoayo huduma za makusanyo ya maegesho kupitia mfumo
eGA	e – Government United Republic of Tanzania.
eGAZ	e - Government of Zanzibar.
eLMIS – CE	Mfumo wa zamani wa TEHAMA unaotumika kwa vituo vya afya na hospitali katika kuagiza na kuripoti dawa na vifaa tiba kutoka Bohari Kuu ya Dawa.
eLMIS – FE	Mfumo mpya wa TEHAMA unaotumika kwa vituo vya afya na hospitali katika kuagiza na kuripoti dawa na vifaa tiba kutoka Bohari Kuu ya Dawa.
FuMIS	Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Mafao ya ZSSF
ICT	Information and Communication Technology.
IFMIS	Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali.
INTOSAI	International Organisation of Supreme Audit Institutions.
ISACA	Information Systems Audit and Control Association.
ISPGG	Institutional Support Project for Good Governance
IT	Information Technology.
JSI	Kampuni inayotengeneza mifumo ya TEHAMA iliyopo Marekani.
LPO	Hati ya Utambulisho wa Manunuzi
MDA	Wizara, Idara na Wakala wa Serikali
MSD	Bohari ya Madawa.
mSupply	Mfumo Mkuu unaotumika kwa ajili ya kupokea taarifa za mahitaji ya dawa na vifaa tiba,kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba.

MUTM	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Mapato
OCAGZ	Office of Controller and Auditor General Zanzibar
PBZ	Benki ya Watu wa Zanzibar
PMU	Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi
POS	Point Of Sales.
SLA	Mkataba wa Kiwango cha Huduma
SLOTTEX ZANZIBAR	Mfumo wa kielektroniki wa makusanyo ya mapato ya maegesho.
STCL	Soft Tech Consultant Limited
SUPRIMA	Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Umeme
SUSOL	Kampuni inayotengeneza mifumo ya TEHAMA iliyopo New Zealand.
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TMS	Treasury Management System
TRA	Mamalaka ya Usimamizi wa Mapato Tanzania
UNICEF	Shirika la Kimataifa la Kusaidia Watoto.
USAID	Shirika la Msaada wa Maendeleo la Marekani.
USD	Dola ya Kimarekani.
UVIKO – 19	Ugongwa wa Virusi vya Korona wa mwaka 2019.
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani.
WAUJWJW	Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.
ZECO	Shirika la Umeme Zanzibar
ZIC	Shirika la Bima Zanzibar
ZRB	Bodi ya Mapato Zanzibar.
ZSSF	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar

SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya marekebisho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa maelekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali zinazochukuliwa katika kuimarisha na kuijengea uwezo Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora pamoja na Bodi ya Utumishi ya Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Claritas International pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Ofisi ya Mdhibili ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia kazi za ukaguzi zilizofanywa na Ofisi hii.

Natumia fursa hii, kuwasihia wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Ofisi ya Mdhibili katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo ya fedha na matumizi ya rasilimali za Umma.

DIBAJI

Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mawizara, Taasisi na Mashirika ya Umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112 pamoja na kifungu nambari 123(4) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 ambapo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na sheria nyenginezo.


Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii imejumuisha jumla ya mifumo Thelathini na Mbili (32) iliyokaguliwa ambapo mambo mbali mbali yaliyobainika kupitia ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA niliufanya katika Wizara tatu (3), Taasisi mbili (2) zinazojitegemea na Mashirika ya Umma matano (5) kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo ukaguzi huo umeangalia mifumo ya udhibiti wa ndani ya TEHAMA (ITGCs & ITACs), Utawala wa TEHAMA (IT Governance), taratibu za ununuzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA (Contracts for IT Systems and Infrastructures), Usalama na udhibiti wa taarifa katika mifumo (IT Security & System Access Controls) pamoja na uzingatiaji wa sheria, kanuni, sera na miongozo.

Nilifanya ukaguzi huu kwa mujibu wa miongozo na Viwango vya Kitaifa (eGAZ na eGA) pamoja na viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Kiafrika la Taasisi za Juu za Ukaguzi Zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E) na Jumuiya ya Kimataifa inayohusu Udhibiti na Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA (ISACA).

Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila taasisi iliyokaguliwa na mapendekezo ya kutekeleza ili kuboresha na kuondoa dosari zilizobainika kwa lengo la kutokujirejea mara nyengine dosari hizo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein A. Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.



DKT. OTHMAN ABBAS ALI

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

ZANZIBAR

MUHTASARI

Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma zilizopo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika shughuli zao kwa kutambua faida za mifumo hii katika kufikia malengo ya Taasisi hizo kwa wakati na kwa gharama nafuu. Matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika sekta za Umma yameongeza utegemezi wa mifumo husika katika shughuli za taasisi za umma na pia kuongeza changamoto mpya zinazohitaji usimamizi Madhubuti. Hii inapelekea umuhimu wa kufanya ukaguzi wa udhibiti katika usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha uendelevu, utengemavu na usalama wa mifumo.

Katika mwaka ya fedha 2020/2021 ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA uliofanyika uliangazia zaidi udhibiti wa mifumo ya taarifa za Usimamizi wa TEHAMA, usimamizi wa miradi ya utengenezaji na usimikaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa jumla wa TEHAMA, pia nilitumia taratibu nyengine za kiukaguzi ambazo zilikuwa muhimu katika kutoa maoni ya kiukaguzi ambapo wakaguzi walifanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia athari za majanga yaani "risk based audit", hivyo basi matokeo ya ukaguzi yanatokana na Kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi ziliwasilishwa kwa usahihi na kwa wakati kwa lengo la kuweza kufanyiwa kazi na wakaguzi wa mifumo.

Ukaguzi uliofanyika umezingatia matakwa ya kimaadili katika kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata uhakika wa kutosha juu ya udhibiti na ufanisi wa mifumo ya TEHAMA. Kwa madhumuni hayo ukaguzi huo ulikua ni kwa mujibu wa Muongozo wa Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA wa AFROSAI-E wa mwaka 2017, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, Miongozo ya Serikali Mtandao ya mwaka 2021, Sera ya TEHAMA ya Serikali ya mwaka 2012 pamoja na miongozo ya Kimataifa kama COBIT-5 na ISO/IEC , ISACA n.k

Aidha, katika ukaguzi uliofanyika imebainika mapungufu yanayotokana na usimamizi wa shughuli za TEHAMA katika taasisi za Serikali yanatokana na kutofuatwa kwa viwango na miongozo ya mtandao wa Serikali, kutokufuatwa kwa miongozo iliyopangwa na kutolewa na E-Gov kwa taasisi za umma katika kusimamia uwajibikaji wa mifumo ya Serikali kunasababishwa na msukumo hafifu wa kuhakikisha taasisi za Serikali zinazingatia viwango na miongozo ya Serikali, uelewa mdogo wa hatari zinazopelekewa na matumizi ya TEHAMA kwa menejimenti, na ukosefu wa mapitio ya mara kwa mara ya udhibiti wa ndani wa TEHAMA. Sababu nyingine ni juhudi hafifu za uratibu, kushindwa kuzingatia vyema shughuli muhimu na udhibiti wa usalama wakati wa uundaji wa mifumo na ufanyaji hafifu wa majaribio ya utendaji kazi wa mifumo.

Katika kuzifanyia kazi dosari zilizobainika katika ukaguzi huo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo yafuatayo kwenye Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (a) Kuweka utaratibu mzuri wa kulazimisha taasisi za Serikali kufuata viwango na miongozo ya Mtandao wa Serikali.
- (b) Kuongeza uelewa kwa maafisa wa uhasibu na uongozi wa taasisi za Serikali juu ya hatari zinazohusiana na matumizi ya TEHAMA.

- (c) Kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa mapungufu yaliyobainishwa kuhusu ujumuishaji wa mfumo ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji mzuri wenye manufaa na kuleta tija kwa taasisi binafsi pamoja na Serikali kwa ujumla.
- (d) Kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mkakati wa usalama wa mtandao wa Serikali.

Hata hivyo, Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo yake kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuyazingatia kwa makini mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuleta maboresho katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama ifuatavyo:-

- i. Kutoa maagizo kwa wakuu wa taasisi za umma juu ya kuyafanyia kazi kwa kina na kwa uweledi mkubwa matokeo ya ukaguzi yanayotolewa kutokana na ripoti za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kutekeleza mifumo ya usimamizi wa fedha za Serikali kufanya kazi kwa ufanisi na hatimae kuleta ufanisi unaokusudiwa kupatikana.
- ii. Kuandaa mpango wa kina juu ya kuratibu utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha kwa taasisi zote za Serikali na kuhakikisha mifumo inayotekelezwa inaweza kuunganishwa/kujumuishwa na Mfumo Mkuu wa Serikali (IFMIS) kwa lengo la kuweka uwazi wa makusanyo yote pamoja na matumizi yanayofanyika kwa lengo la kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu za miamala ya fedha kwa lengo la kupatikanwa kwa usuluhisho wa miamala hiyo kwa wepesi na kwa usahihi jambo ambalo litapelekea kurahisisha utayarishaji wa hesabu jumuisho ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- iii. Kuandaa ramani ya kina (dira) ya kukamilisha utekelezaji wa mfumo wa utambuzi wa mali za kudumu "Asset Management System" ili kurahisisha utambuzi wa mali zote za kudumu za Serikali zilizopo, zilizouzwa, zilizo haribika pamoja na kuweza kuzielewa mahali zilipo na hali ya uchakavu wake ulivyo na Thamani halisi ya fedha iliyotumika kununua mali hiyo, jambo hilo litaisaidia kuzuia viashiria vya upotevu wa mali za umma unaotokana na kuhamishwa kwa mali hizo au kuazimwa kutoka sehemu moja ya taasisi kwenda sehemu nyengine na hatimae kuingia kwenye mikono ya watu wasiokuwa na uadilifu na maadili mema ya kazi kwa kuamua kuziua/kuuziana kwa bei nafuu au kuzifanyia hujuma mali hizo na kuitia hasara Serikali.

Kutokufanya kazi kikamilifu kwa mfumo wa Asset Management System kunapeleka kujitokeza kwa changamoto kubwa kwa Serikali kushindwa kufahamu mali mpya zinazonunuliwa na taasisi za umma pamoja na zile chakavu zinazouzwa jambo ambalo linaleta wakati mgumu kwa Serikali kufunga hesabu ikionesha wingi wa mali walizonazo ambazo haziwezi kuonekana kwa macho unapo zifuatilia na kupelekea kujitokeza kwa baadhi ya taasisi kupata hati zisizoridhisha kwa kuonesha kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na Uwepo wa mali za kudumu ambazo hazionekani kwa macho.

Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapenda kutoa ushauri kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inakamilisha maeneo yote muhimu ya vipengele vinavyotakiwa kuwepo katika mfumo huo na hasa ukizingatia fedha yote iliyotakiwa kutumika kwa uanzishwaji wa mfumo huo imeshalipwa kwa mzabuni wa utengenezaji wa mfumo bila ya kazi iliyotarajiwa

kukamilika ikiwemo kuunganishwa kwa mifumo yote ya "fixed asset" kwa taasisi za umma ili kupatikana uwiyo na usahihi wa mali zinazonunuliwa kuweza kuingizwa kwenye mfumo kama ni mali mpya pamoja na Thamani yake halisi iliyo tumika kununulia pamoja na kuondoa taarifa za mali zote zilizo uzwa na kuondolewa kwenye kumbukumbu za vitabu vya Serikali.

iv. Kuandaa na kuhifadhi hesabu ya mifumo yote katika taasisi za Serikali na thamani zake.

Moja katika changamoto iliyobainika katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kuandaliwa kimakosa kwa Hesabu Jumuishi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuliko sababishwa na kukosekana kwa hesabu sahihi za miamala ya fedha zilizokusanywa na zilizotumika kwa taasisi za umma kwa kukosekana kwa mifumo imara iliyo unganishwa kwa pamoja na kutoa taarifa zenye ukweli na usahihi kwa Serikali jambo ambalo lilijitokeza kubainika upotevu wa taarifa kunakotokana na kutokusuluhishwa kwa miamala ya fedha za umma kwa muda mrefu ambapo baadhi ya miamala ya fedha kutokujuulikana uhalisia wake na kujitokeza kutolewa ripoti isiyo sahihi kwa baadhi ya taasisi za umma.

v. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ni vyema kulinganisha au kuuwianisha mifumo yake na mifumo ya taasisi nyengine ili kuepuka kuwa na mifumo mingi inayofanya kazi za aina moja jambo ambalo linapelekea Serikali kufanya matumizi makubwa ya fedha za umma kusikokua na tija.

Ofisi ya Mdhubi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapendekeza kwa viongozi wakuu wa taasisi za umma kufanya mawailiano ya mara kwa mara na Wakala wa Serikali mtandao pale wanapotaka kuanzisha au kufanya maboresho ya mifumo yao kwa lengo la kupata ushauri wa kiufundi na kitaalamu zaidi kwa lengo la kuipunguzia Serikali kuingia gharama kubwa ya matumizi yasiyo na tija, hata hivyo ni vyema kufahamu ya kwamba Serikali imetoa jukumu la kuhakikisha mifumo yote inakuwa imara na kufanya kazi vizuri kwa lengo la kuweza kufikia makusudio ya Serikali kuanzisha matumizi ya mifumo Serikalini ili kupunguza upotevu mkubwa wa fedha za umma unaotokea kunakosababishwa na kila taasisi kuwa na sera yake ya uwekaji wa mifumo ya TEHAMA.

Ni matumaini ya Ofisi ya Mdhubi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba dosari zilizobainika zitafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria, miongozo ya Taasisi na Serikali pamoja na viwango vya kimataifa ili kuongeza udhibiti na usalama katika usimamizi wa taarifa zilizomo ndani ya Mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za Serikali.

SURA YA KWANZA

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

1.0 UTANGULIZI

Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma zilizopo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika shughuli zao kwa kutambua faida za mifumo katika kufikia malengo ya Taasisi hizo kwa wakati na kwa gharama nafuu. Matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika sekta za Umma yameongeza ufanisi katika shughuli za taasisi za umma na pia kuongeza changamoto mpya zinazohitaji usimamizi Madhubuti. Hii inapelekea umuhimu wa kufanya ukaguzi wa udhibiti katika usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha uendelevu, utengemavu na usalama wa mifumo.

Ukaguzi wa mifumo unatathmini umadhubuti wa usimamizi wa TEHAMA, uthibiti mifumo, udhibiti wa jumla wa TEHAMA, na udhibiti wa usalama wa taarifa zinazochakatwa na mifumo . Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 ulikua na malengo yafuatayo.

- Kuhakikisha kufuatwa kwa sheria kanuni na taratibu za Serikali Mtandao ili kuhakikisha utoaji wa huduma za TEHAMA zenye tija kwa mujibu wa sera, dira na mpango mkakati pamoja na miongozo mbali mbali ya kimataifa yenye mpangilio , udhibiti wa majanga, udhibiti na usalama wa taarifa katika mifumo na miundo mbinu ya ndani.
- Kupima umadhubuti wa uhakika wa taarifa kutoka kwenye mifumo ya taarifa ambayo ina athari katika taarifa za fedha za taasisi husika.
- Kuangalia kama mapungufu katika utumiaji na usimamizi wa mifumo, na kupata uhakika wa mifumo katika upatikanaji pindi inapohitajika, na usahihi na usiri wa taarifa.

Taarifa hii ya jumla inatoa muhtasari wa maoni makuu ya kiukaguzi kutoka katika taasisi kumi (10) ambazo ukaguzi wa mifumo umefanyika na taarifa za ukaguzi kuwasilishwa kwa taasisi husika.

1.1 MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria Nambari 11 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2003 kinatoa haki kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuweza kujiridhisha kwamba kunakuwepo na udhibiti katika matumizi ya mifumo ya tehama katika shughuli mbali mbali za Taasisi za umma ikiwemo ukusanyaji wa fedha ambao unazingatia maslahi ya umma na matumizi ya fedha hizo yanaidhinishwa kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu ili kuhakikisha fedha za umma zinatunika kama ilivyokusudiwa.

Katika kutekeleza wajibu huu ni lazima Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina wa mifumo ya TEHAMA ili kupima kama inafanya kazi kwa ufanisi na kuimarisha usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani yake.

Aidha ni jukumu la Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuangalia usimamizi wa uendeshaji wa mifumo ili kujiridhisha kama inatumika kwa usahihi katika kuhakikisha taasisi za umma zinafikia malengo yaliyojiwekea.

1.2 WIGO NA MADHUMUNI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

Katika mwaka ya fedha 2020/2021 ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA uliofanyika uliangazia zaidi udhibiti wa mifumo ya taarifa za Usimamizi wa TEHAMA, usimamizi wa miradi ya utengenezaji na usimikaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa jumla wa TEHAMA, pia nilitumia taratibu nyengine za kiukaguzi ambazo zilikua muhimu katika kutoa maoni ya kiukaguzi ambapo wakaguzi walifanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia athari za majanga yaani "risk based audit", hivyo basi matokeo ya ukaguzi yanatokana na Kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi ziliwasilishwa kwa usahihi na kwa wakati kwa lengo la kuweza kufanyiwa kazi na wakaguzi wa mifumo.

1.3 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA

Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI) na Shirikisho la Taasisi Kuu za Ukaguzi Barani Afrika zinazo zungumza Lugha ya Kingereza (AFROSAI-E). Ushiriki huo unapatikanwa kwa nafasi ya ushiriki wa NAOT kwa niaba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ukaguzi uliofanyika umezingatia matakwa ya kimaadili katika kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata uhakika wa kutosha juu ya udhibiti na ufanisi wa mifumo ya TEHAMA. Kwa madhumuni hayo ukaguzi huo ulikua ni kwa mujibu wa Muongozo wa Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA wa AFROSAI-E wa mwaka 2017, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, Miongozo ya Serikali Mtandao ya mwaka 2021, Sera ya TEHAMA ya Serikali ya mwaka 2012 pamoja na miongozo ya Kimataifa kama COBIT-5 na ISO/IEC , ISACA n.k

1.4 UDHIBITI WA USALAMA WA MTANDAO

Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya tathmini ya udhibiti wa usalama wa kimtandao katika taasisi za Serikali ambapo mambo mbali mbali yalibainika ikiwemo kujitokeza kwa visa vya mashambulizi ya "Ransomware" katika taasisi za umma, Programu haribifu (malware) zilificha majalada ya mfumo na majalada ya watumiaji katika seva za mfumo. Kutokana na Uwepo wa dosari hiyo ilisababisha upotezaji wa taarifa na kutopatikana kwa mifumo.

Aidha, ilibainika baadhi ya taasisi za Serikali hazina mfumo wa utoaji wa mafunzo kwa watendaji wake na baadhi yao hawafanyi mafunzo ya ufahamu wa usalama wa TEHAMA kwa wafanyakazi wao. Mafunzo ya ufahamu wa usalama wa TEHAMA ni muhimu katika kuongeza uelewa wa wafanyakazi juu ya maswala ya usalama wa mtandao. Pia, yanaweza kusaidia kulinda taasisi dhidi ya shambulio la kimtandao, kwani Kukosekana kwa mafunzo kunaweza kukapelekea kujitokeza

kwa changamoto ya uharibifu mkubwa wa mifumo ya Teknolojia ya TEHEMA basi na kuwa na uwelewa wa kufanya marekebisho ya haraka ya kuweza kuulinda na kuukinga mfumo kufikwa na majanga ya mashambulio. Hata hivyo, imebainika baadhi ya taasisi za umma hazina maafisa usalama wa TEHAMA na baadhi ya taasisi nyengine maafisa hao hawana taaluma ya kutosha katika utekelezaji wa majuku yao kwa mujibu wa viwango na sera za TEHAMA zinavyo elekeza.

1.5 UTENGENEZAJI NA UDUMISHAJI WA MIFUMO

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya ukaguzi wa awali wa kutaka kutambua mbinu zinazotumika kwa taasisi za umma juu ya michakato ya Ununuzi inayofanyika kupitia mifumo ya TEHAMA kwa taasisi kubwa kubwa pamoja na kupima maendeleo, na udumishaji wa mifumo katika taasisi za umma ili kuangalia kama mwongozo wa Serikali wa utengenezaji wa mifumo, upatikanaji, uendesaji na udumishaji wa mifumo unafuatwa kwa mujibu wa sheria na miongozo mbali mbali iliyopo.

Ukaguzi umebaini ya kwamba baadhi ya taasisi hazikufanya majaribio ya utendaji kazi wa mifumo iliyotengenezwa kwa watumiaji wa mifumo hiyo na kupelekea kujitokeza kwa baadhi ya changamoto zifuatazo:-

- Ukosefu wa nyaraka za kutosha za mradi, kutofuatilia gharama za kutengeneza mifumo ambazo zinajumuisha thamani ya mfumo, pamoja na ukosefu wa uratibu katika kusimamia upatikanaji na utengenezaji wa mifumo.

Katika kukagua upatikanaji, utengenezaji, na udumishaji wa mifumo, ukaguzi ulifanya tathmini ya ufanisi na urahisi wa mifumo. Ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali ambazo zilipelekea kujitokeza kwa madhaifu makubwa katika kiwango cha uunganishaji (integration) kati ya mifumo mikubwa ya Serikali (kama vile mfumo wa usimamizi wa fedha za mapato na matumizi (IFMIS) , mfumo wa Ukusanyaji wa taarifa za Mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum (MUTM), Mfumo wa Ukusanyaji wa mapato ya Maegesho (SLOTTEX ZANZIBAR - ECONEX) pamoja na mifumo mengineyo.

- Ukaguzi umebaini matumizi duni ya mifumo kwa watendaji wa umma kunakosababishwa na kutokua na uweledi na ujuzi wa matumizi ya mifumo jambo ambalo linalopelekea kutotumia mifumo ipasavyo kwa kiwango kinachohitajika.
- Ukaguzi umebaini kujitokeza kwa uwepo wa mifumo mingi inayotumika katika taasisi za umma ambayo inafanya kazi sawa au kazi zinazofanana jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha za umma na hatimae Kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.
- Kutokukamilika kwa baadhi ya vipengele muhimu vya utengenezaji wa mifumo kwa wakati jambo ambalo linapelekea baadhi ya taasisi za umma kufanya malipo ya fedha zote kwa wazabuni wanaotengeneza mifumo hiyo bila ya kuzingatia mahitajio ya matumizi ya mifumo hiyo jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa hasara kubwa kwa Serikali pale ambapo itakapo fanya maamuzi ya kuongeza baadhi ya "module" mpya katika mfumo.

Kutokuzingatiwa kwa vipelengele muhimu vya ukamilishaji wa utengenezaji wa mfumo kunapelekea Serikali kutumia gharama kubwa ya fedha kwa kutengeneza mkataba wa ziada (addendum) na kujitokeza kulipa gharama zaidi ya mkataba wa awali jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inawashauri maafisa TEHAMA kuwa Wazalendo na wenye uweledi mkubwa katika kusimamia mifumo ya Serikali kwa lengo la kudhibiti upotevu mkubwa wa fedha za umma zinazotokana na Uwepo wa manunuzi hewa ya vifaa vya TEHAMA, kufanya manunuzi yasiyo zingatia ushindani wa bei, pamoja na kutokuzingatia kwa Sera zinazowekwa katika utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA ambapo kutokuzingatiwa kwa Sera za Serikali za TEHAMA kunapelekea Serikali kuingia hasara kutokana na kupoteza fedha kubwa zinazofanyiwa ubadhirifu kupitia mifumo ya kieletroniki.

1.6 UDHIBITI WA UJUMLA WA TEKNOLOJIA YA HABARI

Tathmini ya udhibiti wa jumla wa TEHAMA ilibaini mapungufu katika ulinganifu baina ya malengo ya TEHAMA na malengo ya mkakati ya Wizara, Mashirika ya umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum, juu ya usimamizi bora wa rasilimali na mwendelezo wa huduma na mipango ya kurejesha huduma baada ya majanga kutokea. Mengine ni ukiukaji wa mgawanyo wa majukumu kwa kazi za TEHAMA, udhibiti wa usimamizi wa mabadiliko katika mfumo, usimamizi usio mzuri wa wazabuni wa TEHAMA, utoaji hafifu wa huduma ya TEHAMA, pamoja na usimamizi wa matukio yasiyotarajiwa.

Katika kufanyika kwa tathmini ya utawala na usimamizi wa TEHAMA ukaguzi ulibaini udhaifu katika upangaji mkakati na sera za TEHAMA, mfumo wa uongozi wa TEHAMA na muundo wake wa kuripoti, uundaji na utendeshaji kazi wa kamati za uendeshaji za TEHAMA na usimamizi wa hatari zinazoweza kuikumba TEHAMA.

Aidha, ukaguzi umebaini katika kipengele cha huduma endelevu na mpango wa kurejesha huduma baada ya majanga kutokea ilibainika kutokuwapo kwa Mpango wa Huduma Endelevu (BCP) kwa baadhi ya taasisi za umma na Mpango wa Kurejesha Huduma Baada ya Majanga kutokea (DRP), jambo ambalo linasababishwa na ukosefu wa mafunzo ya kutosha kwa timu za BCP na DRP, na kujitokeza kwa dosari ya ukosefu wa majaribio ya vipindi tofauti ya BCP na DRP kwa kuzipitia mara kwa mara na kuziboresha.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwa baadhi ya taasisi za umma kutokuwapo kwa eneo mbadala la mbali kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za mifumo, ukosefu wa nyaraka za taratibu za kuhifadhi taarifa za mifumo (backup), pamoja na jinsi ya kurejesha taarifa hizo kwenye mfumo pale inapohitajika.

Katika mgawanyo wa majukumu kwa kazi za TEHAMA ukaguzi ulibaini kwa taasisi nyingi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hakukuwa na mgawanyo wa majukumu kati ya mtengenezaji wa mfumo na msimamizi wa kanzidata, msimamizi wa mfumo na msimamizi wa kanzidata, na msimamizi wa mtandao na msimamizi wa kanzidata.

Baada ya kubainika kwa dosari hizo ukaguzi ulijikita zaidi katika ukaguzi wa kupima ufanisi wa udhibiti wa mabadiliko yanayotakiwa kufanyika katika mfumo na kubainika uwepo wa ukosefu

wa nyaraka za taratibu za usimamizi wa mabadiliko ya mifumo, kutofuata utaratibu au sera za usimamizi wa kubadilisha vipengele vya utendaji kazi vya mifumo, na kutotenganisha mazingira/miundombinu kwa ajili ya kutengeneza, kufanya majaribio na kusimika mifumo "Electronic system Installation".

1.7 USIMAMIZI WA WATOA HUDUMA WA TEHAMA, UTOAJI WA HUDUMA ZA TEHAMA NA USIMAMIZI WA MATUKIO

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulijikita kukagua usimamizi wa watoa huduma wa TEHAMA, utoaji wa huduma za TEHAMA na usimamizi wa matukio yasiyotarajiwa. Katika kadhia hiyo mambo mbali mbali yaliweza kubainika kwa baadhi ya taasisi, mashirika pamoja na Serikali za Mitaa na kubainika ya kwamba baadhi ya taasisi hizo hazina Mkataba wa Kiwango cha Huduma (SLA) na watoa huduma, ukosefu wa taratibu za utatuaji wa matukio ya TEHAMA, na ukosefu wa Mkataba wa Kiwango cha Utendaji (OLA) kati ya idara ya TEHAMA na uongozi au watumiaji wa miundombinu ya TEHAMA. OLA huweka misingi ya kupima kiwango cha utoaji wa huduma za TEHAMA kama vile utendajikazi wa miundombinu, msaada kwa watumiaji wa mwisho wa miundombinu ya TEHAMA na upatikanaji wa mifumo kulingana na matokeo ya ukaguzi.

Aidha, katika ukaguzi uliofanyika imebainika mapungufu mengi yaliyobainishwa hapo juu ya usimamizi wa shughuli za TEHAMA katika taasisi za Serikali yalitokana na kutofuatwa kwa viwango na miongozo ya mtandao wa Serikali, kutokufuatwa kwa miongozo iliyopangwa na kutolewa na E-Gov kwa taasisi za umma katika kusimamia uwajibikaji wa mifumo ya Serikali kunasababishwa na msukumo hafifu wa kuhakikisha taasisi za Serikali zinazingatia viwango na miongozo ya Serikali, uelewa mdogo wa hatari zinazopelekewa na matumizi ya TEHAMA kwa menejimenti, na ukosefu wa mapitio ya mara kwa mara ya udhibiti wa ndani wa TEHAMA. Sababu nyingine ni juhudi hafifu za uratibu, kushindwa kuzingatia vyema shughuli muhimu na udhibiti wa usalama wakati wa uundaji wa mifumo na ufanyaji hafifu wa majaribio ya utendaji kazi wa mifumo.

Katika kuzifanyia kazi changamoto zilizobainika katika ukaguzi huo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo yafuatayo kwenye Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (a) Kuweka utaratibu mzuri wa kulazimisha taasisi za Serikali kufuata viwango na miongozo ya Mtandao wa Serikali.
- (b) Kuongeza uelewa kwa maafisa wa uhasibu na uongozi wa taasisi za Serikali juu ya hatari zinazohusiana na matumizi ya TEHAMA.
- (c) Kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa mapungufu yaliyobainishwa kuhusu ujumuishaji wa mfumo ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji mzuri wenye manufaa na kuleta tija kwa taasisi binafsi pamoja na Serikali kwa ujumla.
- (d) Kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mkakati wa usalama wa mtandao wa Serikali.

Hata hivyo, Ofisi ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo yake kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuyazingatia kwa makini mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuleta maboresho katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama ifuatavyo:-

- i. Kutoa maagizo kwa wakuu wa taasisi za umma juu ya kuyafanyia kazi kwa kina na kwa uweledi mkubwa matokeo ya ukaguzi yanayotolewa kutokana na ripoti za Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kutekeleza mifumo ya usimamizi wa fedha za Serikali kufanya kazi kwa ufanisi na hatimae kuleta ufanisi unaokusudiwa kupatikana.

Hata hivyo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ina jukumu kubwa la kuzijuulisha taasisi za Serikali juu ya kuwa tayari kufanya mabadiliko ya haraka na kufanya maboresho ya mifumo ya uhasibu na kuachana na kufanya miamala ya fedha kwa kununua au kulipa kwa kutumia njia ya fedha taslimu nje ya mifumo jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kunakotokana na Kukosekana kwa malipo ya tozo za kodi mbali mbali ambazo zingeisaidia Serikali kufikia malengo iliyojipangia ikiwemo kusogeza huduma muhimu kwa wananchi na kuwapunguzia kasi ya machungu ya maisha.

- ii. Kuandaa mpango wa kina juu ya kuratibu utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha kwa taasisi zote za Serikali na kuhakikisha mifumo inayotekelezwa inaweza kuunganishwa/kujumuishwa na Mfumo Mkuu wa Serikali (IFMIS) kwa lengo la kuweka uwazi wa makusanyo yote pamoja na matumizi yanayofanyika kwa lengo la kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu za miamala ya fedha kwa lengo la kupatikanwa kwa usuluhisho wa miamala hiyo kwa wepesi na kwa usahihi jambo ambalo litapelekea kurahisisha utayarishaji wa hesabu jumuisho ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- iii. Kuandaa ramani ya kina (dira) ya kukamilisha utekelezaji wa mfumo wa utambuzi wa mali za kudumu "Asset Management System" ili kurahisisha utambuzi wa mali zote za kudumu za Serikali zilizopo, zilizouzwa, zilizo haribika pamoja na kuweza kuzielewa mahali zilipo na hali ya uchakavu wake ulivyo na thamani halisi ya fedha iliyotumika kununua mali hiyo, jambo hilo litaisaidia kuzuia viashiria vya upotevu wa mali za umma unaotokana na kuhamishwa kwa mali hizo au kuazimwa kutoka sehemu moja ya taasisi kwenda sehemu nyengine na hatimae kuingia kwenye mikono ya watu wasiokuwa na uadilifu na maadili mema ya kazi kwa kuamua kuziuzua/kuuziana kwa bei nafuu au kuzifanyia hujuma mali hizo na kuitia hasara Serikali.

Kutokufanya kazi kikamilifu kwa mfumo wa Asset Management System kunapeleka kujitokeza kwa changamoto kubwa kwa Serikali kushindwa kufahamu mali mpya zinazonunuliwa na taasisi za umma pamoja na zile chakavu zinazouzwa jambo ambalo linaleta wakati mgumu kwa Serikali kufunga hesabu ikionesha wingi wa mali walizonazo ambazo haziwezi kuonekana kwa macho unapo zifuatilia na kupelekea kujitokeza kwa baadhi ya taasisi kupata hati zisizoridhisha kwa kuonesha kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na uwepo wa mali za kudumu ambazo hazionekani kwa macho.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapenda kutoa ushauri kwa Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango kuhakikisha inakamilisha maeneo yote muhimu ya vipengele vinavyotakiwa kuwepo katika mfumo huo na hasa ukizingatia fedha yote iliyotakiwa kutumika kwa uanzishwaji wa mfumo huo imeshalipwa kwa mzabuni wa utengenezaji wa mfumo bila ya kazi iliyotarajiwa kukamilika ikiwemo kuunganishwa kwa mifumo yote ya "fixed asset" kwa taasisi za umma ili kupatikana uwiyo na usahihi wa mali zinazonunuliwa kuweza kuingizwa kwenye mfumo kama ni mali mpya pamoja na thamani yake halisi iliyo tumika kununulia pamoja na kuondoa taarifa za mali zote zilizo uzwa na kuondolewa kwenye kumbukumbu za vitabu vya Serikali.

iv. Kuandaa na kuhifadhi hesabu ya mifumo yote katika taasisi za Serikali na thamani zake.

Moja katika changamoto iliyobainika katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kuandaliwa kimakosa kwa Hesabu Jumuishi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuliko sababishwa na kukosekana kwa hesabu sahihi za miamala ya fedha zilizokusanywa na zilizotumika kwa taasisi za umma kwa kukosekana kwa mifumo imara iliyo unganishwa kwa pamoja na kutoa taarifa zenye ukweli na usahihi kwa Serikali jambo ambalo lilijitokeza kubainika upotevu wa taarifa kunakotokana na kutokusuluhishwa kwa miamala ya fedha za umma kwa muda mrefu ambapo baadhi ya miamala ya fedha kutokujuulikana uhalisia wake na kujitokeza kutolewa ripoti isiy sahihi kwa baadhi ya taasisi za umma.

v. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ni vyema kulinganisha au kuuwianisha mifumo yake na mifumo ya taasisi nyengine ili kuepuka kuwa na mifumo mingi inayofanya kazi za aina moja jambo ambalo linapelekea Serikali kufanya matumizi makubwa ya fedha za umma kusikokua na tija.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapendekeza kwa viongozi wakuu wa taasisi za umma kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na Wakala wa Serikali mtandao pale wanapotaka kuanzisha au kufanya maboresho ya mifumo yao kwa lengo la kupata ushauri wa kiufundi na kitaalamu zaidi kwa lengo la kuipunguzia Serikali kuingia gharama kubwa ya matumizi yasiyo na tija, hata hivyo ni vyema kufahamu ya kwamba Serikali imetoa jukumu la kuhakikisha mifumo yote inakuwa imara na kufanya kazi vizuri kwa lengo la kuweza kufikia makusudio ya Serikali kuanzisha matumizi ya mifumo Serikalini ili kupunguza upotevu mkubwa wa fedha za umma unaotokea kunakosababishwa na kila taasisi kuwa na sera yake ya uwekaji wa mifumo ya TEHAMA.

SURA YA PILI

UKAGUZI WA MIFUMO YA BOHARI KUU YA DAWA

2.0 UTANGULIZI

Bohari Kuu ya Dawa (Central Medical Store) ni Taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya Zanzibar ambayo ina lengo la kusaidia kukuza mfumo wa utoaji wa huduma za dawa kwa kuhakikisha kwamba dawa muhimu zenye ubora unaotakiwa pamoja na vifaa tiba vinapatikana katika Vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na Hospitali za Rufaa ili kuweza kufikia mahitaji ya wananchi wa Zanzibar.

Kabla ya mwaka 2011 Bohari Kuu ya Dawa ilikuwa ni kitengo chini ya Mfamasia Mkuu. Katika kuiongeza uwezo kiutendaji, mnamo mwaka 2011 Bohari ilipewa mamlaka ya kuwa Idara na kukabidhiwa Maghala mawili ambayo kwa upande wa Unguja Ghala lipo Maruhubi na kwa upande wa Pemba Ghala lipo Vitongoji.

Bohari Kuu ya Dawa ina jukumu kubwa la kupokea, kuhifadhi na kusambaza dawa muhimu, vifaa tiba, vitendanishi, vifaa vya uchunguzi wa kimaabara na uchunguzi wa mionzi, pamoja na kutoa taarifa mbali mbali za matumizi ya dawa kwa ajili ya kusaidia Serikali katika kuwafikishia wananchi huduma bora za matibabu.

Kwa sasa, Bohari Kuu ya Dawa inatoa huduma ya kusambaza dawa na vifaa tiba kwa vituo zaidi ya 190 vya Serikali pamoja na Vikosi vya Ulinzi na Usalama.

2.1 MUUNDO WA IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA

Bohari Kuu ya Dawa inaongozwa na Mkurugenzi ambae anasaidiwa na Wakuu wa Divisheni na ina jumla ya Divisheni nne (4) kama zifuatazo:-

- a) Divisheni ya Huduma kwa Wateja.
- b) Divisheni ya Uthibiti wa Viwango (Quality Assurance).
- c) Divisheni ya Ununuzi na Usimamizi wa Mwenendo wa Dawa.
- d) Divisheni ya Utawala na Fedha.

2.2 KAZI ZA BOHARI KUU YA DAWA

Bohari Kuu ya Dawa ina majukumu yafuatayo:-

- i. Kupokea dawa na vifaa tiba vinavyonunuliwa na Serikali pamoja na Washirika mbali mbali wa maendeleo.
- ii. Kusimamia uhifadhi na utunzaji dawa na vifaa tiba.
- iii. Kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali zote za Unguja na Pemba.
- iv. Kusimamia mwenendo wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyote vya afya na Hospitali kwa Unguja na Pemba.

- v. Kutoa mafunzo na miongozo mbali mbali juu ya uhifadhi na utunzaji wa dawa na vifaa tiba kwa wafamasia wa Wilaya na Watunza dawa katika vituo vya afya na hospitali.

2.3 MIFUMO YA TEHAMA INAYOTUMIKA BOHARI KUU YA DAWA

Bohari Kuu ya Dawa awali ilikuwa inafanya kazi zake za kutunza taarifa za dawa na vifaa tiba bila ya kutumia mifumo ya TEHAMA ambapo taarifa zilikuwa zinarikodiwa kwenye madaftari ya ghalani (store ledgers) kwa njia ya mkono "manually". Miongoni mwa taarifa hizo zilizokuwa zikirekodiwa ni taarifa za mahitaji ya dawa na vifaa tiba, taarifa za uagizaji wa dawa, upokeaji wa dawa na vifaa tiba, utunzaji na usambazwaji wa dawa na vifaa tiba.

Kuanzia mwaka 2011 Wizara ya Afya ilipata Msaada kwa wataalamu kutoka Shirika la Misaada la Marekani "USAID" na Shirika la Misaada la Denmark "DANIDA" ndipo mifumo ya TEHAMA ilipoanzishwa kupitia Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya kuimarisha huduma za uagizaji, upokeaji, uhifadhi, usambazaji pamoja na usimamizi wa dawa na vifaa tiba na kuanza rasmi mnamo mwaka 2013.

Mifumo hiyo inajulikana kama ifuatavyo:-

- i. Mfumo wa mSupply.
- ii. Mfumo wa Money Works.
- iii. Mfumo wa Electronic Logistics Management Information System Central Edition (eLMIS - CE).
- iv. Mfumo wa Electronic Logistics Management Information System Facility Edition (eLMIS - FE).

2.3.1 Mfumo wa mSupply

Mfumo wa mSupply ni mfumo mkuu wa TEHAMA uliopo Bohari Kuu ya Dawa ambao umetengenezwa na kampuni ya Sustainable Solution (SUSOL) kutoka nchini New Zealand. Mfumo huu ni wa ndani (Local Based System) na hutumika kwa ajili ya utunzaji na usimamizi wa taarifa za dawa na vifaa tiba zinazoingizwa ndani ya Bohari na kusambazwa katika vituo vya Afya pamoja na Hospitali za Unguja na Pemba.

Mfumo huo umeanzishwa rasmi mwaka 2013 kupitia fedha za mkopo kutoka kwa Shirika la Misaada la Marekani "USAID" pamoja na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark "DANIDA".

Mkataba wa awali wa ununuzi wa mfumo huo uliosainiwa mwaka 2013 ambao umebainisha vipengele vya makubaliano baina ya Wizara ya Afya na Kampuni ya SUSOL haukupatikana kwa ajili ya ukaguzi. Kutopatikana kwa mkataba halisi kumepelekea ukaguzi kushindwa kujua gharama kamili, muda wa utekelezaji, mahitaji, upeo wa kazi, tija na ufanisi wa kazi husika.

Hata hivyo, gharama za awali za ununuzi na matumizi ya mfumo huo zililipwa na Shirika la USAID. Kuanzia mwaka 2020 Bohari Kuu ya Dawa yenyewe iliingia mkataba wa miaka mitatu (2020 -2023) na Kampuni ya SUSOL na kukubaliana kuendelea kulipa gharama zenye jumla ya **Dola za Marekani Elfu Nane na Themanini na Tatu nukta Mbili Nne (USD 8,083.24)** kila

mwaka kwa ajili ya kupata leseni ya matumizi ya mifumo na msaada wa kiufundi (support and annual license fees) ambapo mifumo hiyo ni Mfumo wa mSupply, Mfumo wa Money Works pamoja na Mfumo wa eLMIS Central Edition.

Mkataba huo ni wa miaka mitatu na ulisainiwa tarehe 1 Julai 2020. Mchanganuo wa gharama za leseni ya matumizi ya mfumo na msaada wa kiufundi zilizoainishwa kwenye mkataba ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1**.

2.3.2 Mfumo wa Money Works

Mfumo wa Money Works ni mfumo wa mahesabu ambao umetengenezwa na Kampuni ya SUSOL. Mfumo huu ulianza kazi mwaka 2013 sambamba na mfumo wa mSupply ambapo madhumuni yake yalikuwa ni kuhifadhi na kuthibitisha taarifa za fedha kupitia ankara za malipo (invoices) zinazotolewa na mfumo wa mSupply. Aidha mfumo huu ulikuwa na lengo la kutumika katika kitengo cha Wahasibu wa Bohari na kiuhalisia ulitumiwa kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu tu (2013-2016) ambapo kuanzia mwaka 2016 hadi sasa mfumo huu haujatumiwa tena.

Licha ya kwamba mfumo huo haujatumiwa tena tangu mwaka 2016 lakini Bohari Kuu ya Dawa hadi sasa bado inaendelea kulipia gharama za leseni ya matumizi ya mfumo huo na huduma ya msaada wa kiufundi zenye jumla ya **USD 431.49** kila mwaka ambapo mkataba wa mwisho uliosainiwa baina ya Kampuni ya SUSOL na Bohari Kuu ya Dawa ni tarehe 01 Julai 2020 wenye muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2020 hadi 2023. Mchanganuo wa gharama hizo ni kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1**.

2.3.3 Mfumo wa Electronic Logistics Management Information System Central Edition (eLMIS - CE)

Electronic Logistic Management Information System Central Edition (eLMIS-CE) ni mfumo wa TEHAMA uliotengenezwa na kampuni ya SUSOL mnamo mwaka 2016 kupitia fedha za mkopo kutoka kwa wahisani wa maendeleo "USAID na DANIDA". Mfumo huo ulitengenezwa baada ya mifumo miwili kutengenezwa ambayo ni mfumo wa mSupply na mfumo wa Money Works na hadi sasa mfumo huu unafanyakazi pamoja na mfumo mkuu wa mSupply uliopo Bohari Kuu ya Dawa.

Mfumo wa eLMIS Central Edition umetengenezwa ili utumike katika vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za Mkoa na hospitali za Rufaa, ambapo mfumo huo unatumia huduma ya Internet katika kufanya kazi kutokana na uhalisia wake "Web Based System".

Aidha mfumo huo hutumika katika vituo vya afya na hospitali kwa ajili ya kuomba na kuripoti (Request and Report) taarifa za dawa na vifaa tiba zinazohitajika ndani ya Vituo vya Afya na hospitali kutoka Bohari Kuu ya Dawa (Central Medical Store).

Baada ya kukamilika kwa taratibu za kuomba na kuripoti mahitaji ya dawa na vifaa tiba, taarifa hizo huingizwa katika mfumo wa mSupply wa Bohari Kuu kwa ajili ya kumaliza taratibu za maombi ya kituo husika.

Hata hivyo, mkataba wa awali wa utekelezaji wa mfumo huo wenye kubainisha gharama, muda, mahitaji ya Wizara ya Afya, upeo wa kazi (scope of work), malengo na matokeo (objectives and deliverables) haukupatikana kwa ukaguzi.

Kutokupatikana kwa mkataba huo kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha thamani halisi ya fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa mfumo huo pamoja na mahitaji ya utekelezaji wake.

Hata hivyo kupitia mkataba wa leseni za matumizi na huduma za msaada wa kiufundi uliosainiwa tarehe 1 Julai 2020 ukaguzi umebaini Bohari Kuu ya Dawa inaendelea kulipia gharama za msaada wa kiufundi "support & maintenance" zenye jumla ya **Dola za Marekani Mia Saba na Tano nukta nane Tisa (USD 705.89)** ambapo gharama hizo zinaendelea kulipiwa kwa muda wa miaka mitatu na kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2023 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1.**

2.3.4 Mfumo wa Electronic Logistics Management Information System Facility Edition (eLMIS - FE)

Mfumo wa Electronic Logistic Management Information System Facility Edition (eLMIS-FE) ni mfumo mpya wa TEHAMA uliotengenezwa na Mshauri Elekezi ambao ni kampuni ya **John Snow Inc (JSI)** iliyopo Marekani mnamo mwaka 2018.

Mfumo huo umetengenezwa kwa gharama za **Dola za Marekani Hamsini na Saba Elfu Mia Tisa Ishirini na Moja (USD 57,921) bila ya VAT** sawa na **shilingi Milioni Mia Moja Ishirini na Tisa Laki Moja Sitini na Tatu Mia Nne Themanini na Nane (TZS 129,163,488)** ambapo gharama hizo zimepatikana kupitia Mkataba uliosainiwa tarehe 09-07-2018 baina ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Kampuni ya JSI. **Kiambatisho Nambari 2(A) Kinahusika.**

Fedha hizo ikiwa ni msaada kwa Serikali kutoka kwa Mfuko wa Fedha wa Dunia (The Global Fund) wenye lengo la kuimarisha mfumo kwa kutoa huduma mbali mbali za afya kama vile usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na Hospitali.

Aidha Mfumo huo wa eLMIS Facility Edition umekuwa na gharama za ziada ambazo ni gharama za msaada wa kiufundi "Support and Maintenance" zenye jumla ya **Dola za Marekani Ishirini na Tisa Elfu Mia Tano Ishirini na Moja (USD 29,521)**. Gharama hizo zimeongezeka kutokana na makubaliano kupitia mkataba wa ziada uliosainiwa tarehe 12-11-2020 baina ya Wizara ya Afya na Mshauri Elekezi – JSI. **Kiambatisho Nambari 2(B) Kinahusika.**

Kwa ujumla Mfumo wa eLMIS Facility Edition umeiharimu Serikali kwa mwaka wa kwanza **Dola za Marekani Elfu Themanini na Saba Mia Nne Arobaini na Mbili (USD 87,442)**.

Mfumo huu umetengenezwa ili kutatua dosari mbali mbali zilizopo katika Mfumo wa zamani wa eLMIS Central Edition. Aidha mfumo huu umekuwa na lengo la kuongeza uwezo wa kuingiza na kutunza taarifa za wangujwa kuanzia wanapoingia hospitalini au kwenye kituo cha Afya (registration of patients), kumuona Daktari, kupata Vipimo na Kupewa dawa katika maeneo mbali mbali (dispensing areas) kama vile Famasi, Wodini na Maabara n.k.

Aidha mfumo huu ulikuwa na lengo la kuimarisha ubora wa taarifa (data quality) na uonekano wa taarifa (data visibility), uwezo wa kuomba na kutoa taarifa za dawa na vifaa tiba (Report and Request) ambapo huduma hizo hazipatikani kwenye mfumo wa mwanzo wa eLMIS Central Edition.

Hadi sasa mfumo huu wa (eLMIS – FE) unatumika katika hospitali mbili kwa upande wa Unguja ambazo ni Hospitali ya Kivunge iliyoanza kuutumia kuanzia mwezi wa Januari 2021 na Hospitali ya Makunduchi iliyoanza kuutumia kuanzia mwezi wa Februari 2021, kwa upande wa Pemba mfumo huu unatumika katika hospitali ya Wilaya ya Wete pekee kuanzia mwezi wa Juni 2021.

2.3.5 Dhamira ya Utekelezaji wa Mfumo wa eLMIS - FE

Utekelezaji wa mfumo wa eLMIS - FE umetakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- i. Kuondokana na matumizi ya madaftari ya kutunzia kumbukumbu za kutolea dawa na vifaa tiba (daily dispensing register) kwenye hospitali na vituo vya afya na madaftari ya kutunza kumbukumbu za stoo (store ledger).
- ii. Hospitali kubwa kutumia mfumo kwenye Famasi , Wodi, Maabara na kuunganishwa na Famasi kuu.
- iii. Kuunganisha mfumo wa eLMIS - FE na eLMIS - CE kwa ajili ya kupata taarifa za Ripoti na Maombi (Report and Requisition) ya dawa na vifaa tiba kutoka katika vituo vya afya hospitali kwenda Bohari Kuu ya dawa.
- iv. Wizara ya Afya Kupata taarifa za kila wakati (real time data) za vituo vya Afya.
- v. Ripoti na Maombi (Report and Requisition) ya dawa na vifaa tiba zijazwe kwenye mfumo wa eLMIS - FE ambao umeunganishwa na eLMIS - CE.

2.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

2.4.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa Mifumo ya Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa tiba mambo yafuatayo yamebainika:-

2.4.1.1 Kuwepo kwa Idadi ndogo ya watumiaji wa Mfumo wa mSupply

Ukaguzi umebaini kupitia mfumo wa mSupply Bohari Kuu ya Dawa imeweka jumla ya watumiaji (system users) wanane (8) ambapo idadi hiyo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji na kazi zinazofanyika ndani ya mfumo za kushughulikia taarifa za upokeaji wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba , uhifadhi wa dawa unaojumuisha kuhesabu (physical counting), kushughulikia taarifa za maombi kutoka vituo zaidi ya 190, Hospitali za Mikoa na Wilaya, na Hospitali za Rufaa na kuandaa taarifa za dawa na vifaa tiba kwa ajili ya usambazaji kwenye vituo vya afya na Hospitali zote Unguja na Pemba.

Aidha, ukaguzi umebaini kua uhaba huu wa watumiaji wa mfumo wa mSupply umechangiwa kutokana na kuwepo kwa uchache wa leseni za watumiaji wa mfumo (user licences) ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa leseni nane zinazotumika kwenye mfumo wa mSupply kwa wakati mmoja kwa wafanyakazi wa Bohari Kuu ya Dawa waliopo Unguja na Pemba.

Hali hii inaweza kuondoa ufanisi wa kazi na kupelekea kutokea kwa ucheleweshaji wa kusambazwa dawa na vifaa tiba kwa wakati katika vituo vya afya na hospitali jambo linaloweza kusababisha uhaba katika mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na hatimae kutokea ongezeko la maradhi na vifo kwa wakati mmoja kwa wagonjwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuongeza leseni za watumiaji wa mfumo wa mSupply kwa kuwapa ruhusa ya kufanya kazi kwenye mfumo (user licenses and access) kwa kiwango kikubwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwemo kurahisisha upatikanaji wa huduma za usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na Hospitali zote kwa wakati mmoja.

2.4.1.2 Dosari katika Usimamizi na Mgawanyo wa majukumu ya kazi za mfumo wa mSupply (SoD).

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika usimamizi na mgawanyo wa majukumu ya kazi zinazofanywa kwenye mfumo (separation of duties) ambapo mtumiaji mmoja wa mfumo anafanya kazi zaidi ya moja kama vile kupokea taarifa za dawa kutoka kwa wasambazaji, kuhesabu dawa (physical counting), kushughulikia mahitaji ya dawa ya vituo na hospitali zote na kuandaa shehena ya dawa zinazohitajika na kuzisambaza katika vituo mbali mbali vilivyowasilisha mahitaji yao. Uwepo wa dosari hiyo umepelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali katika udhibiti wa dawa na vifaa tiba ndani ya Bohari Kuu ya Dawa.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye ujuzi wa kutumia na kusimamia mahitaji ya mfumo kwa lengo la kunusuru utokeaji wa hali ya kutokupatikana kwa dawa na vifaa tiba kwa wakati ambapo kutatokana na kutokuwepo kwa mgawanyo sahihi wa majukumu, udhibiti imara na usimamizi mzuri wa taarifa za mahitaji ya dawa katika vituo vya Afya na Hospitali.

2.4.1.3 Kukosekana kwa uidhinishaji wa utoaji wa dawa na vifaa tiba kwa kila hatua kupitia mfumo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa watumiaji wachache wa mfumo ambapo mtu mmoja hufanya jukumu zaidi ya moja ikiwemo kupokea taarifa za mahitaji ya dawa na vifaa tiba kutoka katika vituo vya afya na hospitali, kuyafanyia kazi mahitaji hayo, kuhesabu na kuandaa shehena za dawa zinazohitajika na kuzisambaza katika vituo vinavyohitajika bila ya kuwepo mtu mwingine ambae atathibitisha na kuidhinisha uhalisia wa kilichohitajika na kilichoandaliwa kupelekwa sehemu husika ambapo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa vitendo vya upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na hatimae kuingiza hasara Serikali.

2.4.1.4 Kutopatikana ipasavyo kwa huduma ya Msaada wa kiufundi "Technical Support" kutoka kwa Mtengenezaji wa Mifumo (Kampuni ya SUSOL)

Ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa imeingia mkataba wa miaka mitatu na Kampuni ya SUSOL iliyopo New Zealand kuanzia tarehe 1 Julai 2020 ambapo mkataba huo una jumla ya thamani ya **USD 8,083.24** kila mwaka ikiwa ni malipo kwa ajili ya leseni ya matumizi na msaada wa kiufundi kwa mifumo mitatu ambayo ni mfumo wa mSupply, mfumo wa eLMIS - CE na mfumo wa Money Works.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Bohari Kuu haipati vizuri msaada wa kiufundi kutoka kwa kampuni husika (SUSOL) licha ya kwamba gharama hizo bado zinaendelea kulipwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2020.

Kutokupata kwa huduma ya msaada wa kifundi ipasavyo kumepelekea mifumo hiyo kutofanya kazi vizuri "under performance" na kupitwa na wakati "out of date". Hali hii inapelekea kukosekana kwa usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani yake, kutokua na ufanisi katika utendaji kazi kutokana na kutokunufaika na maboresho ya mifumo yanayotolewa na watengeneza mifumo kupitia mitandao.

2.4.1.5 Kupitwa na wakati kwa mfumo wa mSupply unaotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa

Ukaguzi umebaini pamoja na kutokupatikana kwa msaada wa kiufundi unaotegemewa kutolewa na kampuni ya SUSOL kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba yaliyofungwa tarehe 1 Julai 2020 imebainika mfumo wa "mSupply Version 4.12.04 " unaotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa kwa sasa umepitwa na wakati (out of date) kuanzia tarehe 29-07-2020 na kupelekea kujitokeza kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo kutokuwa sahihi na kutokupatikana wakati zinapohitajika na hivyo kupelekea Serikali kuingia hasara kubwa kwa kupoteza kumbu kumbu za dawa na vifaa tiba nchini.

Aidha kwa mujibu wa toleo la tarehe 19-10-2021 lililotangazwa na Mtengenezaji wa Mifumo "Vendor" limebainisha kwa sasa mfumo huo umefanyiwa maboresho na kutolewa toleo jipya la " mSupply Version 5.05 " **Kiambatisho Nambari 3 kinahusika** ambapo licha ya Serikali kuingia gharama za kulipia toleo jipya kwa gharama za dola za kimarekani **USD 3,557.62** sawa na **shilingi 8,193,198.86** bado Bohari Kuu ya dawa haijafaidika na toleo jipya lililotangazwa na "Vendor" na kupelekea kuibebesha Serikali hasara kwa kutumia toleo la zamani ambalo halina usalama wa kutosha wa kutunza taarifa za dawa na vifaa tiba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kufuatilia kwa kina suala la uboreshwaji wa mfumo kuwa katika toleo jipya " mSupply Version 5.05 " pamoja na upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika mifumo yake kwa kampuni ya SUSOL ili kuweza kuimarisha mifumo hiyo iweze kufanya kazi vizuri kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha (VFM) zilizoekwezwa na zinazoendelea kuekezwa na Serikali kila mwaka.

2.4.1.6 Kubadilika kwa gharama za dawa na vifaa tiba zilizowekwa katika Mfumo wa mSupply.

Moja kati ya hatua za uendeshaji zinazofanyika ndani ya mfumo wa mSupply ni kutengeneza ankara za malipo ya dawa na vifaa tiba "Invoices". Ankara hizo hutengenezwa na watumiaji wa mfumo ndani ya Bohari Kuu ya Dawa kupitia mfumo wa mSupply na huonesha bei na thamani halisi ya dawa na vifaa tiba zilizopo sokoni "Market Price" ambapo kama dawa hizo zingekuwa zinazwa katika vituo vya afya na hospitali zingelionesha bei halisi ya soko.

Aidha, dhumuni la kuweka gharama za bei ya dawa na vifaa tiba kwenye ankara za malipo ndani ya mfumo wa mSupply ni kuisaidia Bohari Kuu ya Dawa katika kutengeneza makisio ya bajeti ya ununuzi ya dawa na vifaa tiba kwa mwaka unaofuata.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa mSupply una tatizo la kuzibadilisha wenyewe bei halisi za dawa na vifaa tiba zilizoingizwa kwenye ankara za malipo ndani ya mfumo na kuonesha bei nyengine zisizo na uhalisia jambo ambalo linapelekea kujitofautisha kwa bei zilizooneshwa katika ankara za awali ndani ya mfumo " data integrity issue ". Kubadilika kwa bei za dawa na vifaa

tiba zilizowekwa kunaweza kupelekea kupoteza uhalisia wa taarifa za fedha za dawa zinazolingizwa katika mfumo pamoja na kukosekana kwa makisio ya bajeti za manunuzi na matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa Bohari Kuu ya Dawa kwa miaka inayofuata.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa kufuatilia kwa kina suala la uboreshwaji wa mfumo kuwa katika toleo jipya liliopo sokoni pamoja na upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika mifumo yake kwa kampuni ya SUSOL ili kuweza kuimarisha mifumo hiyo iweze kufanya kazi vizuri kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha (value for money) zilizoekeswa na zinazoendelea kuekezwa na Serikali kila mwaka.

2.4.1.7 Kukosekana kwa miundombinu imara ya Mawasiliano ya Mtandao baina ya Bohari Kuu ya Dawa ya Unguja na Pemba

Bohari Kuu ya Dawa kwa upande wa Unguja ipo Maruhubi ambapo miundombinu pamoja na mfumo mkuu unaoshughulika na taarifa za upokeaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba imewekwa hapo. Kwa upande wa Pemba Bohari Kuu ya Dawa ipo Vitongoji ambapo Bohari hiyo hutumika kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali zote za Pemba.

Ukaguzi umebaini Bohari ya Dawa iliyopo Vitongoji - Pemba haipati huduma nzuri ya matumizi ya mfumo wa mSupply kutoka Maruhubi Unguja. Hali hii imetokana na kukosekana kwa miundombinu imara ya mawasiliano ya mtandao baina ya Bohari Kuu ya Dawa Unguja na Bohari ya Pemba (VPN Connection).

Aidha ukaguzi umebaini kuwepo kwa upungufu wa taaluma katika matumizi ya mifumo hiyo kwa wafanyakazi wa Bohari ya dawa Pemba.

Kutopatikana kwa huduma bora ya mawasiliano ya mtandao pamoja na kukosekana kwa taaluma ya matumizi ya mfumo ya dawa kunaweza kupelekea kutokea kwa ucheleweshwaji wa upatikanaji wa dawa zinazohitajika katika vituo vya afya na Hospitali zilizopo Pemba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya Mtandao baina ya Ofisi zake mbili za Unguja na Pemba pamoja na kuongeza taaluma ya matumizi ya mfumo kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaotumia mifumo ya dawa na vifaa tiba ili kuweza kutumika ipasavyo katika Bohari zote mbili za dawa.

2.4.1.8 Kutotumika Ipasavyo kwa Mfumo wa mSupply ndani ya Bohari Kuu ya Dawa "Under Utilization of mSupply System"

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa mSupply umegawika katika moduli tofauti "*modules and sub modules*" **Kiambatisho Nambari 4 kinahusika** ambapo baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

Customer, Supplier, Item, Reports, Special, Admin, Issuing goods, Incoming Goods, Purchase Orders, Tender Management, Safety Measures, Dispensing, na Patient Medical Records n.k.

Baada ya kufanyika ukaguzi wa matumizi ya moduli hizo, ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa inatumia moduli kidogo ukilinganisha na uhalisia wa moduli zilizomo katika mfumo huo licha ya kwamba Bohari imelipia matumizi ya moduli zote.

Kufanya hivyo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kuingia hasara kutokana na kulipa gharama kubwa ya fedha kwa ajili ya matumizi ya mfumo kinyume na mahitaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa na kufanya malipo kulingana na mahitaji ya moduli zinazohitajika ili kuepusha kuingiza hasara Serikali kwa kufanya malipo yasiyohitajika jambo ambalo lingelipelekea kuokoa gharama kubwa ya fedha za umma.

2.4.1.9 Kufanyika kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba nje ya Mfumo

Ukaguzi umebaini kwamba miongoni mwa wasambazaji wengi wanaouza dawa na vifaa tiba kwa Serikali kupitia Bohari Kuu wanatumia mifumo kwa ajili ya kuuza dawa na vifaa tiba, lakini msambazaji pekee anaajulikana kwa jina la Medical Store Department (MSD) ndiye ambae aliyemuunganisha Bohari Kuu ya Dawa kupitia mfumo wake uitwao ILS ambapo Bohari Kuu hufanya maombi ya dawa na vifaa tiba moja kwa moja kupitia kwenye mfumo huo hali inayopelekea taarifa za maombi ya madawa, taarifa za upokeaji, taarifa za madeni ya dawa na kumbukumbu za malipo yanayofanyika hutunzwa vizuri, kwa usahihi na kupatikana kwa wakati kupitia kwenye mfumo huo wa ILS uliopo kwa msambazaji MSD.

Aidha ukaguzi umebaini sehemu kubwa ya dawa na vifaa tiba vinavyonunuliwa na Bohari Kuu ya Dawa zinatoka kwa wasambazaji binafsi ambapo taratibu za manunuzi hufanyika kwa njia ya kawaida "manually" nje ya mfumo licha ya kuwa wasambazaji hao wanatumia mifumo ya manunuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Hali hii inapelekea upotevu mkubwa wa kumbukumbu za dawa zinazoagizwa na kupokelewa, zinazolipwa pamoja na kukosekana kumbu kumbu za madeni halisi yanayodaiwa na yaliyobaki.

Kwa upande wa Bohari Kuu ya Dawa ukaguzi umebaini mifumo ya Bohari ina uwezo mkubwa wa kufanya taratibu zote za manunuzi ya dawa na vifaa tiba kutoka kwa wasambazaji kuanzia hatua ya awali ya kutangaza na kusimamia zabuni, kuchagua wasambazaji wenye vigezo, kufanya manunuzi ya dawa kwa msambazaji alieshinda Zabuni hadi kukamilika kwa malipo ya dawa na vifaa tiba, lakini Bohari Kuu ya Dawa hutumia taratibu hizo kwa njia ya kawaida "manually" nje ya mfumo.

Kufanyika kwa utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba bila ya kutumia mfumo kunapelekea kupotea au kuchanganyika kwa kumbukumbu za taarifa za dawa na vifaa tiba zilizoagizwa, zilizoletwa na zilizobakia na hatimae kusababisha kupokea idadi pungufu ya dawa.

Aidha kutokutumia mfumo ipasavyo kunapelekea kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na hatimae kuingiza hasara Serikali kutokana na kununua bidhaa za madawa pasipo na mahitaji (duplicates), ukizingatia kwamba wasambazaji hawana kawaida ya kuwasilisha mahitaji kamili kwa mujibu wa mikataba yao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa kufanya utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba kupitia mifumo yake ili kuweza kudhibiti taarifa za manunuzi, mapokezi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba na kuweza kuongeza ufanisi na weledi katika utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba.

Orodha ya Wasambazaji wa dawa na vifaa tiba "Medical Suppliers" waliobainika na ukaguzi kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia mfumo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 1: Wasambazaji ambao hufanya manunuzi na Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia Mfumo.

Namba	Jina la Msambazaji Dawa/Vifaa Tiba	Huduma anayoitoa
WASAMBAZAJI WALIOPO NCHINI (LOCAL SUPPLIERS)		
1	Salama Pharmaceuticals	Dawa na Vifaa Tiba
2	KAT Med Group (T) LTD	Vitendanishi "Reagents" za Maabara na Huduma za za Damu Salama
3	KAS Medics	Vitendanishi "Reagents" za Maabara
4	Abbott Diagnosis	Vitendanishi "Reagents" za Mashine ya PCR (UVIKO -19)
5	Nebula Health Care LTD	Vifaa vya Mfupa na Vipimo vya UVIKO - 19
6	LAB Equip LTD	Vifaa Tiba
7	Bahari Pharmacy	Mikoba ya Vifaa vya Uzazi
8	Indepth Scientific	Vitendanishi "Reagents" za Maabara
9	Anudha LTD	Vitendanishi "Reagents" za Maabara
10	M&D Chemicals	Consumables za Maabara
11	IDA Foundation – Nertherland	Dawa Muhimu
12	DAWA Arus	Dawa na vifaa tiba
13	Life Care	Dawa na vifaa tiba
WASHIRIKA WA MAENDELEO (DONORS)		
14	UNICEF	Virutubisho vya Watoto na Vifaa vya Kipindupindu
15	Global Fund	Dawa za Mradi wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria
16	WHO	Vifaa vya UVIKO – 19
17	UNFPA	Dawa na Vifaa vya Uzazi
18	GLOBAL LIFE SHARING – SOUL, KOREA	Dawa na Vifaa Tiba
19	CHINA GOVERNMENT	Dawa za Kichina
20	USAID	Vifaa vya UVIKO – 19
21	HILL LIFECARE – INDIA	Dawa Muhimu
22	UNDP	Vifaa Tiba
23	ENGEDER HEALTH	Vifaa Tiba
24	SD BIOSENSOR - KOREA	Test kit za Kupima UVIKO – 19

2.4.1.10 Kutofanya kazi ipasavyo kwa Moduli ya Ripoti katika Mfumo wa mSupply

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa mSupply una moduli mbali mbali ikiwemo moduli ya Ripoti ambayo hutumika kwa ajili ya kutoa ripoti za dawa na Vifaa tiba Bohari Kuu ya Dawa, aidha imebainika moduli hiyo haitoi taarifa sahihi za dawa zilizoisha muda au zinazotarajiwa kuisha muda wa matumizi kwa binadamu (expiries).

Hali hii inapelekea kuharibika kwa dawa nyingi kutokana na kubakia katika ghala kwa kutopata taarifa sahihi za dawa zinazoisha muda.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuchukuwa jitihada za makusudi katika kutatua dosari hizo ili kuweza kupatikana ripoti zitakazoonesha taarifa sahihi za dawa zinazokaribia kuisha au zilizoisha muda wa matumizi kwa binadamu jambo ambalo litapelekea kuinusuru Serikali kuingia gharama kubwa za manunuzi ya dawa kutokana na kutokupatikana kwa taarifa sahihi na kwa wakati kwa dawa zinazokaribia kuisha muda wa matumizi.

2.4.1.11 Dosari zilizobainika baina ya Kitengo cha Ununuzi na Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali za kiutendaji baina ya kitengo cha Manunuzi cha Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Bohari Kuu ya Dawa . Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutoshiriki kikamilifu kwa Kitengo cha Ununuzi (PMU) kwenye mchakato wa upokeaji wa dawa na vifaa tiba wakati zinapowasilishwa Bohari Kuu kutoka kwa Wasambazaji ikiwa kitengo hicho ni wahusika wakuu wa uagizaji dawa na ndio wenye taarifa sahihi za dawa zilizoagizwa.
- Kukosekana kwa miongozo na sera imara zilizoandikwa (Documented Standard Operating Procedures) zitakazotumika baina ya Bohari na Kitengo cha Manunuzi/ Wizara ya Afya kuanzia hatua ya mchakato wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba, upokeaji wa dawa hadi kukamilika kwa uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.
- Kuwepo kwa dosari katika mgawanyo wa majukumu na mgawanyo wa kazi kwa wafanyakazi wa vitengo mbali mbali ndani ya Bohari Kuu ya Dawa.

2.4.1.12 Dosari katika Usambazaji wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa Kampuni binafsi.

Ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari mbali mbali kutoka kwa kampuni binafsi za kusambaza dawa na vifaa tiba, baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokuwekwa alama za utambulisho "Code/Nembo" kwa dawa na vifaa tiba vinavyosambazwa na kampuni binafsi. Hali hii inapelekea kutojulikana kwa idadi kamili ya dawa na vifaa tiba vinavyosambazwa na kampuni binafsi jambo ambalo ni tofauti na MSD ambae bidhaa zake za dawa na vifaa tiba zimewekwa alama za utambulisho.

Kutokuwepo kwa alama za utambulisho wa dawa zinazoagizwa na kununuliwa kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba zilionunuliwa na Serikali kuweza kutumika katika maduka binafsi.

- Kujitokeza kwa uwepo wa ankara zenye tarehe tofauti zinazothibitisha kufanyika kwa malipo ya shilingi 976,275,934 kwa kampuni binafsi mbali mbali za usambazaji wa dawa na vifaa tiba ambazo ankara hizo zimerikodiwa nambari ya aina moja ya kumbukumbu ya uthibitisho wa upokezi wa dawa na vifaa tiba zilizopo Bohari Kuu ya dawa jambo ambalo limetia shaka juu ya uwepo wa uhalali wa bidhaa na fedha zilizolipwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 2: Ankara zenye namba za utambulisho uliofanana

Namba	Nambari ya hati ya Uagizishaji	Tarehe ya Ankara	Nambari ya Ankara	Thamani (Tshs)	Tarehe ya kupokea Bohari	SMZ Ref No.
1	4119050	15/08/2019	4128128	5,540,955	19/08/2019	SMZ/RV 01/19/20
2	4131278	3/7/2020	4140149	115,290,000	4/7/2020	SMZ/RV 01/19/20
3	4119143	17/08/2019	4128220	5,200,000	9/8/2019	SMZ/RV 19/19/20
4	4122109	5/11/2019	4131149	244,285,789	7/11/2019	SMZ/RV 19/19/20
5	4122210	7/11/2019	4131249	131,518,816	9/11/2019	SMZ/RV 22/19/20
6	4122539	14/11/2019	4131576	11,929,434	16/11/2019	SMZ/RV 22/19/20
7	4109261	9/11/2018	4118439	8,879,418	14/11/2018	SMZ/RV 23/18/19
8	4108957	2/11/2018	4118143	71,826,563	3/11/2018	SMZ/RV 23/18/19
9	4122323	11/11/2019	4131360	3,450,000	11/11/2019	SMZ/RV 23/19/20
10	4122536	14/11/2019	4131571	68,187,762	16/11/2019	SMZ/RV 23/19/20
11	4113074	28/02/2019	4122212	30,049,698	2/3/2019	SMZ/RV 42/18/19
12	4113234	6/3/2019	4122372	19,785,000	7/3/2019	SMZ/RV 42/18/19
13	4114091	27/03/2019	4123210	103,840	30/03/2019	SMZ/RV 48/18/19
14	4114434	5/4/2019	4123551	79,279,200	8/4/2019	SMZ/RV 48/18/19
15	4125616	31/01/2020	4134601	64,667,450	1/2/2020	SMZ/RV 48/19/20
16	4125618	31/01/2020	4134603	30,621,770	6/2/2020	SMZ/RV 48/19/20
17	4125551	30/01/2020	4134538	1,380,000	30/01/2020	SMZ/RV 52/19/20
18	4126755	27/02/2020	4135721	201,691	28/02/2020	SMZ/RV 52/19/20
19	4127661	18/03/2020	4136611	43,600,000	19/03/2020	SMZ/RV 59/19/20
20	4127785	20/03/2020	4136727	40,478,548	24/03/2020	SMZ/RV 59/19/20
Jumla				976,275,934		

2.4.1.13 Uwepo wa Ankara za madeni ambazo hazikuthibitishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Katika ukaguzi wa madeni imebainika uwepo wa ankara za madeni yenye thamani ya shilingi 1,284,795,591.11 pamoja na USD 750,144.69 kutoka Bohari Kuu ya Dawa ambazo taarifa zake hazikuonekana katika orodha ya ankara zilizowasilishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba katika Ofisi ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi. Aidha ankara hizo hazikuweza kubainika katika kumbukumbu za hati za malipo.

Jadweli Nambari 3 : Ankara za madeni ambazo taarifa zake hazikuthibitishwa na wasambazaji

Namba	Tarehe	Nambari ya Ankara	Hati ya Mapokezi	Kumbukumbu Namba ya Mapokezi Bohari	Kiasi (Tshs)
HARSH					
1	22/10/2018	INV/2018/590	DEL/2018/907	SMZ/RV07/18/19	59,385,000
2	10/04/2018	INV/2018/552	DEL/2018/849	SMZ/RV06/18/19	39,590,000
Jumla Ndogo					98,975,000
LIFE CARE					
3	14/7/2021	154	-	-	3,645,000
4	23/7/2021	156	-	SMZ/RV03/21/22	1,685,000
Jumla Ndogo					5,330,000
SALAMA PHARMACEUTICAL LTD					
5	06/03/2019	4122378	-	SMZ/RV42/18/19	19,785,000
KAT Med					
6	22/09/2021	0242	0265	SMZ/RV28/21/22	1,584,000
7	03/09/2021	0240	0263	SMZ/RV26/21/22	8,560,500
8	06/09/2021	0241	0264	SMZ/RV25/21/22	1,600,000
Jumla Ndogo					11,744,500
ABBOTT					
9	25/2/2021	13-03459317	-	SMZ/RV01/20/21	USD 743,664.69

10	26/2/2021	13-03469585	-	SMZ/RV02/20/21	USD 6,480
					USD 750,144.69
INDEPTH SCIENTIFIC					
11	20/7/2018	12	-	-	5,200,000
12	11/01/2019	87	-	-	2,954,318
13	11/01/2019	88	-	-	13,274,353
14	16/12/2019	99	-	-	25,199,353
15	17/2/2020	100	-	-	5,400,000
16	16/12/2019	90	-	-	8,000,000
17	17/6/2020	1		SMZ/RV06/19/20	9,215,000
Jumla Ndogo					69,243,024
LAB EQUIP					
18	24/6/2020	7668	18411	SMZ/ RV01/2020/21	59,000,000
19	05/07/2021	8218	24483	SMZ/ RV13/2021/22	1,955,200
20	26/8/2020	6992	18337	SMZ/RV04/20/21	86,222,000
21	09/01/2020	7002	18347	SMZ/RV05/20/21	8,778,000
22	07/03/2020	6855	18444	SMZ/RV02/2021	38,000,000
23	29/3/2021	7850	12499	SMZ/RV10/2021	19,781,500
24	24/6/2021	8308	24624	SMZ/RV12/21/22	882,000
Jumla Ndogo					214,618,700
NEBULLA					
25	15/1/2021	NEB/INV.407	-	-	256,000,000
26	22/6/2021	NEB/INV.0114	-	-	647,500
Jumla Ndogo					256,647,500
MEDICAL STORE DEPARTMENT					
27	28/8/2019	6497935	-	-	122,059,095.6

28	31/10/2019	6510176	-	-	90,148,000
29	16/10/2019	6505239	-	-	6,767,020
30	29/11/2019	6520876	-	-	2,546,000
31	19/9/2018	623778	-	-	144,000,000
32	11/03/2018	6347141	-	-	2,588,352
33	10/10/2018	630642	-	-	2,113,800
34	24/10/2018	636043	-	-	25,989,600
35	09/11/2019	6494186	-	-	32,861,904
36	31/7/2019	6477160	-	-	3,998,862.40
37	18/3/2020	6558922	-	-	44,509,400
38	18/2/2020	65546243	-	-	7,354,000
39	17/9/2021	289915	-	-	56,615,842.14
40	16/9/2021	2889116	-	-	86,684,990.97
Jumla Ndogo					628,236,867.11
Jumla Kuu (Tshs)					1,284,795,591.11
Jumla Kuu (USD)					USD 750,144.69

2.4.1.14 Kutokuwepo kwa usalama na udhibiti mzuri wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba

Ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba ipo katika hatari ya kupoteza taarifa zake za dawa na vifaa tiba zinazohifadhiwa ndani ya mifumo yake kutokana na kutotumia njia salama za udhibiti wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo. Hali hii imesababishwa kutokana na kujitokeza kwa mambo yafuatayo: -

- Kutofanyika ipasavyo kwa mchakato wa uwekaji wa nakala za taarifa zilizomo ndani ya mfumo (Daily backup process is not conducted).
- Endapo Janga lolote likitokea katika Taasisi ya Bohari, hakuna mpango imara wa kuokoa taarifa zilizomo ndani ya mifumo yake na kuendeleza utoaji wa huduma zake (No Business Continuity Plan and Disaster Recovery Plan).
- Mifumo ya Bohari kuwa nje ya muda "Systems Out of Date".
- Kutoingizwa programu za kuweka usalama "Antivirus" ndani ya kompyuta za mifumo "Servers".

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kupitia uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kuwajengea uwezo wasimamizi wa mifumo hiyo ikiwemo kuwapatia mafunzo ya udhibiti na usalama wa mifumo ya Bohari ili kuweza kusimamia vizuri na kuimarisha usalama wa taarifa zilizomo.

2.4.1.15 Dosari zilizobainika katika Mifumo ya Dawa na Vifaa Tiba inayotumika katika Vituo vya Afya na Hospitali za Unguja na Pemba

Katika ukaguzi uliofanyika kwa vituo mbali mbali vya Afya na Hospitali za Wilaya na Mkoa kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo ukaguzi huo ulijumuisha ukaguzi wa mifumo ya dawa na vifaa tiba inayotumika katika vituo na hospitali hizo na kukagua sehemu mbali mbali zinazohifadhiwa dawa na vifaa tiba (Stores) kwa lengo la kuangalia udhibiti na usalama wa huduma za dawa na vifaa tiba katika vituo hivyo. Vituo vya afya na Hospitali zilizopitiwa ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

Jadweli Nambari 4: Mifumo inayotumika katika Vituo vya Afya na Hospitali zilizofanyiwa Ukaguzi.

Namba	Jina la Kituo/Hospitali	Mfumo inayotumika
UNGUJA		
1	Hospitali ya Mnazi Mmoja.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – CE • eHMS
2	Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – FE • eLMIS – CE
3	Hospitali ya Wilaya ya Kivunge.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – FE • eLMIS – CE • Aspire – HER
4	Hospitali ya Mpendae.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – FE • eLMIS – CE
5	Kituo cha Afya Shauri Moyo.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – FE • eLMIS – CE
6	Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa tiba Maruhubi	<ul style="list-style-type: none"> • mSupply • eLMIS – FE • eLMIS – CE
PEMBA		
7	Hospitali ya Wilaya ya Wete.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – FE • eLMIS – CE
8	Hospitali ya Abdallah Mzee Mkoani.	<ul style="list-style-type: none"> • HMIS • eLMIS - CE
9	Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – CE
10	Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa tiba Vitongoji Pemba.	<ul style="list-style-type: none"> • eLMIS – CE

Aidha, baada ya kupitia vituo na hospitali hizo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kama zinavyoonekana hapo chini:-

a) Wafanyakazi kukwepa kutumia Mifumo iliyopo katika uwekaji wa kumbukumbu za usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa.

Ukaguzi umebaini wafanyakazi wengi waliopo katika vituo vya afya na hospitali wanaohusika na upokeaji dawa kutoka katika stoo za hospitali pamoja na usambazaji dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa wanakwepa kutumia mifumo iliyopo katika kuweka kumbukumbu za taarifa hizo.

Aidha taarifa za maombi ya dawa zinazotoka katika vitengo vya dawa (pharmacies) na kupelekwa Stoo kwa ajili ya kuomba dawa hurikodiwa kwa njia ya kawaida "manually" ambapo taarifa nyingi zinakuwa haziko sahihi ukilinganisha na idadi kamili ya dawa na vifaa tiba zilizopo au zilizotolewa. Vile vile baadhi ya hospitali kutokuweka kabisa rikodi za dawa zinazotolewa kwa wagonjwa na kupelekea kutojulikana kwa idadi halisi ya dawa zilizotolewa kwa wagonjwa.

Hali hii imebainika katika vituo vya afya na hospitali tofauti kama vile Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake, Hospitali ya Abdallah Mzee wilaya ya Mkoani, Hospitali ya Wilaya ya Wete, Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi na Hospitali ya Wilaya ya Kivunge pamoja na vituo vyote vya afya.

Kutotumia mifumo katika vituo vya afya na hospitali kwa ajili ya mchakato wa kuweka kumbukumbu za upokeaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa kunapelekea kutokea kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba kwa kutopatikana kumbukumbu sahihi za dawa na vifaa tiba zinazotolewa na kusambazwa.

b) Kukosekana kwa vifaa vya kuongeza usalama "CCTV Cameras" pamoja na "Door Security Machines" katika Vyumba vya kuhifadha dawa ndani ya Vituo vya Afya na Hospitali.

Moja kati ya njia bora za kudhibiti na kuongeza usalama wa uhifadhi wa dawa na vifaa tiba ndani ya vituo vya afya na hospitali ni kuweka vifaa maalum vya ulinzi na usalama ambavyo vitasaidia kuonesha kumbukumu za matukio yote yanayofanyika katika vyumba vya kuhifadha dawa na vifaa tiba pamoja na muda wa matukio. Mfano wa vifaa hivyo ni "CCTV Cameras" pamoja na mashine maalum za milango zinazozidhibiti uingiaji wa watu wasiohusika "Door Security Machines".

Ukaguzi umebaini kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Abdallah Mzee ndio vituo pekee vilivyokuwa na kamera katika sehemu za kuhifadha dawa (store).

Hata hivyo Hospitali ya Abdallah Mzee ina kamera moja tu katika sehemu ya kuhifadha dawa na vifaa tiba (store) ambayo haitoshi kwa mujibu wa uhalisia wa dawa zinavyowekwa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuongeza ulinzi kwa kuweka kamera na vifaa vya ulinzi kwenye milango ya sehemu za kuhifadha dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya vyote pamoja na Hospitali kwa Unguja na Pemba.

c) Kukosekana kwa Mafunzo Endelevu ya watumiaji wa Mifumo ya Dawa na Vifaa Tiba.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wanaotumia mifumo iliyopo katika Vituo vya Afya na Hospitali hawana uwelewa mzuri wa utumiaji wa mifumo hiyo, hali hii imepelekea wafanyakazi hao kupata changamoto kubwa za kiutendaji katika matumizi ya mifumo hiyo ambapo baadhi yao kuona usumbufu na kutotumia kabisa mifumo iliyopo kwa utendaji kazi na kuandika kumbukumbu za matumizi ya dawa katika madaftari (manually).

Aidha wafanyakazi wa vituo vyengine kuamua kutumia programu ya "Microsoft Excel" katika kurikodi taarifa za dawa kutokana na kutoelewa vizuri namna ya kutumia mifumo ya dawa iliyopo.

Hali hii inapelekea kutopatikana kwa ufanisi na tija katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba kwa vituo vya afya na hatimae kupelekea kuongezeka kwa upotevu wa dawa na vifaa tiba kwa kisingizio cha kutokuwa na uelewa wa matumizi ya mifumo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kutilia mkazo suala la kujenga uwezo kwa watumiaji wa mifumo ya dawa na vifaa tiba waliopo katika hospitali na vituo vya afya ili kuweza kuimarisha ufanisi na kupatikana kwa tija katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba.

2.4.1.16 Kutofuatwa kwa Taratibu na Miongozo ya Uhifadhi wa Dawa na Vifaa Tiba.

Kwa mujibu wa Muongozo mpya wa utendaji kazi uliotolewa mwaka 2019 na Wizara ya Afya ambao hadi sasa ndio unaotumika " *Logistics Systems Standard Operating Procedure Manual* " unaeleza taratibu zote za utendaji kazi katika vituo vya afya na hospitali ikiwemo miongozo na taratibu mbali mbali zinazopaswa kutumika katika vyumba vya kuhifadhi dawa na vifaa tiba (Stores).

Aidha ukurasa wa 13 wa Muongozo huo umeainisha taratibu 13 zinazotakiwa kufuatwa katika sehemu za kuhifadhi dawa na vifaa tiba (Storage Guidelines).

Hata hivyo ukaguzi umebaini vituo vya afya na hospitali zote kwa Unguja na Pemba hazifuati ipasavyo taratibu 13 za kuhifadhi dawa zilizoainishwa katika Muongozo huo.

Baadhi ya dosari zilizoonekana kujitokeza kutokana na kutokufuatwa kwa miongozo na taratibu za utunzaji dawa na vifaa tiba katika Stoo za hospitali na vituo vya afya ni kama zifuatazo: -

- Kuwepo na hali isiyoridhisha katika mafriji na mafriza ya kuhifadhi dawa ambapo hali hii imebainika katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge. **Kiambatisho Nambari 5 kinahusika.**
- Kuwepo na joto kali katika Stoo ya kuhifadhi dawa ambapo hali hii imebainika katika Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake Pemba na imetokana na ubovu wa muda mrefu wa kiyoyozi kilichopo (Air Condition) ambapo imepelekea kuharibika kwa baadhi ya dawa kutokana na kukosekana kwa "room temperature" iliyo bora.
- Kukosekana kwa vifaa vya kuzimia moto "Fire Extinguisher" ambapo hali hii imebainika katika hospitali ya Wilaya ya Makunduchi kwa vile hospitali nzima haina "fire extinguisher" hata moja.
- Kuwepo kwa "Fire Extinguisher" ambazo zimeshaisha muda wa kufanya kazi (Expired) ambapo dosari hii imebainika katika vituo vingi vya afya na hospitali.
- Kutotumika kwa utaratibu bora wa kupanga dawa katika makabati ya dawa (Shelves) yaliyomo Stoo katika vituo na hospitali zote ambapo utaratibu bora unaohitajika kufuatwa kwenye muongozo wa kupanga dawa ni **(First Expire First Out – FEFO).**
- Kuwepo kwa nafasi ndogo za maeneo ya kuhifadhi dawa na vifaa tiba ukilinganisha na ujazo wa shehena halisi za dawa na vifaa tiba inaotakiwa kuhifadhiwa, hali hii imebainika katika vituo na hospitali zote za Unguja na Pemba.

Kutokufuata taratibu na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya kuhifadhi dawa kunaweza kupelekea upotevu, uharibikaji (expiries) wa dawa, na vile vile kutokea kwa miripuko ya kemikali za dawa zilizopo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhamasisha wafanyakazi wanaohusika na utunzaji dawa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa na Wizara katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba.

Aidha Wizara ya Afya kusambaza nakala za miongozo hiyo (SOP) kwa Vituo na Hospitali zote za Unguja na Pemba ili kuweza kutumika ipasavyo pamoja na kuchukuwa jitihada za makusudi za kuimarisha maeneo ya kuhifadhi dawa na vifaa tiba ikiwemo kuongeza nafasi na kuweka viyoyozi, kudumisha hali ya usafi n.k.

2.4.1.17 Dosari zilizobainika katika Mfumo wa eLMIS - Facility Edition

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya gharama zilizotumika kwa ajili ya utengenezaji na uendeshaji wa Mfumo wa **eLMIS Facility Edition ni USD 87,442**. Gharama hizo zimepatikana kupitia mkataba wa manunuzi ya mfumo huo uliosainiwa tarehe 09-07-2018 baina ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Mshauri elekezi Kampuni ya John Snow Inc (JSI) wenye thamani ya **USD 57,921** na mkataba wa ziada wa msaada wa kiufundi wa mfumo huo uliosainiwa tarehe 12-11-2020 baina ya wahusika hao ambao una thamani ya **USD 29,521**. Taarifa kamili za mikataba hiyo zimebainishwa katika **Kiambatisho Nambari 2(A) na 2(B)**.

Aidha mfumo huo ulikuwa na lengo la kuongeza huduma za kusimamia uwekaji wa kumbukumbu za dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali ambapo mfumo ungepaswa kuendesha vitengo vyote vinavyohitajika kusambazwa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya.

Vitengo vyenyewe ni kama vifuatavyo: -

Medical Store, Pharmacy, Wards, Theatres, Maternity, Outpatient department, Inpatient department, Laboratory, Dental department, Emergency, CTC/ARV n.k.

Aidha, ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali za kiutendaji katika mfumo huo wa **eLMIS Facility Edition** ambapo baadhi ya dosari ni kama zifuatazo:-

- Mfumo kukosa uadilifu wa taarifa (Lack of Data Integrity) kutokana na kujibadilisha wenyewe taarifa za kimahesabu za dawa na vifaa tiba (mathematical Errors) ambazo zimeingizwa na watumiaji wa mfumo hasa wakati wa kuomba dawa katika bohari Kuu.
- Kutopatikana kwa huduma ya mfumo kwa baadhi ya hospitali kutokana na matatizo ya mtandao na kutofanya kazi kwa mashine za **UPS** zilizounganishwa na kompyuta zenye kutumia mifumo ya dawa na vifaa tiba ambazo vifaa hivyo husaidia kuhifadhi umeme wa kompyuta kwa muda endapo umeme mkuu ukikatika.
- Mfumo kutumika katika vitengo viwili tu ambavyo ni kitengo cha Store za Dawa na kitengo cha Pharmacy katika vituo vyote vya afya na hospitali ambapo kiuhalisia mfumo huo una uwezo wa kutumika katika vitengo vyote kama ilivyoainishwa hapo juu.
- Mfumo kutoweza kutoa ripoti kamili ya orodha ya dawa zinazoisha muda (expiries), hivyo kusababisha changamoto kubwa kutaka kujua orodha ya dawa zinazokaribia kuisha muda (expire) katika Store ya Dawa ili zitumike mapema.
- Kutopatikana kwa msaada wa kiufundi wakati mfumo unapoleta changamoto za kiutendaji.

2.4.1.18 Dosari zilizobainika katika Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kwa Unguja na Pemba

a) Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba - Pemba

Ukaguzi ulitembelea Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba iliyopo Vitongoji Pemba ambapo Bohari hiyo hupokea shehena za dawa na vifaa tiba kutoka katika Bohari Kuu ya Unguja na kuhifadhi katika bohari yake ya Vitongoji, baadae kusambaza dawa na vifaa tiba kwa vituo vya afya na hospitali zote za Pemba kwa mujibu wa maagizo yaliyotolewa na uongozi wa Bohari Kuu ya Unguja. Hata hivyo ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali katika Bohari hiyo ya Pemba ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kutofanya kazi wa mfumo wa CCTV Camera zilizopo ndani ya Bohari kutokana na kutokuwepo kwa msimamizi wa matokeo kwenye CCTV Camera.
- Kutofanya kazi kwa Jenereta ambalo limewekwa kwa ajili ya kurejesha umeme katika Bohari ya Dawa na Vifaa Tiba endapo umeme wa ZECO ukikakatika.

Kuwepo kwa uhaba wa mashine za kunyanyulia na kupanga mizigo ya dawa na vifaa tiba (Focal Lift) ndani ya Bohari ambapo kwa sasa ipo mashine moja na jumla ya mashine zinazohitajika ni mbili. Aidha mashine ya kunyanyulia shehena ya dawa iliyopo sasa ni kubwa ukilinganisha na nafasi inayotakiwa mashine hiyo kufanya kazi ambapo inapelekea kutokea kwa usumbufu mkubwa wakati wa kugeuka mashine hiyo kwenye njia zake inazotakiwa kupita na vile vile kutoweza kupanga mizigo ya dawa kwa baadhi ya maeneo. Hali halisi ya Bohari Kuu ya Dawa Pemba ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 6**.

b) Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba - Unguja

Kwa upande wa Unguja ukaguzi ulitembelea Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba iliyopo Maruhubi na kubaini dosari mbali mbali ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kuwepo kwa nafasi ndogo ya kuwekea shehena za dawa na vifaa tiba ndani ya ghala la Maruhubi ambapo hali hii imetokezea kutokana na kubanwa kwa ghala ili kuweza kujengwa Ofisi ya Bohari kupitia nafasi hiyo iliyopo. Kwa upande wa Pemba Ghala ni kubwa na nafasi nzuri kwa vile Ghala lake limetenganishwa na Ofisi ya Bohari ili kuweka mazingira vizuri.
- Kuwepo kwa nafasi ndogo katika chumba cha kompyuta za mifumo "Server Room" ukilinganisha na vifaa vilivyomo.
- Kutokuwepo na vifaa vya kuzimia moto katika chumba cha Kompyuta za Mifumo "Server Room".
- Kuwepo kwa uhaba wa vifaa vya kuzimia moto katika Ghala la Maruhubi.

Hali halisi ya Bohari Kuu ya Dawa Unguja ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 6**.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari za Unguja na Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi ili kuweza kurekebisha dosari zilizobainishwa.

2.4.1.19 Kutofanyika kwa Ukaguzi wa Ndani wa Dawa na Vifaa Tiba katika Hospitali.

Ukaguzi umebaini kwamba Kamati za Ukaguzi wa Ndani wa dawa na Vifaa Tiba (*Hospital Medicines and Therapeutic Committees*) zilizopo katika Hospitali na vituo vya afya hazifanyi zoezi la ukaguzi wa dawa na Vifaa tiba. Hali hii imepelekea Hospitali na vituo vingi vya Afya kutokuwa na kumbukumbu nzuri za upokeaji na usambazaji wa dawa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhamasisha Kamati za Ukaguzi wa ndani wa Dawa na Vifaa Tiba ili kuweza kufanya majukumu yao ipasavyo ikiwemo kufanya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya.

2.4.1.20 Kukosekana kwa Sera ya TEHAMA (ICT Policy)

Moja ya Taratibu zilizo bora za kusimamia Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi ni kuwepo na Sera za TEHAMA ambazo zitaeleza utaratibu mzima wa kutumia mifumo na vifaa vya TEHAMA katika Taasisi ili kuweza kuimarisha usalama wa vifaa na taarifa zilizopo.

Ukaguzi umebaini Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba haina sera za TEHAMA ambazo zingesaidia kuimarisha na kurahisisha matumizi ya mifumo iliyopo ndani yake.

Kutokuwa na sera za TEHAMA kunapelekea kuwepo kwa matumizi mabaya ya mifumo na kukosekana kwa usalama wa taarifa na vifaa vya TEHAMA vilivyopo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kuandaa na kuimarisha sera za TEHAMA ili kuweza kupatikana kwa matumizi bora ya mifumo na kuongezeka kwa usalama wa taarifa zilizomo.

SURA YA TATU

MUENDELEZO WA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA FEDHA (IFMIS) KATIKA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

3.0 UTANGULIZI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefunga Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS) kwa lengo la kusimamia fedha za Serikali kwa upande wa mapato na matumizi. Aidha mfumo wa IFMIS unafanya kazi katika hatua mbali mbali ikiwemo utayarishwaji wa bajeti ya Serikali, uingizwaji wa fedha, utekelezaji wa bajeti pamoja na utoaji wa ripoti za mapato na matumizi ya fedha kwa Mawizara, Idara, Wakala na Sekta za Umma.

3.1 UANZISHWAJI WA MFUMO WA IFMIS

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imeanzisha mfumo huo ikiwa ni moja ya hatua kubwa za maendeleo ya matumizi ya TEHAMA kwa Serikali katika kuimarisha utoaji wa huduma za fedha na kuongeza ufanisi, udhibiti, uwajibikaji, uwazi, usalama wa taarifa za fedha pamoja na utoaji wa taarifa sahihi za bajeti na taarifa za fedha.

Mfumo wa IFMIS umeanzishwa mwaka 2007 na kampuni ya **Soft Tech Consultants Ltd (STCL)** kupitia Mradi wa **Institutional Support Project for Good Governance** ikiwa ni Mkopo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (**African Development Bank**).

Aidha mfumo wa IFMIS una uwezo wa kuingiliana na mifumo mengine kwa vile unafanya kazi katika mazingira (Platform) ya **Window Based Operating System**.

Mfumo wa IFMIS umegawika katika moduli mbali mbali ikiwemo moduli ya wanaodai, moduli ya wanaodaiwa, moduli ya manunuzi, moduli ya mali za kudumu, moduli ya Daftari kuu la uhasibu, moduli ya usimamizi wa fedha taslim pamoja na moduli ya manunuzi mtandaoni.

Mfumo huo umeunganishwa na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA iliyopo katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Mawizara, Maidara pamoja na Mawakala ambapo miundombinu hiyo inasaidia katika kufanya mawasiliano na kusambaza taarifa za fedha pamoja na kuweka usalama wa taarifa za mfumo.

3.2 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa mfumo wa IFMIS umefanyika ikiwa ni muendelezo wa ukaguzi kwa mujibu wa Agizo lililotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** wakati wa uwasilishaji wa Ripoti za Mdhhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 - Ikulu Zanzibar tarehe 23 Mei 2021.

Malengo ya ukaguzi yalikuwa nikufanya tathmini ili kujiridhisha iwapo mfumo wa IFMIS unaisaidia Serikali katika usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali.

Tathmini hiyo ilifanyika kwa kuangalia kiwango cha utendaji kazi wa mfumo, udhibiti na usalama wa taarifa zilizohifadhiwa ndani yake , utunzaji wa siri, mipaka ya matumizi katika mfumo, uadilifu,ufanisi, tija, uwajibikaji wa watumiaji wa mfumo, urahisi wa upatikanaji wa taarifa ndani ya mfumo, pamoja na kuangalia muingiliano na mifumo mengine ya kifedha.

3.2.1 Udhibiti na Utendaji wa Mfumo

Kwa ujumla ukaguzi wa mfumo wa IFMIS ulijikita katika kupima mambo yafuatayo:-

- Udhibiti juu ya uingizaji wa taarifa/miamala ndani ya mfumo,
- Udhibiti juu ya uchakataji wa taarifa,
- Udhibiti juu ya utoaji wa ripoti, na
- Udhibiti juu ya taarifa zilohifadhiwa na mfumo na majalada makuu (Controls over standing data and master files).
- Mapitio ya mikataba inayohusika na huduma za TEHAMA.
- Utendaji wa mfumo kuhusiana na muda sahihi wa upatikanaji wa taarifa.
- Ulinganisho baina ya taarifa za fedha zinazotoka ndani ya mfumo wa IFMIS pamoja na Taarifa za fedha kutoka Taasisi nyengine za kifedha kama vile BOT, PBZ, TRA na MDAs.
- Ulinganisho wa gharama zinazotumika kwa ajili ya kuendeshea mfumo pamoja na hali halisi ya utendaji wa mfumo.

3.3 UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi wa mfumo wa IFMIS umefanyika kwa mujibu wa viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa. Aidha ukaguzi uliangalia mwenendo halisi wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha kwa Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwaka wa fedha 2020/2021.

Taarifa za fedha zilizokaguliwa zimepatikana kupitia vyanzo tofauti ikiwemo taarifa kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika Tawi la Zanzibar pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) katika Tawi la Zanzibar. Hata hivyo katika muendelezo huo, ukaguzi haukuangalia vielelezo halisi ya vyanzo vya mapato kutoka katika Wakala wa Kukusanya Mapato Serikalini na Mawizara mengine kutokana na kwamba lengo kuu la muendelezo wa ukaguzi wa mfumo wa IFMIS ni kuangalia uwezo wa mfumo katika kujilinda na udukuzi kwa njia ya mtandao (Cyber attack), usalama wa mfumo (IT Security) pamoja na mwenendo wa taarifa za fedha katika mfumo, na hatimae kuishauri Serikali kuhusiana na usahihi wa miamala ya fedha inayofanyika ndani ya mfumo.

3.4 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Katika kufanya ukaguzi wa Mfumo wa IFMIS njia na mbinu mbali mbali zilitumika ili kupata uelewa wa mfumo pamoja na utendaji wake wa kazi. Katika kufanya ukaguzi taratibu zifuatazo zilitumika:-

- Kutoa barua ya awali za maandalizi ya ukaguzi kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

- Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) na uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.
- Kupitia taarifa za fedha zinazotoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kufanya tathmini ya vihatarishi katika taarifa za fedha za mfumo wa IFMIS.
- Kupitia taarifa za fedha zinazotokana na mfumo wa IFMIS pamoja na taarifa za fedha za kitengo cha Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Kukusanya taarifa na kufanya mahojiano na wahusika kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
- Kufanya ukaguzi kwa taarifa za fedha zilizopatikana.
- Kufanya kikao cha kumaliza kazi za ukaguzi (Exit meeting) na uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango baada ya kumaliza ukaguzi.
- Kutoa ripoti ya muendelezo wa ukaguzi na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa utaratibu.

3.5 CHANGAMOTO ZA UKAGUZI

Katika kufanya zoezi la muendelezo wa ukaguzi wa Mfumo wa IFMIS kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, taarifa mbali mbali ziliombwa na wakaguzi ili kuweza kuangalia na kuthithibisha usahihi na ukamilifu wa taarifa hizo. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa taarifa hizo kikamilifu. Hii ina maana ya kwamba kuna baadhi ya taarifa ziliombwa lakini zimepatikana pungufu na kuna baadhi ya taarifa hazikupatikana kabisa. Hali hii imepelekea kuathiri upeo wa ukaguzi. Miongoni mwa taarifa zilizokuwa pungufu na zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

Jadweli Nambari 5 : Taarifa zilizokuwa pungufu na zilizokosekana

Namba	Taarifa iliyoombwa	Taarifa iliyokosekana	Kitengo Husika
1	Mikataba halisi yenye kuonesha gharama za ununuzi (utengenezaji) wa mfumo wa IFMIS	<ul style="list-style-type: none"> • Mikataba halisi (original contract document) wa awali wa utengenezaji wa mfumo wa IFMIS (EPICOR Version 7). • Mikataba halisi wa pili (original contract document) wa kuimarisha mfumo (EPICOR Version 10). • Mikataba halisi ya uboreshaji wa utoaji wa huduma (SLA) kwa kipindi cha mwaka 2007 hadi 2014 (original contract document). • Mikataba halisi ya uboreshaji wa utoaji wa huduma (SLA) kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 (original contract document). • Mikataba yenye kuonesha gharama za malipo ya leseni ya matumizi ya Mfumo wa IFMIS kwa kipindi cha mwaka 2007 hadi 2021. 	Application/Technical/Mwanasheria.

2	Taarifa za hesabu za Benki za mapato (Bank Statements).	<p>Taarifa za hesabu za benki za mapato ya kodi ya TRA :-</p> <ul style="list-style-type: none"> • 0754715001 – TRA Zanzibar Dom. Revenue GEPG iliyopo PBZ. • 0754716001 – TRA Zanzibar Cust. and Excise GEPG iliyopo PBZ. • 021101000179/0701695000 – Dep.Comm. Dom. Revenue Tax Bank iliyopo PBZ. • 041103000015/0404368000 – Dep.Comm. Cust. and Excise iliyopo PBZ Pemba. • 041103000070/040403983 – Dep.Comm. Dom. Revenue iliyopo PBZ Pemba. • 041103000069/040404313 – Dep.Comm. Dom. Revenue iliyopo PBZ Pemba. 	Exchequer
3	Taarifa za usuluhishi wa hesabu za kibenki (Bank Reconciliation)	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa za usuluhishi wa hesabu za kibenki za mapato yasiyokuwa ya kodi zilizopo katika benki za kibiashara kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020. • Taarifa za usuluhishi wa hesabu za kibenki za mapato yasiyokuwa ya kodi zilizopo BOT kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. 	IFMIS Revenue
4	Taarifa za uthibitisho wa Bakaa za hesabu za benki (Bank Confirmation Certificates)	Taarifa za uthibitisho wa Bakaa za hesabu za benki za kitengo cha Hazina zilizopo PBZ.	Exchequer
5	Fedha zilizopelekwa Hazina Pemba.	Fedha zilizopelekwa Hazina Pemba kwa kipindi mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021.	Exchequer
6	(Standing Order)	<ul style="list-style-type: none"> • Standing Order za kuhamisha mapato yanayotokana na kodi kutoka hesabu zilizopo PBZ kwenda BOT. • Standing Order za kuhamisha mapato yanayotokana na kodi kutoka hesabu zilizopo BOT kwenda hesabu ya Exchequer Revenue iliyopo BOT. • Standing Order za kuhamisha mapato yasiyokuwa ya kodi kutoka hesabu zilizopo BOT kwenda hesabu ya Exchequer Revenue kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020. 	

7	Taarifa za usuluhishi wa kibenki (Bank Reconciliation)	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa za usuluhishi wa hesabu za kibenki za CPO (Recurrent, Development na Public Dept) kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2017/2018. • Taarifa za usuluhishi wa hesabu za kibenki za hesabu ya CPO - Miscellaneous Deposit kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021. 	CPO
---	--	--	-----

3.6 HALI HALISI YA KIWANGO CHA UTUMIAJI WA MFUMO WA IFMIS KWA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO, WIZARA, IDARA PAMOJA NA WAKALA WA SERIKALI (MDAs).

3.6.1 GHARAMA ZILIZOTUMIKA KATIKA MFUMO WA IFMIS

Mfumo wa IFMIS umetumia gharama mbali mbali katika utekelezaji wake kwa kujumisha gharama za Ununuzi wa mfumo, gharama za kuimarishwa (kubadilishwa), gharama za utoaji wa huduma za mfumo pamoja na gharama za leseni ya matumizi.

3.6.2 Gharama za Ununuzi wa Mfumo wa IFMIS

Mfumo wa IFMIS ulianza kutumika mwaka 2007 katika Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ambapo ulianza kutumia programu ya **EPICOR Version 7**. Hata hivo ukaguzi umeshindwa kujua gharama halisi zilizotumika katika manunuzi ya mfumo huo pamoja na leseni za utumiaji kwa awamu ya kwanza mwaka 2007 kutokana na kukosa kupatikana Mikataba wa awali kuhusiana na manunuzi pamoja na uendeshaji wa mfumo huo.

3.6.3 Gharama za kuimarishwa Mfumo wa IFMIS USD 355,275.40

Mnamo mwaka wa fedha 2015 mfumo wa IFMIS ulibadilishwa kwa kuimarishwa kutoka **EPICOR Version 7** na kuhamia programu ya **EPICOR Version 10** kupitia mkataba uliofungwa tarehe 30 Disemba 2014 baina ya Wizara ya Fedha Zanzibar na kampuni ya M/S Soft – Tech Consultants Ltd iliyopo Dar es Salaam yenye nambari ya usajili 2300. Mkataba huo ulikuwa na gharama za **USD 355,275.40 (Bila ya VAT)** ambapo gharama hizo zilikuwa ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (African Development Bank) kupitia mradi wa "Institutional Support Project for Good Governance (ISPGG - II)" **Kiambatisho Nambari 7 Kinahusika.**

Kwa sasa mfumo wa IFMIS unatumia programu ya **EPICOR Version 10.1.4**. ambapo lengo la kubadilishwa mfumo kutoka EPICOR Version 7 kwenda EPICOR Version 10 lilikuwa ni kama ifutavyo:-

- Mabadiliko ya Teknolojia.
- Kuongeza ufanisikwa watumiaji wa mfumo.
- Upatikanaji rahisi wa taarifa.
- Udhibiti mzuri wa ubora wa mfumo pamoja na gharama.

- e) Upatikanaji wa moduli nyingi za kiuhasibu (Multiple Chart of Accounts).
- f) Wepesi kufanya mageuzi (Flexibility on taking reforms).

Aidha Mkataba huu ulikuwa na dhumuni la kutanua mfumo wa IFMIS kwa kuongeza sehemu za Tawala za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

3.6.4 Gharama za Utoaji wa Huduma katika Mfumo wa IFMIS shilingi 409,554,400.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inalipa fedha kwa kampuni ya M/S Soft – Tech Consultants Ltd kwa kila mwaka ikiwa ni gharama za matengenezo ya mfumo pamoja na gharama za utoaji wa huduma katika mfumo wa IFMIS "Maintenance Support and Services". Gharama hizo hulipwa kupitia mikataba ya makubaliano ya utoaji wa huduma "Service Level Agreement – SLA" ambapo fedha hizo zimeanza kulipwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 na bado zinaendelea kulipwa kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 6: Gharama zinazolipwa za "SLA" kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021.

Nambari	Mwaka wa Fedha	Gharama anazolipwa Mtengenezaji wa Mfumo (Shs)	Kodi ya Thamani (VAT) (Shs.)	Jumla ya Gharama (VAT -Inclusive) (Shs.)
1.	2018/2019	125,000,000	22,500,000	147,500,000
2.	2019/2020	125,000,000	22,500,000	147,500,000
3.	2020/2021	97,080,000	17,474,400	114,554,400
Jumla ya Gharama		347,080,000	62,474,400	409,554,400

Kwa hivyo jumla ya gharama zilizolipwa za "SLA" kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi mwaka wa fedha 2020/2021 ni shilingi 409,554,400. **(Kiambatisho Nambari 8 Kinahusika).**

3.6.5 Gharama za Leseni ya Matumizi ya Mfumo wa IFMIS

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inalipa fedha kwa kampuni ya M/S Soft – Tech Consultants Ltd kwa ajili ya leseni ya matumizi ya mfumo wa IFMIS. Hata hivyo ukaguzi haukupatiwa mikataba ya malipo ya leseni hizo kwa kila mwaka ya mfumo wa IFMIS kwa ajili ya ukaguzi ili kujua gharama halisi zilizolipwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

3.7 KIWANGO CHA UTUMIAJI WA MFUMO WA IFMIS KATIKA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kuangalia taarifa za Mfumo wa IFMIS zilizotumika kwa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2020/2021 kwa upande wa Moduli zilizounuliwa dhidi ya Moduli zinazotumika, ukaguzi umebaini Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imelipia jumla ya Moduli kumi na tano (15) kwa ajili ya matumizi ya mfumo. Kati ya hizo moduli nane (8) ndio zinazotumika sawa na asilimia 60 ya matumizi ya Mfumo na Moduli saba (7) hazitumiki ipasavyo ambapo matumizi yake ni madogo sawa na wastani wa asilimia 40.


Taarifa za matumizi ya Moduli zimepatikana kutokana na miamala iliyokuwa ikifanywa katika Mfumo wa IFMIS ambapo taarifa hizo zimepatikana kutoka kwenye leja ndogo (sub ledgers) kama vile "Account Payables, Account Receivables, Cash Managements, Purchase Managements, Shipping/receiving managements, Budget Management, General Ledger, Imprest Managements, Assets Managements, Inventory Managements, Multiple Books, Multi Currency, Report Portal, Commitment Expenditure, Executive Analysis " .

Jadweli lifuatalo linaonesha baadhi ya Moduli na kiwango cha matumizi yake kwa mujibu wa hesabu za taarifa "Data Counts" zilizo ndani ya moduli za mfumo wa IFMIS.

Jadweli Nambari 7 : Viwango vya matumizi ya moduli za mfumo wa IFMIS

Nambari	Moduli zenye leseni	Kiwango cha matumizi ya Moduli kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2020/2021	Wastani wa Kiwango cha Matumizi ya Moduli kwa mwaka
1	Accounts Payable	415,589	69,265
2	Accounts Receivable	114,626	19,104
3	Cash Management	145,674	24,279
4	General Ledger – Exchequers	3,532	589
5	General Ledger – Budgets	2,220	370
6	Purchase Management	983	164
7	Shipping/ Receiving of PO	827	138
8	Imprest Management	6	1
9	Asset Management	0	0
10	Inventory Management	0	0

Ufafanuzi wa taarifa hizi unaonekana katika mchoro ufuatao:-



Kutokana na uchambuzi uliopo hapo juu ukaguzi umebaini kwamba pamoja na gharama zilizotumika na zinazoendelea kutumika katika kugharamia uendeshaji wa mfumo wa IFMIS lakini bado kiwango cha matumizi ya mfumo hakiendani na gharama za matumizi ya mfumo huo.

Hali hii inamaanisha kwamba kuna baadhi ya kazi zinafanyika "manually" bila ya kupitia mfumo wa IFMIS, vile vile zinafanyika kupitia mifumo mengine ambayo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imeanzisha ambayo haina tija kwa vile mfumo wa IFMIS unaweza kufanya kazi hizo sawa sawa lakini hautumiki.

3.7.1 Moduli ya Ununuzi na Upokeaji (Procurement and Receiving Module)

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa moduli ya Ununuzi ili kujua ni kwa kiwango gani ununuzi wa Serikali unafanyika kupitia mfumo wa IFMIS ili kuhakikisha kunakuwepo kwa udhibiti mzuri wa fedha kwa kuzingatia bajeti.

Ukaguzi umebaini katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2020/2021, moduli ya ununuzi imetumika kwa kipindi cha mwaka mmoja tu 2015/2016 ambapo mafungu (votes) 33 yalitumia moduli hiyo sawa na asilimia 83 ya mafungu yote, na kupelekea asilimia 17 ya mafungu yaliyobakia kutokufanya kazi katika mfumo wa IFMIS au kutokutumika kabisa.

Jumla ya taarifa 983 za ununuzi (Purchase order) zilifanyika katika Mfumo wa IFMIS ambapo kati ya hizo "Purchase Order 827" zilitumika katika mfumo wa IFMIS. Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa taarifa za manunuzi "Purchase order" 772 zenye Ankara ya malipo yake hayakufanyika kupitia mfumo wa IFMIS (**Kiambatisho Nambari 9 Kinahusika**).

Hali hii inaonesha kwamba mfumo wa IFMIS haukuweza kutumika kwa shughuli za manunuzi na upokeaji wa bidhaa na huduma za Serikali zilizoagizwa kutoka 2016/2017 hadi 2020/2021.

3.7.2 Moduli ya Usimamizi wa Malipo ya Masurufu (Imprest Management)

Moduli ya "Imprest Management" ambayo hutumika kwa kufanya malipo ya masurufu kwa watendaji mbali mbali, moduli hii imetumika kwa kiwango cha wastani wa muamala mmoja (1) kwa mwaka jambo ambalo linapelekea Serikali kuendelea kupata hasara ya kulipia moduli hiyo ambayo haitumiki ipasavyo.

Aidha katika uchambuzi wa taarifa, ukaguzi uliangalia usimamizi wa malipo ya masurufu kupitia mfumo kwa lengo la kuweza kujiridhisha ya kwamba masurufu yote yanalipwa kupitia utaratibu wa mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi umebaini kwamba "Votes" mbili zimetumia moduli ya "Imprest" katika mfumo IFMIS kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Hadi ukaguzi unakamilika hakuna malipo yoyote ya masurufu ambayo yalifanyika kupitia mfumo wa IFMIS.

Kwa ujumla mfumo wa IFMIS hautumiki kufanya malipo kwa njia ya masurufu jambo ambalo linaweza kutiliwa shaka juu ya utaratibu unaotumika wa malipo ya masurufu kufanyika nje ya mfumo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali.

3.7.3 Moduli ya Usimamizi wa Mali na Moduli ya Vifaa vya Ghalani (Assets and Inventory Management)

Moduli ya Usimamizi wa Mali hutumika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na Usimamizi mali zote za Taasisi (mali za mpito na mali zisizokuwa za mpito) pamoja na kumbukumbu zinazohusiana nazo kama vile ununuzi wa mali, uchakavu wa mali, tathmini ya mali pamoja na uondoshaji wa mali.

Aidha moduli ya Vifaa vya Ghalani hutumika kuweka kumbukumbu za vifaa vya ghalani ikiwemo taarifa za ununuzi, thamani na utoaji wa vifaa vya ghalani.

Ukaguzi umebaini kwamba moduli hizo mbili hazijawahi kutumiwa kabisa, licha ya kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mali nyingi za mpito na mali zisizo za mpito ambazo zinahitaji kurikodiwa na kusimamiwa katika njia ya uwazi na uwajibikaji kwa kutumia mfumo wa IFMIS.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imenunua Mfumo mwengine kwa ajili ya kufanya shughuli za kuweka kumbukumbu na kusimamia mali zote za Serikali, ingawa mfumo wa IFMIS ulikuwa na uwezo wa kufanya shughuli hizo za uwekaji wa kumbukumbu za mali na vifaa vya Serikali.

3.7.4 Moduli ya Wadaiwa / Usimamizi wa Fedha Taslim (Accounts Receivable/ Cash Management)

Moduli hizi zina uwezo wa kurikodi madeni yote ya Serikali na kufuta madeni wakati fedha zinapo pokelewa. Ukaguzi umebaini moduli hizi zinatumiwa ingawa hazitumiki kikamilifu, hii inamaanisha miamala ya kupokea fedha taslimu hairikodiwi kwa wakati husika ndani ya mfumo wa IFMIS.

3.7.5 Usuluhisho wa Benki (Bank Reconciliation)

Ukaguzi umebaini kwamba taarifa za Usuluhisho wa Kibenki kwa hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo haziantaliwi kwa kutumia Mfumo wa IFMIS, badala yake upatanishi unafanyika kwa kutumia Programu ya **Treasury Management System - TMS**.

Ukaguzi huu haukuweza kuona sababu za kutumia Programu ya TMS kwa ajili ya kuandaa upatanisho wa Kibenki hali ambayo Mfumo wa IFMIS unaweza kufanya kazi sawa kama kazi zinazofanywa na programu ya TMS jambo ambalo lingelipelekea kuweza kuokoa gharama kubwa ya matengenezo ya mfumo inayolipiwa ambazo hutofautiana kwa kadiri ya leseni zinazotumika.

3.7.6 Hesabu za benki za Serikali.

Ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu za benki za mapato na matumizi zilizokuwa zikitumiwa kwa kukusanya mapato na kufanya matumizi ya Serikali. Kwa upande wa mapato ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu 43 zilizopo benki ya BOT na hesabu 76 zilizopo benki ya PBZ ambazo hukusanya mapato yasiyokuwa ya kodi.

Kati ya hesabu 76 zilizopo PBZ ambazo zinakusanya mapato yasiyokuwa ya kodi, hesabu 12 ni kwa ajili ya kukusanya mapato ya fedha za kigeni "USD" na hesabu 64 zinakusanya mapato ya fedha za Kitanzania "Shs."

Kwa upande wa mapato yanayotokana na kodi ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu 6 za TRA za kukusanyia mapato ambapo hesabu 4 zipo PBZ na hesabu 2 zipo BOT. Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu 3 za ZRB za kukusanyia mapato ambapo hesabu mbili zipo PBZ na hesabu 1 ipo BOT. **(Kiambatisho Nambari 10 Kinahusika).**

Aidha ukaguzi ulibaini hesabu zote za kukusanyia mapato yanayotokana na kodi na yasiyokuwa ya kodi hazijaunganishwa kwenye mfumo wa IFMIS. Aidha ukaguzi haukupata taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020 kwa hesabu zinazokusanya mapato yasiyokuwa ya kodi jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha iwapo taarifa za fedha zilizoripotiwa zinawiana na vitabu vya fedha taslimu na taarifa za kibenki.

Kwa upande wa matumizi ya Serikali, hesabu za matumizi zimegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni hesabu za matumizi kupitia Ofisi Kuu ya Malipo (CPO) na hesabu za matumizi kupitia kitengo cha Hazina.

Kwa upande wa CPO ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu 5 zilizopo BOT ambazo ni; "Central Payments recurrent TISS, Central Payments Capital TISS, Central Payments Public Debts TISS, Misc Deposit Accounts, na Unapplied bank account".

Kwa upande wa kitengo cha Hazina ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu 4 zilizopo BOT ambazo zinakusanya mapato nazo ni "Exchequer Recurrent Revenue, GoZ External Revenue, GoZ PAYE Revenue – SMT na Treasury Bond Account".

Aidha imebainika uwepo wa hesabu 3 za benki ambazo hufanya matumizi zilizopo BOT ambazo ni "Exchequer Recurrent Expenditure, Exchequer Development Expenditure na Exchequer Consolidated Fund", vile vile imebainika uwepo wa hesabu 4 za benki zilizopo PBZ ambazo hukusanya mapato na kufanya matumizi ambazo ni Hesabu ya Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu, hesabu ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ya fedha za kigeni, hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina na hesabu ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Ukaguzi umebaini hesabu zote za mapato na matumizi ya kitengo cha Hazina hazijaunganishwa na mfumo wa IFMIS, jambo ambalo limepelekea kitengo hicho kuweka kumbu kumbu za mapato na matumizi ya Serikali nje ya mfumo kwa kutumia madaftari kwa njia ya mkono (Kiambatisho Nambari 11 Kinahusika).

3.8 MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

3.8.1 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi uliweza kubaini dosari mbali mbali ambazo zimeelezwa kwa njia tofauti ikiwemo dosari katika uhakiki wa mfumo wa IFMIS pamoja na taarifa za fedha katika mfumo Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

3.8.1.1 Taarifa za hesabu za Hazina ambazo hazikuunganishwa na Mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu mbali mbali za Hazina za mapato na matumizi zilizopo Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambazo hazikuunganishwa kwenye Mfumo wa matumizi ya fedha za Serikali na taarifa za fedha za hesabu hizo hurikodiwa katika madaftari ya fedha kwa njia ya mkono (Manually).

Orodha za hesabu hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 8: Taarifa za hesabu za hazina zilizokuwa hazijaunganishwa kwenye mfumo.

Namba	Jina la Hesabu	Nambari ya Hesabu	Hali ya Hesabu
Hesabu za Benki za Mapato			
Benki Kuu ya Tanzania (BOT)			
1.	Exchequer Recurrent Revenue	9928170104	Inatumika
2.	GOZ External Revenue	9928139804	Inatumika
3.	GOZ PAYE Revenue – SMT	9928139904	Inatumika
4.	Treasury Bonds	9928170504	Inatumika

Hesabu za Benki za Mapato na Matumizi			
Benki Kuu ya Tanzania (BOT)			
1.	Exchequer Recurrent Expenditure	9928170704	Inatumika
2.	Exchequer Development Expenditure	9928170804	Inatumika
3.	Exchequer Consolidated Fund	9928170904	Inatumika
Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)			
1.	Infrastructure Fund	0403861000	Inatumika
2.	Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango-Zanzibar (Mfuko Mkuu wa Hazina – Fedha za Kigeni)	0400762000	Inatumika
3.	Mfuko Mkuu wa Hazina	0404381000	Inatumika
4.	Katibu Mkuu Wizara ya Fedha	021101000164	Imefungwa

3.8.1.2 Hesabu za mapato ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali ambazo hazikuunganishwa na Mfumo wa IFMIS

Ukaguzi umebaini uwepo wa hesabu mbali mbali za makusanyo ya mapato kwa Wizara na Idara za Serikali ambazo zinakusanya mapato yasiyokuwa ya Kodi (Non-Tax Revenue) na mapato ya kodi (Tax Revenue) ambapo hesabu hizo hazikuunganishwa kwenye Mfumo wa IFMIS, badala yake taarifa za mapato hurikodiwa katika madaftari ya fedha kwa njia ya mkono (Manually). Hali hiyo inapelekea kutokupatikana kwa taarifa sahihi za mapato kutoka katika Wizara au Idara husika kupitia Mfumo wa IFMIS. Orodha ya Wizara na taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 10.**

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa hesabu zote za mapato za Hazina zilizopo katika benki ya BOT na PBZ pamoja na hesabu za mapato kutoka Wizara na Idara za Serikali zinaunganishwa na Mfumo wa IFMIS moja kwa moja ilikuweka udhibitimzuri wataarifa za fedha za mapato na matumizi.

3.8.1.3 Dosari za taarifa za Usuluhishi wa kibenki kwa hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika uandaaji wa taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa Hesabu za CPO zilizoko Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Dosari zenyewe ni kuwa baadhi ya miezi haikuwa na taarifa za usuluhishi wa kibenki zilizokubaliana na bakaa za mwezi husika. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti kati ya bakaa ya fedha kwa mujibu wa daftari la fedha taslim la IFMIS na bakaa ya fedha baada ya kuandaa taarifa ya usuluhishi wa kibenki. Tofauti zilizobainika ni kama ilivyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 9: Tofauti zilizobainika katika taarifa za usuluhishi wa kibenki za hesabu za Ofisi kuu ya malipo

Namba	Nambari ya Hesabu	Jina la hesabu	Tarehe	Bakaa ya Fedha kwa mujibu wa Daftari la Fedha Taslim la IFMS (Tshs)	Bakaa ya Fedha kwa mujibu wa taarifa ya Usuluhishi wa kibenki (Tshs)	Tofauti (Tshs.)
1	9928182104	Hesabu ya Public Debt	31-Oct-19	6,025,476,809	6,025,476,809	(3,828,000)
2	9928182104	Hesabu ya Public Debt	31-Jul-19	6,850,767,050	6,827,296,050	(23,471,000)
3	9928182104	Hesabu ya Public Debt	31-Jan-19	12,062,978,714.55	12,737,950,875.65	674,972,134.10
4	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	30-Mar-20	9,274,033,285.27	9,268,203,615.27	(5,829,670)
5	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	31-May-20	12,861,244,528.63	12,861,219,528.63	(25,000.00)
6	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	30-Apr-19	13,478,451,627.34	13,725,907,947.34	247,456,320.00
7	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	31-Jul-19	6,850,767,050.00	6,827,296,050.00	(23,471,000.00)
8	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	31-Mar-19	23,299,610,482.44	23,547,066,802.44	247,456,320.00
9	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	28-Feb-19	28,724,925,190.34	28,721,636,601.29	(3,288,589.05)
10	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	31-Jan-19	26,640,433,739.51	28,634,443,550.46	(5,990,189.05)
11	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	31-Jul-18	8,847,484,357.82	8,814,533,625.82	(32,950,732.00)
12	9928182004	Hesabu ya Matumizi ya kawaida	30-Nov-18	22,600,878,710.08	22,597,968,710.08	(2,910,000.00)

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa Taarifa za usuluhishi za mwisho wa mwaka (mwezi wa Juni) hazionyeshi kiasi cha miamala ambayo inapaswa kuingizwa katika taarifa ya usuluhishi ikiwemo malipo yasiyo ya fedha taslim (**Kiambatisho Nambari 12 Kinahusika**). Baadhi ya miezi iliyobainika ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 10: Taarifa za fedha ambazo hazikuoneshwa katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki za mwisho wa mwaka.

Namba	Tarehe ya Taarifa ya Usuluhishi wa Kibenki	Mapato yaliyoripotiwa katika Taarifa ya Usuluhishi wa Kibenki kuwa yanaonekana katika Daftari la Fedha Taslim pasi na Kuonekana Benki (Mapato yasiyo Taslim)	Kiasi Halisi cha Mapato yasiyo ya Fedha Taslim Yaliyobainika katika Daftari la 'Cash Book'
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida – 9928182004			
1.	30-Juni-2019	0	1,225,060,847
2.	30-Juni-2020	0	557,762,641
3.	30-Juni-2021	0	37,930,599,035
Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo – 9928190704			
1.	30-Juni-2019	0	238,124,279,510
2.	30-Juni-2020	0	27,216,561,562
3.	30-Juni-2021	0	53,047,873,127
Hesabu ya Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu – 9928182104			
1.	30-Juni-2017	0	22,306,424,725
2.	30-Juni-2018	0	11,943,792,354
3.	30-Juni-2019	0	11,026,878,968
4.	30-Juni-2020	0	1,409,829,582
5.	30-Juni-2021	0	6,389,258,016

3.8.1.4 Fedha zilizotumika nje ya Mfumo wa Usimamizi wa fedha za Serikali (IFMIS).

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa matumizi ya fedha yaliyofanyika nje ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali katika Ofisi Kuu ya Malipo ya Serikali (CPO) kupitia Wizara tofauti kutoka katika hesabu mbali mbali ambazo hazijaunganishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali, fedha ambazo huingizwa katika Mfumo ikiwa ni matumizi yasiyo ya fedha taslimu (Dummy). Hali hii inaweza kuathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti ya matumizi ya fedha kupitia Mfumo.

Ufuatao ni uchambuzi wa matumizi yanayofanyika nje ya mfumo kwa Hesabu ziliopo Ofisi Kuu ya Malipo (CPO).

Jadweli Nambari 11: Uchambuzi wa matumzi ya fedha yaliyofanyika nje ya mfumo wa IFMIS

Mwaka wa fedha	Kiasi cha matumizi yote kwa mwaka (Tshs)	Matumizi yaliyofanyika nje ya Mfumo kwa mwaka (Tshs)	Matumizi yaliyofanyika ndani ya Mfumo kwa mwaka (Tshs)	Asilimia ya matumi zi yaliyofanyika nje ya Mfumo	Asilimia ya matumizi yaliyofanyika ndani ya Mfumo
Hesabu ya Public Debt - 9928181704/9928182104					
2016/2017	151,992,145,939	84,319,080,306	67,673,065,633	55.48	44.52
2017/2018	143,384,251,201	59,318,255,724	84,065,995,477	41.37	58.63
2018/2019	164,726,179,980	65,671,070,567	99,055,109,413	39.87	60.13
2019/2020	159,603,875,705	43,417,698,013	116,186,177,692	27.2	72.8
2020/2021	197,405,701,192	40,349,043,702	157,056,657,490	20.44	79.56
Jumla kwa miaka mitano (5)	817,112,154,017	293,075,148,312	524,037,005,705	36.87	63.13
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida - 9928181804/9928182004					
2016/2017	316,682,677,488	17,931,513,446	298,751,164,042	5.66	94.34
2017/2018	478,378,026,432	10,513,070,102	467,864,956,330	2.2	97.8
2018/2019	553,174,487,536	18,255,318,260	534,919,169,276	3.3	96.7
2019/2020	568,647,621,348	13,116,671,817	555,530,949,531	2.31	97.69
2020/2021	535,418,437,483	48,143,290,714	487,275,146,769	8.99	91.01
Jumla kwa miaka mitano (5)	2,452,301,250,287	107,959,864,339	2,344,341,385,948	4.49	95.51
Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo - 9928190604/9928190704					
2016/2017	141,818,284,217	101,939,820,182	39,878,464,035	71.88	28.12
2017/2018	244,780,048,938	192,054,874,212	52,725,174,726	78.46	21.54
2018/2019	340,929,537,330	290,329,780,248	50,599,757,082	85.16	14.84
2019/2020	212,814,576,026	134,624,312,536	78,190,263,490	63.26	36.74
2020/2021	115,752,785,741	72,621,994,923	43,130,790,818	62.74	37.26
Jumla kwa miaka mitano (5)	1,056,095,232,252	791,570,782,101	264,524,450,151	72.3	27.7

3.8.1.5 Matumizi katika hesabu ya benki ya Katibu Mkuu nambari 021101000164 iliyoko PBZ iliyofungwa

Ukaguzi umebaini kuwa kuna matumizi ya fedha yenye jumla ya shilingi 4,672,307,351 yamefanyika katika kipindi cha miaka miwili (Julai, 2016 hadi Jan, 2018) nje ya mfumo wa IFMIS kupitia hesabu ya 'Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango' yenye nambari 021101000164 iliyokuwa PBZ na matumizi ya fedha hizo hayakuingizwa kabisa katika mfumo huo wa IFMIS. Hii inapelekea matumizi hayo kutokuathiri na kutokutegemea bajeti iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha kufanyika malipo kwa utaratibu huu kunaweza kupelekea kufanyika malipo ambayo tayari yameshalipwa katika Mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi umepitia Taarifa za benki pamoja na hati za malipo za hesabu hiyo na kubaini matumizi yafuatayo:-

Jadwali Nambari 12 : Matumizi yaliyofanyika katika hesabu ya Katibu Mkuu nje ya Mfumo wa IFMIS

Namba	Mwezi	Kiasi Kilichotumika (Shs)	Maelezo
1	Julai, 2016	1,277,451,322	Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na Pensheni ya Wazee Unguja Tsh. 314,521,800, Pensheni ya Wazee Pemba Tsh. 185,263,200 na fedha kwa ajili ya matumizi maalum ya Baraza la Wawakilishi Tsh. 100,000,000 pamoja na matumizi maalum kwa huduma za viongozi wakuu.
2	Agosti, 2016	217,528,955	Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na Pensheni ya Wazee Pemba Tsh. 197,078,000
3	Septemba, 2016	50,022,000	Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na msaada kwa waathirika wa tetemeko – Kagera, Tsh. 50,000,000
4	Oktoba, 2016	2,032,000	Fedha kwa ajili ya matibabu ya viongozi wakuu.
5	Novemba, 2016	503,012,000	Fedha zilizoazimwa katika mradi wa ZUSP kwa ajili kulipia fidia kwa walioathirika na upitishaji wa mitaro, Tsh. 503,000,000
6	Disemba, 2016	40,030,000	Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na matumizi maalum ya Serikali, Tsh. 40,000,000
7	Januari, 2017	14,355,000	Fedha kwa ajili ya matumizi maalum ya Serikali
8	Februari, 2017	10,000	

9	Machi, 2017	2,477,755,574	Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na uhaulishaji wa Tsh. 2,477,735,574.80 kwenda hesabu ya mapato ya hazina EXCHEQUER RECURRENT REVENUE yenye nambari 9928170104 iliyoko BOT kwa ajili ya kuifunga Hesabuu ya 'Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango' yenye nambari 021101000164 iliyokuwa PBZ.
10	April, 2017	10,000	Gharama za benki
11	Mei, 2017	20,000	Gharama za benki
12	Juni, 2017	20,000	Gharama za benki
13	Julai, 2017	20,000	Gharama za benki
14	Agosti, 2017	20,000	Gharama za benki
15	Septemba, 2017	0	Hakuna matumizi
16	Oktoba, 2017	0	Hakuna matumizi
17	Novemba, 2017	0	Hakuna matumizi
18	Disemba, 2017	0	Hakuna matumizi
19	Januari, 2018	90,020,500	Uhaulishaji wa fedha kwenda hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina yenye nambari 051103000084 iliyopo PBZ kwa ajili ya ufungaji wa hesabu.
	Jumla	4,672,307,351	

3.8.1.6 Matumizi katika hesabu ya CPO Recurrent Expenditure 9928181604 iliyoko BOT yanayofanyika nje ya Mfumo.

Ukaguzi umebaini kuwa kuna matumizi ya fedha yanafanyika nje ya mfumo wa IFMIS kupitia hesabu ya CPO Recurrent Expenditure 9928181604 iliyoko BOT na matumizi yake hayakuonekana katika mfumo wa IFMIS pamoja na hati za malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Ukaguzi umepitia Taarifa za benki za hesabu hiyo na kubaini kufanyika matumizi yafuatayo katika kipindi cha miaka 5 iliyopita:-

Jadweli Nambari 13: Matumizi katika hesabu ya CPO iliyopo BOT yanayofanyika nje ya Mfumo

Namba	Mwaka wa Fedha	Fedha zilizoingizwa (Tshs.)	Fedha zilizotumika (Tshs.)
1	2016/2017	4,494,148,284.85	4,494,148,284.85
2	2017/2018	235,905,796	235,905,796
3	2018/2019	395,203	395,203
4	2019/2020	395,203	395,203

3.8.1.7 Taarifa zilizokosekana kwa ukaguzi

Kwa mujibu wa barua yenye Kumb. Na. BC.195/393/01/20 ya tarehe 13 Machi, 2017 kutoka Wizara ya Fedha kwenda Benki ya Watu za Zanzibar inayohusu ufungaji wa hesabu ya 'Katibu Mkuu Wizara ya Fedha' yenye namba 021101000164, ukaguzi umebaini uwepo wa taarifa za hesabu za mapato zilizopo BOT na PBZ ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Taarifa za hesabu za benki zilizokosekana kwa ukaguzi ni kama zifuatazo:-

- a) Taarifa za Benki za Hesabu za mapato za Wizara zilioko Benki Kuu ya Tanzania BOT yenye jina "Min of Finance, Eco Affairs Rec. Rev" nambari 9928140334.
- b) Taarifa za Benki za Hesabu za mapato za Wizara zilioko Benki ya PBZ zenye nambari 021101000039 na 021101000104.

3.8.1.8 Kukosekana kwa miongozo inayoimarisha mfumo wa udhibiti katika uendeshaji wa shughuli za Kitengo cha Hazina ya Serikali

Ukaguzi umebaini kuwa Kitengo cha Hazina ya Serikali kimekosa miongozo inayosaidia kuongeza udhibiti katika uendeshaji wa shughuli za Kitengo cha Hazina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Miongozo hiyo ingesaidia kuelezea majukumu ya watendaji mbalimbali wa kitengo hicho pamoja na kuelezea taratibu za uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali za kiuhasibu za mapato na matumizi ya Serikali. Kwa mfano, Muongozo huo ungesaidia kuelezea mapato gani yaingie katika hesabu gani na matumizi gani yafanyike katika hesabu gani. Aidha muongozo huo ungeelezea taratibu mbalimbali za udhibiti (control activities) zitakazosaidia kutunza na kulinda fedha za serikali dhidi ya upotevu wa aina yoyote ile.

3.8.1.9 Kumbukumbu za mapato na matumizi ya Serikali katika kitengo cha Hazina ya Serikali kuwekwa kwa njia ya mkono (manually) licha ya kuwepo mfumo wa IFMIS

Ukaguzi umebaini kuwa madaftari ya kuwekeakumbukumbu za mapato na matumizi ya Serikali katika kitengo cha Hazina ya Serikali yanarikodiwa kwa njia ya mkono (manually) licha ya kuwepo mfumo wa IFMIS. Hii imepelekea ukaguzi kubani kasoro kadhaa katika kumbukumbu hizo ikiwemo:-

- Taarifa za mapato na matumizi kurikodiwa kimakosa katika baadhi ya madaftari ya mapato na matumizi, ambapo mapato yanamebainika kurikodiwa upande wa 'Credit' na matumizi kurikodiwa upande wa 'Debit' kinyume na taratibu za kiuhasibu (Daftari la Fedha Taslim la Hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina-051103000084). Aidha baadhi ya madaftari yamebainika kuwa yanarikodi bakaa ya salio jumuishi 'cumulative balance' ya makusanyo ya benki kuwa ndio bakaa la makusanyo ya mwezi husika (Exchequer Recurrent Revenue-9928170104).
- Baadhi ya Madaftari ya mapato kutokuonyesha taarifa za matumizi au uhaulishaji wa fedha uliofanyika katikati ya mwezi.
- Kushindwa kuandaa taarifa sahihi za usuluhishi wa kibenki kutokana na kutokukamilika au kuwepo kwa makosa katika madaftari ya fedha taslim.

3.8.1.10 Fedha zilizolipwa benki ambazo taarifa zake hazijaonekana katika Daftari la Fedha taslim la mfumo wa IFMIS

Ukaguzi ulipitia taarifa za usuluhishi wa kibenki na kubaini uwepo wa malipo yaliyolipwa benki moja kwa moja pasi na kulipwa kupitia Daftari la Fedha taslim. Taarifa za malipo hayo na hesabu zinazohusika ni kama zinavyoonekana hapo chini:-

Jadweli Nambari 14 : Fedha zilizolipwa benki ambazo taarifa zake hazijaonekana katika Daftari la Fedha Taslim

Jina la Hesabu	Tarehe ya taarifa ya usuluhishi wa kibenki	Kiasi Kilicholipwa Benki ambacho hakijalipwa katika Daftari la Fedha taslim la IFMIS (Shs)	Tarehe ya kufanyika malipo
Hesabu ya Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu – 9928182104	31-Jan-2019	691,461,290	
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida – 9928182004	31-Mei-2020	3,468,143,983	20-Apr-2020
Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo – 9928190704	31-Oct-2019	27,500,000	29-Aug-2019

3.8.1.11 Miamala ya fedha katika hesabu ya Mfuko wa Miundombinu ambayo imekosa maelezo

Mfuko wa Miundombinu umeanzishwa kwa mujibu wa sheria nambari 9 ya mwaka 2015 kwa lengo la kuhudumia miradi ya maendeleo nchini.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa miamala ya kutoa fedha kutoka hesabu ya Mfuko wa miundombinu (Infrastructure Fund Account) kwenda katika hesabu mbali mbali za matumizi na mapato ambapo ukaguzi haukupata maelezo ya sababu za msingi za kufanya miamala hiyo. Kuwepo kwa miamala hiyo kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za serikali. Mchanganuo wa baadhi ya miamala hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 15: Baadhi ya Miamala ya fedha ya hesabu ya Mfuko wa Miundombinu iliyokosa maelezo

Namba	Hati ya Malipo	Tarehe ya malipo	Jina la Hesabu iliyopokea fedha	Jumla ya fedha (Tshs)
1.	1/11	3-Nov-2020	Miscellaneous Deposit Account	1,067,402,278
2.	2/11	25-Nov-2020	Exchequer Revenue Account	2,447,561,475
3.	3/11	20-Nov-2020	TRA-DRD	73,485,403

4.	1/12	14-Dec-2020	Mfuko Mkuu wa Hazina	744,879,030
5.	2/12	17-Dec-2020	Mfuko Mkuu wa Hazina	1,800,000,000
6.	2/1	7-Jan-2021	Mfuko Mkuu wa Hazina	888,501,630
7.	4/1	28-Jan-2021	Mfuko Mkuu wa Hazina	85,603,992
8.	½	04-Feb-2021	Mfuko Mkuu wa Hazina	819,244,816
9.	3/2	27-Feb-2021	Katibu Mkuu-Wizara ya Afya	664,890,954
10.	1/3	31-Mar-2021	Mfuko Mkuu wa Hazina	188,140,400

3.8.1.12 Fedha ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu za Ofisi Kuu za Malipo ya Serikali (CPO) shilingi 4,359,219,082

Ukaguzi umebaini uwepo wa fedha zilizotoka Hesabu hazina ya Exch.Recc. Expenditure, yenye nambari 9928170704 na kwenda katika hesabu ya Ofisi Kuu za Malipo ya Serikali (CPO) Exchq. Recurrent TISS, yenye nambari 9928182004 ambazo hazikuthibitishwa kupokelewa katika Hesabu hiyo kwa ajili ya matumizi.

Jadwali Nambari 16 : Fedha ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu za CPO-Recurrent

Namba	Tarehe ya malipo	Kutoka hesabu	Kwenda hesabu	Nambari ya kumbukumbu ya Benki	Jumla ya fedha (Tshs)
1.	26-Julai-2016	Exch. Recc. Expenditure	CPO-Reccurent TISS	BGDZNBZN0720163 46582	21,695,000
2.	26-Julai-2016	Exch. Recc. Expenditure	CPO-Reccurent TISS	BGDZNBZN0720163 46581	63,575,666
3.	16-AUG-18	Exch. Recc. Expenditure	CPO-Reccurent TISS	BGDZNBZN0820183 93861	4,173,798,416
Jumla					4,259,069,082

Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa fedha zilizotoka Hesabu hazina ya Exchequer Development Expenditure, yenye nambari 9928170804 na kwenda katika hesabu ya Ofisi Kuu za Malipo ya Serikali (CPO) Development TISS, yenye nambari 9928190604 ambazo hazikuthibitishwa kupokelewa katika Hesabu hiyo kwa ajili ya matumizi.

Jadweli Nambari 17 : Fedha ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu za CPO -Development

Namba	Tarehe	Kutoka Hesabu	Kwenda Hesabu	Nambari ya kumbukumbu ya Benki	Jumla ya fedha (Tshs)
1.	29-JUL-16	Exchequer Dev. Vote – GOZ- 9928170804	CPO Development	BGDZNBZBN0720163 46822	100,150,000
Jumla					100,150,000

3.8.1.13 Fedha za makusanyo ya kodi za TRA ambazo hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu ya Hazina shilingi 1,584,590,853.31

Ukaguzi umebaini uwepo wa fedha zilizohaulishwa kutoka hesabu nambari 021101000137 ya TRA yenye jina la DEPUTY COMMISSIONER, TRA ZANZIBAR – CUSTOM AND EXCISE iliyopo katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), lakini hazikuthibitika kupokelewa katika hesabu nambari 9928134004 ya TRA yenye jina la DEP COM TRA ZNZ - CUSTOMS AND EXCISE iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili ziweze kupelekwa katika hesabu ya Hazina Exchequer Recurrent Revenue yenye nambari 9928170104 kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 18: Fedha za makusanyo ya kodi za TRA ambazo hazikuthibitishwa kupokelewa katika hesabu ya Hazina

Namba	Tarehe	Nambari ya Kumbukumbu ya PBZ	Jumla ya fedha (Shs)
1.	26/Jul/2016	DB::: TRA Auto Transfer 26.7.2016	620,571,772.11
2.	07/Sep/2016	BEING REVERSAL OF STP ERROR ON 09.08....	584,457,188.30
3.	31/Mar/2017	DB::: TRA Auto Transfer 31.3.2017	379,561,892.90
Jumla			1,584,590,853.31

3.8.1.14 Uhaulishwaji wa fedha ambazo zimekosa maelezo shilingi 22,513,124,539

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa miamala ya kuhaulisha fedha kutoka katika hesabu za mapato ya Hazina na kwenda katika hesabu nyengine ambapo ukaguzi haukupata taarifa za mahala fedha hizo zilipopelekwa.

Kufanyika kwa miamala ya uhaulishaji wa fedha bila ya kuwepo kwa maelezo ya uhaulishaji huo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 19 : Uhaulishwaji wa fedha ambazo zimekosa maelezo

Namba	Tarehe	Jina na Nambari hesabu iliyotoa fedha	Nambari ya Kumbukumbu ya Benki	Nambari ya kumbukumbu inayohusiana (Related Reference No.)	Jumla ya fedha zilizohaulishwa (Shs)
1.	24-DEC-18	MIN. OF FINANCE, ECO AFFAIRS DEV. REV – 9928139904	BGDDOMGLD1220184 03057	EA AG 165 02 BKR 139	1,300,000,000
2.	27-SEP-16	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0920163 49820	ZNBKCOR/092016/13 6	285,175,711
3.	20-DEC-16	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN1220163 54841	ZNBKCOR122016101	573,697,611
4.	28-DEC-16	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN1220163 55332	ZNBKCOR122016164	350,352,500
5.	28-DEC-16	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN1220163 55334	ZNBKCOR122016164	599,647,500
6.	23-FEB-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0220173 58792	ZBCOR022017124	5,591,850,000
7.	29-MAR-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0320173 61073	ZBCOR032017131	37,687,981
8.	21-APR-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0420173 62311	ZBCOR0421789	2,600,000

9.	23-JUN-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0620173 67033	ZBCOR062017135B	115,786,200
10.	23-JUN-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0620173 67036	ZBCOR062017135C	151,310,700
11.	23-JUN-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0620173 67027	ZBCOR062017135A	165,375,595
12.	04-OCT-17	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN1020173	ZNBKCOR10201706	393,731,710
13.	01-JAN-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0120194 03383	170104 TO 130504	424,669,342.07
14.	31-JAN-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0120194 08521	9928134104 3101	154,323,648.21
15.	24-APR-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0420194 14006	WEEKLYB23042019	2,499,818,226.16
16.	01-AUG-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0820194 21012	MONTHLY31072019	2,400,000.01
17.	01-AUG-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0820194 21010	MONTHLY 310719E.	393,333,745
18.	02-SEP-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZBN0920194 23098	ZNZ31082019H	4,591,787,809.57

19.	15-OCT-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ1020194 26354	ZNZRT15102019	3,000,000,000
20.	24-OCT-19	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ1020194	2011BOT192940015	31,139,599.99
21.	30-NOV-20	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ1120204 56557	ZNBKCOR301101	140,641,982.10
22.	30-NOV-20	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ1120204 56558	ZNBKCOR30112020	1,700,860,812
23.	25-JAN-21	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ0120214 60570	980120212138	2,229,955.33
24.	25-JAN-21	EXCHEQUER RECURRENT REVENUE – GOZ – 9928170104	BGDZNBZ0120214 60572	70012021211926	4,703,910.50
Jumla					22,513,124,539

3.8.1.15 Fedha za mapato ya ZRB ambazo huchelewa kuhaulishwa kutoka hesabu yake iliyo PBZ na kuingizwa katika hesabu ya BOT

Wakati wa ukaguzi huu, ukaguzi uliomba agizo la kuhamisha fedha za mapato yanayotokana na kodi ikiwemo mapato ya ZRB yanayokukusanywa kupitia hesabu yake iliyopo PBZ kwenda BOT. Hadi tunakamilisha ukaguzi huu ukaguzi haukupatiwa agizo hilo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa mapato ya TRA yalikuwa yakihamishwa kutoka hesabu yake iliyo PBZ kwenda BOT mara 3 kwa wiki.

Ukaguzi umebaini kuwa mapato ya ZRB yanayokusanywa kupitia hesabu iliyopo PBZ yanachelewa kuhaulishwa kupelekwa katika hesabu yake iliyopo BOT hadi mwishoni mwa mwezi, ambapo pia imebainika kuwa kuna miezi ambayo ina bakaa ya kiasi kikubwa cha fedha za makusanyo iliyomo katika hesabu ya benki haihaulishwi mwishoni mwa mwezi bali huchelewesha hadi siku za mbele.

Kuchelewa kuhamisha fedha za mapato ya Serikali kutoka benki za kibiashara na kuzipeleka katika hesabu iliyopo Benki Kuu kunamaanisha kuwa mapato yanachelewa kupelekwa katika

hesabu ya Hazina ya Serikali iliyopo Benki Kuu, jambo linaloweza kuathiri upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za malengo ya Serikali. Orodha ya bakaa ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 20 : Fedha za mapato ya ZRB ambayo huchelewa kuhaulishwa

Namba	Tarehe	Bakaa ya Fedha ya mwisho wa mwezi iliyopo katika hesabu ya benki (Tshs.)	Fedha zilizohaulishwa (Tshs.)	Bakaa ya fedha ambayo haikuhamishwa kwenda BOT (Tshs.)
Hesabu Nambari 021103000669 - ZANZIBAR REVENUE BOARD iliyopo PBZ				
1.	30 Juni,2016			599,649,649.60
2.	31 Julai, 2016	1,168,613,371.87	0	1,168,613,371.87
3.	31 Agosti,2016	1,213,666,123.51	0	1,213,666,123.51
4.	30 Septemba, 2016	685,628,383.24	0	685,628,383.24
5.	31 Oktoba, 2016	824,352,377.81	0	824,352,377.81
6.	31 Agosti, 2017	80,589,107.26	0	80,589,107.26
Hesabu Nambari 0404003001 - ZANZIBAR REVENUE BOARD iliyopo PBZ				
7.	30 Aprili, 2019	5,839,054.75	0	5,839,054.75
Jumla				4,578,338,068.04

3.8.1.16 Kukosekana kwa uthibitisho wa kupokelewa kwa mapato ya ZRB katika hesabu yake iliyopo BOT katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai 2016 hadi Oktoba 2016 shilingi 7,735,974,595.04

Ukaguzi umebaini kuwa ZRB ilikusanya mapato yenye jumla ya shilingi 7,735,974,595.04 kwa kipindi cha miezi mitatu Julai 2016 hadi Oktoba 2016 katika hesabu yake yenye nambari 0211013000669 iliyopo PBZ. Makusanyo hayo yalihaulishwa katika tarehe tofauti kutoka hesabu hiyo ya PBZ kwenda hesabu nyengine. Ukaguzi haukuthibitisha kupokelewa mapato hayo katika hesabu yenye nambari 9928130504 yenye jina la ZANZIBAR REVENUE BOARD iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili ziweze kupelekwa katika hesabu ya Hazina Exchequer Recurrent Revenue yenye nambari 9928170104 kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Badala yake makusanyo ya ZRB yameanza kuingia katika hesabu hiyo ya BOT kuanzia tarehe 30 Novemba, 2016.

Taarifa za uhaulishaji wa fedha zilizokusanywa na ZRB kupitia hesabu yake yenye nambari 0211013000669 iliyopo PBZ kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Oktoba 2016 ni kama zinavyoonekana hapo chini:-

Jadweli Nambari 21 : Fedha za mapato ya ZRB yaliyokosa uthibitisho wa kupelekwa katika hesabu ya BOT katika kipindi cha Julai 2016 hadi Oktoba 2016

Namba	Tarehe	Kumbukumbu	Kiasi Kilichohaulishwa (Tshs.)
1	01/Jul/2016	NBD/TT/594/16	539,210,015.00
2	18/Jul/2016	NBD/TT/664/16	3,108,420.00
3	03/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160803004	321,234,374.00
4	03/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160803003	188,953,559.74
5	03/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160803002	506,212,435.92
6	16/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160816015	103,275,648.00
7	16/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160816014	75,243,546.16
8	16/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160816013	209,521,994.74
9	22/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160822003	106,065,862.98
10	22/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160822002	63,980,452.84
11	22/Aug/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160822001	371,034,509.10
12	25/Aug/2016	TRANSFER TO A/C 021103000623	52,379,023.00
13	02/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160902001	526,031,751.24
14	02/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160902002	34,572,317.00
15	02/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160902003	185,881,095.00
16	06/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160906001	253,151,248.64
17	06/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160906002	65,672,450.00
18	06/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160906003	209,872,390.00
19	21/Sep/2016	INTERBRANCH DEBIT	40,349,630.00
20	26/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160926004	236,551,993.98
21	26/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160926003	143,853,542.38
22	26/Sep/2016	DB:: SWIFT OUT - 008RTG160926002	818,756,087.96

23	05/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161005005	232,594,807.00
24	05/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161005004	63,959,198.25
25	05/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161005003	266,949,070.61
26	08/Oct/2016	INTERBRANCH DEBIT	52,087,604.00
27	17/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161017004	75,819,675.00
28	17/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161017003	129,701,150.61
29	17/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161017002	254,975,958.19
30	27/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161027001	834,342,918.21
31	27/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161027003	226,755,551.00
32	27/Oct/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161027002	106,295,359.38
33	01/Nov/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161101001	276,793,230.11
34	01/Nov/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161101002	31,504,250.00
35	01/Nov/2016	DB::: SWIFT OUT - 008RTG161101003	88,354,120.00
36	18/Nov/2016	TO 021103000623	40,929,355.00
Jumla			7,735,974,595.04

3.8.1.17 Dosari zilizobainika katika mkataba wa kiwango cha utoaji huduma kwa mfumo wa IFMIS

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari mbali mbali zinazotokana na mkataba wa kiwango cha utoaji wa huduma "SLA" katika Mfumo wa IFMIS ambazo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 146,556,000 zimeweza kutumika kwa ajli ya kumlipa mtoa huduma wa mfumo kutoka katika kampuni ya "Soft Tech Consultant Ltd" kwa baadhi ya huduma kujirudia kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo jambo ambalo linapelekea kuongeza gharama zisizo za lazima kwa matumizi ya mfumo ambapo kama ingetolewa taaluma kwa wasimamizi wa mfumo gharama hizo zingeweza kuokolewa. Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini mikataba hiyo haikuwa madhubuti katika kuongeza taaluma kwa watumiaji na wasimamizi wa mfumo wa IFMIS.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 22: Mchanganuo wa malipo ya "Application Consultant"

Mwaka wa fedha	Jina la Mtoa Huduma	Gharama kwa siku (Tshs.)	Idadi ya Siku	Malipo bila ya kodi (Tshs.)	Malipo ya kodi (Tshs.)	Malipo ya jumla (pamoja na kodi) (Tshs.)
2018/2019	Application	1,380,000	30	41,400,000	7,452,000	48,852,000
2019/2020	Consultant	1,380,000	30	41,400,000	7,452,000	48,852,000
2020/2021		1,380,000	30	41,400,000	7,452,000	48,852,000
Jumla		4,140,000	30	124,200,000	22,356,000	146,556,000

- Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 81,420,000 zimeweza kutumika kwa kumlipa mtoa huduma wa mfumo kutoka katika kampuni ya "Soft Tech Consultant Ltd " ambapo baadhi ya huduma hizo zimejirejea kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Aidha huduma hizo zingeliweza kufanyika kwa njia ya kielektroniki (remote desktop support) kwa vile gharama za huduma hizo ni sehemu ya gharama ya zilizolipiwa wakati wa ununuzi wa Mfumo huo kinyume na kuingia gharama mpya ya kumleta mtaalamu wa kurekebisha tatizo ambalo lingeliweza kufanyika kwa njia ya kielektroniki. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 23: Mchanganuo wa malipo ya "Technical Consultant"

Mwaka wa fedha	Jina la Mtoa Huduma	Gharama kwa siku (Tshs.)	Idadi ya Siku	Malipo bila ya kodi (Tshs.)	Malipo ya kodi (Tshs.)	Malipo ya jumla (pamoja na kodi) (Tshs.)
2018/2019	Technical Consultant	1,380,000	20	27,600,000	4,968,000	32,568,000
2019/2020		1,380,000	20	27,600,000	4,968,000	32,568,000
2020/2021		1,380,000	10	13,800,000	2,484,000	16,284,000
Jumla				69,000,000	12,420,000	81,420,000

- Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 108,300,400 zimeweza kutumika kwa kumlipa mtoa huduma wa mfumo kutoka katika kampuni ya "Soft Tech Consultant Ltd" kwa baadhi ya huduma kujirudia kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ambapo mkataba wa kiwango cha utoaji huduma umejumuisha gharama za kumlipa Meneja wa Kampuni iliyouza Mfumo kitu ambacho kiuhalisia Meneja hawi sehemu wa utoaji huduma hizi (on site support) bali mafundi (wataalam) ndio wanaotoa huduma hizo. Ukaguzi umebaini kukosekana kwa mtaalamu ambae atatoa mafunzo na uelewa kwa watumiaji wa Mfumo na kumepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 24: Mchanganuo wa malipo ya "Support Manager"

Mwaka wa fedha	Jina la Mtoa Huduma	Gharama kwa siku (Tshs.)	Idadi ya Siku	Malipo bila ya kodi (Tshs.)	Malipo ya kodi (Tshs.)	Malipo ya jumla (pamoja na kodi) (Tshs.)
2018/2019	Support Manager	1,412,000	25	35,300,000	6,354,000	41,654,000
2019/2020		1,412,000	25	35,300,000	6,354,000	41,654,000
2020/2021		1,412,000	15	21,180,000	3,812,400	24,992,400
Jumla				91,780,000	16,520,400	108,300,400

- Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 73,278,000 zimeweza kutumika kwa mtoa huduma wa mfumo kutoka katika kampuni ya "Soft Tech Consultant Ltd" kwa baadhi ya huduma kujirudia kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ambapo ukaguzi umebaini gharama za Mshauri elekezi kufanyika hata kama tatizo la kiufundi halikutokezea kwani imebainika mshauri huyo atalazimika kuja kwa kila mwaka hata kama hakukuwa na tatizo la kimfumo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 25: Mchanganuo wa malipo ya " System Development Consultant "

Mwaka wa fedha	Jina la Mtoa Huduma	Gharama kwa siku (Tshs.)	Idadi ya Siku	Malipo bila ya kodi (Tshs.)	Malipo ya kodi (Tshs.)	Malipo ya jumla (pamoja na kodi) (Tshs.)
2018/2019	System	1,380,000	15	20,700,000	3,726,000	24,426,000
2019/2020	Development	1,380,000	15	20,700,000	3,726,000	24,426,000
2020/2021	Consultant	1,380,000	15	20,700,000	3,726,000	24,426,000
Jumla				62,100,000	11,178,000	73,278,000

Kutokana na hali hiyo, ukaguzi umebaini gharama za Mikataba ya kiwango cha utoaji huduma zimetokana na idadi ya siku watakazokaa wataalam kutoa huduma hio (on site support) jambo ambalo gharama hizo zingeliweza kupungua endapo kama Wizara ingeliweka Mkataba unaoainisha uhitaji wa wataalamu ikiwa Mfumo unapohitaji msaada wa kitaalamu.

3.9 MAPENDEKEZO

Kutokana na dosari mbali mbali zilizobainika katika mwendelezo wa ukaguzi wa mfumo wa IFMIS unaosimamiwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo kwa Taasisi zinazotumia mifumo ya TEHAMA kama ifuatavyo:-

- Ukaguzi unapendekeza kuwa uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kufanya uhakiki wa kuzitambua hesabu zake zilizopo PBZ na BOT kwa lengo la kuziunganisha katika Mfumo wa IFMIS kwa matumizi ya Seirkali.
- Ukaguzi unapendekeza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inatumia mfumo wa IFMIS kikamilifu ili kuepuka kufanya malipo kwa baadhi ya moduli ambazo hazitumiki kikamilifu na kuweza kuokoa gharama za kuanzisha mifumo mengine inayofanya kazi sawa sawa na mfumo wa IFMIS uliopo.

- c) Kuhakikisha kwamba zinafuata sera, viwango na miongozo ya matumizi ya mifumo iliyowekwa na Serikali.
- d) Kuhakikisha kwamba zinaandaa miongozo mbali mbali ya TEHAMA ambayo itakayokwenda sambamba na sera za Serikali itakayoweza kusimamia utekelezaji wa miongozo hiyo.
- e) Kuwajengea uwezo watumiaji na wasimamizi wa mifumo ili kuweza kupunguza gharama za utoaji wa huduma katika mifumo.
- f) Kufanya upembuzi yakinifu kwa taasisi za umma pale zinapohitaji kufanya mabadiliko ya mfumo ili kuweza kuokoa kuingia gharama zisizokuwa za lazima.
- g) Ukaguzi unapendekeza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ianzishe utaratibu wa kuhakikisha kuwa kitengo cha Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinafunga hesabu zake za kila mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi.

3.10 HITIMISHO

Matokeo ya ripoti hii yanatokana na mashirikiano tuliopatiwa na watendaji mbali mbali wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na wadau wake. Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inawashukuru wote waliofanikisha kumalizika kwa kazi hii ambayo lengo lake ni kurekebisha dosari mbali mbali zilizojitokeza katika udhibiti na usimamizi wa mapato na matumizi kwa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma (IFMIS).

Nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake kubwa anazozichukuwa katika kusimamia nidhamu na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali.

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali inazozichukuwa katika kuimarisha Ofisi hii kiutendaji na watendaji kwa ujumla.

Kwa ujumla, ripoti hii inatambua juhudi za Serikali katika kuboresha miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na programu za kusimamia Mfumo wa Usimamizi wa fedha za Serikali (IFMIS) katika kusimamia mapato na matumizi katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo, masuala yaliyobainishwa ndani ya ripoti hii maalum ya ukaguzi wa mifumo yamepelekea kuhitimisha kwamba bado taarifa nyingi za fedha hazijaunganishwa katika mfumo licha ya kwamba mfumo wa IFMIS una uwezo wa kuratibu taarifa zote za fedha zinazofanyika kwa njia ya mkono (manual).

Ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ikiwa ni msimamizi mkuu wa mfumo wa usimamizi wa fedha za Serikali kuweka mkazo wa kutosha katika kuhakikisha miamala yote pamoja na taarifa zote za kifedha zinazofanyika ndani ya Mfumo ili kupunguza hatari ya uwepo wa mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Ni matumaini yangu kwamba mapendekezo na ushauri uliotolewa katika ripoti hii yatafanyikiwa kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika usimamizi wa fedha za Umma.

SURA YA NNE

UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO KATIKA BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ZANZIBAR (SLOTTEX ZANZIBAR)

4.0 UTANGULIZI

Baraza la Manispaa Mjini ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo taasisi hiyo imekuwa na jumla ya vyanzo vya ndani Ishirini na Nne (24) vya ukusanyaji wa mapato. Baadhi ya vyanzo hivyo ikiwemo Ada za Masoko, Leseni, Kodi za Maduka na Ofisi, Ada za Maegesho, Ada za Mabango n.k.

Kwa upande wa maegesho ya vyombo vya moto, Baraza la Manispaa ya Mjini lilianza kukusanya mapato kuanzia mwaka 1995 kufuatia mamlaka yaliyomo kwenye sheria namba 3 ya mwaka 1995 ya Zanzibar Municipal ambapo hadi kufikia mwaka 2018 Baraza lilikuwa linakusanya wastani wa shilingi **Milioni Mia Nane Thamanini na Sita na Laki Tano (Tshs 886,500,000)** kwa mwaka ambapo makusanyo hayo yalikuwa yakikusanywa kwa njia ya kawaida (manually) bila ya kutumia mfumo wa TEHAMA.

Hata hivyo, katika kutafuta mbinu mpya na njia bora za kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato na kuimarisha udhibiti wa ukusanyaji wa mapato ya maegesho Baraza lilifikia uamuzi wa kukusanya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto kwa njia ya kielektroniki kupitia mfumo wa TEHAMA.

Kutokana na kutokuwepo kwa mfumo wa kufanya huduma hiyo Baraza la Manispaa ya Mjini lilifanya utaratibu wa kutangaza Zabuni na hatimae Kampuni ya ECONEX ZANZIBAR LTD iliweza kushinda zabuni hiyo na kuwa Wakala wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto katika eneo la Manispaa ya Mjini.

Aidha, Baraza la Manispaa Mjini lilifunga mkataba wa awali na kampuni ya ECONEX ZANZIBAR LTD tarehe 9 Agosti 2019 wenye thamani ya shilingi **321,120,000** ambapo mkataba huo ulieleza makubaliano ya kwamba ECONEX ZANZIBAR LTD ndio atakuwa Wakala wa Makusanyo yote ya Mapato ya Maegesho ya Vyombo vya Moto katika Wilaya ya Mjini Zanzibar. Hii inamaanisha kwamba mapato yote ya maegesho yatakusanywa na kampuni husika kwa niaba ya Baraza la Manispaa ya Mjini Zanzibar na huduma hiyo ya makusanyo itafanyika kwa njia ya kielektroniki kupitia mfumo maalum wa TEHAMA. Mkataba huo ni wa muda wa miaka mitatu kuanzia Agosti 2019 hadi Julai 2022 kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 13**.

Hata hivyo, mkataba uliofungwa baina ya ECONEX na Baraza haukuzingatia muendelezo wa matumizi ya mfumo kwa Baraza baada ya mkataba kumalizika (System Sustainability Plan), kwa maana ya kuwa mkataba utakapomalizika kampuni ya ECONEX itabakia na mfumo wake na kuliacha Baraza katika utaratibu wa awali wa ukusanyaji wa mapato (manually).

Aidha, Mkataba huo haukuweza kuzingatia ushirikishwaji kikamilifu wa Baraza katika ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha maslahi ya Baraza yanalindwa wakati wote ambapo Baraza halikuwa

na Mwakilishi hata mmoja anaeshiriki katika kukagua na kushuhudia mchakato wa ukusanyaji wa mapato unaofanyika kwenye maeneo mbali mbali yanayokusanywa mapato na kampuni ya ECONEX.

4.1 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa Mfumo wa Makusanyo ya Mapato ya Maegesho ya Vyombo vya Moto umefanyika kwa lengo la kuangalia ikiwa maslahi ya Serikali yamezingatiwa ipasavyo katika ubinafsishaji wa ukusanyaji wa mapato ya maegesho ya vyombo vya moto kwa kupitia mfumo wa Wakala pamoja na kutoa ushauri kutokana na hatua mbali mbali za utekelezaji wa mfumo. Malengo mengine yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

- a) Kupima utekelezaji kwa mujibu wa sheria, miongozo, kanuni na taratibu zilizowekwa.
- b) Kuhakiki udhibiti katika uchakataji wa taarifa zilizomo ndani ya mfumo kwa lengo la kupima tija na ufanisi ili kuweza kutoa mapendekezo.
- c) Kuzithibitisha na kuzitathmini taarifa kimalengo (objectively).
- d) Kuhakiki usalama na utunzaji wa taarifa za Serikali kwenye mfumo.
- e) Kupima mipango endelevu ya Baraza katika ukusanyaji wa mapato ya maegesho kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

4.2 UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanywa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu Nambari 112 na Sheria Nambari 11 ya mwaka 2003 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aidha, ukaguzi huu ulijikita kutathimini maeneo kadhaa kwenye mchakato wa kubinafsisha na utekelezaji wa ukusanyaji tozo za maegesho ya vyombo vya moto kwa kutumia mfumo wa kielektroniki ambapo mkataba, udhibiti wa utumiaji (Application Controls), uendeshaji wa TEHAMA (ICT Governance), usimamizi wa miradi ya TEHAMA (ICT Project Management), hatari za TEHAMA (ICT Risk Management), udhibiti wa ujumla wa TEHAMA (ICT General Controls) pamoja na uzingatiaji wa miongozo mingine ya ukaguzi iliyoonekana inafaa katika upatikanaji wa hitimisho la ukaguzi huu vilizingatiwa.

Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia misingi ya hatari (Risk Based Audit) ambapo dosari mbali mbali zimebainika kwa mujibu wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka zilizopatikana wakati wa ukaguzi.

4.3 MIONGOZO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa Mfumo wa Makusanyo ya Mapato ya Maegesho ya Vyombo vya Moto umefanywa kwa kuzingatia sheria, miongozo pamoja na viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi ikiwemo eGAZ , eGA , ISACA, AFROSAI-E , COBIT 5, INTOSAI, n.k.

4.4 TAARIFA YA MFUMO UNAOTUMIKA KWA KUKUSANYIA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO

Mfumo unaotumiwa na Kampuni ya ECONEX kwa shughuli za kukusanyia mapato ya maegesho ya vyombo vya moto unaitwa **SLOTTEX ZANZIBAR**. Mfumo huo umetengenezwa na unamilikiwa na Kampuni ya ECONEX na unafanya kazi katika mazingira (Platform) ya mtandao **“Web Based System”**. Vile vile mfumo huo umeunganishwa na mashine za mkononi zinazoitwa Point Of Sell (**POS**) ambazo hutumika kwa ajili ya kutolea Ankara na Stakabadhi za malipo ya maegesho.

Aidha, mkataba uliofungwa haukuweza kubainisha kuwa ni aina gani ya mapato ya maegesho ambayo yatarikodiwa na yale yasiorikodiwa katika mfumo kwa vile mapato hayo yamegawika katika aina tofauti kama zifuatazo:-

- Mapato ya maegesho ya kila siku (daily collections).
- Mapato ya maegesho ya Boda boda na Bajaji (Motor cycle Collections).
- Mapato ya maeneo yaliyotengwa (Reserved Parking).

4.4.1 Mapato ya Maegesho ya Kila Siku (Daily Collections)

Mapato haya hukusanywa na kampuni ya ECONEX kwa kila siku na kumbukumbu za taarifa zake huhifadhiwa ndani ya mfumo wa SLOTTEX ZANZIBAR ambapo mapato hayo hukusanywa na wafanyakazi wa kampuni ya ECONEX kupitia mashine za POS na vile vile hutumia simu za mkononi zenye programu maalum za kutoa taarifa za mapato (App).

4.4.2 Mapato ya Maegesho ya Boda boda na Bajaji (Motor Cycle Collections)

Mapato haya husukanywa kwa wiki na yanajumuisha vyombo vya moto vya maringi mawili na matatu kama vile Boda boda, Bajaji n.k ambapo vyombo hivi vimetengewa maeneo maalum ya maegesho. Fedha zinazokusanywa kutokana na maegesho hayo taarifa zake hazirikodiwi katika mfumo kutokana na udhaifu uliopo kuwa mapato hayo hukusanywa kwa njia ya kawaida bila ya kutumia mashine za POS.

4.4.3 Mapato ya Maegesho ya Maeneo yaliyotengwa (Reserved Parking)

Mapato haya hukusanywa na kampuni ya ECONEX kwa kila mwezi ambapo yamejumuisha maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi maalum ya maegesho (Reserved Parking). Muhusika aliechukuwa eneo hilo kwa ajili ya kuweka vyombo vya moto hulipia kiwango maalum kwa kila mwezi (fixed amount). Hata hivyo taarifa za makusanyo ya mapato ya maegesho hayo hayaingizwi katika mfumo.

4.5 USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA MAKUSANYO YA MAEGESHO

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kwamba Kampuni ya ECONEX haina usimamizi imara wa utunzaji wa taarifa za makusanyo ya maegesho zilizomo ndani ya mfumo wake. Hali hii imebainika kutokana na kuondoshwa taarifa za madeni ndani ya mfumo ambayo yanaonesha Kampuni ya ECONEX inadai vyombo mbali mbali vilivyowahi kukaa kwenye maegesho bila ya kulipa.

Aidha, katika mkataba wa awali uliosainiwa tarehe **9 Agosti 2019** ambao ni wa muda wa miaka mitatu Baraza lilihita kampuni ya ECONEX kukusanya kiwango kisichopungua shilingi **321,120,000** kwa kila mwezi ikiwa ni jumla ya mapato ya mwezi. Kati ya fedha hizo kwa mwaka wa kwanza Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 45 na kampuni ya ECONEX kuchukuwa asilimia 65. Kwa mwaka wa Pili na wa Tatu Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 60 na kampuni ya ECONEX kuchukuwa asilimia 40.

Ukaguzi umebaini mkataba wa awali uliofungwa baina ya kampuni ya ECONEX na Baraza la Manispaa ya Mjini ulishindwa kufuatwa kikamilifu kutokana na Baraza kupunguza kwa makusudi maeneo ya maegesho yaliyokua yakikusanywa na Kampuni ya ECONEX na kuyachukua wenyewe mara baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mkataba huo.

Hali halisi ya mgawanyo wa mapato ya maegesho ya vyombo vya moto yaliyokusanywa na kampuni ya ECONEX na kugawanywa kwa Baraza la Manispaa ya Mjini kupitia Mkataba wa awali (Mkataba Mama) ulioanza mwezi wa Agosti 2019 hadi Disemba 2019 ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 26: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto

Makusanyo ya Mwezi	MAKADIRIO YA MAPATO		MAPATO HALISI	
	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa 45% (Tshs)	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa (Tshs)
Agosti	Kampuni ya ECONEX ililipa jumla ya shilingi 64,000,000 kwa Baraza la Manispaa ya Mjini ikiwa ni fedha za awali kwa ajili ya 20% ya "Security " kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.			
Septemba, 2019	321,120,000	144,504,000	83,000,000	62,000,000
Septemba, 2019	321,120,000	144,504,000	66,000,000	34,000,000
Oktoba, 2019	321,120,000	144,504,000	60,600,000	30,300,000
Novemba, 2019	321,120,000	144,504,000	59,000,000	30,000,000
Disemba, 2019	321,120,000	144,504,000	60,000,000	30,000,000
Jumla	1,605,600,000	722,520,000	328,600,000	250,300,000

Kutokana na jadweli la mwenendo wa ukusanyaji wa mapato liliopo hapo juu linaonesha hali halisi ya kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na kupelekea kubadilishwa makubaliano ya awali zaidi ya mara moja kwa kupitia mkataba wa nyongeza (**Addendum No.1**) uliosainiwa tarehe **1 Januari 2020** kama inavyobainika katika **Kiambatisho Nambari 14**.

Aidha ukaguzi umebaini mkataba huo wa nyongeza (Addendum No.1) ulishusha kiwango cha makusanyo kwa kila mwezi kutoka shilingi **321,120,000** hadi kufikia shilingi **75,000,000** kukiwa na upungufu wa shilingi **246,120,000** sawa na asilimia 76.64 ya upungufu kwa kila mwezi.

Mchanganuo wa makusanyo hayo kupitia makubaliano ya mikataba wa nyongeza (Addendum No.1) ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 27: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto

Mwezi	MAKADIRIO YA MAPATO		MAPATO HALISI	
	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa 45% (Tshs)	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa (Tshs)
Januari, 2020	75,000,000	33,750,000	60,000,000	30,000,000
Februari, 2020	75,000,000	33,750,000	56,000,000	28,000,000
Machi, 2020	75,000,000	33,750,000	67,500,000	33,750,000
Aprili, 2020	75,000,000	33,750,000	50,000,000	25,000,000
Mei, 2020	75,000,000	33,750,000	59,970,000	25,000,000
Juni, 2020	75,000,000	33,750,000	50,000,000	25,000,000
Julai, 2020	75,000,000	33,750,000	54,000,000	27,000,000
Agosti, 2020	75,000,000	33,750,000	60,270,000	30,000,000
Septemba, 2020	75,000,000	45,000,000	59,980,000	30,000,000
Oktoba, 2020	75,000,000	45,000,000	50,330,000	25,000,000
Novemba, 2020	75,000,000	45,000,000	62,670,000	31,000,000
Desemba, 2020	75,000,000	45,000,000	72,600,000	36,300,000
Januari, 2021	75,000,000	45,000,000	74,000,000	37,000,000
Februari, 2021	75,000,000	45,000,000	64,050,000	38,400,000
Machi, 2021	75,000,000	45,000,000	70,000,000	42,000,000
Aprili, 2021	75,000,000	45,000,000	72,500,000	43,300,000
Mei, 2021	75,000,000	45,000,000	90,000,000	54,000,000
Jumla	1,275,000,000	675,000,000	1,073,870,000	560,750,000

Kiwango hicho kilichoshushwa kilikuwa ni makubaliano ya pande zote mbili ambapo sababu zilizopelekea kushushwa kwa kiwango hicho cha awali ni kutokana na kuzuka kwa Janga la Ugonjwa wa UVIKO –19 ambapo limeathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi mbali mbali duniani ikiwemo Tanzania.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kufanyika kwa makubaliano ya mabadiliko ya awamu ya pili yaliyofanyika kupitia mkataba mwingine wa nyongeza (**Addendum No.2**) uliofungwa tarehe 6 Juni 2021 kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Nambari 15**.

Katika mkataba huo wa nyongeza ya pili (**Addendum No.2**) ulieleza uwepo wa kiwango cha makusanyo kisichopungua shilingi **189,625,000** kwa kila mwezi ambapo kiwango hicho kimeongezeka kutokana na kurudishwa kwa baadhi ya maeneo yaliyokuwa yametolewa awali na vile vile kupungua kwa Janga la UVIKO-19. Hata hivyo kiwango cha makusanyo hayo hakikuweza kufikiwa hadi ukaguzi unakamilika jambo ambalo limeathiri upatikanaji wa mapato halisi yaliyokadiriwa na Baraza la Manispaa ya Mjini na kupelekea kushindwa kutelekeza majukumu ya kibajeti waliyojipangia. Halisi ya makusanyo ya maegesho ya kila mwezi yaliyokusanywa kupitia mkataba wa nyongeza ya pili kuanzia mwezi wa Juni 2021 hadi tunakamilisha ukaguzi mwezi wa Septemba 2021 ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 28: Makadirio na mapato halisi ya makusanyo ya mapato ya vyombo vya moto

Mwezi	MAKADIRIO YA MAPATO		MAPATO HALISI	
	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa 45% (Tshs)	Makusanyo yote ya Mapato 100% (Tshs)	Gawio la Makusanyo kwa Manispaa (Tshs)
Juni, 2021	189,625,000	113,775,000	88,102,700	52,861,620
Julai, 2021	189,625,000	113,775,000	120,000,000	60,000,000
Agosti, 2021	189,625,000	113,775,000	126,000,000	63,000,000
Septemba, 2021	189,625,000	113,775,000	95,891,500	57,535,000
Jumla	758,500,000	455,100,000	429,994,200	233,396,620

Hata hivyo, marekebisho mengine yalifanywa kwa njia zilizokuwa nje ya mikataba ambapo kwa kiasi kikubwa yameathiri utekelezaji halisi wa kazi ya makusanyo ya maegesho. Baadhi ya njia nyengine zilizokuwa zikitumika nje ya makubaliano ya mkataba ni kuweza kubadilishwa kwa viwango vya makusanyo kupitia maelekezo ya mdomo kutoka kwa viongozi wa Serikali pamoja na barua mbali mbali zilizokuwa zinatoka Baraza la Manispaa ya Mjini na kwenda katika kampuni ya ECONEX zenye kuonesha kuongezeka au kupungua viwango vya tozo pamoja na maeneo ya maegesho. **Kiambatisho Nambari 16 Kinahusika**

Marekebisho ya mara kwa mara yaliofanywa kwenye mikataba yanaashiria kuwepo kwa udhaifu kwenye mgawanyo wa madaraka na mipaka ya kazi katika nafasi tofauti za uongozi. Wakati wa utekelezaji wa mikataba kulikuwa na uwezo wa kuja tamko kutoka kwa kiongozi yoyote ikiwa ni Waziri, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Diwani na wengineo ambapo tamko hilo likaweza kuathiri utekelezaji mzima wa mkataba.

Hali hii inaashiria kwamba utaratibu wa kuandaa mkataba ulikuwa na dosari katika ushirikishwaji wa wadau wote muhimu wanaoathiriwa na utekelezaji wake ambapo imepelekea mikataba kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara kutokana na mawazo na michango ya wadau wakati wa utekelezaji wake.

4.6 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MAKUSANYO WA MAPATO YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO

MATOKEO YA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Makusanyo ya Mapato ya Maegesho ya Vyombo vya Moto mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo dosari zifuatazo:-

4.6.1 Dosari katika Mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na kampuni ya ECONEX

Baraza la Manispaa Mjini limefunga mkataba na ECONEX COMPANY LTD tarehe 9/8/2019 wa muda wa miaka mitatu kwa ajili ya kuitaka kampuni ya ECONEX kukusanya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto kwa niaba ya Baraza katika maeneo ya Manispaa ya Mjini Unguja kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Mkataba huu uliitaka kampuni ya ECONEX kukusanya kiasi kisichopungua shilingi **321,120,000** kwa kila mwezi ambapo kati ya fedha hizo, kwa mwaka wa kwanza Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 45 na ECONEX kuchukuwa asilimia 65. Kwa mwaka wa Pili na wa Tatu Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 60 na ECONEX kuchukuwa asilimia 40. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika mkataba huo kama zifuatazo:-

4.6.1.1 Kutoainishwa kwa Nambari ya Hesabu ya Benki ya Mapato ya Baraza

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba wa awali uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX haukuainisha Nambari ya Hesabu ya Benki ya Mapato (Revenue Bank Account Number) ya Manispaa Mjini iliyotarajiwa kutumika kukusanyia mapato ya maegesho ya vyombo vya moto.

Hali hii imeweza kupelekea mwanya wa kupotea kwa mapato ya Serikali kwa kuingizwa mapato ya maegesho katika nambari za hesabu za benki (Bank Account Number) zisizokusudiwa kwa ajili ya Mapato ya Baraza la Manispaa ya Mjini na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri kuainishwa kwenye Mkataba na kutumika hesabu ya mapato ya Baraza kwa ajili ya kuweka makusanyo yote ya tozo za maegesho ya vyombo vya moto kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Serikali kwa lengo la kuepusha fedha za mapato kupotea na kuisababishia hasara Serikali.

4.6.1.2 Kutoshirikishwa kwa watumiaji wa mfumo wa Baraza la Manispaa ya Mjini katika kutoa maoni na mahitaji yao wanayotaka yawemo ndani ya mfumo " User Requirements".

Kwa mujibu wa viwango bora (Best Practise) vinaelekeza kwamba Taasisi inapotaka kubadilisha utoaji wa huduma kutoka njia ya kawaida (Manual) na kwenda kwa njia ya kielektroniki kupitia mifumo (Automate) inapaswa kushirikisha wadau wote watakaohusika na matumizi ya mfumo husika ili kuelewa mahitaji yao na kuyazingatia katika kutengeneza, kununua au kuanzisha mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuhakikisha mahitaji yote ya utendaji kazi katika mfumo yanapatikana na kuboreshwa kwa lengo la kurahisisha kazi, kuongeza tija na kuleta ufanisi.

Ukaguzi umebaini utaratibu mzima wa kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki ndani ya Baraza la Manispaa Mjini haukua shirikishi kwa wadau wake ambao ni wafanyakazi wanaotarajiwa kuutumia mfumo huo kwa kupata taarifa za mapato ya maegesho, ambapo wafanyakazi hao hawakushirikishwa katika kuandaa mahitaji ya mfumo ambayo yangezingatiwa na kuingizwa katika Mkataba wa utoaji wa huduma za makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kwa njia ya kielektroniki kutoka Kampuni ya ECONEX , vile vile kutokupatiwa mafunzo ya kutosha katika matumizi ya mfumo husika (intensively user trainings).

Hali hii imepelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali za kiutendaji kwa upande wa watumiaji wa mfumo wa makusanyo ya maegesho katika Baraza la Manispaa ya Mjini. Baadhi ya dosari ni kama zifuatazo: -

- Mtumiaji wa mfumo kutoka Baraza hawezi kuzitoa ripoti za mapato kutoka katika mfumo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za makusanyo ya mapato kwa siku, kwa wiki au kwa mwezi kutokana na mahitaji ya Baraza.
- Taarifa za makusanyo ya mapato ya vyombo vya maringi mawili na matatu kama vile Boda boda, Bajaji n.k hazipatikani katika mfumo, hivyo afisa mapato wa Baraza hawezi kuona na kujua mapato halisi ya vyombo yanayokusanywa na ECONEX na mgao halisi wa Baraza kutokana na mapato hayo.
- Watumiaji wa mfumo katika kitengo cha TEHAMA cha Baraza wanashindwa kuhifadhi taarifa za makusanyo zilizomo katika mfumo wa SLOTTTEX ZANZIBAR (Lack of data Backup Process) kutokana na kutopata elimu na ruhusa kutoka kwa ECONEX kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za mapato kwa mujibu wa mkataba, hivyo Baraza limeshindwa kuthibitisha usalama wa taarifa za makusanyo katika mfumo na miundombinu inayotumika ikiwa kuna uwezekano kwa njia yoyote taarifa kupotea, kuharibika, kubadilishwa au kutumika kinyume na makubaliano kwa upande wa ECONEX.
- Afisa Mapato wa Baraza anaetumia mfumo kutofahamu madeni wanayodai ECONEX kwa vyombo vilivyokuwa havijalipa tozo ya maegesho.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini ufanye utaratibu wa kushirikisha wadau na watumiaji wa mfumo (system users) katika kubaini mahitaji yao yote ya mfumo na kuainishwa katika mikataba na kuyazingatia kwenye mfumo husika kwa lengo la kuleta urahisi wa kazi, kuongeza tija na ufanisi kwa sasa na kwa mifumo itakayoanzishwa.

4.6.1.3 Kutoainishwa umiliki wa mfumo baada ya kumalizika kwa muda wa Mkataba

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kwa kutumia mfumo wa kielektroniki haukuainisha umiliki wa mfumo kama utakua mali ya Baraza au ECONEX baada ya kumalizika muda wa mkataba unaoendelea sasa.

Kwa kuzingatia malipo anayoyapata mtoa huduma (asilimia 55 ya mapato ya maegesho kwa mwaka

wa kwanza na asilimia 40 kwa miaka miwili ya mwisho) ilitarajiwa kwamba huduma (ECONEX) hupata gawio lake kama sehemu ya kurejesha gharama alizotumia kwa ajili ya kutengeneza mfumo na gharama nyingine za ziada alizotumia kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za ukusanyaji wa mapato ya maegesho ambapo mwisho wa mkataba mtoa huduma angemwachia Baraza mfumo ili aweze kuusimamia mwenyewe kwa mujibu wa taratibu zake.

Hata hivyo kutokana na mkataba uliofungwa kutoainisha kifungu hicho muhimu ambacho kingeeleza kuwa mfumo utakua mali ya nani baada ya mtoa huduma kurejesha gharama zake, kuna uwezekano mkubwa kwamba mtoa huduma akaondoka na mfumo wake baada ya mkataba huo kumaliza muda.

Pindipo ikitokezea hivyo Serikali itakua imepata hasara kwa sababu inalipia gharama kubwa ya huduma ya mfumo tofauti na bei za huduma ya mifumo zilizopo sokoni kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa kwenye mikataba.

Ukaguzi unashauri kwamba, uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa upande wa Serikali na uongozi wa kampuni ya ECONEX kwa upande mwingine kukaa pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwenye mkataba utakaozingatia maslahi ya Serikali katika umiliki wa mfumo huu ili kuepuka kuendelea kuisababishia hasara Serikali.

4.6.1.4 Kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya maegesho.

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba yote ya makusanyo ya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na ECONEX haikuweza kufikia malengo ya makusanyo yaliyopangwa awali na haikuweza kubainisha vigezo sahihi vilivyotumika na kuonesha mchanganuo halisi wa makusanyo katika kufikia malengo yaliyopangwa.

Kwa mujibu wa mkataba wa awali wa makusanyo ya maegesho uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX kifungu Nambari 10(a) kimeeleza kwamba kampuni ya ECONEX ilitakiwa kukusanya mapato yasiopungua shilingi **321,120,000** kwa mwezi. Baadae malengo hayo yakapunguzwa kwa asilimia 76 na kufikia shilingi **75,000,000** kupitia mkataba wa Nyongeza Nambari 1 na hatimae malengo haya yakaongezwa kwa zaidi ya asilimia 60, kutoka shilingi **75,000,000** na kuwa shilingi 189,625,000 kupitia mkataba wa Nyongeza Namba 2.

Kutokana na kutokuwa na vigezo sahihi katika upangaji wa malengo ya makusanyo ya mapato kumepelekea Baraza na ECONEX kutofikia malengo ya awali waliyokusudia kukusanya ambayo yalikuwa ni kuanzia shilingi **321,120,000** kwa kila mwezi.

Aidha hali hii imepelekea kusababisha usumbufu na hasara kwa Serikali kutokana na kuibuka kwa mikataba mingi isiyo na tija pamoja na kutolewa kwa barua nyingi za kubadilisha viwango vya makusanyo ambavyo viko nje ya utaratibu wa mikataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya tathmini ya maeneo ya maegesho ili kutambua athari za maeneo yasiyotozwa kwenye maeneo yanayotozwa na kufanya maamuzi sahihi kwa masilahi mapana ya Serikali, kuyaainisha maeneo yote kwenye mkataba pamoja na kuainisha vigezo vyote vilivyotumika katika kufikia malengo ya makusanyo ya kila mwezi.

4.6.1.5 Kukosekana kwa vifungu vinavyobainisha utaratibu wa kutoza na kukusanya fedha za faini kwa maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha vyombo.

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba iliyofunguwa baina ya Baraza na ECONEX haina vipengele vinavyozungumzia faini za maegesho pamoja na utaratibu wa ukusanyaji wa faini hizo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha vyombo.

Kutokuwepo kwa vipengele hivyo katika mikataba kunaweza kupelekea kupotea kwa mapato ya makusanyo ya faini husika kutokana na kukosa utaratibu na usimamizi mzuri wa makusanyo hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuchukua hatua zilizobora katika kulisawazisha jambo hili kupitia mkataba husika ili mapato yanayotokana na faini za maegesho yaweze kusimamiwa vizuri na kukusanywa kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili.

4.6.1.6 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya makusanyo ya maegesho katika Mfumo wa SLOTTTEX.

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba ya makusanyo ya maegesho haikuzingatia utaratibu wa kufuatwa katika kufuatilia madeni kwa vyombo visivyolipa tozo ya makusanyo ya maegesho.

Hali hii imepelekea kampuni ya ECONEX kushindwa kufuatiliza vizuri madeni kwa vyombo vinavyodaiwa tozo ya maegesho na hatimae kufuta au kubadilisha taarifa za madeni hayo kwenye mfumo bila ya kushirikisha Baraza la Manispaa ya Mjini.

Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri kunaweza kupelekea kupotea kwa taarifa muhimu za mapato ya maegesho kutokana na ufutwaji wa kiholela wa madeni au ubadilishwaji wa taarifa za makusanyo katika mfumo na hatimae kusababisha hasara kwa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha mkataba unaonesha utaratibu wa kufuatwa katika kutunza, kubadilisha au kufuta taarifa yoyote kwenye Mfumo wa SLOTTTEX ZANZIBAR na kuweka utaratibu wa ushikirikishwaji wa Baraza katika kuidhinisha na kufanya mapitio ya taarifa za makusanyo katika mfumo kila mara (Regular System Review).

4.6.1.7 Kukosekana kwa usahihi wa taarifa katika vifungu vya Mkataba

Ukaguzi umebaini kwamba Kifungu Nambari 10(a) cha Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kinaeleza kwamba Mtoa huduma lazima awasilishe kiwango cha fedha za makusanyo ya ada za maegesho kwa **kila mwezi** kisichopungua **shilingi Milioni Mia Tatu Ishirini na Moja Laki Moja na Ishirini Efu (Tshs 321,120,000)**.

Kwa upande mwingine wa mkataba huo Kifungu Nambari 13 kinamtaka Mtoa huduma kuwasilisha fedha zote za ada ya maegesho kwa **kila siku** katika hesabu ya benki ya Baraza bila kuainisha kiwango.

Kutokana na maelezo yaliyopo hapo juu ukaguzi umeshindwa kufahamu utaratibu uliokusudiwa wa kuwasilisha mapato benki ikiwa mapato ya makusanyo ya maegesho yanatakiwa kuwasilishwa kila siku au kwa mwezi.

Hali hii inaweza kusababisha mtoa huduma kushindwa kuelewa utaratibu gani unaotakiwa wa kuwasilisha fedha za makusanyo benki ikiwa awasilishe fedha za makusanyo kila siku au kwa mwezi.

Aidha kifungu Nambari 14 kinaeleza kwamba iwapo mtoa huduma atachelewa kuwasilisha fedha za makusanyo ya siku, au unapomalizika mwezi husika kwa mujibu wa kalenda akawa hajawasilisha kiwango cha fedha za makusanyo ya ada za maegesho ya mwezi kwa kiwango kilichotajwa katika mkataba huu atakua na wajibu wa kulipa kiwango alichocheleweshwa kukiwasilisha na asilimia 2 ya kiwango alichocheleweshwa kwa kila siku ambayo atacheleweshwa kuwasilisha fedha hizo.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Baraza la Manispaa na ECONEX upitie tena mkataba huo na kusawazisha dosari zote zilizojitokeza ili kuweza kuondoa changamoto iliyobainika katika uandaaji wa mikataba hiyo.

4.6.1.8 Baraza la Manispaa kushindwa kukagua kazi inayofanywa na Kampuni ya ECONEX

Kwa mujibu wa Kifungu Nambari 22 cha Mkataba wa awali wa makusanyo ya maegesho kinampa mamlaka Baraza la Manispaa ya Mjini kukagua kazi yote inayofanywa na mtoa huduma (ECONEX) kwa ajili ya kujiridhisha hali ya utendaji kazi wa kampuni ya ECONEX na kutoa maelekezo kwa ajili ya kuongeza tija na ufanisi wa kazi hizo.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini halifanyi ufuatiliaji wa kina kujiridhisha kwa huduma zinazotolewa na kampuni ya ECONEX ambapo hali hii imepelekea Baraza kutokua na taarifa sahihi kwa mujibu wa hali halisi ya utekelezaji wa mkataba.

Baadhi ya taarifa ambazo Baraza lilithibitisha kwamba hazina utambuzi nazo ni kama zifuatazo:-

- Uwepo wa vikundi vya watu wanaotoza faini kwa maegesho yasiyoruhusiwa na kukusanya fedha za faini kwa matumizi yao binafsi ambapo watu hao si wafanyakazi kutoka Baraza wala ECONEX.
- Kutowekwa Alama za mabango ya makatazo ya maegesho **"No Parking"** kwa baadhi ya maeneo ambayo hayaruhusiwi kuegeschwa vyombo vya moto.
- Tozo za maegesho ya Boda boda na Bajaji hazikusanywi kupitia mfumo hivyo kutoweza kujua kiwango halisi kinachokusanywa kupitia vyombo hivyo.
- Makusanyo ya mapato ya maegesho kwa maeneo maalum yaliyohifadhiwa (Reserved Parkings) hayaonekani kwenye mfumo.
- Kutokubainishwa kwa alama za michoro ya utambulisho wa maegesho ya vyombo vya moto barabarani na kupelekea uwepo wa maegesho ambayo hayana utambulisho.

Kutokana na hali hiyo, ukaguzi unaona kwamba kuna hatari ya kupotea kwa mapato ya Serikali kutokana na hali ya kwamba Baraza linashindwa kufatilia utendaji kazi wa ECONEX ili kujuwa baadhi ya taarifa muhimu za makusanyo.

Ukaguzi unashauri Baraza kuchukuwa jitihada za makusudi katika kufatilia kwa kina utendaji kazi wa kampuni ya ECONEX ili kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa kazi na kuondoa dosari zitakazojitokeza ikiwemo kuondosha mianya ya upotevu wa mapato.

4.6.1.9 Kutofanyika kwa vikao vya kila mwezi

Kwa mujibu wa mkataba wa makusanyo ya maegesho Kifungu Nambari 30 kinaeleza kwamba Baraza na Mtoa huduma watakua na vikao vya kila mwisho wa mwezi vinavyohusu usimamizi na utekelezaji wa mkataba huo.

Ukaguzi umebaini kwamba vikao hivyo havifanyiki kama inavyoelekezwa katika kifungu hiki jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mkataba huo.

Kupitia vikao vya pamoja vya kila mwezi kungefanyika majadiliano mengi na baadhi ya mambo yangeweza kutekelezeka kwa ufanisi kama vile kuongezeka kwa maeneo mapya ya kukusanya tozo, kupata kujua namna sahihi na yenye tija ya kukusanya madeni, athari za kuwepo kwa maeneo yasiyolipiwa tozo za makusanyo n.k.

Kutofanyika kwa vikao hivi kumpelekea kuwepo kwa changamoto zinazokaa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi na hatimae kuchelewasha ufanisi katika utendaji kazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya vikao na kampuni ya ECONEX kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ili kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa kazi za makusanyo ya maegesho na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

4.6.1.10 Fedha za makusanyo ya maegesho kutoingizwa katika Hesabu ya Benki ya Baraza kila siku.

Kifungu Nambari 13 cha Mkataba wa makusanyo ya mapato ya maegesho kinaeleza kwamba fedha yoyote ya ada ya maegesho ni mali ya Baraza, hivyo mtoa huduma anawajibu wa kuwasilisha fedha zote za ada ya maegesho kwa kila siku katika akaunti ya Baraza.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa kifungu hiki hakijazingatiwa kwa upande wa kampuni ya ECONEX kwani wao hupeleka mapato ya kila siku katika akaunti ya ECONEX ya benki na ikifika mwisho wa mwezi ECONEX huhaulisha kiwango kinachohusika tu cha gawio la Baraza na kuingiza kiwango hicho katika akaunti ya Baraza na fedha nyingine ambazo ni gawio la ECONEX husalia kwenye akaunti yake.

Hali hii ni kwenda kinyume na kifungu hicho na kuingiza hasara kubwa kwa Serikali ambayo ni pamoja na kukosa fursa ya kupata riba za kila mwezi, kukosa fedha za matumizi kwenye mahitaji ya kila siku hali inayoweza pelekea Serikali kukopa fedha benki na kulipa kwa riba.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Baraza na wa ECONEX upitie tena mkataba huo na kusawazisha dosari zote zilizojitokeza katika eneo hili ili kuinusuru Serikali kuendelea kupata hasara.

4.6.1.11 Hasara iliyotokana na dosari katika utekelezaji wa kanuni za maegesho

Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Mabaraza ya Manispaa ya mwaka 2017, inazungumzia faini zinazohusisha maegesho ya vyombo vya moto kwenye maeneo yasiyoruhusiwa ambapo imeweka kiwango cha shilingi **Elfu Hamsini (Tshs 50,000)** kama kiwango cha chini na shilingi **Laki Moja (Tshs 100,000)** kama kiwango cha juu cha faini.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika utekelezaji wa kanuni hizo ambapo kwa

mujibu wa ripoti ya makusanyo ya faini za maegesho iliyoandaliwa na Baraza kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi wa Januari 2021 hadi Juni 2021 imebainika faini zinazotowa ni pungufu ukilinganisha na viwango halisi vilivyoidhinishwa kulipwa kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2017, ambapo zaidi ya asilimia 50 za mapato ya faini hupotea kwa njia hii.

Hali hii inaonesha kwamba Serikali hupoteza mapato mengi kutokana na usimamizi mbaya uliopo kwa Baraza katika kutoza faini za maegesho.

Aidha, kulipa faini kinyume na viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa kanuni zilizopo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa uchocheaji wa rushwa jambo ambalo litasababisha kujitokeza kwa upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuzingatia na kutekeleza kanuni zinazosimamia faini za maegesho katika utekelezaji wa majukumu ili kuepusha uwezekano wa kuvuja kwa mapato kwa Serikali.

Baadhi ya viwango ambavyo vimekua vikitozwa na Baraza kinyume na kanuni katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari 2021 hadi Juni 2021 ni kama inavyoonekana katika jaduweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 29 : Mapato yanayotokana na faini yaliyokusanywa kwa miezi sita kuanzia Januari 2021 hadi Juni 2021

Namba	Kiwango cha faini kwa mujibu wa kanuni (Tshs)	Kiwango kilichotozwa Kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs)	Idadi ya Vyombo	Jumla ya mapato halisi yaliyokusanywa kwa mujibu wa faini iliyoanza Kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs)	Jumla ya mapato yaliyopaswa kupatikana kwa mujibu wa kanuni Kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs)	Mapato yaliyopotea kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs)
1.	50,000	10,000	2	20,000	100,000	80,000
2.	50,000	15,000	3	45,000	150,000	105,000
3.	50,000	20,000	29	580,000	1,450,000	870,000
4.	50,000	30,000	29	870,000	1,450,000	580,000
5.	50,000	40,000	3	120,000	150,000	30,000
Jumla Kuu				1,635,000	3,300,000	1,665,000

4.6.2 Dosari katika Usimamizi wa Mfumo wa SLOTTX ZANZIBAR

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika kusimamizi wa mfumo wa kielektroniki wa makusanyo ya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

4.6.2.1 Kutokamilika kwa usajili wa mashine za POS na wanaokusanya tozo.

Utaratibu wa kukusanya mapato ya maegesho kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unajumuisha mambo mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Wafanyakazi ambao watakusanya mapato ya maegesho katika maeneo husika.
- Mashine za (POS) zitakazotumiwa na wafanyakazi kwa ajili ya kutolea ankara za malipo mwanzoni mwa huduma ya maegesho na kutoa stakabadhi baada ya kufanyika malipo kulingana na muda wa maegesho uliotumika.
- Maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya kuegeshewa vyombo na kulipiwa tozo ya maegesho.
- Mfumo wa kielektroniki utakaoweka kumbukumbu za makusanyo ya mapato na wafanyakazi wanaokusanya mapato hayo kupitia mashine za POS.

Ili kuliwezesha Baraza na Kampuni ya ECONEX kufuatilia na kupata taarifa sahihi za makusanyo ya maegesho kwa kila siku, ECONEX haina budi kuunganisha mashine za POS, watu wanaotumia mashine husika, na maeneo wanayokusanya mapato husika katika mfumo wa SLOTEX.

Lengo la kuunganisha vitu vyote hivyo kwa pamoja katika mfumo ni kupata taarifa sahihi za makusanyo kwa kumtambua mtu anayetumia mashine, eneo anapokusanyia na mashine husika, wakati na kiwango alichokusanya.

Ukaguzi umebaini kwamba kampuni ya ECONEX haijaunganisha katika mfumo kwa pamoja mashine za POS, watumiaji wa mashine pamoja na maeneo husika ya maegesho, badala yake wakusanyaji mapato hukusanya kupitia POS bila ya kujulikana maeneo wanakokusanyia.

Kwa hivyo, kuna uwezekano wa makusanyo kupatikana kwa kiwango kidogo kuliko uhalisia wa eneo husika linalotumika kukusanyia mapato ya maegesho.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha vitendea kazi vyote, wakusanyaji wote na maeneo yao wanasajiliwa kwa pamoja na waonekane katika maeneo yao halisi waliopo ili iwe rahisi kwa Baraza kufuatilia na kupata taarifa sahihi za mapato yaliyokusanywa na kampuni.

4.6.2.2 Uingizwaji wa mapato kwa njia ya mkono "manually" katika mfumo kinyume na utaratibu


Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa SLOTEX ZANZIBAR unaruhusu mtumiaji wa kampuni ya ECONEX kuweza kuingiza taarifa za mapato kwa njia ya kawaida (manually) pamoja na kuzibadilisha taarifa hizo endapo ikihitajika kubadilishwa.

Aidha ukaguzi umebaini taarifa hizo zinaweza kubadilishwa au kuingizwa katika mfumo kwa mkono na watendaji wa kampuni ya ECONEX bila ya kuwepo na utaratibu na idhini maalum kutoka kwa uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini.

Kuingiza taarifa za mapato kwa mkono na kuweza kubadilisha bila ya idhini ya Baraza kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya kufanyika kwa udanganyifu katika taarifa za makusanyo na kupelekea kupotea kwa mapato na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikishiha mapato yote yanakusanywa kupitia vifaa vya kukusanyia mapato vilivyopo na vilivyokwisha sajiliwa (POS na mobile apps) na kuweka usimamizi na udhibiti mzuri kwa kampuni ya ECONEX kuhakikisha kwamba makusanyo hayaingizwi ndani ya mfumo kwa njia ya mkono (manually).

Picha hapo chini iliyozungushiwa alama nyekundu inaonesha mapato yaliyoingizwa katika mfumo kwa njia ya kawaida (manually):-



4.6.2.3 Madeni ya maegesho ambayo yamefutwa katika Mfumo kwa makusudi zaidi ya shilingi 398,536,000

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 28 cha Sheria nambari 11 ya mwaka 2003 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinampa mamlaka Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanyia tathmini hesabu za mapato na kujiridhisha kwamba kiwango kinachotakiwa kukusanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni na vyombo vyengine vinavyosimamia ukusanyaji wa mapato kimekusanywa na kwamba hatua stahiki zimechukuliwa kwa mapato ambayo hayajaweza kukusanywa.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini halijachukuwa hatua stahiki za kukusanya mapato ya madeni ya maegesho kwa kipindi cha mwaka 2019 na 2020. Hali hii imethibitika kutokana na kwamba kampuni ya ECONEX iliyopewa dhamana ya kukusanya mapato ya maegesho kuyafuta madeni ya maegesho katika mfumo yenye thamani zaidi ya shilingi **Milioni Miatatu Tisini na Nane Laki Tano Thalathini na Sita Eflu (Tshs 398,536,000)** kwa makusudi bila ya Baraza kutambua.

Hali hii inaashiria kutokuwepo kwa mpango imara wa ufatiliaji wa malipo ya madeni ya maegesho ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na ada za maegesho na kushirikisha vyombo vya sheria ili kusaidia utekelezaji wa zoezi la ulipaji wa madeni ya maegesho kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kushirikiana na ECONEX kuweka utaratibu mzuri wa kufatilia madeni ya makusanyo ya maegesho yaliyopo katika mfumo kwa wahusika ili kuepuka kuingiza hasara Serikali. Baadhi ya madeni yaliyofutwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 30 : Miamala ya Mapato ya madeni ambayo yamefutwa

Idadi ya Miamala ya Madeni iliyofutwa kwenye Mfumo	Tozo ya kila muamala kwa Siku (Tshs)	Jumla ya mapato ya madeni yaliyofutwa (Tshs)
10,222	4,000	40,888,000
20,222	4,000	80,888,000
8,938	4,000	35,752,000
9,334	4,000	37,336,000
11,771	4,000	47,084,000
17,792	4,000	71,168,000
9,380	4,000	37,520,000
11,780	4,000	47,120,000
195	4,000	780,000
Jumla Kuu ya Mapato yaliyofutwa		398,536,000

Picha inayoonesha baadhi ya madeni yaliyofutwa kwenye mfumo:

Logs				Bulk Ticket Delete ▾
OPERATOR	STATUS	DETAIL	HAPPENED ON	
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 10222 unpaid tickets successfully	Wed - 6th Oct 2021 at 21:00:03	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 20222 unpaid tickets successfully	Wed - 6th Oct 2021 at 20:57:31	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 8938 unpaid tickets successfully	Thu - 17th Jun 2021 at 14:05:50	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 9334 unpaid tickets successfully	Tue - 8th Jun 2021 at 17:56:16	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 0 date specific unpaid tickets for 2020-11-01 successfully	Tue - 1st Jun 2021 at 14:07:06	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 8823 unpaid tickets successfully	Tue - 1st Jun 2021 at 14:05:45	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 11771 unpaid tickets successfully	Fri - 21st May 2021 at 14:54:09	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 17792 unpaid tickets successfully	Thu - 20th May 2021 at 23:45:15	Actions ▾
Slottex Bot bot@slottex.com	Success	deleted 9380 unpaid tickets successfully	Mon - 15th Mar 2021 at 16:13:06	Actions ▾

4.6.2.4 Dosari katika mipaka ya matumizi ya Mfumo

Utaratibu uliobora katika matumizi ya mfumo unaeleza kwamba Mfumo wa kielektroniki unatakiwa kuwa na mipaka kwa watumiaji ili taarifa zilizomo ndani yake zibakie katika hali ya usiri na usalama kwa muda wote. Hii inamaanisha kwamba kila mtumiaji awe na mipaka katika matumizi ya mfumo na aruhusiwe kuzifikia taarifa kwa mujibu wa mipaka yake.

Aidha aina za akaunti za matumizi na mipaka katika mfumo ielezwe kwa uwazi kupitia nyaraka rasmi za mipaka ya matumizi ya mfumo (User Matrix Document) ili kuweza kudhibiti kila mtumiaji kuona au kufanya kila kitu katika mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya ECONEX haina nyaraka nyenye kuonesha mipaka ya matumizi ya mfumo (User Matrix Document). Vile vile ukaguzi umebaini Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya ECONEX hutumia akaunti ya "Super Admin" kwa kufanyia kazi za uhasibu katika mfumo wa SLOTTTEX ZANZIBAR ambapo akaunti hiyo ya Super Admin hutumiwa na "System Developer" wa kampuni kwa ajili ya utoaji wa msaada wa kiufundi katika mfumo.

Kutumika akaunti ya Super Admin kwa shughuli za kihesabu katika mfumo sio sahihi na kunaweza kupelekea athari ya kukosekana kwa taarifa muhimu zitakazosaidia kupatikana ushahidi endapo matukio ya kihalifu yakifanyika katika mfumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuchukuwa jitihada za makusudi katika kuwaelimisha ECONEX kutayarisha nyaraka zinazoonesha mipaka ya matumizi katika mfumo na watumiaji kuwa na akaunti zenye utambulisho kwa mujibu wa kazi zao ndani ya mfumo.

4.6.2.5 Mfumo kutoweza kutoa ripoti za makusanyo ya mapato ya maegesho.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa SLOTTTEX ZANZIBAR haujawekwa uwezo wa kutoa ripoti za aina yoyote za makusanyo ya mapato ya maegesho (export report) ambapo ripoti hizo kama zingepatikana zingeweza kuwekwa katika kumbu kumbu za mafaili ya makusanyo ya maegesho kwa upande wa Baraza. Hivyo Baraza hupata changamoto kubwa katika kuweka rikodi za makusanyo hayo ya maegesho kutoka ndani ya mfumo kwa vile mfumo hauna uwezo wa kutoa ripoti na badala yake taarifa za makusanyo huonekana tu kupitia "screen dash board" katika kompyuta ambapo maafisa mapato wa Baraza hurikodi taarifa hizo katika madaftari kwa njia ya mkono, na wakati mwengine hupiga "screenshot" kwa simu au kompyuta.

Hali hii hupelekea kutokea kwa changamoto kubwa katika kuweka kumbu kumbu na kufanya maamuzi sahihi kwa wakati kwani taarifa zinazohitajika huwa hazipatikani kirahisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa ya Mjini kufanya mawasiliano na mtoa huduma kwa ajili ya kutengeneza moduli maalum itakayoweza kutoa ripoti za aina zote zitakazohitajika na Baraza ili kuweza kupatikana taarifa muhimu kwa urahisi ikiwemo taarifa za makusanyo ya siku, wiki, mwezi na mwaka kwa maeneo husika na kwa wakusanyaji husika, vyombo vya moto vinavyodaiwa, muda wa madeni husika kwenye maeneo husika na wakusanyaji husika.

4.6.3 Mapato ya maegesho yanayokusanywa nje ya Mfumo

Kwa mujibu wa mkataba wa makusanyo ya maegesho Kifungu Nambari 16 kinamtaka mtoa huduma kukusanya tozo za maegesho zote kwa njia ya elektroniki. Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya tozo zinakusanywa nje ya mfumo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu hicho cha mkataba wa makubaliano wa mapato yatokanayo na makusanyo ya maegesho. Mapato ya maegesho yanayokusanywa nje ya mfumo ni kama yafuatayo:-

4.6.3.1 Makusanyo ya maeneo maalum yaliyohifadhiwa ya maegesho (Reserved Parking)

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya ECONEX kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekusanya jumla ya shilingi 7,965,000 ikiwa ni fedha kwa ajili ya mapato ya maegesho ya Boda boda na Bajaji.

Aidha imebainika kuwa mapato hayo hukusanywa kwa njia ya kawaida bila ya kutumia mashine za POS zilizounganishwa kwenye mfumo na vile vile baadhi ya mapato hukusanywa kwa mkono bila ya kutolewa stakabadhi za malipo. Baadhi ya malipo ya mapato yanayokusanywa ni kama yafuatayo: -

Jadweli Nambari 31: Baadhi ya malipo yasiyotolewa stakabadhi (Receipts)

Nambari	Aina ya Chombo	Eneo la Maegesho	Muda wa Malipo	Kiasi cha Malipo kwa wiki (Tshs)	Kiasi cha Malipo kwa mwaka (Tshs)
1.	Makundi ya Bodaboda	Darajani	Wiki	6,000	312,000
2.	Makundi ya Bajaji	Darajani	Wiki	6,000	312,000
3.	Makundi ya Carry	Darajani	Mwezi	30,000	360,000

Jadweli Nambari 32: Baadhi ya malipo yanayotolewa stakabadhi za mkono

Nambari	Aina ya Malipo	Eneo la Maegesho	Muda wa Malipo	Kiasi cha Malipo (Tshs)	Kiasi cha Malipo kwa mwaka (Tshs)
1.	Maegesho kwa wakaazi	Mji mkongwe	Mwezi	30,000	360,000
2.	Maegesho kwa wenye maduka	Maeneo ya mjini	Mwezi	75,000	900,000
3.	Maegesho maalum kwa wenye Taxi	Ngome kongwe	Mwezi	450,000	5,400,000

4.6.3.2 Faini za maegesho ya maeneo yasiyoruhusiwa

Ukaguzi umebaini kampuni ya ECONEX inakusanya mapato yanayotokana na faini za maegesho kwa maeneo yasiyoruhusiwa. Hata hivyo imebainika kwamba mapato hayo hayakusanywi kwa kutumia mfumo uliopo wa SLOTEX ZANZIBAR na hakuna utaratibu wowote unaotumika katika kuweka kumbu kumbu za mapato hayo baada ya kukusanywa.

4.6.4 Maeneo yasiyolipiwa Tozo za Maegesho

Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya maeneo yaliyopo katika Manispaa ya Mjini ambayo hayamo katika orodha ya maeneo yote yanayolipiwa maegesho na kusimamiwa na ECONEX, lakini maeneo hayo yana uwezo mkubwa wa kongeza mapato kwa Serikali kama yakitumika rasmi kwa ajili ya shughuli za kukusanya mapato ya maegesho.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba endapo maeneo hayo yakitumika kwa shughuli za makusanyo ya maegesho Serikali inaweza kuingiza zaidi ya shilingi **471,024,000** kwa kipindi cha miaka miwili.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kufuatilia maeneo hayo na kuandaa utaratibu mzuri wa kuyatumia kwa shughuli za maegesho ili kuongeza ufanisi, tija pamoja na kuongeza mapato kwa Serikali. Orodha ya Maeneo yasiyotumika kwa maegesho ya vyombo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 17**.

4.6.3.1 Kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 131,537,197 katika uwasilishaji wa taarifa za mapato ya maegesho kwa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limeingiziwa jumla ya shilingi **446,861,620** ikiwa ni fedha za gawio la mapato ya maegesho ya Baraza kutoka kwa kampuni ya ECONEX, fedha hizo zimeingizwa katika akaunti ya mapato ya Baraza na zimeonekana kupitia Bank statement ya Baraza.

Kwa upande wa uwasilishaji wa taarifa, ukaguzi ulihitaji Baraza kuwasilisha taarifa za mapato ya maegesho ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo Baraza liliwasilisha jumla ya shilingi **578,398,817** na mapato hayo yamewasilishwa kupitia ripoti za mapato.

Kutokana na mapato yaliyoorodheshwa hapo juu ukaguzi umebaini kujitokeza kwa utofauti wa shilingi **131,537,197** baina ya mapato halisi ya maegesho yanayoingia benki na mapato yaliyowasilishwa kwa ukaguzi kutoka Baraza.

Hali hii ya utofauti inaashiria kwamba kujitokeza kwa udhaifu wa uwekaji wa kumbu kumbu za taarifa za mapato ya maegesho ya vyombo yanayotokana na Baraza la Manispaa ya Mjini.

Ukaguzi unashauri Baraza kuanzisha utaratibu mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu za mapato ili ziwe sahihi na kuweza kupatikana kwa urahisi pale zinapohitajika. Hata hivyo ni vyema kwa mkaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuangalia mwenendo wa makusanyo ya maegesho ya vyombo na Baraza na kufanya mapitio ya taarifa za makusanyo ya maegesho kila mara ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanalindwa.

SURA YA TANO

UKAGUZI WA MFUMO WA KUSIMAMIA MALI ZA KUDUMU ZA SERIKALI (ASSET MANAGEMENT SYSTEM)

5.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kifungu namba 104 na Sheria ya Tume ya Mipango namba 3 ya mwaka 2012 yenye jukumu la kusimamia upatikanaji na matumizi bora ya fedha za Serikali pamoja na kuandaa mipango madhubuti ya maendeleo ya Nchi.

Ili kuongeza ufanisi na tija katika kufanikisha majukumu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupiti idara zake mbali mbali imeanzisha mifumo ya TEHAMA takribani 17 kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 1993. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo Mkuu wa Malipo Serikalini (Intergrated Financial Management Information System-IFMIS) uliopo chini ya Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali, Mfumo wa Mishahara (Government Payroll System) uliopo chini ya Idara ya Bajeti na Mfumo wa Kusajili Mali za Kudumu za Serikali (Asset Management System) uliopo chini ya Idara ya Mitaji ya Umma.

5.1 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimempa Mamlaka kwa Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi anavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nambari 11 ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapoomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

5.2 MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho la kuridhisha kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango una ulinzi na udhibiti kwenye miundombinu inayochakata data , kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake na kuhakikisha kuwa taarifa zinazopatikana zina uadilifu na vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata taarifa zenye tija na ufanisi kupitia TEHAMA.

Aidha, ukaguzi huu pia ulikuwa na malengo maalum kama yalivyoainishwa hapa chini:-

- Kuhakikisha Sheria, Kanuni, Sera, Miongozo na Taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar zinafuatwa kwa mujibu viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Kufanya tathimini ya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.

- Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulingana na thamani halisi ya uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.
- Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zinapohitajika.
- Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo ya Taasisi.

5.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya kitaifa na kimataifa kama vile eGaz, COBIT, e-Government URT, AFROSAI pamoja na kuzingatia mbinu mbali mbali kama zifuatazo:-

- i. Kupitia Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo mbali mbali inayohusiana na shughuli za Wizara.
- ii. Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kupitia mfumo wa udhibiti wa ndani katika kufanya usimamizi wa mali za Serikali na ulipaji wa mishahara Serikalini.
- iii. Kupitia sera na miongozo ya usimamizi na uratibu wa TEHAMA kama inavyotolewa na eGaz.
- iv. Kupitia taratibu zilizotumika katika ununuzi, uwekaji na uondoshaji wa mali zinazohusiana na teknolojia ya TEHAMA.
- v. Kupitishwa kwenye mifumo ya TEHAMA (system demo) ili kuelewa inavyofanya kazi.
- vi. Kufanya majaribio ya udhibiti yaliyomo katika mifumo ya TEHAMA.
- vii. Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizotokana na mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- viii. Kufanya mahojiano na majadiliano pamoja na watumiaji mbali mbali juu ya mifumo ya Mishahara na ule wa Usimamizi wa Mali za Serikali.
- ix. Kutembelea Wizara na Taasisi mbali mbali ili kuweza kujidhirisha kama zina ufikiaji wa mfumo wa Usimamizi wa Mali za kudumu za Serikali.
- x. Kufanya kikao cha kuanza na kumaliza kazi za ukaguzi na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi.

5.4 TAARIFA ZA MFUMO WA USIMAMIZI WA MALI ZA KUDUMU ZA SERIKALI (ASSET MANAGEMENT SYSTEM)

Mnamo mwaka 2017 Idara ya Mitaji ya Umma ilitekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (Asset Management System) ambao ni "Web based" kwa kupitia mzabuni Digiscan Technologies Ltd kwa gharama ya Shilingi Milioni Mia mbili na Ishirini (220,000,000), mfumo huu umewekwa kwenye Seva za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Pamoja na mambo mengine mfumo huu ulitekelezwa ili utumike kwenye ngazi ya Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ukiwa na lengo la kutatua tatizo la utambuzi, uthamini na kujua eneo ziliko mali za Serikali, kitu ambacho kimekuwa kikikosekana kwa muda mrefu katika

usimamizi wa mali za Serikali na kupelekea upotevu, wizi, matumizi mabaya kwa watumishi wa umma na wananchi wasio waadilifu.

5.5 MAMBO YALIYOBAINIKA KWENYE MFUMO WA USIMAMIZI WA MALI

Katika ukaguzi uliofanyika mapungufu mbalimbali yalibainika katika udhibiti, usalama uendeshaji na usimamizi wa mfumo huu. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kwamba, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ilifanya ununuzi wa mfumo zaidi ya mmoja inayofanya kazi zinazofanana, Wizara kushindwa kuusambaza mfumo kwa watumiaji walioko kwenye Wizara nyengine ili waweze kuingiza taarifa za Mali zinazonunuliwa moja kwa moja kwenye Wizara zao, udhaifu katika usimamizi na uratibu wa mfumo wa Mali kiasi cha kushindwa kuendana na kasi ya ununuzi wa mali za Serikali, kutokuwa na mpango endelevu utakao hakikisha kuwa taarifa zote za mali za Serikali zilizopo (backlog data) zinaingizwa kwenye mfumo kwa ukamilifu na kwamba taarifa za mali mpya zinazoendelea kununuliwa zinaingizwa kwenye mfumo kwa wakati (live data entry).

Aidha, ukaguzi ulibaini udhaifu wa udhibiti wa utumiaji wa mfumo (Application Control) ambapo mfumo huu haujawekewa utaratibu wa mgawanyo wa majukumu, kutokuunganishwa kwa mfumo wa usajili wa mali na mfumo wa "Barcode" ambao ndio unaotumiwa kutengeneza vibandiko (barcode stickers) ambavyo hubandikwa kwenye mali za Serikali. Vile vile baadhi ya mapungufu yaliyobainika kwa upande wa uendeshaji na usalama wa TEHAMA ni kama ifuatavyo:-

Kukosekana kwa kamera za ulinzi kwenye chumba cha Seva, Dari kuvuja na kupelekea maji ya mvua kuingia ndani ya chumba cha Seva, kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na maafa (Disaster Recovery Plan), kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan), uchache wa kifaa kinachotumiwa kuhifadhi taarifa za nakala za mfumo (Backup Storage), kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site), kutojaribiwa kwa nakala za taarifa za mfumo (Backup Testing), kutokufuatwa kwa sera na miongozo ya eGaz kwenye kufanya uimarishwaji wa mifumo (Systems Upgrade), kufanyika kwa uimarishwaji wa mfumo huo moja kwa moja kwenye "production server" bila ya kujaribiwa kwenye "test server", kutokuwepo kwa mpango endelevu wa kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huu kwa makundi tofauti ya watumiaji, uelewa hafifu wa namna ya mfumo unavyofanya kazi kwa watumiaji wakuu (core team) wa mfumo waliopo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kutumika kwa majina ya ujumla (general user IDs and Names) kufanya kazi kwenye mfumo.

5.5.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

5.5.1.1 Ununuzi wa mifumo zaidi ya mmoja inayofanya kazi zinazofanana

Ukaguzi umebaini kuwa, mnamo mwaka 2017 Wizara kupitia Idara ya Mitaji ya Umma ilifanya ununuzi wa mfumo wa Usimamizi wa Mali (Asset Management System) bila ya kufanya tathmini na uwezo na utoshelevu wa mfumo wa IFMIS/ Epicor 10 ambao tayari ulishanunuliwa na Serikali katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali tangu mwaka 2015. Mfumo wa IFMIS/Epicor 10 una uwezo na unatosheleza kutumika katika usimamizi wa

mali zote za Serikali, na kwa kuzingatia ukweli kwamba tayari mfumo huu unafikiwa na “MDAs” takribani zote unaweza kutumika kwa ajili ya usimamizi wa mali za Serikali.

Hali hii imeisababishia Serikali hasara ya zaidi ya shilingi Milioni Mia Mbili Ishirini (Tshs. 220,000,000) kwa kununua mfumo wa usimamizi wa mali wakati mfumo wa IFMIS /Epicor 10 uliokuwepo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango unaweza kufanya kazi za usimamizi wa mali zote za Serikali.

Ukaguzi unashauri :

Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutengeneza Sera ya TEHAMA ya Wizara yote kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar pamoja na miongozo ya Kimataifa kama vile COBIT, AFROSAI-E, n.k na kuhakikisha kwamba pamoja na mambo mengine yatakayo kuwemo kwenye sera hiyo liwepo takwa la kufanyika kwa tathmini ya mifumo iliyopo pindi Idara au kitengo fulani kinapopanga kununua mfumo wowote ule ili kujiridhisha kama mifumo iliyopo inaweza kutimiza haja na mahitaji ya watumiaji hao.

Kwa ajili ya kuondoa mgongano wa maslahi ni vyema tathimini hii ifanywe na “team” ambayo itakuwa huru ya wataalamu wa TEHAMA na watumiaji wa mifumo iliyopo Wizarani na kuwasilisha ripoti yake kwenye menejimenti ya Wizara kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi ya ama kununua mfumo mpya, kufanya maboresho kwenye mifumo iliyopo ili ikidhi haja, au kutumia mifumo iliyopo kama ilivyo kwa kuzingatia tathmini ya gharama na manufaa (cost benefits analysis) pasipo kuathiri sera za nchi za TEHAMA wakati ikiweka msisitizo kwenye kupatikana thamani ya fedha, tija na ufanisi.

5.5.1.2 Mfumo wa “Asset Management System” kutounganishwa na mfumo wa “Barcode”

Ili kufikia malengo ya kuanzishwa mifumo ya kielekitroniki ni lazima mifumo hiyo ikidhi takwa la kurahisisha kazi, kuongeza tija na ufanisi kwenye majukumu ambayo awali yalifanywa kwa mikono (manually) na kupelekea kutumia muda mwingi, gharama kubwa, na kutopatikana kwa matokeo tarajiwa kwa wakati. Hata hivyo katika ukaguzi wa mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali ilibainika kwamba mfumo wa Mali haujaunganishwa na mfumo wa “Barcode”.

Hali hii inapelekea watumumiaji wa mifumo hii kufanya kazi mara mbili (double work) kwa kukusanya taarifa za mali wakati wa kufanya utambuzi na kubandika “barcode stickers” lakini pia kulazimika kuingiza taarifa hizi kwenye mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali kwa mikono (manually) jambo ambalo lingeweza kuepukika ikiwa kama mifumo hii miwili ingekuwa inawasiliana na kwamba mfumo wa “barcode” ungelikua unatumika kukusanya taarifa za mali ili zifichwe kwenye “barcodes”.

Mfumo huu wa “Barcode” ndio unaotumiwa kutengeneza vibandiko (Barcode Stickers) ambavyo hubandikwa kwenye mali za Serikali kwa madhumuni ya utambuzi wa mali husika (asset coding) kwa kutumia “Barcode Reader”, vibandiko hivi vinatarajiwa kubeba taarifa zote za mali ikiwa ni pamoja na thamani ya mali, tarehe ya ununuzi wa mali, umiliki wa mali, eneo ilipo mali husika na nambari ya mali. Taarifa hizi zilitakiwa zipatikane kwanza kwenye mfumo wa “Barcode” na kisha

ziende kwenye mfumo wa Mali moja kwa moja kupitia “integration” baina ya mifumo hiyo miwili jambo ambalo ni tofauti na uhalisia uliopo Wizarani.

Ieleweke kwamba, hadi ukaguzi unakamilika wakaguliwa hawakuweza kuonesha namna wanavyoingiza taarifa za mali kwenye mfumo wa “Barcode” badala yake “waliprinti” vibandiko ambavyo vilikua na namba zinazofuatana (serial numbers) na jina la taasisi pasipo kuingiza taarifa zozote za mali iliyokuwa inatengenezwa vibandiko husika, kwa maneno mengine ni kwamba “barcode stickers” zile hazina taarifa yoyote zaidi ya namba inayo onekana kwa macho kwenye kibandiko husika. Hali hii inatilia shaka ufanikiwaji wa malengo ya mfumo wa barcode katika utambuzi wa mali za Serikali kwani hauna tofauti na mfumo wa zamani wa kuchora mali za Serikali kwa kutumia rangi kwa mikono jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kwa Serikali kwa kuwekeza rasilimali muda, fedha na nguvu kwenye mfumo huu ambao haujaweza kurahisisha kazi wala kuleta tija na ufanisi uliokusudiwa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa alama za vifupisho vya taarifa (Barcodes) zinazowekwa kwenye vibandiko ambavyo vinavyowekwa kwenye mali hazijawahi kujaribiwa kusomwa kutumia “barcode readers” zilizopo Wizarani kwa zaidi ya miaka minne (4) tangu kutengenezwa kwake, hivyo hakuna uhakika wowote kuwa zinaweza kutumika kutoa taarifa za mali baada ya kusomwa na kifaa cha “Barcode Reader” kama ilivyotarajiwa.

Hata hivyo, wakaguliwa hawakuweza kuonesha namna ya kutumia “barcode readers” hadi ukaguzi unakamilika kwa maelezo kuwa mashine hizo hazijawekewa programu ambazo zingezivezesha kusoma taarifa za mali zilizopo kwenye “barcode stickers” japokuwa niliwapa nafasi ya kufanya hivyo bila mafanikio jambo ambalo linatilia shaka utendaji kazi wa mashine hizo zilionunuliwa zaidi ya miaka 4 iliyopita na hazijawahi kutumika kwa kazi iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango mambo yafuatayo:

- a) Kumfatilia na kumsimamia mzabuni (Digiscan) kwa karibu na kuhakikisha kwamba anatekeleza majukumu yake ya kimkataba kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuunganisha mfumo wa “Barcode” na ule wa usimamizi wa mali ambayo yote imetekelezwa kwa pamoja na kampuni yake ili kufanikisha dhana ya kurahisisha kazi, kuongeza tija, na ufanisi katika usimamizi wa mali za Serikali kupitia mfumo.
- b) Kuweka utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya matumizi sahihi ya mifumo na vifaa vya TEHAMA watumishi wake angalau mara moja kwa mwaka ili kuhakikisha kwamba watumiaji wanapata maarifa na uelewa wa kutosha kwenye usimamizi na matumizi sahihi ya rasilimali husika katika kuleta tija na ufanisi.
- c) Kuweka utaratibu unaofaa katika utunzaji wa rasilimali mbali mbali za TEHAMA za Wizara ili kuhakikisha kwamba zinaweza kutumika kwa kipindi kirefu zaidi zikiwa katika hali ya usalama na usafi tofauti na hali ilivyo kwa sasa hususani kwenye mashine za “barcode system” ambazo hazikuwa katika hali ya usafi.

5.5.1.3 Uchache wa nafasi katika kifaa cha kutunzia nakala za taarifa za mfumo (Backup storage).

Ukaguzi umebaini kuwa, kifaa kinachotumiwa kutunzia nakala za taarifa za mfumo (Backup storage) kina uwezo mdogo wa kuhifadhi taarifa kiasi cha kushindwa kutunzia taarifa zote zinazochukuliwa ndani ya mfumo kwa kipindi kirefu na kulazimu kuzifuta taarifa za nyuma za nakala ambazo bado hazijafikia muda wa kutakiwa kufutwa ili kuingiza taarifa mpya. Kufanya hivyo, kunaweza kusababisha kupoteza taarifa nyingi muhimu kwa usalama wa mfumo na kuathiri utendaji kazi wa Wizara hususani pale yanapotokea maafa.

Aidha, ukaguzi unapendekeza Wizara kufanya utaratibu wa kupata nafasi ya kutosha (storage capacity) ya kuhifadhi nakala hizi bila kuathiri usalama wa taarifa na mfumo kwa ujumla wake, nafasi hii inaweza kuwa ni kwenye seva, au "external drive".

5.5.1.4 Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza huduma za mfumo baada ya maafa kutokea (Disaster Recovery Site)

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) kutokea ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa katika wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kuharibika au kupotea kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilomita 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa. Eneo hili linatakiwa kuwa na uwezo sawa kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umegundua kuwa Wizara haina eneo mbadala maalumu lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza utendaji kazi kupitia mfumo baada ya matatizo kutokea (Disaster Recovery Site) kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara makubwa kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa "Disaster Recovery Site" ukaguzi unashauri Wizara kutengeneza eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA kitaifa na kimataifa na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kwa uharaka wa kutosha ili kuilinda taarifa mali (information asset) za Serikali ambazo kimsingi zimegharimu Serikali fedha nyingi, muda na nguvu katika kuzikusanya, kuzichakata na kuzihifadhi. Eneo hili ni vyema liwe na uwezo wa kutumiwa na mfumo yote ya Wizara bila kujali Idara ili uwekezaji huu uwe na tija na ufanisi kwenye matumizi ya fedha za Serikali.

5.5.1.5 Kukosekana kwa mpango wa Huduma Endelevu (Business Continuity Plan)

Kwa mujibu wa utaratibu ulio bora (Best Practices) na Sera za Serikali mtandao kifungu cha 4.4.1.2.(d) inazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mipango na miundo mbinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yatakayojitokeza dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea ni kwa utaratibu gani huduma zitaendelea wakati wa majanga na hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo zote yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa hakuna kabisa mpango huo unaotarajiwa kutoa muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo kupotea na kuonesha nini kifanywe baada ya majanga.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu zilizomo ndani ya mfumo kwa sababu Wizara kupitia vitengo vinavyohusika, TEHAMA na Watumiaji wa mfumo (ICT and Application team) kutojua nini kifanyike, hatua gani zichukuliwe na nani na wakati gani ili kupata nini kabla, wakati na baada ya tukio linaloweza kusababisha upotevu mkubwa wa taarifa kama vile moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, wizi, uharibifu wa miundombinu, matumizi mabaya n.k.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuandaa mpango huu kwa mujibu wa miongozo iliyopo na sera za Wakala Serikali mtandao na kwa kuzingatia miongozo na utaratibu unaokubalika kimataifa, aidha Wizara ijiwekee utaratibu wa kuijaribu angalau mara moja kwa mwaka mipango yote inayolenga kulinda taarifa pamoja na miundombinu ya TEHAMA ambayo imeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na juhudi pamoja na jitihada kubwa kuziandaa, kuzichakata na kuzitunza ambazo pia zikiingia mikononi mwa watu wasio na nia njema zinaweza kuleta madhara mengi kiuchumi, kiusalama, na kijamii.

5.5.1.6 Kutofanyika kwa majaribio ya nakala za taarifa za mfumo (Backup Testing)

Kwa mujibu wa miongozo na kanuni za kimataifa kama vile ISACA inaelekeza kwamba nakala za taarifa za mfumo zinazochukuliwa zinatakiwa kufanyiwa majaribio angalau mara moja kila mwaka ya kuhakikisha kwamba nakala zinazo chukuliwa zinatimia kulingana na taarifa zinazo hitajika kwenye nakala husika. Majaribio hayo yakileta majibu mazuri yatahakikisha tija ya taarifa hizo pale zitakapohitajika.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa nakala za taarifa za mfumo wa usimamizi wa Mali za Serikali (Asset Management System) hazifanyiwi majaribio na wala Wizara haina mipango wala mazingira wezeshi ya kuzifanyia majaribio taarifa hizo. Kwa kutokuzijaribu taarifa hizo kunainyima Wizara nafasi ya kufahamu kama taarifa zinazochukuliwa kwenye nakala zimekamilika au la, na kwamba je, kama ikitokea janga kubwa (pandemic) kama vile moto, mafuriko, tetemeko la Ardhi au miundombinu kushindwa kufanya kazi nakala zilizopo zinaweza kutegemewa na kutumika au vyenginevyo.

Ukaguzi unashauri kuandaliwa mpango wa kujaribu nakala za taarifa za mifumo ya Wizara utakaojumuishwa kwenye mpango mkuu wa kuchukua nakala uliopendekezwa ambapo Wizara itatakiwa kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na uwepo wa miundombinu stahiki na nyenzo nyingine muhimu za kuliwezesha zoezi la kuzijaribu taarifa hizi angalau mara moja kila mwaka.

5.5.1.7 Udhaifu katika udhibiti wa utumiaji wa mfumo (Application Control)

Ukaguzi umebaini mfumo haujawekewa utaratibu wa kulazimu taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entry) na kuhakikiwa na mtu mwingine (reviewer/ approver) kabla ya kuziposti taarifa kama hatua ya mwisho ya uingizaji wa taarifa kwenye mfumo. Hii inamaanisha kwamba kwa hali ilivyo sasa muingiza taarifa anaingiza taarifa na kuziposti bila ya kukaguliwa au kuthibitisha usahihi wake na mtu mwingine kwenye mfumo.

Mfumo kutokuwa na kipengele kinachomtaka mtu mwingine kuhakiki na kuzithibitisha taarifa hizo kunaweza kupelekea uingizwaji wa taarifa nyingi ambazo sio sahihi kwa sababu ya makosa ya kibinaadamu au kwa kutumia chanzo cha taarifa kisicho sahihi na kusababisha kutoaminika na kutotumika kwa taarifa zilizomo kwenye mfumo kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri kuwekwa mgawanyiko wa majukumu kwenye mfumo huu ili mtu mmoja asifanye kila hatua ya uingizaji wa taarifa mpaka mwisho na badala yake kuwekwa utaratibu wa mtu mwingine kuhakiki taarifa zilizoingizwa katika mfumo na muingiza taarifa ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazoingizwa ni sahihi kwa kila hali.

5.5.1.8 Kutokuwepo mpango endelevu wa kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo (system sustainability plan)

Ukaguzi umebaini kwamba pamoja na kuwa mfumo wa kusimamia Mali za Kudumu za Serikali (Asset management system) umetumika kwa zaidi ya miaka minne sasa lakini bado wafanyakazi wanaotumia mfumo huo hawana uelewa wa kutosha wa namna ya kuutumia mfumo ipasavyo ili kuleta tija na ufanisi katika kufanya usimamizi kamili wa mali za Kudumu za Serikali zilizoingizwa na zinatotakiwa kuingizwa kwenye mfumo huo, hii ni pamoja na baadhi ya watumiaji wa mfumo kutofahamu namna ya kuthaminisha upya (Re evaluation) mali, kutokufahamu matumizi ya baadhi ya ripoti zilizomo kwenye mfumo. Miongoni mwa watumiaji hao ni waliojiunga na Idara ya Mitaji ya Umma wakati mfumo ukiwa tayari ushatekelezwa na hawajawahi kupewa mafunzo rasmi ya matumizi ya mfumo huu.

Aidha, hao ni moingoni wa watumiaji wakuu (core team) wa mfumo wanaotarajiwa kutowa mafunzo kwa watumiaji wengine kwenye Mawizara na Taasisi za Serikali zinazotarajia kutumia mfumo.

Kushindwa kuufahamu vizuri mfumo huo kunaweza kuathiri utoaji wa mafunzo kwa watumiaji wengine na kusababisha tatizo kubwa zaidi kwenye utumiaji wa mfumo ikiwa ni pamoja na matumizi hafifu ya mfumo, kutumika tofauti na matarajio, uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi, kutopata ripoti za kurahisisha kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati, kutopatikana kwa tija, ufanisi na urahisi wa kazi.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kushirikiana na mtoa huduma (Digiscan Technologies Ltd) kuandaa mpango kazi wa mafunzo na kutekeleza mafunzo hayo

kwa watumiaji wakuu (core team) kabla ya wao kuanza kwenda kufundisha watumiaji wengine katika Mawizara na Taasisi mbali mbali zinazotarajia kuutumia mfumo huu ili kupunguza gharama za kumtumia mzabuni, Digiscan katika kutoa mafunzo hayo lakini pia kujenga uwezo wa ndani pamoja na kuweka utaratibu utakao hakikisha kuwa mafunzo ya mfumo huo yanakuwa endelevu kwa kipindi chote ambacho mfumo utatumika ili kwamba waajiriwa wapya na wahamiaji wanapata nafasi ya kufundishwa matumizi ya mfumo na wakongwe wataongezewa maarifa kulingana na kukua na kupanuka kwa mfumo na mahitaji ya usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali.

5.5.1.9 Kutokufanyika kwa uimarishaji wa mfumo (System Upgrade).

Kuimarisha mfumo (System Upgrade) ni kufanywa mabadiliko ya kuongezea vitu katika mfumo kwa lengo la kurekebisha baadhi ya mapungufu, kuimarisha utendaji kazi, kupanua mfumo kwa kuongeza kipengele (feature) na kuboresha udhibiti.

Miongozo na viwango vinavyokubalika (best practice) vinaelekeza kufanyika kwa uimarishaji kwenye mazingira ya majaribio yanayofanana na mazingira halisi ambayo mfumo utatumika kwanza na kuhakikisha kwamba mfumo unafanya kazi kama inavyotarajiwa kabla ya kuupelekwa kwenye mazingira halisi, hii inaondoa hatari ya kushindwa kuendelea na kazi za kila siku kama uimarishaji umeleta shida kwenye mfumo kwa namna yoyote ile au kama uimarishaji umetambulisha namna tofauti ya kufanya kazi kwenye mfumo kama ilivyokua kabla ya uimarishaji na kuwapa watumiaji nafasi ya kusomeshwa mabadiliko husika kabla ya kuuweka kwenye mazingira halisi. Kutegemeana na sera za mtengeneza mfumo, ipo mifumo ambayo ili mtumiaji apate uimarishaji hana budi kulipia kiasi fulani cha fedha au wengine huwapa watumiaji wa mifumo yao uimarishaji bila gharama.

Hata hivyo, Muongozo ya Wakala wa Serikali mtandao Zanzibar wa mwaka 2021 kipengele cha 3(a) kinaitaka taasisi yoyote ya Serikali kuwasilisha pendekezo na umuhimu wa mahitaji ya uimarishaji wa mfumo (System Upgrade) huo kwa Wakala wa Serikali mtandao.

Ukaguzi umebaini yafuatayo:

- a) Wizara ilifanya uimarishaji wa mfumo wa usimamizi wa Mali za Kudumu za Serikali kwenye Seva halisi zinazotumika katika matumizi ya kila siku bila ya kuanza uimarishaji kwenye seva za majaribio kwanza na kuhakikisha kuwa mfumo unafanya kazi bila shaka na kwamba hakuna madhara hasi yaliyosababishwa na uimarishaji.
- b) Kuwa Wizara imefanya uimarishaji wa mfumo wa kusimamia Mali (Asset Management System) bila ya kupeleka pendekezo hilo kwa wakala wa Serikali mtandao kwa mujibu wa miongozo ya eGaz iliyopo.

Ukaguzi unashauri haya:

- a) Wizara ijiepushe kufanya uimarishaji wa mifumo yake moja kwa moja kwenye seva halisi kwani hali hii inaweza sababisha madhara makubwa kwa taasisi kwenye mfumo husika ikiwa ni pamoja na kusababisha mfumo huo usiweze kutumika. Katika kufanya uimarishaji ni vyema kufanyika majaribio ya uimarishaji mfumo kwenye seva za majaribio na kujiridhisha kwamba mfumo hauna madhara hasi katika utendaji kazi za Wizara pamoja na maarifa yanayohitajika

kuutumia mfumo ipasavyo kabla ya kuhamishia katika Seva halisi ili kutoathiri utendaji kazi na ufanisi.

- b) Kabla ya kufanyika uimarishaji wowote wa mfumo Wizara izingatie takwa la miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao la kupeleka pendekezo la uimarishaji huo kwa Wakala wa Serikali mtandao kwa ajili ya mapitio na kupata idhini ili kupata nafasi ya kufanya tathmini ya manufaa ya uimarishaji ukilinganisha na gharama za uimarishaji huo (cost benefit analysis).

5.5.1.10 Mfumo kutokuwa na sehemu kubwa ya taarifa za Mali za Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwa pamoja na kuendelea kuingizwa taarifa za mali za Serikali kwenye mfumo huu kwa zaidi ya miaka 4 sasa bado kuna taarifa nyingi hazijaingizwa kwenye mfumo na kwamba Wizara haina idadi kamili ya Mali zote za Serikali ambazo hazijaingizwa kwenye Mfumo na wala haizifahamu. Aidha, kwa kuwa kila kundi la mali lina umri wake maalumu wa kutumika na kisha kuondoshwa/ kuuzwa baada kuisha thamani taasisi nyingi za Serikali zitaendelea kununua mali na kuziingiza kwenye matumizi na baadhi hufikia umri wa kuondoshwa/ kuuzwa kabla Wizara kuzifikia taasisi hizo na kuingiza taarifa za mali zake kwenye mfumo kwa sababu inawachukua muda mrefu, zaidi ya miaka 4 sasa na hawajaweza kuzipitia Wizara zote kwa awamu ya kwanza ya kuingiza taarifa zilizopo kabla ya kuongelea taarifa za mali zinazoendelea kununuliwa kila mwaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango yafuatayo:

- a) Kuandaa mpango kazi utakao iwezesha kuingiza mali zote za Serikali kwenye mfumo ndani ya muda mfupi iwezekanavyo, mpango huu ujumuishe kufanya tathmini ya mali za Serikali ambazo hazijaingizwa kwenye mfumo, kufahamu mahitaji ya rasilimali vifaa, fedha na watu wanaotakiwa kuingiza taarifa hizi kwenye mfumo kwa uharaka unaostahili ikizingatia muda na ukubwa wa kazi ili kuepuka kulimbikizwa tena kwa mali mpya zinazonunuliwa kila mwaka na kulifanya zoezi hili kutokamilika na kwenda kwenye uingizaji wa taarifa za mali kama zinavyonunuliwa (live data entry of procured assets).
- b) Kutekeleza mpango kazi huo na kuisadia Serikali kupata tija na ufanisi kwenye matumizi ya mfumo huu ndani ya muda mfupi iwezekanavyo.
- c) Kuhuwisha taarifa za mali za Serikali zilizomo kwenye mfumo hususani kwenye eneo la mali zilizouzwa kwenye taasisi wakati tayari zilikuwa zimeshaingizwa kwenye mfumo na bila ya taarifa za uuzwaji huo kuingizwa kwenye mfumo kwa kuwa mfumo mpaka sasa haujaanza kutumika kwenye kuuza mali za Serikali pindi zinapotakiwa kuuzwa (live data entry).

5.5.1.11 Kutokuwepo kwa mpango wa kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Plan)

Mpango wa kuendeleza mfumo baada ya maafa/ mpango wa kupona maafa (disaster recovery plan) unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mripuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka

baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake kana kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Pia mpango huu unaainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, vile vile unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina Mpango wa kupona maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na "best practice guidelines" ambazo zinasisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango, kuongeza tija kwa wafanyakazi kwa kuwa wanakuwa wanafahamu nini cha kufanya na kinafanywa na nani kwa wakati gani, kuelewa ukubwa wa kazi zinazotakiwa kufanyika na kuendelea kuwahudumia wateja wa taasisi husika.

Athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Wizara haina mpango wa kupona maafa na pindi itakapofikwa na maafa hayo ni pamoja na kusababishiwa hasara kwa kushindwa kuendelea na kutoa huduma au kufanya kazi, kupoteza muelekeo kwa wafanyakazi kwa kutofahamu nini kifanyike na afanye nani kwa wakati gani na kupoteza tija na ufanisi kazini, kupoteza sifa ya Wizara katika kutegemewa kutoa huduma wakati wote.

Ukaguzi unashauri kutengenezwa mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na ile ya kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unakuwa wa kujitosheleza ili kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

SURA YA SITA

UKAGUZI WA MFUMO WA MISHAHARA WA SERIKALI (GOVERNMENT PAYROLL SYSTEM)

6.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango mnamo mwaka 2005 kupitia Idara ya Bajeti ilitengeneza mfumo wa kielektroniki wa Mishahara Serikalini (Government Payroll System) ambao pia ni “Web based” uliotengenezwa na wafanyakazi wa Wizara kwa gharama isiyofahamika mpaka kukamilika kwake, mfumo huu umewekwa kwenye seva ya Idara ya Bajeti ndani ya chumba cha seva cha Muhasibu Mkuu wa Serikali, mfumo unafanya kazi ya kusajili waajiliwa wote wa Serikali, kuandaa taarifa za malipo ya mishahara (payroll), kutunza kumbukumbu za malipo ya mishahara kwa wafanya kazi wote wa Mawizara, Idara, na Taasisi za Serikali (MDAs) ikijumuisha posho, makato na kutoa ripoti tofauti za kila mwezi za taarifa hizo.

Kimsingi mfumo huu uliisaidia Serikali kuanza kutambua kiurahisi waajiliwa wake kwa kuziingiza taarifa zao sehemu moja na kufanya usimamizi wa pamoja. Changamoto kadhaa zilizokua zinaikabili Serikali kabla ya kuanza kutumika mfumo huu (manual management of payroll) ilikuwa ni pamoja na uwepo wa watumishi wengi hewa, tarehe za kuzaliwa zisizo halisi na nyengine nyingi ambazo zilipungua kwa kiasi cha kutia moyo.

6.1 YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MISHAHARA WA SERIKALI

Hata hivyo, pamoja na mfumo huu kuendelea kutumika kwa zaidi ya miaka 15 sasa ukaguzi umebaini uwepo wa mapungufu mbalimbali tangu kuanzishwa kwake, miongoni mwa mapungufu hayo ni kama ilivyoainishwa hapo chini.

Kukosekana kwa nyaraka zote muhimu zinazohitajika kwa ajili ya usimamizi, uendelezaji na matumizi ya mfumo, miongoni mwa nyaraka ambazo hazipo ni pamoja na nyaraka inayoelezea jinsi mfumo ulivyosanifiwa (system architecture document), nyaraka ya usanidi wa mfumo (system configuration manual), nyaraka ya matumizi ya mfumo (system operations manual), daftali la kutunza kumbukumbu za matatizo ya mfumo na ufumbuzi wake (incidence/ issues register), nyaraka ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo (system users requirements document), nyaraka ya kuidhinisha mfumo kuanza kutumika (user acceptance certificate), kutozingatiwa kwa “best practice guidelines” katika utengenezaji wa mifumo (System Development Life Cycle),

Udhaifu wa mfumo kushindwa kubaini hali ya ustaafu kwa wafanyakazi wenyewe, Watumishi waliostaafu kuendelea kulipwa mishahara, kutozingatiwa mgawanyo wa majukumu kwenye mfumo, uwepo wa udhaifu wa kiusalama, Wizara kupitia Idara ya Bajeti haina mipango wa kukabiliana na maafa (Disaster Recovery Plan), kukosekana kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site), kutokuwepo kwa mpango wa kuchukua nakala za taarifa za mfumo (system backup plan), kutofanyiwa majaribio nakala za taarifa za mfumo (backup testing), kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara baada ya maafa (Business Continuity Plan).

6.1.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Malipo ya Mishahara wa Serikali dosari mbali mbali zimebainika kama zifuatazo:-

6.1.1.1 Kutokuwepo kwa nyaraka muhimu za mfumo wa "Payroll".

Ukaguzi umebaini Mfumo huo hauna nyaraka zozote zinazohusiana na mfumo ikiwemo nyaraka muhimu katika matumizi endelevu ya mfumo inayoelezea namna mfumo unavyofanya kazi (system operations manual), mfumo ulivyosanifiwa (system architecture document), mfumo ulivyosanidiwa (system configurations manual), na nyaraka nyingine kama vile za mahitaji ya mfumo (system requirements document), n.k.

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu wenye uwezo wa kufanya kazi za kuchakata taarifa za mabilioni ya fedha za mishahara ya watumishi wa umma kwa kila mwezi ukaguzi umebaini mfumo huu utengenezaji wake haukuzingatia miongozo na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kuanzia hatua ya awali ya utengenezwaji wake mpaka hatua ya mwisho (System Development Life Cycle – SDLC) ambayo inaelekeza kwamba mfumo unatakiwa kutengenezwa kwa kufuata hatua kwa hatua ambapo kila hatua inachangia katika kuhakikisha kwamba mfumo unaotengenezwa unakidhi mahitaji ya watumiaji kwa wakati uliopo na wakati ujao huku ukizingatia mikakati ya taasisi, udhibiti na usalama na kwamba unaongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika.

Kwa mfano, kuandaa mpango kazi wa kutengeneza mfumo (system planning) ni hatua ya kwanza katika "SDCL" ambapo pamoja na mambo mengine yanayofanyika ni kuandaa mpango kazi wa muda mrefu (long term plan), sera za kuchagua miradi ya TEHAMA, bajeti ya muda mfupi na muda mrefu ya TEHAMA, kufanya upembuzi yakinifu wa awali na kupata idhini ya uongozi wa taasisi ya kuendelea na mradi, andiko la pamoja na ratiba ya mradi (project schedule).

Hatua ya pili ni kufanya tathmini ya mfumo (systems analysis) ambapo wataalamu wa TEHAMA wanakusanya taarifa za mahitaji ya watumiaji wa mfumo (system users' requirements) na kuyachakata kisha huandaa nyaraka ya mahitaji (system requirements document), hatua nyingine ni pamoja na tatu mpaka nane katika mfuatano.

Kutokuwepo kwa nyaraka zote zinazohitajika katika utaratibu wa kutengeneza mfumo kunaweza kupelekea athari nyingi ikiwamo zifuatazo:-

- d) Mfumo kuwa mali ya mtu/ watu wachache badala ya taasisi, hii inatokana na ukweli kwamba aliyeutengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofisini basi mfumo huu hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na kuikosesha taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa na taasisi husika.
- e) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k kwani uandishi wa nyaraka

mbalimbali za mfumo unawapa nafasi watu na wadau wengine wa mfumo kuchangia mawazo yao katika namna ambayo ni rasmi ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuidhinisha nyaraka husika ili kuendelea na hatua nyingine jambo linalopelekea kuboresha mfumo utakaotengenezwa.

- f) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa kama kisiwa kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mingine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo linarudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- g) Tasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda, juhudi na jitihada zilizotumika mpaka kuupata mfumo uliokamili, hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- h) Taasisi kushindwa kudhibiti matumizi, muda na ubora wa mfumo husika kwa sababu hakuna mpango wala bajeti iliyoandikwa na kuidhinishwa na uongozi wa taasisi.
- i) Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.
- j) Kuendeleza utegemezi kwa mtoa huduma (system supplier) ikiwa mfumo umetengenezwa na mtoa huduma wa nje kwasababu taasisi inakuwa haina kumbukumbu muhimu ambazo ingeliweza kuzitumia kujenga uwezo wa ndani na kupunguza utegemezi kwa mtoa huduma jambo ambalo linaokoa gharama na kuipunguzia mzigo Serikali.

Ukaguzi unashauri kuzingatiwa kwa miongozo na viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumo kama hii ambapo nyaraka zote za mifumo ikiwa ni pamoja na bajeti, ratiba, usanifu wa mfumo, tija, utendaji kazi wa mfumo, usanidi wa mfumo, mipango kazi, mahitaji ya mfumo na uidhinishwaji wa nyaraka hizo vizingatiwe kabla ya kutengeneza au kununua mfumo wowote.

Aidha, kwa kuwa mfumo huu wa ulipaji mishahara Serikalini bado unatumika ni vyema wataalamu wa TEHAMA kwa kushirikiana na watumiaji wa mfumo ndani ya Wizara waandae nyaraka zote muhimu za mfumo na zipatikane kwa matumizi husika mapema iwezekanavyo ili kuondoa au kupunguza hatari iliyopo ya kupata athari kama zilivyoenezwa hapo juu.

Athari na ushauri huu pia utumike kwenye mifumo yote ya Wizara bila kujali Idara inayohusika na utengenezaji au ununuzi wa mifumo husika ambayo haina nyaraka zote muhimu kama zilivyoenezwa hapo juu iwe inayotengenezwa na wataalamu wa TEHAMA wa ndani au nje ya Wizara au kununuliwa ama kukodishwa.

6.1.1.2 Kutokuwepo kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan) - Rejea Hoja Namba 5.5.1.11

6.1.1.3 Kukosekana kwa mipango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan) - Rejea Hoja Nambari 5.5.1.5

6.1.1.4 Kutofanyika kwa majaribio ya nakala za taarifa za mfumo (Backup testing) – Rejea Hoja Nambari 5.5.1.6

6.1.1.5 Kutokuwa na eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery site/offsite) – Rejea Hoja Nambari 5.5.1.4

6.1.1.6 Mfumo kuwa na taarifa pungufu bila kujali umuhimu wake

Ukaguzi umebaini kuwa katika Mfumo wa mishahara wa Serikali kuna baadhi ya taarifa ambazo hazijakamilika kwa mfano kuna waajiriwa wengi hawana namba za pensheni (pension numbers) lakini pia mfumo umewezeshwa kuwekwa picha za watu ili kurahisisha utambuzi lakini taarifa hizo za picha hazijawahi kuingizwa kwenye mfumo. Kutokamilika kwa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo kunaweza kupelekea usumbufu wakati wa kuhitaji taarifa hizo za wafanyakazi hususani wakati wa kuhakiki wafanya kazi, lakini pia jambo hili linapunguza utegemezi (reliability) wa taarifa zilizomo kwenye mfumo kinyume na malengo ya jumla ya kutekeleza mifumo kama hii ambapo ni kufanya upatikanaji wa taarifa kamili na sahihi kwa wakati ili kurahisisha ufanya maamuzi katika matumizi yake.

Ukaguzi unashauri kuwa, ni vyema taarifa zote za wafanyakazi katika mfumo huo kuingizwa kwa ukamilifu ili kukamilisha malengo yaliyokusudiwa ya kutakiwa kuingizwa taarifa hizo yanatimia na kuepusha athari zinazoweza kutokea kama hatua stahiki hazitachukuliwa kama ilivyoelezewa hapo juu.

6.1.1.7 Mfumo kuwa na taarifa zenye makosa

Usahihi wa taarifa zinazolingizwa ndani ya mfumo ni jambo la muhimu kwa kuwa taarifa hizo hutumiwa kwa matumizi mbali mbali na Serikali ikiwemo kuwalipa watu mishahara na stahiki zao nyengine. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa kuna taarifa zilizomo kwenye mfumo ambazo zinamakosa, mfano wa taarifa hizo ni tarehe za kuzaliwa wafanyakazi hazikuwa sahihi kiasi ambacho ni ngumu kuzitumia kuamua muda wa kustaafu kupitia mfumo huo. Uwepo wa taarifa zenye makosa unapelekea athari zifuatazo:-

- a) Kucheleweshwa waajiriwa kustaafu kwa mujibu wa sheria za nchi kwa wale walioingiziwa tarehe za mbele jambo ambalo litapelekea Serikali kuwa na waajiriwa wengi ambao hawana uwezo wa kuzalisha kama inavyotarajiwa na kuisababishia Serikali hasara kwa kuwalipa watu mishahara wakati hawazalishi au hawatoi huduma kwa viwango vilivyowekwa. Pia, hali hii inaweza kuwazuia vijana kuingia kwenye ajira kwa sababu wazee hawaondoki na Serikali inaweza kuajiri sehemu ndongo tu ya wananchi.
- b) Kuwahisha waajiriwa kustaafu kabla ya umri stahiki kwa wale ambao wameingiziwa tarehe za nyuma tofauti na uhalisia, hali hii inaweza kupelekea Serikali kupoteza nguvu kazi ambayo bado ina uwezo wa kuzalisha kwa tija na ufanisi kwa kuzingatia ujuzi wao na kusabisha kucheleweshwa maendeleo ya nchi kwa ujumla.
- c) Taarifa zilizomo kwenye mfumo kutoaminika na kushindwa kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, jambo hili linaashiria kuikwamisha Serikali kupata matunda ya uwekezaji wake kwenye mfumo huu na TEHAMA kwa ujumla.
- d) Kuitia hasara Serikali kwa kuwalipa watu zaidi ya wanavyostahili kutokana na makosa yaliyofanyika na kwa kuwa mfumo huu unahusiana na malipo
- e) Watu kulipwa pungufu ya wanachostahili.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo:

- a) Wizara izipitie kwa umakini taarifa zote za waajiriwa ili kuweza kubaini zile ambazo haziko sahihi na kuzichukulia hatua.
- b) Wizara iandae mpango kazi wa kuhakiki waajiriwa wote wa Serikali na kukusanya taarifa sahihi ikiwa ni pamoja na tarehe za kuzaliwa, mwaka wa ajira, taasisi wanazofanyia kazi, vyeo, stahiki zao, ustaafu wao, n.k. kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo.
- c) Kuutekeleza mpango kazi husika kwa kuzingatia weledi, tija na ufanisi ndani ya muda muafaka ili kuepusha madhara kama yalivyoelezwa hapo juu kwenye athari.
- d) Uingizaji wa taarifa kwenye mfumo ufanywe na mtu mmoja na pawepo na mtu mwingine anayethibitisha au kuidhinisha usahihi na uhalisia wa taarifa zinazolingizwa kabla ya kwenda kwenye hatua ya kutengenezewa mishahara na kulipwa.

6.1.1.8 Mfumo kushindwa kubaini hali ya ustaafu kwa watumishi wenyewe (automatically).

Moja ya malengo ya kuanzishwa mfumo ni kurahisisha kazi, kuongeza tija na ufanisi na utendaji bora wa kazi hizo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa mfumo huu hauna uwezo wa kubaini hali ya ustaafu ya waajiriwa hali ambayo inaweza kusabisha kuwepo kwa waajiriwa hewa wanatokana na mwajiriwa kustaafu utumishi lakini kwa sababu mfumo hauwezi kutambua hali hii na kwa sababu pia watumiaji wa mfumo wameshindwa kuchua hatua stahiki za kumsitishia mishahara mstaafu husika, basi anaendelea kupokea mishahara kama kwamba bado yuko katika utumishi kwa muda usiojulikana.

Aidha, udhaifu huu wa mfumo unaweza kusababishia Serikali kupata hasara kwa kuwalipa watumishi hewa na kuchelewesha kufanya maendeleo katika huduma nyingine za jamii kama vile ujenzi wa hospitali, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Pia, hali hii inaweza kuweka ugumu katika mipango ya Serikali kwa kutofahamu gharama sahihi za mishahara ya kila mwezi na mwaka mzima.

Ukaguzi unaishauri kuwa, ni vyema kuuboresha mfumo na kuhakikisha kuwa unauwezo wa kubaini muda wa kustaafu na kuzuia malipo ya mishahara wenyewe (automatic detection and block) hususani pale mtumishi anapofikia umri wa lazima wa kustaafu na ikiwezekana mfumo utume ujumbe (message alert) kwa njia ya simu ya mkononi au barua pepe kwa msimamizi wa mfumo (system administrator), Mkurugenzi rasirmali watu wa taasisi ya mtumishi, ili kuwakumbusha kuchukua hatua kwa upande mwingine.

6.1.1.9 Ulipaji wa mishahara kwa watumishi waliostaafu.

Ukaguzi umebaini mfumo wa ulipaji wa mishahara Serikalini umeruhusu ulipaji wa mishahara kwa watumishi walio staafu, katika sampuli iliyofanyika ya uchunguzi ukaguzi umebaini uwepo wa mtumishi aliyestaafu mwezi wa Februari, 2021 lakini aliendelea kulipwa mishahara mpaka mwezi wa Julai, 2021 ambayo ni zaidi ya shilingi 3,129,000.

Aidha, hali hii inaashiria kuwepo kwa udhaifu kwenye taasisi inayosimamia watumishi wa umma

kwa kushindwa kubaini watumishi wanaotarajia kustaafu ndani ya miezi walau mitatu kutoka kila taasisi ya umma na kuchukua hatua stahiki za kuhakikisha kua wanaandaliwa mazingira ya kustaafu salama ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa Ofisi ya Fedha kuhusu kuwasitishia mishahara watumishi husika.

Hivyo basi, ukaguzi unashauri kufanyika uhakiki wa watumishi wote ili kubaini watumishi ambao tayari walisha staaifu lakini bado wameendelea kulipwa mishahara kana kwamba bado wako kwenye utumishi na kisha kuchukua hatua za kuwasitishia mishahara hiyo na kuwaondoa wote kwenye mfumo wa ulipaji wa mishahara Serikalini.

6.1.1.10 Mfumo kutokuwa na usalama wa uhakika (Security)

Moja kati ya vitu muhimu vinavyotakiwa kuzingatiwa sana katika utenegnezaji na utumiaji wa mfumo ni usalama wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo ili taarifa hizo ziendelee kuwepo, ziendelee kuwa kamili na sahihi, na ziwe siri kwa kadri inavyohitajika.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa hakuna usalama wa mfumo na taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo huo kutokana na mfumo kutengenezwa kwa teknolojia ya zamani ya **Visual Basic 6.0** ambayo kwa sasa kampuni ya Microsoft iliyotengeneza teknolojia hiyo imeacha kuiboresha na kuimarishaji kiusalama wa baadhi ya sehemu za programu hiyo tangu tarehe 8 Aprili, 2008. Hali hii inapelekea kuhatarisha usalama wa mfumo na taarifa zinazolingizwa ndani ya mfumo husika kuwa uko katika hatari kubwa ya kuathiriwa kirahisi na virusi au udukuzi na kusababisha taarifa hizo kupotea, kubadilishwa au kuvuja na kuingia mikononi mwa watu wasio na nia njema.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuchukua hatua za makusudi mapema iwezekanavyo ili kupata mfumo mwingine kwa ajili ya malipo ya mishahara kwani mfumo uliopo kwa sasa unahataria kubwa kama ilivyoelezwa hapo juu.

6.1.1.11 Udhaifu kwenye udhibiti wa utumiaji wa mfumo – Rejea Hoja Nambari 5.5.1.7

6.2 MATOKEO YA UKAGUZI KWENYE UDHIBITI WA TEHAMA KWA UJUMLA

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Usajili wa mali za Serikali Mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo dosari zifuatazo: -

6.2.1 Kutokuwa na Sera ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha TEHAMA cha Wizara hakina sera za TEHAMA zilizowekwa kwa kusimamia taratibu na shughuli zote zinazohusiana na TEHAMA, badala yake shughuli za TEHAMA zinafanywa na kusimamiwa kama inavyoombwa na watumiaji wa mwisho, bila kufuata taratibu na miongozo rasmi inayotakiwa na iliyotengenezwa kulingana na mikakati na mipango ya Wizara na matumizi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na miundombinu yake.

Kutokuwepo kwa sera madhubuti za TEHAMA kunaweza pelekea udhaifu katika usalama, udhibiti, uratibu, usimamizi wa shughuli zote za TEHAMA ikiwa ni pamoja na matumizi ya rasilimali za TEHAMA, mawasiliano kwa barua pepe, na uwekezaje kwenye Wizara.

Ukaguzi unaishauri Wizara kupitia cha TEHAMA kuandaa sera za TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala Serikali mtandao na miongozo ya kimataifa kama vile COBIT 2019, AFROSAI-E ambazo zitahidhinishwa na menejimenti ya Wizara. Aidha, Wizara inashauriwa kuzitumia sera hizo ili kupata matokeo bora ya udhibiti na usimamizi wa TEHAMA ndani ya Wizara.

6.2.2 Kutumika kwa barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kiofisi.

Sera za Wakala wa Serikali mtandao kifungu nambari 4.10.1.2(a) inazitaka taasisi zote za Serikali na watumishi wake kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwenye mawasiliano yote ya kiofisi ya kielektroniki ili kuhakikisha usalama wa taarifa zote za Serikali. Hii inamaanisha kwamba mawasiliano yoyote ya kazi za Serikali yanapaswa kufanywa kwa kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwa sababu za kiusalama kwenye taarifa hizo zinasafirishwa toka kwa mtu au taasisi moja kwenda kwa mpokeaji ambaye ni mtumishi au taasisi ya Serikali. Matumizi ya "Gmails", "Yahoo mails", "Hotmails" n.k hayaruhusiwi kwa watumishi wa Serikali.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini sehemu kubwa ya watumishi wa Wizara wanatumia barua pepe zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kikazi kama vile gmail, yahoo na hotmail. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sera za Serikali mtandao lakini pia ni kuhatarisha usalama wa taarifa za Serikali.

Ukaguzi unaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kipitia kitengo cha TEHAMA mambo yafuatayo:-

- a) Kufanya utafiti mdogo wa matumizi ya barua pepe kwenye mawasiliano ya kikazi ili kuelewa ni kwa nini watumishi wengi hawatumii barua pepe za Serikali na kuwasilisha ripoti ya utafiti huo kwenye menejimenti ya Wizara kwa ajili ya kuchukua hatua sitahiki kulingana na yatakayokuwa yamebainika, ikiwa ni pamoja na kuwatengenezea barua pepe rasmi watumishi wote wasio kuwanazo.
- b) Kuwapatia mafunzo endelevu ya namna ya kuzitumia barua pepe hizo ipasavyo na kuleta tija.
- c) Kusimamia na kuratibu miundombinu ya TEHAMA ya Wizara wakati wote kuhakikisha kwamba haikwamishi matumizi ya barua pepe hizo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya barua pepe, mtandao (internet), uwezo wa kutuma na kupokea mafaili ili kuchechemua matumizi ya barua pepe hizo Wizarani.

SURA YA SABA**UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI NA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII
(CRVS)****7.0 UTANGULIZI**

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ni matokeo ya muunguniko wa iliyokuwa Ofisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali na iliyokuwa Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa matukio ya Kijamii nambari 3 ya mwaka 2018 ambayo iliunda Wakala huu tarehe 02 Januari, 2018.

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar inafanya kazi zake chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku, Wakala inawahudumia wateja wake kupitia Vituo vya Usajili wa Matukio ya Kijamii vilivyopo katika wilaya kumi na moja (11) za Unguja na Pemba ambapo Makao Makuu ya Wakala ipo Migombani na ofisi zake nyengine zipo Mazizini Unguja Jengo la Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora.

Wakala inaongozwa na Bodi ya Ushauri ambapo imejumuisha wajumbe mbali mbali waliotajwa katika kifungu nambari 5 cha Sheria ya Usajili wa Matukio ya mwaka 2018. Mkurugenzi Mtendaji ndio Afisa Masuuli wa wakala anayeshughulika na kazi za kiutawala kwa kushirikiana na wakurugenzi wa idara mbali mbali zilizopo chini yake.

7.1 KAZI ZA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

Kifungu nambari 4(1) cha sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kinaeleza kazi za Wakala kama zifuatazo:-

- a) Kusajili na kutoa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.
- b) Kusajili matukio ya kijamii yanayojitokeza ikiwemo vizazi, vifo, ndoa na talaka.
- c) Kutoa vyeti vya matukio ya kijamii kwa matukio yaliyosajiliwa.
- d) Kutoa nambari ya upekee ya utambulisho wa Mzanzibari kwa watu waliotimiza sifa za usajili wa Mzanzibari mkaazi.
- e) Kutengeneza, kusimamia na kuendesha daftari la matukio ya Kijamii.
- f) Kuhakikisha na kuthibitisha taarifa zinazohusiana na usajili wa matukio ya kijamii.
- g) Kuhakikisha ulinzi na usalama wa taarifa zilizokusanywa na kuhifadhiwa kwenye daftari la usajili wa matukio ya kijamii.
- h) Kuanzisha Mifumo ya Kielektroniki ya kuweka kumbukumbu za usajili wa matukio ya kijamii.
- i) Kuunganisha mifumo ya kielektroniki kwa taasisi za Serikali ambazo zitahitajia kupata taarifa zinazohusu matukio ya kijamii.

7.2 MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA

Kutokana na maendeleo ya ukuwaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa kiasi kikubwa inatekeleza kazi zake za usajili wa matukio ya kijamii kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

Kwa sasa Wakala inatumia mifumo mitatu kwa ajili ya kusimamia kazi za kila siku za usajili ambapo mifumo hiyo imejumuishwa Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Takwimu (CRVS System) uliotengenezwa na kampuni ya NDR mwaka 2015 kwa gharama za dola za kimarekani (USD) 149,940 sawa na shilingi 261,114,512.4 za kitanzania, Mfumo wa Usajili wa Mzanzibari Mkaazi (ZanID Registration System) pamoja na Mfumo wa uzalishaji vitambulisho vya kawaida (Multi-ID's system). Taarifa kamili kuhusu mifumo hiyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 18**.

7.3 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi anavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nambari 11 ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

7.4 MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho lakuridhishakwamba Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii una ulinzi na udhibiti kwenye miundombinu inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake nakuhakikisha kuwa zina uadilifu na vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi kupitia TEHAMA. Aidha, ukaguzi huu pia ulikuwa na malengo maalumu kama yalivyoainishwa hapa chini:-

- a) Kubainisha ufuatishwaji wa sheria, kanuni, sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa.
- b) Kufanya tathiminiya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.
- c) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.
- d) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- e) Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.

- f) Kubainisha kama Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ina Mpango wa Mwendelezo wa Biashara pamoja na Mpango wa Kukabiliana na Maafa.

7.5 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya ndani na ya kimataifa kama vile eGaz, COBIT, e-Government URT, AFROSAI n.k. Katika kukagua mifumo ya Wakala nilitumia mbinu mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:-

- a) Kupitia Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo mbali mbali inayohusiana na usajili wa matukio ya kijamii pamoja na usajili wa Mzanzibari.
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kupitia mfumo wa udhibiti wa ndani katika usajili wa matukio ya kijamii.
- c) Kupitia sera za usimamizi pamoja na miongozo ya uongozaji wa teknolojia ya TEHAMA inayotumika kwa wakala.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika ununuzi, uwekaji na uondoshaji wa mali zinazohusiana na teknolojia ya TEHAMA.
- e) Kupitia mifumo ya TEHAMA ili kutazama udhibiti wa ndani uliyopo katika mifumo hiyo.
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti yaliyomo katika mifumo ya TEHAMA.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizotokana na mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano pamoja na watumiaji mbali mbali juu ya mifumo inayotumika na Wakala.
- i) Kutembelea katika vituo mbali mbali vilivyoundwanishwa mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii pamoja na mfumo wa usajili wa Mzanzibari.
- j) Kutembelea vituo vyenye miundombinu ya mitandao ya mifumo ya Wakala pamoja na vituo vya kutunza taarifa za mifumo hiyo.
- k) Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi na kumaliza kazi za ukaguzi na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi, na
- l) Kutembelea ofisi za Wilaya zilizo chini ya Wakala wa Matukio ya Kijamii kwa lengo la kuangalia ufanyaji kazi wa ofisi hizo.

7.6 MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

7.6.1 Mfumo wa Usajili na Takwimu za Matukio ya Kijamii (CRVS)

Matumizi hafifu ya mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, uwepo wa udhibiti hafifu katika kuingiza taarifa kwenye mfumo, ruhusa za kufikia na kufanya kazi kwenye mfumo kupewa watu wasiostahili, utengenezaji wa nambari za utambulisho wa watoto kwa njia ya kawaida (manually), uwepo wa taarifa za usajili zinazojirudia.

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa nambari za utambulisho zaidi ya moja kwa mtoto mmoja, udhibiti

hafifu katika utowaji na utumiaji wa magamba maalum ya kuchapishia vyeti, kutokuwepo kwa makubaliano ya huduma za kitaalumu za mfumo baina ya Wakala na "Supplier" wa mfumo wa CRVS, mfumo kutokutunza kumbukumbu za matukio yote yanayotokea kwenye mfumo kwa ajili ya ukaguzi (audit trails), kutokuwepo kwa orodha ya watu waliosajiliwa na kupewa leseni za kutoa nyaraka za "marriage notification", na kutokuwepo kwa nyaraka inayoonesha utaratibu rasmi wa kufuatwa ili kufanya mabadiliko yoyote kwenye mfumo (change management document)

7.6.2 Udhhibiti wa ujumla na uendeshaji wa TEHAMA

Katika udhibiti wa ujumla na uendeshaji wa TEHAMA ukaguzi umebaini mambo yafuatayo kama vile kutokuwepo kwa nyaraka za sera za TEHAMA, kutokuwepo kwa nyaraka za mikakati na mipango ya TEHAMA, kutokuwepo kwa muongozo wa uanzishaji wa kamati ya uendeshaji ya TEHAMA, kutokuwepo kwa kamati ya uendeshaji ya TEHAMA, kutokuwepo kwa ripoti ya tathimini ya usimamizi wa hatari na ufuatishaji taratibu na miongozo ya TEHAMA (risk management and compliance), kutokuwepo kwa daftali la rasilimali za TEHAMA, kutokuwepo kwa nyaraka inayoonesha utaratibu rasmi wa kufuatwa ili kufanya mabadiliko yoyote kwenye mfumo (change management document), Kutokuwepo kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara (BCP) pamoja na kukosekana kwa mpango wa kupona Maafa (DRP).

7.7 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA USAJILI NA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII (CRVS)

7.7.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

Baada ya kuupitia mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (CRVS) ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:-

7.7.1.1 Mapungufu yaliyobainika katika mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (CRVS)

Baada ya kupitia mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa CRVS, ukaguzi umebaini kwamba tarehe 14 Januari 2014 Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) iliyotambulika kama ni "Mteja" imefunga mkataba na "Norway Registers Development (NRD)" aliyetambulika kama ni "Mshauri Mwelekezi" kwa ajili ya kazi ya kutoa ushauri na kutengeneza Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

Mkataba huo ulifungwa kupitia zabuni nambari NBS/AE/WB/052/2013/2014/ TSMP/C/12 kwa thamani ya jumla ya dola za kimarekani (USD)149,940 ikiwa sawa na shilingi 261,114,512.4 za kitanzania. Miongoni mwa mapungufu yaliyobainika katika mkataba huo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imeingia kwenye mkataba kwa niaba ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar (OCGS) ambapo wao wameiwakilisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kama mdau wao wa takwimu za matukio ya kijamii.
- (ii) Mkataba hauna sahihi ya upande mmoja (Mteja).
- (iii) Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, haijahusika moja kwa moja na Mkataba huo.

Kuwepo kwa mapungufu hayo kunapelekea mkataba kukosa sifa za uhalali wa makubaliano baina

ya pande mbili na hatimae mkataba huo kuwa batili (null and void), na hivyo Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar hatosomeka kama ni mmiliki halali mwenye hatimiliki za mfumo wa CRVS.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kuhakikisha wanayapitia makubaliano ya awali baina ya Wakala na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar ili kujenga misingi imara ya kisheria juu ya umiliki halali wa mfumo wa CRVS pamoja na kuendelea kupata huduma za msaada wa kiufundi kutoka kwa wauzaji wa mfumo huo (NRD).

7.7.1.2 Kutokutumika kikamilifu kwa mfumo wa CRVS

Baada ya kupitia mfumo wa kielektroniki wa usajili wa matukio ya kijamii (CRVS), ukaguzi umebaini kwamba mfumo huo umejumuisha jumla ya moduli nne (4) zenye kujitegemea ambazo zinafanya kazi ya usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka lakini hadi ukaguzi huu unakamilika ni moduli moja tu ndio inayotumika kwa ajili ya kazi za usajili wa vizazi, na moduli zilizobakia hazitumiki na kupelekea kazi za usajili wa vifo, ndoa na talaka kuendelea kufanyika kwa njia ya kawaida ya mkono (manual).

Kushindwa kutumia mfumo kikamilifu kunapelekea kudhoofisha juhudi za uwekezaji wa mifumo ya TEHAMA ambapo malengo yake yanakwenda sambamba na malengo makuu ya Wakala katika kuongeza ufanisi wa usajili wa matukio ya kijamii.

Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4(b) cha Sheria Nambari 3 ya mwaka 2018, ambapo imeitaka wakala kutunza kumbukumbu za usajili wa matukio ya kijamii katika mifumo ya kielektroniki iliyoianzisha.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kuhakikisha moduli zilizomo katika mfumo wa CRVS zinafanyakazi na kutumika katika usajili wa matukio ya kijamii ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi za kuchakata data, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa taarifa zinazohusiana na matukio ya kijamii.

7.7.1.3 Kutokuwepo kwa udhibiti wa uthibitishaji wa taarifa zinapoingizwa kwenye mfumo (data input validation control)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika mfumo wa CRVS hauna udhibiti wa kukagua na kuthibitisha data ili kubaini usahihi wa data iliyoingizwa kwenye mfumo. Kutokuwepo kwa udhibiti wa uthibitishaji data kunaweza kusababisha mfumo kupokea data isiyo sahihi na kupelekea kutoa taarifa zisizo sahihi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4(1) cha sheria nambari 3 ya mwaka 2018 ambapo inaitaka Wakala kuhakikisha taarifa zinazohusiana na matukio ya kijamii zinabakia kwenye usawa na usahihi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari mbali mbali katika uingizwaji wa data kwenye mfumo wa CRVS ambazo zimetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa uthibitishaji data:-

a) **Kubainika kwa tarehe za kuzaliwa zisizo sahihi (unrealistic DWD_OCURRENCE_DATE)**

Kutokana na uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi imepelekea uwepo wa taarifa za watoto waliosajiliwa zilizotolewa katika mfumo wa CRVS ambapo tarehe zao za kuzaliwa haziendani na uhalisia na kupelekea uwepo wa mrundikano mkubwa wa taarifa zisizo sahihi kama zinavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 19.

b) **Makosa yaliyobainika katika Nambari za Utambulisho wa Mtoto**

Katika mfumo wa CRVS, nambari ya utambulisho wa mtoto inatolewa kwa kuzingatia muundo wa **D/N/YYYY** ambapo **D**, ni Wilaya ambayo mtoto amezaliwa na kusajiliwa na kila wilaya imepewa utambulisho wa herufi yake, **N** ni nambari ya idadi ya mtoto aliyesajiliwa na **YYYY** ni mwaka husika wa usajili.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa CRVS unapokea na kuhifadhi nambari za utambulisho wa mtoto ambazo hazipo katika muundo sahihi unaokubalika na wakala.

Jadweli lililopo katika **Kiambatisho Nambari 20** linaonesha nambari za utambulisho wa watoto (**INJ_REGISTRATION_NR**) ambazo hazipo katika muundo sahihi.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kuhakikisha wanafanya maboresho ya mfumo wa CRVS ili kuweka udhibiti wa uthibitishaji data zinapoingizwa (Data Input validation controls), ili kulinda usahihi wa data zinazoingizwa na kuzalisha taarifa zenye usahihi na uadilifu kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 4(1)(I) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ya mwaka 2018.

7.7.1.4 Ruhusa ya kuidhinisha taarifa zilizosajiliwa imepewa kwa watu wasio stahiki

Baada ya kupitia mfumo wa CRVS, ukaguzi umebaini kwamba ruhusa ya kuidhinisha taarifa zilizosajiliwa kabla ya kuchapisha cheti cha kuzaliwa amepewa ofisa msaidizi wa TEHAMA ambaye kimsingi hastahiki kufanya muamala huo ndani ya mfumo kama ilivyobainika katika picha hapo chini ambapo jina la afisa huyo limetiwa kivuli. Hata hivyo ukaguzi haukupatiwa uthibitisho wowote wa afisa huyo kuwa ameidhinishwa kwa mujibu wa sheria.

Kutoa ruhusa ya kuidhinisha taarifa zilizosajiliwa kwa watu wasiostahiki kunahatarisha matumizi sahihi ya idhini hiyo (risk of mis-using access privilege) na kupelekea kusajili na kutoa vyeti kwa watoto wasio stahiki.

Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 26(1) cha sheria nambari 3 ya mwaka 2018 ambapo inamtaka Mkurugenzi Mtendaji au mtu aliyempa dhamana ndie atakuwa na wajibu wa kuidhinisha taarifa zilizosajiliwa pamoja na kutoa vyeti vya usajili wa matukio ya kijamii.

Ukaguzi unashauri kwa Uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba ruhusa ya kuidhinisha taarifa zilizosajiliwa kabla ya kutoa cheti ibakie kwa mtu aliyepewa dhamana na Mkurugenzi Mtendaji kwa mujibu wa kifungu nambari 26(1) cha Sheria Nambari 3 ya mwaka 2018.

7.7.1.5 Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu

Katika ukaguzi wetu, tumebaini kwamba mtumiaji wa mfumo wa CRVS anaweza kukamilisha hatua zote za usajili wa taarifa za kuzaliwa, kuanzia kuthibitisha nyaraka za usajili, kuingiza taarifa za mtoto, kuidhinisha usajili hadi kuchapisha cheti cha kuzaliwa.

Kutoa upendeleo mkubwa wa kuufikia mfumo (too much access privilege) bila ya kuzingatia mgawanyo wa majukumu kunaweza kutoa fursa ya kusajili watoto ambao hawajatimiza vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba utaratibu wa usajili unaofanyika kupitia mfumo wa CRVS, unazingatia utaratibu bora unaokubalika kwa kufuata kanuni ya "Check and Balance" ambapo kila hatua ya usajili inafanywa na mtu tofauti ili kujiridhisha na kuongeza uwajibikaji katika kila hatua ya usajili.

7.7.1.6 Kuwepo kwa nakala za taarifa (duplicate data)

Baada ya kupitia mfumo wa CRVS, ukaguzi umebaini kuwepo kwa kiasi kikubwa cha taarifa zilizofanana (nakala) ambazo zimehifadhiwa ndani ya mfumo huo ikiwemo majina pamoja na nambari za utambulisho wa watoto waliosajiliwa.

Kuwepo kwa nakala za taarifa katika mfumo, kunahatarisha usahihi na uadilifu wa taarifa zinazozalishwa kupitia mfumo huo na kunaweza kupelekea kupotosha watumiaji wa taarifa hizo.

Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo wa nakala za taarifa zilizobainika katika taarifa za vyeti vya watoto vilivyotolewa kuanzia tarehe 1 Julai 2020 hadi 30 Juni 2021 kutoka katika Wilaya sita (6) za Zanzibar.

Jadweli Nambari 33: Mchanganuo wa nakala za taarifa zilizobainika katika taarifa za vyeti vya watoto vilivyotolewa.

NAMBA	OFISI ZA WAKALA ZA WILAYA	JUMLA YA VYETI VYA KUZALIWA VILIVYOTOLEWA (ISSUED)	JUMLA YA NAKALA ZA VYETI ZILIZOBAINIKA (DUPLICATES OBSERVED)	JUMLA YA NAKALA ZA VYETI ZILIZOTOLEWA (DUPLICATE REMOVED)	JUMLA YA VYETI HALISI VILIVYOTOLEWA (ISSUED)
1	Mjini, Unguja	34,250	11,198	6,328	27,922
2	Kaskazini "A", Unguja	13,395	5,519	3,103	10,292
3	Magharibi "B", Unguja	4,395	1,202	694	3,701
4	Kusini, Unguja	1,896	380	210	1,686
5	Micheweni, Pemba	13,489	3,523	1,936	11,553
6	Mkoani, Pemba	15,151	5,364	3,034	12,117
Jumla		82,576	27,186	15,305	67,271

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kufanya zoezi la kusafisha kanzidata ya mfumo wa CRVS ili kuweza kuondoa taarifa zinazojirudia pamoja na taarifa zenye makosa pamoja na kuwekanambari ya utambulisho wa mtoto iwe ndio nambari ya upekee (Primary Key) kwenye kanzi-data ya mfumo wa CRVS badala ya kutumia nambari ya maombi ya usajili ambapo muombaji anaweza kufanya maombi kwa zaidi ya mara moja, hali hii itapelekea kuondosha kuwepo kwa nakala za taarifa za usajili wa matukio ya kijamii.

7.7.1.7 Watoto waliosajiliwa kupewa nambari za utambulisho zaidi ya moja

Ukaguzi umebaini zaidi ya watoto 6,394 waliosajiliwa kupitia mfumo wa CRVS wamepatiwa nambari za utambulisho wa kipekee zaidi ya moja. Kuzalisha na kuwapatia watoto nambari za utambulisho zaidi ya moja kunaweza kupelekea kushindwa kumtambua muhusika halisi endapo utambulisho huo utatumika katika kufanya udanganyifu (fraudulent use) au uhalifu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 21(6) cha Sheria nambari 3 ya mwaka 2018, inayoeleza kwamba "nambari ya usajili itakayotolewa kwa mtoto katika cheti cha kuzaliwa itakuwa ni nambari ya utambulisho wa kipekee na haitobadilishwa kwa kipindi chote cha maisha yake".

Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo wa watoto waliopatiwa nambari za utambulisho zaidi ya moja katika vyeti vilivyotolewa kuanzia tarehe 1 Julai 2020 hadi 30 Juni 2021 kutoka katika Wilaya sita (6) za Zanzibar. Idadi ya watoto wenye nambari za utambulisho zaidi ya moja.

Jadweli Nambari 34 :Orodha ya watoto wenye nambari ya utambulisho zaidi ya moja

Namba	Ofisi za Wakala za Wilaya	Idadi ya watoto wenye nambari za utambulisho zaidi ya moja
1.	Mjini, Unguja	2,655
2.	Kaskazini "A", Unguja	1,150
3.	Magharibi "B", Unguja	388
4.	Kusini, Unguja	115
5.	Micheweni, Pemba	804
6.	Mkoani, Pemba	1,282
Jumla ya Idadi ya Watoto		6,394

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kufanya maboresho ya mfumo wa CRVS kwa kuweka udhibiti unaostahiki ili kuhakikisha kwamba kila mtoto anayesajiliwa anapatiwa nambari moja ya upekee ambayo haitabadilika kama ilivyo elekezwa katika kifungu nambari 21(6) cha Sheria ya Usajili wa Matukio ya Kijamii ya mwaka 2018.

7.7.1.8 Kutokuwepo kwa jukwaa sahihi la kuripoti matatizo ya mfumo na kutoa njia bora za kuyapatia ufumbuzi

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala haina jukwaa sahihi la kuripoti matatizo ya kiufundi yanayojitokeza katika mifumo badala yake wanatumia mtandao wa "WhatsApp" kwa ajili ya kuripoti na kupatiwa maelekezo ya ufumbuzi wa matatizo yanayojitokeza kwenye mifumo.

Kutumia mtandao wa "WhatsApp" kunahatarisha usiri wa taarifa zilizomo katika mifumo lakini pia kunatoa fursa kwa watumishi wanaotoa huduma kuingia kwenye mitandao ya kijamii na kupelekea kudumaza kasi ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuwa na nyenzo bora ya kupokea matatizo ya mfumo, kutunza kumbukumbu za matatizo na ufumbuzi wake ili kutumika kwa siku zijazo na kusaidia kupunguza gharama za utegemezi kwa utaalumu.

7.7.1.9 Kutokuwepo kwa udhibiti katika utowaji na utumiaji wa magamba maalum ya kuchapishia vyeti

Ukaguzi umebaini kwamba magamba ya kuchapishia vyeti vya kuzaliwa yanatolewa kwa maofisa wa usajili bila ya kuzingatia utaratibu wa kudhibiti matumizi sahihi ya magamba hayo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea magamba hayo kutumika katika udanganyifu wa kuchapisha vyeti vya watoto kinyume na utaratibu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuweka na kuzingatia utaratibu bora wa kudhibiti utoaji, usambazaji na utumiaji wa magamba ya kuchapishia vyeti vya kuzaliwa ili kuepusha athari za matumizi mabaya ya magamba hayo.

7.7.1.10 Mapungufu yaliyobainika katika kompyuta za vituo vya kazi (Workstations)


Kompyuta za vituo vya kazi, ni kompyuta maalum ambazo zimeunganishwa na mtandao wa mfumo wa CRVS kwa ajili ya kutoa huduma za usajili wa matukio ya kijamii kwa wananchi wanaofika vituoni hapo. Baada ya kupitia kompyuta hizo, ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo:-

a) Kutokuingizwa programu ya kuzuia virusi

Ukaguzi umebaini kwamba kompyuta za vituo vya kazi hazijaingizwa programu za kuzuia virusi, hali hii inahatarisha usalama wa taarifa za mfumo uliokuwemo katika kompyuta hizo, pia inapunguza ufanisi wa kompyuta na kupelekea kushindwa kutoa huduma za usajili wa matukio ya kijamii kwa ufanisi zaidi.

b) Kutokufungiwa kwa majukwaa ya mitandao ya kijamii (social media platform)

Ukaguzi umebaini kompyuta za vituo vya kazi hazijafungiwa kuingia katika majukwaa ya mitandao ya kijamii, hivyo watumiaji wa kompyuta hizo kwa wakati wowote wanaweza kuingia katika majukwaa ya mitandao ya kijamii kama inavyoonekana katika picha hapo chini.



Hali hii inahatarisha usalama wa taarifa za mfumo kwa kutoweka sera za ulinzi wa mfumo kwa wavamizi wa mifumo wanaotumia mitandao ya kijamii.

Aidha, kufanya hivyo kunatoa fursa kwa watumishi wanaotoa huduma kupitia kompyuta za vituo vya kazi kuingia kwenye mitandao ya kijamii na kupelekea kudumaza kasi ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuandaa sera na miongozo na kuzifungia tovuti za mitandao ya kijamii na kuhakikisha kompyuta zote za vituo vya kazi zinawekewa programu imara ya ulinzi wa kuzuia virusi ili kutunza usalama wa taarifa za mifumo pamoja na kuimarisha ufanisi wa kompyuta hizo.

SURA YA NANE

UKAGUZI WA MFUMO WA UVIKO – 19 NA MFUMO WA MALARIA (MEEDS) KATIKA WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII, WAZEE JINSIA NA WATOTO

8.0 UTANGULIZI

Wizara ya Afya, Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar inasimamia masuala yote yanayohusiana na afya ndani ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu 53 ambacho kinampa Mamlaka Raisi kuanzisha au kufuta ofisi Zanzibar.

Maabara ya Taifa ya Mnazi mmoja (Pathology Lab) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria na inajukumu la kufanya vipimo vya maradhi mbali mbali. Maabara ya Pathologia walianza kupima COVID mnamo OCTOBER 2020 kwa wasafiri “traveller” na washukiwa “suspect” na walikuwa wana kipimo cha RT-PCR “Real-time PolymerizedChain Reaction” tu na baadae kuanza na kipimo cha Antigen Rapid Tests mnamo Januari 2021. Katika vipimo hivyo kipindi cha msimu wa chini “low season” wasafiri walipimwa 300 hadi 400 na kupatikana wenye UVIKO 19 wasiozidi watatu kwa siku, na kipindi cha msimu wa juu “high season” wasafiri walipimwa 600 hadi 900 kwa siku na kwa sasa wanapima watu wanaopewa msamaha , washukiwa na wafanya kazi Serikalini n.k. Maabara ya Pathologia wanatumia mashine inayoitwa ABBOT kwa ajili ya kutest na kutoa majibu ya UVIKO 19 ndani ya masaa 7 na inauwezo wa kuchukua sampuli 94, kutokana na ilivotengenezwa inatumia “Control Reagent” 94 na sampuli kwa uwiyo huo huo. Hivyo basi hata kama kutakuwa na sample kidogo itawalazimu kutumia reagent hizo hizo 94 hivyo kusababisha hasara kwa kutumia “reagent” nyingi hali ya kuwa sampuli ni kidogo sana na kwa sasa wapimaji wamepungua sana hivyo wakati mwengine hupelekea kuchelewa kutoka majibu kwa sababu ya kusubiri idadi ya sampuli angalau ziwe nusu yake na wakati mwengine haifiki hata robo ya 94 na vile vile mashine inauwezo wa kupima vipimo vyengine kama HIV, kisukari n.k.

Mripuko wa janga la UVIKO 19 lililotokea duniani mwishoni mwa mwaka 2019 na kutufikia hapa nchini tarehe 18 Machi 2020 uliishitukiza Wizara ya Afya pamoja na taasisi zake kama vile Hospitali ya Mnazi mmoja pamoja na Maabara yake kwa namna tatizo lilivyokuwa kubwa na uhitaji wa rasilimali mbali mbali katika kukabiliana nalo.

Pamoja na mambo mengine hospitali ya Mnazi Mmoja na Maabara yake kuu ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya mitambo/mashine za kupima kwa haraka na uhakika, virusi vya UVIKO 19, vifaa tiba (reagents) ambavyo havitoshi kulingana na mahitaji yaliyokuwepo hapo awali kwani “reagent” zilihatajika kuazima Tanzania bara ili kukidhi mahitaji yao, uchakataji, uratibu, usimamizi na upatikanaji wa taarifa za UVIKO 19, upotevu wa mapato yaliyotokana na uchangiaji wa huduma za upimaji UVIKO 19, ucheleweshwaji wa majibu ya vipimo, rasilimali fedha na watu kuendana na ukubwa wa janga na miundombinu mengine ikiwa ni pamoja na TEHAMA katika kukabiliana ipasavyo na janga la UVIKO 19 kama ilivyokuwa kwa mataifa mengi ya nchi zinazoendelea.

Hata hivyo Serikali ilifanya jitihada mbali mbali katika harakati za kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo/mashine mbili za ABBOT kwa ajili ya kupima UVIKO 19 zenye

uwezo wa kupima sampuli 94 kwa awamu 4 kwa siku ambapo ni sawa na idadi ya sampuli 376 kwa masaa 24, kutengeneza mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusimamia na kuratibu taarifa za upimaji na uchanjaji wa UVIKO 19 ambao unakua miongoni mwa mifumo zaidi ya 10 iliyopo Wizarani.

Mfumo wa UVIKO 19 ulitengenezwa ili kukabiliana na changamoto kadhaa kwenye uchakataji, usimamizi, uratibu, na upatikanaji wa taarifa za UVIKO 19 pamoja na taarifa za mapato yatokanayo na kuchangia gharama za upimaji na uchanjaji wa UVIKO 19.

Aidha, utengenezaji wa mfumo wa UVIKO 19 ulisimamiwa kupitia mkataba ambao ulihusisha kuratibu na kusimamia taarifa za upimaji wa UVIKO 19 zinazojumuisha hali ya upimaji, majibu ya vipimo, vyeti vya majibu na hali ya malipo. Vile vile, mfumo huo uliongezewa moduli maalumu kwa ajili ya kuratibu na kusimamia taarifa za chanjo za UVIKO 19, upatikanaji wa vyeti vya chanjo na hali ya malipo licha ya kuwa moduli hiyo haina mkataba wowote baina ya Wizara na mtoa huduma.

Kwa upande wa huduma za upimaji wa UVIKO 19 zipo za makundi matatu, kundi la mwanzo ni kwa wasafiri wote isipokuwa waliosamehewa (exempted) kulipia gharama za vipimo vinavyo fanywa na maabara ya kujitegemea (private laboratory) ijulikanayo kama Zanz Medicals ambayo ilipewa zabuni ya kufanya kazi hii kwa gharama ya kila kipimo cha RT-PCR "Real-time Polymerized Chain Reaction" ni USD 80 ambapo mgawanyo kwa upande wa Serikali ni USD 50 na Zanz Medicals wanapata USD 30 na kwa kipimo cha "Antigen Rapid Tests" ni USD 25 na mgawanyo wake kwa upande wa Serikali ni USD 12.5 na Zanz Medicals USD 12.5 kwa kila kipimo.

Tangu tarehe 26 Septemba 2021 Zanz Medicals walitakiwa kuweka vituo takribani 5 vya upimaji ambavyo ni Maabara kuu ya upimaji iliyopo Mkoa wa Mjini, kituo kidogo cha upimaji Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini Unguja vile vile vituo vidogo vya upimaji eneo la bandari na maeneo mengine ya bandari zisizozisizo rasmini kama vile Mkokotoni na Kizimkazi na kwa upande wa Pemba sample zote zitafanyiwa uchunguzi katika maabara kuu ya unguja mjini. Vituo hivyo vipo kwa ajili ya ukusanyaji wa sampuli za wapimwaji na kuzileta kwenye maabara yao iliyopo Migombani.

Kundi la pili ni kwa wasafiri waliosamehewa hupimwa UVIKO 19 kwenye Maabara ya Serikali ya Mnazi mmoja ambapo sampuli zao zinachukuliwa kupitia vituo vya Lumumba na Mfikiwa. Taarifa zote za hali ya upimaji wa UVIKO 19 hususani kwa wasafiri zinasimamiwa na kuratibiwa kupitia mfumo wa UVIKO 19 bila kujali mtu amepimwa na Zan Medics au Maabara ya Serikali.

Kundi la tatu ni la washukiwa (Suspects) wa UVIKO 19, hawa ni watu ambao wanaonesha dalili mbali mbali za UVIKO 19 ambao wanachukuliwa kama wagonjwa wanao hitaji uangalizi wa kitabibu na hivyo basi hushughulikiwa kwa kufuata taratibu zilizopo za kumuhudumia mgonjwa ambapo sampuli zao huchukuliwa katika vituo mbali mbali vilivyowekwa na Serikali kwa Unguja na Pemba, na kupimwa kwenye Maabara ya Serikali ya Mnazi mmoja huku wakiendelea kuwa katika uangalizi wa kitabibu kwenye maeneo walikochukuliwa sampuli. Kundi hili halilipii gharama yoyote kama ambavyo Sera ya Afya za Zanzibar inavyoelekeza, japo kuwa taarifa za hali ya upimaji zinaingizwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa UVIKO 19.

Mfumo huu umerahisisha mchakato wa upimaji wa UVIKO 19 ambapo hivi sasa wapimwaji wanaweza kuweka nafasi "booking" kwa ajili ya kupima UVIKO 19 na kisha kupata majibu yao kupitia mfumo huu wa kielektroniki na kuendelea na safari zao ndani ya masaa 24.

Uchangiaji wa gharama za kufanya vipimo vya UVIKO 19 unafanyika kupitia njia mbali mbali ikiwemo kupitia mitandao ya simu (Tigo pesa), kwenye mtandao wa kibenki (visa/ master card) na kufanya malipo benki (bank deposits/ transfers) na kupelekea kupunguza changamoto nyingi zilizokuwepo kabla ya ujio wa mfumo huu ikiwa ni pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali.

Awamu ya pili ya utengenezaji wa mfumo ni ilihusisha kuengeza moduli kwa ajili ya kusimamia na kuratibu taarifa za chanjo za UVIKO 19 iliyokamilika na kuanza kutumika rasmin 17 Juni 2021, licha ya kuwa moduli hii haina mkataba wowote baina ya Wizara na mtoa huduma. Moduli hii inatumika kwa ajili ya kuweka nafasi "booking" ya kupata chanjo ya UVIKO 19 na vile vile kukuwezesha kulipia ili kupata kadi.

Uchangiaji wa gharama za kufanya vipimo vya UVIKO 19 unafanyika kupitia njia mbali mbali ikiwemo mitandao ya simu (tigo pesa), kwenye mtandao wa kibenki (CRDB Visa/ Master Card) na kufanya malipo benki (bank deposits/ transfers). Hali iliyosaidia kupunguza changamoto nyingi zilizokuwepo kabla ya ujio wa mfumo huu ikiwa ni pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa za mapato zilizomo kwenye mfumo wa UVIKO 19 kwa kipindi cha miezi 10 kuanzia mwezi Machi, 2021 hadi mwezi wa Disemba, 2021 mapato ghafi ya takribani shilingi 26,000,000,000 zilizokusanywa kutoka kwa wasafiri takribani 159,461 waliotoka kwenye mataifa takribani 190, wakati huo huo taarifa zinaonesha kwamba Wizara ya Afya ilisamehe wasafiri wanaofikia 438 watanzia wakiwa 359 na mataifa 18 ya nje wakifikia 79 kwa sababu mbali mbali jambo lililopelekea Serikali kukosa wastani wa shilingi 80,592,000 kwa kipindi hicho. Mchanganuo wa fedha za makusanyo kupitia taarifa za hesabu mbali mbali ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 35 : Mchanganuo wa Wastani wa Makusanyo kupitia taarifa za Hesabu mbali mbali

Mwaka	ORFM PBZ (Tshs)	ORFM PBZ USD (1:2,300)	AFYA PBZ (Tshs)	AFYA PBZ USD (1:2,300)	AFYA CRDB USD (1:2,300)	AFYA TIGO PESA (Tshs)
Machi – Disemba 2021	1,702,113,443	4,215,558.53	29,214,000	2,240	6,200,631	6,200,631
Jumla (Tshs)	1,702,113,443	9,695,784,619	29,214,000	5,152,000	14,261,451,300	6,200,631

8.1 MFUMO WA MALARIA EARLY DETECTION OF DISEASE

Mfumo wa Kugundua Ugonjwa wa Malaria Mapema (MEEDS) ulianza kutekelezwa na Zanzibar Malaria Control Program (ZMCP) mwaka 2008 kwa ajili ya ufuatiliaji wa Vituo vya Afya na kutoa taarifa kwa wakati ili Kufuatilia athari na juhudi za kudhibiti Malaria Zanzibar na kugundua ongezeko la ghafla la maambukizi ya Malaria na kuchukua hatua. Mfumo huu ni "Web based" na unatumia Kanzi data ya MYSQL. Wizara ya Afya inatumia mfumo huu kama huduma kutoka kwa Mmiliki

ambaye ni Kampuni ya Selcom Limited kwa udhamini wa RTI International kwa kushirikiana na Mpango wa Rais wa wa Malaria "President Malaria Initiative (PMI)".

Kila wiki taarifa za uchunguzi wa Malaria kutoka kwenye Vituo vya Afya zinatumiwa kuja ZMCP kwa njia ya simu janja zilizounganishwa na mfumo huu kwa ajili ya kufanya upembuzi na tathmini. Taarifa hizi huiwezesha ZMCP kufanya maamuzi sahihi kuhusu lini na mahala gani ambapo hufanyiwa uchunguzi zaidi kulingana na ongezeko la ghafla la maambukizaji.

Ufuatiliaji (Monitoring) wa MEEDS umekuwa ukifanywa kwa zaidi ya miaka mitano ambapo baada ya kipindi hicho tathmini ilifanyika katika harakati za kujiridhisha kama Malaria inafuatiliwa ipasavyo kwenye visiwa vya Unguja na Pemba.

8.2 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi anavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha Sheria Nambari 11 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapoomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

8.3 UPEO NA MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanyika Wizara ya Afya, Hospitali ya Mnazi Mmoja, kituo cha kupima UVIKO 19 cha Lumumba, Maabara ya Zanz Medicals, kituo cha kuchukua sampuli cha uwanja wa ndege, Ofisi za Programu ya Malaria pamoja na Ofisi ya Kampuni ya Rahisi maeneo yote yapo Unguja ambapo ukaguzi uliangazia michakato wa upatikanaji, usimamizi na matumizi ya mifumo ya UVIKO 19 pamoja na ule wa Malaria kwa kipindi kinachoishia mwezi Disemba, 2021.

Aidha, ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho la kuridhisha kwamba Wizara ya Afya ina ulinzi na udhibiti unaostahili kwenye miundombinu inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinazingatia usiri na uadilifu na kwamba vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi kupitia TEHAMA.

Malengo mengine ya ukaguzi huu wa mifumo ya TEHAMA ya Wizara ya Afya ni kama yalivyo ainishwa hapa chini:-

- a) Kubainisha ufuatishwaji wa Sheria, Kanuni, Sera, Miongozo na Taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa.
- b) Kufanya tathimini ya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.
- c) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.

- d) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- e) Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.
- f) Kubainisha kama Wizara ya Afya ina mipango stahiki katika usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA.

8.4 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya kitaifa na ya kimataifa kama vile eGaz, eGA, ISACA, COBIT, AFROSAI-E n.k.

Katika kukagua mifumo ya UVIKO 19 na Malaria ukaguzi ulitumia njia mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini.

- a) Kupitia Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo mbalimbali inayohusiana na usimamizi na uratibu wa Malaria na UVIKO 19 Zanzibar.
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kuipitia mifumo ya Malaria na UVIKO 19.
- c) Kupitia Sera na Miongozo ya usimamizi, wendeshaji matumizi ya TEHAMA inayotumiwa na Wizara ya Afya.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika upatikanafji wa mifumo husika.
- e) Kupitishwa kwenye mifumo ya Malaria na UVIKO 19 ili kuelewa utendaji kazi wake.
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti uliomo katika mifumo ya Malaria na UVIKO 19.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizomo ndani ya mfumo wa UVIKO 19 ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano na watumiaji wa Mfumo wa UVIKO 19.
- i) Kutembelea ofisi za eGaz kwa ajili ya kupatiwa uelewa wa namna mfumo unavyosimamiwa na kuendeshwa.
- j) Kutembelea ofisi za Rahisi kwa ajili ya kujiridhisha namna mfumo unavyo simamiwa na kufanya kazi.
- k) Kupitia "bank statements" za akaunti za benki za PBZ zinazohusika na kupokea miamala ya UVIKO 19.
- l) Kupitia "statements" ya tigo pesa na "bank statements" za CRDB zinazopokea miamala ya UVIKO 19.
- m) Kufanya kikao cha kuanza kazi ya ukagu na kumaliza pamoja na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi.

8.5 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KWENYE MFUMO WA UVIKO 19.

8.5.1 Kwa upande wa Wizara ya Afya:

Kitengo cha TEHAMA cha Wizara kutokushiriki kikamilifu kwenye utengenezaji na kutekeleza mfumo wa UVIKO 19, Kutokuwepo kwa muongozo wa namna ya kuwahudumia wasafiri waliopimwa Rapid PCR Molecular test Uwanja wa Ndege na kubainika kuwa na maambukizi, Kutofanyiwa usuluhishi wa kibenki hesabu zote za benki zinazopokea miamala ya UVIKO 19, Kutopatikana kwa nakala za stakabadhi za benki za malipo ya upimaji wa UVIKO 19, Kutokuwepo kwa Mkataba kati ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Rahisi kwa ajili ya utengenezaji wa Moduli ya Chanjo, Kutokuwepo kwa Mkataba rasmi baina ya Wizara ya Afya na Hospitali ya Alrahmah katika kutoa Huduma za UVIKO 19, Kutokuwepo kwa Mkataba rasmi baina ya Wizara ya Afya na Tasakhta Global Hospital katika kuchukua sampuli za wapimwaji, Uwepo wa Vyeti vya UVIKO 19 vya kugushi (Fake Certificates), Wizara kushindwa kusimamia mfumo wa UVIKO 19, Kutokuzingatiwa kwa ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19, Ucheleweshwaji wa malipo kwa kampuni ya Rahisi kinyume na makubaliano, Kutokuunganishwa kwa 'Mobile App' ya KoBoCollect na Mfumo wa UVIKO 19, Uhaba wa matenki ya kuhifadhia maji safi na salama kwenye kituo cha kuchukulia sampuli cha Lumumba, Maabara ya Mnazi Mmoja kutokuzingatia udhibiti wa ufikiaji (access control) kwenye komputa zinazotumika kuingiza taarifa za UVIKO 19 kwenye mfumo, Kutokuwepo kwa mfumo wa 'Barcode' kwenye "Viral Transport Media (VTM)", Upungufu wa vitendea kazi (computers) kwa watumiaji wa mfumo (data entrys), Vituo vya Afya kutokuwa na ufikiaji wa mfumo (system access) kwa ajili ya kuingiza taarifa za washukiwa, Ucheleweshwaji wa vyeti vya chanjo ya UVIKO 19,

Vile vile, Kutokuunganishwa kwa mfumo wa UVIKO -19 na kanzi data za NIDA na benki ya PBZ, Udhaifu wa udhibiti wa kuingiza taarifa za malipo ya vipimo vya UVIKO 19 kwenye mfumo, Kutorejeshewa fedha kwa wakati kwa miamala iliyofanyika zaidi ya mara moja kupitia mtandao wa kibenki wa Visa/Master card wa benki ya CRDB, Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan), Kukosekana kwa ushahidi wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19, Mfumo kutotambua uhalali wa stakabadhi za benki za malipo ya UVIKO 19, Udhaifu wa udhibiti wa uingizaji wa Malipo ya Vyeti vya Chanjo ya UVIKO 19, Udhaifu wa udhibiti wa msamaha wa upimaji UVIKO 19, Kusuasua kwa uunganishaji wa Mfumo wa UVIKO 19 na Mfumo wa Vitambulisho vya Mzanzibari (Zan ID System),

8.5.2 Kwa upande wa kampuni ya Zanz Medicals

Kutokuendelea na upimaji kwa wasafiri waliopimwa mwanzo na kubainika kuwa na maambukizi ya UVIKO 19, Udhaifu wa udhibiti wa ufikiaji (access control) kwenye kompyuta zinazotumiwa kuchakata taarifa na kufanya vipimo vya UVIKO 19 Maabara, Udhaifu wa udhibiti wa chumba cha Maabara Zanz Medicals, Kutokufuatwa miongozo ya Wizara ya Afya (SOP) katika utekelezaji wa kazi za upimaji UVIKO 19, Kutokuwekwa vituo vya kupima UVIKO 19 kwenye Bandari za Mkokotoni na Kizimkazi, Ucheleweshwaji wa vyeti vya uthibitisho wa malipo ya kodi ya zuio, Uwepo wa

udanganyifu kwenye malipo ya upimaji wa UVIKO 19, Kubadilisha kwa wataalamu (Key experts) waliothibitishwa kwenye mkataba kwa mujibu wa taaluma zao bila ya idhini ya Wizara ya Afya kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba, Kutokuwepo kwa Udhhibiti mzuri katika kituo cha Migombani kwa watu wanaoingia kwenye kituo cha kupima UVIKO 19.

8.5.3 Kwa upande wa kampuni ya Rahisi Solution

Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada maafa (Disaster Recovery Site/ Offsite), Kukosekana kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan), Kukosekana kwa nyaraka muhimu za mfumo wa UVIKO 19, Udhaifu wa udhibiti katika kuusimamia mfumo wa UVIKO 19, Mapungufu ya mfumo wa UVIKO 19 kwenye kuingiza taarifa za washukiwa wa UVIKO 19, Kukatiwa huduma ya mtandao (internet) kwa vituo vinavyoingiza taarifa kwenye mfumo wa UVIKO 19, Udhaifu wa Mfumo katika kuoanisha huduma za upimaji wa UVIKO 19 na malipo yanayotakiwa kwa kila huduma, Mfumo kutoruhusu usajili binafsi kwa waliosamehewa, Kutokutumika kwa 'Portal' ya usajili binafsi kwa ajili ya Chanjo za UVIKO 19, Udhaifu wa mfumo katika kuingiza tarehe za kufanya chanjo ya Pili (Second dose).

8.6 MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KWENYE UKAGUZI WA MFUMO WA MALARIA.

Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site/Offsite), Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan), Kukosekana kwa mpango wa uhamishaji wa taarifa (Data Migration Plan).

8.7 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA UVIKO 19

Ukaguzi wa mfumo wa TEHAMA unaosimamia taarifa za UVIKO 19 uliofanyika kwenye Wizara ya Afya wajibu, haki na majukumu ya Wizara ya Afya katika usimamizi, uratibu na kutoa huduma za Afya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria kwa kuhusisha TEHAMA viliangaziwa, Miongozo, Sera na Kanuni mbalimbali hususani kwenye eneo la UVIKO 19.

8.7.1 Dosari zilizobainika kwa upande wa Wizara ya Afya

Kwa upande wa Wizara ya Afya ukaguzi ulibaini dosari kama zifuatazo:-

8.7.1.1 Kitengo cha TEHAMA cha Wizara kutokushiriki kikamilifu kwenye utengenezaji na utekelezaji mfumo wa UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini kwamba mchakato wa utengenezaji wa mfumo wa UVIKO 19 ikiwa ni pamoja na Moduli ya Chanjo haukuwashirikisha kitengo cha TEHAMA ipasavyo katika hatua mbalimbali za utengenezaji wa mfumo huo.

Hali hii ilijidhihirisha wakati ukaguzi ulipokuwa unaendelea ambapo ilibainika kupitia majadiriano na wakaguliwa kwamba kwa nyakati tofauti ushauri na mapendekezo ya kitengo cha TEHAMA kwenye hatua za awali za kuutengeneza mfumo huu hayakuwa yakizingatiwa na Menejimenti ya Wizara ya Afya. Ukaguzi ulibaini kwamba kitengo cha TEHAMA cha Wizara ya Afya hakikuwa na ufikiaji wa mfumo huu (access) mpaka wakati wa kukamilika kwa ukaguzi hali inayoashiria kwamba kitengo cha TEHAMA hakikuwa na uelewa wa namna mfumo huu unavyofanya kazi pamoja na changamoto za mfumo wote kwa ujumla wake tangu mwezi Machi 2021 ulipoanza kutumika.

Aidha, ukaguzi uliabaini kwamba kitengo cha TEHAMA hakikupewa mafunzo ya namna mfumo unavyofanya kazi na namna ya kuusimamia na kuuendeleza kinyume na matakwa ya mkataba baina na Wizara ya Afya na Rahisi Solution Company kwa mujibu wa kifungu 7.0 (ix na x) pamoja na kifungu 18.0 ambacho kinachomtaka Mtoa huduma kutoa mafunzo kwa watumiaji mbalimbali wa mfumo.

Kimsingi, kitengo cha TEHAMA ndicho kina jukumu la kuusimamia mfumo huu sawa na mifumo mengine iliyopo Wizarani hivyo, kukosa ufahamu wa kutosha wa vitu vya msingi vya mfumo ambavyo ni pamoja na nyaraka muhimu za mfumo kama vile nyaraka ya mahitaji (user requirements document), nyaraka za usanifu na usanidi, "source codes", na teknolojia iliyotumika kwenye mfumo kunaiweka Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla wake kuwa kwenye hatari kubwa ya utegemezi wa Mtoa huduma kwa muda usiojulikana na kuongeza gharama za kuusimamia na kuuendesha mfumo huu katika namna endelevu ili kupatikana tija na ufanisi uliotarajiwa.

Kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba baina ya pande mbili sehemu 4.0 kwamba Wizara ya Afya itaumiliki mfumo kwa 100% kutoka tarehe ya mfumo kuanza kufanya kazi ilitarajiwa kuwepo na mpango mkakati wa Wizara unaoainisha namna ambavyo Wizara itaweza kulichukua jukumu hilo na kuisaidia Serikali katika kuokoa fedha ambazo vinginevyo zitatumika kumlipa mtoa huduma ili aendelee kuusimamia mfumo kwa muda mrefu zaidi badala ya kupeleka fedha hizo kwenye kutatua changamoto za Wananchi na kuleta maendeleo katika jamii. .

Kwa ujumla, hali hii inaweza kuleta athari za kiuchumi na kijamii kama zilivyoainishwa hapa chini;

- Kuongeza gharama Serikalini kwa kumtegemea mtoa huduma kwenye kuusimamia na kuuendeleza mfumo na kutoa msaada wa kiufundi kwa muda usiojulikana.
- Kudhoofisha jitihada za kujenga uwezo na kuibua vipaji vya wataalamu wa ndani kwa kutowapa nafasi na kutowahamasisha kufanya kazi zilizo ndani ya uwezo wao.
- Kushusha hamasa kwa watumishi wa Serikali kwenye eneo la TEHAMA hususani wale wenye vigezo vyote vya kufanya kazi na
- Kukatisha tamaa wanafunzi walioko vyuoni kusomea fani za TEHAMA.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo kuzingatiwa:-

- Menejimenti ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution Company kuandaa mpando wa mafunzo na kuutekeleza ambao utahakikisha kua kitengo cha TEHAMA cha Wizara kinajengewa uwezo wa kuusimamia mfumo huu kikamilifu kabla ya kuhitimishwa kwa mkataba baina ya pande mbili.
- Kwa kua mfumo huu unatakiwa ufanye kazi masaa 24 siku 7 za wiki, ni vyema Wizara ya Afya ikajipanga kwa kuandaa watumishi wa kitengo cha TEHAMA wa kutosha watakapo fanya kazi kwa "shift" mbili au tatu ndani ya masaa 24/7 ili kutoathiri ratiba na safari za wasafiri ambazo hupangwa muda wowote ndani ya siku.
- Kwa kuzingatia mazingira haya ya kazi kwenye kuhudumia wageni katika upimaji, uchanjaji

na matibabu ya UVIKO 19 kwa kutumia mfumo huu kuna haja kwa Wizara kuangalia namna ya kutoa hamasa (motivation) kwa watumishi wanaohusika na shughuli za UVIKO 19 kwa lengo la kuweza kufanya kazi kwa muda wa saa 24 bila ya vikwazo vyovyote na kupelekea upatikanaji wa huduma bora tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi hizo hufanywa na kampuni ya Rahisi Solution Company.

- Wizara izingatie mapendekezo na ushauri wa wataalamu wake wa TEHAMA kwenye masuala ya mifumo hususani ushauri unaolenga kulinda maslahi mapana ya Serikali na nchi kwa ujumla.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA ifuatilie kwa karibu nyaraka zote zinazohusu usanifu, ujaribu, usanidi, mpangilio, utekelezaji, uhifadhi, utumiaji, uunganishwaji, mafunzo n.k ya mfumo huu kabla ya kumalizika kwa mkataba uliopo baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi Solution Company.
- Kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba na muda wa kumalizika kwa Mkataba huo jitihada za makusudi zichukuliwe na Wizara ya Afya kuhakikisha watendaji wa kitengo cha TEHAMA wanajengewa uwezo na kufahamishwa namna bora ya usimamizi na uendeshaji wa mfumo na kampuni ya Rahisi Solution Company kwa lengo la kuhakikisha tija iliyokusudiwa inaendelea kupatikana baada ya kumalizika kwa Mkataba huo.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA kuupitia vyema mfumo na mkataba kuhakikisha kwamba unafanya kazi kama ilivyotarajiwa kabla ya kuupokea na kuanza kuusimamia pindi mkataba utakapoisha baina ya Wizara na kampuni ya Rahisi.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA kua mstari wa mbele katika hatua zote tangu mwanzo na kupewa nafasi ya kusikilizwa kwenye masuala yote yanayohusu mifumo ya Wizara ikiwa ni pamoja na huu wa UVIKO 19.

8.7.1.2 Kutokuwepo kwa muongozo wa namna ya kuwahudumia wasafiri waliopimwa Rapid PCR Molecular Test Uwanja wa Ndege na kubainika kuwa na maambukizi

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haijaweka mwongozo wala mazingira rafiki ya namna ya kuwahudumia wasafiri wanopimwa Rapid PCR Molecular uwanja wa ndege na kubainika kuwa na maambukizi ya UVIKO 19 (Positive).

Ukaguzi umebaini wasafiri wanaopimwa Rapid PCR uwanja wa ndege na kusubiria majibu wanakaa pamoja, na hata baada ya kupokea majibu waliokutwa na maambuzi na wasiokuwa na maambukizi huendelea kukaa pamoja bila ya kujali hatari iliyopo ya kuendelea kuambukizana maradhi.

Uwepo wa hali hiyo inaweza kuwa chanzo cha kusambaa kwa maambukizi miongoni mwa wasafiri hususani kwa wale waliopimwa mwanzo na kubainika kuwa hawana maambukizi (negative) jambo ambalo linasababisha wanaposafiri kwenda nje ya nchi na kukutwa na maambukizi wakati vyeti vya vipimo vyao wakiwa Zanzibar vinaonesha walikuwa "negative" na kusababisha kutiliwa shaka vipimo na ubora wa Maabara za Zanzibar.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kutengeneza mwongozo na kuhakikisha unatekelezwa utakaohakikisha kwamba wasafiri wote waopimwa UVIKO 19 uwanja wa ndege wanakaa kwa hali ya tahadhari na kwa wale wanaobainika kuwa na maambukizi (positive) wanatengewa eneo lao maalum, sehemu inayoruhusu hewa ya kutosha mbali na watu wengine walio "negative" ili kupunguza hatari ya kusambaa kwa maambukizi ndani ya uwanja wa ndege.

8.7.1.3 Kutofanyiwa usuluhishi wa kibenki hesabu zote za benki zinazopokea miamala ya UVIKO 19.

Wizara ya Afya ikiwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kuongoza katika utoaji wa huduma za afya nchini, kudhibiti mripuko wa UVIKO 19 ni moja ya majukumu yake kisheria, hii inajumuisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na UVIKO 19 kulingana na Sera za nchi. Ukaguzi umebaini uwepo wa Hesabu za Benki zisizopungua 4 zinazotumika kupokea fedha za vipimo na chanjo za UVIKO 19 ambapo hesabu 2 zinazotumika moja ni ya TZS na ya pili ya USD ziko chini ya Wizara ya Afya wakati hesabu 2 zilizosalia TZS na USD zikiwa chini ya Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango. Kwa nyakati tofauti hesabu hizi zote hupokea fedha za vipimo na zile za vyeti vya chanjo za UVIKO 19 kutoka kwa wananchi na wageni mbalimbali wanaohitaji huduma za UVIKO 19.

Aidha, katika hali isiyokuwa ya kawaida ukaguzi umebaini kwamba hesabu zote hizi hazikuwahi kufanyiwa usuluhishi wa kibenki tangu zilipoanza kupokea fedha za UVIKO 19 kinyume na kifungu nambari 105 (1) cha kanuni ya usimamizi wa fedha ya mwaka 2021.

Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupatiwa taarifa za kumbukumbu za Vitabu vya Fedha Taslimu (Cash Books) kwa ajili ya mapato hayo ya UVIKO 19 kwenye hesabu zote 4. Haya yote yalibainika kupitia vikao vilivyoitishwa na ukaguzi kujadili sababu na changamoto zilizowasilishwa kwa wakaguzi na Wizara ya Afya kwa upande mmoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa upande mwingine.

Aidha, ukaguzi umebaini Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa hesabu za benki za UVIKO 19 na kupelekea kila Taasisi kuona haina jukumu la msingi la kufanya usuluhisho wa kibenki na kupelekea Kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato yanayokusanywa kupitia mfumo huo kwa pande zote mbili (Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha).

Kwa vile Mapato ya UVIKO 19 yako chini ya Wizara ya Afya na yanatakiwa kuwa kwenye bajeti yake ya mapato ya kipindi husika lakini kwa sababu ambazo ukaguzi haukuzielewa mapato hayo yaliambiwa kukusanywa kupitia hesabu za benki za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (ORFM) ukiachilia mbali ukweli kwamba ORFM haikuwa na bajeti ya mapato hayo na wala sio chanzo chake cha mapato, hata hivyo ilitarajiwa Wizara ya Afya kuwa ndio msimamizi mkuu wa mapato yote yatokanayo na uchangiaji wa huduma za vipimo vya UVIKO 19 na baadae kuyahaulisha mapato hayo kuingia katika hesabu za UVIKO 19 zilizopo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu zote zinazohusiana na upokeaji wa mapato hayo jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa usuluhishi wa kibenki uliofanyika.

Kwa upande wa Wizara ya Afya hakukuwa na sababu za msingi zilizopelekea kushindwa kutekeleza jukumu lake la kufanya usuluhishi wa kibenki kwa kipindi chote ambacho fedha za UVIKO 19 zilikuwa zinaingia kwenye Hesabu zake za Benki kabla ya kuhamishiwa Ofisi ya Rais Fedha na

Mipango, hata hivyo jukumu hili halikutekelezwa kwa mujibu wa miongozo na kanuni za fedha za mwaka 2021.

Athari za kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki zinajumuisha zifuatazo: -

- Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutofahamu kwa uhakika mapato halisi yanayotokana na UVIKO 19 zaidi ya kutumia taarifa za "Bank Statement" pekee ambazo zinaweza kuwa na mapungufu makubwa.
- Serikali kupata hasara ikiwa kuna fedha ambazo hazikuingizwa kwenye hesabu za benki kwa sababu yoyote ile kama vile muamala kutokukamilika kwa sababu ya matatizo ya mtandao au sababu za kiufundi, kughushi stakabadhi za malipo, makato ya kibenki yasiyotambulika, n.k vitu ambavyo hubainika kupitia usuluhishi wa kibenki pekee.
- Kutumika kama mwanya wa kufanya ubadhirifu, wizi au matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa sababu ya udhaifu uliopo kwenye usimamizi wa mapato husika.
- Kwa kutokuwa na Cash Books za Mapato ya UVIKO 19 Serikali inakosa rejea (reference) ya kufanyia ulinganifu wa mapato yaliyokusanywa benki na kupelekea ugumu katika kazi za ukaguzi na kuinyima Serikali fursa ya kushauriwa ili kuboresha kazi zake.

Kwa kuzingatia athari na hatari zilizopo kupitia udhaifu huu uliobainika ukaguzi unashauri mambo yafuatayo: -

- Kwa kuwa bajeti ya mapato ya UVIKO 19 iko Wizara ya Afya na kwamba makusanyo yake yanatakiwa kuonekana sambamba na bajeti hii ni vyema mapato yote yatokanayo ya ulipiaji/ uchangiaji wa gharama za vipimo na chanjo za UVIKO 19 yakasimamiwa na Wizara ya Afya kwa 100% ikiwa in pamoja na hesabu za benki zinazotumika kupokea mapato husika ziwekwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya.
- Hesabu 2 za UVIKO 19 ambazo kwa sasa ziko chini ya ORFM ni vyema zikawekwa chini ya usimamizi na uangalizi wa Wizara ya Afya ili kurahisisha uendeshaji wa uwajibikaji kwenye hesabu hizi ikiwa ni pamoja na kuzifanyia usuluhishi wa kibenki.
- ORFM iendeleo kubakia na jukumu la kusimamia rasilimali fedha za Serikali kwa ujumla wake kupitia njia mbalimbali kama vile kuomba ripoti za mara kwa mara za mapato, usuluhishi wa kibenki na utekelezaji kutoka Wizara ya Afya kwenye hesabu zote zilizopo chini ya Wizara ya Afya ili kuondoa mkanganyiko wa Wizara gani inafanya nini kwenye hesabu hizi.
- Wizara ya Afya na ORFM kila mmoja atengeneze "Cash Books" na kuingiza kumbukumbu zote za mapato halisi yaliyoingia kwenye hesabu husika za Wizara husika kulingana huduma za vipimo na chanjo za UVIKO 19 zilizotolewa na Serikali kupitia Zanz Medicals kwenye upimaji na Rahisi kwenye taarifa za chanjo za UVIKO 19 kuanzia mwezi Julai, 2021 mpaka sasa. Izingatiwe kwamba, "Cash Books" zinatakiwa kuandaliwa kutokana na stakabadhi za malipo ya huduma na sio kwa kutumia "Bank Statements", hivyo basi Wizara zinatakiwa zifanye mawasiliano na Benki ya PBZ ili kupata nakala zote za stakabadhi za malipo ya huduma za upimaji na chanjo za UVIKO 19 kwa kuwa Wizara ya Afya haina kumbukumbu kamili za

stakabadhi hizo, kwa upande mwingine ziwasiliane na Kampuni ya Rahisi ili kupata taarifa za malipo ya huduma yaliyofanywa kwa kutumia Tigo Pesa na Visa/ Master Card ili kupata miamala yote iliyolipiwa kwa kipindi husika na kuiingiza kwenye Cash Book husika pia kabla ya kuanza usuluhishi wa Kibenki.

- Wizara ORFM ifanye usuluhishi wa kibenki kwenye hesabu zake za benki ili kubaini uhalisia wa mapato ya Serikali kwa kipindi cha Julai, 2021 mpaka sasa na kuendelea kwa mujibu ya Miongozo iliyopo.
- Wizara ya Afya ifanye usuluhishi wa kibenki kwenye sehabu zake za benki kuanzia kuanzia mwezi wa Januari mpaka sasa na kuendelea kwa mujibu ya Miongozo iliyopo.
- Kwa kuwa mfumo wa UVIKO 19 unatumika pia kutunza kumbukumbu za mapato kwa kadri wateja wanavyolipia huduma, na kwa kuwa taarifa hizi huingizwa kwenye mfumo huu kwa kila muamala mmoja kwa mtu mmoja na huduma moja, lakini kwa kuwa fedha zinazohaulishwa kutoka Tigo Pesa na CRDB Bank kuingia kwenye Hesabu za Serikali zinaingizwa kwa mafungu (lumpsum) ya makusanyo ya kipindi fulani kama vile wiki nzima jambo ambalo linasababisha ugumu kwenye kufanya usuluhishi kwa kulinganisha taarifa za mapato zilizomo kwenye mfumo wa UVIKO 19 na zile zilizomo kwenye "Benki Statemnets" ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya uhaulishwaji wa fedha kutoka Tigo Pesa na CRDB Benki kwenda kwenye Hesabu za Benki za Serikali kwa kuzingatia mualamala mmoja mmoja kama ulivyopokelewa ili kuondoa tatizo hili linaloongeza ugumu kwenye usuluhishi wa kibenki.

8.7.1.4 Kutopatikana kwa nakala za stakabadhi za benki za malipo ya upimaji wa UVIKO 19

Ukaguzi umebaini udhaifu mkubwa wa utunzaji wa kumbukumbu za stakabadhi za benki za malipo ndani ya Wizara ya Afya kiasi cha kutopatikana kwa stakabadhi zote za malipo ya huduma za UVIKO 19 kuanzia Januari, 2021 mpaka Disemba 2021 kwa ajili ya ukaguzi. Hizi ni stakabadhi zinazoletwa na wateja kama ushahidi wa kuwa wamelipia huduma ili kupatiwa huduma husika, Wizara inatarajiwa kutunza nyaraka hizi kwenye mazingira safi na salama kwa kwa kipindi kisichozidi miaka 30 kwa mujibu wa sheria nambari 3 ya mwaka 2008.

Kukosekana kwa nyaraka hizo muhimu katika usimamizi wa fedha za umma kunaweza kuashiria uwepo wa rushwa, uvujifu wa mapato na matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya tathmini ili kubaini chanzo halisi na ukubwa wa tatizo kulingana na udhaifu huu uliobainika katika utunzaji wa kumbukumbu hizo muhimu na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria. Pia, Wizara inashauriwa kuweka mikakati mahususi katika kuhakikisha kwamba udhaifu huu unadhibitiwa na kwamba haujirudii tena.

8.7.1.5 Kutokuwepo kwa mkataba kati ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Rahisi Solution Company kwa ajili ya utengenezaji wa Moduli ya Chanjo.

Katika kuupitia mchakato wa utengenezaji wa nyogeza ya mfumo wa UVIKO 19 kwa ajili ya chanjo (Vaccination Module) ilibainika kuwa hakuna makubaliano rasmi baina ya Wizara ya Afya na mtoa huduma (M/S RAHISI SOLUTION COMPANY) katika utengenezaji na utumiaji wa moduli ya chanjo

ya UVIKO 19. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Kukosekana kwa makubaliano ya Mkataba kunaweza kukapelekea kutokuwekwa wazi kwa haki na wajibu wa kila upande, kutojua gharama zote za moduli hiyo zinazojumuisha utengenezaji na utekelezaji wake, kutofahamika utaratibu wa kufuatwa katika upatikanaji wa msaada wa kiufundi (technical support) hususani wakati ambapo moduli hiyo itakapokabidhiwa Serikalini, wataalamu wa TEHAMA wa Wizara ya Afya na watumiaji wengine kutokupewa mafunzo toshelevu na endelevu ya namna ya kuitumia na kuisimamia moduli hii kiufanisi ni sehemu ya athari za kukosekana kwa mkataba.

Kwa kuzingatia mapungufu hayo yaliyobainika ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya ikishirikiana na mtoa huduma kuweka makubaliano ya maandishi kwa mujibu wa sheria na taratibu za manunuzi na kuhakikisha kwamba kuna uzingatiaji wa masilahi mapana ya Serikali kwenye matumizi endelevu ya Moduli ya chanjo ili kuleta tija, ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati na zinazokidhi mahitaji ya Wazara na wadau wengine muhimu kwenye sekta ya Afya.

8.7.1.6 Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Wizara ya Afya na Hospitali ya Alrahmah katika kutoa Huduma za UVIKO 19

Ukaguzi umebaini kuwa hakuna makubaliano yoyote yalipo kati ya Wizara ya Afya na Hospitali ya Alrahmah katika utoaji wa huduma za UVIKO 19. Hali hii inapelekea kutofahamika kwa mipaka, wajibu na haki za Alrahmah dhidi ya Serikali kwa kuzingatia uwepo wa Zanz Medicals ambaye ameingia mkataba na Serikali na mipaka yake kufahamika ikiwa ni pamoja na wajibu na haki zake.

Kutokuwepo kwa makubaliano rasmi baina ya Serikali ya Hospitali ya Alrahmah kunaweza kupelekea Serikali kupoteza mapato yanayotokana na upimaji wa UVIKO 19 tofauti na Maabara binafsi nyengine zinazofanya kazi kama hiyo ambazo zinafahamika gharama na mgawanyo wa mapato ya Serikali pamoja na kupelekea wananchi kutozwa fedha nyingi ili kupata huduma hii kupitia Alrahmah kwani Wizara haifahamu hata gharama zinazotozwa.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka utaratibu mzuri katika kuratibu na kusimamia jambo hili ili lifanyike kwa kuzingatia maslahi mapana ya Serikali.

8.7.1.7 Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Wizara ya Afya na ya Tasakhta Global Hospital katika kuchukua sampuli za wapimwaji

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya haina makubaliano na Tasakhta Global Hospital katika ufanyaji kazi za UVIKO 19 hali inayopelekea Serikali kushindwa kufahamu mazingira ya kazi, miongozo anayotumia, mipaka na wajibu wa Hospitali ya Tasakhta Global Hospital katika utowaji wa huduma za UVIKO 19 nchini. Udhaifu huu unaweza kusababisha Serikali kupoteza mapato kwa kushindwa kuelewa kiasi cha fedha inachotoza Hospitali ya Global kwa watu wanaokwenda kupata huduma mbalimbali za UVIKO 19, pia taarifa sahihi za UVIKO 19 ambazo zinahitajika kwa Serikali kwa lengo la kuweka mikakati na mipango madhubuti zinaweza kupotea kutokana na kutoeleweka Hospitali ya Global inavyokusanya na kutunza taarifa za UVIKO 19 kutoka kwenye jamii.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuchukuwa hatua za haraka za kuweka makubaliano (mkataba) kwa mujibu wa Sheria za nchi na Hospital ya Global katika kujihusisha na utoaji wa huduma za UVIKO 19 na kwamba katika makubaliano hayo Wizara ihakikishe maslahi mapana ya Serikali yanazingatiwa muda wote.

8.7.1.8 Uwepo wa Vyeti vya UVIKO 19 vya kughushi (Fake Certificates)

Ukaguzi umebaini kuwa kuna vyeti vya kughushi ambavyo baadhi ya wananchi huvitumia ili kusafiri ikiwa ni kinyume na utaratibu. Vyeti hivi vimepatikana katika maeneo ya uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume kwa baadhi ya wasafiri wanapokwenda kwa ajili ya safari zao, hali hii imeanza kuwekwa bayana mara baada ya kuanza kutumia "Barcode/ QR Codes" kwenye vyeti vya UVIKO 19 kuanzia mwishoni mwa mwaka 2021, vyeti hivi vinavyotengenezwa kwenye mfumo wa UVIKO 19 ambapo wakati wa kusafiri vyeti vyote humulikwa (scanning) ili kuhakiki taarifa zake na ndipo baadhi hukutwa kwamba taarifa zinazosomeka kwenye cheti hazifanani na taarifa zinazoonekana kwenye "Bar Code/ QR Codes". **Kiambatisho Nambari 21 Kinahusika.**

Jadweli lifuatalo linaonesha takribani vyeti 12 vyenye thamani isiyopungua shilingi **2,208,000** ndani ya muda wa chini ya mwezi mmoja, hali hii inatoa picha ya ukubwa wa tatizo ambalo linahitaji ufuatiliaji wa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na wadau wengine.

Jadweli Nambari 36 : Baadhi ya taarifa za vyeti vya kughushi vilivyobainika na ukaguzi

Nam.	Jina	Uraia	Nambari ya Cheti	Namba ya Kitambulisho cha Maabara	Tarehe ya Kupima	Tarehe ya Kupata Cheti	Kiwango cha fedha Kilichopotea (Tzs)
1.	Abigall Isabella Craven	Afrika Kusini	ZCC20211231160275	12300836	30 Disemba 2021	31 Disemba 2021	184,000
2.	Akintomiwale Boluwatife Awodumila	Nigeria	ZCC202201059449	0401MGG0789	4 Januari 2022	5 Januari 2022	184,000
3.	Matt Feiertag	Afrika Kusini	ZCC20220111232424	1001MGG0600	11 Januari 2022	11 Januari 2022	184,000
4.	Seiran Seropian	Urusi	ZCC2022011222425	0601MGG0070	11 Januari 2022	12 Januari 2022	184,000
5.	James Feiertag	Afrika Kusini	ZCC20220111232425	1001MGG0601	11 Januari 2022	11 Januari 2022	184,000
6.	Jenna Nicole Feiertag	Afrika Kusini	ZCC2022111232423	1001MGG0599	11 Januari 2022	11 Januari 2022	184,000
7.	Ekaterina Linnik	Urusi	ZCC20220112224260	0601MGG0070	11 Januari 2022	12 Januari 2022	184,000
8.	Kastytis Naslenas	Lithuania	ZCC202201116533	ZM/F-4973	11 Januari 2022	12 Januari 2022	184,000
9.	Breedt Herman Van derberg	Afrika Kusini	ZCC202126126814	11100223	12 Januari 2022	12 Januari 2022	184,000
10.	Katarzyna Paulina Karczewska	Poland	ZCC202201021243	Nil	15 Januari 2022	15 Januari 2022	184,000
11.	Kacper Maksymilian Warchol	Poland	ZCC202201021243	Nil	15 Januari 2022	15 Januari 2022	184,000

12.	M.Sosnin Alexander	Nil	Nil	Nil	Nil	Nil	184,000
JUMLA YA FEDHA AMBAZO HAZIKUKUSANYWA							2, 208,000

Kuwepo kwa vyeti vya kughushi kunaharibu sifa za nchi katika udhibiti wa upimaji na usimamizi wa UVIKO 19 katika uwanja wa kimataifa na kupelekea kufifisha jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na janga la UVIKO 19 Zanzibar. Pia inashiria udhaifu kwenye vyombo mbalimbali vya Serikali vyenye jukumu la kuzuia hali hii. Serikali kukosa mapato kwa kuwa uwepo wa vyeti feki unamaanisha kwamba wasafiri hawa hawakufuata njia rasmi za kupima UVIKO 19 ambazo zingehakikisha kwamba wamelipia kihalali Serikalini na kupatiwa vyeti halisi. Kwa ujumla hali hii inaweza kusababisha madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii katika ngazi ya Taifa.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya uchunguzi ili kuwabaini wote wanaohusika na utengezaji wa vyeti feki na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

8.7.1.9 Wizara kushindwa kusimamia mfumo wa UVIKO 19

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Rahisi kifungu 4.0 kinachoelezea kuwa "mfumo ni mali ya Wizara kuanzia tarehe mfumo unapoanza kazi", lakini hadi sasa Wizara imeshindwa kuwa msimamizi mkuu wa mfumo katika matumizi yake na usimamizi wa ujumla ikiwa ni pamoja na kufanya maboresho na kutatua changamoto za mfumo huo kwa kadri unavyotumika na badala yake kazi hizi zinafanywa na kampuni ya Rahisi ambayo ni mtoa huduma.

Athari zinazoweza kutokea kufuatia Wizara ya Afya kushindwa kuusimamia mfumo wa wa UVIKO 19 ipasavyo kama zifuatazo: -

- Mabadiliko yoyote ya mfumo lazima aambiwe mtoa huduma kwa sababu maarifa yote ya mfumo anayo yeye pekee na kusababisha Serikali kumtegemea yeye kwa 100% kufanya mabadiliko yanayoweza kuhitajika muda wowote.
- Ukosefu wa nyaraka muhimu za usimamizi wa mfumo kwa kuwa Wizara haikushirikishwa kikamilifu katika kila hatua ya utengenezaji wa mfumo huu. nyaraka ya madhumuni na faida za mradi (business case), nyaraka ya mahitaji ya mfumo, nyaraka ya vipengele vya mfumo vinavyotakiwa kujaribiwa (test cases), na ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo.
- Kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mfumo hususani baada ya kumalizika kwa mkataba baina ya Wizara na kampuni ya Rahisi kwa sababu Wizara bado inaona haina jukumu la kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwa miaka mingi ijayo kwa kuwa haijaumiliki na kuusimamia.
- Udhaifu katika utoaji wa rufusa za kuufikia mfumo na usimamizi wa watumiaji wa mfumo.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na mtoa huduma kuandaa mpango wa kuchukuwa umiliki na usimamizi wa mfumo mzima kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba ili kuhakikisha kwamba maslahi mapana ya Serikali yanalindwa muda wote na kwamba matumizi endelevu ya mfumo yanazingatiwa na unatumika katika namna inayohakikisha usalama na usiri wa taarifa zake zote zilizomo.

8.7.1.10 Kutokuzingatiwa kwa ushauri wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari L.D 615 VOL.XXV/31 YA 13 May,2021 iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya ushauri wa kisheria wa Rasimu ya Mkataba wa uwekaji wa mfumo UVIKO 19 Zanzibar ambapo alishauri mambo mbalimbali hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya haikuzingatia sehemu kubwa ya ushauri huo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. **Kiambatisho Nambari 22 Kinahusika.**

Miongoni mwa athari zinazoweza kujitokeza kwa kutozingatizwa kwa ushauri wa kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kama zifuatazo: -

- Kutozingatiwa kwa maslahi mapana ya Serikali kwenye mkataba ulioandaliwa na Wizara kwa kukosa ushauri wa Kisheria kutoka chombo huru kilichobobea kwenye masuala ya Sheria ili kulinda maslahi mapana ya Serikali na kuhakikisha haki inatendeka kwa pande zote za Mkataba.
- Kukosekana kwa thamani ya fedha (Value for Money) kwenye mkataba kwa kutozwa fedha nyingi tofauti za bei za soko kwenye huduma/ bidhaa kama hii.
- Uwepo wa vipengele vya taarifa zenye utata kwenye Mkataba vinavyoweza kuisababisha Serikali kupata hasara hususani panapotokea kutoelewana baina ya pande mbili za Mkataba na kulazimika kwenda Mahakamani kupata tafsiri sahihi.
- Kutozingatiwa kwa Sheria, Sera na Miongozo mbalimbali kwenye Manunuzi ya umma na kusababisha matatizo ya Kisheria katika utekelezaji wa mkataba husika.
- Kushindwa kudhibiti (control) na kuumiliki mfumo kwa kuwepo kwa kipengele cha "Software As Service – SAAS" ambacho kinaiondolea Wizara ya Afya haki ya kuumiliki.
- Uwezekano wa kubadilishiwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo na mtu anayesimamia mfumo akiwa na ajenda zake binafsi na kusababisha uwepo wa taarifa zisizoakisi uhalisia wa hali ya mambo.

Hivyo ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:-

- Kwa kuzingatia manufaa ya ushauri wa Kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuwa Wizara haikuzingatia ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya mapitio ya Mkataba huu ili kubaini maeneo yanayoweza kufanyiwa marakebisho na kufanya marekebisho hayo kulingana na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta tija na ufanisi kwenye mkataba huu.
- Wizara ifanye tathmini ya hasara iliyopata kwa kushindwa kuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchukuwa hatua kwa mujibu wa Sheria kwa wote waliohusika katika kusababisha hasara hiyo.
- Wizara kufanya majadiliano mapya na mtoa huduma (re-negotiate) katika bei za Mfumo huu na umiliki wake ili kulinda maslahi mapana ya Serikali.

8.7.1.11 Uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya taarifa zinazolingizwa katika mfumo hazina uhalisia. Hii inatokea pale ambapo mtu wa kwanza anayechukuwa taarifa za wateja (Daktari au Muuguzi) anaandika kwenye fomu maalum ambayo imendaliwa kwa kazi hiyo, lakini mtu huyu kuamua kujaza baadhi tu ya taarifa na kuacha wazi sehemu za taarifa nyengine ambazo ni za muhimu. Inapokuja kwa mtu anayeingiza taarifa hizi kwenye mfumo ambao unalazimisha taarifa zote za muhimu kuingizwa kwenye mfumo hata taarifa ambazo hazikujazwa kwenye fomu muingiza taarifa huyu hujaza kwa kukisia tu anachokiona yeye kinafaa.

Miongoni mwa taarifa zinazojazwa kwa kukisia ni pamoja na Dalili za mgojwa kwa wale ambao ni washukiwa (suspects), Umri, Makazi n.k, muingiza taarifa hufanya hivyo ili aweze kuendelea na hatua inayofuata katika mfumo. Vile vile ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya fomu zilizojazwa zimeandikwa katika namna ambayo inawapa ugumu waingiza taarifa kwenye mfumo kuelewa kilichoandikwa na kupelekea kuandika kwa kubahatisha tu ili aweze kumaliza kazi yake.

Aidha, ukaguzi umebaini kukosekana kwa umakini kwa wanaoingiza taarifa za wanaopimwa UVIKO 19 kupitia vituo mbali mbali kwenye mfumo kuwa miongoni mwa chanzo cha taarifa ambazo sio sahihi zilizomo kwenye mfumo. Kukosekana kwa umakini na kutozingatia athari zinazoweza kujitokeza katika hili kumpelekea kutotegemewa kwa taarifa za jinsia, umri, majina, picha, nambari ya nyumba n.k. Mfano, mtu mwanje jinsia 'ke', hujikuta amapewa majina ya jinsia 'me' na kinyume chake, picha ya jinsia 'me' hupewa majina ya jinsia 'ke', nambari za nyumba huingizwa sizo kwa mfano 1234, nambari ya hati ya kusafiria na mwaka wa kuzaliwa pia huandikwa ili kujaza nafasi iliyowazi. Mchanganuo wa dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika **Kielelezo A,B,C na D.**

Hali hiyo inaweza kupelekea athari zifuatazo:-

- Kutoa vyeti vya chanjo vyenye taarifa zisizo sahihi jambo ambalo litapelekea kutumia gharama mara mbili ili kurekebisha taarifa na kutengeneza vyeti vyengine vyenye taarifa sahihi.
- Vile vile itapelekea kutojua namba za kundi "batch number" gani iliyosababisha madhara ikiwa kati ya waliyochanjwa wamepata athari zitokanazo na chanjo (side effects) kama taarifa za kundi zilizolingizwa sio sahihi.
- Kuipotosha Serikali na wadau wengine kitaifa na kimataifa kuhusiana na takwimu za uchanjwaji kwa kuangalia jinsia, umri, maeneo n.k (demographic data).
- Kudhoofisha utegemezi wa mfumo katika kupata taarifa mbali mbali zilizo sahihi na kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi yenye kuleta tija, mfano kutengeneza sera za kuhamasisha uchanjaji, kujua ni maeneo yapi yako nyuma katika uchanjaji, kujua makundi ya umri au jinsia na mwikio wao katika uchanjaji.
- Kurudisha nyuma jitihada za Serikali za uwekezaji na kupata manufaa ya uwekezaji uliofanywa kwenye mifumo ya TEHAMA.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kuandaa mafunzo kwa kushirikiana na mtoa huduma wa mfumo na kuwafundisha waingizaji wa taarifa kwenye mfumo (data entries) yatakayowajengea uwezo wa kujua umuhimu wa taarifa wanazozingiza na athari zake ikiwa taarifa hizo hazitaingizwa kwa usahihi katika mfumo.
- Kuelimisha na kuhamasisha umma kufahamu umuhimu wa kutoa taarifa sahihi kwa ajili ya chanjo ya UVIKO -19 kwa kutumia njia zitakazowafikia makundi mbali mbali.
- Kuweka udhibiti wa utumiaji wa mfumo (application control) utakaohakikisha usahihi wa taarifa zinazoringizwa kwenye mfumo, mfano taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entry) na zikaguliwe na mtu mwingine (reviewer) ili kuhakikisha ubora na ukamilifu wa taarifa hizo kulingana na matakwa yaliyopo kabla ya kukamilika kwa zoezi hilo.
- Kuweka utaratibu utakaowezesha watu kufanya usajili binafsi na kuweka nafasi (self-registration and booking) kielekitroniki kabla ya kwenda kwenye kituo kuchanja jambo hili litasaidia kuingiza taarifa sahihi na kwa wakati na kupunguza muda unaotukima kuingiza taarifa wakati mtu amekwisha chanjwa ambao pia unaongeza muda wa kusubilia vyeti n.k.

8.7.1.12 Ucheleweshwaji wa malipo kwa kampuni ya Rahisi kinyume na makubaliano.

Kwa mujibu wa Mkataba kifungu 3.0 (iii) kinachotaka malipo yalipwe kila mwenzi na kwamba mtoa huduma atapeleka ankara siku ya 1 ya mwezi na Wizara italipa ankara ndani ya siku 14 baada ya kupokea Ankara. Hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara imeilipa kampuni ya Rahisi mwezi mmoja tu tangu mfumo uanze kufanya kazi mnamo tarehe 21 Mei, 2021 hadi ukaguzi unamalizika mwezi wa Disemba, 2021.

Hali hii inaweza kusababisha athari mbalimbali zikiwemo: -

- Kuzorotesha utoaji wa huduma unaofanywa na watoa huduma binafsi kwa kukosa nguvu za kifedha kutekeleza majukumu yao.
- Pia, mara kadhaa Serikali hushtakiwa na hata kupigwa faini vitu ambavyo vinaweza kuepukika ikiwa watumishi wa Serikali wenye jukumu la kuhakiki madai ya mtoa huduma na kuyaombea malipo watafanya kazi zao kwa uadilifu na uwajibikaji.
- Inaweza kuchochea rushwa inayopelekea huduma mbovu na kurudisha nyuma juhudi za Serikal katika kuleta maendeleo.
- Mtoa huduma kuongeza gharama za huduma (Mkataba) kwenye "tendering process" ili kufidia "time value for money" anayopoteza kwa kusubiria sana malipo yake na kupelekea thamani ya fedha zake kuwa ndogo kulinganisha na muda zilipokusudiwa kupokelewa.
- Kusitishiwa huduma ndani ya muda wa Mkataba kwa kuwa mtoa huduma hajalipwa na kupelekea usumbufu kwa jamii inayotumia huduma hizo.
- Serikali kukosa mapato.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kujipanga vyema na kuhakikisha kwamba madai ya watoa huduma wake yanafanyiwa kazi kwa wakati na kulipwa kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba, Sheria na Sera za nchi na kwamba maslahi ya Serikali ni muhimu yazingatiwe wakati wote.

8.7.1.13 Kutokuunganishwa kwa "Mobile App" ya "KoBoCollect" na Mfumo wa UVIKO 19.

Mwa mujibu wa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) "system interoperability" ni miongoni mwa vigezo muhimu vya kuzingatia katika utengenezaji wa mfumo wowote, hii inamaanisha kwamba mfumo unaweza kuonana/ kuunganishwa na mifumo mengine ili kurahisisha kubadilishana taarifa hali inayopunguza ulazima wa kuwa na mifumo mingi kwa wakati mmoja na kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazojitosheleza sehemu moja jambo linalofanya wepesi katika kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya (EOC) ilianza kutumia App ya Simu Janja (Mobile App) ijulikanayo kama KoBoCollect mnamo mwezi wa Disemba, 2021 katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuingiza taarifa za washukiwa (Suspects) wa UVIKO 19, pia kuna fomu ambayo hutumika kwa ajili ya kuingiza taarifa za wagonjwa wa uviko-19 aidha, imebainika App hii haijaunganishwa na Mfumo mkuu wa UVIKO 19 ambao ndio wenye taarifa nyingi zaidi za hali ya UVIKO 19.

Hali hii inaashiria kwamba mpaka sasa taarifa za UVIKO 19 zimetawanyika ambapo baadhi ziko kwenye mfumo wa UVIKO 19, baadhi bado ziko kwenye makaratasi (fomu) maalumu za kuchukulia taarifa hizo na baadhi ziko kwenye hii App ya Simu Janja tofauti na matarajio ya Serikali na wadau wengine wa kitaifa na kimataifa kwamba taarifa zote za UVIKO 19 zinapatikana kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Aidha, hali hii inaongeza ugumu wa kufanya maamuzi sahihi kwa wakati yanayohusu masuala mbalimbali ya UVIKO 19 ikiwa ni pamoja kutunga Sheria, Sera na miongozo ya usimamizi na uratibu wa UVIKO 19 pamoja na kutoa elimu kwa umma wa Wazanzibari kwa kukosa taarifa kamili sehemu moja na kwa wakati.

Hivyo Ukaguzi unashauri kuwa App ya KoBoCollect iunganishwe na mfumo wa UVIKO 19 taarifa zake kwa kuzingatia "format" ziende kwenye mfumo huu na zote zipatikane sehemu moja ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi kwa Serikali kama ilivyoelezewa hapo juu.

8.7.1.14 Uhaba wa matenki ya kuhifadhia maji safi na salama kwenye kituo cha kuchukulia sampuli cha Lumumba

Ukaguzi umebaini kuwa kituo cha kukusanya sampuli cha Lumumba hakina tenki la kuhifadhia maji safi yanayo hitajika sana kwa ajili ya kunawa mikono kama njia moja wapo ya kujikinga na maambukizi ya UVIKO 19, lakini pia kutumika katika vyoo kwa ajili ya usafi. Hali hii inasababisha usumbufu mkubwa na kuhatarisha usalama wa kiafya kwa wahudumu wa Afya na wapimwaji hususani kipindi inapotokea hakuna maji ya mfereji jambo ambalo linaweza kutokea wakati wowote.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kununua matenki ya kuhifadhia maji safi na salama yenye ujazo mkubwa yasiyopungua mahitaji ya wiki nzima ya kituo na kuhakikisha maji haya yanafika maeneo yanapohitajika kwa ajili ya kunawa mikono (maji tiririka), na usafi wa vyoo.

8.7.1.15 Maabara ya Mnazi Mmoja kutokuzingatia udhibiti wa ufikiaji (access control) kwenye komputa zinazotumika kuingiza taarifa za UVIKO 19 kwenye mfumo.

Kwa mujibu wa Mwongozo Wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti Za Serikali za eGovernment ya Tanzania katika kifungu 3.2 (ii) kinachowataka Maofisa wenye dhamana ya kusimamia Tovuti au kuweka taarifa kwenye Tovuti wawe na nywila (password) ambazo zinapaswa kubadilishwa angalau mara moja kwa kila mwezi”.

Ukaguzi umebaini kuwa komputa zenye mifumo zinatumiwa bila ya kuwa na nywila (password) jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo. Hhusani kama ikitokea mtu mwenye nia ovi akiingia kwenye komputa hizi na kukuta mfumo uko wazi anaweza kubadilisha, kufuta na kuingiza taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo.

Hivyo ukaguzi unashauri kuwa komputa zote ziwe na nywila (password) jambo ambalo litakalo weka usalama wa mfumo.

8.7.1.16 Kutokuwepo kwa mfumo wa ‘Barcord’ kwenye “Viral Transport Media (VTM)”.

Ukaguzi umebaini kuwa Maabara ya Taifa haina mfumo ‘barcord’ ambao ungetumika kwenye vifebeo vya sampuli vinavyojulikana kwa lugha ya kigeni kama ‘Viral Transport Media (VTM)’ kwa ajili ya kurahisisha zoezi la kuingiza taarifa za sampuli kwenye mashine ya kupima UVIKO 19 ambapo mtaalamu wa Maabara angepata taarifa zote kwa kumurika (scan) ile barcord iliyopo kwenye sampuli na kuingia kwenye kumbukumbu za mashine tayari kwa ajili ya kuanza upimaji, kinyume chake ni kwamba, mtaalamu wa Maabara huingiza taarifa sampuli kwa mikono (manually) moja baada ya nyingine, jambo hili linapelekea kuchukua muda mrefu zaidi na kuongeza hatari (risk) ya kufanya makosa ya kibinadamu (human errors) ambayo ni pamoja na kuingiza taarifa za sampuli zisizo sahihi.

Hivyo ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kupitia Maabara ya Taifa kuwa na mfumo ‘barcord’ ambao ungetumika kwenye vifebeo vya sampuli ili kurahisisha zoezi la kuingiza taarifa za sampuli kwenye mashine ya kupima UVIKO 19.

8.7.1.17 Upungufu wa vitendea kazi (computers) kwa watumiaji wa mfumo (data entries).

Kutokana na Mkataba kifungu 6.0 (ii) kinaitaka Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa vituo vyote vina vifaa vya kutosha. Hivyo ukaguzi umebaini kuwa watumiaji wa mfumo wa UVIKO 19 wanauhaba wa vifaa kama kompyuta zinazohitajika kwa ajili ya kuingizia taarifa za upimaji na majibu kwenye mfumo, wakati wa wimbi (wave) likiwa juu Maabara ilikua na waingiza taarifa 6 jambo ambalo kompyuta zilizokuwa zikitumika zilikua 2 pekee.

Hali hii ilichangia sana kuchelewesha uingizaji wa taarifa hizi kwenye mfumo na hivyo kuchelesha upataikanaji wa majibu na taarifa sahihi kwa wakati kwa ajili ya kufanya maamuzi na kuchukua hatua stahiki za kupambana na janga la UVIKO 19.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka vifaa vya kutosha katika vituo vyote vilivyopo Unguja na Pemba.

8.7.1.18 Vituo vya Afya kutokuwa na ufikiaji wa mfumo (system access) kwa ajili ya kuingiza taarifa za washukiwa.

Ukaguzi umebaini kuwa miongoni mwa vituo vya Afya 35 ni kituo kimoja pekee cha Makunduchi ndicho kina ruhusa ya kuingiza taarifa za washukiwa wa UVIKO 19 moja kwa moja kwenye Mfumo wakati wa mahojiano (interview) na mshukiwa ambapo ni sawa na takribani asilimia 3 ya vituo vyote.

Kwa mfano, Kwa sasa Hospitali kama Mnazi Mmoja inayochukua sampuli na kupima UVIKO 19 kwa waliosamehewa na washukiwa ambao wanatokea katika Wodi na vitengo vingine mbalimbali kama 'Emergency' vyote havina uwezo wa kuingiza taarifa moja kwa moja kwenye Mfumo wa UVIKO 19 na badala yake wahusika wanachukua taarifa kwa kutumia fomu maalumu na kuandika kwa mikono (manually) na kuzipeleka kwa waingiza taarifa (data entries) ili ziingizwe kwenye mfumo.

Hali hii inachangia kwa sehemu kubwa kudhohofisha ubora na ucheleweshwaji wa taarifa sahihi za wagonjwa na washukiwa kwa wakati jambo ambalo linaathiri jitihada za mapambano dhidi ya UVIKO 19 hapa nchini kwa kushindwa kujua takwimu kamili za maambukizi na hali ya tatizo kwa wakati ili kuchukua hatua stahiki.

Ukaguzi uishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mtoa huduma ya mfumo kutengeneza mpango kazi utakaoanzia na mambo yafuatayo:-

- Kuainisha maeneo yote ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na vituo vyote vinavyo chukua taarifa za wapimwaji ili kubaini wataalamu wa Afya kama vile madaktari, wataalamu wa Maabara na wengineo wanao hitaji ruhusa (access) ya mfumo wa UVIKO 19.
- Kuwapatia mafunzo hatua kwa hatua yatakayowawezesha kuingiza taarifa sahihi kwa wakati.
- Kuwapa ruhusa ya kuingiza taarifa hizo kwa kuzingatia udhibiti (controls), usalama na ubora wa taarifa husika ili waweze kuingiza taarifa hizo moja kwa moja (live data) wakati wakiwa na wapimwaji.

8.7.1.19 Ucheleweshwaji wa vyeti vya chanjo ya UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini uwepo wa vituo 12 vilivyopo Pemba na 27 kwa upande wa Unguja vinavyotoa chanjo ya UVIKO 19, hata hivyo vituo vyote vinatumia fomu maalumu kuchukua taarifa za wachanjwaji kwa mkono (manually) kisha baada ya muda usiojulikana taarifa hizo huingizwa kwenye mfumo wa UVIKO 19 kupitia waingiza taarifa (Data entries) waliopo kwenye vitengo maalumu (data entry sections) kinyume na viwango bora vinavyokubalika (best practice) vya matumizi ya mifumo ya TEHAMA vinavyoelekeza uingizwaji wa taarifa kama hizi moja kwa moja kwenye mfumo wakati tukio linapotokea (live data entry).

Athari za ucheleweshwaji ya upatikanaji wa vyeti kwa wakati hili ni pamoja na usumbufu mkubwa kwa wananchi hususani kwa wale wanao hitaji vyeti kwa haraka ili kukidhi masharti ya kusafiri kwenda nchi za nje kwani pamoja na kua wamesha kamilisha malipo ya vyeti hawawezi kupata vyeti kwa

sababu taarifa zao mara nyingi zinakua hazijaingizwa kwenye mfumo. Ili kupata cheti cha chanjo kinachotengenezwa Wizarani pekee ni lazima aliyechanjwa asafiri kutoka aliko na kuja Wizarani kuwasilisha stakabadhi ya malipo ambayo itaingizwa kwenye mfumo na kisha kutengenezwa cheti, inapotokea taarifa zake hazijaingizwa kwenye mfumo maana yake ni kwamba hata taarifa za malipo haziwezi kuingizwa na hivyo basi hatopata cheti kwa wakati jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gharama na muda kwa ajili ya kusafiri kuja kufuatilia vyeti Wizarani.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto mambo yafuatayo:-

- Kuweka utaratibu mzuri utakao hakikisha taarifa za wateja wake (Wananchi) zinaingizwa kwenye mfumo kabla au wakati wa kuchanja ili kwamba anapomaliza kuchanjwa taarifa zake ziwemo kwenye mfumo na awe tayari kuendelea na hatua nyingine bila kukwama kama vile kulipia huduma ya cheti na kupatiwa cheti chake bila kuchelewa.
- Wizara ifanye utaratibu wa kuziwezesha Hosipitali za Wilaya kuweza kupokea stakabadhi za malipo na kutoa vyeti ya chanjo ya UVIKO 19 ili kuwapunguzia gharama za usafiri na muda wananchi wanaokaa nje ya mji kwa kulazimika kwenda Wizarani (Mjini Unguja) kupeleka stakabadhi za malipo na kupatiwa vyeti vyao.
- Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba vituo vinavyo tumika kuingiza taarifa za chanjo kwa sasa vinapatiwa huduma ya mtandao (internet) bila kukoma ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti na fedha kwa ajili ya huduma hiyo kulingana na mahitaji yaliyopo kwani pasipokua na mtandao uingizwaji wa taarifa kwenye mfumo pia unasimama jambo ambalo linakwamisha ufanisi wa Wizara katika kupata na kutunza taarifa za uchanjaji kielekitroniki kwa kutumia mfumo ulioigharimu Serikali pesa nyingi.
- Wizara ifanye maboresho au ihuwishe miongozo yake (Standard Operating Procedures –SOP) utaratibu unaojumuisha muda mfupi kwa kuzingatia mahitaji ya wasafiri kwenye kuchanja na kutoa vyeti vya chanjo mfano masaa 24 kila aliyechanja na kukamilisha malipo ya cheti apate cheti chake kwenye Hosipitali za Wilaya ama maeneo ya karibu zaidi na makazi yao.

8.7.1.20 Kutokuunganishwa kwa mfumo wa UVIKO -19 na kanzi data za NIDA na benki ya PBZ.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mfumo unakubali tarakimu zozote zinazolingizwa kwenye sehemu ya nambari ya risiti (receipt number) na nambari ya muamala (transaction number) kwa benki ya PBZ na vitambulisho vya NIDA.

Hali hii inaongeza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuwa hakuna udhibiti wa mfumo kwenye uingizaji wa namba sahihi za miamala na namba za stakabadhi zilizotoka Benki pekee jambo ambalo lingewezekana ikiwa pangekuwepo na kuunganishwa kwa mfumo hiyo miwili.

Ukaguzi unashauri Wizara Afya kushirikiana na Rahisi Solution Company, PBZ and NIDA ili kufanya uunganishwaji wa mfumo huu na kanzi data za NIDA na benki ya PBZ ili kuondosha mianya iliyopo ya upotevu mapato ya Serikali.

Kielelezo E: Kinaonesha kuwa namba ya NIDA sio sahihi imeingizwa kwenye mfumo.

Kielelezo F: Kinaonesha kuwa namba ya muamala na namba ya stakabadhi ni sawa hali ya kuwa hazikutakiwa kuwa sawa.

Kielelezo G: Kinaonesha kuwa nambari ya stakabadhi ya benki tayari imeshatumika lakini baada ya kuodosha sifuri ya mwanzo ya nambari ya stakabadhi imekubalika.

Kielelezo H: Kinaonesha kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote licha ya kuwa si sahihi na hivyo kuonekana mwananchi ameshalipa.

8.7.1.21 Udhaifu wa udhibiti wa kuingiza taarifa za malipo ya vipimo vya UVIKO 19 kwenye mfumo

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya haina utaratibu mzuri wa kuingiza taarifa za malipo ya huduma za UVIKO 19 kwenye mfumo hususani kwa wateja wanaolipia kupitia kuweka fedha benki (bank deposits) ambao wanatakiwa kupeleka stakabadhi za malipo kwa watu walioruhusiwa kuingiza taarifa hizo kabla ya kupewa huduma. Hali ilivyo sasa ni kwamba kuna baadhi ya watu ambao sio wa kada ya uhasibu na wala sio watumishi wa Wizara ya Afya wanafanya kazi ya kuingiza taarifa za malipo kwenye mfumo wa UVIKO 19 na kuruhusu wateja kupewa huduma.

Hali hii inapunguza udhibiti wa mapato ya UVIKO 19 kwa Wizara ya Afya kwa kuwa Wizara imebaki kungojea kupewa taarifa za makusanyo yaliyopatikana pasipo Wizara yenyewe kushiriki ipasavyo ukusanyaji huo ili kuhakikisha kwamba mapato yanayo ripotiwa Serikalini ni sahihi na halisi kwa mujibu wa huduma zilizotolewa. Mfano hai katika hili ni baadhi ya wafanyakazi wa Zanz Medicals wamepewa ruhusa ya kuingiza taarifa za malipo kwenye mfumo wa UVIKO 19 ambao kimsingi hawana dhamana ya kufanya kazi hii kwa upande wa Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha inachukuwa jukumu la kuingiza taarifa zote za malipo ya huduma za UVIKO 19 kwenye mfumo wa UVIKO 19 na jukumu hili lipewe Idara ya Uhasibu wenye dhamana ya kazi hiyo ili kuweza kutumia taaluma zao kama inavyotarajiwa na kuwajibika pale wanapokwenda kinyume na Sheria, Sera na Miongozo kwenye jukumu hilo.

Aidha, watu wengine wote wasio kuwa kwenye Idara ya Uhasibu wa Wizara ya Afya watolewe ruhusa ya kuingiza taarifa za malipo ya huduma kwenye mfumo isipokuwa kwa viongozi wa Wizara wanaotakiwa kufahamu hali ya makusanyo ya fedha hizo wanaweza kupewa ruhusa ya kusoma pekee (read only access).

8.7.1.22 Kutorejeshewa fedha kwa wakati kwa miamala iliyofanyika zaidi ya mara moja kupitia mtandao wa kibenki wa Visa/Master card wa benki ya CRDB

Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto kwenye malipo yanayofanyika kupitia mtandao wa benki ya CRDB wa "Visa/ Master card", changamoto hii hupelekea baadhi ya wateja kufanya malipo zaidi ya mara moja (double payments) kwa kuwa malipo ya awamu ya kwanza yanachelewa kuonekana kwenye mtandao wa UVIKO 19 na kuzuia wateja kupewa huduma kwa wakati jambo ambalo hulazimisha wateja kufanya tena malipo kwa kuweka fedha benki (bank deposit) na kuwasilisha stakabadhi za malipo kwa watoa huduma ili kupewa huduma na kuweza kusafiri.

Hali hii hupelekea migogoro na malalamiko kwa wateja kwenda kwa watoa huduma (Zanz Medicals) yanayotokana na kulipia huduma moja mara mbili kwa sababu wateja wanahitaji warejeshewe fedha zao za miamala ambayo wao walikatwa kwenye benki zao lakini miamala hiyo kuchelewa kuingia au kutoingia kwenye mfumo wa UVIKO 19 na kupelekea kuonekana kuwa hawajalipia huduma husika.

Ukaguzi unashauri yafuatayo: -

- Wizara ya Afya kuweka muwakilishi wake katika eneo la kufanyia vipimo vya UVIKO 19 atakayekuwa na mamlaka ya kusemea miamala yenye shida ili kwamba wateja wote wapeleke malalamiko yao kwa mtu huyu atakae yatolea ufafanuzi wakati wote bila kuathiri kazi za upimaji.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Rahisi Solution Company na CRDB Bank kufanya tathmini ya utendaji kazi wa njia hii ya malipo ili kubaini chanzo cha changamoto hii ya kuipatia ufumbuzi wa kudumu.
- Kwa miamala inayokuwa imezuiliwa na benki ya mteja kwa sababu mbalimbali iwekewe utaratibu utakaoleta ujumbe kwa mteja kwamba muamala umezuiliwa kwa sababu "xyz" ili kupunguza malalamiko mengine ambayo hayana msingi.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution Company kufanya tathmini ya miamala yote iliyolipia huduma moja zaidi ya mara moja na kuweka utaratibu wa kurejesha miamala hiyo kwa wahusika ili kulinda heshima ya Serikali kwa watalii na watanzania kwa ujumla.
- Miamala yote inayoshindwa kukamilika kwa sababu za mtandao pawekwe utaratibu kuibaini na kuirejesha miamala hiyo moja kwa moja (automatically) kila baada ya masaa 24, baada ya kujiridhisha kwamba huduma husika tayari zimeshalipiwa kwa njia nyengine kama vile kuweka fedha benki (bank deposit) n.k.

8.7.1.23 Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan).

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi hawana Mpango wa kuendeleza biashara baada ya maafa kinyume na Sera ya Wakala wa Serikali Mtandao kifungu cha 4.4.1.2.(d), ambapo Taasisi za Serikali zenye mifumo zinatakiwa kuanzisha mpango na miundombinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yanayoweza kujitokeza wakati wowote na kuathiri mifumo ya Taasisi.

Mpango huo unatarajiwa kuelezea hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa zote za mfumo yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Kwa kuwa mfumo wa UVIKO 19 ni mali ya Wizara ya Afya na kwa kuwa mfumo huu unahudumiwa (hosting and administration) na kampuni ya Rahisi, ukaguzi unaishauri Wazara kuhakikisha kwamba inaandaa mpango wa kuendeleza biashara kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi na kuhakikisha

kwamba Rahisi anapata nakala ya mpango huu ili kuwa tayari kuutumia mara yakitokea maafa kwenye chumba maalumu cha Seva katika kupunguza au kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

8.7.1.24 Kukosekana kwa ushahidi wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19.

Kwa mujibu wa kifungu 2.1.6.1 cha mwongozo wa eGaz wa utengenezaji, upatikanaji, uendeshaji na utunzaji wa mifumo (eGAEXT/APA/005), Taasisi za umma zinatakiwa kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo na watumiaji wa mifumo hiyo ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mfumo unakidhi mahitaji ya mtumiaji.

Ukaguzi haukupata uthibitisho wowote wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19 na watumiaji wa Wizara ya Afya kabla ya kuanza kutumika kukusanya, kuratibu na kusimamia taarifa za UVIKO 19 Zanzibar. Hali hii imepelekea uwepo wa maeneo yenye udhaifu katika mfumo ambayo yalitakiwa kubainika wakati wa kufanya majaribio ya mfumo, hili linajumuisha eneo la taarifa za washukiwa (suspects) ambalo halijakidhi mahitaji ya watumiaji wa mfumo. Kwa ujumla, kitendo cha mfumo kutokufanyiwa majaribio na watumiaji kunaweza kuwa na tafsiri mbalimbali ikiwemo, kutokuwa na mahitaji rasmi ya watumiaji wa mfumo ambayo ndio yanayojaribiwa kuhakikisha kwamba yamefanyiwa kazi kikamilifu na watengeneza mfumo, kutozingatiwa kwa miongozo ya kutengeneza mifumo n.k

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuzingatia Sera na Miongozo ya Wakala wa Serikali mtandao (eGaz) na Miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utekelezaji na mifumo ya kielektroniki ili kuhakikisha kwamba mifumo hiyo inakidhi mahitaji ya watumiaji ya sasa na ya wakati uja kulingana na maendeleo ya Teknolojia ya TEHAMA ili kupunguza au kuondoa kabisa wingi wa maboresho yanayofanywa kwenye mfumo muda mfupi baada ya kuanza kutumika ambayo mara nyingi huwa na athari hasi zinazoweza kupunguza tija na ufanisi kwenye matumizi ya mfumo.

Kufanya majaribio ya mfumo mzima ili kubaini mapungufu yote yaliyopo sasa na kuyawasilisha kwa kampuni ya Rahisi ili yatatuliwe kwa pamoja kabla mfumo huu haujakabidhiwa Wizara ya Afya.

8.7.1.25 Mfumo kutotambua uhalali wa stakabadhi za benki za malipo ya UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote zinazoingizwa sehemu ya namba ya stakabadhi (receipt number) na namba ya muamala (transaction number) ya benki ya PBZ. Baada ya kulipia huduma kupitia benki ya PBZ mteja anatakiwa kwenda kituoni na stakabadhi yake ili kuingizwa malipo hayo kwenye mfumo kabla ya kupewa huduma, mfumo hauna uwezo wa kutambuwa namba sahihi na halisi za stakabadhi za Malipo jambo linalo pelekea kukubali namba yoyote ile hata ambayo imekwishatumika na kuruhusu kuendelea na hatua inayofuata.

Udhaifu huu wa mfumo umekuwa ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya uvujifu wa mapato ya Serikali kwa kutokuwa na udhibiti unaostahili na badala yake kutegemea uadilifu wa watu waliopewa ruhusa ya kuingiza taarifa za Malipo kwenye mfumo pekee.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi kufanya uunganishaji wa mfumo huu na kanzi data ya benki ya PBZ ili kuweka udhibiti wa namba za stakabadhi za malipo yote yaliyofanywa kupitia benki ya PBZ kuhakikisha kwamba mfumo unazigundua na kuzizuia/kuzikataa stakabadhi zilizotumika na ambazo hazipo kwenye kanzi data ya PBZ.

Aidha, Wizara inashauriwa kuweka matumizi ya mfumo wa Zan Malipo unaotengeneza namba za ankala (Control Numbers) kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi na eGaz utakao unganishwa na mfumo wa UVIKO 19 ili kudhibiti mianya iliyopo kwa sasa na kuhakikisha kua unawekewa mkakati wa kuutekeleza kwa ufanisi na haraka.

Kielelezo L: Kinaonesha kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote za stakabadhi za malipo za benki ya PBZ (bank deposit slip). *(mteja huyu hakulipa malipo lakini ziliandikwa nambari za kubuni na mfumo ukamtambua kama ameshalipa).*

8.7.1.26 Udhaifu wa udhibiti wa uingizaji wa Malipo ya Vyeti vya Chanjo ya UVIKO 19

Kulingana na udhibiti wa ndani ya Wizara ya Afya, malipo yote yaliyofanywa na wateja kupitia Benki yanatakiwa kuwasilishwa stakabadhi za malipo hayo Wizara ya Afya kwa ajili ya kuingizwa taarifa zake kwenye mfumo ili kutengenezewa cheti ambapo kwa sasa vyeti vyote hutengenezwa Wizarani pekee.

Katika kukagua eneo hili ukaguzi umebaini kwamba wapo baadhi ya wateja ambao wamekuwa wakienda Wizarani kupeleka stakabadhi za malipo ili ziingizwe kwenye mfumo kwa ajili ya kutengenezewa vyeti na kubainika kuwa stakabadhi hizo tayari zimekwisha ingizwa kwenye mfumo na watu wengine tofauti na waliopo Wizarani na kutakiwa kuendelea na hatua nyengine za kufuatilia vyeti kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo J**, hii ina ashiria kwamba kuna watumiaji wengine zaidi ya wale waliopo Wizarani ambao wamepewa ruhusa ya kuingiza malipo ya vyeti kinyume na udhibiti wa ndani wa Wizara (internal control).

Hali hii inaondoa udhibiti wa mapato yatokanayo na vyeti vya chanjo ya UVIKO 19 na kuongeza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali na kutengeneza mazingira ya rushwa kwani watu hawa wenye ruhusa ya kuingiza malipo wanaweza kuingiza malipo hewa kwenye mfumo kwa kua mfumo una udhaifu katika eneo hili kiasi cha kuruhusu nambari yoyote ile ya stakabadhi ya benki kutumika.

Ukaguzi unashauri yafuatayo:-

- Uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Rahisi Solution kuhakikisha kuwa watumiaji wa mfumo wanaoingiza taarifa za malipo ya vyeti vya chanjo za UVIKO 19 wanachujwa na kubakia wale wanaotambulika na wenye jukumu hilo kwa mujibu wa ajira zao Serikalini na kuwaondolea ruhusa wengine wote wasio stahili kufanya kazi hiyo.
- Wizara kuweka fomu maalum ya kuidhinisha watumiaji wa mfumo wa UVIKO 19 itakayo oneshwa majukumu ya kila mtu kwa kipindi husika ambayo itaidhinishwa na kiongozi wake wa kitengo au Idara ndani ya Wizara au taasisi yake kabla ya kuingizwa kwenye mfumo kama mtumiaji ili kuimarisha udhibiti wa watumiaji wa mfumo.
- Uongozi wa Wizara kuwaelimisha wanaoingiza taarifa za mapato juu ya athari za kughushi namba za stakabadhi za malipo za benki wakati wanaingiza taarifa hizo kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na kufanya vitendo vya uhujumu wa uchumi, ubadhirifu wa fedha za Serikali pamoja na matumizi mabaya ya ofisi.
- Kuweka matumizi ya mfumo wa namba za bili (Control Number system) utakao unganishwa

na mfumo wa UVIKO 19 ili kudhibiti mianya iliyopo kwa sasa na kuhakikisha kuwa mfumo unawekewa mkakati wa kutekeleza kwa ufanisi na haraka.

8.7.1.27 Udhaifu wa udhibiti wa msamaha wa upimaji UVIKO 19

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Afya inaudhaifu kwenye mchakato wa kutoa msamaha dhidi ya gharama za upimaji wa UVIKO 19 ambapo haijulikani vigezo rasmi vya kuzingatia ili kutolewa msamaha, utowaji na msamaha kufanywa na mtu mmoja badala ya kamati, kukosekana kwa azimio la Wizara la kutoa msamaha wa gharama za kupima UVIKO 19 kwa makundi mbalimbali ya watu.

Udhaifu huu umepelekea misamaha kutolewa kiholela Wizarani na kuikosesha Serikali mapato kwani baadhi ya waliopewa misamaha hii wanauwezo wa kulipia gharama husika. Aidha, udhaifu huu umepelekea manung'uniko kwa baadhi ya watumishi wanaonyimwa msamaha na kuathiri utendaji wa kazi.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kutengezea vigezo rasmi vitakavyotumika kutoa msamaha na kuviweka wazi kwa umma ili kila anayetimiza vigezo husika apatiwe msamaha husika. Pia, Wizara inashauriwa kwamba mchakato wa kutoa msamaha usifanywe na mtu mmoja badala yake iundwe kamati itakayokuwa na jukumu la kupitia maombi yote ya misamaha na kuyatolea maamuzi.

8.7.1.28 Kukosekana kwa muunganiko "Integration" baina ya Mfumo wa UVIKO 19 na Mfumo wa Vitambulisho vya Mzanzibari (Zan ID System).

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kuwa mfumo wa UVIKO 19 ulikua unatumika pasipo kuunganishwa na mfumo za vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kwa kipindi kisichopungua miezi 10 ya mwaka 2021, jambo ambalo limechangia uingizwaji wa baadhi ya taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Kwa kuwa kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ni moja ya vitambulisho vilivyoenea zaidi miongoni mwa wazanzibari na kwa kua mfumo wa UVIKO 19 unahitaji utambulisho halisi wa anayepimwa au anayechanjwa na kwa kuzingatia ukweli kwamba moja ya malengo ya kuanzisha mfumo huu wa UVIKO 19 ni pamoja na kukusanya taarifa sahihi zinazohusu UVIKO 19 kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi sahihi na kwa haraka katika kukabiliana na janga hili, aidha ilitarajiwa uunganishwaji wa mifumo hii miwili iwe ni miongoni mwa vipaumbele katika utekelezaji wa mfumo wa UVIKO 19 kwani taarifa zao zote muhimu zinazohitajika kwenye mfumo wa UVIKO 19 zinapatikana kwenye mfumo wa Zan ID ukiachilia mbali kwa watu wachache ambao taarifa zao hazijakuwemo.

Hata hivyo mnamo mwezi wa Januari 2022, ukaguzi ulipata taarifa kutoka kwa uongozi wa Wizara ya Afya kwamba uunganishwaji wa mifumo hii miwili umefanyika kikamilifu ambapo katika kujiridhisha ukaguzi uligundua kwamba uwepo wa udhaifu kwenye mfumo katika hatua ya kuchagua kama mteja ana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au hana, na kama anacho kitambulisho bado mfumo ulikuwa unaruhusu kuingiza taarifa kwa mkono, mwanya huu umekuwa chanzo kikuu cha kuingiza taarifa tofauti na zilizopo kwenye mfumo wa Zan ID.

Uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19 unaashiria mambo mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

- Watumiaji wa mfumo kutopewa mafunzo ya mfumo kulingana na maboresho yaliyofanywa ikiwemo “integration” jambo ambalo hupelekea watumiaji kuutumia mfumo kama ilivyokua awali kabla ya kuunganishwa na kupelekea kufanya makosa mbalimbali.
- Mfumo kutokua na udhibiti toshelevu (insufficient controls) kulingana na mazingira yanayotumika hususani pale mteja anapokua na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi, mfumo ulitakiwa usitoe mwanya wa muingiza taarifa kuandika taarifa za mteja huyu badala yake taarifa zote zipatikane kutoka kwenye mfumo wa Zan ID ambao tayari umekwisha unganishwa na mfumo wa UVIKO 19. **Kielelezo K Kinahusika.**
- Kutokuonekana bayana kwa manufaa ya kazi kubwa iliyofanywa ya kuiunganisha mifumo hii miwili kwani lengo la kuhakikisha zinapatikana taarifa sahihi na kwa haraka kutoka kwenye kanzi data ya Zan ID bado halijafikiwa jambo ambalo pia linapunguza morali ya kazi kwa wafanyakazi, kupunguza utegemezi wa TEHAMA kwenye kurahisisha kazi na kuleta tija na ufanisi wa kuwahudumia wananchi.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution kufanya yafuatayo:-

- Kuandaa mpango kazi wa mafunzo kwa watumiaji wote wa mfumo na kutoa mafunzo yatakayo kuwa endelevu ili kukabiliana na mabadiliko mbali mbali yakiwemo ya mfumo au watumiaji wa mfumo angalau mara moja moja kila yanapotokea mabadiliko husika.
- Kuongeza udhibiti kwenye mfumo utakao hakikisha kwamba ikiwa kitambulisho kilichochaguliwa kutumika ni Zan ID basi mfumo usiruhusu uingizwaji wa taarifa kwa kuandika badala yake taarifa zote zipatikane kutoka kwenye kanzi data ya Zan ID. Utaratibu kama huu uzingatiwe pindi mfumo huu utakapounganishwa na kanzi data nyengine kama vile NIDA.
- Ikiwa mteja atakua na kitambulisho cha Zan ID ambacho taarifa zake hazijaonekana kwenye kanzi data ya Zan ID na kupelekea kutotambulika kwa kitambulisho chake au ikiwa hana kabisa kitambulisho cha Zan ID wala chengine chochote kile basi pawepo na mbadala ‘Others’ kwenye aina ya kitambulisho utakao toa ruhusa kwa muingiza taarifa kuweza kuingiza taarifa za mteja huyo kwa kuandika mpaka mwisho.

8.7.2 Dosari zilizobainika katika kampuni ya Zanz Medical

Kwa kuzingatia mkataba wa upimaji wa UVIKO 19 kwa wasafiri ulioingiwa kati ya Wizara ya Afya na kampuni ya Zanz Medicals, Sheria, Sera Miongozo na taratibu zilizopo ukaguzi ulipitia wajibu, majukumu na haki za kampuni ya Zanz Medicals ambapo mambo mbali mbali yalibainika kama ifuatavyo:-

8.7.2.1 Kutokuendelea na upimaji kwa wasafiri waliopimwa mwanzo na kubainika kuwa na maambukizi ya UVIKO 19

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Zanz Medicals "Appendix A" kifungu namba 2(d) kinachosema "wasafiri waliopatikana na virusi wanapaswa kupimwa bila malipo hadi watakapothibitishwa kuwa hawana maambukizi" hata hivyo ukaguzi ulibaini kwamba wasafiri wote wasiosamehewa wanalipia huduma ya kupima UVIKO 19 na baada ya kupimwa wanapobainika kuwa na maambukizi utaratibu unawataka kuahirisha safari na kurejea tena kupimwa baada ya siku saba (7) hata hivyo upimwaji huu haufanywi tena na Zanz Medicals badala yake umehamishiwa kwenye Maabara ya Mnazi Mmoja kinyume na matakwa ya mkataba uliopo baina ya Wizara na Zanz Medicals.

Ukaguzi unashauri kwamba Wizara ya Afya isimamie matakwa ya mkataba uliopo na kuhakikisha kwamba Zanz Medicals anatimiza wajibu wake kama ilivyoainishwa kwenye mkataba huu na kwamba wasafiri wote wanaolipia huduma ya upimaji wanapimwa na Zanz Medicals mpaka wanapokuwa tayari kusafiri kwa mujibu wa miongozo ya Afya kwenye UVIKO 19 na sio kuwahamishia kwenye Maabara ya Serikali huku wakikwepa jukumu lao la msingi.

8.7.2.2 Udhaifu katika kudhibiti ufikiaji wa mfumo wa UVIKO 19 (access control) kwenye kompyuta zinazotumiwa kuchakata taarifa na kufanya vipimo vya UVIKO 19 Maabara.

Ukaguzi umebaini kuwa kompyuta zinazotumika kuingiza na kuchakata taarifa za UVIKO 19 kwenye Maabara ya Zanz Medicals hazina udhibiti wa ufukiaji (access control) na kwamba watumiaji wanaingia bila kutakiwa kuingiza nywila (password) zao jambo ambalo linahatarisha usalama wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo.

Kwa kuzingatia hali halisi ya ugonjwa wa UVIKO 19 duniani na dhana zilizo ambapo sehemu za jamii mbalimbali bado zinaamini kwamba ni ugonjwa uliotengenezwa na unakuzwa kwa malengo ya watu fulani hivyo kufanya mbinu mbalimbali za kurudisha nyuma jitihada za Serikali na wadau wengine katika kuidhibiti hali iliyopo jambo linalomaanisha kwamba taarifa za UVIKO 19 zinatakiwa kulindwa kwani zinaweza kuharibiwa na watu wenye nia mbaya mara kama wakipata nafasi ya kufanya hivyo. Kuziacha bila ya kudhibiti kompyuta zinazotumika kuingiza taarifa za UVIKO 19 ni kuongeza hatari ya kuharibiwa kwa taarifa za UVIKO 19 ndani ya Maabara ya Zanz Medicals.

Kufuatia hali hii, ukaguzi unaishauri Zanz Medicals kuweka udhibiti kwenye kompyuta zake zote zinazotumika kwenye Maabara yake katika kuingiza na kuchakata taarifa za UVIKO 19. Udhibiti huu unaweza kuwekwa kwa kutumia nywila, ambapo kila mtumiaji wa Kompyuta hizi atatakiwa kuwa na akaunti na nywila yake.

8.7.2.3 Udhaifu wa udhibiti wa chumba cha Maabara Zanz Medicals.

Ukaguzi umebaini kuwa Maabara ya Zanz Medicals inayopima UVIKO 19 haina udhibiti unaostahili kwa kukosa kamera za ulinzi (CCTV Camera) na kukosa udhibiti wa milango katika kuingia ndani ya chumba cha Maabara. Kwa mujibu wa "best practice guidelines" milango ya vyumba nyeti kama vile Maabara na chumba cha kuhifadhi vitu vya thamani inapaswa kuwa na udhibiti wa kuingia

ambapo vifaa maalumu huwekwa milangoni ili kuhakikisha kwamba wanaoingia kwenye vyumba hivi ni wahusika pekee au watu walioruhusiwa tu na kwamba watu wengine hawapati kuingia kwenye vyumba hivi. Kamera za ulinzi pia huwekwa ndani ya vyumba hivi ili kuongeza udhibiti na ulinzi wa maeneo haya.

Kutokana na kukosekana kwa udhibiti mzuri wa Maabara kunapelekea hatari ya kufanyiwa hujuma kirahisi na watu wenye nia mbaya na kutobainika kwa haraka jambo ambalo linaweza kusababisha athari za kijamii na kiuchumi kwa kuwa upimaji wa UVIKO 19 unaohusisha watalii na wageni wengine wanaokuja nchini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuwekwa udhibiti mzuri wa usalama katika Maabara ikiwa ni pamoja kuwa kamera za ulinzi sehemu ya kuingilia Maabara (main entrance) na ndani ya Maabara ili kuimalisha ulinzi na usalama wa taarifa za wateja wake kwa niaba ya Serikali ili kuziba mianya iliyopo sasa.

8.7.2.4 Kutokufuatwa miongozo ya Wizara ya Afya (SOP) katika utekelezaji wa kazi za upimaji UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini kuwa Zanz Medicals hawana miongozo (SOP) kutoka Wizara ya Afya wanayoifuata katika kuendesha shughuli za Maabara Zanzibar. Aidha ukaguzi umebaini kwamba Maabara ya Mnazi Mmoja ina miongozo mbali mbali inayotakiwa kuzingatiwa na Maabara zinazofanya kazi hapa Zanzibar tofauti na hali halisi tuliyoikuta Zanz Medicals. Hali hii inatilia shaka ubora na viwango vya kazi za upimaji wa UVIKO 19 unaofanywa na Zanz Medicals kutokana na kutokufuata miongozo iliyopo kutoka Wizara ya Afya.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya yafuatayo: -

- Kuipatia kampuni ya Zanz Medicals miongozo yote ya Maabara iliyopo nchini na kuisimamia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba inafuata miongozo hiyo (SOP) kwa lengo la kupatikana tija na ufanisi.
- Kuhakikisha kuwa inaifanyia ukaguzi kampuni ya Zanz Medicals angalau mara mbili kwa mwaka katika jitihada za kupata utekelezaji wa miongozo iliyowekwa na kubaini changamoto nyenginezo zilizopo ili kuzipatia ufumbuzi kwa haraka kwa kuwa mafanikio ya Zanz Medicals kwenye upimaji wa UVIKO 19 ni mafanikio ya Serikali kwa ujumla wake.

8.7.2.5 Kutokuwekwa vituo vya kupima UVIKO 19 kwenye Bandari za Mkokotoni na Kizimkazi.

Kwa mujibu wa makubaliano baina ya Wizara ya Afya na Zanz Medicals, palitakiwa kufunguliwa vituo vya upimaji wa UVIKO 19 kwenye maeneo ya Mkokotoni na Kizimkazi hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa mpaka sasa maeneo hayo hayajanzishwa. Kutoanzishwa kwa maeneo hayo ni kwenda kinyume na mkabata halali uliopo kati ya pande hizo mbili jambo ambalo linaongeza changamoto ya umbali kwa wasafiri wanaotumia Bandari hizo kuingia na kutoka nchini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kusimamia utekelezaji wa mkataba huu na kuhakikisha kwamba Zanz Medicals inatimiza wajibu wake kwa mujibu wa makubaliano kama

ilivyoainishwa kwenye mkataba husika. Aidha, vituo vya kupima UVIKO 19 vya Mkokotoni na Kizimkazi vianzishwe na kufanya kazi kwa haraka ili kuwafanyia wepesi wa kuchukuwa sampuli na kupimwa wasafiri wanatumia njia ya maji kuingia na kutoka nchini katika maeneo hayo.

8.7.2.6 Ucheleweshwaji wa vyeti vya uthibitisho wa malipo ya kodi ya zuio

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2019 kifungu cha 85(2) kinaeleza kuhusu muda wa kupatiwa cheti cha kodi ya zuio kuwa ni ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi ambamo kodi husika ilizuiwa. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa vyeti vya kodi ya zuio (with holding tax certificate) unaofanywa na Wizara ya Afya dhidi ya Zanz Medicals kinyume na matakwa ya Sheria kwenye kodi iliyozuiwa na Wizara ya Afya katika malipo ya kwanza ambayo Zanz Medicals ilipata kutoka Wizarani.

Kutokutolewa kwa vyeti vya kodi ya zuio kwa wakati kunapelekea Zanz Medicals kukosa ushahidi wa kufanyika kwa malipo ya kodi husika jambo ambalo linaiweka kwenye mazingira magumu ya kimahesabu na uwajibikaji kwa wamiliki na wawekezaji wake. Aidha, hali hii pia inatilia shaka utekelezaji wa malipo ya kodi ya zuio kwa Bodi ya Mapato ambapo inawezekana kwamba Wizara ya Afya haijafanya malipo hayo na ndio maana haijapewa vyeti husika.

Ili kuboresha mazingira ya kufanyia biashara ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha inatimiza mashariti ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 na kanuni zake kwenye kodi ya zuio ili kuwapa Zanz Medicals nafasi ya kufanya uwajibikaji kwa wamiliki na wawekezaji wake pasipo shaka, na kuongeza tija kwa upande wake.

8.7.2.7 Uwepo wa udanganyifu kwenye malipo ya upimaji wa UVIKO 19.

Katika ukaguzi huu uliofanyika kwenye mfumo wa UVIKO 19 imebainika kuwepo kwa udanganyifu wa malipo ya huduma za upimaji unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya PBZ kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya Zanz Medicals. Hali hii imejidhihirisha kwenye baadhi ya stakabadhi za malipo za PBZ zinazoonesha kuwa mteja amelipia kipimo cha UVIKO 19 cha PCR ambacho kimsingi bei yake ni Dola za Marekani 80.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana wakati wa ukaguzi huu zinasema kwamba wengi wa wasafiri wanaokumbwa kwenye tatizo hili ni wageni ambao wanakuwa hawana uelewa mzuri wa mfumo wa benki zetu jambo linalopelekea kushindwa kuhoji kiwango kinachokuwa kimeandikwa kwenye stakabadhi za malipo wanazopewa na benki ya PBZ.

Kielelezo L : kinaonesha malipo ya shilingi za kitanzania Themanini (Tshs.80) na shilingi za kitanzania Eflu Tatu (Tshs. 80 and Tshs. 3,000) kupokelewa na benki ya PBZ kama malipo ya kipimo cha UVIKO 19 cha PCR jambo ambalo ni kinyume na bei zote za vipimo vya UVIKO 19 kama ilivyoielezwa kwenye utangulizi.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyopatikana kupitia mahojiano (interview) na ukaguzi ulifahamishwa kwamba kwa nyakati tofauti wageni hawa walilipia USD 80 lakini stakabadhi za malipo hayo ziliandikwa Tshs. 80 na Tshs. 3,000 na Maafisa wa benki ya PBZ kwa sababu zao binafsi.

Aidha, stakabadhi hizi ilipofikishwa Zanz Medicals ambako ndiko inakopokelewa na kuingizwa

kwenye mfumo kabla ya mteja kupewa huduma Zanz Medicals ilizipokea na kuziingiza kwenye mfumo bila kujali tofauti hiyo kubwa ya malipo iliyokuwa wazi kwenye stakabadhi hizo. Jambo hili limewezekana kufanikiwa kwa ushirikiano wa baadhi ya watumishi wasio waaminifu wa PBZ na Zanz Medicals. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 37: Baadhi ya Miamala ya USD 80 iliyoingizwa kwenye Hesabu ya TZS ya PBZ COVID RESCUE FUND TZS kama TZS 80 na baadhi ya Maafisa wa PBZ na kutumika kutoa huduma kwa wateja kupitia baadhi ya wahudumu wa Zan Medicals.

TRA_DATE	BANK NAME :THE PEOPLE'S BANK OF ZANZIBAR LIMITED BANK ACCOUNT NAME :COVID-19 RESCUE FUND BANK ACCOUNT NUMBER :0748946001 BANK ACCOUNT CURRENCY :TZS NB COLUMN F9. 2= CREDIT, 1= DEBIT EXPLANATION TEXT	VAL_DATE	TRANSACTION SEQUENCE NO.	TRA_AMT	DEB_ CRE_IND
23-01-21	POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:102309887268::01-23 09:21:27	23-01-21	15547	80.00	2
25-01-21	MOHAMEDSADEGH SHAHI	25-01-21	14279	80.00	2
28-01-21	POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:102810336665::01-28 10:18:56	28-01-21	17012	80.00	2
29-01-21	POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:102913228662::01-29 13:13:48	29-01-21	37757	80.00	2
05-02-21	SANE NHAMBURO	05-02-21	4960	80.00	2
06-02-21	POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:103709127607::02-06 09:15:27	06-02-21	10639	80.00	2
08-02-21	dayer catherine	08-02-21	10679	80.00	2
08-02-21	DAYER GERALD	08-02-21	10683	80.00	2
11-02-21	POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:104212352905::02-11 12:22:32	11-02-21	19520	80.00	2
24-03-21	HASSAN ADEN	24-03-21	2451	80.00	2

08-04-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:109714919467::04-07 14:45:19	08-04-21	23321	80.00	2
15-04-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:110509974676::04-15 09:42:54	15-04-21	7915	80.00	2
15-04-21	TIAGO MANUEL	15-04-21	5419	80.00	2
22-04-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:111209693344::04-22 09:24:53	22-04-21	7699	80.00	2
12-05-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:113213225709::05-12 13:10:25	12-05-21	36443	80.00	2
25-05-21	MOHAMMED ISSA	25-05-21	6880	80.00	2
03-06-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:115410993596::06-03 10:23:13	03-06-21	13507	80.00	2
04-06-21	MARIE CHRISTINE GUINARD	04-06-21	1725	80.00	2
05-06-21	BIRHAN T ABRAH	05-06-21	3954	80.00	2
07-06-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:115711422230::06-06 11:17:02	07-06-21	11128	80.00	2
07-06-21	MARY GEORGIA BRUCE-JONES	07-06-21	7133	80.00	2
15-06-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:116608242443::06-15 08:17:22	15-06-21	2244	80.00	2
22-06-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:117309713292::06-22 09:01:53	22-06-21	14274	80.00	2
28-06-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:117908495450::06-28 08:51:35	28-06-21	48586	80.00	2
16-07-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:119714264464::07-16 14:34:24	16-07-21	28607	80.00	2
09-08-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:122010210449::08-08 10:53:30	09-08-21	11054	80.00	2

03-09-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:124614942367::09-03 14:02:22	03-09-21	20420	80.00	2
20-09-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:126209013420::09-19 09:13:33	20-09-21	13189	80.00	2
25-09-21	GREGORY ALLEN	25-09-21	6173	80.00	2
06-10-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:127911830239::10-06 11:10:30	06-10-21	18292	80.00	2
07-10-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:128012509356::10-07 12:38:29	07-10-21	26326	80.00	2
08-10-21	ALI MOHAMED MBARUK	08-10-21	551	80.00	2
11-10-21	TSUYOSHI SHIMAOKA	11-10-21	14833	80.00	2
13-10-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:128613383765::10-13 13:19:43	13-10-21	23494	80.00	2
12-11-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:131609247468::11-12 09:24:07	12-11-21	13511	80.00	2
12-11-21	POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:131612184118::11-12 12:09:44	12-11-21	24325	80.00	2
18-11-21	AKIDAH	18-11-21	3399	80.00	2
21-12-21	PAULA HERRAN BAIGORRA - 41791498R	21-12-21	5784	80.00	2

Hali hii inapelekea kutokea kwa athari mbalimbali kwa Serikali zikiwemo zifuatazo: -

- Kuisababishia hasara Serikali kwa ubadhirifu wa fedha ambazo ilipaswa kuzipata.
- Kuchochea rushwa miongoni mwa jamii katika kupata huduma zinazotolewa na Serikali kupitia mawakala wake.
- Kurudisha nyuma maendeleo ya nchi kwa kuhujumu uchumi wa Taifa na kuendeleza umaskini uliopo ambao Serikali inaweka jitihada za kuupunzua ama kuuondoa kabisa.
- Kukwamisha jitihada za uwekezaji na utegemezi wa TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii kwa kutumia mianya iliyopo kwa manufaa binafsi.

Kwa kuzingatia athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza kufuatia udanganyifu uliobainika kwenye ukaguzi huu tunashauri mambo yafuatayo:

- Vyombo vya ulinzi na usalama vinavyohusika na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ukubwa wa tatizo hili na kuchukuwa hatua stahiki kwa wote waliohusika na udanganyifu huu kwa mujibu wa Sheria.
- Wizara ya Afya kuwaondolea ufikiaji wa mfumo kwenye eneo la kuingiza malipo watu wote wasio watumishi wa Wizara ya Afya Idara ya Uhasibu na kuirejesha kazi hii kwa wahasibu walioko chini ya Wizara ambapo inaweza kulazimu kuwapeleka kwenye vituo mbalimbali wahasibu hao kunakofanywa upimaji wa UVIKO 19 ili kufanyia kazi zao huko katika kurahisisha kazi ya kuwahudumia wasafiri kwa haraka.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Zanz Medicals na Benki ya PBZ kufanya uchunguzi wa kubaini binu zilizotumika na kiwango cha fedha kilichopotea kwa kupitia udanganyifu wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na udanganyifu huu uliobainika kwenye ukaguzi na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia hali hii kujirudia tena siku zijazo.
- Zanz Medicals kufanya uchunguzi kwa baadhi ya wafanyakazi wake wasio waaminifu na mabao wameshiriki kwa namna moja au nyengine kufanikisha udanganyifu huu na kuwachulia hatua za kinidhamu na kisheria ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zote zilizochepushwa.
- Benki ya PBZ kufanya uchunguzi kwa baadhi ya wafanyakazi wake wasio waaminifu na walioshiriki kutenda udanganyifu huu na kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zote zilizochepushwa.

8.7.2.8 Kubadilisha “Key experts” bila ya idhini ya Wizara ya Afya

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Zanz Medicals kipengele cha 30.1 kinachosema isipokuwa Mteja kukubali kwa maandishi, hapatakuwa na mabadiliko ya “Key Experts”, key experts ni wataalamu muhimu katika zoezi la upimaji wa UVIKO 19 ambao wasifu wao uliambatishwa kwenye mkataba baina ya Wizara ya Afya na Zanz Medicals.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba Zanz Medicals ilifanya mabadiliko kwenye baadhi ya key experts wake bila ya kupata idhini ya maandishi ya Wizara ya Afya jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya mkataba. Athari nyengine ni pamoja na kufanya udanganyifu kwa Serikali kwa kuweka wataalamu wenye wasifu mkubwa ili kupata zabuni ambao wanahalalisha bei za juu za watoa huduma lakini inapokuja kwenye utekelezaji wa kazi husika wataalamu hawo hawaletwi kwenye maeneo ya kazi bila sababu za msingi.

Kwa kuwa Zanz Medicals imevunja moja ya mashariti ya mkataba huu Wizara ya Afya inashauriwa kuchukuwa hatua stahiki za kisheria kulingana na uvunjanji uliofanyika ikiwa ni pamoja na kuitaka Zanz Medicals kuandika barua na kujieleza ni kwanini isichukuliwe hatua kwa kisheria kwa kuvunja moja ya vipengele muhimu vya mkataba na mipango yake yake ya kuhakikisha kwamba wataalamu hao wote wanapatikana kazini kama ilivyotarajiwa na vinginevyo kuleta mbadala wa wafanyakazi hao kwa mujibu wa mkataba.

8.7.2.9 Kutokuwepo kwa udhibiti wa watu wanaoingia kwenye kituo cha kupima UVIKO 19 cha Migombani

Ukaguzi umebaini kuwa kwenye kituo cha kupima UVIKO 19 cha Migombani hakuna utaratibu maalum wa kiudhibiti uliowekwa kwenye geti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu naoingia kwenye eneo hili ni wale wanaohusika na upimaji wa UVIKO 19 pekee. Kufuatia hali hii ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya watu wanaoingia kwenye vituo na kuwadanganya wasafiri hususani watalii namna ya kukwepa kulipia fedha halali za vipimo na kuwapa namna nyengine ambazo zinapelekea kutengenezewa vyeti feki. Athari nyengine ni pamoja na kusababisha mkusanyiko mkubwa wa watu kwenye eneo hili na kuongeza hatari za maambukizi ya UVIKO 19 kwa wasafiri.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Zanz Medicals kuweka utaratibu utakao hakikisha kwamba watu wanaoingia ndani ya geti la Maabara ya Migombani ni wale wanaohusika na upimaji wa UVIKO 19 pekee.

8.7.2.10 Dosari kwa upande wa kampuni ya Rahisi Solution

Kwa kuwa Wizara Afya iliingia makubaliano na kampuni ya Rahisi katika utengenezaji wa mfumo unaotumika kusimamia na kuratibu taarifa za UVIKO 19 ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ulifanyika katika kuchambua wajibu, haki na majukumu ya Rahisi Solution kwa kuzingatia sheria, miongozo na sera mbalimbali zilizopo na kubaini dosari zifuatazo:-

8.7.2.11 Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada maafa (Disaster recovery site/ offsite).

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kushindwa kuzipata taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilometa 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa.

Eneo hili linatakiwa kuwa na ukamilifu wote kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umegundua kuwa kampuni ya Rahisi Solution pamoja na Wizara hazina eneo mbadala maalum lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwekwa eneo la kuendeleza utendaji kazi mfumo baada ya matatizo kutokea kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa "Disaster Recovery Site" ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi kutengeneza eneo la kuendeleza mifumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa (best practice).

8.7.2.12 Kukosekana kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan)

Mpango wa kuendeleza mfumo baada ya maafa/ mpango wa kupona maafa (disaster recovery plan) unalenga kuikinga taasisi kuelewa madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mripuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Vile vile, mpango huu una ainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba kampuni ya Rahisi Solution pamoja na Wizara ya Afya hazina Mpango wa kupona maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume "Best Practice Guidelines" ambazo zinasisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution kutengeneza mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na ile ya kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unakuwa wa kujitosheleza katika kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

8.7.2.13 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za mfumo wa UVIKO 19.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa mfumo wa UVIKO 19 hauna nyaraka zozote zinazohusiana na matumizi endelevu ya mfumo ambapo miongoni mwa nyaraka hizo ni kama zifuatazo:-

- System Operations Manual.
- System Architecture Document.
- System Configurations Manual.
- System Requirements Document.
- System Users Acceptance Testing.
- System Setups.

Aidha, imebainika kwamba mfumo huu muhimu katika kusimamia na kuratibu taarifa za UVIKO 19 nchini katika utengenezaji wake haukuzingatia miongozo na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kuanzia hatua ya awali ya utengenezwaji hadi hatua ya mwisho ya ukamilishaji wa mfumo (System Development Life Cycle – SDLC).

Kutokuwepo kwa nyaraka zote zinazohitajika katika utengenezaji, usimamizi, uendeshaji na utaratibu wa mfumo kunaweza kupelekea athari mbalimbali ikiwamo zifuatazo: -

- Mfumo kuwa mali ya mtu/ watu wachache badala ya Taasisi, hii inatokana na ukweli kwamba aliyetengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote ile, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofisini basi mfumo huu hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na kuinyima Taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa katika namna endelevu.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa kama kisiwa kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mingine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo linalorudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- Taasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda, juhudi na jitihada zilizotumika mpaka kuupata mfumo uliokamili, hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.
- Kuendeleza utegemezi kwa mtoa huduma (system supplier) ikiwa mfumo umetengenezwa na mtoa huduma wa nje kwasababu Taasisi inakuwa haina kumbukumbu muhimu ambazo ingeliweza kuzitumia kujenga uwezo wa ndani na kupunguza utegemezi kwa mtoa huduma jambo ambalo linaokoa gharama na kuipunguzia mzigo Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuisimamia kampuni ya Rahisi Solution na kuhakikisha kwamba inapata nyaraka zote muhimu za mfumo kama ilivyo ainishwa hapo juu, pia kuhakikisha kwamba nyaraka hizo zinakidhi vigezo vinavyokubalika.

8.7.2.14 Udhaifu wa udhibiti katika kuusimamia mfumo wa UVIKO 19

Ukaguzi umebaini kuwa usimamizi wa watumiaji wa mfumo na miundombinu yake havina utaratibu rasmi wa kukagua shughuli zinazofanywa na watumiaji wenye haki zote za kwenye mfumo kwa kutumia akaunti za upendeleo (priviledge accounts). Pia, ukaguzi ulibaini udhaifu wa ubatilishwaji kwa haki za watumiaji ambapo hali iliyopelekea uwepo wa wafanyakazi waliokoma utumishi wao kuendelea kuwa na haki za kuingia katika mfumo wa UVIKO 19.

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa udhaifu katika eneo la mgawanyo wa majukumu kwa watumiaji wa mfumo kulingana na majukumu ya mtu husika kwa mujibu wa majukumu ya kazi katika mfumo huo.

Uwepo wa makundi ya watumiaji yasiyokuwa na ulazima kwenye mfumo huu ni miongoni mwa udhaifu uliobainika katika ukaguzi huu ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo katika kukabiliana na udhaifu wa usimamizi wa mfumo huu:-

- Jukumu la usimamizi wa mfumo wa UVIKO 19 lipewe Wizara ya Afya kwa kuzingatia hatua nyengine zote muhimu za makabidhiano ya mfumo huu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba inapewa nyaraka zote muhimu za mfumo na inajengewa uwezo unaostahili kufanya usimamizi huo.
- Kuwaondolea ruhusa watumiaji wengine wote wenye nguvu za super admin ili kuondoa muingiliano wa kazi zinazofanana kwa wakati mmoja.
- Kuhakikisha kuna mgawanyo wa majukumu katika utekelezaji wa kazi za kila siku kwenye mfumo.
- Kubatilisha akaunti zote za waliokuwa watumishi ambao kwa sasa utumishi wao umemaliza.
- Kufanya upitiaji wa mfumo wa mara kwa mara ili kubaini akaunti ambazo hazitumiki kila baada ya kipindi kisichozidi miezi 3 na kuziweka katika hali ya kutotumika (disabled).

Kielelezo M: kinaonesha kuwa mtumiaji bado yupo active hali ya kuwa kwasasa si mtumiaji wa mfumo.

Kielelezo N : kinaonesha uwepo wa Supper Admin zaidi ya mmoja wenye access sawa.

Kielelezo O : Kinaonesha uwepo wa Moh-fedha (muhasibu) katika mfumo ambae hajulikani na yupo active na wapo ambao hawatumii mfumo lakini katika mfumo wapo active, vile vile majina ya akaunti yamejirejea.

8.7.2.15 Mapungufu ya mfumo wa UVIKO 19 kwenye kuingiza taarifa za washukiwa wa UVIKO 19

Ukaguzi umebaini mfumo wa UVIKO 19 haujakidhi haja ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo (user requirements) kwenye eneo la kuingiza taarifa za washukiwa (suspects) ambapo mfumo unaruhusu kuingizwa baadhi ya taarifa zinazohitajika na watumiaji wa mfumo na kuacha sehemu ya taarifa ambazo ni muhimu katika usimamizi na uratibu wa masuala ya Afya nchini.

Kitendo cha mfumo wa UVIKO 19 kushindwa kupokea taarifa zote za washukiwa wa UVIKO 19 kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo (users requirements) kunapelekea mfumo huu usitumike ipasavyo katika kuingiza taarifa hizi na badala yake watumiaji kutafuta njia mbadala ya kutunza kumbukumbu za taarifa hizo ambapo kwa sasa Wizara ya Afya inatumia programu ya simu janja ijulikanayo kama "KoboCollect" jambo ambalo linasababisha taarifa za UVIKO 19 zisipatikane sehemu moja na kuweka ugumu wa kupata tathimini ya haraka ya hali ya UVIKO 19 ili kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati kwa kuwa baadhi ya taarifa ziko kwenye programuya simu janja na baadhi ziko kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kumpatia mtoa huduma mahitaji yake yote ambayo hayakuzingatiwa wakati wa utengenezaji wa mfumo huu ikiwemo mahitaji ya taarifa za washukiwa "suspects" na kumsimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba anakamilisha kazi yake kwa mujibu wa mkataba na Sheria za nchi.

8.7.2.16 Kukatiwa huduma ya mtandao (internet) kwa vituo vinavyoingiza taarifa kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Mtandao (internet) unahitajika kwa ajili ya kuingiza taarifa za upimaji na majibu ya UVIKO 19 kwenye mfumo unaohifadhi na kutoa taarifa hizo. Mfumo huu ulianza kutumika tangu Mwezi Machi 2021, ukaguzi ulibaini kuwa Maabara ya Mnazi Mmoja ilipata mtandao kwa muda wa miezi mitatu pekee yaani, kuanzia mwezi Septemba mpaka Novemba 2021 na kwamba kwa kipindi cha takribani miezi mitano watumiaji wa mfumo walikuwa wanaingiza taarifa kwenye mfumo kwa kutumia "internet" ya simu zao za mkononi wakati kituo cha Lumumba (EOC) kilikuwa hakina huduma hii kwa Zaidi ya mwezi mmoja mpaka tunakamilisha ukaguzi wetu mwezi wa Disemba, 2021 ambapo ili kuingiza taarifa kwenye mtandao na wao pia walilazimika kutumia "internet" za simu zao za mkononi (Mobile Wi-Fi).

Katika kupitia mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi ukaguzi ulibaini kwamba kifungu 3.0 (i) kinaitaka kampuni ya Rahisi kutoa huduma ya mtandao kwenye vituo vyote vinavyoingiza taarifa za UVIKO 19 kwenye mfumo ambapo Rahisi ilikata huduma hiyo baada ya kinachodaiwa kucheleweshewa malipo kwenye huduma zake alizokuwa akizitoa kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kusimamia vyema utekelezaji wa mkataba huu kwa maslahi mapana ya Serikali kwani sababu iliyotolewa za Rahisi ya kucheleweshewa malipo na kupelekea kukata huduma ya mtandao ingeliweza kuepukika kama Wizara ingelikuwa na usimamizi mzuri wa mkataba huu.

8.7.2.17 Udhaifu wa Mfumo katika kuoanisha huduma za upimaji wa UVIKO 19 na malipo yanayotakiwa kwa kila huduma

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo UVIKO 19 hauna uwezo wa kuoanisha vipimo vya UVIKO 19 vilivyopo na bei ya kila kipimo, hali hii inapelekea mazingira ambayo mteja anaweza kulipia kipimo cha bei ndogo na kufanyiwa kipimo cha bei kubwa hususani kama muingiza taarifa za malipo hatakuwa na uadilifu na uzalendo kwa nchi yake kwa kuwa kila kipimo kina bei yake. Kutokana na dosari hizo mfumo unaweza kuisababishia hasara Serikali na kuchochea mazingira ya rushwa kwa watu wanaohusika na kuingiza taarifa za malipo ya vipimo mbalimbali vya UVIKO 19.

Kielelezo P: Kinaonesha kuwa mfumo hauna uwezo wa kuonesha na kulinganisha bei ya huduma.

Kielelezo Q: Kinaonesha mteja amepima kipimo cha RT-PCR (Polymerized Chain Reaction) ambacho ni USD 80 lakini amelipia USD 25 ambacho ni malipo ya kipimo cha "Antigen Rapid Test" bila ya mfumo kutambua.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya Serikali kufanya uchunguzi ili kuweza kubaini ukubwa wa tatizo hili na kujuwa chanzo chake ili kuweza kuchukuwa hatua stahiki.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana ya kampuni ya Rahisi kufanya maboresho husika kwenye mfumo huu ili kuondoa udhaifu huu uliobainika kwa haraka iwezekanavyo.

8.7.2.18 Mfumo kutoruhusu usajili binafsi kwa waliosamehewa

Ukaguzi umebaini kwamba wapimwaji waliosamehewa (exempts) ambao ni pamoja na wanafunzi wanaosoma nje ya nchi, madaktari wanaojitolea nchini, watumishi wa umma, na watu wengine wasiolipia upimaji wa UVIKO 19 hawajawekewa utaratibu wa kufanya usajili binafsi (self registration) kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Hali hii inasababisa ucheleweshwaji wa uingizwaji wa taarifa za watu hawa kwa kua inalazimu muingiza taarifa (data entry) kuchukua taarifa za mpimwaji zilizojazwa kwenye fomu maalumu na mtabibu ili kuweza kuziingiza kwenye mfumo, pia taarifa kama vile umri, jinsia, makazi n.k zinaweza kuingizwa kwenye mfumo bila kuzingatia usahihi wake na kupoteza maana ya matumizi ya mfumo.

Ukaguzi unashauri kufanyike marekebisho kwenye mfumo huu ili wapimwaji wote walio samehewa wawekewe utaratibu maalum ili kuweza kufanya usajili binafsi (self registration) kwenye mfumo wa UVIKO 19 hii itasaidia kuingiza taarifa zilizo sahihi na kuondoa ucheleweshwaji wa kuingizwa taarifa zao kwenye mfumo kunakopelekea kucheleweshewa huduma.

8.7.2.19 Kutokutumika na 'Portal' ya usajili binafsi kwa ajili ya Chanjo za UVIKO 19.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa "Portal" maalumu iliyotengenezwa sambamba na moduli ya chanjo za UVIKO 19 yenye uwezo wa kuwaruhusu wanaotaka kuchanjwa kuingiza taarifa zao wenyewe (self registration) kabla ya kufika kwenye kituo kupata chanjo na kuomba nafasi (booking).

Hata hivyo ukaguzi umebaini "portal" hii haijawahi kutumika tangu kutengenezwa kwake.

Moja ya athari za kutotumika kwa portal hii ni pamoja na kucheleweshwa kwa upatikanaji wa vyeti vya chanjo kwa wakati kwa kua inachukua muda mwingi kuingiza taarifa za wachanjwaji kwenye mfumo na zikiingizwa mara kadhaa zinakua sio sahihi kama inavyotarajiwa.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa chanjo za UVIKO 19 itoe elimu kwa wananchi na kuwahamasisha juu ya uwepo na matumizi ya "Portal" hii na namna ya kuitumia pamoja na mufaa yake ili ianze kutumika na kupunguza ugumu wa kazi za uingizwaji wa taarifa kama ilivyo sasa na tija kwenye taarifa zinazo kusanywa.

8.7.2.20 Udhaifu wa mfumo katika kuingiza tarehe za kufanya chanjo ya pili (Second Dose).

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kwamba Moduli ya chanjo ina udhaifu kwenye kuingiza tarehe ya chanjo ya pili wakati mchanjwaji amekwisha chanjwa ambapo mfumo unarudisha nyuma tarehe kwa siku moja. Kwa mfano, mtu amechanjwa tarehe 21/01/2022 ukiingiza kwenye mfumo tarehe hii unakupeleka tarehe 20/01/2022.

Hali hii inawalazimu waingiza taarifa za chanjo kwenye mfumo wawe wanaweka tarehe ya siku moja mbele ili kupata tarehe sahihi ya chanjo kwenye kumbukumbu za mchanjwaji.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara kuisimamia kampuni ya Rahisi Solution katika kutatua changamoto hii ya mfumo mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu kwa waingiza taarifa na hatari ya kukosea kuingiza tarehe.

8.8 UKAGUZI WA MFUMO WA MALARIA (MEEDS)

8.8.1 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO MALARIA

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Malaria unaosimamiwa na Programu ya Kudhibiti Malaria ya Zanzibar (Zanzibar Malaria Control Program) mambo mbali mbali yalibainika ikiwemo dosari zifuatazo:-

8.8.1.1 Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery site/offsite).

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kushindwa kuzipata taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilometa 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa.

Eneo hili linatakiwa kuwa na ukamilifu wote kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa kampuni ya "Zanzibar Malaria Control Program (ZMCP) au Zanzibar Malaria Elimination Program (ZAMEP)" wala Wizara hazina eneo mbadala maalumu lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwekwa eneo la kuendeleza utendaji kazi mfumo baada ya matatizo kutokea kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kutengeneza eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa (best practice) kwa uharaka wa kutosha ili kuilinda taarifa mali (information asset) za Serikali ambazo kimsingi zimeigharimu Serikali fedha, muda na nguvu katika kuzikusanya, kuzichakata na kuzihifadhi.

8.8.1.2 Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan).

Kwa mujibu wa Sera za eGaz kifungu cha 4.4.1.2.(d) inazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na miundo mbinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yatakayojitokeza dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo zote yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundo mbinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara kupitia ZAMEP haina kabisa mpango huo unaotarajiwa kutoa muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo

kupotea na kuonesha nini kifanywe baada ya majanga. Vile vile ukaguzi umebaini kuwa mpaka sasa taarifa za mfumo huu wa Malaria hazijulikani zitakuwa wapi baada ya kumalizika mkataba baina na ZAMEP na mtoa huduma licha ya kuwa taarifa hizo zilitakiwa kuendelea kupatikana kwa mujibu wa Sheria za nchi.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa zote zilizowekwa ndani ya mfumo kwa kutokufuatwa taratibu sahihi za kupambana na majanga hayo kabla na baada ya hayo kutokea.

8.8.1.3 Kukosekana kwa mpango wa uhamishaji wa taarifa (Data Migration Plan)

Uhamishaji wa Taarifa ni mchakato wa unaohakikisha kwamba taarifa zote zinazohitajika kwa kuzingatia "format" ya taarifa zinahamishwa kutoka kwenye kanzidata moja kwenda nyengine ambayo itaruhusu taarifa husika kutumika kwa mujibu wa matarajio ya watumiaji. Vitu vya kuzingatia kwenye zoezi la kuhamisha data ni pamoja na "data conversion" pale inapobidi ambayo inachangiwa na tofauti kwenye "field formats or sizes", miundo ya faili/kanzi data na "coding schemes".

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa ZAMEP pamoja na Wizara ya Afya hakuna mpango wa kufanya uhamishaji wa taarifa za Malaria zilizomo kwenye mfumo wa Malaria ambao unatarajiwa kukoma kutumika ndani ya kipindi cha miezi michache kuanzia sasa.

Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa taarifa zote muhimu wakati wa zoezi la kuhamisha taarifa kutoka kwenye mfumo wa awali kuja kwenye mfumo mpya, pia inaweza pelekea zoezi la kuhamisha taarifa kuonekana kuwa gumu na lisilo na tija kwa Serikali kwa sababu ya kukosekana kwa mpango sahihi.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na ZAMEP kuandaa mpango huu kabla ya kuanza zoezi la kuhamisha taarifa husika na kuutumia mpango huo wakati wa kutekeleza uhamishaji wa data hizo.

8.8.2 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo ya Wizara ya Afya, Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Aidha, Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Wiza ya Afya, Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na wadau wake kama vile kampuni za Zanz Medicals na Rahisi kwa ushirikiano mzuri walivyotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi wetu ujao.

SURA YA TISA

UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI WA VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI

9.0 UTANGULIZI

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ni matokeo ya muunguniko wa iliyokuwa Ofisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali na iliyokuwa Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari, hii ni kwa mujibu wa Sheria uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa matukio ya Kijamii nambari 3 ya mwaka 2018 ambayo iliunda Wakala huu tarehe 02 Januari, 2018.

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar inafanya kazi zake chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku, Wakala inawahudumia wateja wake kupitia Vituo vya Usajili wa Matukio ya Kijamii vilivyopo katika wilaya kumi na moja (11) za Unguja na Pemba ambapo Makao Makuu ya Wakala ipo Migombani na ofisi zake nyengine zipo Mazizini Unguja Jengo la Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora.

Wakala inaongozwa na Bodi ya Ushauri ambapo imejumuisha wajumbe mbali mbali waliotajwa katika kifungu nambari 5 cha Sheria ya Usajili wa Matukio ya mwaka 2018. Mkurugenzi Mtendaji ndio Afisa Masuuli wa wakala anayeshughulika na kazi za kiutawala kwa kushirikiana na wakurugenzi wa idara mbali mbali zilizopo chini yake.

9.1 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzianavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nambari 11 ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapoomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

9.2 MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho lakuridhishakwamba Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii una ulinzi na udhibiti kwenye miundombinu inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake nakuhakikisha kuwa zina uadilifu na vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi kupitia TEHAMA. Aidha, ukaguzi huu pia ulikuwa na malengo maalumu kama yalivyoainishwa hapa chini:-

- a) Kubainisha ufuatishwaji wa sheria, kanuni, sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa.
- b) Kufanya tathiminiya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.
- c) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.
- d) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- e) Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.
- f) Kubainisha kama Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ina Mpango wa Mwendelezo wa Biashara pamoja na Mpango wa Kukabiliana na Maafa.

9.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya ndani na ya kimataifa kama vile eGaz, COBIT, e-Government URT, AFROSAI n.k. Katika kukagua mifumo ya Wakala nilitumia mbinu mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:-

- a) Kupitia Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo mbali mbali inayohusiana na usajili wa matukio ya kijamii pamoja na usajili wa Mzanzibari.
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kupitia mfumo wa udhibiti wa ndani katika usajili wa matukio ya kijamii.
- c) Kupitia sera za usimamizi pamoja na miongozo ya uongozaji wa teknolojia ya TEHAMA inayotumika kwa wakala.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika ununuzi, uwekaji na uondoshaji wa mali zinazohusiana na teknolojia ya TEHAMA.
- e) Kupitia mifumo ya TEHAMA ili kutazama udhibiti wa ndani uliyopo katika mifumo hiyo.
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti yaliyomo katika mifumo ya TEHAMA.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizotokana na mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano pamoja na watumiaji mbali mbali juu ya mifumo inayotumika na Wakala.
- i) Kutembelea katika vituo mbali mbali vilivyoundwa mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii pamoja na mfumo wa usajili wa Mzanzibari.
- j) Kutembelea vituo vyenye miundombinu ya mitandao ya mifumo ya Wakala pamoja na vituo vya kutunza taarifaza mifumo hiyo.

- k) Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi na kumaliza kazi za ukaguzi na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi, na
- l) Kutembelea ofisi za Wilaya zilizo chini ya Wakala wa Matukio ya Kijamiikwa lengo la kuangalia ufanyaji kazi wa ofisi hizo.


9.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA USAJILI WA VITAMBULISHO VYA MZANZIBARI MKAAZI

Baada ya kuupitia Mfumo wa Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (Zan ID Registration System) ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali kama ifuatavyo:-Kukosekana kwa nyaraka muhimu za usanidi wa mfumo (system configurations manual), kutokuwepo kwa nyaraka za utendaji kazi wa mfumo (system operations manual), kutokuwepo kwa nyaraka za mahitaji ya mfumo, kukosekana kwa mkataba wa utekelezaji wa mfumo, mfumo kutokutunza kumbukumbu za matukio yote yanayotokea kwenye mfumo kwa ajili ya ukaguzi (audit trails/ logs).

9.4.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

9.4.1.1 Mapungufu ya udhibiti wa uthibitishaji wa data zinapoingizwa

Ukaguzi umebaini mapungufu ya udhibiti katika uthibitishaji wa data kwenye Mfumo wa Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari ambapo mfumo unashindwa kugundua na kuzuia tarehe za siku ambazo hazijafika (future date) kwenye kipengele cha kujaza tarehe ya maombi ya kitambulisho cha Mzanzibari kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



Kushindwa kugundua na kuzuia tarehe za siku ambazo hazijafika (future date) kwenye kipengele cha kujaza tarehe ya maombi ya kitambulisho cha Mzanzibari hali hiyo inapelekea mfumo kupokea data zenye makosa na hatimae kuzalisha taarifa zisizo na usahihi ambapo kufanya hivyo ni kwenda

kinyume na kifungu nambari 4(1) cha Sheria Nambari 3 ya mwaka 2018 ambapo inaitaka Wakala kuhakikisha taarifa zinabakia kwenye usawa na usahihi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kufanya maboresho ya Mfumo wa Usajili Vitambulisho vya Mzanzibari kwa kuweka udhibiti wa kuthibitisha data zinazolingizwa kwenye mfumo huo ili kuepusha kuzalisha taarifa zisizo sahihi.

9.4.1.2 Mapungufu yaliyobainika katika moduli ya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari kwa njia ya mtandao (Online Registration)

Moduli ya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari kwa njia ya mtandao (online registration) ambapo kwa sasa ipo katika majaribio (pilot phase) inatoa fursa kwa Mzanzibari aliyetimiza vigezo na masharti kuweza kujaza taarifa zake katika fomu ya usajili kwa njia ya mtandao kupitia kompyuta au simu yake bila ya kuenda kwenye kituo cha usajili wa matukio ya kijamii. Baada ya kupitia moduli hiyo, ukaguzi umebaini kuwepo kwa mapungufu mbali mbali kama ifuatavyo:-


a) Kutokuwepo kwa udhibiti wa kubaini taarifa za muombaji kwenye kanzidata ya mfumo wa ZanID

Ukaguzi umebaini kwamba, mfumo unashindwa kubaini uwepo wa taarifa za muombaji kwenye kanzidata ili kutambua na kuepusha kujirudia kwa taarifa za muombaji. Hali hiyo imebainika baaya ya kufanya majaribio ya maombi kwa kutumia taarifa za muombaji ambaye tayari ameshasajiliwa na mfumo umeweza kupokea maombi hayo yenye kumbukumbu nambari MBBBM-CACAB-RCB kama inavyobainika katika picha hapo chini.




b) Kujirudia kwa taarifa zinazotakiwa kujazwa katika fomu ya usajili

Ukaguzi umebaini kujirudia kwa baadhi ya taarifa zinazotakiwa kujazwa katika fomu ya maombi ya usajili wa vitambulisho cha Mzanzibari kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



c) Kutokuwepo kwa udhibiti wa kuthibitisha data zinazolingizwa

Baada ya kufanya majaribio ya kuingiza data kwenye fomu iliyopo mtandaoni, ukaguzi umebaini kwa baadhi ya vipengele havijaekewa udhibiti wa kuthibitisha uhalali wa data zinazolingizwa. Kufanya hivyo kunapelekea mfumo kupokea data zenye makosa na hatimae mfumo kutoa taarifa zisizokuwa na usahihi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-



Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanafanya maboresho katika moduli ya maombi ya vitambulisho kwa njia ya mtandao ili kurekebisha dosari zote zilibainishwa na ukaguzi kabla haijaanza kutumika rasmi moduli hiyo.

9.4.1.2 Kutokuwepo kwa makubaliano ya ushirikiano katika kuunganisha mifumo ya Wakala na taasisi nyengine

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inafanya mashirikiano na taasisi mbali mbali katika kutoa taarifa za utambulisho wa mwanzibari mkaazi pamoja na taarifa au takwimu zinazohusiana na matukio ya kijamii.

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa makubaliano ya ushirikiano (MoU) kwa taasisi ambazo zimeunganishwa na mfumo wa Usajili wa Vitambulisho vya Mwanzibari, hali hiyo inahatarisha usiri na usalama wa taarifa binafsi za wananchi waliosajiliwa katika mifumo ya Wakala.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala, kuzingatia taratibu bora zinazokubalika kwa kuweka makubaliano ya ushirikiano kwa kila taasisi inayopewa fursa ya kupata taarifa za mifumo, ambayo yatafafanua kiwango cha matumizi ya taarifa hizo pamoja na mipaka yake ili kuweka misingi ya uthibiti wa matumizi sahihi ya taarifa binafsi za watupamoja na kufanya tathmini ya huduma

hii kuwa ni miongoni mwa chanzo cha kukusanyia mapato kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 14(d) cha sheria nambari 3 ya mwaka 2018.

9.4.2 Mapungufu yaliyobainika katika Udhhibiti wa Tehama

Baada ya kupitia Udhhibiti wa TEHAMA kwa Ujumla ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali kama ifuatavyo:-

9.4.2.1 Kutokuwepo kwa nyaraka za usimamizi wa TEHAMA

Nyaraka za usimamizi wa rasilimali za TEHAMA ni nyenzo muhimu sana kwa taasisi inayofanya kazi zake kwa kutegemea teknolojia ya TEHAMA, nyaraka hizo hutoa miongozo bora ya kutumia na kuendeleza rasilimali za TEHAMA. Miongoni mwa nyaraka hizo ni kama vile Sera ya TEHAMA, Mpango mkakati wa TEHAMA pamoja na Muongozo wa Kamati ya Usimamizi wa TEHAMA (Steering committee charter).

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala haina nyaraka za usimamizi wa TEHAMA (ICT Policy), kufanya hivyo ni kwenda kinyume nakifungu nambari 4(2) cha sheria nambari 3 ya uanzishwaji wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii ambapo imewataka Wakala kufuata uzoefu na taratibu zinazokubalika katika kutekeleza kazi zake.

Kutokuwepo kwa nyaraka za usimamizi wa TEHAMA kunaweza kupelekea wakala kushindwa kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali za TEHAMA na hivyo mifumo kushindwa kuongeza tija na ufanisi katika kutekeleza kazi za wakala kwa mujibu wa malengo na mikakati waliojiwekea.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha unajenga misingi imara ya matumizi ya rasilimali za TEHAMA kwa kuweka miongozo katika nyaraka mbali mbali ili kuenda sambamba na miongozo, pamoja na taratibu zilizokubalika za usimamizi bora wa TEHAMA kama ilivyoainishwa katika kifungu nambari 4(2) cha sheria nambari 3 ya uanzishwaji wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar ya mwaka 2018.

9.4.2.2 Kutokuwepo kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara (BCP) na Mpango wa kukabiliana na Majanga (DRP)

Mpango wa muendelezo wa biashara unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kubakia katika hali ya kutoa huduma kwa kutumia mifumo ya TEHAMA bila ya kusita ili kuenda sambamba na malengo pamoja na mikakati iliyojiwekea. Aidha, Mpango wa kukabiliana na Majanga unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinuya utoaji wa huduma. Aidha taratibu zilizobora na zinazokubalika zinataka kila taasisi kuwa na Mpango wa kuendeleza biashara pamoja na Mpango wa kukabiliana na majanga.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala haina Mpango wa muendelezo wa biashara pamoja na Mpango wa kukabiliana na maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4(2) cha sheria nambari 3 ya uanzishwaji wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii ambapo imewata Wakala kufuata uzoefu na taratibu zinazokubalika katika katika kutekeleza kazi zake.

Kutokuwepo kwa Mpango wa muendelezo wa biashara pamoja na Mpango wa kukabiliana na majanga kunaweza kupelekea Wakala kushindwa kurejesha huduma ilizilizokuwa ikitoa kwa wakati mara baada ya kutokezea majanga katika miundombinu ya utoaji huduma zake.

Ukaguzi unashauri kwa Wakala kuhakikisha inatengeneza na kuweka Mipango hiyoili kuenda sambamba na taratibu zilizobora kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 4(2) cha sheria nambari 3 ya uanzishwaji wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar ya mwaka 2018.

9.4.2.3 Kutokuwepo kwa makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA)

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inapokea huduma mbali mbali za TEHAMA kutoka kwa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) ikiwemo kuwapatia chumba cha kuweka sava zao, kusimika (hosting) tovuti na mifumo yao, kuwapati huduma ya intaneti kwa njia ya mkonga pamoja na huduma ya ulinzi wa miundombinu yao, vile vile Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inatumia chumba kilichopo katika jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Tawi la Makunduchi kama ni kituo mbadala cha kuhifadhi data (secondary site).

Ukaguzi umebaini kwamba hakuna makubaliano ya kiwango cha huduma baina ya pande hizo mbili ambayo yatatoa ufafanuzi wa majukumu ya kila upande na kuelezea matarajio ya kiwango cha huduma itakayotolewa. Kutokuwepo kwa makubaliano ya kiwango cha huduma kunapelekea upande mmoja kushindwa kuwajibika endapo itatokea dosari wakati wa utowaji wa huduma hizo.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wakala kuzingatia taratibu bora zinazokubalika kwa kuhakikisha wanaingia katika makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) na wadau wote wanaotoa huduma za kusaidia mifumo ya TEHAMA ili kuweka misingi imara ya uwajibikaji endapo kutatokea dosari katika utowaji wa huduma hizo na kuathiri shughuli zinazotegemea mifumo ya TEHAMA.

9.4.2.4 Taarifa zilizokosekana kwa ukaguzi

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika taarifa mbali mbali ziliombwa kwa ajili ya matumizi ya kazi za ukaguzi hazikuweza kupatikana ambapo taarifa hizo ikiwa kama ni vielelezo vitakavyotumika katika kujiridhisha juu ya uwepo wa hoja zitazobainika, lakini pia taarifa hizo zingeweza kutumika kama ni nyenzo za kufanikisha kazi za ukaguzi. Miongoni mwa taarifa hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 38: Orodha ya taarifa zilizoombwa na kukosekana kwa ukaguzi

Namba	Taarifa Iliyoombwa	Siku Iliyoombwa	Hali Halisi	Athari ya Kukosekana kwa Taarifa hiyo katika kazi za ukaguzi
1.	Hati ya Sera au Miongozo ya Usimamizi wa TEHAMA	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kubaini miongozo inayozingatiwa katika kuendesha na kusimamia rasili za TEHAMA ili ziweze kuongeza tija na ufanisi wa kazi za Wakala.
2.	Hati ya Mpango Mkakati wa TEHAMA	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kubainisha kwamba mipango ya Idara ya TEHAMA inakwenda sambamba na mipango mikuu ya Wakala ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Namba	Taarifa Iliyoombwa	Siku Iliyoombwa	Hali Halisi	Athari ya Kukosekana kwa Taarifa hiyo katika kazi za ukaguzi
3.	Hati ya Kamati ya Uongozi wa TEHAMA	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uwepo wa Kamati ya Uongozi wa TEHAMA, ambayo ina jukumu la kusimamia rasilimali na shughuli zote zinazoendeshwa na Idara ya TEHAMA.
4.	Ripoti ya Usimamizi wa Vihatarishi vitokanavyoo na mifumo ya TEHAMA	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kufanya uchambuzi wa kina juu ya uthibiti wa vitaharishi vitokanavyo na mifumo ya TEHAMA, hali hiyo imepelekea kushindwa kuvifikia viharishi vyote katika ukaguzi wetu.
5.	Hati ambatanishi za Mifumo ya TEHAMA	29/11/2021	Hazipo	Ukaguzi umeshindwa kufanya uchambuzi wa mahitajio ya mfumo uliotekezwa, ukaguzi umeshindwa kupata miongozo ya utumiaji ili kupima matarajio yatoakanayo na matumizi ya mifumo hiyo kama yameakisi mahitajio ya watumiaji.
6.	Daftari la Mali za Kudumu za TEHAMA	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kubaini rasilimali zote za TEHAMA zilizopo na kutambua gharama zake ili kupima uwekezaji uliofanywa kama unakwenda sambamba na malengo ya taasisi.
7.	Mkataba wa Utekelezaji wa Mfumo wa ZanID	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kupitia mkataba wa utekelezaji wa Mfumo wa ZanID ili kujiridhisha uwepo wa mzabuni anaendelea kutoa huduma za msaada katika mfumo huo.
8.	Makubaliano ya Kiwango cha Huduma kwa Huduma zote za TEHAMA zinazotolewa na wadau wa nje	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kubaini usahihi wa cha huduma zote zinazotolewa na wadau wa nje ili kupima tija itokanayo na utuoaji wa huduma hizo.
9.	Daftari la kumbukumbu za hitilafu za mifumo	29/11/2021	Haipo	Ukaguzi umeshindwa kubaini aina za hitilamu zinazojitokeza kwenye mifumo ya TEHAMA ili kupima athari zake juu ya mwendelezo wa kazi za Wakala.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa wakala kuhakikisha nyaraka zilizohitajika kwa ukaguzi zinapatikana kwa wakati stahiki. Aidha, ukaguzi unashauri uongozi wa wakalakuchukuwa juhudi za makusudikatika kuandaa nyaraka zote ambazo hazipo ili kuweza kuenda sambamba na mahitajio ya ukaguzi pamoja na kuwa na nyenzo za kutoa miongozo katika kufanikisha kazi za wakala.

9.4.3 HITIMISHO

Kufuatia hitimisho la ukaguzi uliofanyika tarehe 10 Februari 2022 kupitia kikao cha kumaliza kazi za ukaguzi pamoja na mambo mengine Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kwa mwaka unaofuata kuona mabadiliko chanya katika Mifumo ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa kuzingatia dosari zilizobainika, athari pamoja na ushauri uliotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi.

Aidha, Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani kwa uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa kurejesha ushirikiano uliopelekea kufanikisha kazi ya ukaguzi na matarajio yetu kwamba ushirikiano huo utaboreshwa zaidikatika ukaguzi ujao.

SURA YA KUMI

UKAGUZI WA MFUMO WA MALIPO YA PENSHENI JAMII KWA WAZEE WALIOTIMIZA UMRI WA MIAKA SABINI (70) NA KUENDELEA

10.0 UTANGULIZI

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar inasimamia na kuratibu masuala yote yanayohusiana na Afya ndani ya Zanzibar, Wizara hii ilianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Katiba ya Zanzibar 1984. Wizara inatekeleza majukumu yake kupitia Idara zake mbalimbali ambapo Idara ya Pensheni Jamii ndiyo yenye jukumu kuu la kusimamia na kuratibu Pensheni Jamii kwa Wazee Zanzibar.

Idara hii iliunganishwa kwenye Wizara ya Afya kutoka Wizara Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto mnamo mwaka 2020 ambapo tangu kipindi hicho utekelezaji Sera na Programu za Pensheni Jamii umekuwa chini ya Wizara ya Afya Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

10.1 CHIMBUKO LA PENSHENI JAMII

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwezi Machi, 2015 iliamua kutekeleza tamko la sera ya Hifadhi ya Jamii katika kuwahudumia Wazee kwa kuanzisha rasmi Mpango wa Pensheni Jamii kwa Wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea ambapo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto ndiyo iliyopewa jukumu la kufanya matayarisho yote yaliyohitajika ili kuiwezesha programu ya Pensheni Jamii iweze kufanyakazi kwa ufanisi. Mpango wa Pensheni jamii ulizinduliwa rasmi tarehe 15 Aprili 2016 ukiwa na lengo la kuimarisha kipato cha Wazee kwa lengo la kupunguza ukali wa maisha unaowakabili.

Maamuzi ya Ulipwaji wa Pensheni Jamii yalifikiwa kutokana na kupitishwa kwa Sera ya Hifadhi ya Jamii ambayo imebeba mkakati mzima "Kushajiisha uanzishwaji wa pensheni kwa wote ili kupunguza idadi ya wazee wanaoishi katika umasikini uliokithiri, kutegemea na uwezo wa kifedha". Uanzishwaji wa malipo ya mafao ya uzeeni yanayoendelea kulipwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yanatokana na dhana njema ya kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1984.

10.2 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PENSHENI JAMII KISHERIA

Kifungu nambari 32 cha Sheria ya Wazee nambari 2 ya mwaka 2020 kimetoa fursa ya kuanzishwa kwa Mpango wa Pensheni Jamii ambapo utekelezaji wake ulipaswa kuratibiwa na Wizara inayohusiana na masuala ya Wazee ambapo kwa sasa Wizara hii inaitwa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto. Aidha, Kifungu nambari 33 cha Sheria hii kinaeleza kuhusu kiwango kitakachotolewa kila mwezi ambapo kwa sasa ni shilingi 20,000 kwa kila mzee kwa mwezi kama Pensheni Jamii.

10.3 MAOMBI NA SIFA ZA Kuingizwa Katika Pensheni Jamii

Kifungu cha 33(1) cha sheria ya Wazee kinaeleza kwamba "Mzee ataomba katika Wizara kupitia Sheha wake na Mkuu wa Wilaya kuingizwa katika mpango wa Pensheni Jamii". Hata hivyo kifungu

cha 33 (2) kinaeleza kuhusu sifa za Mzee ili kuruhusiwa kuingizwa katika Mpango wa Pensheni Jamii, ambapo vitu vitatu vimeangaziwa:-

- Umri wa miaka 70 au zaidi,
- Mzanzibari, na
- Amekuwa mkaazi wa Zanzibar kwa zaidi ya miaka kumi mfululizo.

Aidha, kifungu cha 33(2) cha sheria ya Wazee kinaeleza kwamba "Maombi yanayofanywa chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hichi yataambatana na mambo yafuatayo":-

- Picha mbili za karibuni,
- Cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo ya kuzaliwa,
- Kitambulisho cha Mzanzibar mkaazi.

10.4 KUSITISHWA AU KUONDOLEWA KATIKA MPANGO WA PENSHENI JAMII

Kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Wazee nambari 2 ya mwaka 2020 kimebainisha kwamba "Mpokeaji pensheni atasita au kuondolewa kupokea pensheni ya mwezi ikitokea moja kati ya mambo yafuatayo":-

- Kifo
- Hadaa
- Udanganyifu

10.5 MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA

Kutokana na maendeleo na ukuwaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Wizara ya Afya kwa kiwango kikubwa inafanya shughuli zake mbalimbali kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ikiwa ni pamoja na ulipaji wa wa Pensheni za Wazee. Kwa sasa Idara ya Pensheni Jamii inatumia mifumo miwili ya Kielektroniki kwa ajili ya kusajili na kuwalipa Wazee. Mfumo wa kwanza ni MS Access Database System Wazee na wa pili ni Zanzibar Universal Pension Scheme Management Information System (ZUPS MIS).

10.5.1 MS Access Database System Wazee

Mfumo wa MS Access Database System Wazee ulitengenezwa na mtaalamu wa ndani mwaka 2016, mfumo huu unafanya kazi kupitia mtandao wa ndani (LAN) na taarifa za usajili na Pensheni zinahifadhiwa kwenye moja ya komputa zilizopo Idarani inayotumika kama Seva. Katika utengenezwaji wake mfumo ulikuwa na malengo ya kuchukuwa na kutunza kumbu kumbu za usajili na ulipaji wa Pensheni za Wazee.

Kufuatia ongezeko la wazee wa Pensheni Jamii na ukubwa wa Malipo yanayofanyika pamoja na hitaji la kuwasiliana (interoperability) baina ya mifumo ya kielektroniki mfumo wa MS Wazee ulionekana kutokidhi mahitaji na kupelekea Wizara ya Kazi kutangaza zabuni ya kutengenezwa mfumo mpya, zabuni hiyo ilipelekea kupatikana kwa mfumo wa Zanzibar Universal Pension Scheme Management

Information System (ZUPS MIS). Hata hivyo ukaguzi haukuweza kujua thamani halisi ya fedha iliyotumika kutengenezea mfumo wa MS Access Database System Wazee.

10.5.2 Zanzibar Universal Pension Scheme Management Information System

Mfumo wa Zanzibar Universal Pension Scheme Management Information System ni mfumo unaosimamia na kuratibu usajili na malipo Pensheni Jamii, mfumo huu uliotengenezwa na kampuni ya Ms. Web Technologies Tanzania Ltd iliyopo Dar es Salaam kupitia zabuni yenye kumbukumbu namba MLEEYWCH/PMU/RFP/01/2017/2018 kwa mujibu wa mkataba wa tarehe 18 Julai 2018 baina ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto na kampuni ya Ms. Web Technologies Tanzania Ltd kwa gharama ya shilingi 104,902,000 ambapo lengo kuu la mfumo huu lilikuwa ni kuhifadhi taarifa binafsi za Wazee pamoja na malipo yao kwa Wazee walio na umri wa miaka 70 na kuendelea.

Aidha mfumo wa ZUPS unapatikana kupitia miundombinu ya ZICTIA na unafanya kazi katika mazingira ya Mtandao (Web based) ambao umeunganishwa na vifaa vya "Point of Sales" vyenye lengo la kurahisisha zoezi la ulipaji wa fedha kwa wazee. "POS" zimeunganishwa na mfumo wa alama za vidole (finger prints system) kwa lengo la kupata taarifa sahihi za wazee pamoja na kutoa stakabadhi za Malipo.

10.6 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi anavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nambari 11 ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

10.7 MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho la kuridhisha kwamba Wizara ya Afya ina ulinzi na udhibiti kwenye miundombinu inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zina uadilifu na kwamba vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi kupitia TEHAMA.

Malengo mengine ya ukaguzi huu wa mifumo ya TEHAMA ya Wizara ya Afya ni kama yalivyo ainishwa hapa chini:-

- a) Kubainisha ufuatishwaji wa sheria, kanuni, sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa.
- b) Kufanya tathimini ya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.

- c) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.
- d) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- e) Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.
- f) Kubainisha kama Wizara ya Afya ina mipango stahiki katika usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA.

10.8 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya kitaifa na ya kimataifa kama vile eGaz, eGA, ISACA, COBIT, AFROSAI-E n.k.

Katika kukagua mifumo ya Pensheni Jamii ukaguzi ulitumia njia mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini.

- a) Kupitia sheria, kanuni, sera na miongozo mbalimbali inayohusiana Malipo ya Pensheni kwa wazee kupitia mpango wa Pensheni Jamii.
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kuupitia mfumo wa ZUPS MIS na ule wa MS Wazee.
- c) Kupitia sera na miongozo ya usimamizi, wendeshaji matumizi ya TEHAMA inayotumiwa na Wizara ya Afya.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika upatikanaji wa mifumo pamoja na vifaa vinavyotumika katika zoezi la ulipaji wa Pensheni Jamii.
- e) Kupatiwa uelewa wa awali wa utendaji kazi wa mifumo ya ZUPS MIS na MS Wazee ili kuelewa utendaji kazi wa mifumo husika.
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti yaliyomo katika mifumo ya TEHAMA.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano na watumiaji wa Mifumo ya Pensheni Jamii.
- i) Kutembelea vituo mbali mbali vya Unguja na Pemba wakati wa zoezi la malipo ya wazee ili kujionea mwenendo wa malipo ya wazee na kubaini changamoto za Mifumo hiyo.
- j) Kutembelea kituo cha ZICTIA ambacho kimehifadhi taarifa za mfumo wa ZUPS MIS kwa niaba ya Wizara ya Afya.
- k) Kufanya kikao cha kuanza na kumaliza kazi za ukaguzi pamoja na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi.

10.9 MUHTASARI WA HOJA ZA UKAGUZI

10.9.1 Mfumo wa MS Access Database System

Kukosekana kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kutengeneza mfumo wa MS Access Wazee, kutozingatiwa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika kutengeneza mfumo "Systems Development Life Cycle", mfumo kutokuhifadhiwa kwenye chumba maalumu cha Seva, kuendelea kutumika kwa mfumo wa Microsoft Access Database Wazee, kukosekana kwa udhibiti wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo, uwepo wa nakala za taarifa (duplicate data), udhaifu wa udhibiti kwenye kompyuta zinazotumika kuufikia mfumo (computer access control).

10.9.2 Mfumo wa ZUPS MIS

Kutotumika kwa mfumo wa ZUPS MIS kufanya malipo kielektroniki, kukosekana kwa udhibiti wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo, uwepo wa nakala za data (duplicate data), usajili wa taarifa za Wazee kutofanyika kwenye Seva moja kwa moja kupitia mtandao, kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mfumo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya mfumo wa ZUPS MIS, Wizara kutokutumia Mkonga/ Mtandao wa Serikali kwenye Mifumo yake, mfumo kuruhusu usajili wa baadhi ya Wazee wasiokidhi matakwa ya Kisheria, kutozingatiwa mgawanyo wa majukumu kwenye mfumo (Segregation of Duties), kukosekana kwa ripoti mbalimbali za taarifa za Wazee kwenye Mfumo, kukosekana kwa mawasiliano baina ya taarifa za Unguja na zile za Pemba ndani ya mfumo wa ZUPS MIS, udhaifu wa usimamizi wa mfumo, kutozingatiwa kwa usahihi wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo, kutotumika kwa alama za vidole katika kufanya malipo kwa wazee, kutosajiliwa kwa "Point of Sales (POS)" kwenye mfumo wa ZUPS MIS.

10.9.3 Udhibiti wa Ujumla wa TEHAMA.

Kukosekana kwa muongozo wa uundwaji na majukumu ya kamati ya uendeshaji ya TEHAMA (ICT Streering Committee Charter), kukosekana kwa kamati ya uendeshaji wa TEHAMA (ICT Streering Committee), kutokuwepo kwa makubaliano ya kuhifadhi Seva ya Wizara ZICTIA, udhaifu katika ushirikiano baina ya Wizara ya Afya na Kitengo cha Pensheni Jamii katika kuyapatia ufumbuzi matatizo na changamoto za Mfumo, kukosekana kwa mpango wa kuchukua nakala za taarifa za mifumo (Systems Backup Plan), kutopatikana kwa ripoti za majaribio nakala za taarifa za mifumo (Backup testing report), kukosekana kwa Msimamizi rasmi wa mfumo wa ZUPS MIS, ufinyu wa Ofisi ya kitengo cha TEHAMA cha Kitengo cha Pensheni Jamii, kutokuwepo kwa mpango wa kuendeleza Biashara (Business Continuity Plan), kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na Maafa (Disaster Recovery Plan), kutokuwepo kwa makubaliano ya msaada wa ufundi wa mfumo wa ZUPS MIS (Service Level Agreement), kukosekana kwa Sera za TEHAMA (ICT Policy), kukosekana kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site).

10.10 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MS ACCESS DATABASE SYSTEM WAZEE

10.10.1 MATOKEO YA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa Mfumo wa MS Access Database System Wazee dosari mbali mbali zimebainika kama zifuatazo:-

10.10.1.1 Kukosekana kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kutengeneza Mfumo wa MS Access Wazee.

Kuandaa bajeti ya kutengeneza mfumo ya muda mfupi na muda mrefu ni moja ya nyaraka zinazoandaliwa katika hatua ya kwanza ambayo ni kuandaa mpango wa kutengeneza mfumo (system planning) kwa kuzingatia matakwa ya "System Development Life Cycle – SDLC", bajeti hizi ndizo hutumika katika kufanya udhibiti wa gharama za kutengeneza mfumo ili kuhakikisha kwamba vinafanyika vitu au kazi zilizopo kwenye mpango pekee na kama kuna kazi za ziada nje ya mpango sinasajiliwa na gharama zake kuingizwa kwenye bajeti ili kuweza kupata udhibiti kamili wa gharama zote za kutengeneza mfumo.

Nyaraka nyengine zinazoandaliwa kwenye hatua ya "system planning" ni pamoja na kuandaa mipango kazi wa muda mrefu (long term plan), sera za kuchagua miradi ya TEHAMA, kufanya upembuzi yakinifu wa awali na kupata idhini ya Menejimenti ya taasisi ya kuendelea na mradi, andiko la pamoja na ratiba ya mradi (project schedule).

Katika ukaguzi wetu tulibaini Wizara ya Afya haina kumbukumbu yoyote ya gharama zilizotumika katika kutengeneza mfumo wa MS Access Database Wazee uliotengenezwa mwaka 2016 jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) jambo amabalo ni kinyume na sheria ya matumizi ya fedha za za Umma.

Kitendo cha kutokuwepo kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kwenye utengenezaji wa mfumo kinaweza kuashiria ubadhirifu wa fedha za Umma uliojificha kwenye kivuli cha gharama za kutengeneza mfumo, pamoja na kukosa fursa ya kufanya tathmini ya gharama na faida za mfumo katika kubainisha thamani ya fedha (value for money) kwenye utengenezwaji wa mfumo husika, kushindwa kurikodiwa kwa taarifa za mfumo kwenye "Asset Register" ya Wizara kwa kutojulikana thamani halisi ya fedha iliyotumika.

Aidha, Kukosekana kwa taarifa za matumizi ya fedha kunapelekea Wizara kukosa fursa ya kuboresha mipango na bajeti zake miaka ijayo kwa kuwa haina kumbukumbu za matumizi kwa miaka iliyopita kwenye utengenezaji wa mfumo na kuweka ungumu wa kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Serikali na kuinyima fursa Selikali ya kupata ushauri kwa lengo la kuboresha zaidi usimamizi wa raslimali zake.

Ukaguzi unashauri kuzingatiwa kwa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mfumo kama hii ambapo nyaraka zote za mfumo ikiwa ni pamoja na bajeti na matumizi halisi kutunzwa kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, kwa kuwa mfumo huu bado unatumika kwa ajili ya kufanya usalili wa Wazee ili kupata taarifa

za usajili huo (Eligible), ukaguzi unashauri ni vyema ukafanyiwa tathmini ya gharama zilizotumika kuutengeza ili kujua thamani halisi ya fedha kwa kipindi cha sasa kwa lengo la kuingizwa kwenye daftali la mali za TEHAMA (ICT Asset Register) za Wizara ya Afya na kwenye Asset Register ya Wizara kwa ujumla.

10.10.1.2 Kutozingatiwa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika kutengeneza mifumo "Systems Development Life Cycle".

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo huu hauna nyaraka zozote zinazohusiana na mfumo ikiwa ni pamoja na nyaraka muhimu katika matumizi ya mfumo inayoelezea namna mfumo unanyofanya kazi (system operations manual), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanifiwa (system architecture document), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanidiwa (system configurations manual), na nyaraka nyingine kama vile za mahitaji ya mfumo (system requirements document), na ile ya kuidhinisha matumizi ya mfumo baada ya kujarbiwa na kukidhi vigezo (Users Acceptance Certificate) n.k.

Pia, katika ukaguzi huu ilibainika kwamba mfumo huu muhimu katika ulipaji wa Pensheni za Wazee wote wenye umri wa kuanzia miaka 70 Zanzibar zinazokadiriwa kuwa zaidi ya shilingi Bilioni Moja kila mwezi katika utengenezaji wake haukuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) kuanzia hatua ya awali ya utengenezwaji wake mpaka ile ye mwisho (System Development Life Cycle – SDLC) ambayo inaelekeza kwamba mfumo unatakiwa kutengenezwa kwa kufuata hatua kwa hatua ambapo kila hatua inachangia katika kuhakikisha kwamba mfumo unaotengenezwa unakidhi mahitaji ya watumiaji kwa wakati uliopo na wakati ujao huku ukizingatia mikakati ya taasisi, udhibiti na usalama na kwamba unaongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika.

Kwa mfano, kuandaa mpango kazi wa kutengeneza mfumo (systems planning) ni hatua ya kwanza katika "SDCL" ambapo pamoja na mambo mengine yanayofanyika ni kuandaa mpango kazi wa muda mrefu (long term plan), sera za kuchagua miradi ya TEHAMA, bajeti ya muda mfupi na muda mrefu ya TEHAMA, kufanya upembuzi yakinifu wa awali na kupata hidhini ya menejimenti ya taasisi ya kuendelea na mradi, andiko la pamoja na ratiba ya mradi (Project Schedule).

Hatua ya pili ni kufanya tathmini ya mfumo (systems analysis) ambapo wataalamu wa TEHAMA wanakusanya taarifa za mahitaji ya watumiaji wa mfumo (system users' requirements) na kuyachakata kisha huandaa nyaraka ya mahitaji (system requirements document), hatua nyengine ni pamoja ile ya tatu mpaka ya nane katika mfuatano.

Kutokuwepo kwa nyaraka zote zinazohitajika katika utaratibu wa kutengeneza mifumo kunaweza kupelekea athari mbali mbali zikiwemo zifuatazo:-

- a) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k kwani uandishi wa nyaraka mbalimbali za mfumo unawapa nafasi watu na wadau wengine wa mfumo kuchangia mawazo yao katika namna ambayo ni rasmi ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuhidhinisha nyaraka husika ili kuendelea na hatua nyingine jambo linalopelekea kuboresha mfumo utakaotengenezwa.

- b) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa kama kisiwa kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mingine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo linarudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- c) Tasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na dharama, muda, juhudi na jitihada zilizotumika mpaka kuupata mfumo uliokamili, hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- d) Taasisi kushindwa kudhibiti matumizi, muda na ubora wa mfumo husika kwa sababu hakuna mipango wala bajeti iliyoandikwa na kuhidhinishwa na menejimenti ya taasisi.
- e) Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.

Kuendeleza utegemezi kwa mtoa huduma (system supplier) ikiwa mfumo umetengenezwa na mtoa huduma wa nje kwa sababu taasisi inakuwa haina kumbukumbu muhimu ambazo ingeliweza kuzitumia kujenga uwezo wa ndani na kupunguza utegemezi kwa mtoa huduma jambo ambalo linaokoa gharama na kuipunguzia mzigo Serikali.

Ukaguzi unashauri kuzingatiwa kwa miongozo na viwango bora vinavyokubalika (best practice) katika utengenezaji wa mifumo kama hii ambapo nyaraka zote za mfumo ikiwa ni pamoja na bajeti, ratiba, usanifu wa mfumo, tija, utendaji kazi wa mfumo, usanidi, mpango kazi, mahitaji ya mfumo na uhidhinishwaji wa nyaraka hizo vizingatiwe kabla ya kutengeneza au kununua mfumo wowote.

Aidha, kwa kuwa mfumo huu wa ulipaji wa Pensheni za Wazee bado unatumika ni vyema wataalamu wa TEHAMA wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na watumiaji wa mfumo ndani ya Wizara waandae nyaraka zote muhimu za mfumo kama zilivyoainishwa hapo juu na zipatikane kwa matumizi ya ndani pamoja na matumizi ya ukaguzi mapema iwezekanavyo ili kuondoa au kupunguza hatari iliyopo inayoweza kupelekea kupata athari kama zilivyoelewa hapo juu.

10.10.1.3 Mfumo kutokuhifadhiwa kwenye chumba maalumu cha Seva

Chumba kinachohifadhi vifaa vya TEHAMA (IT Equipment/ Server Room) ni sehemu muhimu zaidi ya Taasisi inayotunza damu ya uhai wa taasisi yoyote hususani taasisi ambayo inategemea taarifa ili kuendesha kazi zake. Inapotokea moto, tetemeko la ardhi, mafuriko, au umeme kukatika kwa muda mrefu chumba muhimu zaidi kwenye taasisi ni chumba cha Seva. Bila chumba hiki taasisi haiwezi kufanya kazi zake za kila siku kwa ufanisi na tija. Chumba cha Seva kilichosanifiwa kinyume na viwango vinavyokubalika (best practice) na kisicho na udhibiti na usalama ni mzigo (liability) kwa Taasisi.

Mbali na kukiweka katika hali ya usafi na usalama, chumba cha Seva kinatakiwa pia kuzingatia hali ya joto, unyevunyevu, udhibiti wa moto, udhibiti wa kuingia na kutoka. Madhumuni hasa ya kukiwekea udhibiti na kukilinda chumba cha Seva ni kuhakikisha kwamba taarifa za Serikali na miundombinu inayotumika katika kurikodi, kuchakata, kusafirisha na kuzitunza taarifa hizo inakuwa salama muda wote ndani ya chumba cha Seva ili kuhakikisha kwamba Taasisi haikwami kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kwa usalama.

Moja wapo ya vifaa muhimu vya kiudhibiti vinavyoshauriwa kuwekwa kwenye chumba cha Seva ni kifaa cha kielektroniki cha kudhibiti uingiaji kwenye chumba cha seva (Biometric Lock Device) ambapo kwa kila anayeingia kwenye chumba hiki ni lazima awe amesajiliwa kwenye kifaa hiki na kwamba kitamruhusu aingie baada ya kuweka kidole au sura yake, pamoja na kifaa hiki pia panatakiwa kuwepo na mlango/ geti linalofungwa kwa ufunguo muda wote kwa ajili ya udhibiti wa uingiaji hususani umeme ukiwa umekatika isipokua pale mtu anapofungua ili kuingia chumbani, chumba cha Seva pia kinashauriwa kiwe na mfumo wa kuzima moto (fire suppression system) ambao unafanya kazi wenyewe (automatic) kwa ajili ya kulinda Seva na miundombinu ya TEHAMA ndani ya chumba hicho dhidi ya moto, pia chumba hiki kinashauriwa kuwa na kamera za ulinzi (CCTV Camera) kwa ajili ya kurikodi matukio yote yanayotokea ndani ya chumba ili kusaidia udhibiti wa usalama.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini Wizara ya Afya kwa kupitia Kitengo cha Pensheni Jamii haina chumba cha Seva na badala yake Seva inayotumika kuhifadhi taarifa za mfumo wa MS Access Database System Wazee imehifadhiwa kwenye chumba cha ofisi ya TEHAMA ya Pensheni Jamii ambacho hakijazingatia vigezo vyovyote kama vilivyofafanuliwa hapo juu.

Hali hii inaziweka taarifa za Serikali katika usajili na ulipaji Wazee kwenye tahari kubwa (high risk) kwani hazina udhibiti wowote ule na kwamba mtu yeyote anayeingia kwenye ofisi hii anaweza kuzifikia taarifa hizo na kufanya chochote bila ya kujulikana kwa wakati

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Idara ya Pensheni Jamii kufanya mambo yafuatayo:-

- a) Mfumo huu uhifadhiwe kwenye chumba maalum ambacho kitajulikana kama ni chumba cha Seva za Wizara na chumba hiki kizingatie vigezo na miongozo "best practice" ya ndani na nje katika kuandaa chumba cha Seva kama ilivyofafanuliwa hapo juu.
- b) Kwa kuzingatia ukubwa na thamani ya fedha zinazopitia kwenye mfumo huu kila mwezi kwa ajili ya malipo ya Pensheni Jamii kwa Wazee ni vyema Wizara ikahakikisha kwamba kompyuta, Seva, na mtandao unatumika kufanya usajili na malipo ya Wazee vinawekewa udhibiti madhubuti muda wote ili kupunguza au kuondoa hatari iliyopo kwa sasa.
- c) Usimamizi wa mfumo huu ufanyike kwa pamoja na mifumo mengine ya Wizara (Centralized Administration) ili kuhakikisha kwamba tija na ufanisi vinapatikana katika matumizi ya fedha za Serikali kwenye uendeshaji wa TEHAMA Wizarani.

10.10.1.4 Kuendelea kutumika kwa mfumo wa Microsoft Access Database Wazee.

Kupitia majadiliano, mahojiano na kufanya uchunguzi kwa watumiaji mfumo wa MS Access Database Wazee ukaguzi ulibaini kwamba mfumo huu bado unatumika kinyume na matarajio ya ukaguzi kwamba mfumo wa ZUPS MIS ulitengenezwa kwa gharama ya zaidi ya milioni mia moja ili itumike kama mbadala wa MS Access tangu mwaka 2018, hata hivyo ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa MS Access bado unatumika mpaka sasa kufanya usajili wa Wazee sambamba na ule wa ZUPS MIS (parallel systems) sababu ya kufanya hivyo ikielezwa kuwa ni kuwepo kwa udhaifu kwenye mfumo wa ZUPS MIS hususani kwenye "format" ya fomu maalumu ijulikanayo kama "eligible" ambayo haijakidhi mahitaji ya watumiaji kwenye sehemu ya kuweka sahihi ama dole gumba kwa Wazee jambo ambalo limekuwa sababu kuu ya kwanini mfumo huu wa zamani bado unatumika.

Kwa kuwa mfumo wa MS Access ndio unatumika kama “primary system” kwa ajili ya kusajili wazee na kwa kuwa udhaifu wa mfumo huu bado uko pale pale kama ilivyokuwa mwanzo mpaka kupelekea kufanywa uwekezaji mpya kwenye mfumo wa ZUPS MIS matumizi ya mfumo huu yana ashiria kukubalika kwa changamoto na udhaifu uliopo na kwamba Serikali kupitia Wizara ya Afya imekubali kuzikabili athari zinazoweza kujitokeza kwa kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na kupata hasara kwa kulipa Wazee zaidi ya mara moja, kukosa taarifa sahihi za idadi ya Wazee wanaostahili kulipwa Pensheni na kupelekea kuathiri katika namna hasi mipango ya Serikali kuanzia kwenye bajeti na utekelezaji wake.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya ufuatiliaji wa mfumo huu wa ZUPS MIS kuhakikisha kwamba changamoto au udhaifu uliopo unapatiwa ufumbuzi na kwamba mfumo wa ZUPS MIS unatumika ipasavyo katika kufanya usajili, kutengeneza “eligible” na kufanya malipo ya Wazee na kwamba mfumo wa MS Access unatolewa kwenye matumizi haya.

10.10.1.5 Kukosekana kwa udhibiti wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo haujawekewa utaratibu wa kulazimu taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entrant) na kuhakikiwa na mtu mwengine (reviewer/ approver) kabla ya kuzituma “post” taarifa hizo kama hatua ya mwisho ya uingizaji wa taarifa kwenye mfumo. Hii inamaanisha kwamba kwa hali ilivyo sasa muingizaji wa taarifa anaingiza na kukamilisha hatua zote zinazohitajika kuingizwa katika mfumo peke yake bila ya kukaguliwa au kuthibitisha usahihi wake na mtu mwengine kwenye mfumo.

Mfumo kutokuwa na kipengele kinachomtaka mtu mwengine kuhakiki na kuthibitisha taarifa za Wazee zinazoingizwa kwenye mfumo kunaweza kupelekea uingizwaji wa taarifa nyingi ambazo sio sahihi au zisizokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria kwa sababu ya makosa ya kibinaadamu, kutumia chanzo cha taarifa kisicho sahihi, au kwa makusudi akiwa na nia ovyu na kusababisha kutoaminika kwa taarifa hizo jambo linaloweza pelekea kutotumika kwa mfumo na kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kuwekeza na kutumia TEHAMA ili kuboresha utowaji wa Huduma kwa wananchi wake.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuweka mgawanyiko wa majukumu kwenye matumizi ya mfumo kwa lengo la kuleta uwazi na uwajibikaji.

10.10.1.6 Uwepo wa nakala za taarifa (duplicate data).

Baada ya kuupitia mfumo wa Microsoft Access Database Wazee, ukaguzi umebaini kwamba mfumo huu unaruhusu kusajili Mzee mmoja zaidi ya mara moja, ikiwa na maana kwamba mfumo hauna uwezo wa kutambua kwamba Mzee husika amekwisha sajiliwa na ukazuiya usajili wake kwa mara ya pili jambo ambalo limepelekea uwepo wa nakala za taarifa zaidi ya moja kwa baadhi ya Wazee waliosajiliwa ndani ya mfumo huu. Kwa mujibu wa majadiliano na watumiaji wa mfumo ukaguzi ulifahamishwa kwamba hizi zilikuwa ni miongoni mwa changamoto za mfumo huu zilizopelekea kutengenezwa kwa mfumo wa ZUPS MIS hata hivyo ukaguzi haukuweza kuelewa ni kwa sababu gani mfumo huu bado unaendelea kutumika.

Hali hii inaweza kupelekea Wazee wenye nakala za taarifa kufanyiwa malipo zaidi ya mara moja jambo ambalo litakuwa chanzo cha hasara kwa Serikali kulingana na “double paymantes” zilizofanyika.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuupitia mfumo huu ili kuzibaini nakala zote za taarifa za Wazee na kisha kuziondoa kwenye mfumo. Ili kuondoa matumizi ya mifumo miwili kwa wakati mmoja kwa lengo la kutatua mapungufu yaliyomo kwenye mfumo wa ZUPS MIS hususani kwenye kutoa “Eligible” zisizokidhi mahitaji ya watumiaji ili kazi hiyo ifanywe kwenye mfumo wa ZUPZ MIS tofauti na hali ilivyo kwa sasa ambapo fomu za eligible zinatolewa kwenye MS Access Database Wazee.

10.10.1.7 Udhaifu wa udhibiti kwenye kompyuta zinazotumika kuufikia mfumo (Computer Access Control).

Ukaguzi umebaini kuwa kampyuta zinazotumika kuufikia mfumo huu wa MS Access hazina udhibiti unastahili kiasi kwamba mtu yeyote anaweza kuingia kwenye kompyuta hizo na kuufikia mfumo wa MS Access kiarahisi. Hali hii inakwenda kinyume na miongozo ya “best practices” inayo elekeza kwamba ni muhimu kompyuta zinazotumika kuufikia mfumo kama huu ziwe na udhibiti na ulinzi wa kutosha kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali zinazoweza kufikiwa kupitia kompyuta hizi.

Komputa hizi zinapaswa kuwekewa udhibiti kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na nywila (Password) kwa kila mtumiaji kulazimika kungia kwenye kompyuta husika kwa “user ID” na nywila yake pekee.

Ukaguzi unashauri kuondolewa kwenye matumizi mfumo huu mapema iwezekanavyo mara baada ya kutatua changamoto zilizomo kwenye mfumo wa ZUPS MIS ili kuepuka athari zinazoweza kutokea kama mfumo huu utaendelea kutumika ikiwa ni pamoja uwezekano wa taarifa za Wazee ambazo sio rasmi kuingizwa kwenye mfumo kwa kuwa komputa hizi hazina udhibiti.

10.10.1.8 Udhaifu wa udhibiti wa mfumo kwenye kuufikia (System access control).

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo huu wa MS Access hauna udhibiti wa kuufikia, yaani mtu yeyote anaweza kuingia kwenye mfumo huu wakati wowote ilimradi aweze kuingia kwenye chumba chenye kampyuta zilizounganishwa na mfumo huu.

Hali hii inaongeza shaka dhidi usalama wa taarifa zilizomo kwenye mfumo huu ambapo ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya maamuzi ya haraka ya kusitisha matumizi ya mfumo huu hususani baada ya kufanyiwa kazi changamoto zilizomo kwenye mfumo wa ZUPS MIS katika kutoa “eligible”.

10.11 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA ZANZIBAR UNIVERSAL PENSION SCHEME MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM

10.11.1 MATOKEO YA UKAGUZI

Katika kuupitia Mfumo wa Zanzibar Universal Pension Scheme Management Information System (ZUPS MIS) ukaguzi ulibaini mambo mbali mbali ikiwemo dosari zifuatazo:-

10.11.1.1 Kutotumika kwa mfumo wa ZUPS MIS kufanya malipo ya kielektroniki.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa ZUPS MIS hautumiki kufanya malipo kielektroniki na badala yake wazee wa Pensheni Jamii wanalipwa fedha zao mkononi "cash payment" kinyume na matakwa ya mkataba baina ya Wizara na kampuni ya Ms. Web Technologies Tanzania Ltd kwenye kipengele cha 6 sehemu ya mahitaji ya watumiaji (user requirements) kinachoelezea takwa la watumiaji kwamba mfumo ulitakiwa kuwezesha njia mbadala za malipo kama vile Benki na Mitandao ya Simu "Support Alternative Payment Methods, Banks and Mobile Phones" .

Athari za ulipaji wa fedha za Pensheni Jamii kwa njia ya mkono (cash payment):-

- Hatari ya kuvamiwa na wahalifu wakati wa kusafirisha fedha au wakati wa kufanya malipo na kusababisha wizi wa fedha hizo jambo ambalo litakuwa hasara kubwa kwa Serikali.
- Hatari ya kufanya malipo zaidi ya mara moja kwa wazee, hii inaweza kutokea kwa kuzingatia mazingira magumu yanayokuwepo wakati wa kulipa fedha hizo kwa wazee ambapo uhibitaji na uratibu wa zoezi zima linakumbwa na changamoto za kufanana kwa majina ya wazee ambayo yanajitokeza katika shehia mbali mbali.
- Hatari ya kupoteza fedha kama ikitokea ajali wakati wa usafirishaji kutoka Wizarani kuelekea eneo la kufanyia malipo kwa wazee.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkataba huu ili kubaini utendaji (performance) wa mtoa huduma katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa mkataba na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria za nchi kwenye maeneo ambayo mtoa huduma hajatimiza wajibu wake kama ilivyoainishwa kwenye mkataba huu.

Aidha, ukaguzi unashauri kwamba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mtoa huduma iweke mkakati na utaratibu utakaohakikisha kwamba wazee wa Pensheni Jamii wanalipwa fedha zao kielektroniki kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mitandao ya simu, benki n.k moja kwa moja kutoka kwenye mfumo wa ZUPS MIS ili kuondoa hatari zilizoainishwa hapo juu zinazoweza kutokea kwa kufanya malipo mkononi (cash payments).

Hata hivyo ukaguzi unapendekeza ni vyema Wizara kupitia kitengo cha Pensheni Jamii kujifunza namna bora na salama ya kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki kama vile inavyofanyika katika Mradi wa TASAF katika malipo ya kaya masikini.

10.11.1.2 Kukosekana kwa uhibitaji wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo haujawekewa utaratibu wa kulazimu taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entry) na kuhakikiwa na mtu mwingine (reviewer/ approver) kabla ya kuzituma "post" taarifa hizo kama hatua ya mwisho ya uingizaji wa taarifa kwenye mfumo. Hii inamaanisha kwamba kwa hali ilivyo sasa muingizaji wa taarifa anaingiza na kukamilisha hatua zote zinazohitajika kuingizwa katika mfumo peke yake bila ya kukaguliwa au kuthibitisha usahihi wake na mtu mwingine kwenye mfumo.

Mfumo kutokuwa na kipengele kinachomtaka mtu mwingine kuhakiki na kuthibitisha taarifa za

Wazee zinazolingizwa kwenye mfumo kunaweza kupelekea uingizwaji wa taarifa nyingi ambazo sio sahihi au zisizokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria kwa sababu ya makosa ya kibinaadamu, kutumia chanzo cha taarifa kisicho sahihi, au kwa makusudi akiwa na nia ovu na kusababisha kutoaminika kwa taarifa hizo jambo linaloweza pelekea kutotumika kwa mfumo na kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kuwekeza na kutumia TEHAMA ili kuboresha utowaji wa Huduma kwa wananchi wake.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuweka mgawanyiko wa majukumu kwenye matumizi ya mfumo kwa lengo la kuleta uwazi na uwajibikaji.

10.11.1.3 Uwepo wa nakala za data (duplicate data).

Baada ya kuupitia mfumo wa ZUPS MIS, ukaguzi umebaini kwamba mfumo huu unaruhusu kusajili Mzee mmoja zaidi ya mara moja, ikiwa na maana kwamba mfumo hauna uwezo wa kutambua kwamba Mzee husika amekwisha sajiliwa na ukazuiya usajili wake kwa mara ya pili jambo ambalo limepelekea uwepo wa nakala za taarifa zaidi ya moja kwa baadhi ya Wazee waliosajiliwa ndani ya mfumo huu.

Hali hii ni kinyume na mahitaji ya watumiaji wa mfumo huu (user requirements) kipengele namba 2 kwenye mkataba baina ya Wizara na Mtoa huduma ambapo ilitarajiwa kwamba mfumo utazuiya usajili wa waombaji ambao wamekwisha sajiliwa "Be able to refuse registration of an applicant who has already been registered".

Hali hii inaweza kupelekea Wazee wenye nakala za taarifa kufanyiwa malipo zaidi ya mara moja jambo ambalo litakuwa chanzo cha hasara kwa Serikali kulingana na kufanyika malipo zaidi ya mara moja kwa mzee mmoja.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuupitia mfumo huu ili kuzibaini nakala zote za taarifa za Wazee na kuziondoa kwenye mfumo. Pamoja na hilo, ni vyema kuhakikisha kwamba mtoa huduma anatimiza wajibu wake kulingana na matakwa ya mkataba ambapo kwa sababu mtoa huduma huyu tayari ameshalipwa malipo yake yote ya fedha katika mkataba huu, hivyo Wizara ichukuwe hatua za makusudi kuwasiliana naye ili aje na atimize wajibu wake ambao ameacha kwa uharaka unaostahili katika kulinda maslahi ya Serikali na nchi kwa ujumla.

10.11.1.4 Usajili wa taarifa za Wazee kutofanyika kwenye Seva moja kwa moja kupitia mtandao.

Ukaguzi umebaini kwamba taarifa za usajili wa Wazee zinaingizwa kwanza kwenye "POS" ambazo hutumika zikiwa "offline" na baada ya kurejea ofisini watumishi huzipandisha (upload) kwenye mfumo wa ZUPS MIS. Hata hivyo ukaguzi umebaini baadhi ya POS zinazotumika zinauwezo wa kufanya usajili wa moja kwa moja kwenye mfumo ikiwa zitawekewa "sim card" za mtandao wa simu na kuunganishwa na vifurushi vya mtandao kwa lengo la kufanya usajili moja kwa moja.

Hali hii imechangia upotevu wa taarifa zinazokusanywa na watumishi wa Wizara ya Afya wakati wa usajili kwa sababu ya kutegemea POS kukusanya taarifa na baadae kuzipeleka taarifa hizo kwenye mfumo ambapo katika kipindi hicho baadhi ya taarifa hupotea hususani pindi POS zinapokuwa zimeishiwa na nafasi (storage capacity).

Ili kuondoa hatari hii ya upotevu wa taarifa ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuziwekea “sim cards and internet bundles POS” zote zinazotumika kufanya usajili na malipo ya Wazee kwa kutumia njia ambazo ni bora na zenye kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya ulipaji wa Pansheni Jamii.

10.11.1.5 Kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mfumo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya mfumo wa ZUPS MIS.

Ukaguzi umebaini kwamba, pamoja na kuwa mfumo wa ZUPS MIS unatumiwa kwa zaidi ya miaka 4 sasa lakini bado wafanyakazi wanaotumia mfumo huo hawana uelewa wa kutosha wa namna ya kuutumia mfumo ipasavyo ili kuleta tija na ufanisi katika kusimamia, kuratibu na kuutumia mfumo wa ZUPS MIS. Hali hii imepelekea uwepo wa matumizi hafifu ya mfumo huu kwa kuwa watumiaji walio wengi hawana uelewa wa kutosha katika matumizi sahihi ya mfumo kiasi cha kushindwa kuwapitisha wakaguzi kwenye maeneo mbalimbali ya mfumo ikiwa ni pamoja na namna ya kupata ripoti tofauti za taarifa za Wazee na namna ya kuprinti taarifa kwenye mfumo.

Aidha, hawa ni moingoni wa watumiaji wakuu (core team) wa mfumo wanaotarajiwa kuwa na uelewa mpana wa mfumo mzima ili kuweza kutoa mafunzo kwa watumiaji wengine kwenye maeneo yao ya kazi jambo ambalo linasababisha matumizi hafifu na mabaya ya mfumo ikiwa ni pamoja na uingizwaji wa taarifa ambazo sio sahihi na kuisababishia Serikali hasara kwa kuwalipa Wazee wasio stahiki.

Ukaguzi unaishauri Wizara kwa kushirikiana na mtoa huduma iandae mpango kazi wa mafunzo na kutoa mafunzo hayo kwa watumiaji wa mfumo na kwa wataalamu wa TEHAMA ili kuwajengea uwezo stahiki angalau mara moja kila mwaka. Aidha, Wizara iweke utaratibu utakao hakikisha kuwa mafunzo ya mfumo huu yanakuwa endelevu kwa kipindi chote ambacho mfumo huu utatumika ili kwamba waajiriwa wapya na wahamiaji wapate nafasi ya kufundishwa matumizi ya mfumo na watumiaji wa mfumo wenye uzoefu kuongezewa taaluma kulingana na kukua na kupanuka kwa mahitaji ya mfumo.

10.11.1.6 Wizara kutokutumia Mkonga/ Mtandao wa Serikali kwenye Mifumo yake

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Idara ya Ustawi wa Jamii kitengo cha Pansheni jamii wanatumia mtandao wa (internet) TTCL kinyume na miongozo ya Serikali SMZ ambayo inaelekeza kwamba Taasisi za uma zinatakiwa kutumia Mkonga wa Serikali unaoratibiwa na ZICTIA katika kazi zao zote za kila siku.

Katika mahojiano wa wakaguliwa ukaguzi ulifahamishwa kwamba kabla ya kufanya maamuzi ya kutumia mtandao wa TTCL kitengo cha Pansheni Jamii kilikuwa kinatumia Mkonga wa Serikali lakini walikuwa wanashindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi kwa sababu ya kasi ndogo ya mtandao waliyokuwa wanapata ambayo ilipelekea kushindwa kuingia kwenye mfumo na kufanya kazi kwa uharaka kama inavyotarajiwa.

Athari mojawapo ya kutotumia Mkonga wa Serikali ni pamoja na kutumia fedha za Serikali kulipia huduma ya mtandao ambayo kimsingi ilitakiwa kupatikana bure kwa kutumia Mkonga.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya mambo yafuatayo:-

- a) Kufanya mazungumzo na ZICTIA yatakayo pelekea kufanyika kwa tathmini ya kubaini chanzo cha kupungua kwa kasi ya mtandao uliopo Wizarani wakiwa wanatumia Mkonga na kuipatia ufumbuzi wake kwa muda muafaka.
- b) Baada ya kutatuliwa kwa changamoto ya "slowness" Wizara inashauriwa kurejea kutumia Mkonga wa Serikali ambao kwa sasa hauna gharama yoyote kwa Taasisi za Serikali zinazo utumia.

10.11.1.7 Mfumo kuruhusu usajili wa baadhi ya Wazee wasiokidhi matakwa ya Kisheria. (validation)

Ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya Wazee waliosajiliwa ambao hawajakidhi matakwa ya Sheria ya Wazee nambari 2 ya mwaka 2020 ambapo kifungu 33(2) kinaeleza kuhusu sifa za Mzee ili kuruhusiwa kuingizwa katika mpango wa Pensheni Jamii, kifungu hiki kimeweka bayana masharti 3 ambayo yanatakiwa kutimizwa kwa pamoja ili Mzee aweze kuingiwa kwenye mpango huu kama vinavyojieleza hapo chini:-

- Umri wa miaka 70 au zaidi,
- Mzanzibari, na
- Amekuwa mkaazi wa Zanzibar kwa zaidi ya miaka kumi mfululizo.

Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha 1: Fomu ya usajili wa wazee inayoonesha kutozingatiwa kwa takwa la umri.

The screenshot shows a web-based registration form titled 'ZUPS - FOMU YA USAJILI WA MZEE'. The form is divided into several sections for data entry. Two specific fields are highlighted with red boxes to indicate validation issues related to age:

- Tarehe ya Kuzaliwa:** The date '1972-01-01' is entered, which is less than 70 years old, failing the age requirement.
- Nambari ya kitambulisho:** The value 'jumaakakakak' is entered, which is not a valid ID number.

 Other visible fields include:

- Namba ya Fomu:** 1221
- Zanzibar ID:** A field for entering the ID number.
- Jina la Babu:** HASSAN
- Umri wakati wa usajili:** 50
- Alma Ya Kitambulisho:** KITAMBULISHO CHA TALFA
- Wilaya:** KASKAZINI - A
- Shahia:** Danda Kuu
- Simu:** A field for entering the phone number.
- Wazaomtegemea:** 3
- Blood Group:** A+

Kitendo cha mfumo kuruhusu usajili wa Wazee kinyume cha Sheria ni uvunjifu wa sheria za nchi jambo ambalo halikubaliki kwani hali hii inaweza kusababisha mkanganyiko na migongano isiyo ya lazima kwenye jamii hususani kwenye vyombo vyenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi na utoaji haki.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo:-

- a) Wizara ya Afya ifanye uhakiki wa Wazee wote waliosajiliwa kwenye mifumo ya MS Access Wazee na ule wa ZUPS MIS kwa kupitia taarifa zao za usajili kuhakikisha kwamba zinakidhi matakwa ya Sheria ya Wazee ya mwaka 2020.
- b) Kwa kubaini idadi ya Wazee waliosajiliwa na kupokea mafao ya Pensheni Jamii kinyume cha Sheria Wizara inashauriwa kufanya tathmini ya hasara kwa Serikali ambayo imetokana na kutokuzingatiwa kwa Sheria hii ya Wazee tangu kuanza kufanya kazi ili kubaini ukubwa wa tatitizo na kuweka mikakati mahsusi ya kulizuia tatizo hili kutojirudia tena.
- c) Kufanya maboresho kwenye mfumo wa ZUPS MIS ili usaidie kwenye udhibiti wa usajili na malipo kwa Wazee kulingana na matakwa ya Sheria badala ya kutegemea uadilifu wa "data entry" pekee.
- d) Kuhakikisha kwamba kuna mfumo mmoja tu (ZUPS MIS) ambao unatumika katika kufanya usajili na kutoa fomu maalumu za uthibitisho wa kukamilika kwa usajili zijulikanazo kama "Eligibles" ili kuboresha udhibiti wa zoezi la usajili.

10.11.1.8 Kutozingatiwa mgawanyo wa majukumu kwenye mfumo (Segregation of Duties).


ISACA inaelezea watumiaji wa mfumo (system users) kama ni watu wanaotumia mfumo (application) au kifaa (tool) ili kufikia matokeo tarajiwa ya biashara/ kazi. Kwa ujumla kwenye TEHAMA watumiaji wa mfumo wapo katika makundi makuu mawili ambayo ni watumiaji kwenye upande wa Teknolojia (IT users) na watumiaji kwenye upande wa kazi/ biashara (business users).

Kwa sababu ya umuhimu wa taarifa zinazopatikana kwenye mifumo ya TEHAMA na kwa kuzingatia hatari za kiusalama zinazoweza kusababishwa na ufikiaji wa mifumo (system access) ikiwa ufikiaji huo utatumika kwa nia mbaya ambapo inaweza kupelekea kupotea, kuibiwa, kuharibiwa kutokana na udukuzi, shambulio la virusi n.k. kila taasisi inalo jukumu la kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu wa kulinda taarifa zake ikiwa ni pamoja na vifaa/miundombinu ya TEHAMA inayotumika katika kuzichakata, kuzisafirisha na kuzihifadhi taarifa zake ili kuweka udhibiti madhubuti, miongoni mwa udhibiti huu ni namna ya kudhibiti watumiaji ili kupunguza au kumaliza kabisa uwezekano wa watumiaji kuwa chanzo cha matumizi mabaya, upotevu, wizi na uharibifu wa taarifa za Serikali.

Miongozo na viwango vinavyokubalika (best practices) vinaelekeza kwamba kila mtumiaji wa mfumo apewe ruhusa ya kuingia kwenye mfumo (system access) kulingana na majukumu yake ya kazi kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu (Segregation of Duties) ambapo mfumo utahakikisha kwamba mtumiaji mmoja hawezi kufanya kila kitu peke yake na kwamba, "IT users" hawapaswi kupewa "system access" kwenye upande wa "business users" ili kuingiza taarifa kwenye mfumo, kufanya hivyo kunaongeza udhaifu wa udhibiti wa taarifa zilizomo au zinazoingizwa kwenye mfumo.

Aidha, katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo Afisa TEHAMA ambaye anafanya kazi kama "IT user" na wakati huo huo amepewa ufikiaji wa mfumo kama "business user" kinyume na "best practice guidelines" kama zilivyoainishwa kwenye Jarida la ISACA 'ISACA Journal - Evaluating Access Control, January 2012'. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha 2 : Inaoenesha kutozingatiwa kwa mgawanyo wa majukumu



Hali hii inaongeza uwezekano wa mtu mmoja kufanya kila kitu peke yake bila kudhibitiwa kwa namna yoyote kwenye mfumo na ikiwa ataitumia vibaya nafasi hii inaweza kuleta madhara makubwa kwenye Wizara ambayo yanaweza kusababisha hasara kwa Serikali.


Ukaguzi unaishauri Wizara kuzingatia miongozo ya "best practice" kwenye mgawanyo wa majukumu ndani ya mfumo ili kuimarisha udhibiti wa mifumo yake ya kielektroniki katika kulinda taarifa za Serikali.

10.11.1.9 Kukosekana kwa ripoti mbalimbali za taarifa za Wazee kwenye Mfumo.


Ukaguzi umebaini udhaifu wa mfumo katika kutoa ripoti mbalimbali za taarifa za Wazee ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi kwa haraka katika kuongeza tija na ufanisi katika kutoa huduma. Hali hii inakwenda kinyume na mkataba baina ya Wizara na Mtoa huduma sehemu ya 4.0 "User Requirements" kipengele cha 15 ambacho kinasema "*Be able to generate various customized reports, including payments, registered people, claims registered during specified period (daily, weekly, monthly, yearly, and any user defined period. These reports have to be disaggregated by gender, location etc.*"

Miongoni mwa taarifa ambazo hazikuweza kupatikana kwenye mfumo huu ni pamoja na taarifa za Wazee waliofariki dunia, Wazee wapya, Wazee ambao hawajalipwa kwa kipindi fulani kama vile miezi 3, Wazee waliokataliwa maombi n.k. Hali halisi ya taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika Picha hapo chini.


Picha 3: Kukosekana kwa taarifa za wazee wapya.



Picha 4 : Taarifa ya Wazee waliokataliwa maombi.



Picha 5: Taarifa za Wazee ambao hawajalipwa kwa kipindi cha miezi 3.



Kukosekana kwa ripoti mbalimbali za taarifa za Wazee kwenye mfumo kunapunguza umuhimu na manufaa ya mfumo kwa Serikali kwani matarajio ya kurahisisha kazi kutokana na uwepo wa mfumo hayajapatikana kikamilifu, udhibiti na tija kwa kutumia mfumo bado havijadhahirika wazi wazi na kusababisha mfumo kutotegemewa katika kuongeza ufanisi kwenye kuwahudumia Wazee.

Mpaka sasa uwekezaji huu haujaonesha kuzaa matunda kama ilivyotarajiwa na Serikali kwa ujumla wake ambapo Wizara inashauriwa kusimamia mfumo huu kwa karibu chini ya kitengo cha TEHAMA cha Wizara ya Afya na kufanya "central management and administration" ili kuhakikisha kwamba matakwa ya mkataba baina ya pande mbili yanafuatiliwa kwa karibu katika kulinda maslahi mapana ya Serikali na nchi kwa ujumla.

Wizara inashauriwa kufanya tathmini ya ripoti zote zilizotakiwa kutengenezwa na mtoa huduma kwa mujibu wa "users requirements" kama ilivyoinishwa kwenye mkataba na kuhakikisha kwamba zinapatikana na zinafanya kazi ipasavyo kwa kushirikiana na mtoa huduma kwa kuwa kazi hizo zote tayari zilishalipiwa kwenye mkataba.

10.11.1.10 Kukosekana kwa mawasiliano baina ya taarifa za Unguja na zile za Pemba ndani ya mfumo wa ZUPS MIS.

Ukaguzi umebaini kwamba katika mfumo wa ZUPS MIS taarifa za Wazee wa Unguja zinapatikana kwa watumiaji wa Unguja pekee na taarifa za Wazee wa Pemba zinapatikana kwa watumiaji wa Pemba tu. Hii inamaanisha kwamba hata ikihitajika kupata taarifa zote kwa pamoja katika ngazi ya Wizara, Wazee wa Pemba na Unguja itapelekea kufanyika jitihada za ziada katika kufanikisha hilo.

Athari za jambo hili ni pamoja na kuongeza ugumu katika kufanya tathmini mbalimbali na upatikanaji wa taarifa kwa haraka katika kurahisisha ufanyaji wa maamuzi.

Kwa kuwa Wizara ya Afya ni moja kwa Pemba na Unguja na kwa kuwa mfumo pia ni mmoja wenye kanzidata moja ni vyema Wizara iliangalie upya suala hili katika kuhakikisha kwamba angalau katika ngazi ya Wizara taarifa hizi zote ziweze kupatikana kwa pamoja kwenye ripoti zote zilizomo kwenye mfumo.

10.11.1.11 Udhaifu wa usimamizi wa mfumo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa udhaifu wa usimamizi wa mfumo ZUPS MIS kinyume na mingozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) ambapo ukaguzi ulibaini mambo mbalimbali ikiwemo Wizara ya Afya kutokuwa na mtu rasmi aliyepewa jukumu la kuusimamia mfumo huu wa ZUPS MIS na kwamba maafisa wanaofanya kazi hii wamejipangia majukumu hayo pasipokuwa na ridhaa ya uongozi wa Wizara. Uwepo wa baadhi ya watumiaji wa mfumo waliosajiliwa zaidi ya mara moja kama inavyo onekana kwenye jedwali hapa chini:-

Jadwali Nambari 39 : Udhaifu wa usimamizi wa mfumo

	Jina la Afisa	Tarehe alosajiliwa	Cheo alichopewa
1	Zacharia Fabian Kitinde	20/12/2021	Data Clerk
2	Zacharia Fabian Kitinde	20/01/2021	Cashier
3	Moh'd Masoud Juma	02/01/2022	Pension Officer
4	Moh'd Masoud Juma	22/01/2021	Pension Officer

Ukaguzi umeendelea kubaini uwepo wa taarifa za Masheha 17 wa Unguja kwenye mfumo walio hai (active users) ambao wameshamaliza muda wao wa utumishi na walitakiwa kuondolewa mara tu baada ya kumaliza muda wao. Jumla ya Masheha waliopo kwenye mfumo ni **276** wakati Shehia zote za Unguja ni **259** ambapo kuna ongezeko la Masheha 17 kinyume na hali halisi.

Kwa mujibu wa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kama ilivyochapishwa kwenye Jarida la ISACA "*ISACA Journal - Evaluating Access Control, January 2012* " inaelekeza kwamba Tasisi inatakiwa kuwa na Sera na Taratibu (policies and Procedures) zinazohakikisha kwamba taarifa (credentials) za watumishi ambao muda wao wa utumishi umeisha/ ajira zao zimesitishwa zinatolewa au wanasitishwa ufikiaji wa mfumo (disabled) kwa wakati kwa sababu za kiusalama.

Athari zinazoweza kusababishwa na udhaifu wa usimamizi wa mfumo ni pamoja na:-

- Kwa kushindwa kuchukuwa hatua za kuwaondosha na kurekebisha taarifa za watumishi waliomaliza muda wao wa utumishi kwenye mfumo mara tu baada ya utumishi wao kumalizika kunaweza kupelekea mfumo kutoa taarifa zisizokuwa sahihi kwa Serikali na kuweza kusababisha Serikali kukosa takwimu sahihi za wa wahusika wanaoingizwa katika mfumo huo.
- Kwa watumiaji waliopewa majukumu tofauti katika mfumo wanaweza kupelekea kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu (SoD) na hatimae kuweza mtu moja tu kuweza kuingiza taarifa na kufanya malipo.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya udhaifu wa usimamizi wa mfumo huu wa ZUPS MIS, ukaguzi unashauri mambo yafuatayo:-

- Wizara ya Afya inashauriwa kurasmisha usimamizi wa mfumo huu wa ZUPS MIS kwa kumteuwa kwa barua afisa wa TEHAMA atakayekuwa na jukumu la kuusimamia mfumo kwenye usanidi, mipangilio, usimamizi wa sera za nywila n.k na kuhakikisha kwamba msimamizi huyu hana uwezo wa kuingiza taarifa kwenye mfumo (read only access). Kwa ajili ya kuhakikisha kuwa


kuna matumizi endelevu ya mfumo ni vyema kama msimamizi huyu akawa na msaidizi wake ambaye pia atakuwa na majukumu yake tofauti ya yale ya msimamizi mkuu.

- Kusimamia na kudhibiti kikamilifu zoezi la kutengeneza watumiaji ndani ya mfumo wa ZUPS MIS ambapo inashauriwa kuweka fomu maalumu itakayo idhinishwa kwa kusainiwa na mtendaji mkuu wa Idara au Kitengo ambacho mtumiaji anatokea kabla ya kutengezwa kwenye mfumo, fomu hii ni vyema ikaainisha wajibu na majukumu ya kila mtumiaji ambayo yatakuwa ni sambamba na "job description" za mtumiaji husika ambazo hazikiniani na miongozo ya udhibiti kwenye TEHAMA. Hatua hii inatarajiwa kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la watumiaji kutengenezwa zaidi ya mara moja kwenye mfumo na wakati mwingine wanakuwa na majukumu tofauti au majukumu yanayofanana.
- Pia, ukaguzi unaishauri Wizara kufanya uhakiki wa taarifa za Masheha ili kubaini Masheha waliomaliza muda wao na kuwaondoa kwenye mfumo.
- Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka utaratibu wa kupata taarifa za mara kwa mara za mabadiliko ya Masheha kutoka ofisi za Wakuu wa Mikoa angalau kila baada ya miezi 3 na kuzihuwisha taarifa hizo kwenye mfumo wa ZUPS MIS.
- Kufanya mapitio ya Sera na taratibu zake kwenye eneo hili la ufikiaji wa mfumo na usimamizi wake ili kubaini udhaifu uliopo kama ilivyobainika kwenye mfumo huu na kuchukuwa hatua stahiki za kufanya maboresho kwa mujibu wa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

10.11.1.12 Kutozingatiwa kwa usahihi wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba waingiza taarifa za usajili wa Wazee kwenye mfumo hawazingatii usahihi wa taarifa zinazolingizwa kwenye baadhi ya "fields" zilizopo kwenye fomu za usajili ndani ya mfumo, miongoni mwa taarifa zinazolingizwa bila ya kuzingatia umakini ni pamoja na nambari ya kitambulisho cha Taifa na Mtaa anaishi Mzee. Kuingizwa baadhi ya taarifa za Wazee ambazo sio sahihi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini.

Picha Nambari 6: Kutozingatiwa kwa usahihi wa uingizaji wa taarifa katika Mfumo



Hali hii inaweza kusabibisha ugumu kwenye zoezi la uhakiki wa Wazee ikiwa kama taarifa zao za makaazi na utambulisho hazijakamika ama zimeingizwa bila kuzingatia usahihi. Athari nyengine ni pamoja na kutopata taarifa sahihi za ujumla za Wazee kwa kuangalia vigezo mbalimbali kama vile eneo la makaazi (mtaa), aina ya kitambulisho, umri, n.k. ambapo Wizara itashindwa kufanya tathmini ya haraka na kuchukuwa hatua stahiki kwa kutumia taarifa zilizomo kwenye mfumo na hivyo kuondoa utegemezi wa TEHAMA katika kuleta tija na ufanisi kwenye kutoa huduma kwa jamii.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa taarifa sahihi za Wazee kupitia mfumo ukaguzi unashauri Wizara kuweka kwenye mfumo utaratibu utakaolazimu uwepo wa watu angalau wawili kwenye zoezi la kuingiza taarifa za usajili wa Wazee ambapo mmoja ataingiza taarifa na mwengine atathibitisha na kuidhinisha taarifa hizo kwa kuhakikisha kwamba ziko sahihi katika kila hali kabla ya kwenda hatua ya kuprinti fomu za "Eligible".
- Kwa kuwa vitambulisho vinavyotambulika kwenye Sheria ya Wazee Nambari 2 ya mwaka 2020 ni kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na Cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo ya kuzaliwa ambapo, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na Cheti cha kuzaliwa taarifa zote zimo kwenye mifumo ya kielektroniki ya Serikali, ukaguzi unashauri Wizara kwa kushirikiana na mtoa huduma ifanye "integration" na mifumo hiyo kama walivyokubaliana kwenye mkataba baina ya Wizara na Mtoa huduma, sehemu "4.0 Users Requirements" Kipengele cha 4 "Link/ communicate with other systems (like ZANID, Birth & Death registration etc.) for information verification or any other purpose that may apply" ili kwamba taarifa zote za Wazee ziwe zinatoka kwenye

kanzidata za Serikali ambazo tayari ilishazikusanya kwa kutumia fedha na muda mwingi ili kurahisisha zoezi la usajili wa Wazee kwa kutumia taarifa ambazo ni sahihi na zinapatikana kwa wakati.

10.11.1.13 Kutotumika kwa alama za vidole katika kufanya malipo kwa wazee.

Ukaguzi umebaini kwamba ulipaji wa Pensheni jamii kwa Wazee unafanyika bila ya kutumia alama za vidole kwa Wazee ambao alama za vidole vyao zimo kwenye mfumo, katika jitihada za kuelewa chanzo udhaifu huu ukaguzi ulifahamishwa kwamba inachangiwa na changamoto zinazojitokeza kwa baadhi ya Wazee ambao alama za vidole vyao hazisomeki vizuri kwenye vifaa vinavyotumika kufanya utambuzi wakati wa malipo hali inayochangiwa na mfumo wa maisha kwa Wazee wetu walio wengi na umri wao pia.

Kwa kuwa lengo na nia ya kutumia alama la vidole katika utambuzi bado inamashiko kwenye kurahisisha utambuzi wa Mzee au mnufaika wa Pesheni Jamii ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mtoa huduma kuangalia uwezekano wa kutumia njia nyengine za kielektroniki za utambuzi wa Wazee unaoenda sambamba na hali ya umri na mtindo wao wa maisha kama vile utambuzi wa uso (face recognition) au utambuzi wa alama za vidole kwa njia ya kamera ambayo ni bora zaidi na kuitekeleza kwa wakati ili kuhakikisha kwamba malipo yanayofanyika kila mwezi wanalipwa wazee wanaostahili na kuziba mianya iliyopo kwa sasa ya upotevu wa fedha za Serikali.

10.11.1.14 Kutosajiliwa kwa "Point of Sales (POS)" kwenye mfumo wa ZUPS MIS.

Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vinavyotumika katika kusajili Wazee na kutoa stakabadhi za Malipo (receipts) wakati wa malipo kwa Wazee "POS" havijasajiliwa na havitambuliki kwenye mfumo wa ZUPS MIS, hali hii inaondoa udhhibiti wa vifaa hivi kwa kuwa havijulikani na hata taarifa za usajili na malipo ya Wazee zilizomo kwenye vifaa hivi haziwezi kuhusianishwa na kifaa kimoja kimoja na mtumiaji wake.

Kutosajiliwa kwa "POS" ndani ya mfumo kunaweza sababisha matumizi mabaya ya vifaa hivyo ikiwa ni pamoja na kubadilishwa kwa POS zenye taarifa sahihi na POS zisizo na taarifa kabisa au zenye taarifa pungufu kwa kuzingatia ukweli kwamba POS hizi hutumika kufanya usajili na malipo kwa Wazee, jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kwa Serikali na kupoteza taarifa sahihi bila kubainika mtumiaji aliyesababisha tatizo hilo kwa wakati.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuhakikisha kwamba POS zote zinasajiliwa kwenye mfumo kwa haraka iwezekanavyo ili kuondoa hatari iliyopo ya kupoteza taarifa za usajili na Malipo ya Wazee na kushindwa kubaini watumiaji na vifaa vilivyohusika.

10.11.1.15 Uwezo mdogo wa POS katika kuhifadhi taarifa za usajili wa Wazee.

Wizara ilifanya ununuzi wa Vifaa vya Kielektroniki kupitia Mkataba Namba 01/Q/MLEWCH/2018/2019 wenye thamani ya shilingi 42,261,000 baina ya Wizara ya Afya na Kamuni ya Web Technologies (T) Ltd kwa ajili ya kutumika pamoja na mfumo wa ZUPS MIS ambapo miongoni mwa vifaa hivyo ni POS zinazotumika kufanyia usajili na malipo ya Wazee, ambapo katika mkataba huo walikubaliana pamoja na mambo mengine, vipimo (specifications) vya "POS" kuwa "1GB RAM and 8GB Space,

2GB RAM and 16GB Space,” hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba katika POS zilizowasilishwa na Mtoa Huduma zinaonesha kuwa vipimo tofauti na matakwa ya Mkataba ambapo POS zilizopo zina vipimo vya “897MB RAM na 4.13GB Space”.

Hali hii imepelekea kuongeza tatizo la upotevu wa taarifa za Wazee zinazochukuliwa kupitia POS kwa sababu ya uwezo mdogo wa POS hizo katika kufanya kazi usajili na malipo kwa Wazee. Pia, kitendo cha mtoa Huduma kuwasilisha POS zenye vipimo tofauti na vilivyokubaliwa kwenye Mkataba na kupokelewa na Wizara kunaashiria uwezekano wa kutokuwa makini kwa upande wa Wizara kwani Mtoa Huduma alilipwa 100% ya fedha zake.

Ukaguzi unaishauri Wizara kufanya tathmini ili kubaini mapungufu ya utekelezaji wa Mkataba huu kati ya Wizara na Mtoa Huduma na kuchukuwa hatua zinazostahili katika kuhakikisha kwamba maslahi ya Serikali yanapatikana kwenye fedha zilizolipwa kupitia Mkataba huu.

Pia, ili kuhakikisha kwamba tatizo la uwezo mdogo wa POS zinazotumika linatatuliwa ni vyema Wizara ikafanya jitihada za kuwasiliana na Mtoa Huduma kwa kumtaka atimize wajibu wake kwa mujibu wa Mkataba vinginevyo arejeshe Serikalini sehemu ya fedha alizolipwa ambazo ni juu/ zaidi ya POS alizowasilisha Wizarani.

10.11.2 MAMBO MENGINEYO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA UDHIBITI WA UJUMLA WA TEHAMA

Udhibiti wa ujumla wa TEHAMA uliopitiwa kwenye Wizara ya Afya katika Idara ya Ustawi wa Jamii kitengo cha Pensheni Jamii ulibaini mapungufu yafuatayo:-

10.11.2.1 Kukosekana kwa “ICT Steering Committee Charter” na “ICT Steering Committee”.

Kwa mujibu wa miongozo ya uendeshaji wa kamati za TEHAMA iliyotolewa mwaka 2020 na eGA ambayo pia imo kwenye “COBIT 2019”. “ICT steering committee Charter” ni nyaraka inayoelezea uundaji na majukumu ya kamati katika uendeshaji wa TEHAMA kwenye Taasisi, ambapo pamoja na mambo mengine yanayokuwemo kwenye nyaraka hii ni mgawanyo wa majukumu kwa upande wa Idara/ Kitengo cha TEHAMA na majukumu ya Kamati.

“Charter” inaweka bayana shughuli za utekelezaji wa mikakati, mipango na kazi za TEHAMA kuwa chini ya Idara/ Kitengo cha TEHAMA wakati kwa upande mwingine “ICT Steering Committee” ikiwa na majukumu ya kupanga mikakati na mipango ya TEHAMA na kuhakikisha kwamba inakwenda sambamba na malengo na mikakati ya Taasisi, kufanya maamuzi uwekezaji yanayo kwenda sambamba na malengo ya Taasisi, kuhakikisha kuwa taasisi inapata thamani ya pesa (value for money) katika uwekezaji wake kwenye TEHAMA, na kwamba kazi zinazofanywa na Taasisi zinakamilika kwa wakati kwa gharama nafuu (cost effective) na ndani ya budget husika.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara haina “ICT steering Charter” wala “ICT Steering Committee” kinyume na “best practice guidelines” ambapo kufanya hivyo ni kuinyima Serikali haki ya kupata manufaa chanya, tija na ufanisi kwenye uwekezaji unaofanyika kwenye TEHAMA hapa inchini na kupelekea kukosa thamani ya fedha (value for money) ambapo vyote kwa pamoja vinapelekea hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kufanyia kazi udhaifu huu kwa uharaka unaostahili kwa kuanza na uandishi wa muongozo wa uendeshaji wa TEHAMA (ICT steering Charter) na kisha kuunda kamati ya uendeshaji wa TEHAMA kwa kuzingatia “best practice guidelines” zilizopo kwenye TEHAMA.

10.11.2.2 Kutokuwepo kwa makubaliano ya kuhifadhi Seva ya Wizara ZICTIA.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya ilipeleka Seva yake ZICTIA kwa ajili ya kuhifadhiwa (hosting) bila ya kuwa na makubaliano yoyote kimaandishi. Hali hii imesababisha sintofahamu kwenye haki na wajibu wa pande zote mbili ambapo Wizara haijui haki zake na wala haijui wajibu wake kwenye swala hili na kusababisha ugumu katika ukaguzi kwenye eneo hili na malalamiko yanayosababishwa na sintofahamu hii.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka makubaliano rasmi na ZICTIA ambapo pamoja na mambo mengine haki na wajibu wa kila upande uzingatiwe kwenye makubaliano hayo, ni vyema, hii ikajumuisha usimamizi wa Seva (Server administration), ufikiaji wa Seva (Server access), usalama na ulinzi wa taarifa zilizomo ndani ya Seva, nakala ya taarifa zilizomo ndani ya Seva, mtandao n.k.

10.11.2.3 Udhaifu katika ushirikiano baina ya Wizara ya Afya na Idara ya Pensheni Jamii katika kuzipatia ufumbuzi changamoto za Mfumo.

Ukaguzi umebaini kusuasua kwa utatuzi wa changamoto za mfumo wa ZUPS MIS kwenye ngazi ya Wizara pamoja na kuandikiwa maombi mengi ya kupatiwa msaada katika kuzitatua changamoto mbalimbali za mfumo huu zinazokikabili kitengo cha Pensheni Jamii kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii iliyunganishwa na Wizara ya Afya mwaka 2020.

Udhaifu huu uliobainika unaweza kuwa miongoni mwa vyanzo vya udhaifu wa usimamizi wa mfumo huu kwa kuwa watumiaji wanajihisi kutopewa nafasi ya muhimu kwenye ngazi ya Wizara.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuboresha mashirikiano na kitengo cha Pensheni Jamii katika kufuatilia na kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zilizopo za mfumo wa ZUPS MIS kwa haraka ili kuinua morali kwa wafanyakazi kwa kitengo hiki kwenye eneo la mfumo.

10.11.2.4 Kukosekana kwa mpango wa kuchukua nakala za taarifa za mifumo (Backup Plan).

Kwenye eneo la udhibiti wa jumla wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA mipango wa kuchukua nakala za mfumo (Backup plan) ni moja wapo ya vitu muhimu vya kuzingatia katika usimamizi wa TEHAMA, huu ni mpango wa kutengeneza nakala za taarifa za mfumo unaowekwa kwenye maandishi kama nyenzo mojawapo ya “system sustainability” kwa lengo kuu la kuhakikisha kwamba taarifa za mfumo zinahifadhiwa pembeni kama nakala na kuleta hakikisho la mfumo kuendelea kufanya kazi au kutoa taarifa zote muhimu bila kuyumba hususani pale inapotokea maafa au shambulio la virusi na kusababisha kuharibika/ kupotea kwa taarifa zilizomo kwenye mfumo.

Mpango huu unatakiwa kuweka bayana ratiba ya kutengeneza nakala, taarifa zipi zichukuliwe nakala, na utaratibu mwengine wote pamoja na wataalamu wanaotakiwa kutengeneza nakala, utunzaji wa nakala, kuzijaribu nakala ili kujiridhisha kama zimekamili na kwamba zinaweza tumika kama inavyotarajiwa n.k.

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara kupitia kitengo cha Pensheni Jamii haina mpango huu jambo linalotilia shaka kuhusu maandalizi ya Wizara katika kupambana ya nyakati ngumu ambazo zinaweza kutokea wakati wowote. Aidha, kutokuwepo kwa mpango huu kumepelekea kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kutegemewa wa kuchukua nakala ikiwa ni pamoja na ratiba ya kuchukua nakala, mtaalamu anayechukua nakala, aina ya nakala zinazotakiwa, namna ya kuzijaribu na kuzihifadhi nakala husika ambapo vyote hivi kwa kutozingatiwa na Wizara vinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizofanyiwa kazi kwa muda wa miaka mingi ambazo zinaweza zisipatikane tena na kuathiri kazi za Serikali na kuleta hasara ya muda na fedha.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kutokea Ukaguzi unashauri yafuatayo:

- a) Wizara iandae mpango wa kuchukua nakala itakayotumiwa na Wizara nzima bila kujali Idara kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa katika usalama wa TEHAMA kwa kutumia wataalamu wake wa TEHAMA na ikilazimu ili kupata mipango bora iwashirikishe wataalamu nje ya Wizara.
- b) Menejimenti ya Wizara ishiriki katika kuidhinisha mpango huo na ifanye ufuatiliaji wa utekelezaji wake angalau mara moja kila mwezi kuhakikisha kwamba unafuatwa ili kupata matokeo yaliyo tarajiwa.
- c) Kwa kuzingatia ukubwa wa Wizara ni vyema Wizara ikafanya usimamizi, uratibu na uendeshaji wa TEHAMA kupitia ofisi moja (centralized management of ICT) ili iweze kuhakikisha kwamba wadau na watumiaji wa mifumo na miundombinu mbalimbali ya TEHAMA ya Wizara wanafuata miongozo, taratibu na kanuni zilizopo tofauti na hali ilivyo sasa ambapo baadhi ya Idara za Wizara zinaendesha shughuli zake za TEHAMA kama Taasisi zinazo jitegemea na kuinyima Menejimenti ya Wizara fursa ya kuelewa kinachoendelea kwa wakati.

10.11.2.5 Kutopatikana kwa ripoti za majaribio nakala za taarifa za mifumo (Backup Testing Reports).

Kwa mujibu wa miongozo na kanuni za kimataifa kama vile ISACA inaelekeza kwamba nakala za taarifa za mifumo zinazochukuliwa zinatakiwa kufanyiwa majaribio angalau mara moja kila mwaka ya kuhakikisha kwamba nakala zinazochukuliwa zinatimia kulingana na taarifa zinazohitajika kwenye nakala husika. Majaribio hayo yakileta majibu mazuri yatahakikisha tija ya taarifa hizo pale zitakapohitajika.

Aidha, ukaguzi haukupata uthibitisho wa kufanyiwa majaribio kwa nakala za taarifa za mifumo ya MS Access Database System na ule ZUPS MIS na wala Wizara haina mpango wala mazingira wezeshi ya kuzifanyia majaribio taarifa hizo. Kwa kutozjaribu taarifa hizo kunainyima Wizara nafasi ya kufahamu kama taarifa zinazochukuliwa kwenye nakala zimekamilika ama zinamapungufu, na wala Wizara haina uhakika kama ikitokea janga kubwa (pandemic) kama vile moto, mafuriko, tetemeko la Ardhi au miundombinu kushindwa kufanya kazi nakala zilizopo zinaweza kutegemewa na kutumika au la.

Ukaguzi unashauri kuandaliwa mpango wa kujaribu nakala na kujumuishwa kwenye mpango wa kuchukua nakala za taarifa za mifumo ya Wizara kama ilivyopendekezwa hapo juu ambapo katika

hili Wizara itatakiwa kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na uwepo wa “test server” na nyenzo nyingine muhimu za kuliwezesha zoezi la kujaribu taarifa hizi angalau mara moja kila mwaka.

10.11.2.6 Ufinyu wa Ofisi ya kitengo cha Pensheni Jamii.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba Kitengo cha Pensheni Jamii kinatumia chumba kimoja cha Ofisi kwa ajili ya watumishi takribani wote ikiwa ni pamoja na Kitengo cha TEHAMA.

Kukosekana kwa chumba cha Ofisi maalum kwa ajili ya shughuli za TEHAMA kunaongeza hatari ya uharibifu, upotevu wa vifaa vya TEHAMA pamoja na kuzorota kwa utoaji huduma kwa watumiaji wa mifumo inayotumiwa wa Pensheni Jamii kwa kazi zake za kila siku kwa sababu ya kukosa usiri unaostahili wakati wa kuwahudumia watumiaji kwa sababu za kiusalama.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba kitengo cha TEHAMA kinapatiwa ofisi kwa ajili ya kuendeshea kazi zao kwa kuzingatia usiri na usalama wa mifumo na vifaa vya TEHAMA vinavyotumika kwenye kazi hizo.

10.11.2.7 Kutokuwepo kwa mpango wa kuendeleza Biashara (Business Continuity Plan).

Kwa mujibu wa miongozo ya “best practices” na Sera za eGaz kifungu cha 4.4.1.2.(d) inazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na miundombinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yatakayojitokeza dhidi ya mfumo husika. Mpango huu unatarajiwa kuelezea ni kwa utaratibu gani huduma zitaendelea wakati wa majanga na hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo zote yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubili au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara haina mpango unaotarajiwa kutoa muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo kupotea na kuonesha nini kifanywe baada ya majanga.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu zilizomo ndani ya mfumo kwa sababu ya kutojua nini kifanyike, hatua gani zichukuliwe na nani kwa wakati gani ili kupata matokeo gani kabla, wakati na baada ya tukio linaloweza sababisha upotevu mkubwa wa taarifa.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuandaa mpango huu kwa mujibu wa miongozo iliyopo na sera za Wakala Serikali mtandao na kwa kuzingatia miongozo na utaratibu unaokubalika kimataifa (best practice guidelines), aidha Wizara ijiwekee utaratibu wa kujaribu mpango huu angalau mara moja kwa mwaka

10.11.2.8 Kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na Maafa (Disaster Recovery Plan).

Mpango wa kukabiliana na maafa / mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan) unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali,

makosa ya kibinadamu, moto au mripuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha Taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake kana kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana.

Mpango huu unaainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina Mpango wa kupona maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume "best practice guidelines" ambazo zinasisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango, kuongeza tija kwa wafanyakazi kwa kuwa wanakuwa wanafahamu nini cha kufanya na kinafanywa na nani kwa wakati gani, kuelewa ukubwa wa kazi zinazotakiwa kufanyika na kuendelea kuwahudumia wateja wa Taasisi husika.

Athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Wizara haina mpango wa kupona maafa na pindi itakapofikwa na maafa hayo ni pamoja na kusababishiwa hasara kwa kushindwa kuendelea na kutoa huduma au kufanya kazi, kupoteza muelekea kwa wafanyakazi kwa kutofahamu nini kifanyike na afanye nani kwa wakati gani na kupoteza tija na ufanisi kazini, kupoteza sifa ya Wizara katika kutegemewa kutoa huduma wakati wote.

Ukaguzi unashauri kutengenezwa mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na ile ya kimataifa ili kuhakikisha kwamba mpango huo unajitosheleza kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

10.11.2.9 Kutokuwepo kwa makubaliano ya msaada wa ufundi wa mfumo wa ZUPS MIS (Service Level Agreement).

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya haina makubaliano ya kupata msaada wa kiufundi na mtoa huduma wa Mfumo wa ZUPS MIS hali ambayo imesababisha mrundikano wa changamoto nyingi za utendaji wa mfumo kwa muda wa zaidi ya mwaka bila kupewa ufumbuzi ambazo sasa zina athiri utendaji kazi wa mfumo na kuondoa tija na ufanisi uliokusudiwa.

Kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu wa malipo ya Pensheni Jamii kwa Wazee na kwa kuangalia uhalisia uliopo kwamba watumishi wengi waliokuwepo wakati wa utekelezaji wa mfumo huu hawapo tena kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii kwenye kitengo cha Pensheni Jamii jambo ambalo limechangia zaidi changamoto ya uelewa wa namna mfumo unavyofanya kazi kwa watumishi wapya waliopo kwenye kitengo hiki kwa sasa, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuingia makubaliano na Ms. Web Technologies Tanzania Ltd kwa ajili ya kupatiwa msaada wa ufundi (Service Level

Agreement) angalau kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara Afya kwa “business users and IT users”.

Makubaliano haya ni vyema yakajikita kwenye kuwajengea uwezo wa namna mfumo unavyofanya kazi, kutatua changamoto za mfumo huu zilizopo kwa sasa na zitakazojitokeza na kukamilisha kazi ambazo mtoa huduma hakuzikamilisha kikamilifu japo kuwa alilipwa fedha zote.

10.11.2.10 Kukosekana kwa Sera za TEHAMA (ICT Policy).

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina sera za TEHAMA zilizowekwa ili kusimamia taratibu na shughuli zote zinazohusiana na TEHAMA, badala yake shughuli za TEHAMA zinafanywa na kusimamiwa kama inavyoombwa na watumiaji wa mwisho, bila kufuata taratibu na miongozo rasmi inayotakiwa na iliyotengenezwa kulingana na mikakati na mipango ya Wizara na matumizi ya TEHAMA pamoja na miundombinu yake.

Kutokuwepo kwa sera madhubuti za TEHAMA kunaweza kupelekea udhaifu katika usalama, udhibiti, uratibu, usimamizi wa shughuli zote za TEHAMA ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali za TEHAMA, kuongezeka kwa hatari ya usalama na ulinzi wa taarifa za Serikali jambo linaloweza kupelekea upotevu wa taarifa za Serikali au taarifa hizo kuingia mikononi mwa watu wenye nia ovyu na kusababisha madhara kiuchumi na kijamii.

Ukaguzi unaishauri Wizara kupitia Idara ya Pensheni Jamii kuandaa sera za TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala Serikali mtandao na miongozo ya kimataifa kama vile COBIT 2019, AFROSAI-E ambazo zitahidhinishwa na Menejimenti ya Wizara. Aidha, Wizara inashauriwa kuzitumia sera hizo ili kupata matokeo bora ya udhibiti na usimamizi wa TEHAMA ndani ya Wizara. Ni vyema zaidi ikiwa kama Sera hizi zitatumikiwa na Wizara nzima bila kujali Idara.

10.11.2.11 Kukosekana kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site).

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa katika wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kuharibika au kupotea kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilomita 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathirika kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa. Eneo hili linatakiwa kuwa katika hali ya ukamilifu kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina eneo mbadala maalum lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza utendaji kazi kupitia mfumo baada ya matatizo kutokea (Disaster Recovery Site) kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara makubwa kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa "Disaster Recovery Site" Ukaguzi unaishauri Wizara kutengeneza eneo la kuendeleza mifumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kwa uharaka wa kutosha ili kuilinda taarifa mali (information asset) za Serikali ambazo kimsingi zimeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na nguvu katika kuzikusanya, kuzichakata na kuzihifadhi. Eneo hili ni vyema liwe na uwezo wa kutumika na mifumo yote ya Wizara bila ya kujali Idara ili uwekezaji huu uwe na tija na ufanisi.

10.11.2.12 Udhaifu katika utekelezaji wa mkataba wa kutengeneza wa Mfumo wa ZUPS MIS

Baada ya kupitia mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa ZUPS MIS ukaguzi ulibaini uwepo wa utekelezaji hafifu wa baadhi ya vipengele vya mkataba kinyume na matarajio, miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na vifutavyo:-

- i) Kipengele kinachoelekeza kuwa nyaraka za wazee kama vile vyeti vya kuzaliwa, picha, barua na nyaraka nyengine kuhifadhiwa kwenye mfumo jambo ambalo ukaguzi haukuweza kuoneshwa mpaka kukamilika kazi ya ukaguzi huu.
- ii) Kipengele kinachoongelea kuhusu mfumo kutoa taarifa kupitia SMS juu ya usajili wa ndugu au jamaa wa karibu wa Mzee ambae atahitajika kupokea fedha hizo kwa niaba ya Mzee husika ambapo mfumo hautimiza takwa hili.
- iii) Kipengele kinachozungumzia utoaji wa namba za utambulisho wa Wazee hali ambayo haifanyiki kwenye mfumo huu.
- iv) Mfumo kuweza kutumika kuchukuwa maoni na mawazo au malalamiko kutoka kwa wazee na wadau mbali mbali.
- v) Mfumo kuweza kutumia njia mbalimbali za kufanya malipo kupitia mitandao ya simu na Benki.

Pamoja na uwepo wa udhaifu huo katika utekelezaji wa mkataba huu ukaguzi ulibaini kwamba Mtoa huduma alikwisha lipwa asilimia mia (100%) ya gharama za mkataba wakati kazi haijafanyika kwa asilimia zote mia moja. Hali hii imeisababishia hasara Serikali kwa kiwango cha huduma ambayo haikutolewa na mzabuni, athari nyengine pamoja na mfumo kushindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwa kulingana na matakwa ya mkataba jambo ambalo limepunguza tija na ufanisi uliotarajiwa kupataikana kulingana na uwekezaji uliofanyika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya mapitio ya mkataba huu na utekelezaji wake ili kuchukua hatua stahiki za kurekebisha mapungufu yaliyobainika ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Mzabuni anatumia wajibu wake kulingana na makubaliano ya mkataba na kwamba Wizara inatoa ushirikiano kwa Mzabuni kama inavyotakiwa. Aidha, ikiwa Mzabuni hataweza kutekeleza matakwa ya mkataba kikamilifu ni vyema akarejesha sehemu ya fedha aliyolipwa kwa kazi ambazo hakuzitekeleza ili zitumike kutafuta mzabuni mwingine mwenye uwezo wa kutoa huduma hizo.

10.11.3 UKAGUZI WA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA MALIPO YA PENSHENI JAMII – PEMBA

MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

10.11.3.1 Kutokuwasilishwa kwa Bakaa ya fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 38,240,000

Ukaguzi umebaini kuwa jumla shilingi 38,240,000 ni bakaa ya fedha za malipo ya pensheni ambazo hazikurejeshwa katika mfuko Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miezi kumi na moja (11) kuanzia Januari 2021 hadi Novemba 2021 ambapo kwa mujibu wa muongozo wa ulipaji wa malipo ya pensheni jamii unaelekeza kwamba bakaa ya fedha inapaswa kurejeshwa katika Mfuko mkuu wa Serikali baada ya kupitiwa na muda wa miezi mitatu.

Uwepo wa bakaa ya fedha iliyopitiwa na muda bila ya kurejeshwa katika Mfuko mkuu wa Serikali kunaweza kukapelekea upotevu wa fedha za Serikali pamoja na kufanyika kwa matumizi yasiokusika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. **Kiambatisho Nambari 23 Kinahusika.**

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kwamba unafanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni pamoja namiongozo mbalimbali ili kuepusha ukiukwaji wa taratibu na kufanyika kwa matumizi yasiokubalika ambayo yatapelekea uwepo wa viashiria vinavyohusu ubadhirifu wa fedha na rasilimali za Umma.

10.11.3.2 Kukosekana kwa udhibiti katika matumizi ya mafuta lita 9,628

Katika ukaguzi ulifanyika imebainika kwamba Kitengo cha Pensheni Jamii kimefanya malipo ya mafuta yenye jumla ya lita 9,628 kwa kipindi cha miezi 11 kuanzia Januari 2021 hadi Novemba 2021 kwa ajili ya kazi za ulipaji pamoja na ufuatiliaji wa taarifa za pensheni jamii ambapo mafuta hayo hutolewa kwa wastani wa lita 800 ambayo hutumiwa kwa siku 9 kwa kila mwezi bila ya kuzingatia masafa ya eneo katika utekelezaji wa kazi za Pensheni Jamii ambapo matumizi ya mafuta hayo ni makubwa ukilinganisha na uhalisia wa maeneo yaliopangwa katika ulipaji wa pensheni jamii hivyo kupelekea matumizi ya mafuta yaliokosa udhibiti, **Kiambatisho Nambari 24 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii kutoa mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za pensheni jamii kulingana na masafa ya vituo vinavyofanyiwa kazi hizo ili kuepusha matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali ya mafuta.

10.11.3.3 Kutokuwepo watendaji wenye taaluma ya kusimamia mfumo (IT Technician)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo wafanyakazi walio na taaluma ya Tehama katika Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii Pemba ili kuweza kusimamia utekelezaji wa kazi za ulipaji wa pensheni jamii kupitia mfumo ZUPS hali ambayo inapelekea kukosekana kwa ufanisi katika

matumizi ya vifaa vinavyohusiana na mfumo mzima wa uwendeshaji wa shughuli za pensheni jamii kupitia mfumo huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba kuhakikisha inaweka watendaji wenye uwezo wa kusimamia ipasavyo mifumo ya malipo ya penchi jamii ili kuweza kupatikana kwa ufanisi wa kiutendaji kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa kazi za mifumo iliopo.

10.11.3.4 Malipo ya fedha za Pensheni Jamii kinyume na Muongozo shilingi 77,780,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 77,780,000 zimelipwa kwa ajili ya wasimamizi wa malipo ya pensheni jamii kwa kipindi cha Januari 2021 - Januari 2022 lakini utaratibu wa ulipwaji wa fedha hizo haukufuatwa ambapo imebainika kuwepo kwa dosari mbalimbali katika utaratibu wa ulipaji wa malipo hayo, **Kiambatisho Nambari 25 Kinahusika**. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Uwepo wa maafisa mbalimbali ambao wamelipwa malipo ya zaidi ya inavyostahiki ambapo kiwango stahiki cha malipo kwa siku ni shilingi 20,000.
- Kuwepo kwa maafisa mbalimbali ambao wamelipwa malipo kwa ajili ya huduma ya utoaji wa pensheni lakini maafisa hao hawakupaswa kulipwa malipo hayo.
- Kuwepo kwa maafisa mbalimbali ambao wamelipwa malipo kwa ajili ya huduma ya utowaji wa pensheni lakini maafisa hao hawakuwa na vituo vya kazi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za Serikali ambapo pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

10.11.3.5 Dosari zilizobainika katika taarifa za mfumo wa ZUPS.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa tofauti katika taarifa za mfumo juu ya idadi ya wazee wanaostahiki kufanyiwa malipo ya pensheni pamoja na mawakala mbalimbali walioidhinishwa kwa ajili ya upokeaji wa fedha za pensheni jamii. Katika ufuatiliaji wa taarifa za mfumo wa ZUPS kwa upande wa Pemba dosari mbalimbali ziliweza kubainika ambapo miongoni mwa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Uwepo wa tofauti baina ya idadi ya mawakala katika Mfumo wa ZUPS na idadi halisi ya wazee wanaostahiki kufanyiwa malipo ambapo imebainika kwamba idadi ya mawakala walioidhinishwa kwa ajili ya upokeaji wa fedha imeonekana kuwa kubwa ambayo ni 13,676 ikilinganishwa na idadi ya wazee wanaolipwa 11,423 kwa mujibu wa eligible hivyo kupelekea ongezeko la idadi ya mawakala 2,253 ambao wanatiliwa shaka juu ya uhalisia ya uwepo wao katika mfumo wa malipo.
- Uwepo wa tofauti baina ya idadi ya wazee inayopatikana katika eligible ambayo ni 11,499 ikilinganishwa na idadi ya wazee iliobainishwa katika ripoti ya ujumla ya mfumo wa ZUPS ambayo 11,423 hivyo kupelekea ongezeko la idadi ya wazee 76 ambao wanatiliwa shaka juu

ya uhalisia ya uwepo wao katika mfumo wa malipo. Kufanya hivyo kunapelekea kuingizia hasara Serikali kwa kuendelea kufanya malipo yasioendana na uhalisia (fictitious payments) ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba kufanya marekebisho ya mfumo ili kuimarisha utendaji na upatikanaji wa taarifa sahihi zinazo akisi uhalisia.

10.11.3.6 Dosari zilizobainika katika matumizi ya ving'amuzi (POS)

Ukaguzi umebaini kitengo cha Pensheni Jamii kina jumla ya ving'amuzi 16 ambavyo hutumika kwa ajili ya kufanya malipo, kusajili na kufanya marekebisho katika taarifa za malipo ya wazee. Katika ufuatiliaji wa taarifa kuhusu utumiaji wa ving'amuzi imebainika kwamba kati ya ving'amuzi 16 vinavyotumika ni ving'amuzi 10 na hivyo kupelekea idadi ya ving'amuzi 6 kuwepo bila kutokutumika kutokana na kuwa ni vibovu, vile vile kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana katika matumizi ya ving'amuzi 10 dosari zifuatazo zimebainika:-

- Baadhi ya wazee kufanyiwa malipo ya fedha zao bila ya kuweka uthibitisho wa alama za vidole (fingerprints) kwenye ving'amuzi vinavyotumika wakati wa malipo ya Pensheni.
- Kutokuwepo kwa ufanisi katika matumizi ya ving'amuzi kutokana na uhalisia wa matumizi ya ving'amuzi vilivyopo kupelekea mara kwa mara kushindwa kufanya kazi.

Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kufanyika malipo bila ya walengwa kuwepo au kuwathibitisha ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba kufanya marekebisho katika matumizi ya ving'amuzi ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi zinazo akisi uhalisia wa malipo ya pensheni jamii yanayofanyika.

10.11.3.7 Dosari zilizobainika katika udhibiti wa matumizi ya program na komputa

Utaratibu uliobora (best practice) unaeleza kwamba Taasisi ambazo zinatumia mifumo muhimu ya TEHAMA zinatakiwa kuweka udhibiti na usalama mkubwa wa taarifa ambazo zitahifadhiwa ndani ya mifumo hiyo. Moja kati ya njia imara za kudhibiti na kuweka usalama wa taarifa za kwenye mifumo ni kuweka sera zilizobora katika matumizi ya kompyuta za ofisi pamoja na sera za matumizi ya programu (software) zinazotumika katika kompyuta hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya kompyuta za Idara ya wazee na ustawi Jamii Pemba zina dosari mbali mbali za kiusalama ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizohifadhiwa ndani yake na kupelekea kutokea kwa hatari ya kushambuliwa kwa mfumo mzima wa ZUPS. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Utumiaji wa programu za mfumo wa uendeshaji wa Kompyuta (Operating Systems) ambazo hazina leseni za matumizi na nyengine zimeshapitwa na wakati (Absolute mfano Windows 7,8).

- Utumiaji wa vifaa (laptop,desktop) za mda mrefu ambazo uwezo wake ni mdogo na hivyo kuzorotesha utendaji kazi kwa ufanisi na kuongeza gharama za matengezezo mara kwa mara.
- kutokuwa na ulinzi dhidi ya virusi vya mtandao " Antivirus ".
- kutokuwepo na ulinzi imara wa mfumo wa ZUPS dhidi ya mashambulizi ya mitandao.

Kufanya hivyo kunaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa muhimu za taasisi na kupelekea uharibifu wa mifumo na hivyo kutokupata taarifa zilizokuwa sahihi ambapo ni kwenda kinyume na IT SOP (Standard Operating Procedures) zinazotambulika Kitaifa na Kimataifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba kuweka udhibiti mzuri katika matumizi ya programu za kompyuta ili kupunguza vihatarishi (risk) vinavotokana na uharibifu wa kompyuta pamoja na upotevu wa taarifa za malipo ya pensheni jamii.

10.11.3.8 Kutokuwepo kwa mpango endelevu wa mafunzo ya mifumo.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii Pemba haina mpango endelevu unaohusu kuwapatia mafunzo watendaji wa Idara hiyo kuhusu matumizi sahihi ya mfumo ambapo imebainika kuwa watendaji hao kwa mara ya mwisho waliweza kupatiwa mafunzo katika kipindi cha mwaka 2018 kinyume na matakwa ya kanuni na miongozo ya usimamizi na matumizi ya mifumo.

Kufanya hivyo kunapelekea kuendelea kuwa na watendaji wanaotumia mfumo kwa kufuata maelekezo walioyapata katika kipindi cha muda mrefu uliopita na kwamba utekelezaji mkubwa wa kazi zao unategemea uzoefu walionao bila kuzingatia mabadiliko yanayoendelea kujitokeza siku hadi siku ulimwenguni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba kuandaa mpango endelevu wa mafunzo kwa watendaji wanaohusika na matumizi ya mfumo wa malipo ya Pensheni Jamii ili kuweza kuboresha ufanisi katika usimamizi na matumizi ya mifumo.

10.11.4 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo ya Wizara ya Afya katika kitengo cha Pensheni Jamii kwa Unguja na Pemba.

Aidha, Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Wiza ya Afya, Ustawi Wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa ushirikiano mzuri mliyotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi wetu ujao.

SURA YA KUMI NA MOJA

UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA MAPATO (MUTM) KWA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

11.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Idara Maalum (OR-TMSMIM) imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 121 cha Uanzishwaji wa Idara Maalum na kifungu cha 128 Uanzishwaji wa Serikali za Mitaa OR-TMSMIM.

Taasisi hiyo ina majukumu ya kusimamia Sera, Sheria na Kanuni mbali mbali za Ofisi, Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kudumisha Amani, Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Shehia, pamoja na kukusanya mapato ya Serikali kupitia Serikali za Mitaa.

Katika kutafuta vyanzo vipya na njia bora za kuongeza ukusanyaji na kuimarisha udhibiti wa mapato pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kuongeza tija na ufanisi, OR-TMSMIM ilifikia uamuzi wa kutengeneza mfumo wa kusimamia na kuratibu taarifa za mapato mnamo mwaka 2017 kwa kutumia wataalumu wa ndani ujulikanao kama "MUTM" yaani **M**fumo wa **U**kusanyaji wa **T**aarifa za **M**apato.

Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Mapato unafanya kazi kwenye ngazi ya Serikali za mitaa. Aidha mnamo mwaka 2021 Wizara ilitengeneza toleo jipya la mfumo huo ili kuweza kukabiliana na mahitaji ya kuwasiliana na mifumo mengine (Integration with other system) kama vile mfumo wa ZanMalipo, mfumo wa usajili wa Vitambulisho kwa Wajasiriamali n.k, kwa lengo la kuimarisha na kurahisisha huduma za malipo kwa wananchi pamoja na kuwaondoshea usumbufu unaojitokeza katika kufanya malipo hayo.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa MUTM bado haujaunganishwa na Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali (IFMIS) na kupelekea kutokuwa na uwezo wa kutambua miamala ya fedha zilizohaulishwa kutoka katika akaunti ya makusanyo ya Baraza la Mji Wete kwenda katika akaunti ya matumizi.

Aidha mfumo ulikuwa na lengo la kutoa huduma za malipo kwa kutumia njia za simu na mawakala wa benki, kurahisisha upatikanaji wa huduma karibu ya maeneo ya wananchi, pia kujua usahihi wa fedha zinazolingia katika akaunti za malipo za Halmashauri za Manispaa na fedha zinazokusanywa kupitia mfumo wa MUTM.

Majukumu ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ni kusimamia utendaji kazi kwa mifumo na kwa upande wa Manispaa pamoja na Halmashauri taasisi hizo ndio wenye kuutumia mfumo huo katika utekelezaji wa kazi za makusanyo ya mapato. Hata hivyo kila Manispaa ina uwezo wa kuwasajili watumiaji wa mfumo pamoja na kusajili mashine za POS kwa matumizi ya Manispaa husika.

Mfumo wa MUTM unapatikana kupitia miundombinu ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) na vile vile mfumo wa MUTM ambao ni wa majaribio umewekwa katika Wizara ya Nchi - ORTSMIM kwaajili ya kufanyia majaribio na mafunzo mbali mbali kupitia miondombinu ya Tehama iliyopo Wizarani. Mfumo wa MUTM unatumika kukusanyia mapato kwa kutumia njia mbili kama zifuatazo:-

- a) Ukusanyaji wa mapato kupitia kompyuta.
- b) Ukusanyaji wa mapato kupitia mashine za POS (Point of Sales) ambazo zimeunganishwa na mfumo huo kupitia mtandao.

Kwa mfumo wa MUTM wa awali, Afisa anaekusanya mapato kwa kutumia POS au kompyuta huingiza taarifa za makusanyo kutoka kwa mteja mmoja mmoja kwa kuzingatia chanzo cha mapato ambapo mwisho wa baada ya kumaliza muda wa kazi mkusanyaji anatakiwa kufunga kazi kupitia mfumo jambo ambalo linapelekea mfumo kutengeneza nambari ya Udhibili (Control Number) inayolingana na makusanyo yote ya siku husika na kutakitakiwa mapato hayo kuyapeleka benki kwa kila siku bila ya kuchelewesha.

11.1 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi kama anavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha Sheria Nambari 11 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

11.2 MALENGO NA UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata hakikisho na kujiridhisha kwamba OR-TSMIM ina ulinzi na udhibili imara katika miundombinu iliyowekwa, insafrisha na kuhifadhi taarifa zake kwa usalama na uadilifu na kwamba vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi katika matumizi ya TEHAMA kwa taasisi hiyo.

Malengo mengine ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya OR-TSMIM ni kama yalivyoainishwa hapo chini:-

- a) Kubainisha ufuatishwaji wa sheria, kanuni, sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa.
- b) Kufanya tathimini ya udhibili wa mifumo na udhibili wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.
- c) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.

- d) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- e) Kubainisha kama uwekezaji katika teknolojia ya TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.
- f) Kubainisha kama OR-TMSMIM ina mipango stahiki katika usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA.

11.3 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya kitaifa na ya kimataifa kama vile eGaz, eGA, ISACA, COBIT, AFROSAI-E n.k.

Katika kukagua mifumo ya OR-TMSMIM ukaguzi ulitumia njia mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini.

- a) Kupitia sheria, kanuni, sera na miongozo mbalimbali
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kuupitia mfumo wa MUTM
- c) Kupitia sera na miongozo ya usimamizi, wendeshaji matumizi ya TEHAMA inayotumiwa na OR-TMSMIM.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika upatikanaji wa mifumo pamoja na vifaa vinavyotumika katika zoezi la ukusanyaji wa mapato
- e) Kupitishwa kwenye mifumo ya MUTM ili kuelewa utendaji kazi wake
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti yaliyomo katika mifumo ya TEHAMA.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano na watumiaji wa Mifumo ya MUTM.
- i) Kutembelea Manispaa mbali mbali za Unguja na Pemba ili kubaini changamoto za Mifumo hiyo.
- j) Kufanya kikao cha kuanza kazi ya ukagu na kumaliza pamoja na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi.

11.4 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA MUTM

11.4.1 Muhtasari wa dosari katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ

Kwa upande wa OR-TMSMIM ukaguzi ulibaini kukosekana kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kutengeneza mfumo wa MUTM, kutokuwepo kwa bajeti ya kitengo cha TEHAMA, Mfumo kushindwa kutoa baadhi ya ripoti muhimu za makusanyo ya mapato, mfumo kutoa taarifa zisizo sahihi kwenye ripoti mbalimbali, kutokufanya kazi kwa baadhi ya moduli kwenye mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti kwenye mfumo wa MUTM,

kutokuwepo na daftari maalum (issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo, kukosekana kwa muongozo rasmi wa vigezo vya POS, kutozingatiwa kwa utaratibu wa kutengeneza mifumo (system development life cycle), kufanywa uimarishwaji wa mfumo bila ya kupeleka pendekezo kwa wakala wa serikali mtandao, kutokuwepo kwa mikakati ya tehama, kukosekana kwa sera za Tehama na kutokufanyiwa majaribio nakala za taarifa za mfumo (backup data restoration test).

Aidha, ilibainika kwamba Wizara haina Mipango ifuatayo ikiwemo kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan) na kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na maafa (Disaster Recovery Plan), mpango wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo (System Change Management Plan) mipango kazi ya TEHAMA na mpango wa kutengeneza nakala za taarifa za mfumo (Backup plan).

kutokuwepo kwa ripoti za nakala za taarifa za mfumo (backup report), kukosekana kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (disaster recovery site/off site), kukosekana nyaraka inayoonesha mfumo kufanyiwa majaribio na watumiaji (user acceptance test document), matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

11.4.2 Muhtasari wa Dosari katika Baraza la Manispaa ya Mjini

Baadhi ya dosari zilizobainika katika Baraza la Manispaa ya Mjini ni pamoja na ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki, udhibiti hafifu wa ufikiaji wa mfumo pamoja na vifaa vyengine vya Tehama (user access control), kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation), uongozi kutokushiriki kikamilifu katika kufuatilia matumizi ya mifumo, kutokamilika kwa usajili wa POS na wanaokusanya mapato, kukosekana na daftari maalum (issue register) kwa ajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti (control numbers), matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

11.4.3 Muhtasari wa dosari katika Manispaa ya Magharibi 'A'

Baadhi ya dosari zilizobainika katika Manispaa ya Magharibi 'A' ni pamoja na kutokamilika kwa usajili wa POS na wanaokusanya mapato, kukosekana na daftari maalum (issue register) kwa ajili ya kusajili changamoto za mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti kwenye mfumo wa MUTM, kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation), uwelewa duni wa mfumo wa MUTM kwa watumiaji walio wengi, kukosekana kwa tovuti ya taasisi kwaajili ya kutoa taarifa za huduma zinazotolewa na baraza, matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

11.4.4 Muhtasari wa dosari katika Baraza la Mji Chake Chake

Baadhi ya dosari zilizobainika katika Baraza la Mji Chake Chake ni pamoja na kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato katika mfumo wa MUTM, kukosekana na daftari maalum (issue register) kwa ajili ya kusajili changamoto za mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti (control numbers), matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali pamoja na dosari katika mfumo wa taarifa za leseni za biashara kwa katika Wilaya ya Chake Chake.

11.4.5 Muhtasari wa Dosari katika Baraza la Mji Wete

Baadhi ya dosari zilizobainika katika Baraza la Mji Wete ni pamoja na kukosekana kwa taarifa muhimu katika mfumo wa MUTM, kukosekana na daftari maalum (issue register) kwa ajili ya kusajili changamoto za mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti (control numbers) pamoja na matumizi ya program uhuru "free anti-virus, free os, ms office" katika kompyuta za taasisi pamoja na matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

11.4.6 Muhtasari wa Dosari katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni

Baadhi ya dosari zilizobainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni pamoja na kukosekana kwa taarifa muhimu katika mfumo wa MUTM, kukosekana na daftari maalum (issue register) kwa ajili ya kusajili changamoto za mfumo, udhaifu wa udhibiti wa utengenezwaji na matumizi ya nambari za udhibiti (control numbers), matumizi ya program uhuru "free anti-virus, free os, ms office" katika kompyuta za taasisi pamoja na matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

11.5 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUMO WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA MAPATO (MUTM)

11.5.1 OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa MUTM kwa OR-TMSMIM dosari mbali mbali zilibainishwa na kutolewa athari pamoja na mapendekezo kwa uongozi wa ofisi ili kuweza kuimarisha utendaji kazi wa mfumo, watumiaji wa mfumo pamoja na miundombinu ya TEHAMA inayotumika katika mfumo huo. Baadhi ya dosari zilizobainikani kama zifuatazo:-

11.5.1.1 Kukosekana kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kutengeneza mfumo wa MUTM

Ukaguzi umebaini kwamba OR-TMSMIM haina kumbu kumbu za gharama zilizotumika kwenye utengenezaji na utekelezaji wa mfumo wa MUTM kwa matoleo yote mawili ambayo ni toleo la kwanza na toleo jipya linalotumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kutokuwepo kwa nyaraka zenye kuonyesha kumbu kumbu za gharama za malipo ya mfumo ni kwenda kinyume na matakwa ya miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa kwenye utengenezaji wa mfumo ya kielektroniki pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake za mwaka 2021.

Udhaifu kwenye utunzaji wa kumbu kumbu za gharama halisi za utengenezaji na utekelezaji wa mfumo wa MUTM unaweza kutumika kama ni mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za umma, aidha, hali hii inaweza kupelekea kupungua kwa hadhi ya mfumo ambayo inatengenezwa na wataalamu wa ndani kutokana na kutokujulikana kwa thamani yake na kupelekea kushindwa kuingizwa kwenye daftari la mali za Serikali (Asset Register) jambo ambalo linaweza kupelekea kuinyima fursa Serikali ya kupata tathmini ya maamuzi yaliyofanywa ya kutengeneza mfumo

husika kwa kutumia wataalamu wa ndani yakilinganishwa na maamuzi ya kununuwa mifumo katika kuangalia gharama.

Ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais TMSMIM kuhakikisha kwamba inakusanya taarifa zote za matumizi halisi (actual expenditures) yaliowahi kufanyika na yanayoendelea kufanyika kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa MUTM kuanzia kwenye kuandaa mikakati, mipango kazi, kukusanya na kuratibu mahitaji ya biashara na watumiaji, kununua miundombinu (mtandano, vifaa na programu), utengenezaji wa mfumo, mafunzo, usaidizi wa kutumia mfumo (Go Live Support) na kuendelea kutoa msaada kwa watumiaji wa mfumo (implementation support) ili kuweza kujua thamani halisi ya mfumo huo kuanzia toleo la kwanza hadi toleo la pili.

Aidha, kwa lengo la kubaini ufanisi wa uliopatikana kwenye mipango dhidi ya matumizi ya fedha za umma kwenye eneo la mfumo huu wa MUTM ukaguzi unashauri kufanyike ulinganifu wa bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya kazi ya kutengeneza mfumo wa MUTM dhidi ya matumizi halisi ili OR-TMSMIM iweze kupata tathimini hiyo na kuweza kuboresha maamuzi yake siku zijazo.

11.5.1.2 Kutokuwepo kwa bajeti ya Kitengo cha TEHAMA

Bajeti ni mchakato wa kuweka mipango ya mapato na matumizi ambayo kwa ujumla inachangia kupatikana kwa tija kwenye usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, inasaidia mgawanyo sahihi wa rasilimali fedha kwenye taasisi, kurahisisha upimaji wa ufanisi wa taasisi, kuwezesha ufuatiliaji (monitoring) wa utendaji kazi wa taasisi, kusaidia uwekaji wa malengo, kuboresha ufanyaji wa maamuzi na kuongeza hamasa kwa wafanyakazi.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha TEHAMA hakina bajeti kwa ajili ya kazi za TEHAMA zinazofanyika Wizarani ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kwenye uendeshaji wa TEHAMA. Hali hii inaweza kupelekea kuzorota kwa kazi za kitengo cha TEHAMA kwa kukosa uhuru wa kuweka mipango na kuitekeleza kwa wakati, kushindwa kupima ufanisi wa kitengo kwenye mipango dhidi ya utekelezaji na kudhoofisha ufanisi wa watumishi wa kitengo cha TEHAMA.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuhakikisha inaweka utaratibu utakaokiwezesha kitengo cha TEHAMA kuwa na bajeti yake kwa kuzingatia utaratibu wa kuandaa bajeti Serikalini.


11.5.1.3 Mfumo kushindwa kutoa baadhi ya ripoti muhimu za mapato.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka OR-TMSMIM inaeleza kuwa mfumo wa MUTM mpya unauwezo wa kuonesha taarifa za makusanyo kwa siku, wiki, mwezi, robo mwaka, mwaka na kipindi chochote kinachohitajika. Ikiwa kwa mkusanyaji, Zoni au vyanzio vya mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa MUTM unaudhaifu mkubwa wa kutoa baadhi ya ripoti muhimu za mapato kwa vyanzo tofauti. Mfumo umeshindwa kutoa ripoti za mapato ikiwemo ripoti za kila mwezi, ripoti za kila chanzo cha mapato, ripoti ya kila mkusanyaji kwa Zoni, n.k hali hii imepelekea kukosekana kwa taarifa usahihi za mapato halisi jambo ambalo linaweza kusababisha kurudisha nyuma hamasa na morali kwa wakusanyaji wa mapato, mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kupanga mipango yenye tija katika ukusanyaji wa mapato kwa kukosa kuwa na taarifa sahihi za hali ya ukusanyaji kwa kipindi kilichopita ili kufanya ulinganifu, kukosekana kwa kumbu


kumbu za kiwango cha fedha zilizokusanywa na kusababisha udhaifu kwenye uwazi na uwajibikaji, kudhoofisha jitihada za kutegemea TEHAMA katika kurahisisha kazi na upatikanaji wa huduma kwa umma na kuathiri ufanyaji wa maamuzi sahihi na kwa wakati.

Picha 1: Kinaonesha taarifa za mapato zisizo na uhalisia kwa kila chanzo ukilinganisha na fedha taslimu zilizokusanywa benki na jumla ya mapato na makadirio pia kuwa sio sahihi.



#	Chanzo Kikuu	Mwaka wa bajeti	Makadirio	Mapato
5	MAZAO YA BAHARINI	01-07-2021 - 30-06-2022	1,500,000.00/=	95,716,000.00/=
12	MAZAO YA HISITU	01-07-2021 - 30-06-2022	85,500,000.00/=	95,716,000.00/=
15	MAUZAJI YA MAZAO NA NICHE	01-07-2021 - 30-06-2022	10,000,000.00/=	95,716,000.00/=
20	VYETI VYA MAZAO	01-07-2021 - 30-06-2022	26,970,000.00/=	43,546,500.00/=
43	VYETI VYA MAZAO	01-07-2021 - 30-06-2022	24,100,000.00/=	52,297,000.00/=
50	ADA YA VYETI VYA MAZAO	01-07-2021 - 30-06-2022	10,000,000.00/=	28,305,500.00/=
63	HUDUMA ZA BIDHAA NA MAZAO	01-07-2021 - 30-06-2022	1,550,000.00/=	290,247,600.00/=
	Jumla		4,066,905,000.00	7,585,795,800.00

Picha 2: Kinaonesha vyanzo tofauti vya mapato na mapato yaliyopatikana kutokuwa na uhalisia, jumla ya mapato na makadirio kutokuwa sahihi.



#	Chanzo Kikuu	Mwaka wa bajeti	Makadirio	Mapato
1	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	15,000,000.00/=	870,742,800.00/=
2	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	15,000,000.00/=	870,742,800.00/=
3	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	533,000,000.00/=	870,742,800.00/=
14	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	18,700,000.00/=	95,716,000.00/=
52	USHURU WA USAFIRISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	109,550,000.00/=	28,305,500.00/=
	Jumla		4,066,905,000.00	7,585,795,800.00

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kufanya jitihada za upitiaji wa kina wa mfumo mzima kwenye upande wa ripoti mbali mbali zinazotarajiwa kutolewa na mfumo kwa kuzingatia mahitaji ya biashara na watumiaji na kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zilizopo kwa sasa ili mfumo uweze kuleta tija katika kazi ya kukusanya mapato.

11.5.1.4 Kutokuwepo kwa daftari maalum (Issue register) kwa ajili ya kusajili mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais – TSMIM haina daftari/ jukwaa maalum la kusajili mapungufu na changamoto za mfumo kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika. Daftari hili linaweza kuwekwa kidijitali ambapo watumiaji wa mfumo wanasajili changamoto na matatizo mbali mbali ya mfumo kwa lengo la kurahisisha mawasiliano na wataalamu wa mfumo ili kupatiwa ufumbuzi kwa haraka na kuweka kumbu kumbu za changamoto na ufumbuzi wake ili kuwa na udhibiti madhubuti na matumizi endelevu ya mfumo wa MUTM.

Ukaguzi unashauri kuwekwa utaratibu maalum kama vile daftari au mfumo wa utaokao hakikisha kwamba watumiaji wa mfumo wanaweza kusajili changamoto za mfumo wakati wote na kwamba wataalamu wa mfumo wanapata nafasi ya kuzipitia na kuzipatia ufumbuzi changamoto zote kwa uharaka iwezekanavyo kwa kuzingatia athari za "issue" yenyewe kwenye kazi za ukusanyaji wa mapato na utoaji wa ripoti mbali mbali. Aidha, matokeo yatakayotolewa na wataalamu yanatakiwa kuwekwa kwenye daftari au mfumo uliowekwa ili kutunza kumbu kumbu zote zenye lengo la kuboresha mfumo.

11.5.1.5 Kukosekana kwa muongozo rasmi wa vigezo vya POS

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina muongozo rasmi wa vigezo vinavyokubalika vya mashine za POS ambazo zinaingiliana na mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa MUTM. Hali hii inapelekea harasa kwa Serikali pale ambapo Halmashauri zinanunua POS kwa utashi wake na kubainika kwamba POS hizo haziendani na matakwa ya mfumo wa MUTM, kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri ambazo hazina POS za kutosha zinazokidhi vigezo, mfumo wa MUTM kushindwa kuisaidia Serikali kwenye kurahisisha mchakato wa ukusanyaji wa mapato na kuleta tija.

Ukaguzi unashauri Wizara kuandaa muongozo rasmi wa vigezo (specifications), matumizi na usimamizi wa POS na kuusambaza kwenye mamlaka zote za Serikali za mitaa na kufuatilia utekelezaji wake na kuhakikisha kwamba unaleta tija na kuongeza ufanisi wa makusanyo ya mapato kupitia mfumo wa MUTM kwa kila Halmashauri.

11.5.1.6 Kutozingatiwa kwa Miongozo ya Viwango bora vinavyokubalika kama vile "Software Development Life Cycle – SDLC" katika utengenezaji wa mifumo

"Software Development Life Cycle (SDLC)" ni mpangilio wa kimantiki (logical process) unaotumiwa na wachambuzi na wasanidi wa mifumo ya kielektroniki (system analysts and developers) kujenga mifumo. "SDLC" inapelekea kupata mifumo yenye ubora wa juu inayokidhi au kuzidi mahitaji ya biashara na yale ya watumiaji na kwamba mifumo husika inakamilika ndani ya wakati na bajeti husika ikileta tija na ufanisi. Mifumo inayotengenezwa kwa kuzingatia "SDLC" pia huwa na gharama nafuu za matengenezo na maboresho ambazo zinahakikisha matumizi endelevu ya mfumo (cost effective maintenance and enhancements).

Ukaguzi umebaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa MUTM haukuzingatia miongozo ya "SDLC" jambo ambalo limepelekea mfumo huu kushindwa kukidhi haja za biashara na mahitaji ya watumiaji tangu toleo la kwanza mpaka kwenye toleo la sasa linalotumika hali inayopelekea matumizi hafifu ya mfumo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, mfumo kushindwa kutoa ripoti mbali mbali zinazotakiwa na watumiaji, mfumo kutoleta tija na ufanisi uliotarajiwa. Aidha, kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kutegemea TEHAMA ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama kwa Serikali, udhaifu huu ambao ungeweza kuepukika kama miongozo ya "SDLC" ingezingatiwa tangu mwanzo ya utengenezaji wa mfumo huu.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuzingatia "best practice guidelines" kama vile "SDLC" katika utengenezaji wa mifumo yote ya kielektroniki ili kuisaidia Serikali kuepuka athari mbali mbali kama zilivyojadiliwa hapo juu na kuongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wananchi na kuongeza makusanyo ya Serikali. Aidha, Wizara inashauriwa kufanya mapitio (review) ya utengenezaji wa mfumo wa MUTM kwa kuzingatia muongozo wa "SDLC" ili kubaini mapungufu yaliyopo na kuyafanyia kazi kwa uharaka iwezekanavyo kwa lengo la kuboresha mfumo.

11.5.1.7 Mfumo kushindwa kutoa taarifa sahihi kwenye baadhi ya ripoti

Nyaraka ya mfumo wa MUTM inayoitwa "**Training introduction**" imeainisha ripoti mbali mbali za mfumo zinazoweza kutolewa kwenye mfumo. Ili kupata taarifa sahihi kwenye ripoti mbali mbali ni lazima kuwepo na uingizaji wa taarifa sahihi (data entry) kwenye mfumo, ambapo katika mfumo wa MUTM waingizaji wa taarifa hizi ni Manispaa husika. Japokuwa inawezekana kinachoingizwa kuwa sahihi lakini kinachotoka kupitia ripoti mbali mbali kisiwe sahihi kutegemeana na visababishi vyengine kama vile kanuni (formula) iliyopo kwenye ripoti husika ambayo inaweza isiwe sahihi na kusababisha taarifa zilizopo kwenye ripoti kutokua sahihi.


Katika kupitia mfumo wa MUTM ukaguzi umebaini kwamba ripoti ya **Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka** inayoonesha taarifa za makusanyo kutoka kwenye vyanzo vyote vya mapato za Manispaa zote, kuwa jumla ya makusanyo halisi kwa kipindi cha kunzia Julai mosi 2021 hadi tarehe 18 Januari 2022 ni shilingi bilioni saba milioni mia tano thamanini na tano laki saba tisini na tano mianane **(TZS 7,585,795,800)** ambazo zinatarajiwa kuwa ni fedha taslimu zilizowekwa benki ukifananisha na ripoti ya **Namba za Udhhibiti/Control Number** zilizolipwa inayo oneshwa jumla ya makusanyo kwa kipindi kama hicho kutoka kwenye vyanzo vyote vya mapato ya Manispaa zote ni shilingi bilioni moja milioni mia mbili thalathini na tano laki saba sabini na moja mia tisa kumi na tatu **(TZS 1,235,771,913)**.

Ripoti hizi mbili zinatakiwa kutoa taarifa zinazofanana zikiangaliwa kwa kipindi kimoja kwani zote zinatakiwa kutoa taarifa za makusanyo halisi ya fedha japo katika uhalisia ziko tofauti kama inavyoonekana hapo juu ambapo kuna tofauti ya shilingi bilioni sita milioni mia tatu hamsini na ishirini na tatu elfu mia nane thamanini na saba **(TZS 6,350,023,887)**.

Athari moja wapo ni kurudisha nyuma jitihada za Serikali za kuwekeza katika mifumo ya TEHAMA kwakua inaonesha kutokutegemeka (unreliable) na kutokuaminika kwa mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi sahihi. Pia, inapunguza morali kwa watumiaji wa mfumo katika kuutumia mfumo ili kurahisisha kazi zao za

kila siku kwani mfumo hauna uwezo wa kutoa taarifa sahihi za makusanyo kwa vipengele tofauti kama vile ripoti kwa vyanzo, ripoti kwa mkusanyaji.

Picha 3: inaonesha Ripoti ya orodha ya mapato kwa mkusanyaji kutofautiana na jumla ya mapato husika.



Ukaguzi unashauri yafuatayo kwa Wizara OR-TSMIM: -

- Kutengeneza mpango kazi utakaoweka utaratibu mzuri na muda wa kukusanya, kurikodi na kuzipatia ufumbuzi changamoto/matatizo yote ya MUTM mpya ndani ya kipindi kifupi ili kuepusha madhara kama ilivyoainishwa hapo juu.
- Kufuata viwango bora vinavyokubalika (best practise) vya utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA ambavyo vinataka kuwepo kwa hatua mbali mbali kama vile ukusanyaji wa mahitaji ya watumiaji, ushirikishwaji wa watumiaji katika kuthibitisha mahitaji yao, kutengeneza mifumo kwa viwango vinavyokubalika, kutumia wataalamu wenye sifa zinazostahiki katika kutengeneza mifumo, kutoa mafunzo toshelevu na endelevu kwa watumiaji wa mifumo, kuijaribu mifumo kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji kabla ya kuidhinisha matumizi ya mifumo husika ili kuhakikisha kwamba inakidhi vigezo, mahitaji na matakwa yaliyowekwa.
- Kuwajengea uwezo toshelevu wataalamu wa mifumo (programmers) katika kutambua viwango (standards) miongozo na Sera mbalimbali zinazosimamia kazi za kihisibu, manunuzi, mishahara, mapato, mali na madeni ili kuhakikisha kwamba mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa katika matumizi yake haikinzani na viwango, miongozo na sera hizo.
- Kutumia muda toshelevu katika kupanga utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA unaozingatia mahitaji kamili ya wakati uliopo na mahitaji ya wakati ujao angalau kwa kipindi kisichopungua miaka 5 wakitilia maanani kasi iliyopo kwenye mabadiliko ya teknolojia ya TEHAMA.


11.5.1.8 Kutokufanya kazi kwa baadhi ya moduli kwenye mfumo wa MUTM

Kwa mujibu wa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika mfumo unatakiwa kufanyiwa majaribio kabla ya kuanza kutumiwa na kuhakikisha kwamba unakidhi mahitaji ya biashara na ya watumiaji, mahitaji haya yanajumuisha ripoti mbali mbali pamoja na moduli zote za mfumo zinazotarajiwa kutumika kwenye kazi za kila siku.

Ukaguzi umebaini kwamba kwenye mfumo wa MUTM kuna baadhi ya moduli ambazo hazifanyi kazi kabisa, na zipo nyengine ambazo zinatoa taarifa zisizo sahihi.

Ukaguzi unaishauri Wizara kuupitia upya mfumo wa MUTM kwa umakini na kuzifanyia marekebisho moduli zote ambazo hazifanyi kazi kama inavyotarajiwa kwa urahaka unaostahili.

Picha 4: Kinaonesha baadhi ya moduli ambazo hazifanyi kazi ipasavyo.



11.5.1.9 Mapungufu katika utengenezaji wa Nambari za Udhibiti (Control Numbers)

Ili kudhibiti makusanyo ya mapato na kuhakikisha kwamba malengo/bajeti za ukusanyaji wa mapato yanaenda sambamba na mapato halisi yanayokusanywa, Serikali iliamua kuanzisha mfumo maalum kwa ajili ya namba za Udhibiti (Control Number) ambazo huunganishwa na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato ikiwa pamoja na mfumo wa MUTM.

Kupitia mfumo wa MUTM, afisa anaokusanya mapato kwakutumia POS au kompyuta huingiza taarifa za makusanyo kutoka kwa mteja mmoja mmoja kwa kuzingatia chanzo cha mapato ambapo mwisho wa siku ya kazi mkusanyaji anatakiwa kuwasilisha makusanyo ya siku hiyo kielektroniki, kitendo kinachopeleka taarifa kwenye mfumo wa mama wa kutengeneza namba za Udhibiti ambazo baada ya hapo kuletwa kwenye mfumo wa MUTM kwaajili ya kuenda kufanya malipo benki.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya namba za Udhibiti zinazotengenezwa kwa utaratibu huo zinaudhaifu katika maeneo yafuatayo: -

Kutokutambulika kwa baadhi ya namba za udhibiti (Control Number) kwenye mfumo wa benki uliunganishwa na mfumo wa namba za udhibiti. Hali hii inatokea pindi ambapo mkusanyaji mapato anapeleka fedha benki kulingana na namba za udhibiti aliyonayo na kugundulika kwamba namba hiyo haitambuliki benki, jambo ambalo linamlazimu kuomba kutengenezwa namba nyengine. Miongoni mwa namba hizi zinabaki kwenye mfumo wa MUTM mpaka muda wake wa malipo kumalizika (expired) wakati mwengine husitishwa mara moja (cancelled).

Udhaifu huu unapelekea kujitokeza kwa athari mbali mbali kadhaa ikiwa ni Pamoja na kupatikana kwa mwanya wa kuziacha namba za udhibiti kumalizika muda wake au kusitishwa namba hizo kwenye mfumo kwa makusudi.

11.5.1.10 Kufanywa uimarishaji wa mfumo (System Upgrade) bila kuzingatia miongozo ya eGAZ.

Uimarishaji wa mfumo (System Upgrade) ni moja kati ya vipengele muhimu vya kuboresha mfumo wa TEHAMA ambapo mchakato huo hutekelezwa kwa kufanywa mabadiliko ya kuongezea vitu katika mfumo kwa lengo la kurekebisha baadhi ya mapungufu, kuimarisha utendaji kazi, kupanua mfumo kwa kuongeza kipengele (feature) na kuboresha udhibiti. Kwa ajili ya ushindani na msukumo uliopo katika soko la mifumo huwa inatokea mifumo kuletwa kwa watumiaji wakati ikiwa na mapungufu au madhaifu kadhaa na wakati mwingine kwa sababu za kutofautiana kwa mazingira yaliyotumika kutengenezewa na kujaribiwa mifumo ukilinganisha na mazingira yanapokwenda kutumika inaweza kusababisha mfumo kushindwa kufanya kazi kwenye mazingira ya watumiaji.

Kwa sababu hizi miongozo na viwango vinavyokubalika (best practice) vinaelekeza kufanyika kwa uimarishaji kwenye mazingira ya majaribio yanayofanana na mazingira halisi ambayo mfumo utatumika kwanza na kuhakikisha kwamba mfumo unafanya kazi kama inavyotarajiwa kabla ya kupelekwa kwenye mazingira halisi, hii inaondoa hatari ya kushindwa kuendelea na kazi za kila siku kama uimarishaji umeleta shida kwenye mfumo kwa namna yoyote ile. Au kama uimarishaji umetambulisha namna tofauti ya kufanya kazi kwenye mfumo kama ilivyokua kabla ya uimarishaji na kuwapa watumiaji nafasi ya kusomeshwa mabadiliko husika kabla ya kuuweka kwenye mazingira halisi. Kutegemeana na sera za mtengeneza mfumo, ipo mifumo ambayo ili mtumiaji apate uimarishaji hana budi kulipia kiasi fulani cha fedha au wengine huwapa watumiaji wa mifumo yao uimarishaji bila gharama.

Hata hivyo, miongozo ya Wakala wa Serikali mtandao Zanzibar wa mwaka 2021 kipengele cha 3(a) kinaitaka taasisi yoyote ya Serikali kuwasilisha pendekezo na umuhimu wa mahitaji ya uimarishaji wa mfumo (System Upgrade) huo kwa wakala wa Serikali mtandao.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara imefanya uimarishaji wa mfumo wa MUTM bila ya kupeleka pendekezo kwa wakala wa Serikali mtandao kwa ajili ya kujua mapendekezo yao, kuwasilisha ripoti ya utekelezaji na kwa ajili ya kufanya majaribio ya mfumo na kuhakikisha unakidhi viwango vinavyotarajiwa na watumiaji wa mfumo

Ukaguzi unashauri kwamba, kabla ya kufanyika uimarishaji wowote wa mfumo Wizara izingatie takwa la Sera na miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao la kupeleka pendekezo la uimarishaji huo kwa Wakala wa Serikali mtandao kwa ajili ya mapitio na kupata idhini ili kupata nafasi ya kufanya tathmini ya manufaa ya uimarishaji ukilinganisha na gharama za uimarishaji huo (cost benefit analysis).

11.5.1.11 Kukosekana kwa Sera za TEHAMA

Sera za TEHAMA ni nyaraka zinazozungumzia matumizi ya vifaa vya TEHAMA na Mifumo ambazo ndani yake zimekusanya miongozo, uthabiti, uwajibikaji, ufanisi na uwazi kuhusu jinsi Taasisi inavyofanya kazi inayoonesha matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA na mifumo, pamoja na sheria za matumizi hayo na adhabu zinazoweza kutolewa kutokana na ukiukwaji wa sheria hizo. Sera hizo

zinapoandaliwa zinatakiwa zizingatie vihatarishi vyote ambavyo vinavyoweza kutokea wakati wa utumiaji wa vifaa hivyo pamoja na mifumo ya TEHAMA kwa wafanyakazi.

Ukaguzi umebaini kwamba OR-TSMIM haina sera za TEHAMA zinazotakiwa kuwekwa kwa kusimamia taratibu na shughuli zote zinazohusiana na TEHAMA, katika matumizi ya teknolojia hiyo, badala yake shughuli za TEHAMA zinafanywa na kusimamiwa kama inavyoombwa na watumiaji wa mwisho au menejimenti ya Mamlaka, bila kufuata taratibu na miongozo rasmi inayotakiwa na mfumo wa teknolojia yenyewe.

Kutokuwa na sera madhubuti za teknolojia hiyo kutapelekea matumizi na udhibiti duni na usimamizi usioratibiwa wa rasilimali za kitengo cha teknolojia ya habari, shughuli zake, utunzaji wa matukio yake, barua pepe na matumizi ya mtandao.

Ukaguzi unashauri Wizara kutengeneza Sera mahususi za kitengo cha TEHAMA Pamoja na sera za wizara ili kuwa na udhibiti na kuboresha utendaji kazi wake.

11.5.1.12 Kutokupepo kwa Mpango Mkakati ya TEHAMA

Kwa mujibu wa ISACA na COBIT 2019 inaelezea juu umuhimu wa uwepo wa Mpango Mkakati wa TEHAMA na kufuatwa ipasavyo ili kuhakikisha uwajibikaji, ufanisi na tija zinapatikana kupitia matumizi ya Tehama kwa lengo la kusaidia kufanikisha malengo makuu yaliyopangwa na taasisi.

Ukaguzi, umebaini kwamba Wizara ya Nchi OR-TSMIM haina mpango mkakati ambao unatoa mwelekeo wa kimkakati wa uwekezaji wa TEHAMA, usawa kati ya malengo ya Taasisi na mipango ya TEHAMA na kuhakikisha kuwa shughuli za TEHAMA zinaleta thamani kwa Taasisi.

Kutokuwepo kwa mpango huo kunaweza kupelekea Wizara kutokuzingatia kwa uwekezaji na mipango ya TEHAMA na kufanya hivyo kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya rasilimali za TEHAMA. Pia kutokuwepo kwa mpango huo kunapelekea kutokujua mipango ya muda mrefu na mwelekeo wa maendeleo ya Taasisi kwa upande wa TEHAMA.

Ukaguzi unashauri uongozi wa OR-TSMIM kuhakikisha kuwa mpango mkakati wa TEHAMA unaanzishwa, unaaandikwa na kupitishwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi kwa maendeleo ya Idara na Wizara kwa ujumla.

11.5.1.13 Kutofanyiwa majaribio nakala za Taarifa za mfumo (backup data restoration test)

Kwa mujibu wa miongozo na kanuni za kimataifa kama vile ISACA inaelekeza kwamba nakala za taarifa za mfumo zinazochukuliwa zinatakiwa kufanyiwa majaribio angalau mara moja kila mwaka ya kuhakikisha kwamba nakala zinazo chukuliwa zinatimia kulingana na taarifa zinazo hitajika kwenye nakala husika. Majaribio hayo yakileta majibu mazuri yatahakikisha tija ya taarifa hizo pale zitakapohitajika.

Ukaguzi umebaini kuwa nakala za taarifa za mfumo wa MUTM hazifanyiwi majaribio yoyote kuhakikisha kuwa zitafanya kazi kwa usahihi pale zitakapohitajika baada ya maafa kutokea katika taarifa halisi za mfumo na wala hakuna mpango maalum wa kufanya mchakato wa backup. Hivyo, ikiwa nakala za taarifa zitakuwa na hitilafu haitokuwa rahisi kubaini hitilafu hizo na jambo

ambalo linaweza kupelekea kutokuwa na msaada wala manufaa yoyote pale yatakapotokea maafa ya kuharibika, kupotea, kufutika katika mfumo.

Ukaguzi unashauri kuwa, ni vyema kuzifanyia majaribio nakala za taarifa za mfumo ili kuhakikisha kuwa zinaweza kuleta tija pale zitakapo hitajika kutumika wakati itakapotokeza hitilafu katika sehemu kuu ya kuhifadhia taarifa.

Kutokuwa na mpango maalum wa kuzifanyia majaribio nakala za taarifa za mfumo huo kunaweza kupelekea kushindwa kufanya kazi kwa taarifa hizo kutokana na kuharibika. hivyo, hazitokuwa na tija yoyote ya uokozi pale mfumo huo utakapokutwa na majanga na kupelekea kupoteza taarifa zake zote zilizoingizwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuandaa mpango maalumu utakaowezesha namna ya kuhifadhi taarifa hizo na jinsi ya kuzifanyia majaribio na kubaini ufanisi wake na hatimae kuandaliwa ripoti maalumu zitakazoonesha matokeo ya majaribio hayo.

11.5.1.14 Kukosekana kwa Mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan)

Kwa mujibu wa Sera za Serikali mtandao kifungu cha 4.4.1.2.(d) inazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na miundo mbinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yatakayojitokeza dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo zote yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaumbile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Nchi ORTMSMIM haina mpango huo unaotarajiwa kutoa muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo kupotea na kuonesha nini kifanywe baada ya majanga.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu zilizomo ndani ya mfumo kwa sababu Wizara kupitia vitengo vinavyohusika, TEHAMA na Watumiaji wa mfumo (ICT and Application team) kutojua nini kifanyike, hatua gani zichukuliwe na nani na wakati gani ili kupata nini kabla, wakati na baada ya tukio linaloweza sababisha upotevu mkubwa wa taarifa kama vile moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, wizi, uharibifu wa miundombinu, matumizi mabaya n.k.

Ukaguzi unashauri Wizara kuandaa mpango huu kwa mujibu wa miongozo iliyopo na sera za Wakala Serikali mtandao na kwa kuzingatia miongozo na utaratibu unakubalika kimataifa, aidha Wizara ijiwekee utaratibu wa kuijaribu walau mara moja kwa mwaka mipango yote inayolenga kulinda taarifa pamoja na miundombinu ya TEHAMA ambayo imeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na juhudi pamoja na jitihada kubwa kuziandaa, kuzichakata na kuzitunza ambazo pia zikiingia mikononi mwa watu wasio na nia njema zinaweza kuleta madhara mengi kiuchumi, kiusalama, na kijamii.

11.5.1.15 Kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na Maafa (Disaster Recovery Plan).

Mpango wa kuendeleza mfumo baada ya maafa/ mpango wa kupona maafa (Disaster Decovery Plan) unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mlipuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha Taasisi kurejeshwa kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake kama kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Mpango huu una ainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejeshwa huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina Mpango wa kupona maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume "best practice guidilines" ambazo zinasisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango, kuongeza tija kwa wafanyakazi kwa kuwa wanakuwa wanafahamu nini cha kufanya na kinafanywa na nani kwa wakati gani, kuelewa ukubwa wa kazi zinazotakiwa kufanyika na kuendelea kuwahudumia wateja wa Taasisi husika.

Athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Wizara haina mpango wa kupona maafa na pindi itakapofikwa na maafa hayo ni pamoja na kusababishiwa hasara kwa kushindwa kuendelea na kutoa huduma au kufanya zaki, kupoteza muelekeo kwa wafanyakazi kwa kutofahamu nini kifanyike na afanye nani kwa wakati gani na kupoteza tija na ufanisi kazini, kupoteza sifa ya Wizara katika kutegemewa kutoka huduma wakati wote.

Ukaguzi unashauri kutengenezwa mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na ile ya kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unajitosheleza kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

11.5.1.16 Mpango wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo (System Change Management Plan).

Mpango wa usimamizi wa mabadiliko ni mpango ambao hutumika kama ramani kwa ajili ya kutoa muongozo ambao Taasisi itachukua ili kutekeleza mchakato wa usimamizi wa mabadiliko. Kwakuwa mabadiliko yataathiri shughuli za utendaji wa mfumo huo, mpango wa usimamizi wa mabadiliko unahitajika ili kutoa muongozo juu ya mtiririko wa kazi na ufanisi juu ya mabadiliko hayo pamoja na matumizi ya zana zitakazotumika. Lakini pia Mpango wa usimamizi wa mabadiliko unalengo la

kuhakikisha kuwa mabadiliko yoyote yatayo fanyika kwenye mfumo iwe ni uimarishaji wa mfumo (system upgrade) au kuhama kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine hayaleti mabadiliko hasi kwenye mfumo huo. Mpango wa usimamizi wa mabadiliko husaidia kudhibiti mchakato wa mabadiliko, na pia kuhakikisha udhibiti katika bajeti, ratiba, upeo, mawasiliano na rasilimali.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina mpango wa kufanya mabadiliko ya mifumo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo iliyo bora ambayo inasisitiza uwepo wa mpango huu kwakuzingatia manufaa yake kwa mifumo.

Kutokuwepo kwa Mpango wa usimamizi wa mabadiliko kunapelekea kutokujua mikakati sahihi ya kuitumia kwenye mabadiliko ya mfumo na jambo hilo linaweza kupelekea kupungua kwa tija na ufanisi kwenye mfumo pamoja na watumiaji wa mfumo, vile vile kunaweza kupelekea kutokujua bajeti ambayo inatakiwa kutumika kwenye kipindi hicho cha kufanya mabadiliko jambo ambalo linaweza kusababisha uchelewaji wa kumaliza kufanya mabadiliko kwenye mfumo pamoja na kusababisha kushindwa kwa mfumo kufanya mabadiliko au kusababisha kuharibika kwa mfumo wote na kushindwa kuutumia tena baada ya kufanya mabadiliko hayo.

Ukaguzi unashauri kwamba Wizara iandae Mpango wa usimamizi wa mabadiliko kwakuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha kuwa mabadiliko yoyote yatakayofanywa na mfumo huo yatakua na tija na ufanisi unaoaminika.

11.5.1.17 Mpango wa kutengeneza nakala za taarifa za mfumo (Backup plan)

Kwenye eneo la udhibiti wa jumla wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA mpango wa kuchukua nakala za mfumo (Backup plan) ni mojawapo ya vitu muhimu vya kuzingatia katika usimamizi wa TEHAMA, huu ni mpango unaowekwa kwenye maandishi wa kutengeneza nakala za taarifa za mfumo kwa lengo la kuzitumia taarifa hizo pale unapotokea uhitaji wa kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na yanapotokea maafa, ikitokea udukuzi wa taarifa, kuvamiwa na virusi katika miundombinu na mfumo unaotumika kila siku na kusababisha kuharibika/ kupotea kwa taarifa zilizomo kwenye mfumo.

Mpango huu unatakiwa kuweka bayana ratiba ya kutengeneza nakala, taarifa zipi zichukuliwe nakala, na utaratibu mwingine wote pamoja na wataalamu wanaotakiwa kutengeneza nakala, utunzaji wa nakala, kuzijaribu nakala ili kujiridhisha kama zimekamilika na kwamba zinaweza kutumika kama inavyotarajiwa au la n.k.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara haina mpango huu jambo linalotilia shaka kuhusu maandalizi katika kupambana ya nyakati ngumu ambazo zinaweza kutokea wakati wowote. Aidha, kutokuwepo kwa mpango huu kumepelekea kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kutegemewa wa kuchukua nakala ikiwa ni pamoja na ratiba ya kuchukua nakala, mtaalamu anayechukua nakala, aina ya nakala zinazotakiwa, namna ya kuzijaribu na kuzihifadhi nakala husika ambapo vyote hivi kwa kutozingatiwa na Wizara vinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizofanyiwa kazi kwa muda wa miaka mingi ambazo zinaweza zisipatikane tena na kuathiri kazi za Serikali na kuleta hasara ya muda na fedha.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kutokea Ukaguzi unapendekeza yafuatayo:

- a) Wizara iandae mpango wa kuchukua nakala itakayotumiwa na Wizara nzima bila kujali Idara na Mabaraza ya Manispaa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa katika usalama wa TEHAMA kwa kutumia wataalamu wake wa TEHAMA na ikilazimu ili kupata mpango bora iwashirikishe wataalamu wa nje ya Wizara.
- b) Menejimenti ya Wizara na Manispaa zake zishiriki katika kuidhinisha mpango huu na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wake walau mara moja kila mwezi kuhakikisha kwamba unafuatwa ili kupata matokeo yaliyo tarajiwa.

11.5.1.18 Kukosekana kwa ripoti za nakala za taarifa za mfumo (Backup report)

Kwa mujibu wa viwango bora (Best Practice) vinazitaka taasisi zenye mifumo kuwa na ripoti maalum unaoelezea jinsi gani nakala za taarifa za mfumo zilivyotolewa kwenye mfumo na wapi zimehifadhiwa nakala hizo lakini pia ripoti zioneshe siku na saa ambazo nakala hizo zilitolewa kwenye mfumo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa hakuna ripoti yoyote iliyoandaliwa kuhusiana nakala za taarifa za mfumo, hivyo hali hii inaashiria kuwa utowaji wa nakala za taarifa za mfumo hauna utaratibu maalum wenye tija kwa serikali. Kushidwa kuwepo kwa ripoti zinazoonesha utolewaji wa nakala hizo kunaweza kusababisha Wizara kutokua na ripoti sahihi za nakala za taarifa za mfumo wa MUTM.

11.5.1.19 Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site)

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa katika wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kuharibika au kupotea kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilomita 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa. Eneo hili linatakiwa kuwa na kamilifu kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza kuchukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara haina eneo mbadala maalumu lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwekwa eneo la kuendeleza utendaji kazi kupitia mfumo baada ya matatizo kutokea (Disaster Recovery Site) kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara makubwa kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa "Disaster Recovery Site" ukaguzi unashauri Wizara ya OR-TMSMIM kutengeneza eneo la kuendeleza mifumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA kitaifa na kimataifa na viwango bora vinavyokubalika (best

practice) kwa uharaka wa kutosha ili kuulinda taarifa mali (information asset) za Serikali ambazo kimsingi zimeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na nguvu katika kuzikusanya, kuzichakata na kuzihifadhi. Eneo hili ni vyema liwe na uwezo wa kutumika na mifumo yote ya Wizara bila kujali Idara ili uwekezaji huu uwe na tija na ufanisi kwenye matumizi ya fedha za Serikali kwa Wizara nzima.

11.5.1.20 Kukosekana nyaraka inayoonesha mfumo kufanyiwa majaribio na watumiaji (User acceptance Test Document).

Utaratibu uliobora katika utengenezaji wa mifumo, mifumo kabla ya kuanza kutumika baada ya kukamilika kwa utengenezaji inapaswa kufanyiwa majaribio na watumiaji na badala ya hapo wanatakiwa kutoa taarifa ya dosari watazozibaini kwa mujibu wa kazi zao zinavyotakiwa kufanywa.

Ukaguzi umebaini Mfumo wa MUTM haukufanyiwa majaribio kikamilifu kwa hususan kwa watumiaji wa mfumo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa dosari nyingi za kutuendaji katika mfumo huo wa MUTM ikiwemo dosari katika ripoti za makadirio ya makusanyo dhidi ya makusanyo halisi kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha 5: Inaonesha dosari katika mfumo wa MUTM kwenye makadirio na mapato halisi.

#	Chanzo Kikuu	Mwaka wa bajeti	Makadirio	Mapato
1	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	15,000,000.00/=	870,742,800.00/=
2	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	15,000,000.00/=	870,742,800.00/=
3	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	533,000,000.00/=	870,742,800.00/=
14	USHURU NA UZALISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	18,780,000.00/=	95,716,000.00/=
52	USHURU WA USAFIRISHAJI	01-07-2021 - 30-06-2022	109,550,000.00/=	28,385,500.00/=
	Jumla		4,066,905,000.00	7,585,795,800.00

11.5.1.21 Matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali.

Sera za Wakala wa Serikali mtandao kifungu nambari 4.10.1.2(a) inazitaka taasisi zote za Serikali na watumishi wake kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwenye mawasiliano yote ya kiofisi ya kielektroniki ili kuhakikisha usalama wa taarifa zote za Serikali. Hii inamaanisha kwamba mawasiliano yoyote ya kazi za Serikali yanapaswa kufanywa kwa kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwa sababu za kiusalama kwenye taarifa hizo zinasafirishwa toka kwa mtu au taasisi moja kwenda kwa mpokeaji ambaye ni mtumishi au taasisi ya Serikali. Matumizi ya "Gmails", "Yahoomails", "Hotmails" n.k hayaruhusiwi kwa watumishi wa Serikali.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa sehemu kubwa ya watumishi wa Wizara wanatumia barua pepe zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kikazi kama vile gmail, yahoo na hotmail. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sera za Serikali mtandao lakini pia ni kuhatarisha usalama wa taarifa za Serikali. Ukaguzi unaishauri Wizara kufanya mambo yafuatayo:-

- a) Kuwatengenezea barua pepe rasmi watumishi wote wasio kuwanazo.
- b) Kuwapatia mafunzo endelevu ya namna ya kuzitumia barua pepe hizo ipasavyo na kuleta tija.
- c) Kusimamia na kuratibu miundombinu ya TEHAMA ya Wizara wakati wote kuhakikisha kwamba haikwamishi matumizi ya barua pepe hizo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya barua pepe, mtandao (internet), uwezo wa kutuma na kupokea mafaili ili kushajihisha matumizi ya barua pepe hizo Wizarani.

11.5.2 MANISPAA YA MJINI

11.5.2.1 Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki

Ukaguzi umebaini uwepo wa ucheleweshaji wa fedha za makusanyo ya kila siku kupelekwa benki kwa wakati unaofanywa na baadhi ya watumishi wa Baraza la Manispaa Mjini kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu, ubadhirifu au matumizi mabaya ya rasilimali hizo tofauti na mipango ya serikali.

Ukaguzi unashauri Baraza kuweka udhibiti utakaohakikisha kwamba fedha zote zinazokusanywa zinapelekwa benki kila siku ya makusanyo hayo. Aidha, Baraza liwe na utaratibu wa kuandaa ripoti ya mapato ya kila siku kwa kila mkusanyaji kwa kila chanzo tofauti na ripoti inayotoka kwenye mfumo.

Kufanya usuluhishi wa mapato wa taarifa zinazotoka kwenye mfumo dhidi ya taarifa za makusanyo halisi.

11.5.2.2 Udhibiti hafifu wa ufikiaji wa mfumo pamoja na vifaa vyengine vya TEHAMA (User Access Control)

Kwa kuhakikisha udhibiti wa ufikiaji (access control) kwenye mfumo taasisi inatakiwa kuweka Sera ya usimamizi wa ufikiaji wa mfumo (user access control policy) ambayo itaelezea ni nani anastahili kuwa na ufikiaji wa mfumo na kwa kiwango gani cha kupata na kwa muda upi na kuidhinishwa na uongozi.

Ukaguzi umebaini kwamba Manispaa ya Mjini haina udhibiti mzuri juu ya ufikiaji wa mfumo hali hii inapelekea watu wasiostahiki kutumia mfumo kupata ufikiaji na kuweza kutumia mfumo huo.

Aidha, uongozi wa Manispaa ya mjini hauna ufikiaji (access) kwenye mfumo na wala hawana njia yoyote ya udhibiti na kuangalia matukio yanayofanyika kwenye mfumo

Kutokufanya hivyo kunapelekea watu wasiostahiki kupewa ufikiaji kwenye mfumo bila kujulikana na pia utambuzi mdogo kwenye mfumo.

Ukaguzi unashauri kwamba kuwe kuna sera maalum za usimamizi wa ufikiaji wa mfumo ambazo

ndani yake zinaonesha utengenezwaji, usimamishwaji na nani mwenye mamlaka ya ukaguzi wa ufikiaji mtumiaji (user access review) wa mfumo Aidha, Kutekeleza udhibiti wa kuzuia katika mfumo ili mtumiaji asiweze kuidhinisha marekebisho ambayo ameyanzisha yeye mwenyewe.

Pia kufanya mapitio ya mara kwa mara kwa haki za ufikiaji wa mfumo kwa mtumiaji ili kuhakikisha kila mtumiaji ana haki sahihi za kuufikia mfumo kulingana na majukumu ya utendaji wake.

11.5.2.3 Kutokufanyika kwa Usuluhishi wa Kibenki (Bank Reconciliation) kwa Nambari ya Benki 0404007000 ya Kukusanyia Mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba Manispaa ya Mjini inamiliki nambari ya benki 0404007000 inayojulikana kwa jina la **Halmashauri ya Manispaa** katika Benki ya PBZ, ambayo inatumika kwa ajili ya kukusanyia mapato ya Manispaa ya Mjini. Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2020-2021 Manispaa ya mjini haikua ikiandaa Taarifa za Usuluhishi wa Kibenki kwa ajili ya nambari hiyo kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha.

Kutokuandaa kwa taarifa za usuluhishi wa kibenki kunaweza kupelekea upotevu wa taarifa sahihi za kifedha na kufanya hivyo ni kuenda kinyume na kifungu nambari 27 (1) na (2)(a) cha sheria namba 12 ya Usismamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa ya Mjini kuwa na mpangilio mzuri wa kufanya usuluhishi wa taarifa za nambari ya benki hiyo kwa kila mwezi ili kuweza kufahamu kama kuna kasoro ambazo zinaweza kujitokeza.

11.5.2.4 Uongozi kutoshiriki kikamilifu katika kufuatilia matumizi ya Mifumo

Ukaguzi umebaini kwamba usimamizi na ukaguzi watumiaji wa mfumo wa MUTM ni mdogo kitu ambacho kinaweza kupelekea matumizi mabaya kwenye mfumo kama kusajili watumiaji wasiostahiki Pamoja na kutumia accounts hizo vibaya.

Ukaguzi ushauri kwamba kuwe na udhibiti mzuri wa matumizi ya mfumo hakuna fomu wanazojaza watumiaji wapya kwenye mfumo.

11.5.2.5 Kutokamilika kwa usajili wa POS na wanaokusanya mapato.

Utaratibu wa kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unajumuisha mambo mbali mbali kama ifuatavyo: -

- Wafanyakazi ambao watakusanya mapato katika maeneo husika.
- Mashine za (POS) zinazotumiwa na wafanyakazi kwa ajili ya kutolea stakabadhi za malipo baada ya kufanyika malipo
- Vyanzo ambavyo vitatumika kwa ajili ya kukusanyia mapato
- Mfumo wa kielektroniki utakaoweka kumbukumbu za makusanyo ya mapato na wafanyakazi wanaokusanya mapato hayo kupitia mashine za POS au kompyuta.

Ili kuiwezesha wizara Pamoja na mabaraza yake kufuatilia na kupata taarifa sahihi za makusanyo ya mapato kwa kila siku, wizara haina budi kuunganisha mashine za POS, watu wanaotumia

mashine husika na maeneo wanayokusanya mapato husika katika mfumo wa MUTM.

Lengo la kuunganisha vitu vyote hivyo kwa pamoja katika mfumo ni kupata taarifa sahihi za makusanyo kwa kumtambua mtu anayetumia mashine, na eneo anapokusanyia na mashine husika, wakati na kiwango alichokusanya.

Ukaguzi umebaini kwamba mabaraza ya manispaa haijaunganisha katika mfumo kwa pamoja mashine za POS, watumiaji wa mashine pamoja na maeneo husika ya makusanyo, badala yake wakusanyaji mapato hukusanya kupitia POS bila ya kujulikana kwenye mfumo maeneo wanakokusanyia na POS wanazotumia.

Ukaguzi unashauri vitendea kazi vyote, wakusanyaji wote na maeneo yao wasajiliwe kwa pamoja na wajulikane mashine zao na maeneo halisi waliopo ili iwe rahisi kwa wizara na Baraza kufuatilia na kupata taarifa sahihi za mapato yaliyokusanywa.

11.5.2.6 Kutokuwepo kwa daftari maalum (Issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo - Rejea Hoja Nambari 11.5.1.4

11.5.2.7 Mapungufu katika utengenezaji wa nambari za Udhhibiti (control numbers)

Rejea Hoja Nambari 11.5.1.9

11.5.2.8 Matumizi ya barua pepe (E-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali - Rejea Hoja Nambari 11.5.1.21

11.5.2.9 Kukosekana kwa udhibiti unaotumika kuhakikisha mapato yaliyokusanya na kuingia kwenye mfumo ndo yanayo pelekwa benki

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa MUTM wa zamani imebainika uwepo wa tofauti kubwa kati ya taarifa za makusanyo ya mapato zilizomo ndani ya mfumo na taarifa za kibenki (bank statements) ambazo zinaonesha mapato halisi yaliyolipwa. Tofauti hiyo imebainika kwa kupitia ripoti za mfumo zinazoonesha kwamba katika mfumo jumla ya shilingi 612,822,900 zimekusanywa katika kipindi cha kuanzia tarehe 1/3/2021 hadi tarehe 30/6/2021 kupitia ripoti ya mfumo lakini taarifa za kibenki (bank statements) zinaonesha kwamba mapato yaliyokuwanywa yana jumla ya shilingi 1,783,354,983.96 katika kipindi hicho hicho.

Kukosekana kwa udhibiti huo kunapelekea upotevu wa mapato na kuwapa mwanya wakusanya mapato. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika Picha hapo chini:-

Picha : Jumla ya mapato kwa vyanzo vyote kutoka 1/3/2021 hadi 30/6/2021

8	SIKUKUU	32,563,000
9	PAPO KWA PAPO	530,000
10	AFYA	785,000
11	SEARCH	10,000
12	KODI ZA VYOO	1,450,000
13	MAHAKAMA	765,000
14	KODI ZA MADUKA	0
15	KODI ZA OFISI	300,000
16	MCHANGO WA MWENGE	0
17	FOMU	0
18	DENI LA OFISI	0
19	MIKATABA	0
20	KITAMBULISHO	0
21	ZABUNI	0
	Total	612,822,900

11.5.3 MANISPAA YA MAGHARIBI 'A'

11.5.3.1 Kutokamilika kwa usajili wa POS na wanaokusanya mapato

- Rejea Hoja Nambari 11.5.2.5

11.5.3.2 Kutokuwepo na daftari maalum (Issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo -Rejea Hoja Nambari 11.5.1.4

11.5.3.3 Kutokufanyika kwa Usuluhishi wa Kibenki (Bank Reconciliation) kwa Nambari ya Benki 0403995000 ya Kukusanyia Mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba Manispaa ya mjini inamiliki nambari ya benki 0403995000 inayojulikana kwa jina la BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A katika Benki ya PBZ, ambayo inatumika kwa ajili ya kukusanyia mapato ya Manispaa ya Mjini. Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2020-2021 Manispaa ya mjini haikua ikiandaa Taarifa za Usuluhishi wa Kibenki kwa ajili ya nambari hiyo kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha.

Kutokuandaa kwa taarifa za usuluhishi wa kibenki kunaweza kupelekea upotevu wa taarifa sahihi za kifedha na kufanya hivyo ni kuenda kinyume na kifungu nambari 27 (1) na (2)(a) cha sheria namba 12 ya Usismamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.


Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa ya Magharibi A kuwa na mpangilio mzuri wa kufanya usuluhishi wa taarifa za nambari ya benki hiyo kwa kila mwezi ili kuweza kufahamu kama kuna kasoro ambazo zinaweza kujitokeza.

11.5.3.4 Kukosekana kwa udhibiti unaotumika kuhakikisha mapato yaliyokusanywa na kuingia kwenye mfumo ndio yanayo pelekwa benki

Ukaguzi umebaini kwamba katika mfumo wa zamani wa MUTM imebainika uwepo wa tofauti kubwa ya mapato yaliyobainishwa kwenye mfumo na mapato yaliyolipwa benki, kulingana na ripoti

ya mapato ya vyanzo vyote kwenye mfumo kuanzia 1/4/2021 mpaka 30/4/2021 ambapo jumla ya mapato hayo ni 103,648,386. Aidha kwa mujibu wa bank statement kwa kipindi hichohicho mapato yalionyesha jumla ya shilingi 65,576,686. Aidha, kukosekana kwa udhibiti huo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato kwa kuwapa mwanya wakusanyaji mapato. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha: Tofauti ya mapato iliyobainika katika mfumo



19	MINARA	1,581,786
20	UKUMBI	50,000
21	FAINI	586,000
22	MAZAO	24,000
23	DIKO LA DAGAA BUBUBU	0
24	DIKO LA DAGAA KAMA	0
25	VITALU	732,600
26	KOKOTO	0
27	KOKOTOTO	0
28	FAINI YA MAJENZI	400,000
29	KITALU CHA SAMAKI	0
30	GAWIO	25,600,000
31	BODABODA	0
32	KODI YA CHOO	0
	Total	103,648,386

11.5.3.5 Uelewa duni wa mfumo wa MUTM kwa watumiaji walio wengi

Ukaguzi umebaini kwamba watumiaji wengi wa wa mfumo wa Magharibi A hawana uwelewa wa kutosha juu matumizi ya mfumo kwenye maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuutumia mfumo kwenye kutoa ripoti zilizomo kwenye mfumo. Hali hii inapelekea kuongeza utegemezi kwa watumishi wakitengo cha TEHAMA katika kufanya kazi ambazo hawastahili kuzifanya.

Aidha, hali hii inapelekea watu wa kitengo cha TEHAMA kufanya kazi za watumiaji wengine nje ya majukumu yao ya kazi jambo ambalo linaondoa ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya kitengo cha TEHAMA kama inavyoathiri ufanisi na tija wa majukumu hayo ya nyongeza.

Udhaifu kwenye udhibiti wa jumla wa Taasisi kwenye kazi zinazofanywa kwenye mfumo jambo ambalo linaweza kupelekea ubadhirifu, wizi, udanganyifu katika mapato kwakua mtu mmoja ana uwezo wa kufanya mzunguko mzima wa miamala, hili linatikana na kuwa na nywila (passwords) kadhaa za watumiaji wa mfumo.

Ukaguzi unashauri kuandaa na kutekeleza programu ya mafunzo ya utayari wa kubadilika (Change management training) kwa ajili ya watumishi wote wa Serikali za mitaa kwa wanaotumia mfumo wa MUTM Pamoja na vifaa vyake (POS), ili kuhakikisha kwamba wanajua faida za mabadiliko yatokanayo na mfumo wa MUTM kiuchumi na kijamii kwa lengo la kupunguza au kuondoa kabisa ukinzani wa kubadilika.

Kuandaa na kutekeleza programu ya mafunzo ya nyongeza ya mfumo wa MUTM na vifaa vyake ili kuwajengea uwezo mzuri kwa watumiaji wa mfumo huo ambao walishafundishwa mwanzo na kwa wale ambao hawajawahi kufundishwa.

11.5.3.6 Kukosekana kwa tovuti ya Taasisi kwaajili ya kutoa taarifa mbalimbali

Ukaguzi umebaini kwamba Manispaa ya Magharib A haina tovuti, hali hii imesababisha kukosekana kwa taarifa muhimu zinazotakiwa kuwafikia wananchi kwa wakati kuhusiana na huduma zinazotolewa na Baraza.

Kutokuwa na tovuti ya Baraza kunaweza kupelekea uchelewashaji wa huduma za maendeleo katika jamii kutokana na kutoonekana kwa taarifa muhimu za kimaendeleo zitakazotolewa na Serikali kupitia Baraza.

Ukaguzi unashauri Manispaa ya magharib A kutengeneza tovuti yake kwa haraka na kuitumia kwa ajili ya kutoa taarifa muhimu za huduma za kimaendeleo kwa wananchi wake ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi wa Baraza na Serikali kwa ujumla.

11.5.3.7 Matumizi ya barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali

Rejea Hoja Nambari 11.5.1.21

11.5.4 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

11.5.4.1 Kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato katika mfumo wa MUTM

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa MUTM hautoi taarifa sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo cha mapato kilichoainishwa na Baraza la Mji Chake Chake. Kwa mujibu wa maelezo kutoka kwa Afisa Mapato wa Baraza la Mji Chake Chake imebainika Baraza limekusanya mapato halisi yenye jumla ya shilingi 14,620,500 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato kwa mwezi wa Novemba 2021. Hata hivyo katika taarifa ya makusanyo ya mapato iliyotolewa kutoka kwenye mfumo kwa kipindi cha mwezi wa Novemba 2021 imeonesha kuwa mfumo umekusanya jumla ya shilingi 248,548,500 kwa vyanzo vyote vya mapato ya Baraza la Mji Chake Chake ambapo jumla hiyo imetokana na makusanyo yaliyojirejea ya kiasi cha shilingi 14,620,500 kwa kila chanzo jambo ambalo ni tofauti na uhalisia wa makusanyo ya mapato ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwezi huo.

Hali hii inapelekea mfumo kukosa sifa za utendaji kazi kulingana na taratibu za kimataifa za matumizi ya mifumo (ISO 9001-2005).

Kutokupatikana kwa taarifa sahihi ya makusanyo ya mapato kunaweza kupelekea kujitokeza kwa kuendelea kutumia utaratibu wa zamani wa kurikodi taarifa za mapato ya mwezi kwa njia ya kawaida "manually" jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake kupitia Wizara ya Nchi OR-TMSMIM kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuboreshwa mfumo wa MUTM ili uweze kuonesha uhalisia wa mapato yanayokusanywa kwa kila chanzo kwa kila mwezi.
- Kuweza kutoa ripoti za kila mwezi na mwaka kupitia mfumo.

- Kuweza kupatiwa wataalamu wa marekebisho ya Mfumo kwa upande wa Pemba.

Hali halisi ya muonekano wa taarifa za makusanyo kwenye mfumo kwa MUTM kuanzia tarehe 01 Novemba 2021 hadi tarehe 30 Novemba 2021 ni kama inavyoonekana katika kielelezo hapo chini:-

Picha : Dosari katika taarifa za makusanyo ya kila chanzo kwa mwezi wa Novemba 2021.

#	Chanzo Kikuu	Kiasi
1	USHURU NA UZALISHAJI	14,620,500.00
2	HAEGESHO	14,620,500.00
3	KWARE	14,620,500.00
4	KODI YA MILANGI	14,620,500.00
5	MADIKO	14,620,500.00
6	KODI YA UKUMBI	14,620,500.00
7	USAFIRISHAJI MADAGAA	14,620,500.00
8	ADA YA VIKUTA	14,620,500.00
9	ADA YA UENZI	14,620,500.00
10	USAFI	14,620,500.00
#	Jumla	248,548,500.00

11.5.4.2 Dosari katika Mfumo wa leseni uliopo Baraza la Mji Chake Chake

Baraza la Mji Chake Chake limeanzisha na kutumia mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za wafanya biashara waliopo katika Wilaya ya Chake Chake Pemba kwa lengo la kuwatambua, kuwafuatilia na kuweza kurahisisha kazi za makusanyo yatokanayo na leseni za biashara katika Wilaya hiyo.

Ukaguzi umebaini kuwa hakuna mkataba rasmi wa makubaliano ya utengenezaji wa mfumo, mkataba wa utoaji huduma na maboresho ya mfumo pamoja na hadidu rejea "TOR" zinazohusiana na matengenezo ya mfumo huo zilizoandaliwa baina ya Baraza la Mji Chake Chake na watengenezaji wa mfumo, jambo ambalo limepeleka kutokujulikana kwa gharama halisi zilizotumika katika utengenezaji wa mfumo huo.

Kukosekana kwa mkataba wa utoaji huduma (Service Level Agreement SLA) ni kwenda kinyume na viwango vya usimamizi wa mifumo ITIL-ISO 20000, aidha kunapelekea uwezekano wa kutokupatikana kwa msaada wa kiufundi na kusababisha mfumo kukosa matengenezo na maboresho kwa wakati na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake kuzingatia taratibu bora zinazokubalika kwa kuhakikisha kuwa wanaingia katika makubaliano ya kimkataba na wadau (watengenezaji) wote wanaotoa huduma za kusaidia mifumo ya TEHAMA ili kuweka misingi imara ya uwajibikaji endapo kutatokea dosari zozote katika utoaji wa huduma za mifumo na kuathiri shughuli zinazotegemea mifumo ya TEHAMA.

11.5.4.3 Kutokuwepo kwa daftari maalum (Issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo -Rejea Hoja Nambari 10.5.1.4

11.5.4.4 Mapungufu katika utengenezaji wa nambari za Udhibiti (control numbers) Rejea Hoja Nambari 11.5.1.9

11.5.4.5 Matumizi ya barua pepe (E-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali -Rejea Hoja Nambari 11.5.1.21

11.5.5 BARAZA LA MJI WETE

11.5.5.1 Kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato katika mfumo wa MUTM

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa MUTM hautoi taarifa sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo cha mapato kilichoainishwa na Baraza la Mji Wete. Kwa mujibu wa maelezo kutoka kwa Afisa Mapato wa Baraza la Mji Wete imebainika Baraza limekusanya mapato halisi yenye jumla ya shilingi 15,017,500 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato kwa mwezi wa Disemba 2021. Hata hivyo katika taarifa ya makusanyo ya mapato iliyotolewa kutoka kwenye mfumo kwa kipindi cha mwezi wa Disemba 2021 imeonesha kuwa mfumo umekusanya jumla ya shilingi 195,227,500 kwa vyanzo vyote vya mapato ya Baraza la Mji Wete ambapo jumla hiyo imetokana na makusanyo yaliyojirejea ya kiasi cha shilingi 15,017,500 kwa kila chanzo jambo ambalo ni tofauti na uhalisia wa makusanyo ya mapato ya Baraza la Mji Wete kwa mwezi huo.

Hali hii inapelekea mfumo kukosa sifa za utendaji kazi kulingana na taratibu za kimataifa za matumizi ya mifumo (ISO 9001-2005).

Kutokupatikana kwa taarifa sahihi ya makusanyo ya mapato kunaweza kupelekea kujitokeza kwa kuendelea kutumia utaratibu wa zamani wa kurikodi taarifa za mapato ya mwezi kwa njia ya kawaida "manually" jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kupitia Wizara ya Nchi OR-TMSMIM kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuboreshwa mfumo wa MUTM ili uweze kuonesha uhalisia wa mapato yanayokusanywa kwa kila chanzo kwa kila mwezi.
- Kuweza kutoa ripoti za kila mwezi na mwaka kupitia mfumo.
- Kuweza kupatiwa wataalamu wa marekebisho ya Mfumo kwa upande wa Pemba.

Hali halisi ya muonekano wa taarifa za makusanyo kwenye mfumo kwa MUTM kuanzia tarehe 01 Disemba 2021 hadi tarehe 31 Disemba 2021 ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

Picha: Dosari katika taarifa za makusanyo ya kila chanzo kwa mwezi wa Disemba 2021.

#	Chanzo Kikuu	Kiasi
1	USHURU WA UTALISHAJI	15,017,500.00
2	LESENTI ZA BTASHABA	15,017,500.00
3	DIKO	15,017,500.00
4	SOKO	15,017,500.00
5	MAROGOSHU	15,017,500.00
6	UKUPBI	15,017,500.00
7	USAFI	15,017,500.00
8	CHINDIO	15,017,500.00
9	KODI YA NILANGO	15,017,500.00
10	UYEJI VYA HAZAO	15,017,500.00
	Jumla	150,175,000.00

11.5.5.2 Kutokuwepo kwa daftari maalum (Issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo -Rejea Hoja Nambari 11.5.1.4

11.5.5.3 Mapungufu katika utengenezaji wa nambari za Udhhibiti (control numbers) Rejea Hoja Nambari 11.5.1.9

11.5.5.4 Matumizi ya barua pepe (E-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali -Rejea Hoja Nambari 11.5.1.21

11.5.6 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

11.5.6.1 Kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato katika mfumo wa MUTM

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa MUTM hautoi taarifa sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo cha mapato kilichoainishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Kwa mujibu wa maelezo kutoka kwa Afisa Mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imebainika

Halmashauri imekusanya mapato halisi yenye jumla ya shilingi 3,331,250 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato kwa mwezi wa Oktoba 2021. Hata hivyo katika taarifa ya makusanyo ya mapato iliyotolewa kutoka kwenye mfumo kwa kipindi cha mwezi wa Oktoba 2021 imeonesha kuwa mfumo umekusanya jumla ya kiwango cha fedha kwa vyanzo vyote vya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambapo jumla ya kiwango hicho imetokana na makusanyo yaliyojirejea ya kiasi cha shilingi 3,331,250 kwa kila chanzo jambo ambalo ni tofauti na uhalisia wa makusanyo ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwezi huo.

Hali hii inapelekea mfumo kukosa sifa za utendaji kazi kulingana na taratibu za kimataifa za matumizi ya mifumo (ISO 9001-2005).

Kutokupatikana kwa taarifa sahihi ya makusanyo ya mapato kunaweza kupelekea kujitokeza kwa kuendelea kutumia utaratibu wa zamani wa kurikodi taarifa za mapato ya mwezi kwa njia ya kawaida "manually" jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kupitia Wizara ya Nchi OR-TSMIM kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuboreshwa mfumo wa MUTM ili uweze kuonesha uhalisia wa mapato yanayokusanywa kwa kila chanzo kwa kila mwezi.
- Kuweza kutoa ripoti za kila mwezi na mwaka kupitia mfumo.
- Kuweza kupatiwa wataalamu wa marekebisho ya Mfumo kwa upande wa Pemba.

Hali halisi ya muonekano wa taarifa za makusanyo kwenye mfumo kwa MUTM kuanzia tarehe 01 Oktoba 2021 hadi tarehe 31 Oktoba 2021 ni kama inavyoonekana katika Picha hapo chini:-

Picha: Dosari katika taarifa za makusanyo ya kila chanzo kwa mwezi wa Oktoba 2021.

#	Chanzo Kikuu	Kiasi
1	USHURU NA UZALISHAJI	3,331,250.00
2	LESENI	3,331,250.00
3	ADA YA MASOKO	3,331,250.00
4	ADA YA MAEGESHO	3,331,250.00
5	ADA YA VYETI VYA MAZAO	3,331,250.00
6	ADA YA CHINJIO	3,331,250.00

11.5.6.2 Kutokuwepo kwa daftari maalum (Issue register) kwaajili ya kuweka mapungufu yanayojitokeza kwenye mfumo - Rejea Hoja Nambari 11.5.1.4

11.5.6.3 Mapungufu katika utengenezaji wa nambari za Udhhibiti (control numbers)

Rejea Hoja Nambari 11.5.1.9

11.5.6.4 Matumizi ya barua pepe (E-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kazi za Serikali - Rejea Hoja Nambari 11.5.1.21


11.5.6.5 Matumizi ya program uhuru "free anti virus, free OS,MS Office" katika kompyuta za Taasisi

Utaratibu uliobora (best practice) unaeleza kwamba Taasisi ambazo zinatamia mifumo muhimu ya TEHAMA zinatakiwa kuweka udhibiti na usalama mkubwa wa taarifa ambazo zitahifadhiwa ndani ya mifumo hiyo. Moja kati ya njia imara za kudhibiti na kuweka usalama wa taarifa za kwenye mifumo ni kuweka sera zilizobora katika matumizi ya kompyuta za ofisi pamoja na sera za matumizi ya programu (software) zinazotumika katika kompyuta hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya kompyuta za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni zina dosari mbali mbali za kiusalama ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizohifadhiwa ndani yake na kupelekea kutokea kwa hatari ya kushambuliwa kwa mfumo mzima wa MUTM.

Baadhi ya dosari hizo ikiwemo utumiaji wa "Antivirus" zilizokuwa huru, hazina leseni za matumizi pamoja na utumiaji wa programu za mfumo wa uendeshaji wa Kompyuta (Operating Systems) ambazo hazina leseni za matumizi na baadhi yao zimeshapitwa na wakati (Windows 7). Hali halisi ni kama inavyoonekana katika Picha hapo chini:-

Picha: Anti virus zilizokuwa hazina leseni ya matumizi



Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na IT SOP zinazotambulika kitaifa na kimataifa pamoja na ISO/IEC Standard 27002:2003. Kutoweka udhibiti mzuri katika matumizi ya kompyuta kunaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa muhimu za taasisi na kupelekea kuharibika kwa mfumo.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuweka udhibiti imara katika matumizi ya kompyuta ili kuweza kulinda taarifa zilizomo ndani ya kompyuta na mfumo pamoja na kununua programu halisi (Original and Genuine Software) zenye ubora na za kisasa ili kuweza kupata usalama katika kuendeshea "Security Updates" na leseni za matumizi halali ya programu hizo kwa ajili ya Ofisi zikiwemo "Windows Operating Systems, Computer Antiviruses" pamoja na "Office Packages".

11.5.7 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo ya MUTM ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (OR-TMSMIM).

Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhiti kwa uongozi wa Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa Na Idara Maalum za SMZ kwa ushirikiano mzuri mliyotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio OCAGZ kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi wetu ujao.

SURA YA KUMI NA MBILI

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR – (eGAZ)

12.0 UTANGULIZI

Wakala wa Serikali Mtandao ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kupitia Sheria Nambari 12 ya Wakala wa Serikali Mtandao ya mwaka 2019 ambapo awali ilijulikana kama Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano chini ya kifungu nambari 97 cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao, miongoni mwa majukumu ya Wakala ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za TEHAMA, Kanuni na miongozo katika utumishi wa umma, kusimamia maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma, kutekeleza maagizo ya kiseru na maamuzi mengine ya Serikali kuhusiana na matumizi ya TEHAMA, kushauri Mamlaka husika na taasisi yoyote ya umma juu ya matumizi bora ya TEHAMA katika usimamizi na utoaji wa huduma za umma, kuandaa na kuweka kumbukumbu za wataalamu wa TEHAMA, kupendekeza maslahi na kuratibu matumizi ya wataalamu wa TEHAMA.

Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Wakala ya mwaka 2019 malengo ya Wakala yanajumuisha kuratibu shughuli za Serikali mtandao kwenye taasisi za umma na utoaji wa huduma za Serikali kupitia matumizi ya TEHAMA, kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inawekwa, inaimarishwa na inaendelezwa kwa mujibu wa Sera na viwango vitakavyopelekea kuwa na matumizi bora ya pamoja ya habari yenye gharama nafuu, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za Serikali nchi nzima kwa urahisi, ufanisi, uthabiti kwa kutumia mifumo sahihi ya TEHAMA, kushajihisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma na kuwa kitovu cha utaalamu katika kuandaa na kuendeleza Sera, viwango na taratibu nyengine kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma Zanzibar.

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kisheru Wakala eGAZ imepata mafanikio mbali mbali ambayo ni pamoja na kutoa Sera na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa TEHAMA ambapo Wakala imefanikiwa kutoa miongozo miwili na Sera moja tangu kuanzishwa kwake. Mwaka 2012 Wakala ilitoa Sera ya Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government Policy), miaka tisa baadae, mwezi Julai, 2021 Wakala ilitoa miongozo miwili yaani muongozo wa sifa za vifaa na mifumo Serikalini (Government Hardware and Software Specification) na muongozo wa manunuzi na ufungaji wa mifumo na vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) katika Sekta ya umma.

Aidha, Wakala imefanikiwa kutoa mafunzo mbali mbali ya TEHAMA na inatekeleza mifumo mitatu ya kielektroniki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali mtandao ya Tanzania (eGA), mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Malipo wa Serikali (ZanMalipo), Mfumo wa Barua Pepe za Serikali (Government Mails) na Mfumo wa Ofisi Mtandao (E-Office System).

12.1 UKAGUZI WA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI

Katika ukaguzi uliofanyika ulihakiki mfumo wa kielektroniki wa ZanMalipo wa zamani na mfumo mpya wa ZanMalipo ambapo mifumo hiyo kwa pamoja ilipitiwa kwa lengo la kuweza kujiridhisha utendaji kazi wake ili kuweza kuona tija na ufanisi inayopatikana kutokana na matumizi ya mifumo hiyo.

12.1.1 Mfumo wa ZanMalipo wa zamani

Mfumo wa Usimamiaji ukusanyaji wa mapato wa Serikali Zanzibar Government Electronic Payment Gateway (ZanMalipo wa zamani) ulitengenezwa na wataalamu wa ndani chini ya usimamizi na uratibu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa gharama ya takriban shilingi 96,000,000.

Mfumo huu ulikuwa na lengo la kurahisisha ulipaji wa huduma za umma kwa kumuwezesha mlipaji kupata njia mbalimbali na rafiki za kufanya malipo kama vile kulipa kwa kutumia Simu za mkononi, Benki na Mawakala wa malipo, ambapo kufikia mwezi Julai 2021 mfumo huu ulianza kutumika kwa baadhi ya taasisi za umma zinazokusanya mapato Zanzibar.

Mwishoni mwa mwaka 2021 usimamizi na uratibu wa mfumo huu ulihamishwa kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kwenda Wakala wa Serikali mtandao. Aidha, mfumo huu umetumika katika kukusanya mapato yaliyofikia jumla ya shilingi **1,269,341,376** sawa na asilimia 73 ya nambari za utambuzi 'Control Number' zote zilizotengenezwa, wakati jumla ya shilingi **16,188,560,007,597** sawa na asilimia 27.24 ya nambari za utambuzi 'control number' zote zilizotengenezwa hazikukusanywa kwa sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kupita kwa muda wa matumizi wa nambari za utambuzi (Expired control numbers), nambari za utambuzi zilizositishwa (Cancelled control numbers) na "Verified" kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2021. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 40 : Nambari za utambuzi na kiwango cha Makusanyo katika Mfumo wa zamani wa ZanMalipo

Makundi ya Nambari za Utambulisho	Idadi ya Nambari za Utambuli sho	Kiwango cha fedha (Tshs)	Asilimia ya Nambari za Utambulisho (%)	Asilimia ya Fedha (%)
Nambari za Utambulisho zilizolipwa (Paid)	60,112	1,269,341,376.00	72.76	0.01
Nambari za Utambulisho zilizokuwa hazijalipwa (Unpaid)	19,560	17,263,240,072.34	23.67	0.11
Nambari za Utambulisho zilizopitwa na muda (Expired)	2,033	412,680,122.00	2.46	0.00
Nambari za Utambulisho zilizoghairishwa (Cancelled)	916	16,170,884,087,403.30	1.11	99.88
Jumla Kuu	82,621	16,189,829,348,973.60	100	100

Aidha, baada ya miezi mitano kupita tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa ZanMalipo ulianzishwa mfumo mwingine kufuatia changamoto mbali mbali zinazoukabili na kupelekea kutopatikana kwa tija na ufanisi uliotarajiwa. Ikumbukwe kwamba kuna baadhi ya taasisi za umma hususan Mabaraza ya Manispaa ambayo bado yanaendelea kutumia mfumo huu wa ZanMalipo wa zamani.

12.1.2 Mfumo mpya wa ZanMalipo

Mfumo wa ZanMalipo Mpya ulitengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania (e-GA) ambapo kwa Tanzania unajulikana kama Government Electronic Payment Gateway (GEPG), mfumo huu wa GEPG umerithiwa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (e-Goz) mwishoni mwa mwaka 2021 na kupewa jina la Zanzibar Government Electronic Payment Gateway (ZanMalipo).

Zanzibar ina taasisi za umma zisizopungua **117** zinazokusanya mapato ya ndani ambazo ndizo zinazolengwa kutumia mfumo wa ZanMalipo, hata hivyo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022 Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar ilisajili taasisi **30** pekee sawa na asilimia **26** kwa ajili ya kuanza kukusanya mapato ya Serikali kupitia mfumo wa ZanMalipo mpya ambapo ni taasisi **18** sawa na asilimia **15** ya taasisi zote ndizo zinazotumia mfumo wa ZanMalipo katika kukusanya mapato yake kutoka vyanzo vya ndani. Aidha, taasisi **17** kati ya taasisi **30** zilizosajiliwa zinatarajia kutumia "Generic ZanMalipo" kwa ajili ya kutengeneza nambari za Utambuzi wa Miamala (Control numbers) na kupata ripoti mbali mbali za mapato, wakati taasisi **13** zimesajiliwa kutumia mifumo yao iliyounganisha (integrated) na ZanMalipo. Taasisi za Serikali zilizosajiliwa na zinazotumia mfumo mpya wa ZanMalipo mpya ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 41: Taasisi za Serikali zilizosajiliwa na zinazotumia mfumo mpya wa ZanMalipo

Taasisi zinazokusanya mapato ya ndani	Taasisi zilizosajiliwa kwenye mfumo wa ZanMalipo Mpya	Taasisi zinazotumia mfumo wa ZanMalipo Mpya	Asilimia ya taasisi zilizosajiliwa kwenye mfumo mpya wa ZanMalipo	Asilimia ya taasisi zinazotumia mfumo mpya wa ZanMalipo
117	30	18	26%	15%

Aidha, mfumo huu umefanikisha kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 1,666,286,410 na kukosa kufanikisha kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 612,090,940 kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuisha muda wa matumizi wa Nambari za Udhhibiti wa miamala (Expired Control Numbers), Nambari za Udhhibiti zilizositishwa (Cancelled Control Numbers) na "Verified" kwa kipindi cha kuanzia mwezi wa Novemba 2021 hadi Disemba 2021. Hali halisi ya makusanyo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 42: Nambari za utambuzi na kiwango cha Makusanyo katika Mfumo mpya wa ZanMalipo

Aina za Nambari za Utambulisho (Control Numbers)	Idadi ya Nambari za Utambulisho	Kiwango cha fedha Kilichokusanywa (Tshs)	Asilimia ya Nambari za Utambulisho(%)	Asilimia ya Fedha (%)
Nambari za Udhibiti zilizolipwa (Paid)	20,688	1,666,286,410	88.77	73.13
Nambari za Udhibiti zilizokuwa hazijalipwa (Unpaid)	82	44,958,313	0.35	1.97
Nambari za Udhibiti zilizopitwa na muda (Expired)	2,426	212,955,033	10.41	9.35
Nambari za Udhibiti zilizoghairishwa (Cancelled)	109	354,177,594	0.47	15.55
Jumla	23,305	2,278,377,350	100	100

12.2 WAJIBU WA KUKAGUA MIFUMO YA TEHAMA

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu nambari 112(3)(c) kimetoa mamlaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Katika kutekeleza wajibu huo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya kila aina ya ukaguzi anavyoona inafaa kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kutimiza matakwa ya kikatiba.

Aidha, kupitia kifungu nambari 14 cha Sheria Nambari 11 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2003, kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mkaguzi anapata taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya kielektroniki wakati anapoomba kwa madhumuni ya ukaguzi bila kuathiri mifumo hiyo.

12.3 UPEO NA MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanyika kwa kipindi kinachoanzia mwezi wa Januari 2021 mpaka Disemba 2021 ambapo tulikagua Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na kutembelea watumiaji wa Mfumo wa ZanMalipo kwenye taasisi mbali mbali za umma zilizopo Unguja.

Ukaguzi ulikua na lengo kuu la kupata ithibati na kujiridhisha kwamba Wakala wa Serikali Mtandao ina ulinzi na udhibiti kwenye miundombinu inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa zake na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinazingatia takwa la usiri na uadilifu na kwamba vyote hivi kwa ujumla wake vinachangia kupata tija na ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato kupitia TEHAMA.

Malengo mengine ya ukaguzi huu wa mifumo ya TEHAMA ya Wakala wa Serikali Mtandao ni kama yalivyo ainishwa hapa chini:-

- Kufanya tathmini ya ufanisi katika utendaji kazi wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

- b) Kubainisha ufuatishwaji wa Sheria, Kanuni, Sera, Miongozo na Taratibu zinazohusiana na TEHAMA Zanzibar ikiwa ni pamoja na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines).
- c) Kufanya tathimini ya udhibiti wa mifumo na udhibiti wa jumla ili kujiridhisha kama inakidhi matakwa yaliyopo.
- d) Kupima tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki kulinganisha na uwekezaji uliofanyika kwenye mifumo hiyo.
- e) Kuthibitisha kama taarifa zilizohifadhiwa kwenye mifumo zinabakia na usiri, usalama, usahihi na zinaweza kupatikana wakati wowote zitakapohitajika.
- f) Kubainisha kama uwekezaji kwenye TEHAMA unakwenda sambamba na malengo makuu ya taasisi.
- g) Kubainisha kama Wakala wa Serikali Mtandao ina mikakati na mipango stahiki katika usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA inchini.

12.4 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia miongozo ya ukaguzi ya kitaifa na ya kimataifa kama vile eGAZ , e-GA, ISACA, COBIT, AFROSAI-E n.k.

Katika kukagua mifumo ya ZanMalipo ukaguzi ulitumia njia mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini.

- a) Kupitia Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo mbalimbali inayohusiana na usimamizi na uratibu wa mapato Zanzibar.
- b) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi (risk assessment) kwa kuupitia mfumo wa ZanMalipo.
- c) Kupitia Sera na Miongozo ya usimamizi, uendeshaji matumizi ya TEHAMA inayotumiwa na Wakala wa Serikali Mtandao.
- d) Kupitia taratibu zilizotumika katika upatikanaji wa mfumo wa ZanMalipo.
- e) Kupitishwa kwenye mifumo ya ZanMalipo ili kuelewa utendaji kazi wake.
- f) Kufanya majaribio ya udhibiti uliomo katika mifumo ya ZanMalipo.
- g) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo ili kujiridhisha usahihi na uadilifu wake.
- h) Kufanya mahojiano na majadiliano na watumiaji wa mifumo ya ZanMalipo.
- i) Kutembelea Ofisi za eGoz kwa ajili ya kupatiwa uelewa wa namna mifumo unavyosimamiwa na kuendeshwa.
- j) Kutembelea ofisi za watumiaji wa mifumo ya ZanMalipo kwa ajili ya kujiridhisha namna mifumo inavyofanya kazi.
- k) Kufanya kikao cha kuanza kazi ya ukaguzi na kumaliza pamoja na kujadili mambo yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kabla ya kuendelea na taratibu nyengine za ukaguzi.

12.5 MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA MFUMO WA ZAMANI WA ZANMALIPO

Uwekezaji usiokuwa na tija kwenye kutengeneza mfumo na kusababisha hasara ya zaidi ya shilingi 96,000,000, kutozingatiwa kwa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kama vile "System Development Life Cycle" katika utengenezaji wa mifumo, kukosekana kwa nyaraka muhimu za matumizi na usimamizi wa mifumo, kutokuwepo kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo, udhaifu wa mfumo kwenye utengenezaji wa Namba za Ankara (Control Numbers), kutumika vibaya kwa mianya inayotokana na udhaifu wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani, udhaifu wa udhibiti wa matumizi ya Nambari za Ankara, kukosekana kwa ripoti za mapato kutoka kwenye mfumo.

12.6 MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA MFUMO MPYA WA ZANMALIPO

Kukosekana kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo, kutojulikana kwa gharama zilizotumika kwenye utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya mpaka sasa, kukosekana kwa mpango wa mafunzo (training plan) kwa mafunzo yanayoendeshwa na eGoz kwa watumiaji wa ZanMalipo, kasi ndogo ya usajili wa taasisi za umma kwenye kutumia mfumo wa ZanMalipo mpya, kukosekana kwa nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo (System users' matrix document), kukosekana kwa ripoti mbali mbali za mapato kwenye mfumo wa ZanMalipo, **kukosekana kwa nyaraka mbali mbali za matumizi na usimamizi wa mfumo.**

12.7 MUHTASARI WA YALIYOBAINIKA KATIKA UDHIBITI WA JUMLA NA UENDESHAJI WA TEHAMA

Kwa upande wa uendeshaji wa TEHAMA (ICT Governance) ilibainika kuwa na mapungufu mbali mbali yanayojumuisha kukosekana kwa muongozo wa uendeshaji wa TEHAMA (ICT Governance framework), kukosekana kwa Sera na Miongozo toshelevu ya usimamizi na matumizi ya TEHAMA, kukosekana kwa Mpango Mkakati wa maendeleo ya TEHAMA, kukosekana kwa makubaliano ya ushirikiano (Memorandum of Understanding - MoU) kati ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (e-GOz) na Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania bara (e-GA), kukosekana kwa mipango madhubuti na endelevu ya usalama wa mifumo inayorithiwa kutoka Tanzania bara.

Kukosekana kwa kumbukumbu za taasisi za Serikali zilizopeleka nyaraka au maombi mbalimbali kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wakala, kutofahamika kwa hali ya umiliki wa mifumo ya ZanMalipo, kutopitishwa kwa wakati Rasimu ya Sera za TEHAMA na Bodi ya Washauri ya Wakala, kukosekana kwa mkataba wa huduma kwa wateja wanaohudumiwa na Wakala wa Serikali mtandao yaani taasisi za umma, kukosakana kwa Mpango wa kuendeleza huduma/ biashara (Business Continuity Plan) baada ya maafa kuathiri mfumo, kutokuwepo kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan), kutokuwepo kwa mpango wa usimamizi na uratibu wa kufanya mabadiliko kwenye Mfumo (System Change Management Plan).

12.8 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO WA ZANMALIPO

Katika ukaguzi uliofanyika wa mifumo ya ZanMalipo mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo dosari za kiutendaji ambapo ukaguzi umebainisha dosari hizo na kuweza kufafanua athari zake na vile vile kutoa mapendekezo kwa uongozi wa taasisi kuhusiana na dosari zilizobainishwa.

12.8.1 Dosari katika Mfumo wa zamani wa ZanMalipo

Ukaguzi wa mfumo wa kielektroniki wa ZanMalipo wa zamani uliofanyika kwa Wakala wa Serikali Mtandao umeangalia vipengele mbali mbali ikiwemo wajibu, haki na majukumu ya eGAZ katika usimamizi, uendeshaji, uratibu na kutoa ushauri kwa masuala ya TEHAMA Zanzibar kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa kwake ya mwaka 2019 viliangaziwa ambapo ukaguzi ulibaini mambo mbalimbali ikiwemo dosari zifuatazo.

12.8.1.1 Uwekezaji usiokuwa na tija kwenye kutengeneza mfumo shilingi 96,000,000

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa uwekezaji usiokuwa na tija wenye thamani ya zaidi ya shilingi 96,000,000 kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa ZanMalipo wa zamani, kazi iliyofanywa na wataalamu wa ndani chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango mwaka 2021 ambapo mfumo huo haukuweza kukidhi mahitaji ya biashara (business requirements) na mahitaji ya watumiaji (users' requirements) ndani ya kipindi kifupi cha miezi 5 na kupelekea kusitishwa utekelezaji wake.

Hali hii imeisababishia Serikali hasara ya moja kwa moja isiyopungua shilingi 96,000,000 na hasara nyengine zisizo za moja kwa moja kama vile muda uliotumiwa na wataalamu wa Serikali kwenye utengenezaji wa mfumo husika, rasilimali nyengine kama vile umeme, mtandao na miundombinu ya TEHAMA iliyonunuliwa kwa ajili ya mfumo huo n.k. ambavyo havikuweza kuthaminishwa kwenye fedha kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu zake.

Ukaguzi unashauri kufanyika mambo yafuatayo: -

- eGAZ kuhakikisha inazingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kama vile "Software Development Life Cycle" katika utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki ili kuepusha hatari za kushindwa kukidhi matakwa ya kiusalama, usiri, tija na ufanisi kwa kuzingatia mahitaji ya biashara na watumiaji kwa kuwa miongozo hiyo imekwisha tumika kwenye sekta ya TEHAMA kwa muda mrefu na kuthibitika kuwa na ufanisi wa kutosha.
- Kuzingatiwa kwa weledi katika kazi zote za utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki kwenye hatua mbali mbali bila kujali misukumo (pressures) inayokuwepo kutoka kwa wadau mbali mbali ambayo mara nyingi inakuwa haizingatii weledi, ukubwa na uzito wa kazi, na masuala mengine kama vile usalama, usiri, tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki.
- eGAZ kufanya tathmini ya kina na kuandika ripoti kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwenye visababishi vilivyopelekea mfumo wa ZanMalipo wa zamani kushindwa kufikia malengo yake na kupelekea kusitishwa na kuanzisha mfumo mwengine ili kupata fundisho lililotokana na mazingira ya ndani ya nchi litakalo weza kutumika kama rejea (reference) kwenye kuboresha utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki kwa kutumia wataalamu wa ndani.

12.8.1.2 Kutozingatiwa kwa miongozo ya Viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mfumo "SDLC"

"Software Development Life Cycle (SDLC)" ni mpangilio wa kimantiki (logical process) unaotumiwa na wachambuzi na wasanidi wa mifumo ya kielektroniki (system analysts and developers) katika kutengeneza mifumo. "SDLC" inapelekea kupatikana kwa mifumo yenye ubora wa juu inayokidhi au kuzidi mahitaji ya biashara na yale ya watumiaji na kwamba mifumo husika inakamilika ndani ya wakati na bajeti na kuleta tija na ufanisi. Mifumo inayotengenezwa kwa kuzingatia "SDLC" pia huwa na gharama nafuu za matengenezo na maboresho ambazo zinahakikisha matumizi endelevu ya mfumo (cost effective maintenance and enhancements).

Ukaguzi umebaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani haukuzingatia miongozo ya "SDLC" jambo ambalo limepelekea mfumo huu kushindwa kukidhi haja za biashara na mahitaji ya watumiaji ndani ya kipindi cha miezi 5 tangu ulipoanza kutumika hali iliyopelekea kuisababishia Serikali hasara ya moja kwa moja kwenye gharama za uwekezaji wa kutengeneza mfumo zinazozidi shilingi 96,000,000 na hasara nyengine za kushindwa kudhibiti na kusimamia ukusanyaji wa mapato kama ilivyotarajiwa na kusababisha upotevu wa mapato. Aidha, kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kutegemea TEHAMA ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama kwa Serikali za kuwafikiwa wananchi vimekwamishwa na udhaifu huu ambao ungeweza kuepukika kama miongozo ya "SDLC" ingezingatwa tangu mwanzo wa utengenezaji wa mfumo huu.

Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuzingatia "best practice guidelines" kama vile "SDLC" katika utengenezaji wa mifumo yote ya kielektroniki ili kuisaidia Serikali kuepuka hasara za aina mbali mbali kama zilivyojadiliwa hapo juu na kuongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wananchi na kuongeza makusanyo ya Serikali.

12.8.1.3 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za usimamizi wa matumizi ya mfumo.

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani hauna nyaraka zozote zinazohusiana na mfumo ikiwa ni pamoja na nyaraka muhimu katika matumizi ya mfumo inayoelezea namna mfumo unavyofanya kazi (system operations manual), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanifiwa (system architecture document), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanidiwa (system configurations manual), na nyaraka nyingine kama vile za mahitaji ya mfumo (system requirements document), na ile ya kuidhinisha matumizi ya mfumo baada ya kujaribiwa na kukidhi vigezo (Users Acceptance Certificate) n.k ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumi ya kielektroniki kama vile SDLC. Kutokuwepo kwa nyaraka hizo kunaweza kutokezea athari zifuatazo:-

- Mfumo kuwa ni mali ya mtu/watu wachache badala ya taasisi, hali hii inatokana na ukweli kwamba aliyeutengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote ile, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofisini basi mfumo hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na kuinyima taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa na Serikali.

- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k kwani uandishi wa nyaraka mbalimbali za mfumo unawapa nafasi wadau mbali mbali wa mfumo kuchangia mawazo yao katika namna ambayo ni rasmi ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuidhinisha nyaraka husika ili kuendelea na hatua nyengine jambo linalo changia kuboresha mfumo unaotengenezwa.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa na upeo mdogo kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mengine kirahisi kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo ambalo linarudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- Tasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda na jitihada zilizotumika hadi kukamilika kwa mfumo , jambo hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- Taasisi kushindwa kudhibiti matumizi, muda na ubora wa mfumo husika kwa sababu hakuna mpango kazi ulioandikwa na kuidhinishwa na uongozi wa taasisi.
- Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.

Kwa kuzingatia uhalisia uliopo kwamba, mfumo wa ZanMalipo wa zamani bado unatumika kwenye baadhi ya taasisi za umma na kwamba eGAZ haina mpango maalumu unao oneshwa muda ambao mfumo utakuwa umetolewa kwenye matumizi, ukaguzi unaishauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

- a) Kuchukuwa jitihada za makusudi za kuandaa nyaraka zote muhimu za matumizi, usimamizi na uendeshaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.
- b) Kuhakikisha kwamba nyaraka husika zinapatikana kwa ajili ya matumizi ya ndani ya taasisi ikiwa ni pamoja na matumizi ya ukaguzi.
- c) Kutatua changamoto mbali mbali zinazokabili mfumo wa ZanMalipo wa zamani ili kuondoa udhaifu uliopo sasa unaosababisha Serikali kupoteza mapato kwa njia mbali mbali.

12.8.1.4 Kutofahamika kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo wa zamani wa ZanMalipo

Kwa mujibu wa Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2021 kumewekwa utaratibu unaolazimisha taasisi za umma kuandaa bajeti kwa ajili ya kutekeleza mipango ya taasisi husika kabla ya kuanza utekelezaji wa kazi husika, bajeti hii hupaswa kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kabla ya kuanza kutumika. Pamoja na manufaa mengine yaliyopo kwa kuandaa bajeti ni udhibiti wa matumizi yanayofanywa na taasisi za umma pamoja na kuweka uwazi na uwajibikaji.

Hata hivyo, Wakala wa Serikali Mtandao imeshindwa kuupatia ukaguzi nyaraka za Bajeti ya utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani ambazo nyaraka hizo zilitarajiwa kuonesha kiwango cha makisio ya fedha yaliyotarajiwa kutumika kwa ajili ya utengenezaji, usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa mfumo huo.

Kutokuwepo kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo huo kunapelekea taasisi kushindwa kufanya tathmini ya ufanisi wa mipango yake kwa kulinganisha na gharama halisi kwenye utekelezaji (budget Vs actual costs), kunasababisha ugumu kwenye kazi za ukaguzi, ni kuvunja Sheria na Kanuni za Nchi zilizowekwa kwa nia njema ya kufanya usimamizi na matumizi bora ya rasilimali za Serikali. Uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa jina la gharama za utengenezaji wa mfumo ni mojawapo ya athari zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya kutokuwa na bajeti ambayo inaweka udhibiti wa matumizi hayo.

Ukaguzi unaishauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

- Kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inapata bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani kwa matumizi ya ndani ya taasisi kwa madhumuni kama ilivyoainishwa hapo juu.
- Kwa manufaa ya siku zijazo, ukaguzi unashauri eGAZ kuhakikisha takwa la uwepo wa bajeti linazingatiwa kabla ya kutengeneza au kununua mfumo au miundombinu yoyote ya TEHAMA ili kuepuka kuvunja Sheria za nchi.

12.8.1.5 Udhaifu wa mfumo katika utengenezaji wa Nambari za Udhibiti (Control Numbers)

Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu katika hatua ya kuchakata taarifa (Data processing) katika Mfumo wa ZanMalipo wa zamani hali ambayo imepelekea kutolewa nambari za udhibiti zaidi ya moja zenye taarifa zinazofanana kwenye ombi moja la kutengeneza "control number" kwa wakati mmoja, kurudia namba za udhibiti lakini pamoja na kutoa nambari za udhibiti ambazo zikipelekwa benki ya PBZ kwa ajili ya kufanyiwa Malipo zinabainika kuwa hazifanyi kazi kunapelekea kujitokeza kwa usumbufu mkubwa kwa wananchi na kusababisha kuikosesha mapato Serikali. Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali Mtandao kufanya yafuatayo:-

- Kuhakikisha kuwa mfumo wa ZanMalipo mpya unafanyiwa majaribio kwa kina katika kuangalia changamoto za ZanMalipo ya zamani ili kuhakikisha kwamba hazijirudii kwenye ZanMalipo mpya.
- Kufanya tathmini ya kina ili kubaini chanzo cha kutofanya kazi kwa baadhi ya nambari za udhibiti pindi zinapopelekwa benki ya PBZ kufanyiwa malipo kwa kushirikiana na wataalamu wa mfumo wa MUTM na Benki ya PBZ.
- Kutatua changamoto itakayobainika kwenye chanzo cha changamoto husika ili kundoa kabisa tatizo hili.
- Kutekeleza mfumo wa ZanMalipo mpya kwa uharaka wa kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa ili kuona kama udhaifu wa nambari za udhibiti kutofanya kazi wakati wa kufanyiwa Malipo litatatulika.

12.8.1.6 Kutumika vibaya kwa mianya inayotokana na udhaifu wa mfumo

Ukaguzi umebaini kuwa kuna mianya ambayo imekuwa ikitumika vibaya na baadhi ya watumiaji wa mfumo wa MUTM uliunganishwa na mfumo wa ZanMalipo wa zamani katika kutengeneza

nambari za udhibiti kupitia POS zilizounganishwa na mfumo wa MUTM na kupeleka fedha benki ya PBZ.

Wakusanya mapato wanapewa Nambari ya udhibiti (Control Number) kila mwisho wa siku ya kazi kwenye maeneo yao, nambari hiyo inaendana na kiwango walichokusanya ili waweze kuzipeleka fedha hizo benki. Hata hivyo, ukaguzi umebaini baadhi ya wakusanya mapato hawaendi benki kwa wakati na kuziacha nambari za udhibiti kumaliza muda wake kwa makusudi (expire) au kuzungumza na mtu mwenye akaunti yenye uwezo wa kuzighairisha "Cancel" na kupanga kulipa siku anayoitaka mkusanya mapato, kama akiaumwa basi huomba atengenezewe "control number" nyengine na mtu mwenye uwezo wa kutengeneza namba hiyo ambapo anaweza kutengeneza nambari ya udhibiti na kuipa kiwango chengine ambacho sio halisi kama kilivyokusanywa katika siku husika.

Hali hii inaweza kusababisha wakusanya mapato kutumia fedha za Serikali kwa lengo la kuzirejesha siku nyengine lakini wakashindwa kuzilipa kwa uaminifu na kuisababishia upotevu wa mapato na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri Wakala kufanya tathmini ya mapungufu yaliyobainika kwenye matumizi ya mfumo wa ZanMalipo wa zamani uliunganishwa na mfumo wa MUTM na mifumo mengine ili kuchukuwa hatua za makusudi kuzuia upotevu wa fedha za Serikali kwenye mifumo yote miwili ya ZanMalipo (wa zamani na wa sasa)

Aidha, ukaguzi unaishauri Wakala kuhakikisha kwamba tatizo la kutofanya kazi kwa nambari za udhibiti zinapotakiwa kulipiwa Huduma ya benki ya PBZ kunapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili isitumike kama chanzo cha upotevu wa mapato ya Serikali.

12.8.1.7 Kukosekana kwa ripoti mbali mbali za mapato kutoka kwenye mfumo

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani hauna uwezo wa kutoa ripoti mbali mbali za makusanyo ya mapato ya Serikali kwa lengo la kurahisisha ufanyaji wa Kimaamuzi kwa wakati. Aidha, Wakala wa Serikali Mtandao umeshindwa kuupatia ukaguzi ripoti mbali mbali za mapato zilizoombwa kwa ajili ya kazi za ukaguzi kutoka kwenye mfumo, ripoti hizo zilitarajiwa kuwa na uwezo wa kuonesha taarifa za makusanyo ya fedha za Serikali kwa kuzingatia "parameters" mbali mbali kama vile makusanyo kwa kila taasisi au taasisi zote za Serikali, kwa siku, wiki, mwezi, miezi mitatu, nusu mwaka na mwaka mzima, makusanyo kwa kuzingatia vyanzo mbali mbali vya mapato n.k.

Kukosekana kwa ripoti hizo kunauweka mfumo wa ZanMalipo kwenye kundi la mifumo isiyokuwa na ufanisi katika kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya uwepo wa mfumo husika na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa eGAZ kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba mfumo huu unakuwa na ripoti zote muhimu (basic reports) zinazoweza kuwasaidia maafisa masuuli na Serikali kwa ujumla kupata taarifa zilizochakatwa na kutafsiriwa ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi sahihi na kwa wakati ili kuleta tija na kuongeza ufanisi, uwazi, na uwajibikaji kwenye taasisi za umma.

12.8.2 Dosari kwa upande wa Mfumo wa ZanMalipo mpya

Katika ukaguzi wa mfumo mpya wa ZanMalipo mambo mbali mbali yalibainika zikiwemo dosari zifuatazo.

12.8.2.1 eGAZ kutokuwa na bajeti ya utekelezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo

Ukaguzi umebaini kwamba eGAZ inafanya utekelezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo ambao ulianza kufanya kazi mwishoni mwa mwaka 2021 pasipo kuwa na bajeti ya kufanya kazi hizo. Ukaguzi ulifahamishwa kwamba bajeti ya utekelezaji wa ZanMalipo mpya iko Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (ORFM) na kwamba panapohitajika fedha kwa ajili ya kazi mbali mbali za utekelezaji wa mfumo huo eGAZ inaandaa mpango kazi kwa ajili ya kutekeleza kazi husika na kuuwasilisha ORFM kwa ajili ya kufanyiwa Malipo.

Hali hii inaweza kupelekea kutopatikana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mfumo ikiwa ni pamoja na kazi za mbali mbali za mfumo kutofanyika kwa wakati na kukosa urahisi wa kubadilisha mipango kazi "flexibility" katika utekelezaji kwa sababu bajeti na fedha za utekelezaji huo zipo kwenye taasisi nyengine ambayo pia inaweza kuwa na vipaumbele tofauti katika majukumu yake ya kila siku na kuweka mipango kazi ya eGAZ kwenye umuhimu mdogo.

Aidha, hali hii inaongeza ugumu wa kutunza kumbu kumbu za bajeti dhidi ya gharama halisi, thamani kamili ya mfumo, kuongeza ugumu kwenye kazi za ukaguzi kwa kuwa inalazimisha ukaguzi wa mfumo mmoja kufanyika kwenye taasisi zaidi ya moja hali ambayo inachangia ukaguzi kuchukuwa muda mrefu tofauti na mpango wa ukaguzi ili kukamilika.

Ukaguzi unashauri kwamba, ili kuhakikisha eGAZ inatekeleza mifumo ya kielektroniki kwa ufanisi na tija, bajeti na fedha zinazohitajika kwa ajili ya kufanikisha kazi za utekelezaji wa mifumo hiyo zipewe eGAZ ili iweze kupanga na kutekeleza kazi hizo kwa kuzingatia rasilimali na vipaumbele vyake. Aidha, hatua hii itarahisisha utunzaji wa kumbukumbu za bajeti na gharama halisi zilizotumika katika kutengeneza mfumo husika, itahakikisha pia kwamba kazi za ukaguzi zinafanyika kwa kuzingatia mpango wa ukaguzi kwani nyaraka zote zinazo hitajika zitapatikana kwenye taasisi moja, thamani halisi ya mfumo itaweza kupatikana kiurahisi na kuingizwa kwenye daftari la mali (asset register) za taasisi.

12.8.2.2 Kutojulikana kwa gharama zilizotumika kwenye utekelezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo

Ukaguzi umebaini kwamba eGAZ kama mtekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo na msimamizi mkuu wa masuala yote ya Serikali Mtandao hapa nchini haina kumbukumbu za gharama halisi zilizotumika kwenye utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2022 ambapo ni kinyume na matakwa ya Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake za mwaka 2021.

Udhaifu kwenye utunzaji wa kumbu kumbu za gharama halisi za utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo unaweza kutumika kama mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali, aidha, hali hii ni chanzo kikuu cha mifumo inayotengenezwa na wataalamu wa ndani kutojulikana thamani yake na

kushindwa kuingizwa kwenye daftari la mali za Serikali (Asset Register), pia kuinyima Serikali fursa ya kupata tathmini ya maamuzi iliyofanya ya kutengeneza mfumo husika kwa kutumia wataalamu wa ndani yakilinganishwa na maamuzi ya kununuwa mifumo.

Ukaguzi unashauri eGAZ kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inakusanya taarifa zote za matumizi halisi (actual expenditures) yaliyowahi kufanyika na yanayoendelea kufanyika kwa ajili ya mfumo wa ZanMalipo mpya kuanzia kwenye kuandaa mikakati, mipango kazi, kutengeneza mahitaji ya biashara na watumiaji, kununua miundombinu (mtandao, vifaa na programu), utengenezaji wa mfumo, mafunzo, usaidizi wa kutumia mfumo (Go Live Support) na kuendelea kutoa msaada kwa watumiaji wa mfumo (implementation support) ili kuweza kujua thamani halisi ya mfumo huo na kulinganisha na bajeti yake ili kubaini ufanisi uliopatikana kwenye mipango na matumizi ya fedha za umma.

12.8.2.3 Kukosekana kwa mpango kazi wa utekelezaji wa mfumo (implementation plan) wa ZanMalipo mpya unaojumuisha mafunzo, majaribio ya mfumo, na kuanza kutumika kwa mfumo kwenye taasisi za umma

Ukaguzi umebaini kuwa eGAZ haina mpango kazi wa utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya, mpango kazi huu ulitarajiwa kuonesha pamoja na mambo mengine ratiba jumuishi ya matukio yote yanayotarajiwa kufanyika ili kukamilisha utekelezaji wa mfumo huu. Matukio haya ni pamoja na ukusanyaji wa mahitaji ya biashara na watumiaji wa mfumo, uchambuzi wa mahitaji, kujenga mfumo (system customization), mafunzo ya mfumo, majaribio ya mfumo, usambazaji wa mfumo (system deployment), kuanza kutumia mfumo (Go Live), na kufunga mradi (project closure) kwa taasisi zote za umma.

Aidha, ukaguzi uliomba kupewa ripoti ya mafunzo ambayo yametolewa na eGAZ kwa taasisi za umma tangu kuanza utekelezaji wa mradi wa ZanMalipo mpya, hata hivyo ukaguzi haukupatiwa ripoti hiyo kwa majibu kwamba haipo.

Kukosekana kwa mpango kazi wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa utengenezwaji wa mfumo wa ZanMalipo ambao unatarajiwa kuzifikia taasisi za umma zisizopungua 117 na watumiaji wasiopungua 250 na kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu kwenye kusimamia mapato ya nchi ni udhaifu mkubwa kwenye usimamizi wa mradi wa TEHAMA chini ya uangalizi wa Wakala wenye dhamana ya kusimamia TEHAMA nchini.

Hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi na tija ya mradi kwenye idadi ya taasisi za umma zilizotakiwa kufikiwa baada ya muda uliopangwa kwa sababu ya kukosekana kwa vigezo husika ambavyo vingekuwemo kwenye mpango kazi, muda unaotumika kukamilisha kazi husika ni eneo jengine ambalo limeachwa huru na linaweza pelekea mradi kutumia muda mrefu kukamilika na kupelekea kukosekana kwa tija, rasilimali zinazohitajika pia zimeachwa huru kwa kutoingizwa kwenye mpango kazi na inaweza kupelekea mradi kutumia rasilimali nyingi au chache na kukwamisha ufanisi wa mradi. Aidha, kukosekana kwa mpango kazi kunapelekea kuongeza ugumu kwenye kazi ya ukaguzi hususani kwenye kufanya tathimini ya utekelezaji wa mradi kwa kukosa vigezo (benchmarks) vya kufanyia ulinganifu.

Hivyo, ukaguzi unashauri Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha kuwa inaandaa mpango kazi maalumu wa utekelezaji wa mradi huu utakao jumuisha vigezo (parameters) mbali mbali kama vile taasisi zinazotakiwa kufikiwa, watumiaji wanaotarajiwa kufundishwa, na matukio mengine yote yaliyomo kwenye mradi kama vile kufanya majaribio ya mfumo (Users Acceptance Testing), kuanza kutumia kwa mfumo kwenye taasisi moja moja (Go Live), n.k. Mpango kazi huu unatakiwa uidhinishwe na Menejimenti ya eGAZ kabla ya kuanza kutumika.

12.8.2.4 Kasi ndogo ya usajili wa taasisi za umma kwenye mfumo wa ZanMalipo mpya

Katika ukaguzi uliofanyika wa Mfumo mpya wa ZanMalipo kwa Wakala wa Serikali Mtandao imebainika kwamba hadi sasa asilimia **26** pekee ya taasisi zote za umma ndio ambazo zilizosajiliwa kwenye mfumo tangu utekelezaji wa mfumo huu ulipoanza miezi mitano iliyopita kuanzia mwezi wa Novemba, 2021. Hata hivyo ni asilimia **18** ya taasisi za umma zilizosajiliwa ndizo ambazo zimeanza kutumia mfumo wa ZanMalipo mpya hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Machi, 2022.

Kiujumla hali hii ni sawa na usajili wa wastani wa asilimia **5** ya taasisi za umma kwa mwezi ambapo kwa kasi hii inaashiria kwamba eGAZ itachukuwa wastani wa miezi **20** ili kukamilisha usajili wa taasisi zote za umma.

Kuwepo kwa kasi ndogo ya usajili wa taasisi za umma katika mfumo mpya wa ZanMalipo kunaweza kupelekea kukosa udhibiti wa mapato jambo ambalo litapelekea kutitokeza kwa upotevu wa mapato na hatimae kuchelewesha maendeleo kwenye Jamii. Matumizi ya rasilimali nyingi zaidi kwenye utekelezaji wa mradi iliyosababishwa na muda wa utekelezaji kuongezeka.

Ukaguzi inaishauri eGAZ kufanya tathmini ya kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kubaini vikwazo vinavyopelekea kutumia muda mwingi kwa kaisi kilichoainishwa hapo juu na kuchukuwa hatua za kutatua vikwazo hivyo kwa haraka ili kunusuru hasara kwa Serikali inayotokana na upotevu wa mapato kwa kukosa udhibiti madhubuti unaotarajiwa kupatikana kupitia matumizi ya mfumo wa ZanMalipo mpya.

12.8.2.5 Kukosekana kwa ripoti mbali mbali za mapato kwenye mfumo wa ZanMalipo

ZanMalipo ni mfumo wa usimamiaji ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambao unalengo la kurahisisha ulipaji wa huduma za umma kwa kumuwezesha mlipaji kupata njia mbalimbali na rafiki za kufanya malipo kama vile kulipa kwa kutumia simu za kiganjani, Benki na Mawakala wa malipo. Hivyo, mfumo huu unatarajiwa kuwa na kumbukumbu zote za mapato yote ya Serikali yaliyopita katika mfumo huo kwa utaratibu wa kutumia nambari za udhibiti (Control Numbers) zilizotumika kulipia huduma kwenye taasisi za umma.

Hata hivyo, ukaguzi uliomba ripoti mbali mbali za mapato kutoka kwenye mfumo lakini ripoti hizo hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, miongoni mwa ripoti zilizoombwa ni pamoja na ripoti ya mapato ya taasisi moja moja kwa kila mwezi wa ukusanyaji, ripoti ya jumla ya ukusanyaji wa mapato, n.k. Kwa kuzingatia matarajio yaliyopo ya mfumo wa ZanMalipo mpya kwa watumiaji na wadau mbali mbali mfumo huu unatarajiwa kutoa taarifa toshelezi kubaini makusanyo kwa taasisi

moja moja, kwa ngazi ya Wizara nzima, kwa Serikali yote kwa kila wakati (real time collections), kwa siku, wiki, mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, mwaka n.k taarifa ambazo ni za msingi kuwepo kwenye mfumo ili kupata tija na udhibiti kwenye makusanyo.

Kitendo cha mfumo wa ZanMalipo kukosa ripoti hizo ni udhaifu wa mkubwa kwenye mfumo kwani matarajio ya watumiaji, Serikali na wadau mbali mbali hayajafikiwa na kuashiria kutopatikana kwa tija na ufanisi wa mfumo kwa hatua uliyofikia.

Kwa kuwa ripoti hizi zinatarajiwa kurahisisha kuonekana (visibilty) kwa picha kamili ya mapato kuanzia ngazi ya taasisi mpaka kwenye ngazi ya Serikali nzima ukaguzi inaishauri eGAZ kuhakikisha ripoti hizo zinatangenezwa na kuwekwa kwenye mfumo na kwamba zinapatikana kwa ajili ya matumizi ya wadau mbali mbali wa mfumo huo kulingana na nafasi zao.

12.8.2.6 Kukosekana kwa nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo (System users' matrix document)

"System user's matrix" ni nyaraka inayofafanua majukumu ya makundi mbali mbali yanayotumia mfumo ikiwa ni pamoja na wasimamizi wa mfumo, nyaraka hii huandaliwa kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu na udhibiti wa ndani wa taasisi (internal controls) na kuhakikisha kwamba mtumiaji mmoja hawezi kufanya kazi kwenye mfumo zinazomuwezesha kukamilisha mzunguko mzima peke yake, hususani kwenye maeneo yenye hatari. Hivyo nyaraka hii ni muhimu ili kuweza kutambua watumiaji wa mfumo wanafanya kazi kulingana na majukumu yao ya kazi za kila siku na kuweza kuwazuia kufanya vitendo nje ya majukumu na mamlaka yao.

Msingi wa nyaraka hii ni "Segregation of Duties (SoD)" kama ilivyo ainishwa kwenye miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) ya ISACA. Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kupata nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo mpya wa ZanMalipo.

Kutokuwepo na hati hii kunaweza kupelekea mtumiaji wa mfumo kupewa ruhusa ya kufanya kazi kinyume na majukumu yake pamoja na mipaka yake jambo ambalo linaweza kusababisha kujitokeza kwa mianya ya upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali wa kufanya ubadhirifu wa fedha za umma, kubadilisha taarifa za mapato kwenye taasisi kwa manufaa binafsi, chanzo cha rushwa n.k.

Hivyo, ukaguzi unashauri kuwa itengenezwe nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo kwa nafasi zao kama vile Muhasibu, Muhasibu Msaidizi, Afisa TEHAMA, n.k ili kuweza kubainisha wazi majumu ya watumiaji wa mfumo na kuona kama kuna uwiyo na kazi zao za kila siku pia kuweza kuhakikisha kuwa mtumiaji wa mfumo anapata taarifa kutoka katika mfumo kulingana na majukumu yake.

12.8.2.7 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za mfumo mpya wa ZanMalipo

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo mpya wa ZanMalipo hauna nyaraka muhimu zinazohusiana na mfumo ikiwa ni pamoja na nyaraka za mahitaji ya mfumo (system requirements document), nyaraka ya kujaribu na kuidhinisha matumizi ya mfumo (Test Cases and Users Acceptance Certificate) n.k ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumi ya kielektroniki kama vile SDLC. Miongoni mwa athari zinzoweza kutokea kwa kukosekana kwa nyaraka hizo muhimu ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya mfumo ya sasa na ya wakati ujao katika upande wa biashara, watumiaji, usalama, udhibiti, ufikiaji, urahisi wa matumizi n.k.
- b) Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kukosa sifa ya kuingilianoan "interoperability" na mifumo mengine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia.
- c) Kusababisha hasara kwa Serikali kwa kutengeneza mfumo ambao haujakidhi matakwa ya biashara na mahitaji ya watumiaji wa mfumo na kusababisha mfumo kutokuendelea kutumika.

Kwa kuzingatia uhalisia uliopo kwamba, mfumo wa ZanMalipo mpya ndo kwanza unaanza utekelezwaji wake na kwamba Serikali bado ina kumbu kumbu za kutofanikiwa kwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani. Ukaguzi unashauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

- d) Kuchukuwa jitihada za makusudi za kuandaa nyaraka ya mahitaji ya mfumo ya mfumo ili kuhakikisha kwamba mfumo unaotekelezwa unaweza kupimwa ufanisi na tija yake.
- e) Kuandaa nyaraka ya vigezo vya majaribio ya mfumo (test cases document) na kuhakikisha kuwa inatumiwa kuujaribu na kudhibitisha ufanisi wa mfumo kabla haujaendelea kutumika kwenye taasisi zote za umma ili kuhakikisha kwamba mahitaji yote muhimu ya watumiaji nay ale ya biashara yamezingatiwa na kama kuna mapungufu yawekewe utaratibu wa kuyapatia ufumbuzi.
- f) Kuhakikisha kwamba nyaraka husika zinapatikana kwa ajili ya matumizi ukaguzi.

12.8.3 Dosari kwenye udhibiti wa jumla na uendeshaji wa TEHAMA

12.8.3.1 Kukosekana kwa Mpango wa uendeshaji wa TEHAMA kwa ngazi ya eGAZ na ngazi ya nchi (ICT Governance Framework).

Mpango wa uongozaji wa TEHAMA kwa ujumla unatoa muongozo kwa taasisi za Umma katika kutengeneza sera, viwango na taratibu bora zinazokubalika katika uongozaji na usimamizi wa rasilimali za TEHAMA ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaongeza tija na ufanisi katika kufanikisha taasisi kufikia malengo waliyojiwekea.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao bado haijatoa Mpango wa Uongozaji wa TEHAMA katika sekta za Umma. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5(e) cha Sheria Nambari 12 ya mwaka 2019 ambapo Wakala imetakiwa kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine za kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa Umma Zanzibar.

Athari za kukosekana kwa "ICT Governance Framework" inajumuisha: -

- Taasisi za umma kukosa muongozo rasmi wa kufuatwa katika uendeshaji wa TEHAMA nchini jambo linalopelekea ugumu kwenye kupima tija na ufanisi wa uendeshaji wa TEHAMA nchini.
- Kukosekana kwa udhibiti madhubuti wa TEHAMA kwa taasisi za umma kwa kuwa kila taasisi inakuwa huru kufuata au kutofuata framework yoyote ile.
- Kuhatarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA nchini.

Ukaguzi unashauri Wakala wa Serikali Mtandao, kuhakikisha wanaandaa na kutoa mpango wa uongozaji wa TEHAMA kwa taasisi za Umma ili kuenda sambamba na madhumuni ya uanzishwaji wa Wakala kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 5 (e) cha sheria nambari 12 ya mwaka 2019.

12.8.3.2 Kukosekana kwa Sera na Miongozo toshelevu ya Usimamizi na matumizi ya TEHAMA katika ngazi ya eGAZ na Taifa kwa ujumla

Sera, Miongozo na Kanuni za matumizi, usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA ni nyenzo muhimu sana katika kufikia adhima ya Serikali Mtandao ambayo inalenga kuwezesha utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa mbali mbali kwa umma kwa gharama nafuu na kwa uharaka zaidi ili kuleta tija na ufanisi Serikalini kupitia TEHAMA. Taasisi za umma zinatarajia kupata Sera, Miongozo na Kanuni mbali mbali za matumizi sahihi, salama, na endelevu ya TEHAMA kutoka kwa eGAZ ili kuhakikisha kwamba uwekezaji kwenye TEHAMA unakwenda sambamba na thamani ya fedha, manufaa ya uwekezaji husika (Return on Investments), miradi inakamilika kwa wakati, inakidhi malengo na dira ya taifa n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar imebainika kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika eneo la kutengeneza Sera, Miongozo na Kanuni zinazojitosheleza ambazo zitatumika kwenye usimamizi, uendeshaji, na matumizi ya TEHAMA nchini, hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na Wakala kujikita zaidi kwenye utengenezaji, utekelezaji (implementation), usimamizi (administration) wa mifumo ya TEHAMA, kazi ambayo inahitaji uzingatiaji na muda mwingi ili kuzifanikisha na kupelekea kudorora kwa utengenezaji wa Sera, Miongozo na Kanuni za TEHAMA. Aidha, uchache wa rasilimali watu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha kwenye eneo la kutengeneza Sera na Miongozo ni sababu nyengine iliyochangia kutokea kwa udhaifu katika utengenezaji wa sera na miongozo ambapo linapelekea athari hususan linapokuja suala la usimamizi, uendeshaji na matumizi sahihi ya TEHAMA yenye kuleta tija na ufanisi katika utumishi wa umma.

Miongozo kama vile Mikakati ya TEHAMA ya taifa iliyoimarishwa (updated) ni chanzo muhimu kwa taasisi za umma kutengeneza mikakati yao kwa kuzingatia muelekeo wa taifa ambapo linashajihisha matumizi ya rasilimali za umma kwenye njia na malengo yaliyopangwa kuanzia ngazi ya taifa.

Kwa mara ya mwisho Sera ya TEHAMA ilitengenezwa mwaka 2012, hata hivyo Sera hii haijaelezea kwa undani namna ya utekelezaji wake, na hakuna sera nyengine yoyote iliyoelezea miongozo na viwango vya kufuata mpaka mwaka mnamo mwaka 2021 ambapo eGAZ ilipotoa toleo la manunuzi na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA.

Kukosekana kwa Sera, Miongozo na Viwango toshelevu vya TEHAMA ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5 (e) cha sheria Nambari 12 ya mwaka 2019 ambapo Wakala imetakiwa kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine za kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa Umma Zanzibar. Aidha, hali hii inachelewesha kupatikana kwa manufaa yaliyotarajiwa ya uwekezaji unaofanywa na taasisi mbali mbali za umma kwenye TEHAMA kwa sababu ya kukosa uangalizi na usimamizi wa karibu kupitia Sera, Miongozo na Viwango vya TEHAMA. Uwepo wa mifumo zaidi ya mmoja ambayo kwa sehemu kubwa inafanya kazi zinazofanana ndani ya taasisi moja ni mojawapo ya athari za mdororo wa usimamizi wa TEHAMA katika ngazi ya nchi.

Ukaguzi unashauri mabo yafuatayo: -

- Wakala wa Serikali Mtandao iwekeze muda na jitihada zake nyingi zaidi kwenye kutengeneza Sera, Miongozo na Viwango toshelevu kwa ajili ya matumizi, usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA kwenye taasisi za umma ili kuziwezesha taasisi hizo kujiongoza kwa kufuata miongozo hiyo na kuleta tija kwa wingi na kwa mara moja.
- Ili kwenda na kasi ya mabadiliko yanayotokea kwenye TEHAMA katika kubaini mabadiliko ya teknolojia zilizopo, mpya na hatari (risks) zinazoambatana nazo na kuzitengenezea Miongozo na Viwango toshelevu vya kukabiliana nazo Wakala inashauriwa kuweka utaratibu na mazingira wezeshi ya kukutana na wadau wa kimkakati muhimu kwenye TEHAMA wanaojumuisha sekta za umma na binafsi ili kuchukuwa mawazo yao na kuyaratibu katika utekelezaji angalau mara moja kwa mwaka.
- Kufanya mapitio ya Sera, Miongozo na Viwango vya TEHAMA angalau kila baada ya miaka 3 ili kubaini mapungufu na kuyafanyia kazi katika kuhakikisha kwamba miongozo husika inabakia hai na yenye tija.

12.8.3.3 Kukosekana kwa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa na kwa ngazi ya eGAZ

Mpango mkakati wa TEHAMA hufafanua maono ya taifa/taasisi ya TEHAMA na kuunda ramani ya kimkakati ya kutumia TEHAMA, rasilimali za kidijitali na maarifa ya kiufundi ili kuunda thamani ya taifa/taasisi husika.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 6(a) cha Sheria ya kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao kinaelezea kuwa moja katika kazi za Wakala wa Serikali mtandao ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera za TEHAMA, kanuni na miongozo katika utumishi wa umma. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao haijaandaa mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa ikiwa ni moja kati ya majukumu yake kwa mujibu ya sheria. Aidha, Wakala wa Serikali mtandao imebainika kutokuwa na Mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA katika ngazi ya Wakala yenyewe.

Kukosekana kwa mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kunaweza kupelekea taifa kutokuwa na muelekeo mzuri wa TEHAMA utakofahamika kwa wadau na taasisi za umma jambo ambalo linaweza kupelekea taasisi za umma kushindwa kutegemea, kupanga na kufuata ipasavyo mikakati na malengo endelevu ya Taifa na kupelekea kutopatiakana kwa ufanisi na kupungua kwa kasi ya maendeleo ya Nchi kwa ujumla.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali Mtandao kufanya jitihada za makusudi za kuandaa Mpango Mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa kuzingatia dira na muelekeo wa nchi kwa ngazi ya Wakala na ngazi ya Taifa, na kuhakikisha kwamba mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa unawafikia wadau mbali mbali pamoja na taasisi zote za umma.

12.8.3.4 Kutokuwepo kwa makubaliano ya ushirikiano (MoU) kati ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na Wakala wa Serikali Mtandao Tanzania bara

Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafanya mashirikiano na Wakala wa Serikali Mtandao Tanzania bara katika kupatiwa huduma na rasilimali mbali mbali za TEHAMA. Hadi ukaguzi unakamilika, Wakala wa Serikali Mtandao umeshindwa kutoa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo mbili.

Kutokuwepo kwa makubaliano rasmi baina ya pande hizi mbili zinazofanya kazi za kusimamia mifumo, kushirikiana katika kazi za mifumo ikiwa ni pamoja na kuchangia wataalamu na rasilimali nyengine za TEHAMA kunaweza kupelekea athari mbali mbali kwenye mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika maeneo ya usalama, matumizi endelevu ya mifumo na hali ya umiliki wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kwa kuweka makubaliano ya ushirikiano (Memorandum of Understanding) ambapo kimsingi makubaliano hayo yatatoa ufafanuzi wa haki na wajibu wa kila upande na kuelezea matarajio ya kiwango cha huduma kitakachotolewa ili kuhakikisha kwamba muda na rasilimali nyengine zilizotumika kutengeneza mifumo iliyokamilika na inayoendelea kutengenezwa zinalindwa kwa makubaliano rasmi.

12.8.3.5 Udhaifu katika uelewa na mipango endelevu ya usalama wa mfumo wa ZanMalipo

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na masuala ya usalama wa mfumo "System Security" kwa mfano, hawana uelewa wa namna ya kuhakikisha taarifa za Serikali zinazohifadhiwa kwenye miundombinu ya eGA na kubakia salama kwa muda wote. Usalama wa mfumo huelezea vidhibiti na ulinzi ambao taasisi huhakikisha mfumo na miundombinu mengine iko salama dhidi ya kuingiliwa kwa nia mbaya. Hivyo lengo kuu la usalama wa mfumo ni ulinzi wa taarifa na miundombinu dhidi ya wizi, na uharibifu wa aina nyengine, huku ukiruhusu taarifa na miundombinu kupatikana wakati wote inapohitajika na kuleta tija.

Kutokana na kuwa Wakala wa Serikali Mtandao ina uelewa duni wa masuala ya usalama wa mfumo wa ZanMalipo katika masuala ya usalama kunaweza kupelekea kutofahamu njia zinazofaa kutumika kwa ajili ya kuendelea kuuweka mfumo salama pale ambapo utakapokuwa chini ya uangalizi wa Serikalini ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unashauri, wakala Serikali mtandao Zanzibar (eGAZ) kushirikiana na Mamlaka ya Serikali mtandao Tanzania (e-GA) ili kupata uelewa mpana na taaluma juu ya masuala ya usalama wa mfumo wa ZanMalipo kwa upana wake ambapo itasaidia katika kupunguza au kumaliza kabisa utegemezi kwenye eneo hili.

12.8.3.6 Kutofahamika kwa hali ya umiliki wa mifumo

Katika mapitio ya mfumo wa ZanMalipo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao haina uelewa kamili juu ya hali ya umiliki wa mfumo husika, hadi ukaguzi unakamilika haikuweza kujulikana bayana mfumo wa ZanMalipo ni mali ya SMZ kwa kupewa kama zawadi (grant), umekodishwa au kupewa na kwamba SMZ inautumia kama huduma tu.

Hivyo, kutofahamika kwa hali ya umiliki wa mfumo huo kunapelekea kutishia uendeleu wa mfumo (system sustainability) kwa sababu inakuwa ni vigumu kufahamu mipaka iliyopo baina ya pande mbili hizo. Ama kuwekeza kwenye mfumo, kununua miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kuusimamia mfumo ipasavyo au la.

Ukaguzi unashauri kuwa, Wakala wa Serikali Mtandao ifanye mazungumzo yaliyo bayana na eGA tangu mwanzo kuhusu hali ya umiliki wa mfumo huo na mifumo mengine iliyokuwa katika hali hiyo mapema iwezekanavyo na kuyaweka kwenye "MoU" makubaliano hayo ili yapatikane kwa matumizi ya ndani ya ofisi pamoja na kazi za ukaguzi na kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na utata wa hali ya umiliki.

12.8.3.7 Kukosekana kwa kumbu kumbu za taasisi za umma zilizopeleka maombi ya kufanyiwa tathimini, kuidhinisha ama kupatiwa ushauri wa kitaalamu na eGAZ kwenye masuala ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala hauna kumbu kumbu za taasisi za umma zilizowahi kupeleka maombi ya kufanyiwa tathimini, kupewa ushauri wa kitaalamu na kuidhinishwa mipango ya miradi ya TEHAMA kwa mujibu wa Toleo la Wakala la Manunuzi na Ufungaji wa Vifaa vya TEHAMA kwenye Sekta za Umma la mwaka Julai, 2021.

Kwa mujibu wa toleo la manunuzi na ufungaji vifaa vya TEHAMA katika sekta za umma lililotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao 13, Julai 2021 kipengele nambari 1(a) – (g) kinazitaka taasisi kupeleka maombi mbali mbali kwa ajili ya kupitiwa, kushauriwa na kuidhinishwa kabla ya utekelezaji (implementation), uimarishaji (upgrade) au ununuzi wa mfumo.

Kukosekana kwa kumbu kumbu hizo kunaashiria udhaifu wa Wakala katika kutimiza majukumu yake yaliyopo kisheria na kinyume na miongozo yake yenyewe, udhaifu wa Wakala katika kutunza kumbu kumbu, Wakala kutofanya tathmini ya utekelezaji wa miongozo na matoleo yake aidha, hali hii inaweza kupelekea athari mbali mbali zikiwemo zifuatazo: -

- Kukwamisha ufanyaji wa tathmini ya kupima ufanisi wa Wakala katika kuzihudumia taasisi za umma kwa mujibu wa miongozo yake.
- Ucheleweshwaji wa majibu ya mapitio, idhini, na ushauri wa kitaalamu kwa taasisi za umma.
- Kushindwa kupima ufanisi wa utekelezaji wa toleo/ miongozo kwa upande wa taasisi za Serikali.

12.8.3.8 Kutopitishwa kwa wakati Rasimu ya Sera za TEHAMA na Bodi ya Washauri ya eGAZ

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12(2) cha Sheria Nambari 12 ya Wakala wa Serikali mtandao ya mwaka 2019 kinaitaka Bodi kukaa vikao vyake kila robo mwaka na kuwasilisha ripoti yake kwa Waziri. Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba kwa kipindi cha miaka miwili 2020 na 2021 Bodi imekaa vikao 2 pekee kati ya vikao 8 ambavyo vilitakiwa kukaa.

Kwa mujibu wa kifungu 12(1)(b) Bodi ina jukumu la "kumshauri Waziri katika masuala ya maendeleo ya kisera na mikakati ya Serikali Mtandao".

Kupitia majadiliano na wakaguliwa ukaguzi ulifahamishwa kwamba Wakala iliandaa Rasimu ya Sera za uendeshaji na usimamizi wa TEHAMA ambayo haijakamilika kwa ajili ya matumizi kwasababu ilitakiwa ipitie kwenye vikao vya Bodi ili kuweza kumshauri Waziri kwa mujibu wa kifungu 12(1) (b) jambo ambalo limechukua muda mrefu kufanyika kwa sababu ya uchache wa vikao vya Bodi kama ilivyoainishwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri Wakala kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba Bodi inakaa vikao vyake kwa mujibu wa Sheria na kwamba Rasimu za Sera zinawasilishwa kwenye Bodi kwa ajili ya kupitiwa na kumshauri Waziri kama watakavyoona inafaa ili kupata Sera imara na kwa wakati kwani mabadiliko na vihatarishi vinavyojitokeza kwenye TEHAMA hayaangalii changamoto za ndani ya nchi.

12.8.3.9 Kukosekana kwa mkataba wa huduma kwa wateja wanaohudumiwa na Wakala wa Serikali mtandao (taasisi za umma).

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao haina mkataba wa Huduma kwa wateja kinyume na Sheria na Miongozo iliyopo Zanzibar, inayoelekeza kwamba taasisi za umma zinatakiwa kuwa na mkataba wa Huduma kwa wateja, ambapo pamoja na mambo mengine mkataba huu unatarajiwa kuonesha muda ambao eGAZ itachukuwa kuweza kukamilisha utoaji huduma zake kwa wateja mbalimbali na taratibu nyengine za kufuatwa na wateja ili kupatikana huduma kwa haraka na kwa ufanisi.

Kukosekana kwa mkataba wa Huduma kwa wateja kunaweza kupelekea kuzorota kwa utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuwa Wakala anajuwa kwamba wateja wake hawana misingi ya vipimo vya ubora wa huduma zinazotakiwa kutolewa ikiwa ni pamoja na muda na Huduma kwa wateja. Aidha, hali hii inaweza kusababisha kuongeza ugumu kwenye ufanyaji wa tathmini za ufanisi wa taasisi hususani wakati wa ukaguzi.

Hivyo basi, ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuandaa na kuutumia mkataba wa Huduma kwa wateja kwa kuzingatia miongozo ya ndani na viwango bora vinavyokubalika kwenye eneo hilo.

12.8.3.10 Kukosekana kwa Mpango wa kuendeleza huduma/ biashara baada ya kutokea maafa (Business Continuity Plan)

Kwa mujibu wa Sera za Wakala wa Serikali mtandao ya mwaka 2012 kifungu cha 4.4.1.2.(d) kinazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na kuweka miundombinu ya kuendeleza huduma za mfumo na taarifa zake baada ya kutekezea maafa dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea ni kwa utaratibu gani huduma zitaendelea wakati wa majanga na hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo wakati yatakapotokea majanga kama kwa mfano udukuzi, majanga ya kimaubile, yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala haina mpango huo unaotarajiwa kuwa ni muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo kupotea na kubainisha utaratibu wa kufanyika baada ya majanga kutokezea.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu zilizomo ndani ya mfumo kwa sababu Wakala kupitia taasisi mbali mbali za umma zinazotumia mifumo inayosimamiwa na Wakala kutojua nini kifanyike, hatua gani zichukuliwe na nani na wakati gani ili kupata matokeo tarajiwa kabla, wakati na baada ya tukio linaloweza sababisha upotevu mkubwa wa taarifa kama vile moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, wizi, uharibifu wa miundombinu, matumizi mabaya n.k.

Ukaguzi unaishauri Wakala kuandaa mpango huu kwa mujibu wa miongozo na sera za Wakala wa Serikali mtandao na kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa, aidha Wakala ijiwekee utaratibu wa kufanya majaribio angalau mara moja kwa mwaka mipango yote inayolenga kulinda taarifa pamoja na miundombinu ya TEHAMA ambayo imegharimu Serikali fedha nyingi, muda na juhudi kubwa kuziandaa, kuzichakata na kuzitunza.

12.8.3.11 Kutokuwepo kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan)

Mpango wa kupona maafa (disaster recovery plan) ni mpango ambao unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mlipuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake bila ya kutambua kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake mikuu kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Aidha, mpango huu una ainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali mtandao haina Mpango wa kupona maafa ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa vinavyosisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango, kuongeza tija kwa wafanyakazi kwa kuwa wanakuwa wanafahamu nini cha kufanya na kinafanywa na nani kwa wakati gani, kuelewa ukubwa wa kazi zinazotakiwa kufanyika na kuendelea kuwahudumia wateja wa taasisi husika.

Athari zinazoweza kujitokeza ikiwa eGAZ haina mpango wa kupona maafa na pindi itakapofikwa na maafa hayo ni pamoja na kusababisha hasara kwa kushindwa kuendelea na kutoa huduma ya ukusanyaji wa mapato kwa taasisi za umma zinazotumia mfumo wa ZanMalipo au kushindwa kufanya kazi kwenye mifumo mengine ya Serikali kama vile "e-Office", mfumo wa "Government Mail", kupoteza muelekeo kwa wafanyakazi kwa kutofahamu nini kifanyike na afanye nani kwa wakati gani na kupoteza tija na ufanisi kazini, kupoteza sifa ya Wakala katika kutegemewa kutoka huduma wakati wote.

Ukaguzi unashauri kutengenezwe mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unakuwa wa kujitosheleza kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

12.8.3.12 Kutokuwepo kwa mpango wa usimamizi na uratibu wa kufanya mabadiliko kwenye Mfumo (System Change Management Plan).

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao haina mpango rasmi wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo. Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea mifumo inayosimamiwa na Wakala kukosa muendelezo wa ubora (consistence of good quality) kwani inaweza kuwepo baadhi ya mabadiliko yanayofanywa kwenye mfumo ambayo madhara yake ni makubwa na kusababisha kushuka kwa ubora wa mfumo. Kwa sababu hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba mabadiliko yoyote yale yanaratibiwa vyema, yanafanyiwa tathimini kwa kina kwenye faida na hasara zake, gharama na muda unaohitajika ili kuyafanya pamoja na yanaidhinishwa na mtu mwenye uwezo (capacity) wa kubaini uchambuzi ulofanyika na kuwa na uhakika kwamba mabadiliko husika yanapelekea uimarikaji wa mfumo.

Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuhakikisha kwamba inaandaa na kuutumia mpango rasmi wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

12.8.4 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka ujao Ofisi ya Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa mashirikiano waliyotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio Ofisi ya Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwamba ushirikiano huu utaboreshwa zaidi katika ukaguzi ujao ili kuhakikisha kwamba kazi za ukaguzi zinakamilika kwa mujibu wa ratiba ya ukaguzi.

SURA YA KUMI NA TATU

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BODI YA MAPATO ZANZIBAR-ZRB

13.0 UTANGULIZI

Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA iliyopo Bodi ya Mapato Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanyika kwa lengo la kupima tathmini katika matumizi ya Tehama kwa kuangalia kiwango cha utendaji kazi wa mfumo iliyopo, udhibiti na usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani ya mifumo hiyo, utunzaji wa siri katika mifumo, mipaka ya matumizi ya mfumo, uadilifu, ufanisi, tija, uwajibikaji wa watumiaji wa mfumo, urahisi wa upatikanaji wa taarifa ndani ya mfumo, pamoja na kuangalia muingiliano na mifumo mengine.

13.1 UANZISHWAJI WA BODI YA MAPATO ZANZIBAR

Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) ilianzishwa chini ya Sheria ya ZRB namba 7 ya mwaka 1996 kama wakala mkuu wa Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya ukusanyaji na usimamizi wa kodi zote kutoka vyanzo vya mapato ya ndani isipokuwa ushuru wa forodha, ushuru (excise) na mapato ya kodi ambayo yanasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Bodi ya Mapato Zanzibar ilianza rasmi kufanya kazi za makusanyo ya mapato na kodi kuanzia mwezi wa Julai, 1998.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ZRB imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa kuimarisha huduma za makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wakati pamoja na kudhibiti uvujaji wa mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali vya mapato.

13.2 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MIFUMO YA ZRB

Miongoni mwa hatua zilizofanyika za uboreshaji wa huduma za mifumo ya ZRB ni pamoja na uanzishwaji wa mfumo mpya wa makusanyo ya mapato yanayokusanywa kupitia mashine za EFD ambapo mfumo huo unajulikana kwa jina la "Virtual Fiscal Management System".

Hata hivyo imebainika kwamba ZRB bado inaendelea kutumia mifumo ya awali iliyokuwepo ikiwemo mfumo mkuu wa ukusanyaji wa mapato (ZITAS) ambapo kwa sasa mifumo mingi ya ZRB imebainika kuwa na dosari za kiutendaji na kupelekea baadhi ya mifumo kutokufanya kazi kabisa kutokana na dosari zilizojitokeza katika mifumo hiyo.

Aidha, ukaguzi uliweza kubaini baadhi ya dosari mbali mbali zilizojitokeza katika mifumo ya Tehama ya ZRB iliyokaguliwa na kuweza kuonyesha athari zinazotokana na dosari hizo pamoja na kuzitolea mapendekezo kwa uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa lengo la kuzifanyia kazi ili kuondoa dosari hizo na hatimae kuimarisha huduma zinazotolewa katika mifumo. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

13.1.1.1 Kukosekana kwa nyaraka za Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato wa "Virtual Fiscal Management System – VFMS"

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ilibainika kuwa ZRB imeanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato unaojulikana kama "Virtual Fiscal Management System - VFMS". Mfumo huo umetengenezwa kupitia wataalam wa ndani wa Idara yake ya Tehama ambapo kwa kiasi kikubwa mfumo umeweza kufanikisha malengo yake ya utendaji kazi na kuanza kutumika kuanzia Julai, 2021.

Aidha mfumo huo umeunganishwa moja kwa moja na mashine za kelektroniki "EFD" kwa ajili ya kutolea risiti za malipo kwa wafanya biashara mbali mbali waliopo Unguja na Pemba. Takriban asilimia kubwa ya walipa kodi wakubwa ikiwemo mahoteli na walipakodi wadogo wamesajiliwa na kuanza kuutumia mfumo huo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa nyaraka muhimu zinazohusiana na matumizi ya mfumo pamoja na mipangilio mbali mbali iliyopo katika mfumo huo ambayo ingeweza kuonesha na kuweka kumbu kumbu za mfumo ulivyotengenezwa na matumizi yake kwa ujumla.

Nyaraka hizo zilizokosekana ni pamoja na nyaraka za usanidi "system configuration documents", miongozo ya kuwasaidia watumiaji wa mfumo "user support manuals", nyaraka zenye kubainisha usalama wa mfumo "security configuration documents", nyaraka za mahitaji ya utendaji wa mfumo "system requirements specification - (SRS) documents ", nyaraka zinazoonyesha uwepo wa muingiliano na mifumo mengine kama vile mifumo ya malipo ya kibenki "API Support documents" n.k.

Kukosekana kwa nyaraka muhimu za usimamizi na uendeshaji wa mfumo mpya wa VFMS kunaweza kupelekea Idara ya TEHAMA ya ZRB kushindwa kuusimamia, kuulinda na kuuendeleza mfumo ipasavyo hasa ikitokea wafanyakazi waliotengeneza mfumo huo kuondoka ZRB kwa njia yoyote ikiwa kupata uhamisho wa kikazi katika taasisi nyengine, kwenda likizo za muda mrefu kama vile masomoni, na vyenginevyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kupitia idara ya TEHAMA ya ZRB kufanya yafuatayo:-

- Kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kuandaa nyaraka zote zinazohusiana na usimamizi, utendaji kazi pamoja na usalama wa mfumo wa VFMS, mfano wa nyaraka hizo ni "system configuration documents", "user support manuals", "security configuration documents", "system requirements specification documents " , "API Support documents" n.k. ambapo baada ya kukamilika nyaraka hizo zitathibitishwa na uongozi wa ZRB ili ziwe rasmi.
- Kutunza kumbu kumbu na kuzilinda wakati wote "source codes" zilizotumika kutengeneza mfumo huo pamoja na kuweka kumbu kumbu za matokeo ya majaribio ya utendaji kazi na kuangalia ukubalikaji wa mfumo kwa watumiaji, kuwepo kwa kumbukumbu hizo kutaweza kurahisisha kufanyika kwa zoezi la kuimarisha mfumo wa VFMS "system update processes" wakati itakapohitajika.

- Mabadiliko yoyote yanayofanywa na yatakayofanyika baadae katika mifumo yatapaswa kujaribiwa na kuwashirikisha watumiaji wa mifumo ili kuweza kupatikana ithibati na uhalisia wa matokeo ya utendaji kazi wa mfumo baada ya kufanyika kwa mabadiliko hayo.
- Idara ya TEHAMA kutoa msaada wa kiufundi na mafunzo endelevu kwa watumiaji wa mfumo kwa lengo la kuweza kutumika vizuri mfumo huo na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kwa kupitia mfumo huo kulingana na thamani yake.

13.1.1.2 Mapitio ya Mifumo ya ZRB

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa ujumla wa utendaji kazi wa mifumo ya ZRB kwa kulinganisha na thamani iliyotumika kutengeneza mifumo hiyo ambapo imebainika baadhi ya mifumo iliyonunuliwa haifanyi kazi na kuwa imelala "dormant" licha ya kwamba fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mifumo hiyo, baadhi yao haifanyi kazi ipasavyo kama ilivyotarajiwa ikiwemo Mfumo Mkuu wa Makusanyo ya Mapato (**ZITAS**) na mengine michache ndio inayotumika kwa kuendeshea shughuli za ZRB ambapo haina dhamana kubwa ya utendaji kazi katika siku zijazo kutokana na dosari mbali mbali zinazoendelea kujitokeza.

Hali hii imesababishwa kutokana na mifumo mingi ya ZRB kuwa na dosari za kiujumla kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa huduma za kuimarishwa mifumo hiyo kutoka kwa watengenezaji (lack of software updates and security patches from Vendors).
- Kukosekana kwa kiwango kikubwa cha msaada wa kiufundi (technical updates) kutoka kwa watengenezaji wa mifumo hiyo (vendors).
- Wataalam wa ndani wa Tehama wa ZRB kuwa na uwezo mdogo wa kuendesha na kuikwamua kitaalam mifumo wakati inapokuwa na changamoto za kiufundi, hali hii imetokana na ZRB kununua mifumo mingi kutoka kwa Vendors walio nchi za nje ambao hutumia teknolojia zisizokuwa rafiki na maarufu kwa mazingira ya nchi za kwetu katika kutengenezea mifumo hiyo, vile vile ZRB kutopatiwa "Source Codes" zinazotumika kutengenezea mifumo hiyo kutoka kwa Vendors ambazo zingeliweza ZRB kupata uelewa wa namna ya mifumo yao ilivyotengenezwa na kuzisimamia Codes hizo kwa lengo la kuimarisha mifumo yao kwa baadae.
- Kukosekana kwa mafunzo ya kina (advanced courses – "Certifications") kwa watendaji wa ZRB wanaosimamia mifumo ili kuwajengea uwezo wa kuelewa na kufahamu kwa upana teknolojia zinazotumika kuhusiana na mifumo iliyopo ZRB pamoja na kupata mafunzo endelevu ya kiufundi na kusimamia mifumo kwa ujumla.
- Kukosekana kwa nyaraka muhimu za kusimamia utendaji kazi wa mifumo.
- Watumiaji wa mifumo (ZRB system users) kukataa kutumia mifumo ya ZRB kutokana na sababu tofauti ikiwemo kutoamini utendaji kazi wa mifumo yao kutokana na mifumo kutoa matokeo tofauti na inavyotarajiwa (unexpected results), uelewa mdogo wa utumiaji wa mifumo unaopelekea mifumo hiyo kutumika kwa kiwango kidogo na sehemu kubwa ya mifumo kutotumika ipasavyo na hatimae kusababisha watumiaji kufanya kazi nje ya mfumo "manually".

Aidha ukaguzi ulipitia baadhi ya mikataba ya mifumo iliyofungwa baina ya ZRB na watengenezaji wa Mifumo (Vendors) na kuifanyia tathmini na kubaini kwamba mikataba mingi haikuwa vizuri katika maswala ya kisheria baina ya wauzaji wa mifumo na ZRB hivyo kusababisha watengenezaji hao kushindwa kuwatengenezea ZRB mifumo kwa mujibu wa mahitaji halisi yaliyotakiwa na ZRB , vile vile kukosekana kwa upembuzi yakinifu wa kina na kutokushirikishwa kwa watumiaji katika hatua za awali za uanzishwaji wa mfumo ambapo hali hiyo imepelekea kutengeneza mifumo ambayo haijakidhi matakwa ya watumiaji (user requirements) na kupelekea wakati mwingine kutokufanya kazi ipasavyo au kutoa matokeo tofauti na ilivyotarajiwa hususan katika vipengele vya kukokotoa mahesabu ya kodi na mapato jambo ambalo limepelekea kuingiza hasara Serikali.

Aidha, baadhi ya dosari za kimkataba zilizobainika kwa baadhi ya mikataba ni kukosekana kwa vifungu vitakavyowabana (bondi ya mkataba) watengenezaji hao kisheria jambo ambalo limepelekea watengenezaji hao kutotoa msaada ipasavyo au kutoonekana eneo la kazi pindipo wanapohitajika kwa ajili ya kutoa huduma za msaada wa kiufundi katika mifumo ya ZRB na bila ya kuchukuliwa hatua zozote za kisheria kwa mujibu wa mkataba. Jadweli lifuatalo linaonesha hali halisi ya kiwango cha utendaji kazi wa mifumo ya ZRB pamoja thamani ya fedha zilizotumika kutengenezea mifumo hiyo.

Jadweli Nambari 43 : Hali halisi ya Utendaji kazi wa mifumo ya ZRB

Namba	Aina ya Mfumo	Muda ulionunuliwa	Kiasi cha fedha kilicholipwa (USD/ Tshs.)	Hali halisi ya Mfumo hadi ukaguzi unakamilika
1	Web-portal	31 Januari, 2018	USD 366,405.70	Haufanyi kazi / Umelala
2	e-Tax (Hotel Tax Collection Management System (HTCMS)	2017	Uligharamiwa na Wizara ya Fedha/Mkataba umekosekana kwa ukaguzi	Haufanyi kazi / Umelala
3	Tax Block Management System (TBMS)	Mei, 2019	Tshs. 210,545,544	Haufanyi kazi ipasavyo/Umelala
4	Enterprise Resource Planning (ERP)	Juni, 2016	Tshs. 464,916,000	Mfumo unatumika kwa chini ya asilimia 30.
5	Virtual Fiscal Device Management System (VFDMS)	24 Aprili, 2019	Gharama zilizotumika USD 473,417.7 Gharama zilizobaki USD 879,204.3 Jumla ya Gharama USD 1,352,622	Haufanyi kazi / umelala.
6	ZITAS (Zanzibar Integrated Tax Administration System)	01/11/2010	USD 80,000	Moduli 3 zinafanya kazi kati ya moduli 10 zilizopo
7	Pastel Accounting Package	Taarifa hazijapatikana	Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi	Unafanya kazi
8	Revenue Forecast Module	2018/2019	USD 133,693	Unafanya kazi

9	Call Centre	Umetenenezwa 2018/2019 (Umeanza kazi 2021)	Tshs. 280,674,173	Unafanya kazi
10	Forensic	2017/2018	Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi	Unafanya kazi

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kufanya mambo yafuatayo ili kuweza kuimarisha mifumo yake pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo hiyo:-

- Kuweka kipaombele cha kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA cha ZRB hususan katika eneo la utengenezaji wa mifumo (System Development) kwa lengo la kuwafanya waweze kusimamia na kuimarisha mifumo iliyopo kwa ufanisi mkubwa pasi na kutumia wataalamu kutoka nchi za nje, jambo ambalo litapelekea wataalamu wa ndani kupunguza gharama za uendeshaji na kutoa msaada wa kifundi kwa wakati katika mifumo hiyo.
- Kuhakikisha unazingatia na kutekeleza matakwa na mahitaji yanayotolewa na watumiaji wa mifumo wa ZRB na kuwashirikisha ipasavyo kuanzia hatua za awali za utengenezaji hadi kukamilika kwa mfumo.
- Kuandaa sera madhubuti za kuhakikisha mifumo yote inayotengenezwa kwa ajili ya matumizi ya ZRB inafuata taratibu zilizobora, misingi imara pamoja na miongozo sahihi kutoka ZRB, eGov na miongozo ya kimataifa inayotumika katika utengenezaji wa mifumo (System Development Life Cycle - SDLC) kama vile kukusanya mahitaji ya watumiaji wa mifumo "user requirements", kufanya upembuzi yakinifu "system analysis", kufanya ubunifu wa kutengeneza mifumo "system design and implementation" pamoja na kufanya majaribio mbali mbali ya utendaji wa mifumo kabla ya kuanza kutumika moja kwa moja "system testing". Hali hii itaweza kupunguza dosari kubwa za kiutendaji katika mfumo na kupelekea kupatikana kwa tija na ufanisi katika matumizi ya mifumo hiyo.

13.1.1.3 Uwepo wa Uhaba wa Bajeti katika Idara ya TEHAMA ya ZRB

Taratibu zilizo bora kuhusiana na bajeti za TEHAMA zinaeleza kwamba, katika hali ya kawaida, Bajeti ya TEHAMA iliyoandaliwa vizuri inapotekelezwa kikamilifu huweza kuisaidia Taasisi katika kuleta maendeleo ya haraka ikiwemo kuweka mifumo madhubuti na miundombinu imara ya kurahisisha utendaji kazi na hatimae kuweza kufanikisha dira na malengo ya kimkakati yaliyopangwa na taasisi kwa ufanisi na uwiano mkubwa.

Katika ukaguzi uliofanyika wa Bodi ya Mapato Zanzibar imebainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 makadirio ya matumizi ya Idara ya Tehama yalikuwa ni shilingi bilioni 1.4 .Hadi kufikia tarehe 30 Juni,2021 jumla ya shilingi Milioni 800 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya Idara ya TEHAMA ambazo ni sawa na asilimia 57.14 ya makadirio. Kati ya shilingi Milioni 800 zilizoingizwa kiasi cha shilingi Milioni 400 zilitumika kwa ajili ya kulipia gharama za vifurushi vya INTERNET pamoja na gharama za huduma za muunganisho wa mtandao wa ZRB (VPN Connection Services) katika ofisi zake za Unguja na Pemba ikiwemo matawi yake yanayotoa huduma za makusanyo ya mapato na huduma za leseni kwa niaba ya taasisi, na shilingi milioni 400 zimetumika kwa ajili ya kusaidia

na kuimarisha miundombinu ya vifaa pamoja na mifumo ya TEHAMA ya ZRB inayotumika kwa ajili ya kufanyia kazi mbali mbali ikiwemo kazi za usimamizi wa makusanyo ya mapato na kodi, usimamizi wa malipo ya mishahara, usimamizi wa mali za Bodi pamoja na usimamizi wa rasimiali watu.

Ukaguzi baada ya kufanya mahojiano na watendaji pamoja na wasimamizi wa Idara ya TEHAMA kuhusiana na upatikanaji wa bajeti hiyo, umebaini kwamba kiasi hicho cha shilingi milioni 400 kilichoingizwa kwa ajili ya kusaidia na kuimarisha miundombinu ya vifaa pamoja na mifumo ya TEHAMA ya ZRB ni hafifu ukilinganisha na mipango mikakati ya kimaendeleo iliyopangwa na Idara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo mikakati hiyo inajumuisha usimamizi na uboreshaji wa miundombinu yote ya TEHAMA ya ZRB ikiwemo kompyuta, programu na mifumo, vifaa vya mawasiliano na ulinzi, mafunzo mbali mbali kwa watumiaji wa mifumo na watendaji wa Idara ya TEHAMA n.k jambo ambalo limepelekea kutotekelezeka ipasavyo kwa mpango huo kutokana na ufinyu wa bajeti iliyopatikana.

Kuwepo kwa ufinyu wa bajeti katika Idara ya TEHAMA kunaweza kupelekea Idara kushindwa kufanikisha kwa ufanisi malengo waliyojipangia kwa ujumla ambayo yangeweza kuisaidia taasisi katika kufanikisha malengo makuu ya kimkakati yaliyopangwa na taasisi hiyo.

Vile vile kuwepo kwa ufinyu katika bajeti ya TEHAMA kunaweza kupelekea kutokezea mambo yafuatayo:-

- Kufanyika kwa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA vilivyo chini ya viwango na ubora wa kazi jambo ambalo litapelekea kuhatarisha usalama wa taarifa zitakazokuwa zinaingizwa, kutumika na kuhifadhiwa ndani ya vifaa hivyo.
- Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mifumo (system users) pindipo yanapotokezea mabadiliko ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo.
- ZRB kushindwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kusimamia na kuimarisha mifumo ya taasisi kwa kupitia wataalamu wa ndani na sio kutegemea makampuni ya nje ambayo yanaongeza hasara kwa Serikali katika mtazamo mwengine.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kutoa kipaombele cha utekelezaji wa bajeti ya TEHAMA kwa kuzingatia sera ya Bodi ya Mapato Zanzibar inayohitaji kuimarisha udhibiti ili kuondoa upotevu wa mapato na kuongeza makusanyo ya mapato kupitia mifumo na miundombinu ya TEHAMA jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gawio la Serikali na hatimae kupatikana huduma bora za kimaendeleo nchini kutokana thamani ya fedha inayotolewa kwa walipa kodi.

13.1.1.4 Kukosekana kwa njia imara za kuhifadhi taarifa na nyaraka muhimu zilizopo katika mifumo ya ZRB

Katika ukaguzi uliofanyika wa Bodi ya Mapato Zanzibar imebainika kuwa ZRB haijaweka njia imara na salama kwa ajili kuzilinda, kuzidhibiti na kuzihifadhi taarifa zake zilizokuwa muhimu na zenye usiri wa hali ya juu (classified information) kwa taasisi.

Kwa mfano, hapakuwa na utumiaji wa programu maalum za kufichia taarifa nyeti zilizokuwa ndani

ya mifumo (data encryption software) ambazo programu hizo zingeweza kutumika kwa kudhibiti na kuzilinda taarifa nyeti zilizokuwa ndani ya mifumo. Vile vile hapakuwa na vifaa au zana maalum kwa ajili ya kufichia taarifa na nyaraka nyeti zilizokuwa 'hard copy' jambo ambalo lingeweza kusaidia Bodi kuzilinda taarifa zake zilizokua muhimu na nyeti.

Kukosekana kwa njia imara za kudhibiti, kuzilinda na kuziwekea kinga taarifa zilizokuwa muhimu na za zenye unyeti mkubwa kunaweza kupelekea taarifa hizo kuonekana na wasiohusika na hatimae kuweza kuzisoma, kuzifahamu, kuzichukuwa na kuzibadilisha (kuzichezea) pamoja na kuzitumia kinyume na matakwa ya taasisi jambo ambalo kwa njia moja au nyengine linaweza kusababisha kutokezea kwa upotevu wa taarifa, ubadhirifu wa fedha au upotevu wa mapato na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuandaa na kufuata sera, taratibu na miongozo madhubuti ya kudhibiti, kuzilinda na kuzihifadhi taarifa zake zilizomo ndani ya mifumo 'softcopy' na nje ya mifumo 'hardcopy', ili kuweza kuzinusuru taarifa hizo kutokana na kutumiwa na wasiohusika na kusababisha kutokezea kwa upotevu wa taarifa, ubadhirifu wa fedha au upotevu wa mapato na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuongeza jitihada za kuwajengea uwezo Wasimamizi wa mifumo waliopo ZRB ili kuongeza ufahamu juu ya jukumu lao la kulinda na kusimamia mifumo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kuchezea na kubadilisha taarifa kinyume na matakwa ya ZRB kwa lengo la kuepuka kuitia hasara Serikali.

13.1.1.5 Kutokuwepo kwa Mkaguzi wa Ndani wa TEHAMA wa kusimamia na kukagua mifumo na miundombinu ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar pamoja na kuwa imefunga na kutumia mifumo na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA ikiwemo application programs, komputa, seva, network, firewalls n.k, lakini imebainika kuwa katika kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakuna mkaguzi wa mifumo ya miundombinu ya TEHAMA. Aidha ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wanaohusika na Idara na kubaini kuwa kitengo hicho hakina utaalumu au wataalam wa TEHAMA ambao wangeweza kufanya uhakiki wa hali ya juu wa mifumo ya kukusanyia mapato na kodi, mifumo ya mishahara, mifumo ya rasilimali watu, kompyuta, vifaa vya mawasiliano pamoja na mtandao wa ZRB kwa ujumla na kuweza kutoa ripoti mbali mbali za kushauri uongozi wa ZRB namna bora ya kuimarisha mifumo pamoja na miundombinu ya mawasiliano iliyopo na kupelekea kuweza kudhibiti upotevu wa mapato kupitia mifumo.

Kutokuwepo kwa wakaguzi wa ndani wenye elimu ya TEHAMA na uwezo wa kukagua mifumo pamoja na taarifa zake zinazozalishwa kupitia mifumo hiyo kunaweza kupelekea uongozi wa ZRB kuchelewa kubaini na kuchukuwa hatua za kudhibiti changamoto zinazojitokeza katika mifumo hususan kwa mifumo inayotumika kukusanyia mapato na kodi katika taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kufanya jitihada za uwepo wa mkaguzi wa ndani wa mifumo ya TEHAMA (Internal Information System Auditor) ili kuweza kuishauri taasisi kuhusiana na mwenendo mzima wa mifumo ya ZRB ikiwemo kutoa ushauri katika michakato ya

manunuzi ya mifumo pamoja na kuishauri taasisi kutokana na changamoto na dosari zinazojitokeza katika utendaji wa mifumo hiyo na miundombinu ya tehamu ya kwa ujumla, hali hii itaweza kupelekea dosari nyingi za mifumo kuweza kurekebisha mapema katika hatua za awali kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji wa mapato na kupelekea kuongezeka kwa udhibiti na kuondoa mainya ya upotevu wa mapato.

13.1.1.6 Kukosekana kwa Mfumo rasmi wenye leseni ya kuchunguza, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZRB (Licensed Network Monitoring System).

Mfumo wa kuchunguza, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao (Network Monitoring System - NMS) ni moja kati ya zana muhimu za kiusalama ambazo taasisi kubwa zenye kutumia mifumo na miundombinu ya tehamu hupaswa kutumia zana hizo kwa lengo la kupima, kudhibiti pamoja na kufanya tathmini ya viwango vya matumizi ya mtandao na miundombinu ya tehamu iliyopo katika taasisi.

Tathmini hiyo hufanyika katika kipindi cha muda mfupi kwa njia ya kielektroniki kupitia mifumo ya aina hiyo ambapo hupima kasi ya mtandao, trafiki, matumizi ya data, huchunguza uwepo wa usalama na hali ya mtandao (network status & security updates), hudhibiti mashambulizi yanayotokana na udukuzi (cyber attacks) pamoja na kuweza kufanya utambuzi wa aina gani ya kifaa cha tehamu au chanzo kinachopelekea kutokea kwa hitilafu katika mtandao wa Taasisi. Aidha, baada ya kumalizika kufanyika kwa tathmini mfumo huwasilisha ripoti ya matokeo kwa maafisa wasimamizi wa Mtandao (network administrators) kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe au ujumbe mfupi "sms" kulingana na maafisa watakvyouseti mfumo namna ya kuwasilisha taarifa za matokeo.

Kwa ujumla mfumo wa Network Monitoring System huwasaidia na kuwarahisishia kazi Maafisa wanaosimamia Mtandao katika Taasisi kwa kuweza kugundua haraka chanzo cha hitilafu wakati inapotokezea tatizo katika mtandao wa taasisi ambapo bila ya uwepo wa mifumo hiyo maafisa wangekuwa wanafanya kazi kubwa ya kukagua vifaa na miundombinu ya tehamu iliyopo kwenye taasisi kwa njia ya kawaida "manually" ili kubaini chanzo cha hitilafu jambo ambalo lingepelekea kupoteza muda, nguvu na usumbufu ikiwa miundombinu ya taasisi ni mikubwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Bodi ya Mapato Zanzibar imeweka mtandao mkubwa wa mawasiliano kwa lengo la kuwezesha upatikanaji mzuri wa mifumo yake ya makusanyo ya mapato katika ofisi zake zote ikiwemo na matawi na vituo vyake vya makusanyo ya mapato vilivyopo Unguja na Pemba. Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mfumo ulio rasmi wenye leseni maalum ya matumizi (Licensed Network Monitoring System) kwa ajili ya kuchunguza usalama wa mtandao wa ZRB, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao na mifumo, kudhibiti mashambulizi yanayotokana na uhalifu wa udukuzi wa mtandao na mifumo ya ZRB pamoja na kufanya tathmini ya mwenendo wa utendaji kazi wa vifaa na miundombinu ya tehamu inayotumika ZRB kwa lengo la kuendelea kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ili kuweza kupatikana huduma bora za makusanyo ya mapato kutoka kwa walipa kodi.

Aidha ukaguzi ulibaini Bodi ya Mapato walikuwa wakitumia zana (software tools) zilizokuwa na

uwezo mdogo, zisizo salama na hazikuwa halali zenye leseni ya matumizi, ambazo zilipatikana bure kwenye Internet “ free downloaded software/pirated software” na kutumika kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mtandao wa ZRB jambo ambalo ni kinyume na sera na utarabu wa Bodi ya Mapato na Serikali kwa ujumla.

Kukosekana kwa Mfumo rasmi wenye leseni ya kuchunguza, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZRB kunaweza kupelekea ZRB kushindwa kulinda mtandao na mifumo yake dhidi ya uhalifu unaoweza kutokezea ikiwemo mifumo kufanyiwa udukuzi, kushambuliwa na virusi, kuchezeza kwa makusudi na hatimae kuweza kujitokeza kwa upotevu wa mapato jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuhakikisha unafanya jitihada za kununua na kumiliki mfumo madhubuti wenye leseni ya matumizi na uwezo mkubwa wa kusimamia, kuchunguza, kudhibiti, kufanya tathmini na kuongeza ulinzi katika mtandao, vifaa pamoja na miundombinu ya tehama iliyofungwa katika ofisi na matawi yote ya ZRB yaliyopo Unguja na Pemba ili kuweza kuhakikisha kwamba usalama wa matumizi ya mtandao na mifumo unaimarika kwa kiwango kikubwa pamoja na kurahisisha kazi ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwa walipa kodi.

Aidha ukaguzi unashauri kwa ujumla taasisi za Serikali kutotumia zana zilizokuwa hazina leseni ambazo hupatikana bure kutoka mitandaoni (free software tools) kwani zana hizo zinakuwa na uwezo mdogo wa kufanya kazi husika kwa mujibu wa namna zinavyotengenezwa ambapo mara nyingi hutengenezwa kwa majaribio au matangazo tu.

Vile vile kupitia zana hizo kunaweza kusababisha mifumo ya kuendeshea kompyuta (Operating Systems) kushambuliwa na virusi kwa urahisi na kupelekea kuharibika kwa taarifa zilizomo ndani ya kompyuta kutokana kuwa baadhi ya zana hizo pia hufanya na kazi nyengine ya kutumika kama ni programu maalum kwa ajili ya kuchunguza taarifa zilizohifadhiwa ndani ya mifumo ya kompyuta na kuzipeleka kunakohusika (malwares and spywares).

13.1.1.7 Uwezo mdogo wa kifaa cha kurikodia matokeo katika kamera za CCTV (NVR)

Moja kati ya njia bora za kudhibiti na kuongeza usalama wa uhifadhi wa taarifa pamoja na mali za ofisi ni kufunga vifaa maalum vya ulinzi na usalama ambavyo vitasaidia kuonesha kumbukumu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya ofisi na kubainisha muda uliofanyika wa matukio hayo kukiwa na lengo kusaidia kupatikana ushahidi kwa waliohusika kufanya matukio. Baadhi ya vifaa hivyo ni “CCTV Cameras” n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imbainika Bodi ya Mapato Zanzibar imefunga takribani kamera 110 katika jengo lake la Makao Makuu Unguja kwa ajili ya kurikodi matukio mbali mbali yanayofanyika katika nje na ndani ya ofisi hiyo ambapo taarifa hizo huhifadhiwa katika mtambo maalum wa kuhifadhia kumbu kumbu za matukio ya video (Network Video Camera - NVR) ambapo mtambo huo umeunganishwa moja kwa moja na CCTV cameras za Bodi.

Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mtambo huo wa kuhifadhia kumbu kumbu za matukio yanayorikodiwa moja kwa moja kupitia kamera una ujazo mdogo wa 8TB ukilinganisha

na idadi kubwa ya kamera zilizofungwa na kurikodi katika maeneo yote ya nje na ndani ya ofisi ambazo ni takriban 110. Hali hii imepelekea mtambo kuwa na uwezo wa kuhifadhi kumbu kumbu za matukio kwa kipindi cha muda wa siku 45 pekee na baadae kuzifuta moja kwa moja ili kupatikana nafasi ya kuweka kumbu kumbu nyengine za matukio jambo ambalo linapelekea kutokupatikana kwa ushahidi wa matukio yaliyofanyika katika kipindi cha muda mrefu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato kuhakikisha unaboresha uwezo wa mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio yanayorikodwa kutoka katika kamera za CCTV ili kupata nafasi kubwa ya ujazo wa kuhifadhi kumbu kumbu angalau kwa matukio yaliyofanyika katika kipindi cha miezi sita mfululizo ya nyuma kabla ya kufutika.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuhakikisha picha na video za matukio ya kihalifu zinazorikodiwa na CCTV zinatakiwa kuhifadhiwa kwa umakini na kuhakikisha zinafanyiwa nakala (backup) kumbu kumbu hizo katika sehemu nyingine nje ya mtambo ili kuepusha kumbu kumbu hizo kufutika wenyewe au kufutwa kwa makusudi na kupelekea kupoteza kwa ushahidi wa matukio yaliyofanyika.

13.1.2 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Bodi ya Mapato Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa ushirikiano mzuri mliotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi yetu kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi ujao.

SURA YA KUMI NA NNE

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR - PBZ

14.0 UTANGULIZI

Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama katika Benki ya Watu wa Zanzibar Ltd kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa mifumo. Matokeo ya kazi hii yanayotokana na ukaguzi pamoja na tathmini iliyofanywa juu wa uwepo wa usimamizi wa shughuli zote zinazohusiana na vifaa vya Tehama.

Ukaguzi ulilenga kuhakikisha kwamba ufanisi mkubwa wa kiutendaji kupitia mifumo hiyo unapatikana kwa kuzingatia sheria, Sera, Miongozo na taratibu bora zinazotumika na zinazokubalika kitaifa na kimataifa katika usimamizi na utumiaji wa mifumo ya Tehama ambayo inahitaji uangalifu mkubwa wa Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar.

Aidha katika ukaguzi uliofanyika uliangalia utendaji kazi wa mifumo ya biashara iliyopo PBZ ikiwemo Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Benki 'BANKS' pamoja na mifumo mengine inayosaidia kutoa huduma za uendeshaji wa biashara katika benki ya PBZ ikiwemo mfumo wa Internet Banking (Retail and Cooperate), ChequePoint , BANKBI Reporting, BANKBI AML, SWIFT Alliance, Helpdesk And IT Asset Management , Agency Banking and Merchant Services, Revenue Collection and Bills Payment, Estp, Tax Bank/Real Bus , ATM SWITCH, Fixed Asset , Epicor pamoja na programu za Microsoft Office.

Aidha, ukaguzi ulijikita katika kuangalia usahihi na usalama wa taarifa zilizomo katika mifumo ya Tehama kwa kuzingatia usiri na udhibiti wa taarifa, uadilifu na usalama pamoja na upatikanaji wa taarifa kwa lengo la kuleta tija na ufanisi katika matumizi ya Tehama.

14.1 UANZISHWAJI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR

Benki ya Watu wa Zanzibar Limited (PBZ) ni benki ya biashara inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inatoa huduma za kibenki za Kiislamu na za Kawaida, PBZ ilianzishwa mnamo tarehe 30 Juni, 1966, na kutambuliwa chini ya Sura ya 153 ya Sheria ya Makampuni ya Zanzibar ambayo baadae sheria hiyo imefutwa na nafasi yake kuchukuliwa na Sheria Nambari 15 ya Makampuni ya mwaka 2013. Benki hiyo ina kampuni mwenza ndogo moja inayoitwa MuCoBa Bank Plc ambapo PBZ inaimiliki kwa asilimia 75.

14.2 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa mifumo ya Tehama ya PBZ umefanyika kwa mujibu wa sheria, miongozo na viwango mbali mbali vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi ikiwemo eGAZ , eGA , ISACA, AFROSAI-E , COBIT 5, INTOSAI n.k ambapo lengo la ukaguzi huo ni kutaka kuhakikisha na kujiridhisha kwamba kunakuwepo na ulinzi, usiri, uadilifu na udhibiti wa mifumo na miundombinu ya Tehama kwa Benki ya Watu wa Zanzibar ikiwa ni pamoja kuangalia Utawala wa Tehama (IT Governance) unaojumuishia masuala ya sera, miongozo, kanuni, sheria, mipango na mikakati pamoja taratibu bora zinazokubalika kutumika katika masuala wa Tehama.

Aidha ukaguzi umeangalia njia na mbinu mbali mbali zilizotumiwa na PBZ katika kuzilinda na kuzihifadhi taarifa za kibenki ikiwemo kufanya uhakiki juu ya uwepo wa Mpango wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Benki (BCP), Mpango wa Kupona na na kujikinga na Maafa (DRP), udhibiti wa Ujumla katika masuala ya Tehama (ITGCs), udhibiti katika matumizi ya Mifumo ya Tehama (ATACs) pamoja na usalama uliopo katika kuzifikia na kuzitumia taarifa kwenye mifumo (Access Controls).

14.2.1 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Katika ukaguzi uliofanyika wa mifumo ya PBZ mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo uwepo wa dosari za kiutendaji ambapo athari zake zimefafanuliwa pamoja na kutolewa mapendekezo kwa uongozi wa PBZ kwa lengo la kuzifanyia kazi ili kuondoa dosari hizo na kuimarisha huduma zinazotolewa katika mifumo. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

14.2.1.1 Dosari katika utawala na Utawala wa Tehama (IT Governance)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inatumia mifumo ya kielektroniki katika kuendesha shughuli mbalimbali muhimu za kiutendaji hususan katika utoaji wa huduma za kifedha kwa wananchi. Hata hivyo katika kusimamia Utawala wa Tehama dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainika kama zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa mpango wa mkakati wa Tehama (IT Strategic Plan).
- Kukosekana kwa mpango wa uongozi wa usimamizi wa Tehama (IT Capacity Management Plan).
- Uwepo kwa sera za Tehama zisizokidhi haja kutokana na kutokufanyiwa mapitio na maboresho (updates) ambapo imebainika PBZ kwa mara ya mwisho ilifanya mapitio ya sera hizo mwaka 2018.
- Kutokuwepo kwa sera ya matumizi ya miradi ya Tehama pamoja na miongozo ya huduma za Tehama.
- Kukosekana kwa vipengele muhimu katika daftari linalotumika kuweka kumbukumbu za matokeo hatarishi na ya kuchukuwa tahadhari (IT Risk register).
- Kutokufanyika mafunzo kwa muda mrefu ya udhibiti na usalama katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa watumiaji na wasimamizi wa TEHAMA wa Benki.

Kutokana na kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika utendaji kazi wa mifumo ikiwa ni pamoja na kuchelewesha upatikanaji wa huduma za msingi na kwa wakati jambo ambalo linaweza kuisababishia hasara Taasisi kutokana na kuweza kujitokeza uharibifu au upotevu wa fedha unaoweza kusababishwa na kutokuwepo kwa umakini katika kusimamia masuala mazima ya utawala na uongozi wa mifumo ya Tehama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa PBZ kuhakikisha unasimamia upatikanaji wa nyaraka muhimu za Tehama pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wake katika usimamizi na matumizi ya mifumo

na kufanya tathmini ya viashiria hatarishi pamoja na kufanya majaribio ya kupenya kwa lengo la kubaini udhaifu uliopo katika mifumo na miundombinu ya Tehama ili kuweza kudhibiti na kulinda mifumo dhidi ya mashambulizi na udukuzi wa taarifa.

14.2.1.2 Dosari katika Mpango wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Biashara (Business Continuity Management Plan)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4.4.1.2(d) cha Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2012 kinazitaka Taasisi za Serikali zenye kutumia mifumo kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao kuanzisha Mipango wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Mifumo na Miundombinu (BCP) pamoja na kuanzisha Mpango wa kupona maafa (DRP) endapo yakitokezea majanga dhidi ya miundombinu na mifumo katika taasisi.

Mpango huo unatarajiwa kuelezea utaratibu gani utatumika katika kuendeleza utoaji wa huduma wakati janga au dharura itakapotokezea katika taasisi, na hatua gani za kuchukuliwa kabla na baada ya janga kutokezea ili kuweza kudhibiti na kupunguza athari zinazoweza kutokezea pamoja na kurudisha huduma zinazotolewa na taasisi kwa wakati. Majanga yanayoweza kutokezea katika mifumo na miundombinu ya Tehama ni kama vile moto, mafuriko, udukuzi, virusi, wizi n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ haikujiandaa ipasavyo katika kukabiliana na majanga pamoja na maafa yanayoweza kutokezea dhidi ya mifumo na miundombinu ya Tehama iliyopo, hali hii imebainika kutokana na kutokufanyiwa majaribio na kutokuimarishwa kwa Mpango uliopo wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Biashara (BCP) endapo janga au dharura itakapotokezea, vile vile kutokufanyiwa mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na wasimamizi wa mifumo na miundombinu ya Tehama ya Taasisi.

Kutokufanyiwa majaribio na kutokuimarishwa kwa mpango huo kunaweza kusababisha benki kuwa katika hali ya mazingira hatarishi na kutokezea athari zifuatazo:-

- Kushindwa kurejesha utoaji wa huduma za biashara kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza wateja kutokana na kukosa huduma na kusababisha hasara kwa Serikali.
- Kujitokeza kwa uharibifu na upotevu wa taarifa za benki, nyaraka mbali mbali, mali na miundombinu ya benki, fedha taslimu pamoja na maisha ya watu.
- Kuingia hasara kwa kulipa fidia kutokana na aina ya janga lililotokea katika benki, kwa mfano kulipa fidia ya kukomboa dhidi ya shambulizi la mtandao linaloweza kufanyika katika mifumo ya benki (Ransomware), kulipa fidia kwa wateja n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya maboresho ya Mpango huo kwa mujibu wa miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na kuzingatia miongozo na taratibu zinazokubalika kimataifa, aidha PBZ inashauriwa kujiwekea utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kufanya majaribio angalau mara moja kwa mwaka katika mipango yote inayolenga kulinda taarifa na kuendeleza huduma za biashara ambayo imegharimu fedha za Serikali, muda pamoja na jitihada kubwa katika utayarishaji wa mipango hiyo.

14.2.1.3 Dosari katika usimamizi na udhibiti na matumizi ya Tehama (IT General Controls and Application Controls)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ inatumia mifumo mbalimbali ya kielektroniki katika kuendesha shughuli muhimu za kiutendaji zinazowawezesha kutoa huduma kwa ubora na kwa wakati. Ukaguzi uliangalia maeneo mabalimbali ya kiutendaji ikiwemo programu za kuendesha mifumo (operating System), utaratibu na usimamizi katika mabadiliko ya mifumo ya Tehama (System Change Management) udhibiti wa upatikanaji wa taarifa kwa watumiaji (User Access Controls & Management) pamoja na utendaji kazi wa Tehama (IT operations). Dosari zilizobainika katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Tehama ni kama ifuatavyo:-

- Kutokufanyika kwa tathmini ya Vihatarishi katika mifumo kwa muda mrefu (Vulnerability Assesment).
- Kutowahi kufanyika kwa majaribio ya kupenya katika mifumo kwa lengo la kupima udhibiti, uimara na usalama uliowekwa katika miundombinu ya Tehama (PenTest).
- Kukosekana kwa kumbukumbu za matokeo ya maboresho ya mfumo.

Aidha ukaguzi umebaini kukosekana kwa kumbukumbu za matokeo ya maboresho yaliyofanyika katika mifumo iliyokaguliwa ili kuthibitisha kuwa maboresho hayo yalifuatiliwa na kufanyiwa kazi baada ya kuombwa kufanyika.

Miongoni mwa maboresho ambayo ushahidi wake haukupokelewa yalikuwa ni Ombi la kufanyika kwa maboresho mapya katika mfumo wa "Internet Banking". (Change Request for applying new update on Internet Banking).

Kutokuwepo kwa usimamizi na udhibiti mzuri katika matumizi ya Tehama kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki ambapo Taasisi inaweza kuingia hasara inayotokana na matumizi mabaya na usimamizi usioridhisha wa mifumo na vifaa vya Tehama.

14.2.1.4 Dosari katika usimamizi wa matukio (Inadequate Incident Management Process)

Ukaguzi umebaini kwamba PBZ wameanzisha mfumo wa Dawati la Usaidizi (Helpdesk System) ambao unatumwa na wafanyakazi wa PBZ kwa ajili ya kuripoti changamoto na dosari zinazojitokeza katika mifumo ya biashara ya benki kwa lengo la kuzitambua, kuzipatia ufumbuzi na kuzitatua kwa wakati.

Hata hivyo imebainika kwamba PBZ haina utaratibu mzuri wa kufanya mchakato wa kuyaripoti na kusimamia matukio kuanzia yanapotokezea, hatua ya ufuatiliaji hadi kukamilika na kupatiwa ufumbuzi. Aidha imebainika kutokuwepo kwa mkataba wa utoaji wa huduma (SLA) baina ya kitengo cha Tehama (IT Unit) na kitengo cha Biashara (Business Unit) jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuwepo kwa maelewano ya utoaji na upatikanaji wa huduma za kibiashara baina ya vitengo hivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ uanzishe utaratibu wa kina wa usimamizi wa matukio na

kuhakikisha matukio yote yanaainishwa kulingana na vipaumbele vyake. Zaidi ya hayo, makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) kati ya vitengo vya IT na Biashara yanapaswa kutekelezwa ili kudumisha uwajibikaji na utatuzi wa matukio kwa wakati.

14.2.1.5 Kutokufanyiwa mapitio ya mara kwa mara shughuli za watumiaji na matukio ya mfumo (User activities and system events).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali za taarifa za watumiaji wa mfumo pamoja na taarifa za mfumo husika ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokukaguliwa kwa shughuli za wasimamizi wa mfumo, mifumo ya uendeshaji na hifadhidata (database).
- Kutokufanyika kwa uhakiki na uchunguzi wa kumbukumbu za matukio yanayofanyika ndani ya mifumo pamoja na kompyuta za benki (Centralized Log Management).
- Kukosekana kwa kifaa cha kufuatilia na kuchuja taarifa zinazolingia na kutoka pamoja na kusimamia matukio yanayofanyika ndani ya mfumo (Firewall).

Kutokukaguliwa kwa shughuli za Msimamizi wa mfumo (System Administrator) ambae mwenye uwezo mkubwa wa kuzifikia taarifa zote za mfumo, huduma, usalama, na uwezo wa kubadilisha utendaji kazi pamoja na mipaka ya matumizi katika mfumo kunaweza kupelekea kufanyika mabadiliko yoyote kinyume cha sheria kwenye mifumo bila ya kutambuliwa na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha kwamba shughuli zote za msimamizi wa mfumo pamoja na vipengele vya usalama zinapaswa kurekodiwa na kuchunguzwa. Aidha, marekebisho yote yatakayofanyika yanapaswa kuchunguzwa na kuthibitisha uhalali wake ambapo Afisa muhusika wa usalama wa mifumo (System Security Officer) ndie pekee anayepaswa kufikia taarifa za ndani za mfumo (System log).

14.2.1.6 Dosari ya utumiaji wa akaunti za asili za Mifumo na Kanzidata (Default System Account – Administrator Account)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa matumizi ya akaunti za asili katika mifumo ya mbalimbali inayotumika kwa kundeshea shughuli za biashara za PBZ. Miongoni mwa mifumo inayotumika akaunti za asili ni pamoja na Mfumo wa "ChequePoint(SQL Server 2014) unaofanya kazi katika Windows Server 2012 pamoja na akaunti asili ya Active directory." Aidha imebainika kuwa Akaunti ya asili "sa" haijazuliwa kutumika katika kanzidata ya CTS (MS SQL Server 2008).

Kuendelea kutumika kwa akaunti hizo kunaweza kupelekea kutoa nafasi kwa wahalifu na wadukuzi wa mitandao kuweza kufanya mashambulio ya kimtandao (Cyber Attack) ambapo kunaweza kuisababishia upotevu wa taarifa na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kutokuendelea kuzitumia akaunti hizo ikiwa hakuna sababu ya msingi au kuzibadili majina ili kudhibiti na kuziba mianya ya uwezekano wa kutokezea uhalifu katika mifumo ya Benki.

14.2.1.7 Dosari katika usajili na ufuatiliaji wa akaunti zinazotumika katika Mifumo na Kanzidata

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa PBZ haina program maalum za kuchunguza na kusimamia akaunti zinazotumika katika uendeshaji wa mifumo ya PBZ (service accounts), aidha imebainika kuwa akaunti hizo hazifanyiwi usajili kwa lengo la kuzitambua na kuzifatilia matumizi na huduma zinazofanya katika mifumo na kanzidata za benki. Baadhi ya akaunti zilizobainika ambazo hazijafanyiwa usajili katika System Account Register na hazifuatiliwi na kuboreshwa matumizi yake ni kama zifuatazo:-

Akaunti za ujumla (generic account) katika "Active Directory" ambapo majina yake yamebainishwa kama ifuatavyo:-

- Cert Publishers
- DefaultAccount
- Administrator
- DnsAdmins
- DnsUpdateProxy
- echannels3
- Electronic Channels
- Electronic channels 2
- Guest
- sheha
- temp1
- sqlstart Epic
- IUSR_BRSERVER
- BANKING OP. OPERATION

Kutokana na kuwepo kwa akaunti za ujumla zisizosajiliwa na kusimamiwa katika utendaji wake kunaweza kupelekea uwezekanao wa matumizi mabaya ya mfumo yanayoweza kufanywa na watendaji wasio waaminifu ambao mara nyingi huzitumia akaunti hizi kwa maslahi binafsi kwa vile hazina majina mahsus ya watumiaji ambapo kutapelekea kujitokeza vitendo vya ubadhirifu wa fedha na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha kwamba kila mtumiaji anapewa akaunti kwa mujibu wa miongozo na taratibu za kibenki na kuhakikisha anawekewa mipaka ya matumizi katika mfumo, aidha kuhakikisha kwamba hakuna utengenezaji na utumiaji wa akaunti za jumla kukiwa hakuna umuhimu wa matumizi yake, na kama zikihitajika kutumiwa zinatakiwa kusajiliwa na kupewa idhini ya matumizi kwa watu maalum katika mfumo.

14.2.1.8 Udhhibiti usiofaa wa Akaunti za Watumiaji kwenye "Active Directory"

Katika ukaguzi uliofanyika imabainika kuwepo kwa orodha ya watumiaji wa "Active Directory" 78 ambao wamepewa dhima (Priviledge) ya kuwa wasimamizi wa mfumo (System Admin) hali ya kuwa wao ni watumiaji wa kawaida, pamoja na dosari hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa akaunti zenye kujirudia mara mbili kwa watumiaji wa mfumo hiyo. **Kiambatisho Namba 26 kinahusika.**

Kuwepo kwa idadi kubwa ya wasimamizi katika mfumo ambao hawakupaswa kuwa na ulazima wa kupewa dhima ya usimamizi katika akaunti zao za mfumo (Admin priviledges) kunapelekea kupewa haki zisizostahiki katika matumizi ya mfumo jambo ambalo linaweza kusababisha hatari ya kufanyika kwa vitendo vya kihalifu na ubadhirifu wa fedha katika mfumo ya benki.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kufanya uhakiki wa kina kwenye akaunti za watumiaji waliomo kwenye "Active Directory " pamoja na kanzidata za mfumo ya kibiashara inayotumika katika benki na kuhakikisha kuwa kila mtumiaji anamiliki akaunti moja katika mfumo na kwamba haki za usimamizi wa mfumo zinatolewa kwa wanaohusika tu kwa lengo la kuongeza udhibiti na usalama katika usimamizi wa mfumo.

14.2.1.9 Dosari katika chumba maalum cha kuhifadha taarifa (Physical Access to Data Centre)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ wanamiliki sehemu maalum kwa ajili ya uzalishaji wa taarifa pamoja na vituo vya uokozi wa taarifa (Production and Disaster recovery Center) ambapo dosari mbalimbali za kiukaguzi zimebainika katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

- Kutokuwepo kwa kamera za CCTV zinazosaidia kuimarisha ulinzi wa maeneo.
- Kuwepo kwa vitu vinavyoweza kushika moto kwa haraka na kuongeza kasi ya mripuko wa moto (maboksi) katika Kituo cha Uokozi wa Taarifa (DR Center).
- Kutokutunzwa kwa kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva.
- Kukosekana ushahidi wa ukaguzi wa mara kwa mara katika kituo cha Uokozi wa Taarifa.
- Kukosekana kwa mafunzo ya kupambana na majanga ya moto kwa wafanyakazi wa TEHAMA.

Bila ya kuwepo kwa utaratibu mzuri ulioidhinishwa, uingiaji wa kiholela katika vyumba vya kuhifadha taarifa hauwezi kugunduliwa kwa urahisi jambao ambalo linaweza kusababisha kutokea athari mbali mbali ikiwemo kupotea vifaa vilivyomo ndani ya chumba kwa kuchukuliwa kinyume na utaratibu, kupotea au kuharibiwa kwa taarifa pamoja na kupelekea kujitokeza kwa majanga yasiyotarajiwa kutokana na kutofahamika kwa sheria na miongozo ya Sehemu hizo.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa PBZ kuongeza usalama katika vituo hivyo ikiwa ni pamoja na kuweka miongozo na utaratibu uliobora wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo na kuweka kumbu kumbu nzuri za wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo hayo pamoja na kuweka vifaa maalum vya kudhibiti na kusimamia usalama kama vile CCTV Kamera na walinzi ili kuepusha kujitokeza kwa mambo ya kihalifu.

14.2.1.10 Dosari katika matumizi ya programu zilizoisha muda (Unsupported Software Versions)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa programu mbambali zinazotumiwa katika kuendeshea mifumo ya kielektroniki. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuendelea kutumika programu ambazo muda wake wa matumizi umepitwa na wakati kutokana na viwango vya matumizi na matoleo mapya yanayotolewa na kuboreshwa na watengenezaji wa programu (software vendors), miongoni mwa programu zilizobainika kuisha muda wa matumizi (End Life Support) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 44 : Programu zinazoendelea kutumika PBZ ambazo zimeisha muda wa matumizi

Namba	Programu Husika (Software)	Toleo (Version)	Muda wa Mwisho wa Matumizi (End of Life Support)
1.	Microsoft SQL Server	9	12 Aprili,2016
2.	Microsoft Windows Server	2008,7	14 Januari,2020
3.	PHP	5	01 Januari,2019
4.	Python	3.6.8	12 Disemba,2021
5.	OpenSSL	0.9.8x	01 Januari,2016
6.	Microsoft IIS	7.x	14 Januari,2020
7.	Cisco IOS	15.3	04 Juni,2020

Kendelea kutumia programu ambazo zimeshamaliza muda wa matumizi kunaweza kusababisha mifumo kutokuwa na kinga, usalama na ulinzi imara wa kuzilinda taarifa pamoja na kutoa huduma kwa ufanisi, jambo ambalo litapelekea mifumo kuweza kushambuliwa kwa urahisi dhidi ya virusi na wadukuzi wa mtandao na kusababisha kutokezea athari kubwa ya kuharibika na kupotea kwa taarifa za benki na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuimarisha mifumo na programu zake zote zinazotumika katika uendeshaji na utoaji wa huduma za biashara ili kuweza kuendelea kutoa huduma zenye kiwango bora, kwa wakati na kwa ufanisi pamoja na kuweza kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza katika utoaji wa huduma za benki.

14.2.2 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Benki ya Watu wa Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kwa ushirikiano mzuri mliotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi yetu kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi ujao.

SURA YA KUMI NA TANO

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR – ZECO

15.0 UTANGULIZI

Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu, miongozo na pamoja na viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa vilivyopo, ukiwa na madhumuni ya kupima tathmini katika matumizi ya Tehama kwa kuangalia kiwango cha utendaji kazi wa mfumo iliyopo, udhibiti na usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani ya mifumo hiyo, utunzaji wa siri katika mifumo, mipaka ya matumizi ya mfumo, uadilifu, ufanisi, tija, uwajibikaji wa watumiaji wa mfumo, urahisi wa upatikanaji wa taarifa ndani ya mfumo, pamoja na kuangalia muingiliano na mifumo mengine.

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ni moja katika ya Mashirika yaliyopo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo shughuli zake kuu ni kusimamia upatikanaji wa huduma ya umeme ikiwa ni pamoja na uuzaji wa umeme kwa wananchi wa Zanzibar, ununuzi na usafirishaji wa vifaa vya umeme vinavyotumika kusambazia Umeme katika maeneo yote ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Shirika la Umeme Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi zinazotumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika kuhakikisha linawafikishia wananchi upatikanaji wa huduma za nishati ya umeme kwa ufanisi, njia rahisi na kwa gharama nafuu. Miongoni mwa mifumo ya Tehama inayotumiwa na Shirika la Umeme ni pamoja na mfumo wa Mkuu wa Usimamizi wa huduma za Biashara za Umeme SUPRIMA ambao unatumika kwa ajili ya usimamizi matumizi ya umeme kupita mita za TUKUZA zinazotumia njia ya malipo kabla ya matumizi (Prepaid Billing), mfumo wa EQUILLIUM unaotumika kwa ajili ya usimamizi wa mita zinazotumia utaratibu wa kufanya malipo baada ya kutumia umeme (Post paid Billing), na mfumo wa SAP unaotumiwa na Shirika kwa ajili ya utendaji kazi wa shughuli zake za ndani za Shirika ikiwemo kusimamia shughuli za rasilimali watu pamoja na shughuli nyengine zinazosaidia huduma za uendeshaji wa biashara za umeme kwa Shirika.

15.1 UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

Shirika la ZECO limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 3 ya mwaka 2006 na kuchukua nafasi ya lililokuwa Shirika la Mafuta na Umeme la Serikali. Shirika linategemea asilimia kubwa ya fedha itokanayo na mauzo ya umeme na malipo ya ada ya huduma nyenginezo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake.

15.2 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa mifumo ya Tehama katika Shirika la Umeme Zanzibar umefanyika kwa lengo la kuangalia udhibiti na usalama wa mifumo ya Shirika, kufanya tathmini ya ujumla ya matumizi ya Tehama (IT Governence) kuanzia hatua ya upatikanaji wa mikataba ya ununuzi wa mifumo, sera zinazosimamia matumizi bora ya Tehama ndani ya shirika, changamoto zinazojitokeza za mifumo inayotumiwa na Shirika na namna Shirika linavyochukua hatua ya kuzitatua. Mbinu na nyenzo mbali mbali zilitumika katika ukaguzi (Auditing tools and Techniques) zikiwemo sheria, kanuni,

sera, miongozo na viwango mbali mbali vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi wa mifumo ikiwemo eGAZ , eGA , ISACA, AFROSAI-E , COBIT 5, INTOSAI n.k.

15.2.1 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Katika ukaguzi uliofanyika wa mifumo ya Tehama ya ZECO mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo uwepo wa dosari za kiutendaji ambapo athari zake zimefafanuliwa pamoja na kutolewa mapendekezo kwa uongozi wa Shirika kwa lengo la kuzifanyia kazi ili kuondoa dosari hizo na kuimarisha huduma za Umeme zinazotolewa kupitia mifumo hiyo. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

15.2.1.1 Kutokuwepo kwa wataalamu wa Mifumo (System Developers) katika muundo wa Idara ya Tehama

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kitengo cha Tehama, kina jumla ya watumishi saba (7) ambapo watumishi wawili kati yao walibainika kutokuwepo kazini kwa sababu tofauti, hali hiyo imepelekea kitengo kwa muda mrefu kuwa na watumishi watano tu waliopo kazini ambao ndio wanaotekeleza majukumu yote yanayohusiana na kazi za Tehama. Hali hii imepelekea kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu ya kusimamia mifumo na miundombinu ya Tehama jambo ambalo linaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kupelekea kujitokeza kwa usumbufu ikiwemo ucheweshaji wa upatikanaji wa huduma za umeme zilizo bora na kwa wakati kwa wananchi.

Aidha ukaguzi umebaini licha ya kuwa Shirika limewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye mifumo mbalimbali katika utendaji wake wa kazi za kila siku lakini bado lina uhaba katika fani ya watengenezaji wa mifumo pamoja na programu (system developers/programmers) jambo ambalo linalosababisha kuongezeka kwa ugumu katika kazi ya kusimamia mifumo, kubuni, kusasisha au kuboresha mifumo kupitia programu za kuboresha mfumo (system patches) na pia kupatikana ushauri wa kitaalamu juu ya ya uwepo wa aina gani za mifumo inayoendelea kuhitajika kwa Shirika ikiwa ni pamoja na miundombinu ya mtandao na Seva zinazotoa huduma hizo kupitia ofisi na vituo vyake vya kuuzia umeme ili kuweza kukidhi mahitaji ya utendaji kazi wa mifumo, kufahamu umuhimu na kumiliki misimbo (source codes) zinazotumika katika kutengeneza, kusimamia na kuimarisha utendaji kazi wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kuhakikisha unaweka kipaumbele katika mpangilio wake kuwajengea uwezo watendaji waliopo wa kitengo cha TEHAMA pamoja na mpangilio wa ajira zijazo kuongeza maafisa tehama watakaokuwa na fani ya Utengenezaji na usanifu wa mifumo/ programu (system developers/programmers) ambao watakuwa na uwezo mkubwa katika kusanifu, kuboresha, kutengeneza na kusimamia mifumo yote ndani ya shirika ambapo wataalam hawa pia watasaidia kutoa muongozo wa namna ya kuwa na mfumo bora inayohitajika kwa Shirika ikiwa ni pamoja na kutunza na kusimamia 'source codes' , kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utendaji kazi wa mifumo na vile vile kuweza kusaidia kutoa vigezo vinavyohitajika katika uingiaji wa mikataba ya manunuzi ya Mifumo kutoka kwa wauzaji wa mifumo (System Vendors) ili kuweza kuendelea kupatikana huduma bora zenye tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za umeme kwa Shirika.

15.2.1.2 Kutokuwepo kwa umiliki wa mifumo inayoitumiwa na ZECO

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ZECO haina Mkataba wa kumiliki mifumo wa Programu (source code) kutoka kwa watengenezaji wa mifumo wanayoitumia kama vile mfumo wa Suprima, mfumo wa tukuza (Aquillium), mfumo wa SAP na mfumo wa Call Center.

Ukaguzi umebaini kwamba shirika lipo mbioni kuacha kutumia mfumo wa Aquillium (post-paid system) kwa sababu mfumo huo kwa sasa unakosa msaada wa matengenezo ambapo muuzaji wa mfumo huo anaonekana hayupo tena sokoni hali ambayo imepelekea shirika kupata taabu sana kuendelea na matumizi ya mfumo huo. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa umakini kwa ZECO ambapo kupitia makubaliano ya mkataba baina ya ZECO na muuzaji wa mfumo huo wa Aquillium, pia mfumo huu haujaboreshwa (system patch) tangu mwaka 2012 pamoja na kuwepo na mabadiliko mengi na ya muda mrefu kuanzia mwaka 2012 hadi 2022 kutoka kwa watengenezaji wa mfumo.

Aidha shirika lilinunua mifumo inayoitumia bila kuzingatia matakwa ya mikataba na bila kupata ushauri mzuri wa kitaalamu kabla ya kununua au kukubaliana jinsi ya kumiliki mifumo endapo wauzaji hawatokuwapo tena sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba mifumo yote inayonunuliwa na kutumiwa na ZECO, inapaswa kuwa na mikataba ilio imara yenye vifungu vya kumbana kisheria muuzaji, hali ambayo itasaidia endapo kutatokea sababu zisizotarajiwa kwa wauzaji wa mifumo hiyo kuacha biashara, kufilisika au kushindwa kusimamia mifumo hiyo kutaliwezesha shirika kupata usaidizi kwa kushirikiana na mtoa huduma mwingine kuendesha mifumo endapo mtengenezaji wa mifumo wa awali ataacha kutoa msaada kwa watumiaji/wateja.

15.2.1.3 Kukosekana ulinzi wa taarifa muhimu za mifumo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) halijaweka udhibiti wa taarifa muhimu kama vile (password) na (security keys) za mifumo ambazo hutumika wakati wa kutuma na kuhifadhi taarifa muhimu za mifumo ili kuhakikisha kunakuwepo na usiri na uadilifu katika upatikanaji wa taarifa za mifumo hiyo. Hali hii imepelekea kuwepo na udhaifu katika kulinda rasilimali muhimu za taarifa za mifumo na udhaifu wa udhibiti wa rasilimali ya taarifa muhimu za mfumo, mbapo udhibiti wa taarifa (data encryption), upatikanaji na utumiaji (access control) wa taarifa muhimu za mifumo unaweza kuwafikia mtumiaji ambae hakuruhusika kiutaratibu na hivyo kuweza kupelekea kupata uwezo ambao utamruhusu mtu huyo kukwepa vipengele vya usalama wa mifumo na taarifa na hivyo kuweza kusoma, kurekebisha, au kuharibu taarifa au rasilimali nyingine za mifumo kama seva na kompyuta.

Ukaguzi unashauri wasimamizi wa usalama wa mifumo na taarifa (IT Security) wa ZECO kuchukuwa juhudi za makusudi katika kulinda taarifa muhimu za mifumo ya Shirika dhidi ya uwezekano wa mashambulizi ya programu zinazoathiri mifumo (ransom-ware), virusi vya mtandao (internet virus) pamoja na wizi wa taarifa za mifumo na mashambulizi ya kimtandao (Cyber attack) jambo ambalo linapotokea linaweza kupelekea shirika kuingia hasara kubwa kwa kulipa ada ya kugomboa taarifa (ransom).

15.2.1.4 Kutokukidhi vigezo kwa eneo la kuokoa maafa (Data Recovery Center)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme ZECO linamiliki eneo la kuokoa maafa (Data Recovery Center) ambapo kikawaida eneo hili hutumika kwa kuwekea vifaa vinavyo huhifadhi nakala za taarifa (Data Backup) kwa ajili ya matumizi ya baadae endapo kukitokea hitilafu au kuimarisha mifumo(Updates). Aidha imebainika kwamba maeneo ambayo kipo kituo cha kuokoa maafa Saateni ni masafa ambayo ni mafupi kutoka zilipo Ofisi kuu ya Shirika Gulioni,jambo ambalo endapo kutatokea maafa kuna uwezekano mkubwa wa kuathiri hadi kituo cha kuokoa maafa.hali hii imepelekea kituo hicho kukosa sifa na vigezo vinavyokubalika kulingana na utendaji kazi bora na viwango vya kimataifa kama vile ISO Standard 7031 vinavyozingatia mahitaji ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ITC) kwa ajili ya kuendelea na biashara na kujitayarisha kwa maafa.

Utendaji kazi bora unahitaji taasisi inayotumia mifumo ya TEHAMA kama nguzo katika uendeshaji wa shughuli muhimu za kiutendaji ni lazima iwe na Mpango wa Kuokoa Maafa (DRP) na Mpango wa Kuendeleza Biashara (BCP) ambao unahitaji kuwa na maelezo muhimu na yenye kujitosheleza juu ya uendeshaji ambayo yanaruhusu uhuwishaji wa shughuli za kazi kama ulivyoandaliwa, kwa utaratibu na kwa wakati.

Ukaguzi umebaini hati na miongozo ifuatayo haikuwepo kama vile maelezo ya mawasiliano ya dharura, timu za uokoaji, hifadhi rudufu ya data muhimu nje ya sehemu ya kuhifadhi data kwa ajili ya dharura, mbinu mbadala ya mawasiliano na awamu ya waokoaji kama fire brigade, polisi na kadharika, ingawa baadhi ya hatua za usalama zilizopo sasa zinaweza kutumika kurejesha huduma za Tehama, kuna uwezekano mkubwa kwamba iwapo maafa makubwa yatatokea kwenye chumba cha kompyuta, uendelezaji wa shughuli za Tehama unaweza kuathirika. Aidha taarifa (data) zinazohifadhiwa kwa ajili ya kujikinga na maafa hazijaribiwi kwa ajili ya urejeshaji na hakuna utaratibu wa mara kwa mara wa kufanya nakala rudufu (backups) kwa ajili ya urejeshaji na mpango wa mwendelezo wa biashara hali hii inaweza kupelekea taarifa (data) za shirika kuwa katika hatari kubwa ya kutopatikana ikiwa janga litatokea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuhakikisha kwamba wasimamizi wa usalama wa Tehama kupitia Kamati ya Uongozi ya Tehama kutafuta mahali panapofaa kwa ajili ya eneo la pili la uokoaji ambalo litakidhi vigezo vya mafasa (mahali pa mbali na mazingira ya ZECO HQ) pamoja na kupitia upya na kusasisha mara kwa mara na kwa wakati (Business continuity and Disaster Recovery Plans) ikiwa ni pamoja na kuandikwa upya,kusambazwa pamoja na kuhifadhiwa nje ya sehemu ya uhifadhi wa taarifa (data) makao makuu.

15.2.1.5 Kutokufanya majaribio ya kupima usalama (Penetration Test)

Kwa mujibu wa viwango (ISO 27001 mfumo wa usimamizi wa usalama wa habari) unahitaji kwamba upimaji wa usalama (Penetration Test) ufanywe kwa kuangalia uimara wa mifumo dhidi ya wavamizi ambao hawajaidhinishwa kutumia taarifa za mifumo husika. Hali hii inahitaji taasisi kufanya tathmini ya mara kwa mara ya tishio na udhaifu ili kugundua na kurekebisha mapungufu ya kiusalama kwenye Tehama na vifaa ili kuzuia ueneaji wa mashambulizi yoyote na matishio ya mara kwa mara kuhusu usalama wa Tehama.

Ukaguzi umebaini kwamba Uongozi wa Shirika la Umeme (ZECO) haukutayarisha miongozo kuhusiana na masuala ya kupima usalama wa mifumo ambapo hata Sera za sasa za Tehama za ZECO hazina vipengele vinavyosisitiza juu ya umuhimu wa kufanyika kwa upimaji wa usalama (Penetration Test) hali ambayo inatilia shaka ubora na uimara wa usalama wa mifumo ya Tehama ya Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa shirika kuhakikisha kwamba Jaribio la upimaji wa usalama kwenye mifumo ya Tehama linafanywa mara kwa mara kwa kuwatumia wataalama wa ndani na nje angalau mara mbili katika kila baada ya miaka miwili kama ilivyoenezwa katika viwango vya kimataifa na utendaji bora wa Tehama na ripoti za majaribio hayo zinapaswa kuandikwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya ubora na uimara wa mifumo ya shirika.

15.2.1.6 Mapitio ya kanzidata ya mfumo (System Database)

Utendaji bora unahitaji kwamba, kila baada ya miaka miwili hadi mitatu kanzidata (System Database) inapaswa kufanyiwa mapitio ili kubaki na taarifa (data) sahihi ambazo zitakuwa za kuaminika na zenye ubora kwa ajili ya kufanya maamuzi, pia vipengele vya ubora wa taarifa vinavyoamua ubora huhitaji uchunguzi wa sifa na vigezo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba shirika lilikuwa likiendelea kutumia taarifa (data) zisizo sahihi ambazo nyingi hazifai tena kuendelea kuwapo au zinahitaji maboresho ndani ya na kanzidata ya mfumo wa SAP (SAP system Database) tokea kuanzishwa mwaka 2014 ambapo wateja wote walipewa nambari za SAP, kabla ya wateja hao kuingizwa katika mfumo wa Suprima kwa kukosa nambari za akaunti za SAP. Hali hii inaweza kupelekea watumiaji wa mifumo wa ZECO kutokuutumia mfumo na kutegemea kutengeneza Ripoti nje ya mfumo kwa kutumia 'Microsoft Excel' ambapo inaweza kupelekea thamani ya fedha iliyowekezwa kwenye mfumo kuweza kutokupatikana.

15.2.1.7 Dosari zilizobainika katika mfumo wa ulipaji mishahara (Payroll)

Mfumo wa ulipaji, nyongeza na ukataji wa kodi kutoka kwenye mishahara uliotengenezwa kwa ajili ya shirika haukidhi mahitaji ya kimsingi kwa michakato ya malipo kama ifuatavyo:

- Mfumo wa malipo kuendela kuwatambua wafanyakazi ambao hawapo kazini wastaafu na walioachishwa kazi.
- Mfumo kukosa uwezo wa kuchakata taarifa katika ulipaji wa malipo na makato kama muda wa ziada.
- Mfumo hauna udhibiti (access control) ambapo imebainika watumiaji ambao hawajaidhinishwa wanaweza kufikia majedwali ya mishahara (payroll tables) ambayo huhifadhi taarifa (data) muhimu za malipo ambazo zinapaswa kufikiwa na wafanyakazi walioidhinishwa pekee.
- Mfumo hauwezi kujumuisha nambari za malipo na makato kwa madhumuni ya kutengeneza jarida la malipo (payroll journal).
- Kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu kati ya idara ya Utumishi na Idara ya Fedha katika usimamizi wa taarifa za wafanyakazi (creation and deactivation) na usimamizi wa mishahara.

- Kukosekana kwa ripoti ya udhibiti wa mfumo wa malipo inayoonyesha malipo na makato kwa muda.
- Kufanyika malipo kwa kutumia Ms excel na SAP ambapo tofauti ya taarifa za malipo kutoka kwa excel na SAP zinatilia shaka juu ya uhalisia wa ripoti za kifedha.

Kushindwa kutumia mfumo katika kushughulikia taarifa za wafanyaaazi kunaweza kupelekea uwezekano wa wafanyakazi kupokea mshahara hata baada ya kuondoka kwenye shirika jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vinavyoweza kuasabisha upotevu wa fedha.

15.2.1.8 Dosari katika ripoti za mfumo wa SAP

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ripoti zinazotayarishwa na mfumo wa SAP hazikuandaliwa na kubainishwa (customized) vya kutosha katika mfumo huo ambapo katika ripoti hizo kumekuwa na hali ya kukosekana kwa taarifa muhimu ambazo mfumo wa SAP unashindwa kuzitoa. Miongoni mwa taarifa muhimu zilizokosekana ni pamoja na taarifa za wadai, wadaiwa, ghala za vifaa ambapo uandaaji wa hesabu za mwaka bado zinafanywa kwa mfumo wa kawaida (Manual System) jambo ambalo hupelekea mchakato wa kuripoti kutengenezwa kwa njia ya kawaida "mkono" ambapo kunaweza kunatumia muda mwingi na kusababisha taarifa kutokupatikana kwa urahisi na uhakika kwa wafanyakazi walioidhinishwa.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba watumiaji wa mifumo wa shirika hawana mafunzo ya kutosha ya utendakazi wa ripoti za SAP na hivyo kushindwa kurekebisha au kufanya mabadiliko katika vipengele vya kuripoti ili kukidhi mahitaji yanayotakiwa.

Kushindwa kwa mfumo wa SAP kutoa taarifa muhimu kulinganana na mahitaji ya Shirika, na kuandaa taarifa hizo za mwongozo, kutasababisha watumiaji wa mfumo huo kutokuwa na imani nao jambo linalosababisha kuwepo kwa mifumo miwili yaani mmoja usio wa kieletroniki (manual) na mfumo wa SAP kwa wakati mmoja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuwasiliana na mtengenezaji wa mfumo wa SAP ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuwezesha upatikanaji wa ripoti zote kwenye mfumo.

15.2.1.9 Dosari katika matengenezo na upatikanaji wa mikataba na changamoto za Tehama.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba shirika lina utaratibu uliojiwekea wa utunzaji wa mikataba yote kupitia ofisi ya mwanasheria wa shirika. Ukaguzi umebaini kukosekana kwa utaratibu mzuri wa kuhifadhi mikataba katika ofisi ya mwanasheria, vile vile ukaguzi umebaini kwamba mikataba hiyo inahifadhiwa kwa njia ya nakala ngumu (hard copy) pekee ambazo zimehifadhiwa katika ofisi ya mwanasheria tu hali iliopolekea kuwepo kwa changamoto katika kupata mikataba ya mifumo inapohitajika kwa nakala za kielektroniki.

Kutokuwepo au kutopatikana kwa mikataba ya Tehama inayohusiana na ununuzi na mikataba ya uwezesaji wa mifumo kuwa salama (Service Level Agreement) kunapelekea kutilia shaka uhalali wa makubaliano kati ya shirika na mtoa huduma jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya upotevu wa fedha na mikataba isiyo na tija.

15.2.1.10 Kukosekana kwa programu ya Ufuatiliaji wa leseni zilizokwisha muda wake wa matumizi vifaa vya Tehama,program/software na mifumo ya Tehama.

Usimamizi wa leseni ya programu ni sehemu ya usimamizi wa tathmini ya programu nani mchakato ambao lengo lake kuu ni kupunguza na kudhibiti gharama za Tehama kwa ujumla. Kwa urahisi ni mpango wa matengenezo wa kudhibiti leseni zote za programu za shirika na kupunguza hatari na kuokoa matumizi ya Tehama kama ifuatavyo:-

- Kupata picha ya jumla ya programu zilizoidhinishwa kwa matumizi yaliyo sahihi na kubaini program zisizo na leseni.
- Kupunguza hatari za usimamizi wa leseni na kuendelea kufuatilia tarehe za mwisho wa leseni na kutoa taarifa mapema.
- Kuboresha ununuzi wa leseni kwa kuwa na mwonekano wa pamoja wa idadi ya leseni ambazo hazijatumika na ambazo hazitumiki sana.
- Kutambua ukiukaji wa leseni kwa njia ya kielektroniki (automatic) kwa kuratibu ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya kazi na kupitia ukaguzi kwa urahisi.

Katika ukaguzi wa Tehama na uhalali wa leseni ya mfumo wa uendeshaji na programu, ukaguzi umebaini shirika lina zaidi ya kompyuta 250 na seva nane kwa mfano, Seva sita ziko katika ofisi ya makao makuu na seva mbili ziko ofisini Pemba. Hata hivyo, imebainika kuwa baadhi ya kompyuta zilikuwa zikifanya kazi bila leseni sahihi au za kisheria kutoka kwa Microsoft Corporation pia seva za HP ProLiant 380 G8 5 ambazo zinatumiwa na shirika kwa mfano Seva 2 ambazo ziko Pemba ni kwa ajili ya Aquillium na bakup na seva 2 za kuhudumia mfumo wa Aquillium na Antivirus zilizopo Makao Makuu na seva 1 ya Aquillium iliyopo kwenye kituo cha kuhifadhi nakala za (backup) zimeisha rasmi muda wake tangu tarehe 30/06/2021 na hazijapata tena updates/viendeshi, usasishaji na uboreshaji tangu tarehe ilipotangazwa na hakukuwa na programu ya ufuatiliaji wa programu ili kutambua na kutahadharisha hali ya Shirika ya Leseni zilizopo kwa ajili ya kupanga kuepuka leseni zinazoisha muda wake na kuepuka faini mbalimbali kutoka kwa Microsoft Corporation na mtandao wa ushirika kwa matumizi yasiyo salama ya programu na hardware zilizoisha muda wake. .

Mbinu bora inasema kwamba kufuatilia orodha ya programu, matoleo, na uwekaji halisi unaweza kutekelezwa na Taasisi za Umma ili kudhibiti programu/vifaa vilivyo na leseni na pia itafanya ukaguzi wa programu kwenye kompyuta ya mezani,seva na Local Area Network (LAN).

Ufuatiliaji wa utoaji leseni na utiifu wa programu huhakikisha kwamba michakato ya usimamizi wa programu inafanya kazi kwa ufanisi na kwamba programu zisizo na leseni halali hazitumiki.

Kuendelea kutumika kwa programu zisozokuwa na leseni ya matumizi ya Shirika kunaweza kujitokeza kwa athari zifuatazo:-

- Kuathiri usalama wa mtandao wa shirika.
- Kutokupatikana kwa usaidizi wa kiufundi na matumizi yake yanayoweza kusababisha upotevu wa tija ndani ya mtandao wa shirika.

- Inaweza kuharibu taswira na sifa ya kitaaluma ya shirika.

Ili kuhakikisha kuwa shirika linatumia programu halisi na yenye leseni, ukaguzi unapendekeza yafuatayo:-

- Shirika kununua programu ya usimamizi wa Leseni inayoweza kufanya vipengele vyote vya mchakato wa ufuatiliaji, taarifa na ununuzi wa leseni kiotomatiki na kufuatilia leseni zote za programu za shirika kwa kuhalalisha, kuinisha na kutambua kiotomatiki aina za leseni, kufuatilia matumizi ya leseni ya programu na kudhibiti orodha ya leseni ya mifumo mbalimbali .
- Idara ya Tehama, kupitia program yenye leseni ilizohifadhiwa katika kitengo cha Tehama kuthibitisha/kutathmini programu inayotumiwa ili kuhakikisha kwamba programu ni ya kweli na ina hitaji la leseni inayolingana.
- Kuimarisha usimamizi kuhakikisha kuwa programu inatumika kwa mujibu wa masharti ya makubaliano ya leseni husika.

15.2.1.11 Matumizi ya programu zilizokwisha muda wake.

Katika ukaguzi ulifanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme (ZECO) linatumia vifaa ambavyo vimeisha muda wake wa matumizi na havipati msaada wa kinga toka kwa watengenezaji wake kama vile HP ProLiant DL350 G8 kupangisha programu muhimu ikiwa ni pamoja na mfumo mkuu wa biashara yaani Aquillium na seva ya backup ya mfumo huo wa Aquillium. Seva ya HP ProLiant DL350 ilifikia mwisho wa mtumizi mnamo Novemba 30, 2014. Mwisho wa matumizi ya huduma ya seva aina ya IBM System x3650 M4 ambayo ina program ya Anti virus ni tarehe 31 Desemba 2021. Biashara zinazotegemea miundo mbinu ya zamani zinaweza kuishia kutofaulu katika usanifu wa mfumo wao, na pia huweka afya na usalama wa vifaa vyote vilivyounganishwa katika hatari kubwa. Utaratibu huu katika mitandao ya biashara unaweza kuathiri tija na uwezo wa shirika kuhudumia wateja wake wa ndani na nje.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa shirika linatumia Mfumo wa Uendeshaji wa seva ya Windows 2003 ambao haukuwa na msaada tena, kutokana na wamiliki wa programu hiyo (Microsoft) kutangaza rasmi Julai 14, 2015 kusitisha kutoa msaada wa aina yoyote kwa programu hio.

Kuendelea kutumia Window Server 2003 kunaweza kupelekea athari kushambuliwa na virusi na kuharibiwa kwa mfumo wa EQUILLIUM ulioingizwa ndani ya kompyuta hiyo ya zamani kutokana na kukosekana kwa udhibiti, ulinzi na usalama katika seva hiyo pamoja na kukosa msaada wa maboresho kutoka kwa wamiliki waliotendeneza program hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kuhakikisha unapata toleo jipya la mfumo wa uendeshaji unaotumika ambapo kwa sasa mfumo mpya wa uendeshaji wa kompyuta uliopo sokoni ni Windows Server 2019.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kusitisha matumizi ya mfumo wa zamani na kuimarisha ikiwa huduma zinazoendeshwa kwenye mfumo wa Windows Server 2003 hazihitajiki tena, au zinaweza kuunganishwa kwenye seva zingine, ukaguzi unashauri kuondoa seva kutoka katika

mtandao wa shirika (network) inayohatarisha na kukaribisha mashambulizi toka kwa wizi wa mtandao (Cyber-Attackers).

15.2.1.12 Kukosekana nyaraka muhimu za makabidhiano ya mifumo

Uhamisho wa mfumo wa programu kutoka kwa mtaalam anayehusika na uundaji wake hadi kwa mnunuzi anayehusika na matengenezo yake hurejelewa kama makabidhiano ya mfumo wa programu au mpito. Kukabidhi ni mchakato muhimu katika mzunguko wa maisha wa programu na ni muhimu kwamba ufanyike kwa urahisi iwezekanavyo.

Lengo la makabidhiano ni mawasiliano sahihi ya kuaminika ya taarifa zinazohusiana na kazi iliyofanywa na mtengenezaji kwa mujibu wa makubaliano na mtumiaji au watumiaji wa mfumo na hivyo kuhakikisha uendeleu wa kufanya kazi kwa usalama na kwa ufanisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Umeme halina nyaraka muhimu zinazoonesha kuwepo kwa makabidhiano ya mifumo yao yote kutoka kwa watengenezaji mifumo ili kuthibitisha kuwa wamekabidhiana mfumo kwa kuzingatia masharti ya mikataba na kwamba mifumo hio inamilikiwa wa shirika. Hali hii inapelekea shirika kutokuwa na umiliki halali kisheria kwa mifumo iliyopo kutokana na kukosa nyaraka za umiliki.

Katika siku zijazo, uongozi unapaswa kuhakikisha kuwa:-

- Mfumo wa kukabidhi vyeti upo kama ushahidi wa umiliki. Makabidhiano ya mfumo ni wakati muhimu wa kuhakikisha mwendeleo wa utunzaji na usalama wa shirika na kwamba ripoti inayotolewa wakati mtaalamu muuzaji wa mfumo anahamisha jukumu la mfumo kwa shirika na kuanishwa ni muhimu.
- Hati lazima ziandikwe kwa watumiaji wa mwisho (system user). Huenda ikahitaji seti tofauti za hati kwa watumiaji tofauti lakini ili uwekaji wa hati kusaidia uhamishaji wa maarifa unahitaji kuwa wa maana, utumike na unaofaa kwa watumiaji wa mwisho.
- Watumiaji (uongozi) kukubaliana na Watengenezaji au wauza mifumo, na kuhakikisha kwamba wahusika wote wana uwasilishaji ulio wazi, na kujua kile kinachotarajiwa kutoka kwao na kujitahidi kufikia lengo tangu mwanzo wa mradi.

15.2.2 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Shirika la Umeme Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kwa ushirikiano mzuri mliotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi yetu kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi ujao.

SURA YA KUMI NA SITA

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR – (ZSSF)

16.0 UTANGULIZI

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye dhamana ya ukusanyaji, utunzaji salama, uwekezaji unaowajibika, na ulipaji wa fedha za kustaafu kwa wafanyakazi wote katika sekta zote za Umma pamoja na sekta binafsi. Katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuimarisha maisha bora kwa wananchi wa Zanzibar Mfuko wa ZSSF umekuwa ukiongeza huduma mbalimbali za mafao kwa wanachama wake ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa waajiriwa wapya (start-up life loan), mafao ya uzazi (maternity Benefits), mikopo ya kujiendeleza kielimu kwa wanachama wake waliotimiza vigezo pamoja na mafao kwa wanachama waliopatwa na ulemavu au ugonjwa uliowasababishia kushindwa kuendelea na majukumu ya kazi.

16.1 UANZISHWAJI WA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ilianzishwa chini ya Sheria Na. 2 ya mwaka 1998 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 9 ya mwaka 2000 na kufanyiwa tena marekebisho kwa Agizo la Serikali la mwaka 2004 na hatimaye kutungwa na kupitishwa upya Sheria ya ZSSF Na.2 ya mwaka 2005 .

16.2 LENGU LA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA YA ZSSF

Ukaguzi wa TEHAMA katika mfuko wa Hifadhi ya Jamii umefanyika kwa madhumuni ya kufanya kutathmini ya muundo wa ndani wa udhibiti wa mfumo na ufanisi (Internal Control and Affectiveness) kuangalia ufanisi na usalama wa mifumo iliyopo, michakato ya maendeleo ya utawala na usimamizi katika masuala ya Tehama au (IT Governence) kutathmini mifumo ambayo iko katika nafasi ya kulinda taarifa za Mfuko pamoja na kutathmini uwezo wa shirika kulinda mali zake kwa kuzingatia sera, miongozo, na mikataba ya makubaliano katika upatikanaji wa vifaa na miundombinu ya mifumo ya TEHAMA.

16.2.1 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi umebaini Mfumo wa hifadhi ya Jamii unatumia mfumo wa Usimamizi wa Taarifa na Michango ya Wanachama (FUMIS na MIMS), Mfumo wa Usimamizi wa Michango ya Hiari (VOMIS) na Mfumo wa Usimamizi wa Masuala ya Fedha (Microsoft Navision), Mfumo wa kutunza nyaraka kwa njia ya Kielektroniki (EDMIS) n.k.

Hata hivyo katika utumiaji wa mifumo hiyo ukaguzi umebaini dosari mbalimbali za kiutendaji katika mifumo hio ambapo dosari hizo zilibainishwa na kufafanuliwa athari zinazotokana na dosari hizo na kutolewa maoni na mapendekezo kwa Uongozi wa ZSSF kwa lengo la kuzirekebisha dosari hizo ili kuweza kuendelea kutoa huduma bora za mafao kupitia mifumo iliyowekwa. Miongoni mwa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

16.2.1.1 Mapitio ya Mfumo Mkuu wa Malipo kupitia tovuti ya ZSSF (Web Portal)

Ukaguzi ulipitia mfumo wa malipo ya michango inayotolewa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia mfumo mkuu wa malipo wa BOT (Central Payment System) kwenda kwenye akaunti za benki husika za ZSSF zinazopokea michango PBZ huwasilisha michango ya wafanyakazi na hatimaye kuwasilisha kwenye akaunti za benki za ZSSF kupitia akaunti zilizopo.

Ukaguzi umebaini kutokuwepo na muunganisho wa mfumo kati ya BOT (Central Payment System) na benki husika ambazo zinawajibika kupokea michango kwa niaba ya ZSSF kwenye Mfuko wa akaunti za benki. Aidha ilibainisha kuwa mara michango inapowekwa kwenye akaunti za benki za ZSSF na benki husika utambuzi wa kiasi kilichowekwa kwenye vitabu vya hesabu vya Mfuko ulifanyika kwa mikono (manually) baada ya maofisa wa taasisi zinazolingia kwenye malipo ya kati kupeleka risiti na nakala zilizotengenezwa kwa excel yenye orodha ya wafanyakazi waliochangia katika mwezi fulani ambao hatimae orodha hiyo kutumwa kwa kitengo cha kuingiza data kwa njia isiyokuwa ya muunganisho wa mifumo.

Kukosekana kwa muunganisho wa mfumo (System integration) kati ya akaunti ya BOT (Central Payment System) na benki nyingine kunapelekea ZSSF kupokea michango mikubwa ambayo haijapitia kwenye mtandao wa ZSSF portal (control number) na kusababisha ugumu wa kufanya mlinganisho (reconciliation) kati ya fedha taslimu na miamala ya benki kwa amana zote zisizotambulika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuchukua juhudi za ziada kujadiliana na benki husika zinazohusika na kupokea michango ya waajiri ili kuwasiliana na BOT kuhusu muunganisho wa mifumo ya benki na mfumo wa BOT ili malipo yote ya michango yaweze kupokelewa kupitia mfumo wa tovuti (web Portal) kwa kutumia namba za uhibititi ili kurahisisha utambuzi wa michango kwa wakati na kwa usahihi.

16.2.1.2 Dosari katika Kituo cha kuendeleza upatikanaji wa huduma za ZSSF wakati ikitokezea maafa (Disaster Recovery Site)

Eneo la kuendeleza huduma baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumika wakati ikitokezea maafa au janga katika eneo kuu linalotoa huduma (Primary Site) na kupelekea miundombinu inayotumika kutoa huduma katika eneo kuu kuharikibika au kupotea na hatimae kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system).

Katika utaratibu uliobora eneo hili hutengwa mbali na eneo kuu kwa angalau masafa ya umbali wa kilomita 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja endapo ikitokezea maafa au janga. Aidha eneo hili linatakiwa kuwa na uwezo wa kufanya kazi sawa sawa kama lilivyo eneo kuu linalotumika kila siku, kwa maana ya kuwa miundombinu yote ya TEHAMA, usalama pamoja na taarifa zinazohifadhiwa (data backup) zinatakiwa kuwepo na kufanya kazi kwa vile wakati wowote eneo hili linaweza kuchukua nafasi ya eneo kuu linalotumika kila siku.

Ukaguzi umebaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) una kituo chengine kilichopo Mwanakwerekwe ambacho kimewekwa kama ni kituo mbadala cha kuendeleza huduma za Mfuko (disaster recovery site) endapo janga likitokezea katika makao makuu ya ZSSF yaliyopo Kilimani Mnara wa Mbao.

Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa kituo hicho kilichopo Mwanakwerekwe hakiko katika umbali wa masafa marefu kutoka katika eneo la makao makuu yaliyopo Kilimani Mnara wa Mbao, jambo ambalo ni kinyume na taratibu bora na miongozo ya Disaster Recovery Site. Aidha imebinika kuwa taarifa zinazohifadhiwa katika kituo hicho cha disaster Recovery hazijawahi kufanyiwa majaribio kwa lengo la kuhakikisha kwamba taarifa hizo zinafanya kazi sawa sawa na zinaweza kutegemewa wakati ikitokezea maafa au janga katika eneo la makao makuu ya ZSSF Kilimani.

Kutokana na ukaribu wa masafa uliopo baina ya maeneo hayo, iwapo maafa au janga kubwa likitokezea kunaweza kupelekea uwezekano wa vituo vyote viwili kuathirika na janga hilo na kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na wananchi jambo ambalo litapelekea kuathiri utendaji kazi wa Mfuko kutokana na kukosekana kwa huduma kwa muda usiojulikana.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kubadilisha eneo lililokuwa katika mazingira mazuri, ya usalama na yenye masamba ya umbali mrefu angalau kuanzia kilomita 50 kulingana na uhalisia wa mazingira ya Visiwa vya Zanzibar.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF uandae sera maalum na kuitekeleza kwa kufanya majaribio ya mara kwa mara ya taarifa zote zinazohifadhiwa katika miundombinu ya kituo mbadala cha kuendeleza huduma za Mfuko (Disaster Recovery Site) ili kuweza kubaini hali halisi ya utendaji kazi wa taarifa zinazohifadhiwa.

16.2.1.3 Ukosefu wa nyaraka rasmi za msingi za kiulinzi katika mtandao/network ya ZSSF (Udhibiti wa Firewall na Udhibiti wa Ufikiaji/Udhibiti wa Mipaka katika mifumo ya Tehama)

Ukaguzi umebaini ZSSF imeweka kinga za ulinzi wa kulinda mazingira ya mtandao wake kupitia vifaa maalumu vilivyofungwa vya kudhibiti usalama katika mtandao na miundombinu ya TEHAMA (firewall). Hata hivyo, ukaguzi umebaini ZSSF haijaweka sera imara ya utaratibu wa kukagua mara kwa mara mipangilio ya vifaa na kuchuguza ubora wake wa kupambana na kudhibiti matumizi ya proramamu na tovuti mbali mbali zisizohitajika kuangaliwa katika ofisi ambazo zinaweza kusababisha athari mbali mbali na zinazoenda kinyume na sheria, taratibu, miongozo na maadili ya ZSSF ambazo pia zinaweza kupelekea kuhatarisha usalama wa mifumo ya ZSSF.

Sera bora za kimitandao, zinaeleza kwamba sera ya ulinzi wa mitandao (firewall) unapaswa kuamuru jinsi ulinzi wa mitandao unavyoweza kushughulikia taarifa zote za mtandao kulingana na sera za usalama wa habari za shirika, na uchanganuzi wa hatari unapaswa kufanywa ili kubaini aina za trafiki zinazohitajika na shirika. Sera inapaswa pia kujumuisha mwongozo maalum wa jinsi ya kushughulikia mabadiliko ya sheria iliyowekwa.

Kushindwa kutayarisha sera ya usanidi wa ulinzi wa mitandao (firewall) na kudhibiti mipangilio kunaweze kupelekea kuongeza athari kwa ZSSF kwa kushindwa kukabiliana na wingi wa majanga ya kimtandao na usalama wa mitandao ya ZSSF.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa ZSSF uandae sera imara za usanidi na matumizi ya vifaa vya usalama (firewall configuration) na kuweka katika kumbu kumbu za nyaraka za mifumo pamoja na kutekeleza mchakato wa kukagua mara kwa mara na kuboresha sera za ulinzi wa mifumo zilizosanidiwa ndani ya firewall ili kuruhusu tovuti ambazo hazitakuwa na madhara kwa mtandao wa ZSSF.

16.2.1.4 Kukosekana kwa Mfumo wa kuchunguza, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZRB (Licensed Network Monitoring System).

Mfumo wa kuchunguza, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao (Network Monitoring System - NMS) ni moja kati ya zana muhimu za kiusalama ambazo taasisi kubwa zenye kutumia mifumo na miundombinu ya tehamu hupaswa kutumia zana hizo kwa lengo la kupima, kudhibiti pamoja na kufanya tathmini ya viwango vya matumizi ya mtandao na miundombinu ya tehamu iliyopo katika taasisi.

Tathmini hiyo hufanyika katika kipindi cha muda mfupi kwa njia ya kielektroniki kupitia mifumo ya aina hiyo ambapo hupima kasi ya mtandao, trafiki, matumizi ya data, huchunguza uwepo wa usalama na hali ya mtandao (network status & security updates), hudhibiti mashambulizi yanayotokana na udukuzi (cyber attacks) pamoja na kuweza kufanya utambuzi wa aina gani ya kifaa cha tehamu au chanzo kinachopelekea kutokea kwa hitilafu katika mtandao wa Taasisi. Aidha, baada ya kumalizika kufanyika kwa tathmini mfumo huwasilisha ripoti ya matokeo kwa maafisa wasimamizi wa Mtandao (network administrators) kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe au ujumbe mfupi "sms" kulingana na maafisa watakavyo seti mfumo namna ya kuwasilisha taarifa za matokeo.

Kwa ujumla mfumo wa Network Monitoring System huwasaidia na kuwarahisishia kazi Maafisa wanaosimamia Mtandao katika Taasisi kwa kuweza kugundua haraka chanzo cha hitilafu wakati inapotokezea tatizo katika mtandao wa taasisi ambapo bila ya uwepo wa mifumo hiyo maafisa wangukuwa wanafanya kazi kubwa ya kukagua vifaa na miundombinu ya tehamu iliyopo kwenye taasisi kwa njia ya kawaida "manually" ili kubaini chanzo cha hitilafu jambo ambalo lingepelekea kupoteza muda, nguvu na usumbufu ikiwa miundombinu ya taasisi ni mikubwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ZSSF imeweka mtandao mkubwa wa mawasiliano kwa lengo la kuwezesha upatikanaji mzuri wa mifumo yake ya makusanyo ya mafao katika ofisi zake kwa Unguja na Pemba. Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mfumo ulio rasmi na maalum (Licensed Network Monitoring System) kwa ajili ya kuchunguza usalama wa mtandao wa ZSSF, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao na mifumo, kudhibiti mashambulizi yanayotokana na uhalifu wa udukuzi wa mtandao na mifumo ya ZSSF pamoja na kufanya tathmini ya mwenendo wa utendaji kazi wa vifaa na miundombinu ya tehamu inayotumika ZSSF kwa lengo la kuendelea kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ili kuweza kupatikana huduma bora za makusanyo ya mapato kutoka kwa walipa kodi.

Kukosekana kwa Mfumo rasmi wa kuchunguza, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZSSF kunaweza kupelekea Mfuko kushindwa kulinda mtandao na mifumo yake dhidi ya uhalifu unaoweza kutokezea ikiwemo mifumo kufanyiwa udukuzi, kushambuliwa na virusi, kuchezeza kwa makusudi na hatimae kuweza kujitokeza kwa upotevu wa mapato jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha unafanya jitihada za kununua na kumiliki mfumo madhubuti wenye leseni ya matumizi na uwezo mkubwa wa kusimamia, kuchunguza, kudhibiti, kufanya tathmini na kuongeza ulinzi katika mtandao, vifaa pamoja na miundombinu ya tehama iliyofungwa katika ofisi zake kwa Unguja na Pemba ili kuweza kuhakikisha kwamba usalama wa matumizi ya mtandao na mifumo unaimarika kwa kiwango kikubwa pamoja na kurahisisha kazi ya ukusanyaji wa mafao kutoka kwa wanachama wa ZSSF.

16.2.2 HITIMISHO

Kutokana na maoni pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ya ukaguzi, kwa mwaka unaofuata Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kuona mabadiliko chanya katika Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar inapenda kutoa shukurani za dhati kwa uongozi wa ZSSF kwa ushirikiano mzuri mliotupatia katika kufanikisha kazi ya ukaguzi, ni matarajio ya Ofisi yetu kwamba ushirikiano huu utaendelea na kuongezeka zaidi katika ukaguzi ujao.

SURA YA KUMI NA SABA

UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR –(ZIC)

17.0 UTANGULIZI

Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 umefanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu, miongozo na pamoja na viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa vilivyopo, ukiwa na madhumuni ya kupima tathmini katika matumizi ya Tehama kwa kuangalia kiwango cha utendaji kazi wa mfumo iliyopo, udhibiti na usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani ya mifumo hiyo, utunzaji wa siri katika mifumo, mipaka ya matumizi ya mfumo, uadilifu, ufanisi, tija, uwajibikaji wa watumiaji wa mfumo, urahisi wa upatikanaji wa taarifa ndani ya mfumo, pamoja na kuangalia muingiliano na mifumo mengine.

Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) ni Taasisi inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo shughuli zake kuu ni kusimamia upatikanaji wa huduma za bima zisizohusiana na vyombo vya moto na bima zisizohusiana na vyombo vya moto (Motor and Non Motor Insurance) kwa wananchi wa Tanzania.

Shirika la Bima Zanzibar ni miongoni mwa mashirika yanayotumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika kuhakikisha kwamba huduma za bima zinapatikana kwa njia ya urahisi ili kuwaondolea usumbufu wananchi pamoja na Taasisi zinazohitaji huduma hiyo.

17.1 UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR

Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) lilianzishwa mwaka 1969 chini ya Sheria ya uanzishwaji wa Mashirika ya Umma Zanzibar ya mwaka 1966 (Legal Notice No. 11 of 1969) na baadae kufanyika tena mabadiliko ambapo kwa sasa Shirika linafanya kazi chini ya Sheria ya Uwekezaji wa Umma Na. 4 ya mwaka 2002.

Aidha Shirika katika mchakato wa kuimarisha huduma zake za biashara ya Bima limefanikiwa kuongeza upeo wa kutanua huduma zake bima kwa kuongeza ofisi na matawi ya bima katika visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Mikoa iliyopo Tanzania Bara.

17.2 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi wa mifumo ya Tehama katika Shirika la Bima Zanzibar umefanyika kwa lengo la kuangalia udhibiti na usalama wa mifumo ya Shirika, kufanya tathmini ya ujumla ya matumizi ya Tehama (IT Governence) kuanzia hatua ya upatikanaji wa mikataba ya ununuzi wa mifumo, sera zinazosimamia matumizi bora ya Tehama ndani ya shirika, changamoto zinazojitokeza za mifumo inayotumiwa na Shirika na namna Shirika linavyochukua hatua ya kuzitatua. Mbinu na nyenzo mbali mbali zilitumika katika ukaguzi (Auditing tools and Techniques) zikiwemo sheria, kanuni, sera, miongozo na viwango mbali mbali vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi wa mifumo ikiwemo eGAZ, eGA, ISACA, AFROSAI-E, COBIT 5, INTOSAI n.k.

17.2.1 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Matokeo ya ukaguzi wa mifumo ya Tehama katika Shirika la Bima Zanzibar yanatokana na kazi ya ukaguzi iliyofanyika ambapo katika ukaguzi huo dosari mbali mbali pamoja na athari zilizotokana na dosari hizo zilibainishwa na kutolewa mapendekezo kwa uongozi wa Shirika kwa lengo la kuzirekbisha na kuendelea kuimarisha huduma za bima kupitia mifumo iliyopo, baadhi ya dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

17.2.1.1 Dosari katika Mkataba wa matengenezo ya mfumo wa CIMIS shilingi **1,962,857,200**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) liliingia mkataba tarehe 13 Aprili 2019 wenye thamani ya jumla ya shilingi **1,546,980,000** na kampuni ya IMATIC Technology Company Ltd (ITL) iliyopo Dar es Salaam kwa ajili ya kutengenezewa Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa huduma za Bima "Core Insurance Management Information System (CIMIS)".

Aidha katika kutafuta njia za kuweza kufanikisha mchakato huo Shirika la Bima Zanzibar liliingia mkataba na kampuni nyengine inayojuulikana kwa jina la BITZ iliyopo Zanzibar wenye thamani ya shilingi **104,000,000** kwa ajili ya kuwa Mshauri Elekezi (Consultant) kwa upande wa Shirika ili kuweza kulisaidia Shirika katika kufanikisha mchakato huo wa utengenezwaji wa mfumo wa CIMIS ambapo kampuni ya BITZ ilikuwa inakusanya mahitaji kutoka katika Shirika na kuyawasilisha kwa Kampuni ya ITL inayotengeneza Mfumo kwa mujibu wa utaratibu waliokubaliana katika mkataba.

Hata hivyo katika ukaguzi uliofanyika dosari mbali mbali zimebainika katika utekelezaji wa mchakato huo wa utengenezwaji wa Mfumo wa CIMIS ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa awali baina ya Shirika na kampuni ya IMATIC (ITL), kampuni ilikubali kufanya kazi ya kutengeneza, kujaribu hadi kukamilisha na kuufunga mfumo wa CIMIS kwa ajili ya matumizi kwa kipindi cha muda wa miezi 24 kuanzia tarehe 13 April 2019 hadi to tarehe 13 April 2021. Ukaguzi ulibaini kwamba kampuni ilishindwa kutimiza masharti ya mkataba na kupitisha mda waliokubalina na kulazimika kuomba mda wa ziada ambapo Shirika lilikubaliana na maombi hayo na kuongeza mda wa miezi 8 hadi tarehe 31 disemba 2021 ili kukamilisha kazi hiyo kwa ufanisi. Aidha, pamoja na nyongeza hiyo ya muda Kampuni haikukamilisha kazi kwa ufanisi jambo lililopelekea ZIC kuendelea kuutumia mfumo huo kinyume na matarajio yaliowekwa.
- Kuongezeka kwa gharama kutokana na kufanyika mikataba ya ziada yenye jumla ya shilingi **213,127,200** sawa na asilimia 13.78 ya ongezeko kutoka mkataba wa awali wenye jumla ya shilingi **1,546,980,000** na kupelekea jumla ya fedha zilizolipwa kwa Kampuni ya ITL kuongezeka na kufikia shilingi **1,760,107,200** ambapo gharama hizo zilitokana na kampuni ya ITL kupitiliza mda wa kukamilisha kazi ya kutengeneza mfumo wa CIMIS.
- Kuongezeka kwa gharama za mshauri elekezi kwa thamani ya shilingi **98,750,000** kutoka mkataba wa awali wenye jumla ya shilingi **104,000,000** na kupelekea jumla ya fedha alizolipwa mshauri elekezi kufikia shilingi **202,750,000** ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 95.0. Kuwepo kwa ongezeko hilo bila ya kupata idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa

Serikali kumejitokeza ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi ambapo kifungu nambari 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba “Iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba kwa zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval).”

Hadi ukaguzi unakamilika jumla ya gharama zilizoobainika kutumika katika utengenezaji wa mfumo mpya wa CIMIS ni shilingi **213,127,200** ambazo zimelipwa kwa Mshauri Elekezi (BITZ) na shilingi **1,760,107,200** zimelipwa kwa Mtengenezaji Mfumo (System Vendor – ITL) na kupelekea jumla ya fedha zote zilizotumika kwa malipo ya Mfumo wa CIMIS ni shilingi **1,962,857,200**.

17.2.1.2 Kutokufikia malengo ya matumizi ya mfumo wa CIMIS

Shirika la Bima Zanzibar liligharamika kutengenezesha mfumo wa CIMIS kwa ajili ya kufanya kazi za usimamizi wa Huduma za biashara za Bima pamoja na kufanya shughuli nyengine za uendeshaji wa Shirika kama vile shughuli za kusimamia ununuzi, masuala ya mishahara, Ukekezaji, bajeti, kutunza taarifa za mali za ofisi, Malipo Janja “Smart Pay”, Sera Janja “Smart Policy”, n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba CIMIS haikuweza kufikia malengo yaliotarajiwa na shirika kutokana kuwepo kwa dosari mbalimbali zilizojitokeza kama

inavyoonkana katika jadweli lituatalo:-

Jadweli Nambari 45: Malengo ya mfumo wa CIMIS ambayo hayakuweza kufikiwa

Lengo Namba	Lengo lililotarajiwa	Matokeo baada ya kutengenezwa na kutumika mfumo wa CIMIS
1.	Kuimarisha udhibiti wa usimamizi na kuboresha uwajibikaji kwa kufanya maamuzi katika shirika juu ya masuala yanayohusiana na bima, shughuli za fedha na uwekezaji.	Halikufanikiwa kutekelezwa kutokana na CIMIS hutoa ripoti tofauti ambazo na uhalisia na hivyo haziwezi kutegemewa kwa uamuzi juu ya masuala ya fedha, bima na uwekezaji pia na kwa watumiaji wengine wa ripoti hizo.
2.	Kuliwezesha Shirika kufunga akaunti za hesabu za kifedha 31 Januari kila mwaka.	Lengo halikufikiwa kutokana na Mfumo kutoa taarifa zisizo sahihi (key input) ambazo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za kifedha hali iliopelekea baadhi ya ripoti kuandaliwa na kufanyiwa mlingano(reconciliation)kwa njia ya kawaida (manual) mikono na taarifa yengine zilikosekana kabisa kwenye mfumo kwa mfano; taarifa za kibenki (Banc Assurance) pamoja na shughuli za mawakala (brokers transaction)
3.	Kuboresha mchakato wa ufuatiliaji wa madai kwa kujumuisha sera ya bima na moduli za reinsurence ili kumpa mtumiaji uthibitisho wa muda wa malipo kulingana na tarehe iliyoripotiwa madai au tokeo.	Ripoti za “Reinsurance” hutolewa na moduli ya smart policy kupitia “Smart ERP” ambayo hutoka taarifa zisizo sahihi hali ambayo hupelekea ripoti za “reinsurance” zinazozalishwa na CIMIS (ERP) kutokuwa za kutegemewa.

4.	Kupangilia mikataba ya bima ya ZIC na mipangilio ya uwezesaji pamoja na kuunganisha kielektroniki mchakato wa "reinsurance" katika usimamizi wa sera na utaratibu mzima wa madai.	Mikataba na ripoti za uwezesaji zinazotolewa na moduli ya "Smart Policy" kupitia smart ERP hutoa taarifa zisizo sahihi na kupelekea taarifa za "reinsurance" zinazozalishwa na CIMIS (ERP) kutokutegemewa kwa maamuzi.
----	---	--

Kushindwa kutekelezeka ipasavyo kwa malengo hayo malengo ya kiufundi kunapelekea mfumo wa CIMIS kutokuwa na manufaa kwa kutokufikia lengo lililokusudiwa na hivyo kuliingiza Shirika hasara ya upotevu wa fedha kwa kutokuwepo kwa uwiano wa faida na gharama ya fedha ambayo imetumika kutengenezea mfumo huo.

17.2.1.3 Mfumo wa CIMIS kuanza kutumika "GO-LIVE" kabla ya kufanyiwa Majaribio ya kutosha kwa moduli zake.

Kwa mujibu wa taratibu zilizobora (best practices) pamoja na muongozo kutoka Wakala wa Serikali Mtandao wenye Hati namba eGA/EXT/APA/005 toleo nambari 1.0 la Novemba 2018 kifungu cha 2.1.6 unaohusiana na kufanya majaribio ya mfumo "System Testing" kabla ya kuanza kutumika unaeleza kwamba majaribio ya mifumo yanapaswa kufanyika kulingana na mahitaji yaliyoainishwa na watumiaji wa mfumo. Hii ina maana ya kwamba katika kila kipengele cha mfumo (moduli) ni lazima kifanyiwe majaribio ya kutosha na kujiridhisha kabla ya kuanza kutumika ili kuweza kubaini usahihi wa utendaji kazi wa mfumo kama ilivyotarajiwa kutokana na mahitaji ya watumiaji wa mfumo. Aidha matokeo ya majaribio hayo ni lazima yawekwe katika kumbu kumbu na kutolewa mapendekezo utayari wa mfumo kutokana na matokeo hayo.

Baadhi ya majaribio ambayo hufanyika katika utendaji kazi wa mfumo kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo ni kama vile Jaribio la application, Jaribio la utendaji kazi (performance test), Jaribio la usalama (security test), Jaribio la kukubalika kwa mfumo (User acceptance test) n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Bima Zanzibar halijafanya majaribio ya kutosha katika kila kipengele cha mfumo wake wa CIMIS kuhusiana na utendaji wake wa kazi. Hali hii imebainika kutokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu inayoonesha kuwa mfumo umejaribiwa na kukubalika kwa watumiaji wote (User Acceptance Test Document) na kwamba uko tayari kwa matumizi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kama ilivyoielezwa katika kifungu nambari 23 na 24 cha Mkataba huo. Aidha, nyaraka hiyo huthibitishwa rasmi na uongozi wa Shirika.

Kutokufanyika kwa majaribio ya kutosha na kujiridhisha katika uanzishaji au uboreshaji wa mfumo kunaweza kupelekea mfumo kuzalisha taarifa (ripoti) zisizokuwa sahihi. Vile vile mfumo unaweza kusababisha kutokezea mabadiliko kadhaa baadae na kupelekea Shirika kuingia hasara ya kulipia gharama zisizotarajiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha kuwa mfumo mpya unafanyiwa majaribio ya kutosha kuhusu utendaji wake kwa kila kipengele (moduli) ili kuweza kubaini kama unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na kutoa matokeo bora.

17.2.1.4 Kukosekana kwa mazingira mazuri ya kufanyia majaribio ya Mifumo (Poor Test Environment)

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba, Taasisi inatakiwa kuandaa mazingira mazuri ya TEHAMA "Reliable Test Environment " kwa ajili ya kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mifumo kabla ya kuanza kutumika katika mazingira halisi ya kazi "Go - Live".

Mazingira mazuri ya kufanya majaribio ni pamoja na kuwepo kwa kompyuta zilizo salama na zenye uwezo mkubwa wa kufanya kazi (Test servers), miundombinu ya mtandao iliyo imara itakayoweza kusaidia zoezi la majaribio kufanyika kwa weledi na ufanisi na vile vile kushirikishwa kwa ngazi tofauti za watumiaji wa mfumo ili kuweza kuthibitisha matokeo kulingana na mahitaji yao ya kazi na hatimae kuandikwa nyaraka za kukubali mfumo (User Acceptance Report / Installation Certificates etc).

